



MISINGI YA ELIMU KWA MWANADAMU



ROHO YA UNABII
VITABU MAJUMBANI UHAMISHONI UGHAIBUNI

RohoYaUnabii.Org, MaarifaMtandaoni.Africa, MaarifaMtandaoni.Com

Kimetafsiriwa Kutoka Kitabu cha

Roho ya Unabii

Uhamishoni Ughaibuni Mtandaoni Majumbani

FUNDAMENTALS OF EDUCATION

ENENDENI MTANDAONI KOTE

MISINGI YA ELIMU YA KILA MWANADAMU
{Shuleni, Nyumbani na Kwenye Taifa}
{Fundamentals of Education for home, school, and community}
{WATOTO, WATU WAZIMA, VIJANA, NA WAZEE}
Kulea Ni Mwenye Dhambi mmoja
kumkuza Mwenye dhambi mwingine

By RYU
VITABU MTANDAONI UHAMISHONI UGHAIBUNI MAJUMBANI
SHUKRANI KWA MWENYEZI MUNGU WA MBINGUNI
Enendeni Mtandaoni Kote

TABARUKU Kwa Mwenyezi Mungu

Maelezo ya Muhtasari wa Kitabu

Kitabu cha Christian Education kinaelezea kwamba elimu ya kweli ni ukuaji wa usawa wa nguvu za kimwili, kiakili, na kiroho, unaolenga kurejesha taswira ya Mungu katika nafsi. Kinalenga kumjua Mungu, kukuza tabia kwa ajili ya huduma, na kutumia Biblia kama msingi wa maarifa. Kuelimisha watoto na watu wazima kurudisha sura ya Mungu na kuwa tayari kwa umilele ndiyo lengo la Mungu kwa elimu, japo kuweza kukabiliana na mazingira yetu ya kila siku na kujikimu kimaisha, ni jambo muhimu tunaposafiri hapa duniani, na kitabu hiki kimeelezea kwa undani jambo hili!

Watafsiri, Waombezi, Wahariri, Washauri, Wenye njozi, Wataalamu wa Teknolojia, na watia moyo wote

- 1. Grace Momadi-Masaka wa New Jersey, Marekani**
- 2. Mrs and Mrs Aaron Weber - Alaska, Marekani**
- 3. Mapesa Kambira Jonathan- Pennslyvania, Marekani**
- 4. Ngusa Mayunga-Rukwa, Tanzania**
- 5. Eliakimu Mabula- Bariadi**
- 6. Philemon Mswanyama- Tabora, Tanzania**
- 7. Chris Gideon wa Geita, Tanzania**
- 8. Niwaeli Mburuja - Suji, Tanzania**
- 9. Cindy Tustch - Washington State, Marekani**
- 10. John na Judi Mugane -Boston, Massachusets**
- 11. Daniel Nyangaresi Masaka - Kisii Kenya**
- 12. Mbusi Mpagalushu - Arusha, Tanzania**
- 13. Sandra Baron - Kentucky, Marekani**
- 14. Daudi Jabez Masaka - Pennslyvania, Marekani**
- 15. Paul Momadi Masaka - New Jersey, Marekani**
- 16. Sarah Akinyi Nyangoe, - Rorya, Tanzania**

17. Ibrahimu Ibare Ngibhombi - Butiama, Tanzania

Wenu Mjoli, Grace Momadi-Masaka - New Jersey, Marekani

ROHO YA UNABII

Pen of Inspiration -Spirit of Prophecy- SOP

Runinga ya Upendo

YALIYOMO (Tafuta Kurasa zilipo!)

Dibaji.....	viii
Sura ya 1	
ELIMU SAHIHI.....	1
Kufungiwa ndani ya vyumba vya Shule siku nzima.....	4
Kupungua nguvu za Kimwili kwa jamii.....	6
Umuhimu wa Mafunzo ya Nyumbani.....	8
Kazi ya Kimwili kwa Wanafunzi {kazi za mikono}.....	13
Kwa marejeleo ya Ziada.....	23
Sura ya 2	
KRISTO MWALIMU.....	24
Kwa rejea za Ziada.....	26
Sura ya 3	
WITO KWA WANAFUNZI WETU.....	27
Kwa marejeleo ya Ziada.....	31
Sura ya 4	
MASHAURI JUU YA ELIMU.....	33
Kwa marejeleo ya Ziada.....	36
Sura ya 5	
KUTEMBELEA MJI WA COLLEGE CITY AMBAPO KUNA CHUO KIKUBWA.....	37
Sura ya 6	
NYUMBANI NA SHULENI.....	39
Kwa Marejeleo ya Ziada.....	43
Sura ya 7	
Umuhimu wa Mafunzo ya Kimwili.....	44
Kwa marejeleo ya Ziada.....	48
Sura ya 8	
UADILIFU WA DANIELI KATIKA JARIBU (ALIPOTAHINIWA).....	49
Kwa Marejeleo ya Ziada.....	52

Sura ya 9	
UMUHIMU WA ELIMU.....	53
INAENDELEA.....	57
Umuhimu wa Elimu.....	57
Sura ya 10	
HATARI YA KUSOMA HADITHI ZA KUBUNI NA VITABU VYA KIKAFIRI - {FICTION, NOVELS}.....	61
Kwa marejeleo ya ziada.....	62
Sura ya 11	
SHULE ZA WAEBRANIA WA KALE.....	63
Kwa marejeleo ya ziada.....	66
Sura ya 12	
UCHUMBA NA NDOA.....	67
Kwa Marejeleo ya ziada.....	71
Sura ya 13	
UMUHIMU WA MAFUNZO KATIKA KAZI YA MUNGU.....	72
Sura ya 14	
ELIMU SAHIHI KWA VIJANA.....	76
Kwa marejeleo ya Ziada.....	82
Sura ya 15	
THAMANI YA KUJIFUNZA BIBLIA.....	83
Sura ya 16	
KITABU CHA VITABU.....	87
Kwa marejeleo ya ziada.....	93
Sura ya 17	
WAJIBU WA MZAZI.....	94
Sura ya 18	
ELIMU NA AFYA.....	99
Sura ya 19	
ELIMU YA NYUMBANI.....	102

Sura ya 20	
WALEVI WA AKILI.....	112
Kwa Marejeleo ya Ziada.....	114
Sura ya 21	
VITABU KATIKA SHULE ZETU.....	116
Sura ya 22	
MWALIMU WA UKWELI NDIYE MWELIMISHAJI PEKEE ALIYE SALAMA.....	121
Sura ya 23	
HAZINA ZA KUHFADHI AKILI.....	126
Sura ya 24.....	130
SAYANSI YA WOKOVU NI YA KWANZA KATIKA SAYANSI ZOTE.....	130
Sura ya 25	
TABIA YA KIKRISTO IDHIHIRISHWE KWA MFANO KWA WALIMU NA WANAFUNZI.....	134
Sura ya 26	
ULIMWENGU KWA HEKIMA HAUKUMJUA MUNGU.....	138
Sura ya 27	
UHUSIANO WA ELIMU KATIKA KAZI YA MUNGU.....	142
Sura ya 28	
HAJA YA WATENDAKAZI WALIOFUNZWA.....	150
Sura ya 29	
KWA WALIMU NA WANAFUNZI.....	156
Sura ya 30	
ELIMU BORA NA MADHUMUNI YAKE.....	163
Sura ya 31	
KRISTO KAMA MWALIMU.....	166
Sura ya 32	
ELIMU MUHIMU SANA KWA WATENDA KAZI WA INJILI.....	170
Sura ya 33	
WANAFUNZI KUAMUA HATIMA YAO YA MILELE.....	172

Sura ya 34	
URASIMU, NA SIO TARATIBU, ULIO WA UOVU.....	177
Sura ya 35	
KWA WAALIMU.....	182
Sura ya 36	
KUSIMAMISHWA SHULE KWA WANAFUNZI (SUSPENSION).....	193
Sura ya 37	
KWA WANAFUNZI WA CHUO CHA BATTLE CREEK.....	199
Sura ya 38	
WANAFUNZI WANAHAITAJIKA KUWA WATENDAKAZI PAMOJA NA MUNGU.	
203	
Sura ya 39	
MANENO KWA WANAFUNZI.....	207
Sura ya 40	
JIFUNZENI BIBLIA KWA AJILI YENU WENYEWEE.....	215
Sura ya 41	
KAZI NA ELIMU.....	218
Sura ya 42	
MAANDALIZI YA HARAKA YA KAZI.....	231
Sura ya 43	
ELIMU MUHIMU.....	254
Sura ya 44	
ELIMU KAMILI NA YENYE UADILIFU.....	258
Sura ya 45	
VITABU NA WAANDISHI KATIKA SHULE ZETU.....	264
Kwa Marejeleo ya Ziada.....	269
Sura ya 46	
KITABU KIKUU CHA KUJIFUNZIA.....	270
Sura ya 47	
ELIMU YA JUU.....	272

Sura ya 58	
MWALIMU WA KIMBINGU-MWALIMU WA MBINGUNI.....	275
Sura ya 49	
ELIMU YA KWELI.....	281
Rejea za ziada.....	288
Sura ya 50	
MAFUNZO YA KAZI ZA MIKONO.....	289
Sura ya 51	
MVUTO WA KIELIMU KWA MAZINGIRA.....	293
Sura ya 52	
UMUHIMU WA UTAMADUNI WA KIMWILI.....	296
Sura ya 53	
ELIMU YA JUU YA KWELI.....	299
Sura ya 54	
MFANO WA KRISTO KINYUME NA MAONESHU YA NJE.....	306
Kwa marejeleo ya Ziada.....	308
Sura ya 55	
KIELELEZO CHA KIMBINGU.....	309
Sura ya 56	
BIBLIA KITABU MUHIMU ZAIDI KWA ELIMU KATIKA SHULE ZETU.....	311
Kwa Marejeleo ya Ziada.....	317
Sura ya 57	
NIDHAMU SAHIHI YA SHULE.....	318
Sura ya 58	
BIBLIA KATIKA SHULE ZETU.....	328
Kwa Marejeleo ya Ziada.....	333
Sura ya 59	
USHUHUDA MAALUM KUHUSIANA NA SIASA.....	334
Kwa Marejeleo ya Ziada.....	340
Sura ya 60	

KUPANDA KANDO YA MAJI YOTE.....	343
Sura ya 61	
KAZI YA SHULE ZETU ZA MAFUNZO.....	344
Sura ya 62	
JE, SOTE TUTAHAMIA KARIBU NA TAASISI ZETU NA KUJAZANA HUKO {KUFANYA KOLONI}.....	347
Kwa Masomo ya Ziada.....	350
Sura ya 63	
MASOMO KUTOKA KATIKA MAISHA YA SULEMANI.....	352
Sura ya 64	
WALIMU KAMA MIFANO YA WAKRISTO WAADILIFU.....	356
Sura ya 65	
UMUHIMU KATIKA ELIMU.....	362
Sura ya 66	
UJUMBE KWA WALIMU.....	365
Kwa Marejeleo ya Ziada.....	367
Sura ya 67.....	368
UTOAJI ULIOFANYWA KWA AJILI YA SHULE ZETU.....	368
Sura ya 68	
MWALIMU, JITAMBUE.....	372
Kwa Marejeleo ya Ziada.....	374
Sura ya 69	
KAZI ILIYO MBELE YETU.....	375
Sura ya 70	
USHAURI KWA WALIMU.....	378
Kwa marejeleo ya ziada.....	382
Sura ya 71	
UELEWA BORA WA KWELI KWA VIJANA WETU.....	384
Kwa Masomo ya Ziada.....	387
Sura ya 72	

Dibaji

Mkusanyiko wa kwanza wa makala kutoka katika kalamu ya Bibi E. G. White juu ya swala la elimu ya Kikristo ulichapishwa mwaka 1886. Kijitabu chenye maagizo haya kilikuwa na kichwa kisemacho "Chaguzi Kutoka katika Shuhuda kuhusu suala la Elimu." Na kisha kuchapishwa tena na upanuzi wa kijitabu hiki ukatolewa mwaka wa 1893, chini ya kichwa kisemacho "Elimu ya Kikristo." Baadaye nyongeza ya "Elimu ya Kikristo" ilitolewa ikiwa na mambo ya ziada. Mnamo mwaka 1897, "Shuhuda Maalum juu ya Elimu" ilichapishwa. Toleo hili dogo lina makala zenye thamani isiyohesabika kwa walimu wetu. Maelekezo katika hiki kitabu hayajawahi kutolewa hapo awali na hujumuisha sehemu kuu za maandishi ya mwandishi juu ya elimu wakati wa miaka 1893-1896. Katika mwaka wa 1900 hakimiliki ilitolewa kwa Shuhuda, gombo la VI. Toleo hili lilijumuisha sehemu kubwa ya elimu na kuisitiza haja ya mageuzi ya elimu.

Kitabu kiitwacho "Elimu" kilitolewa mnamo 1903, kikishughulika na matatizo makubwa Zaidi na kanuni katika kazi ya shule, huku mwaka wa 1913 "Mashauri kwa Walimu, Wazazi, na Wanafunzi Kuhusu Elimu ya Kikristo" ilionekana kwa mara ya kwanza, kukabiliana na matatizo mengi ya kina ambayo ni ya kawaida katika elimu.

Makala katika juzuu hili la sasa yametolewa kutoka vyanzo mbalimbali. Yamechaguliwa kutoka katika "Elimu ya Kikristo (*Christian Education*)," "Shuhuda Maalum juu ya Elimu," "Kiasi cha Kikristo na Usafi wa Biblia (*Christian Temperance and Bible Hygiene*)," *Review and Herald*, Ishara za Nyakati, Maelekezo kwenye gazeti la *Youth Instructor*, na *Bible Echo*. Isipokuwa makala moja, "Elimu inayofaa (*Proper Education*)," Hakuna chaguzi zilizofanywa kutoka majuzuu mengine yoyote ya maandishi ya mwandishi ambayo tayari yameshapishwa. Makala mbili za maandishi, "Kusimamishwa kwa Wanafunzi Suspension of Students" na "Nidhamu Sahihi ya Shule (*Correct School Discipline*)," yameingizwa kwa idhini ya Wadhamini wa Bi. E. G. White Estate na mashauriano ya ndugu wa konferensi Kuu. Makala hizi mbili ziliandikwa zaidi ya miaka ishirini na tano iliyopita na zilipatikana wakati huo kwa wakuu wa shule. Makala hizi mbili zinapaswa kusomwa pamoja.

Makala zote zimechapishwa bila ufupi na zimepangwa kwa mpangilio. Faida ya kusoma makala kamili iliyopangwa katika utaratibu ambao imeandikwa utakuwa na mvuto wake maalum kutokana na mpangilio wake wa kihistoria. Orodha ya nyongeza ya makala mwishoni mwa sura mbalimbali, pamoja na Jedwali la Yaliyomo, litajumuisha orodha kamili ya maandishi ya mwandishi juu ya swala la Elimu ya Kikristo.

Kitabu hiki kimetolewa kwa matumaini kwamba kinaweza kuwa na thamani isiyopimika kwa mamilioni ya walimu ambao hawajapata fursa hiyo ya kusoma maelekezo haya. Kinaweza pia kuamsha nia mpya na kujifunza kwa wale ambao

wanaweza kuwa wameisoma hapo awali, na hebu sote tuhamasike kwa undani kufuata kwa uaminifu zaidi katika mienendo yetu ya kila siku kanuni hizi zilizowekwa wazi.

Idara ya Elimu ya konferensi Kuu (General Conference).

Sura ya 1

ELIMU SAHIHI

Kazi nzuri zaidi kuwahi kupewa kwa wanaume na wanawake ni kushughulikia akili za ujana. Tahadhari na uangalifu mkubwa zaidi unapaswa kuchukuliwa katika elimu ya vijana katika kubadilisha mbinu na namna ya kufundisha ili kuweza kuziamsha na kisha kuzileta kwenye utendaji nguvu bora na za hali ya juu za akili na nia. Wazazi na walimu wa shule, hakika hawastahili kuwaelimisha watoto vema, ikiwa wenyewe hawatajifunza kwanza somo la kiasi, kutawala nafsi, saburi, uvumilivu, utu wema na upendo. Hii ni nafasi muhimu kiasi gani kwa wazazi, walezi, na walimu basi! Ni wachache sana wanaotambua mahitaji/matakwa muhimu zaidi ya akili, na namna ya kuelekeza ubongo unaokua, mawazo yanayokua na hisia za ujana. {FEsw 15.1}

Kuna wakati wa kuwaelekeza na kuwafundisha watoto na wakati wa kuelimisha vijana; na ni muhimu kwamba shuleni, yote haya mawili yaunganishwe kwa kiasi kikubwa. Watoto wanaweza kufunzwa kwa ajili ya huduma ya dhambi au kwa utumishi wa haki. Elimu ya awali ya vijana hutengeneza tabia yao ya maisha ya kiulimwengu na ya maisha ya kidini. Sulemani asema, "Mlee mtoto katika njia impasayo; naye hataiacha hata atakapokuwa mzee," Lugha hii ni chanya. Mafunzo ambayo Sulemani anayaamuru ni kuelekeza, kuelimisha na kuendeleza. Ili wazazi na walimu wafanye kazi hii, ni lazima wao wenyewe waelewe "njia" impasayo mtoto kuiendea. Hii inatia moyo kuliko kuwa na ujuzi wa vitabu tu. Inahusiha kila kitu ambacho ni chema, cha wema, haki, na kitakatifu. Huzingatia utendaji wa kuwa na kiasi, utauwa, upendano wa kindugu, na upendo kwa Mungu na kwa wenzetu. Ili kufikia lengo hili, elimu ya kimwili, kiakili, kimaadili na ya kidini ya watoto lazima izingatiwe (ipewe umakini mkubwa). {FEsw 15.2}

Elimu ya watoto, nyumbani ama shuleni, haipaswi kuwa kama mafunzo ya wanyama walio bubu; kwani watoto wana nia ya akili, ambayo inapaswa kuelekezwa ili kutawala na kudhibiti nguvu zao zote. Wanyama bubu wanahitaji kuelekezwa; kwani hawana uamuzi na akili. Lakini akili ya mwanadamu lazima ifundishwe kujitawala. Ni lazima ielimishwe kumtawala mwanadamu, wakati wanyama wanadhhibitiwa na bwana wao, na wamezoezwa kuwa wanyenyekevu kwake. Bwana wa yule mnyama ndiye akili, uamuzi, na mapenzi ya mnyama wake. Mtoto anaweza kufunzwa kutokuwa na mapenzi yake mwenyewe, kama mnyama. Hata upekee, yaani utu wake na utambulisho wake, unaweza kuunganishwa katika yule anayesimamia mafunzo yake; mapenzi yake, kwa nia zote na madhumuni, yakiwa/yakawa chini ya mapenzi ya mwalimu. {FEsw 15.3}

Watoto ambao wameelimishwa hivyo watakuwa na mapungufu ya nguvu za maadili na wajibu binafsi. Hawajafundishwa kutembea katika uamuzi na kanuni; mapenzi yao yametawaliwa na mwingine, na akili haijashughulishwa ili ipanuke na kuimarika kwa kutumiwa. Hawajaelekezwa na kunidhamishwa kuhusiana na maumbile yao ya kipekee na uwezo wao wa akili, kuzitumia nguvu zao za juu zinapohitajika. Walimu wasiishie hapa, bali watilie maanani hili, hasa katika ukuzaji wa nguvu zilizo dhaifu zaidi, ili nguvu zote ziweze kutumiwa, na kukuzwa kutoka kiwango kimoja cha nguvu hadi kingine, ili akili ipate uwiano unaostahili. {FEsw 16.1}

Kuna familia nyingi za watoto ambao wanaonekana kuwa wamefunzwa vizuri, wakati wawapo chini ya mafunzo ya nidhamu na ratiba fulani; lakini wakati mfumo ambao umewashikilia ili kuweka sheria unapovunjika, wanaonekana kutokuwa na uwezo wa kufikiri, kutenda, au kujiamulia. Watoto hawa wamekuwa kwa muda mrefu chini ya utawala wa chuma, nao hawakuruhusiwa kufikiria na kutenda wao wenyewe katika mambo yale ambayo ilikuwa ni sahihi sana kuyaishi na iliwapasa iwe hivyo, na wanakosa ujasiri ndani yao wenyewe wa kutembea katika uamuzi wao wenyewe, na kuwa na maoni yao wenyewe. Na wanapokwenda mbali na wazazi wao ili wajitendee wenyewe kwa utashi wao, wanaongozwa kwa urahisi kwa uamuzi wa wengine katika mwelekeo mbaya. Hawana uimara wa tabia. Hawakuachwa katika uamuzi wao wenyewe kwa haraka na kadri inavyowezekana, na kwa hiyo akili zao hazikuendelezwa na kuimarishwa ipasavyo. Wamekuwa hivyo kwa muda mrefu wakidhibitiwa kabisa na wazazi wao kiasi kwamba wanawategemea kabisa wao; wazazi wao ndiyo akili na uamuzi kwao. {FEsw 16.2}

Kwa upande mwingine, vijana hawapaswi kuachwa kufikiri na kutenda kwa uhuru bila ya uamuzi wa wazazi na walimu wao. Watoto wanapaswa kufundishwa kuheshimu uamuzi wenye uzoefu, na kuongozwa na wazazi na walimu wao. Wanapaswa kuelimishwa kwamba akili zao zitaunganishwa na akili za wazazi wao na walimu, na kufundishwa ili waweze kuona kufaa kutii shauri lao. Kisha Baadaye watakapoondoka katika mkono wa kulea wa wazazi wao na walimu, tabia zao hazitakuwa kama mwanzi utetememeshwao kwa upepo. {FEsw 17.1}

Mafunzo makali ya vijana, bila kuwaelekeza ipasavyo kufikiri na kutenda wenyewe kama uwezo wao wenyewe wa nia ya akili itakavyowaruhusu, ili kwa njia hii wawe na ukuaji wa mawazo, hisia za kujistahi, na kujiamini katika uwezo wao wenyewe wa kufanya kila jambo, yatazalisha kundi ambalo ni dhaifu katika nguvu ya kiakili na kimaadili. Na watakaposimama ulimwenguni ili kutenda kwa ajili yao wenyewe, itafichua ule ukweli kwamba wamefunzwa, kama wanyama, na sio kuelimishwa (trained or conditioned but not educated). Nia zao, badala ya kuongozwa, walishurutishwa kutii kwa marudi makali ya wazazi na walimu. {FEsw 17.2}

Wazazi na walimu wale wanaojivunia kuwa na udhibiti kamili wa akili na nia za watoto walio chini ya uangalizi wao, wangeacha majigambo yao, wangeweza

kufuatilia maisha ya baadaye ya watoto ambao wametawaliwa kwa nguvu au kwa hofu. Hawa hawajaandaliwa kabisa kushiriki katika majukumu makali ya maisha. Wakati vijana hawako tena chini ya wazazi na walimu wao, na wanalazimika kufikiri na kutenda wao wenyewe, wako katika uhakika wa kuchukua njia mbaya, na kujitoa katika nguvu za majaribu. Hawafanyi maisha haya kuwa na mafanikio, na mapungufu yale yale huonekana katika maisha yao ya kidini. Laiti matokeo ya baadaye ya nidhamu potofu ya walimu wa watoto na vijana ingewekwa mbele yao, wangebadiisha mpango wao wa elimu. Lile tabaka la walimu ambao wameridhika kwamba wana udhibiti kamili wa nia ya wanazuoni wao, sio walimu waliofanikiwa zaidi, ingawa muonekano wa wakati huu unaweza kuwa wa kupendeza au kudanganya. {FEsw 17.3}

Kamwe Mungu hakupanga kwamba akili ya mtu mmoja iwe chini ya udhibiti kamili wa mwingine. Na wale wanaofanya juhudi kuwa na utu wa wanafunzi wao ukiunganishwa ndani yao wenyewe, ikiwa ni akili, mapenzi, na dhamiri kwao, hujitwalia majukumu ya kutisha. Wanazuoni hawa wanaweza, katika mazingira fulani, kuonekana kama askari waliofunzwa vizuri kupigwa gwaride la maisha. Lakini kizuizi kitakapoondolewa, kutaonekana haja ya kuchukua hatua huru kutokana na kanuni thabiti iliyopo ndani yao. Wale wanaofanya kusudi lao kuwa ni kuwaelimisha wanafunzi wao ili waweze kuona na kuhisi kwamba nguvu iko ndani yao wenyewe kuwa wanaume na wanawake wa kanuni imara, wanastahili kwa nafasi yoyote katika maisha {wana sifa inayofaa}, ni walimu muhimu na wenye mafanikio ya kudumu. Kazi yao inaweza isioneshe kuwa na manufaa bora zaidi kwa watazamaji wasiojali, na utumishi wao unaweza kutothaminiwa sana kama ule wa mwalimu ambaye hushikilia akili na utashi wa wanazuoni wake kwa nguvu zake zote bila ya kuwapa uhuru; lakini maisha ya baadaye ya wanafunzi yataonyesha matunda ya mpango bora wa elimu. {FEsw 18.1}

Kuna hatari ya wazazi na walimu kuamuru kama madikteta na kulazimisha sana, huku wanashindwa kuja vya kutosha katika kuwa na uhusiano wa kijamii au Roho yenye urafiki kwa kiasi fulani na watoto wao au wanafunzi. Mara nyingi hujiweka katika kujilinda kupita kiasi na kutokuwa na ucheshi au urafiki (wanajiweka mbali katika mahusiano ili wasifikawe-reserved), na kutumia mamlaka yao kwa njia ya ubaridi, isiyoonyesha huruma au ambayo haiwezi kuvutia mioyo ya watoto wao na wanafunzi (moyo wao unakuwa si laini au mwororo). Ikiwa wangepaswanya watoto karibu yao, na kuonyesha kwamba wanawapenda, na wangeponyesha kupendezwa na juhudi zao zote, na hata katika michezo yao, wakati mwingine hata kuwa kama 'watoto' miongoni mwao, basi wangepafurahisha sana watoto, na wangepata upendo wao na kuipata imani na ujasiri wao. Na kwa wepesi watoto wangepeshimu na kupenda mamlaka ya wazazi na walimu wao. {FEsw 18.2}

Tabia na kanuni za mwalimu zinapaswa kuzingatiwa kuwa za umuhimu mkubwa zaidi kuliko sifa zake za kitaaluma. Kama ni Mkristo mwaminifu, atahisi haja ya

kuwa na shauku sawa juu ya elimu ya kimwili, kiakili, kimaadili, na kiroho ya wanafunzi wake. Ili kutoa mvuto sahihi, anapaswa kuwa mkamilifu katika kujitawala mwenyewe, na moyo wake unapaswa kujazwa sana na upendo kwa wanafunzi wake, ambao utaonekana katika mwonekano wake, maneno, na matendo yake. Anapaswa kuwa na uthabiti wa kitabia, na ndipo anaweza kuzifinyanga akili za wanafunzi wake, na vilevile kuwaelekeza katika sayansi. Elimu ya awali ya vijana kwa ujumla huunda tabia zao kwa maisha yote. Wale wanaoshughulika na vijana wanapaswa kuwa waangalifu sana katika kuwa na sifa za kiakili, ili wapate kujua vyema jinsi ya kuzielekeza nguvu zao, ili ziweze kutumiwa katika matokeo yaliyo bora. {FEsw 19.1}

Kufungiwa ndani ya vyumba vya Shule siku nzima

Mfumo wa elimu uliotekelezwa kwa vipindi vya nyuma umekuwa ukiharibu afya na hata maisha yenyewe. Vijana wengi wadogo wametumia masaa matano kila siku katika madarasa yasiyo sahihi ambavyo hayana hewa ya kutosha, wala ukubwa wa kutosha kwa ajili ya hifadhi yenye afya ya wanafunzi. Hewa katika vyumba hivyo punde huwa sumu kwa mapafu yanayoivuta. Watoto wadogo, ambao viungo vyao na misuli yao sio yenye nguvu, na ambao akili zao hazijaimarika au kumaliza mchakato wa kupevuka, wamefungiwa ndani kwa uharibifu wao. Wengi wamekuwa ni dhaifu sana kiafya kabla ya hapa na hivyo wanashikilia kidogo sana uimara wa maisha ya miili yao, hata kabla ya kuwekwa kwenye mazingira haya tata. Kufungiwa shuleni siku hadi siku huwafanya kuwa na wasiwasi na wagonjwa wa mfumo wa fahamu. Miili yao hudhoofishwa kwa sababu ya uchovu wa hali ya mfumo wa neva. Na ikiwa taa ya uzima itazimika, wazazi na walimu hawafikirii kuwa walikuwa na ushawishi wa moja kwa moja katika kuzima hizi cheche muhimu za maisha. Wanaposimama kando ya makaburi ya watoto wao, wazazi waliopata msiba hutazama kufiwa kwao kama 'kipindi maalumu cha Majaliwa ya Mungu kimewafikia', kumbe, kwa ujinga usio na udhuru, mwenendo wao wenyewe umeharibu maisha ya watoto wao. Na ndipo hushutumu kifo chao kwa Mtoaji uzima au husema ni majaliwa ya Mungu (Mungu amempenda kuliko sisi tulivyompenda, Mwenyezi Mungu ameruhusu apumzike), jambo ambalo ni kufuru. Mungu alitaka hawa wadogo waishi na kuadibishwa, ili wawe na tabia nzuri, na wamtukuze Yeye katika dunia hii, na kumsifu Yeye katika ulimwengu ulio bora. {FEsw 19.2}

Wazazi na walimu, katika kubeba jukumu la mafunzo kwa watoto hawa, hawahisi kuwajibika kwao mbele za Mungu ili waweze kuujua mwili unavyofanya kazi, ili kwamba waweze kuitibu miili ya watoto wao na wanafunzi kwa namna ya kuhifadhi maisha na afya. Maelfu ya watoto wanakufa kwa sababu ya ujinga wa wazazi na walimu. Akina mama watatumia muda mwingi juu ya kazi isiyo ya lazima, juu ya nguo zao na za watoto wao, ili kukidhi muonekano au maonyesho, na ndipo watadai kwamba hawawezi kupata muda wa kusoma, na kupata habari muhimu ili

kutunza afya ya watoto wao. Wanafikiri ni rahisi kwao kujipunguzia bughudha kwa kuwakabidhi na kuwaamini madaktrari kuhusiana na miili yao na hivyo huwaachia maamuzi ambayo wao wangepaswa wayafanye. Ili kuendana na mitindo na desturi, wazazi wengi wametoa kafara afya na maisha ya watoto wao. {FEsw 20.1}

Kuufahamu uumbaji wa ajabu wa mwanadamu, kuelewa mifupa, misuli, tumbo, ini, utumbo, moyo na matundu ya ngozi; na kuelewa utegemezi wa kiungo kimoja juu ya kingine kwa faida ya kiafya ya vyote, ni somo ambalo akina mama wengi hawana shauku nalo. Hawajui chochote kuhusu mvuto wa mwili juu ya akili, na mvuto wa akili juu ya mwili. Akili, ambayo huunganisha vyenye ukomo na Visivyo na vyenye ukomo, hawaonekani kuelewa. Kila kiungo cha mwili kimefanywa kuitumikia akili. Akili ni kitovu cha mwili (akili ndiyo injini inayoendesha mwili wote). Watoto wanaruhusiwa kula vyakula vya nyama-nyama, viungo, siagi, jibini, nyama ya nguruwe, vyakula vya unga vilivyokaangwa au kuokwa kwa unga uliokobolewa (pastry-kama vile keki, donut, pizza, croissant, vitumbua, maandazi, sambusa, na mapochopocho kama hayo), na vitafunio/vitoweo kwa ujumla hivi si vyakula au mlo wenyewe ila huongezewa vitu fulani na kutumika kama vikolezo au viburudisho kwenye chakula {condiments}. Pia wanaruhusiwa kula mara kwa mara na kati ya mlo chakula kisicho na afya. Haya mambo hufanya kazi ya kuharibu tumbo, kulisimua mishipa kwa matendo yasiyo ya asili, na kuidhoofisha akili. Wazazi hawatambui kwamba wanapanda mbegu ambayo itazaa maradhi na kifo. {FEsw 20.2}

Watoto wengi wameharibiwa maisha kwa kusesitiza au kuhimiza mambo yahasuyo akili, na kupuuza kuimarisha nguvu za kimwili (kazi za mikono na mazoezi). Wengi wamekufa utotoni kwa sababu ya hatua iliyochukuliwa na wazazi wasio na haki na waalimu wa shule katika kulazimisha akili zao changa, kwa kubembeleza, kudanganywa, kudekeshwa au kwa hofu, walipokuwa wadogo sana kuona ndani ya chumba cha shule. Akili zao zimejazwa na masomo, wakati hawakupaswa kupewa, bali kuwekwa hadi mfumo wa mwili umekuwa na nguvu za kutosha kustahimili shughuli za kiakili. Watoto wadogo wanapaswa kuachwa huru kama wana-kondoo kukimbia nje, wawe huru na wenye furaha, na wanapaswa kupewa fursa bora zaidi za kuweka msingi wa mfumo mzuri. {FEsw 21.1}

Wazazi wanapaswa kuwa walimu pekee wa watoto wao hadi wamefikia umri wa miaka minane au kumi. Kwa haraka kadri akili zao zinavyoweza kuelewa, wazazi wanapaswa kufungua mbele yao ukuu wa Mungu katika kitabu cha asili/uumbaji. Mama anapaswa kuwa na upendo mdogo kwa vitu bandia katika nyumba yake, na katika maandalizi ya mavazi yake kwa ajili ya muonekano, na anapaswa kupata muda wa kujiimarisha, ndani yake na kwa watoto wake, upendo kwa maua mazuri yaliyochanua na vikonyo vyake. Kwa kuweka umakini wa watoto wake kwa rangi zake tofauti tofauti na aina mbalimbali za maumbo ya maua, anaweza kuwafanya wamfahamu Mungu, aliyeumba vitu vyote vizuri vinavyowavutia na kuwafurahisha.

Anaweza kuongoza akili zao kwa Muumba wao, na kuamsha katika mioyo yao michanga mapenzi kwa Baba yao wa Mbinguni, ambaye amedhihirisha upendo mkuu kwao. Wazazi wanaweza kumshirikisha Mungu kwa kazi Zake zote alizoziumba. Chumba pekee cha shule kwa watoto kutoka umri wa miaka minane hadi kumi lazima kiwe katika angahewa ya wazi, katikati ya maua yaliyochanua na mandhari nzuri ya asili. Na kitabu chao pekee kinapaswa kuwa hazina za asili. Masomo haya, yakitiwa chapa katika akili za watoto wadogo katikati ya picha za kupendeza na za kuvutia za asili hazitasahaulika hivi karibuni. {FEsw 21.2}

Ili watoto na vijana wawe na afya, furaha, uchangamfu, nishati, na misuli na akili iliyositawi vizuri, wanapaswa sana kuwa katika hali ya hewa ya wazi, na kuwa na shughuli na burudani iliyodhibitiwa vyema. Watoto na vijana wanaowekwa shuleni na kufungiwa kwenye vitabu, hawawezi kuwa na mfumo mzuri wa kimwili. Kushughulisha ubongo katika kusoma, bila kuhusisha mazoezi ya kimwili, huwa na tabia ya kuvuta damu kwenye ubongo, na mzunguko wa damu katika mfumo unakosa kuwa na usawa. Ubongo unakuwa na damu nyingi sana, na kwingine mwilini kidogo sana. Kunapaswa kuwa na utaratibu wa kudhibiti masomo yao kwa saa fulani, na kisha sehemu ya muda wao unapaswa kutumika katika shughuli ya kimwili/mikono. Na kama tabia zao za kula. kuvaa, na kulala ni kwa mujibu wa sheria ya kimwili, wanaweza kupata elimu bila kuharibu afya ya mwili na akili. {FEsw 21.3}

Kupungua nguvu za Kimwili kwa jamii

Kitabu cha Mwanzo kinatoa maelezo kamili ya kijamii na maisha ya mtu binafsi, na bado hatuna rekodi ya mtoto mchanga kuzaliwa kipofu, kiziwi, kilema, mwenye upungufu, au utindio wa ubongo. Hakuna tukio juu ya kumbukumbu ya kifo cha asili katika uchanga, utoto, au utu uzima wa mapema. Hakuna hesabu ya wanaume na wanawake wanaokufa kwa ugonjwa. Matangazo ya kumbukumbu za vifo katika kitabu cha Mwanzo yanaoneshwa hivi: "Siku zote za Adamu alizoishi ni miaka mia kenda na thelathini; naye akafa." "Siku zote za Sethi ni miaka mia kenda na kumi na mbili; naye akafa." Kuhusu wengine, kumbukumbu inasema: Aliishi katika uzee mwema; naye akafa. Ilikuwa ni nadra sana kwa mwana kufa kabla ya baba, na tukio kama hilo lilizingatiwa kuwa linastahili kukumbukwa: "Na Harani akafa kabla ya baba yake Tera." Harani alikuwa baba wa watoto kabla ya kifo chake. {FEsw 22.1}

Mungu alimjalia mwanadamu nguvu kubwa sana ambayo imestahimili mlundikano wa magonjwa yanayoletwa katika ubinadamu kama matokeo ya tabia potovu, na imeendelea kwa miaka elfu sita. Hoja hii ya ukweli kwa yenyewe inatosha kuthibitisha kwetu nguvu na nishati ya umeme ambayo Mungu alimpa mwanadamu katika kuumbwa kwake. Ilichukua zaidi ya miaka elfu mbili ya uhalifu na tamaa za mwili kuleta ugonjwa wa mwili juu ya ubinadamu kwa kiwango

chochote kikubwa. Ikiwa Adamu, katika kuumbwa kwake, hangekuwa amejaliwa nguvu kwa umuhimu mara ishirini Zaidi ya wanadamu walizo nazo sasa, binadamu, kwa tabia zao za sasa za kuishi kwa kukiuka sheria za asili, wangetoweka. Wakati wa ujio wa kwanza wa Kristo, ubinadamu ulikuwa umeharibika kwa kasi sana hivi kwamba mlundikano wa maradhi ulishinikiza juu ya kizazi hicho, na kuleta wimbi la ole, na uzito wa taabu usioelezeka. {FEsw 22.2}

Hali mbaya ya ulimwengu kwa wakati huu imekuwa ikiwasilishwa mbele yangu. Tangu anguko la Adamu, ubinadamu umekuwa ukizidi kuzorota. Baadhi ya sababu za hali mbaya ya sasa ya wanaume na wanawake, walioumbwa kwa mfano wa Mungu, zilioneshwa kwangu. Na hisia ya yapi lazima yafanyike ili kuzuia, hata kwa kiwango, kuharibika kimwili, kiakili na kimaadili, kulisababisha moyo wangu kuwa mgonjwa na kuzimia. Mungu hakuiumba jamii katika hali yake dhaifu ya sasa. Hali hii ya mambo si kazi ya Mungu, bali ni kazi ya mwanadamu; imeletwa na tabia mbaya na ukengeufu, kwa kukiuka sheria ambazo Mungu ameweka ili kudhibiti uwepo wa mwanadamu. Kupitia kwa majaribu ya kuendekeza tamaa ya kula, Adamu na Hawa kwanza walianguka kutoka katika hali ya juu, takatifu na yenye furaha. Na ni kupitia jaribu lile lile kwamba jamii ya ubinadamu imedhoofika. Wameruhusu tamaa na hamu ya kula kutawala, na kushusha chini akili na fikra. {FEsw 23.1}

Ukiukwaji wa sheria ya kimwili, na matokeo yake, mateso ya binadamu, yametawala kwa muda mrefu hivi kwamba wanaume na wanawake wanatazama hali ya sasa ya ugonjwa, mateso, unyonge, na kifo cha mapema kama sehemu iliyoteuliwa kwa ubinadamu. Mwanadamu alitoka katika mkono wa Muumba wake, mkamilifu na mzuri wa umbo, na aliyejawa na nguvu za mwili muhimu kiasi kwamba ilikuwa zaidi ya miaka elfu moja kabla ya hamu na tamaa zake mbovu, na ukiukwaji wa jumla wa sheria ya kimwili, ulipotambuliwa juu ya jamii ya wanadamu. Vizazi vya hivi karibuni vimehisi zaidi shinikizo la udhaifu na magonjwa yaliyopo kwa haraka zaidi na kwa uzito kwa kila kizazi. Nguvu muhimu zimedhoofishwa sana kwa kujifurahisha kwa hamu ya kula na tamaa za mwili. {FEsw 23.2}

Wazee kutoka kwa Adamu hadi Nuhu, isipokuwa wachache tu waliishi karibu miaka elfu moja. Tangu siku za Nuhu, urefu wa maisha umekuwa ukipungua kwa kasi. Wale waliokuwa na magonjwa waliletwa kwa Kristo kutoka katika kila jiji, mji na kijiji ili awaponye; kwani walikuwa wamepatwa na magonjwa ya kila namna. Na ugonjwa umekuwa ukiongezeka kwa kasi kupitia vizazi vilivyofuata tangu kipindi hicho. Kwa sababu ya kuendelea kukiuka sheria za maisha, vifo vimeongezeka kwa kiasi cha kutisha. Miaka ya mwanadamu inafupishwa, hata kizazi cha sasa kinaingia kaburini, hata kabla ya umri ambao vizazi vichache vilivyoishi miaka elfu ya kwanza baada ya uumbaji kufika kwenye hatua ya utendaji. {FEsw 24.1}

Ugonjwa umekuwa ukipitishwa kutoka kwa wazazi kwenda kwa watoto, kutoka kizazi hadi kizazi. Watoto wachanga katika utoto wanateseka sana kwa sababu ya

dhambi za wazazi wao, ambazo zimepunguza nguvu zao muhimu. Tabia zao mbaya za kula na kuvaa, na jumla ya ukiukaji wao, hupitishwa kama urithi kwa watoto wao. Wengi wanazaliwa wendawazimu, walemavu, vipofu, viziwi, na tabaka kubwa sana wana upungufu wa akili. Ukosefu wa ajabu wa kanuni ambao hutambulisha kizazi hiki, na ambao unaonyeshwa kwa kutozingatia kwao sheria za maisha na afya, ni wa kushangaza. Ujinga unatawala juu ya swala hili, huku Nuru ikiangaza pande **zote. Pamoja na walio wengi, mahangaiko yao makuu ni, Nitakula nini?** ninywe nini? Na nitavaa nini? Licha ya yote yaliyosemwa na yaliyoandikwa kuhusiana na jinsi tunavyopaswa kuitendea miili yetu, uchu wa kula ndiyo sheria kuu inayotawala wanaume na wanawake kwa ujumla. {FEsw 24.2}

Nguvu za kimaadili zimedhoofishwa, kwa sababu wanaume na wanawake hawaishi katika utii wa sheria za afya, na kufanya jambo hili kubwa kuwa jukumu la binafsi. Wazazi wanawarithisha watoto wao tabia potovu, na magonjwa ya kuchukiza hugaribu damu na kudhoofisha ubongo. Wengi wa wanaume na wanawake wanabaki katika ujinga wa kutojua sheria za uwepo wao, na kujiingiza katika tamaa na uchu wa kula kwa gharama ya akili na maadili, na kuonekana tayari kubaki katika ujinga wa matokeo ya ukiukaji wao wa sheria za asili. Wanaendekeza uchu mpotofu katika utumiaji wa sumu polepole, ambayo hugaribu damu, na kudhoofisha nguvu za neva, na matokeo yake wanajiletea magonjwa na kifo. Marafiki zao wanayaita matokeo ya mwenendo huu kuwa ni majaliwa ya Mungu. Katika hili wanaitukana Mbingu. Waliasi dhidi ya sheria za asili, na kupata adhabu kwa kutumia vibaya sheria zake. Mateso na vifo sasa vimeenea kila mahali, hasa miongoni mwa watoto. Tofauti ni kubwa kiasi gani kati ya kizazi hiki, na wale ambao waliishi katika miaka elfu mbili ya kwanza! {FEsw 24.3}

Umuhimu wa Mafunzo ya Nyumbani

Niliuliza kama wimbi hili la ole haliwezi kuzuilika, na kwamba jambo gani lifanyike ili kuwaokoa vijana wa kizazi hiki dhidi ya maangamizi ambayo yanawakabili. Nilionyeshwa kwamba sababu moja kuu ya hali hii mbaya yenye kutia aibu ya mambo yaliyopo sasa ni kwamba wazazi hawajisikii kuwa na wajibu wa kulea watoto wao kuendana na sheria za kimwili. Akina mama wanawapenda watoto wao kwa upendo wa ibada ya sanamu, na kuendekeza uchu wao wakati wanajua kwamba utadhuru afya zao, na kwa hivyo kuwaletea maradhi na huzuni. Aina hii ya wema ambao hakika ni ukatili unadhihirika kwa kiasi kikubwa katika kizazi cha sasa. Matamanio ya watoto yanatimizwa kwa gharama ya afya na mihemko ya furaha, kwa sababu itakuwa rahisi kwa mama kwa wakati huo, kuwafurahisha watoto wake kuliko kuwanyima vile wanavyovitamani, yaani tamaa zao, ambazo zinapiga mayowe. {FEsw 25.1}

Hivyo ndivyo akina mama wanapanda mbegu itakayochipuka na kuzaa matunda. Watoto hawajafundishwa kuzuia uchu wao katika kula na tamaa zao za mwili. Na

wanakuwa wabinafsi, wakaidi, wasiotii, wasio na shukrani, na wasio watakatifu. Akina mama wanaofanya kazi hii watawuna kwa uchungu matunda ya mbegu waliyopanda. Wametenda dhambi dhidi ya Mbingu na watoto wao, na Mungu atawawajibisha wao. {FEsw 25.2}

Iwapo elimu ya vizazi vya nyuma ingeendeshwa kwa mpango tofauti kabisa, vijana wa kizazi hiki hawangelikuwa wapotovu kimaadili na wasio na faida. Wasimamizi na walimu wa shule walipaswa kuwa wale wanaoielewa fiziolojia yaani viungo vya mwili na jinsi vinavyofanya kazi, na ambao wana maslahi ya watoto, sio tu katika kuelimisha vijana kwenye fani za sayansi, bali pia kuwafundisha jinsi ya kuhifadhi afya, ili wapate kutumia ujuzi wao kwa namna bora baada ya kuupata. Wangepaswa kuunganishwa na shule, uanzishwaji wa aina mbalimbali wa shughuli za mikono ili wanafunzi wapate vibarua, na mazoezi ya lazima nje ya saa za darasani. {FEsw 26.1}

Shughuli na burudani za wanafunzi zingepaswa kuwa zinadhibitiwa kwa kuzingatia sheria ya kimwili, na zinapaswa kuchukuliwa ili kuwahifadhi afya njema ya nguvu zote za mwili na kiakili (hasa wakati wetu huu wa media na simu za mikono ukizingatia haya yaliandikwa miaka 140 iliyopita!). Kisha ujuzi wa vitendo wa biashara na shughuli unaweza kutolewa wakati elimu yao ya masomo ya darasani inapokuwa ikiendelea. Wanafunzi shuleni wanapaswa kusaidiwa katika kuamsha utambuzi wao wa maadili ili waone na kuhisi kwamba jamii ina madai juu yao, na kwamba wanapaswa kuishi katika utii wa sheria ya asili, ili waweze, kwa uwepo na ushawishi wao, kwa kanuni na mfano, kuwa faida na baraka kwa jamii. Inapaswa kusesitizwa kwa vijana kwamba, wao wote wana ushawishi ambao daima unazungumza kwenye jamii wanayoishi. ushawishi unaoweza kuboresha na kuinua, au kushusha chini na kuharibu. Somo la kwanza linalopaswa kujifunzwa na vijana ni kujijua wao wenyewe na jinsi ya kuweka miili yao katika afya. {FEsw 26.2}

Wazazi wengi huwaweka watoto wao shuleni karibu mwaka mzima. Watoto hawa hupitia mchakato na ratiba ambayo ni kama desturi au mazoea tu, lakini hawahifadhi kichwani yale wanayojifunza. Wengi kati ya wanafunzi hawa wa daima (waliobobea) wanaonekana kukosa akili ya maisha na mambo ya msingi katika elimu ya kweli. Uchovu wa kuendelea kusoma bila ya kubadilisha shughuli huichosha akili, na hawapendezwi sana na masomo yao; na kwa wengi matumizi ya vitabu huwaletea maumivu. Hawana upendo wa ndani wa fikra, na tamaa ya kujipatia maarifa. Hawajihimizi kwa mazoea ya kutafakari na uchunguzi. {FEsw 26.3}

Watoto wanahitaji sana elimu sahihi ili waweze kuwa wa manufaa duniani. Lakini juhudi zozote zinazoinua utamaduni wa kiakili juu ya mafunzo ya maadili zinaelekea kwenye njia isiyo sahihi, yaani zimepotoka. Kufundisha, kuimarisha, kung'arisha, na kuwasafisha vijana na watoto kuwa bora ndio uwe mzigo mzito wa wazazi pamoja na walimu. Wanafikra wa kina, wanaofikiria mambo ya yatakayoleta

tofauti katika utendaji na wenye fikra za kimantiki ni wachache, kwa sababu ushawishi wa uwongo umeathiri ukuzaji wa akili. Maoni ya wazazi na walimu kwamba kuwa kwenye kitabu saa zote kunaweza kuimarisha akili, yameonekana kuwa na makosa; kwa maana mara nyingi imeonekana kuwa kinyume katika matokeo. {FEsw 27.1}

Katika elimu ya awali ya watoto, wazazi wengi na walimu hushindwa kuelewa kwamba umakini mkubwa unahitaji kuwekwa kwenye mfumo wa kimwili, ili kwamba hali ya afya ya mwili na ubongo iweze kuwa salama. Imekuwa desturi ya kuwatia moyo Watoto kuhudhuria shule wakiwa wachanga tu, wanaohitaji uangalizi wa mama. Wakati wa umri tete/nyeti, watoto mara nyingi husongamana kwenye vyumba vya shule visivyo na hewa ya kutosha, ambapo wanakaa kwa mkao usio sahihi juu ya madawati yaliyotengenezwa vibaya, na matokeo yake vijana na maumbo yao dhaifu yanatiwa ulema. {FEsw 27.2}

Mielekeo na tabia za vijana zitaweza kudhihirika sana kwenye utu uzima. Unaweza kuupinda mti mchanga katika umbo lolote unalochagua, na ikiwa unabaki na kukua kama ulivyoupinda, utakuwa mti uliopata ulema, na daima utakuwa ukinena juu ya jeraha hilo na unyanyasaji uliotoka mkononi mwako.

Unaweza, baada ya miaka ya ukuaji, kujaribu kuunyoosha mti, lakini juhudi zako zote hazitafanikiwa. Daima utakuwa mti uliopinda. Hivi ndivyo ilivyo katika akili za vijana. Wanapaswa kufundishwa kwa uangalifu na kwa upole katika utoto. Wanaweza kufunzwa katika mwelekeo sahihi au usio sahihi, na katika Maisha yao ya baadaye watafuata mkondo ambao walielekezwa katika ujana. Tabia zinazoundwa katika ujana zitakua na ukuaji na kujiimarisha kwa nguvu, na kwa ujumla zitakuwa zilezile katika maisha ya baadaye, zikizidi tu kuwa na nguvu. {FEsw 27.3}

Tunaishi katika kipindi ambacho karibu kila kitu ni cha hovy na cha juu juu (cha kubabaisha). Kuna utulivu na uimara kidogo wa tabia, kwa sababu mafunzo na elimu ya watoto tangu utoto wao ni ya juu juu. Tabia zao zimejengwa juu ya mchanga unaoteleza. Kujikana nafsi na kutawala nafsi hakujaundwa katika tabia zao. Wamekuwa wakidekeshwa, wakiendekezwa na kufurahishwa hadi kuharibiwa kwa maisha yao ya utendaji na uhalisia wa kila siku. Upendo wa starehe/anasa hutawala akili, na watoto wanasifiwa kwa kutia chumvi na kuendekezwa kwa uharibifu wao. Watoto wanapaswa kufundishwa na kuelimishwa kiasi kwamba wataweza kutarajia majaribu, na wajiandae kukutana na magumu na hatari. Wanapaswa kufundishwa kuwa na udhibiti juu yao wenyewe, na kwa ubora kuyashinda magumu; na ikiwa hawatakimbilia hatarini kwa makusudi. na kujiweka wenyewe katika njia ya majaribu bila sababu; kama watajiepusha na mivuto mibaya na jamii zenye maadili mabaya, na kisha kama jambo lisiloepukika walazimishwe kuwa katika jamii hatarishi, watakuwa na nguvu ya tabia ya kusimama kwa ajili ya haki na kuhifadhi kanuni, na watatokeza mbele kwa nguvu za Mungu na maadili

yasiyo na doa. Ikiwa vijana ambao wameelimishwa ipasavyo, wanamfanya Mungu kuwa tumaini lao, nguvu za maadili yao zitasimama dhidi ya mitihani na majaribu ya nguvu zaidi. {FEsw 28.1}

Lakini ni wazazi wachache wanaotambua kwamba watoto wao ni mfano wao na vile nidhamu yao imewafanya kuwa, na kwamba wanawajibika kwa tabia zinazozitengenezwa na watoto wao. Ikiwa mioyo ya wazazi Wakristo ingekuwa katika utii kwa mapenzi ya Kristo, wangeitii Amri na Maagizo ya Mwalimu wa kimbingu: “Bali utafuteni kwanza ufalme ya wa Mungu na haki Yake; na hayo yote mtazidishiwa.” Ikiwa wale wanaokiri kuwa wafuasi wa Kristo wangepanya hivi tu, basi wangetoa, si kwa watoto wao tu, bali pia kwa ulimwengu usioamini, mifano ambayo ingewakilisha ipasavyo dini ya Biblia. {FEsw 28.2}

Ikiwa wazazi Wakristo waliishi kwa kutii kulingana na matakwa ya Mwalimu wa kimbingu, wangehifadhi ushahidi katika kula na kuvaa, na wangeishi zaidi kwa mujibu wa sheria ya asili. Wasingeutumia muda mwingi kwa maisha ya bandia, katika kujijali wenyewe na masumbufu na mizigo ambayo Kristo hakuweka juu yao, bali amewataka waiepuke. Ikiwa ufalme wa Mungu na Haki Yake ndiyo vingekuwa jambo la kwanza na la muhimu sana kuzingatiwa na wazazi, ni muda mchache wa thamani ungepotezwa kwa mapambo ya nje yasiyo na sababu, wakati akili za watoto wao zi karibu kabisa kupuuzwa. Muda wa thamani unaotumiwa na wazazi wengi kwa kuwavalisha watoto wao kwa kujionesha katika maonyesho yao ya burudani ingekuwa bora, bora zaidi, kutumiwa katika kukuza akili zao wenyewe, ili kwamba waweze kuwa na uwezo wa kuwafundisha watoto wao ipasavyo. Sio muhimu kwa wokovu au furaha ya wazazi hawa kwamba wanatumia muda wa thamani ambao Mungu amewapa kabla ya mlango wa rehema kufungwa, katika kuvaa, kuzurura, na kusengenya. {FEsw 29.1}

Wazazi wengi hudai kwamba wana mengi ya kufanya kiasi kwamba hawana muda wa kuimarisha akili zao, kuelimisha watoto wao katika Maisha ya vitendo, au kuwafundisha jinsi wanavyoweza kuwa wana-kondoo katika zizi la Kristo. Ni wakati wa ile hukumu ya mwisho, wakati kesi za wote zitakapoamuliwa, na matendo ya maisha yetu yote kuwekwa wazi mbele yetu katika uwepo wa Mungu na wa Mwanakondoo na wa malaika wote watakatifu, ndipo wazazi watatambua thamani isiyo na kikomo ya muda wao ambao ulitumiwa vibaya (kwa upumbavu). Ndipo wengi sana wataona kuwa mwenendo wao mbaya ndio umeamua hatima ya watoto wao. Sio tu kwamba wameshindwa kupokea maneno ya sifa kutoka kwa Mfalme wa Utukufu, “Vema, mtumwa mwema na mwaminifu ingia katika furaha ya Bwana wako.” lakini wanasikia hukumu ya kutisha ikitamkwa juu ya watoto wao, “Ondokeni!” Hili hutenganisha watoto wao milele na furaha na Utukufu wa Mbinguni, na kutoka kwa uwepo wa Kristo. Na wao wenyewe pia wanapokea hukumu, Ondokeni, “ninyi watumwa waovu na walegevu.” Yesu hatasema kamwe, “Vema,” kwa wale ambao hawajatenda “vema” kwa maisha yao ya uaminifu ya kujikana

nafsi na kujitoa mhanga/sadaka katika kuwafanyia wengine mema na kukuza Utukufu Wake. Wale ambao kimsingi wanaishi ili kujifurahisha wenyewe badala ya kuwafanyia wengine mema, watakutana na hasara isiyo na kikomo. {FEsw 29.2}

Ikiwa wazazi wanaweza kuamshwa kuhisi jukumu la kutisha ambalo linakaa juu yao katika kazi ya kuelimisha watoto wao, Muda wao mwingi ungetumiwa kwa maombi, na kidogo sana kwa maonesho yasiyo ya lazima. Wangetafakari, wangecheua mambo na kusoma kwa kuchunguza, na kuomba kwa dhati kwa Mungu kwa ajili ya hekima na msaada wa Bwana, ili kuwazoeza na kuwalea watoto wao ili wakuze tabia ambazo Mungu atazikubali. Wasiwasi wao usingekuwa kujua jinsi wanavyoweza kuwaelimisha watoto wao ili wapate sifa na kuheshimiwa na ulimwengu, bali jinsi wanavyoweza kuwaelimisha kuunda tabia nzuri ambayo Mungu anaweza kuikubali. {FEsw 30.1}

Kujifunza sana na maombi ya dhati na bidii kwa ajili ya hekima ya kimbangu vinahitajika ili kujua jinsi ya kushughulika na akili za vijana; kwani wengi hutegemea sana mwelekeo ambao wazazi hutoa kwa akili na nia za watoto wao. Kuwianisha akili zao katika mwelekeo sahihi na wakati sahihi, ni kazi muhimu zaidi; kwa maana hatima yao ya milele inaweza kutegemea juu ya maamuzi yaliyofanywa wakati fulani wa dharura/nyeti. Ni muhimu kiasi gani, basi, fikira za wazazi ziwe huru kadiri iwezekanavyo na mifadhaiko/mahangaiko; kuelemea mawazo katika mambo yapitayo, ili waweze kufikiri na kutenda kwa tafakuri ya utulivu, hekima, na upendo, na kufanya wokovu wa Roho za watoto wao kuwa jambo la kwanza kabisa! Kitu kikubwa ambacho wazazi wanapaswa kutafuta kufikia kwa watoto wao wapendwa kinapaswa kiwe pambo la ndani. Wazazi hawawezi kuruhusu wageni na watu wanaowatembelea kudai umakini wao, na kwa kuwapora muda, ambao ni mtaji mkubwa wa maisha, na hivyo kufanya iwe vigumu kwao kutoa kwa watoto wao kila siku mafundisho ya subira ambayo ni lazima wanapaswa kutoa kwa mwelekeo sahihi wa akili zao zinazokua. {FEsw 30.2}

Muda wa maisha ya mwandamu duniani mfupi sana kuweza kutapanywa kwa vitu vya ubatili, na mambo madogo na hata kuacha njia sahihi, kama kutembelea watu kusiko na faida yaani katika uzururaji usiofaa na kwa kujiingiza katika mambo yasiyo na maana, katika mavazi yasiyo ya lazima ili kujionesha; au katika burudani za kuisimua. Hatuwezi kumudu kudumu katika kuupoteza muda tuliopewa na Mungu ili tuwabariki wengine, na ambao ndani yake tunajiwekea hazina sisi wenyewe Mbinguni. Hatuna muda mwingi sana kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu muhimu. Tunapaswa kutoa muda kwa utamaduni wa mioyo na akili zetu wenyewe, ili tuwe wa kustahili kazi yetu ya maisha. Kwa kupuuza majukumu haya muhimu, na kupelekana na tabia na desturi za mitindo, miunganiko ya kiulimwengu, tunajifanyia sisi na watoto wetu kosa kubwa. {FEsw 31.1}

Akina mama ambao wana akili za ujana za kufundisha majumbani mwao, na kuunda tabia za watoto, hawapaswi kutafuta msisimko wa ulimwengu ili kuwa na

raha na uchangamfu. Wao Wana kazi muhimu ya maisha, na hawawezi kumudu kutumia muda katika namna isiyo na faida. Muda ni moja ya talanta muhimu ambayo Mungu ametukabidhi, na kwa ajili yake ataitua sisi kutoa hesabu. Kupoteza muda ni kupoteza akili. Nguvu za akili zina uwezo wa kukuzwa kwa ubora wa hali ya juu sana. Ni wajibu wa akina mama kukuza akili zao, na kutunza mioyo yao iwe safi. Wanapaswa kuboresha kila namna ndani ya uwezo wao wenyewe kwa ajili ya uboreshaji wa kiakili na kimaadili, ili wao waweze kustahili kuboresha akili za watoto wao. Wale ambao huendekeza tabia yao ya kuchangamana na wengine mara zote, hivi punde watajisikia kutotulia (wahaka) isipokuwa wanatembelea watu mahali fulani au wanawaburudisha wageni majumbani mwao. Hawa hawana nguvu ya kukabiliana au kuendana na mazingira. Majukumu ya lazima, na yale matakatifu ya nyumbani yataonekana kuwa ya kawaida na yasiyopendeza kwao. Hawapendezwi na kujichunguza au kuinidhamisha nafsi. Akili ina njaa kwa ajili ya matukio mbalimbali yenye kuisimua ya maisha ya kidunia; watoto wanatelekezwa/ wanapuuzwa kwa ajili ya kufurahisha nafsi; na malaika anayeandika kumbukumbu huandika, "Watumishi wasio na faida." Mungu hupanga kwamba akili zetu zisiwe bila makusudi, bali zinapaswa kutimiza mema katika maisha haya. {FEsw 31.2}

Lau wazazi wangehisi kuwa ni jukumu lao zito waliloamuriwa na Mungu kuwaelimisha watoto wao kwa manufaa katika maisha haya; kama wao wangepamba hekalu la ndani la Roho za wana na binti zao kwa maisha ya kutokufa, tungeona mabadiliko makubwa katika jamii yaliyo bora zaidi. Hakutakuwa, hivyo basi, na kutojali kukubwa katika kuishi maisha ya utauwa, na haingekuwa vigumu sana kuamsha hisia za maadili za watoto kuelewa madai ambayo Mungu anayo juu yao. Lakini wazazi wanakuwa wazembe zaidi na Zaidi katika elimu ya watoto wao katika matawi muhimu. Wazazi wengi huwaruhusu watoto wao kujenga mazoea mabaya na kufuata mielekeo yao wenyewe, na kushindwa kuweka kwenye akili zao hatari ya wao kufanya hivi, na ulazima wa wao kutawaliwa na kanuni. {FEsw 32.1}

Watoto mara nyingi huanza kipande cha kazi kwa shauku, lakini, wakifadhaishwa au kuchoshwa nayo, wanatamani kubadilisha na kuanza kitu kipya. Kwa hivyo wanaweza kushika vitu kadhaa, na kisha kukutana na kuvunjika moyo kudogo, na kukata tamaa; na hivyo hupita kutoka kitu kimoja hadi kingine, bila kukamilisha au kuboresha chochote. Wazazi wanapaswa wasiruhusu upendo wa mabadiliko kuwatawala watoto wao. Wanapaswa wasijishughulishe sana na mambo mengine hata wakawa hawana muda wa kunidhamisha kwa subira akili zinazokua. Maneno machache ya kutia-moyo, au msaada kidogo kwa wakati ufaao, huweza kuwabeba juu ya shida zao na kuvunjika moyo, na kuridhika watakokupata kutokana na kuona kazi iliyokamilika waliyoifanya, itawachochea kwa kuwa na msukumo wa bidii zaidi. {FEsw 32.2}

Watoto wengi, kwa kukosa maneno ya kutia moyo, na msaada kidogo katika

juhudi zao, hukata tamaa, na kubadilika kutoka kwa jambo moja hadi lingine. Na wanabeba kasoro hii ya kusikitisha pamoja nao katika maisha ya utu uzima (ukomavu). Wanashindwa kufanikiwa kwa chochote wanachojihusisha nacho, kwani hawajafundishwa kustahimili chini ya hali zenye kukatisha tamaa. Kwa hivyo maisha yote ya wengi yanathibitisha kutofaulu, kwa sababu hawakufanywa kuwa na nidhamu sahihi wakati wakiwa wadogo. Elimu iliyopokelewa kipindi cha utoto na ujanani, huathiri kazi yao yote ya uzalishaji katika maisha ya ukomavu, na uzoefu wao wa kidini una alama inayoendana na hilo. {FEsw 32.3}

Kazi ya Kimwili kwa Wanafunzi {kazi za mikono}

Kwa mpango wa sasa wa elimu, mlango wa majaribu/vishawishi umefunguliwa kwa vijana. Ingawa kwa ujumla wana masaa mengi sana ya masomo, wana masaa mengi bila kuwa na chochote cha kufanya. Masaa haya ya kustarehe bila kufanya lolote hutumiwa mara kwa mara kwa njia ya uzembe. Uelewa wa tabia mbaya husambaa kutoka kwa kijana au mtu mmoja hadi mwingine, na ubatili huongezeka kwa kiwango kikubwa. Vijana wengi sana ambao wamefundishwa mambo ya kiroho nyumbani, na ambao huenda shuleni wakiwa hawana uovu au hatia moyoni, na ni wema kwa ujumla kwa kulinganisha, huwa mafisadi kwa kushirikiana na makundi ya waovu. Wanapoteza kujiheshimu wenyewe, na kuziacha kanuni bora. Kisha wanakuwa tayari kufuata njia ya kuelekea chini kuzimu; kwa kuwa wamezitumia vibaya sana dhamiri zao hivi kwamba dhambi haionekani kuwa ya kutisha sana kwao. Maovu haya, ambayo yapo katika shule zinazoendeshwa kulingana na mpango uliopo sasa, unaweza kurekebishwa na kuboreshwa kwa kiwango kikubwa ikiwa masomo na kazi vinaweza kuunganishwa. Maovu kama haya yapo katika shule za upili/sekondari, kwa kiwango kikubwa tu; kwani vijana wengi wamejielimisha katika maovu, na dhamiri zao zimeungua moto. {FEsw 33.1}

Wazazi wengi hutia chumvi sana uimara na sifa nzuri za watoto wao. Hawaonekani kuzingatia kwamba wataingizwa katika mivuto ya udanganyifu ya vijana waovu. Wazazi wana hofu wanapowapeleka watoto wao shule za mbali, lakini wanajidanganya wenyewe kwamba kwa vile wamekuwa na mifano mizuri na mafundisho ya kidini, watakuwa wakweli kulingana na kanuni katika maisha yao ya shule ya upili. Wazazi wengi wana mawazo hafifu ni kwa kiwango gani uasherati au uovu wa ngono upo katika hizi taasisi za elimu. Mara nyingi wazazi wamefanya kazi ngumu na kuteseka kwa ufukara kwa ajili ya kuthamini kuwa watoto wao wapate kumaliza elimu. Na baada ya juhudi zao zote, wengi wana uzoefu mchungu wa kupokea watoto wao kutoka katika masomo yao wakiwa wenye tabia potofu na afya iliyoharibikiwa sana. Na mara nyingi hawana heshima kwa wazazi wao, na ni wasio na shukrani, na wasio watakatifu. Wazazi hawa walionyanyasika, ambao hutuzwa na watoto wasio na shukrani, wanaomboleza kwamba waliwatuma watoto wao kutoka kwao, ili wajiingize kwenye majaribu, na kurudi kwao wakiwa na uharibifu wa kimwili, kiakili, na kimaadili. Kwa matumaini yaliyovunjika na mioyo

iliyo karibu kuvunjika, wanaona watoto wao, ambao walikuwa na matumaini makubwa kwao, wakiufuata mwenendo mbaya na kuwa na maisha duni na ya huzuni. {FEsw 33.2}

Lakini kuna wale walio na kanuni thabiti, ambao hujibu matarajio ya wazazi na walimu. Wanapitia masomo ya shule kwa dhamiri safi, na kutoka wakiwa na akili nzuri, na maadili yasiyotiwa madoa na ushawishi wenye ufisadi. Lakini idadi yao ni chache hakika. {FEsw 34.1}

Wanafunzi wengine huweka utu wao wote katika masomo yao, na kuelekeza akili zao kwenye lengo la kupata elimu. Wanafanyia kazi ubongo, lakini huruhusu nguvu za mwili zibaki bila kufanya kazi. Ubongo unashughulishwa kupita kipimo na kazi nyingi, na misuli inakuwa dhaifu kwa sababu haifanyiwi mazoezi. Wanafunzi hawa wanapohitimu, ni dhahiri kwamba wamepata elimu yao kwa gharama ya maisha. Wamesoma mchana na usiku, mwaka baada ya mwaka, wakinyumbulisha akili zao daima katika taaluma, wakati wanashindwa kufanya mazoezi ya kutosha na misuli yao. Wametoa vyote sadaka kwa ajili ya ujuzi wa sayansi, na hupita kuelekea kwenye makaburi yao. {FEsw 34.2}

Vijana wa kike mara nyingi hujitoa kusoma, kwa kupuuza matawi mengine ya elimu ambayo ni muhimu zaidi kwa maisha halisi ya vitendo kuliko kusoma vitabu. Na baada ya kupata elimu yao, mara nyingi huwa ni vilema maishani. Walipuuzia afya zao kwa kukaa sana ndani ya nyumba, wakajinyima hewa safi ya Mbinguni, na mwanga wa jua waliopewa na Mungu. Vijana hawa wa kike wangeweza kutoka shuleni wenye afya, kama wangechanganya masomo yao na kazi za nyumbani na mazoezi katika hewa ya wazi. {FEsw 34.3}

FEswAfya ni hazina kubwa mno. Ni mali ya thamani kubwa ambayo wanadamu waweza kuwa nayo. Utajiri, heshima, au elimu hununuliwa kwa gharama kubwa sana, ikiwa itakuwa kwa kupoteza nguvu ya afya. Hakuna mojawapo ya mafanikio haya inaweza kuleta furaha, ikiwa afya haipo au imepungua. Ni dhambi mbaya kutumia vibaya afya ambayo Mungu ametupa; kwani kila matumizi mabaya ya afya hudhoofisha maisha yetu, na kutufanya tupoteze sana, hata ikiwa tutapata elimu ya kiwango chochote cha juu, hiyo ni hasara tu. (haijalishi tumepata elimu ya kiwango cha juu kiasi gani). {FEsw 35.1}

Katika visa vingi wazazi ambao ni matajiri hawahisi umuhimu wa kuwapa watoto wao elimu ya majukumu ya uhalisia na kiutendaji ya maisha kama vile ilivyo katika kuwapa ya sayansi. Hawaoni ulazima, kwa wema wa akili na maadili ya watoto wao, na kwa manufaa yao ya baadaye, ya kuwapa ufahamu kamili wa kazi yenye manufaa. Kuwafundisha hili watoto wao ni deni linalopaswa kutimizwa, kwamba, kama bahati mbaya ingekuja, wangeweza kusimama na kujitegemea vyema, wakijua jinsi ya kutumia mikono yao. Ikiwa wanao mtaji wa nguvu, hawawezi kuwa maskini, hata kama hawana senti au ndururu. Wengi ambao katika ujana walikuwa

katika hali ya kujiwezea kimaisha, au kuwa na mali, wanaweza kunyang'anywa mali zao zote, na kuachwa na wazazi na ndugu na dada wanaowategemea kwa riziki. Basi ni muhimu kwa kiasi gani kwamba kila kijana aelimishwe kufanya kazi, ili awe tayari kwa dharura yoyote! Hakika mali ni laana wakati walio nayo wanapoiruhusu isimame katika mahali pa wana na binti zao kupata ujuzi wa kazi yenye manufaa, ili waweze kufaa kwa maisha halisi ya kiutendaji. {FEsw 35.2}

Wale ambao hawajalazimishwa kufanya kazi au (maisha hayajawalazimisha kufanya kazi) mara nyingi hawana mazoezi ya kutosha kwa afya ya mwili. Vijana wa kiume, ambao akili na mikono yao haijijhusishi katika kazi, huwa na tabia za uvivu/ugoigoi, na mara kwa mara hupata kile ambacho ni cha kuogopwa zaidi, elimu ya mtaani, kukaa pembezoni mwa maduka, kuvuta sigara, kunywa pombe, na kucheza kamari. {FEsw 35.3}

Vijana wa kike watasoma riwaya, wakitoa udhuru wa kutofanya kazi kwa sababu wana afya dhaifu. Unyonge wao wa kiafya ni matokeo ya ukosefu wa mazoezi ya misuli ambayo Mungu amewapa. Wanaweza kufikiria kuwa ni dhaifu sana kufanya kazi za nyumbani, lakini watafanya kazi za kutarizi, nakshi na kufuma, na kuhifadhi kupauka kwa mikono na nyuso zao huku mama zao wakilemewa na kazi ngumu ya kufua na kupiga pasi nguo zao (watu wenye ngozi nyeupe wasio na afya kwa vile damu haitembei vizuri wanakuwa hawana rangi ya afya kwenye ngozi yao, ambayo ni pink. Wanakuwa na weupe usio na afya (pale), watu wasio na mazoezi nao hupata rangi hii). Wasichana hawa si Wakristo, kwa maana huvunja amri ya tano. Hawaheshimu wazazi wao. Lakini mama yao ndiye wa kulaumiwa zaidi. Amewadekesha/ameweadekeza mabinti zake na kuwatolea udhuru ili wasibebe sehemu yao ya majukumu ya nyumbani, mpaka kazi imekuwa na ladha mbaya kwao, nao wanapenda na kufurahia kukaa kivivu bila kazi (wanakuwa laini laini). Wanakula, na kulala, na kusoma riwaya, wakati wanazungumzia juu ya mitindo, na huku maisha yao hayana maana au manufaa yoyote. {FEsw 35.4}

Umaskini, katika kesi nyingi, ni mbaraka; kwani huzuia vijana na watoto kuharibiwa kutokana na kutojishughulisha. Nguvu za kimwili na vile vile nguvu za kiakili zinapaswa kutumiwa na kukuzwa ipasavyo. Huduma ya kwanza na ya kudumu ya wazazi inapaswa kuwa ni kuona watoto wao wakiwa na afya thabiti, ili waweze kuwa wanaume na wanawake wema, wenye busara, raia wema hapa duniani na Mbinguni na wenye uwiano. Haiwezekani kufikia lengo hili bila mazoezi ya kimwili. Kwa afya zao wenyewe za kimwili na maadili mema, watoto wanapaswa kufundishwa kufanya kazi, hata kama siyo masikini (yaani familia haina shida ya fedha). Kama wangekuwa na tabia safi na njema, lazima wawe na nidhamu ya kazi iliyoratibiwa vyema, ambayo italetwa mwili wote kuwa katika mazoezi ya misuli. Kuridhika moyo ambako watoto hawa watakuwa nako kwa kutumika, na katika kujinyima ili kusaidia wengine, kutakuwa raha ya afya zaidi watakayowahi kuifurahia. Kwa nini basi watu matajiri wajiibie wenyewe na watoto wao wapendwa

baraka hii kuu? {FEsw 36.1}

Wazazi, kutokujishughulisha ni laana kuu iliyowahi kuwaangukia vijana. Binti zenu hawapaswi kuruhusiwa kujigaragaza vitandani mwao saa za asubuhi na kuyaangamiza masaa ya thamani (saa moja na kuendelea! Walale mapema, kama saa tatu waamke mapema na kujishughulisha, RYU yasema kulala kabla ya saa tatu na nusu usiku ndiyo bora kwa afya! Masaa nane mpaka tisa yanatosha kwa vijana), kulala huondoa masaa ya thamani waliyoazimwa na Mungu kutumika kwa ajili ya kusudi bora zaidi, na ambayo kwa hayo watalazimika kutoa hesabu Kwake. Mama huwadhuru binti zake kwa kubeba mizigo ambayo wanapaswa kushirikiana naye kwa manufaa yao ya sasa na ya baadaye. {FEsw 36.2}

Njia ambayo wazazi wengi hufuata katika kuwaruhusu watoto wao wawe wavivu, na kukidhi hamu yao ya kusoma riwaya za mapenzi (novels), haiwafai wao kwa maisha halisi. Usomaji wa riwaya na hadithi ndio uovu mkubwa zaidi ambao vijana wanaweza kuendelea, na kujifurahisha nao. Wasomaji wa riwaya na hadithi za mapenzi hushindwa kutengeneza akina mama bora wenye uhalisia wa maisha na wanaojishughulisha (mfano: *huota ndoto za mchana kwamba wataolewa na mtu mwenye mahaba mengi nao na pesa, nao wataishi raha mstarehe, wakupata kwamba hizo ni ndoto katika pambano kuu la maisha, wao huishi kwa huzuni wakiwalinganisha waume zao na mambo ya kufikirika nk*). Wao ni wajenzi wa ngome zinazoelea hewani, wanaoishi katika ulimwengu usio wa kweli, na wa kufikirika. Wanakuwa wa kihisia, na kuwa wagonjwa wa mapenzi/taharuki. Maisha yao ya bandia huwaharibu kwa lolote lililo lenye manufaa duniani hapa. Wao ni mbilikimo kiakili, japo wanaweza kujidanganya wenyewe kwamba wao ni bora kiakili na kwa adabu zao. Kufanya mazoezi kupitia kazi za nyumbani ni faida kubwa kwa wasichana wadogo. {FEsw 37.1}

Kazi za mikono hazitazuia ukuzaji au ustawi wa akili. Hilo la kuzuia ukuaji liko mbali sana, badala yake ni faida. Faida zinazopatikana kwa kazi ya kimwili/mikono humsawazisha mtu na kuleta uwiano, kwa kuzuia akili kufanya kazi kupita kiasi. Kazi ngumu itakuja juu ya misuli, na kuipa afueni akili iliyochoka. Kuna wasichana wengi walio goigoi, wasio na na faida/manufaa na ambao wanaona kuwa sio kuwa mdada kujihusisha katika kazi (work is not for ladies). Lakini tabia zao zipo wazi sana kuwalaghai watu wenye akili timamu na busara kuhusiana na kutokuwa na thamani yoyote. Wanajirahisisha kwa kulazimisha tabasamu za uongo na kujichekesha kipumbavu, kwa tabia na mazungumzo feki ili kuwavutia watu. {FEsw 37.2}.

Wanakuwa kama vile hawawezi kutamka maneno yao kwa usahihi na kwa usawa/uzuri, lakini wanaharibu-haribu maneno yote wanayozungumza kama vitoto vidogo kwa kithembe na kutabasamu kipumbavu kwa kejeli ili kuvutia watu. Je hawa ni wadada/wanawali kweli? Hawakuzaliwa wajinga, lakini walielimishwa/wamefundishwa hivyo. Haihitaji mtu dhaifu, mnyonge, mwenye

kuvaa kupita kiasi, na mwenye kuvutia watu kwa kicheko cha kipumbavu na kujirahisisha ili kuwa mdada/mwanamwali (lady). Uthabiti wa mwili au mwili wenye afya unahitajika ili kuwa na akili timamu yenye afya. Utimamu wa kimwili, na ujuzi wa kivitendo wa stadi zote muhimu za nyumbani, kamwe haviwezi kuwa kizuizi katika ukuzaji wa akili vyema; vyote viwili vina umuhimu wa juu kwa mdada/mwanamke (kuwa na akili pungufu au udhaifu wa mwili, hakumfanyi mwanamke awe mrembo au awe wa kuvutia watu). {FEsw 38.1}

Uwezo wote wa akili unapaswa kutumika na kuendelezwa, ili wanaume na wanawake wawe na akili zilizosawazika vizuri (zenye uwiano au balansi). Ulimwengu umejaa wanaume na wanawake wa mlengo mmoja (wameelemea upande mmoja), ambao wamekuwa hivyo kwa sababu sehemu moja ya uwezo wao ilikuzwa, wakati nyingine ikachwa mbilikimo au iliachwa kudumaa kutokana na kutoshughulishwa. Elimu ya vijana wengi imeshindwa, yaani imefeli. Wanasoma kupita kiasi, na wanapuuza yanayohusu maisha halisi ya shughuli za vitendo (practical). Wanaume na wanawake huwa wazazi bila kuziingatia wajibu wao, na watoto wao huzama chini zaidi yao, katika upungufu wa jamii ya ubinadamu kuliko wao wenyewe. Hivyo jamii ya ubinadamu huzorota kwa kasi. Kujishughulisha mara na kusoma au kujifunza, kama shule sasa zinavyoendesha, haziwaandai vijana kufaa kwa maisha halisi na shughuli zake. Akili ya mwanadamu itakuwa na utendaji. Na hivyo ikiwa haifanyi kazi katika mwelekeo sahihi, itakuwa na bidii katika ubaya/makosa. Ili kuhifadhi usawa wa akili, kazi na masomo viunganishwe mashuleni. {FEsw 37.3}

Mpango ulipaswa kufanywa katika vizazi vilivyopita kwa ajili ya elimu kwa kiwango kikubwa. Kuhusiana na mashule kunapaswa kuwe na uanzishaji wa taasisi za kilimo na viwanda vya kutengeneza bidhaa. Lazima pia kuwe na walimu wa kazi za nyumbani. Na sehemu ya muda kila siku inapaswa kutolewa kwa ajili kazi za mikono, ili kwamba nguvu za kimwili na za kiakili ziweze kutumika kwa usawa. Kama shule zingeanzishwa juu ya mpango tulioutaja, kusingekuwa na akili nyingi zisizo na usawa (hazina balansi/uwiano). {FESWsw 38.1}

Mungu aliwaandalia Adamu na Hawa bustani nzuri. Aliwapatia kila kitu ambacho walihitaji. Alipanda kwa ajili yao kila aina ya miti yenye kuzaa matunda. Kwa mkono Wake ulio na ukarimu aliwajazia fadhila Zake. Miti ya manufaa na uzuri, na maua ya kupendeza, ambayo yalieneza uzuri, na kustawi katika wingi wa utajiri karibu nao, hawakuweza kujua chochoteya cha kuoza. Adamu na Hawa walikuwa matajiri kwelikweli. Walimiliki Edeni. Adamu alikuwa bwana {mkubwa} katika milki yake nzuri. Hakuna anayeweza kuhoji ukweli kwamba alikuwa tajiri. Lakini Mungu alijua kwamba Adamu hangeweza kuwa na furaha isipokuwa ana kazi ya kufanya. Kwa hiyo akampa shughuli ya kufanya; nayo ilikuwa kuitunza bustani. {FEsw 38.2}

Ikiwa wanaume na wanawake wa kizazi hiki kibaya wana kiasi kikubwa cha hazina ya dunia, basi imepwelea sana kwa kulinganisha na paradiso ile ya uzuri na

mali aliyopewa Adam, kwani ni duni sana, wanajihisi wenyewe kuwa kwamba wako juu ya kazi, (yaani kazi haina maana), na kisha huwaelimisha watoto wao kuitazama kazi kama ni jambo la kudhalilisha. Wazazi hao matajiri, kwa maagizo na mifano yao, huwafundisha Watoto wao kwamba pesa huwafanya wao kuwa mabwana na mabibi waungwana/waheshimiwa. Lakini wazo letu la bwana na bibi linapimwa kwa akili na thamani ya maadili mtu aliyo nayo. Mungu hutupimi sisi kwa mavazi. Maonyo ya mtume Petro aliyevuviwa ni, “Kujipamba kwenu kusiwe kujipamba kwa nje, yaani, kwa kusuka nywele; na kujitia dhahabu, na wa kuvalia mavazi; bali kuwe utu wa moyoni usioonekana, katika mapambo yasiyoharibika, yaani, Roho ya upole na utulivu, iliyo ya thamani kuu mbele za Mungu.” Mwenye Roho ya upole na ya utulivu ameinuliwa juu ya heshima au utajiri wa kidunia. {FEsw 38.3}

Bwana anaonyesha jinsi anavyowapima matajiri wa dunia hii, ambao huziinua nafsi zao katika ubatili kwa sababu ya mali zao za kidunia; kwa yule tajiri aliyebomoa ghala zake na kujenga kubwa zaidi, ili aweze kuwa na nafasi ya kujiwekea bidhaa zake na kuzitukuza zaidi. Akiwa amemsahau Mungu, alishindwa kutambua mali zake zote zimetoka wapi. Hakuna shukurani zilizopanda juu kwa Mpaji wake Mkarimu. Alijipongeza mwenyewe akisema kwamba: “Nafsi yangu, una vitu vingi vyema ulivyojiwekea akiba kwa miaka mingi; pumzika basi, ule, unywe, ufurahi.” Bwana, ambaye alikuwa amemkirimia utajiri wa kidunia wa kuwabariki wanadamu wenzake na kumtukuza Muumba wake, kwa haki alimkasirikia kwa kukosa shukurani kwake, na akasema, “Mpumbavu wewe, usiku huu wa leo wanataka Roho yako! Na vitu ulivyojiwekea tayari vitakuwa vya nani? Ndivyo alivyo mtu ajiwekeaye nafsi yake akiba, asijitajirishe kwa Mungu.” Hapa tuna kielelezo jinsi Mungu asiye na mwisho anavyompima mwanadamu. Kuwa na bahati kubwa, au kiwango chochote cha mali, haikupi wewe upendeleo wa Mungu. Fadhila zote hizi na baraka hutoka Kwake, kuthibitisha, kupima, kutahini na kuendeleza tabia ya mwanadamu. {FEsw 39.1}

Watu wanaweza kuwa na utajiri usio na mipaka; lakini kama wao si matajiri kuelekea kwa Mungu, na ikiwa hawana nia ya kujiwekea hazina ya Mbinguni na hekima ya kimbingu, wanahesabiwa kuwa wapumbavu na Muumba wao, nasi tunawaacha pale tu Mungu alipowaacha. Kazi ni mbaraka. Haiwezekani kwetu kuifurahia afya bila kazi. Vitivo vyote vya mwanadamu vinapaswa kutumiwa ili viweze kuendelezwa ipasavyo, na ili wanaume na wanawake wawe na akili zenye usawa/balansi. Ikiwa vijana wangelipewa elimu ya kina katika aina mbalimbali za kazi, kama wangefundishwa kazi pamoja na sayansi, elimu yao ingekuwa na manufaa makubwa zaidi kwao. {FEsw 39.2}

Kuushughulisha sana ubongo wakati misuli haifanyi kazi, hudhoofisha neva, na wanafunzi huwa na shauku isiyoweza kudhibitiwa ya mabadiliko na maburudisho ya kuisisimua. Na wanapoachiliwa, baada ya kufungiwa kwenye masomo kwa

masaa kadhaa kila siku, hukaribia kuwa kama wanyama wa porini (wanafyatuka). Wengi hawajawahi kudhibitiwa nyumbani. Wameachwa kufuata mielekeo yao, na wanadhani kuwa kuzuiliwa wakae ndani ili wasome ni mzigo mzito juu yao; na jambo la kutokuwa na chochote cha kufanya baada ya saa za masomo, linamfanya Shetani apendekeze michezo na matendo yenye uovu kama badiliko kutoka kukaa darasani. Ushawishi wao juu ya wanafunzi wengine unamomonyoa maadili. Wale wanafunzi ambao wamekuwa na mafundisho ya manufaa ya kidini/kiroho nyumbani, na ambao hawajui maovu ya jamii, mara kwa mara hushikamana zaidi na wale ambao akili zao zimetupwa katika ukungu duni, na ambao faida za mazoea ya kiakili na mafunzo ya kidini yamekuwa machache sana. Na wako katika hatari, kwa kuchanganyika katika jamii ya tabaka hili, na kwa kuvuta angahewa hiyo isiyoinua, bali inayoelekea kushusha na kuporomoa maadili, na kuzama kwa kiwango cha chini sawa na wenzao wanaochangamana nao. Ni furaha ya tabaka kubwa la wanafunzi, katika saa zao za kukosa kazi, kuwa na wakati wa kufurahi (fun au high time kingereza). Na wengi sana wa wale waliotoka majumbani mwao bila hatia na wakiwa na usafi wa moyo, huchafuliwa na makundi ya wenzao shuleni.

{FEsw 40.1}

Nimeongozwa kuuliza, Je, lazima yote ambayo ni ya thamani kwa vijana wetu yatolewe dhabihu ili wapate elimu ya shule? Ikiwa kungeekuwapo na uanishwaji wa kilimo na viwanda vilivyounganishwa na shule zetu, na kukawa na walimu waliobobea, nao wakaajiriwa ili kuwaelimisha vijana katika nyanja mbalimbali za masomo na kazi, kwa kujitolea sehemu ya kila siku kwa kukuza akili, na sehemu ya kazi za kimwili/mikono, sasa kungekuwa na kundi la juu zaidi la vijana linalokuja siku za mbeleni katika shughuli na kuwa na ushawishi katika kujenga jamii. Wengi wa vijana ambao wangehitimu katika taasisi hizo wangetoka wakiwa na uimara wa tabia. Wangekuwa na Subira wakati wa maumivu, na ujasiri wa kushinda vikwazo, na kanuni kama hizo kiasi kwamba wasingeyumbishwa na ushawishi mbaya, hata ushawishi huo uwe unapendwa na wengi. Kulipaswa kuwa na walimu wenye uzoefu wa kuwapa masomo vijana wa kike mambo ya upishi. Wasichana wadogo wanapaswa kufundishwa kutengeneza vitambaa vya kushona mavazi ya kuvaa, kuvikata, kutengeneza nguo, na kurekebisha nguo, na hivyo kuwa na elimu kwa ajili ya kazi za kiutendaji ya maisha (kazi halisia za maisha). {FEsw 40.2}

Kwa vijana wa kiume, kunapaswa kuwa na vituo ambapo wanaweza kujifunza stadi mbalimbali, ambayo ingeshughulisha misuli yao pamoja na nguvu zao za kiakili. Ikiwa kwamba vijana watapatiwa elimu ya upande ya aina moja tu, jambo gani basi ambalo lina matunda mabaya zaidi, wachukue ujuzi wa sayansi, pamoja na hasara zake zote kwa afya na maisha, au wachukue ujuzi wa kazi za vitendo? Tunajibu bila kusita, lile la mwisho yaani kama imetokea kwamba wachukue moja tu kati ya haya basi wachukue ujuzi wa kazi za vitendo na kuacha lile la kwanza. Hiyo ni Ikiwa moja lazima lipuuzwe, basi iwe ni kusoma vitabu na siyo kazi za mikono (mara nyingi tuna uchaguzi wa fani zote mbili, ila kazi ya Mikono, ndiyo iwe

na kipaumbele toka utotoni, na kisha vitabu maana itamfanya mtoto amudu maisha yake ya kila siku). {FEsw 41.1}

Kuna wasichana wengi sana ambao wameolewa na wana familia, ambao wana ufahamu mdogo wa kiutendaji wa majukumu yanayohusisha kuwa mke na mama. Wanaweza kusoma, na kucheza vyombo vya muziki (ala); lakini hawawezi kupika. Hawawezi kutengeneza mkate mzuri (ugali)*, ambayo ni muhimu sana kwa afya ya familia. Hawawezi kukata na kutengeneza mavazi, kwa maana hawakujifunza yanatengenezwaje. Walyaona mambo haya kuwa yasiyo ya muhimu, na katika maisha yao ya ndoa wanategemea wengine kuwafanyia mambo haya kama watoto wao wadogo. Ni kwa ujinga huu usio na udhuru kuhusiana na shughuli/stadi zinazohitajika sana maishani, ndizo ambazo zimefanya familia nyingi kutokuwa na furaha. {FEsw 41.2}

*(kupika nafaka vizuri, kwetu itakuwa ugali na nafaka zisizokobolewa, kama mchele wa kahawia si mweupe na nafaka zingine). Hisia kwamba kazi inadhalilisha maisha ya mitindo/fasheni Imewaweka maelfu kaburini ambao wangeweza kuishi. Wale wanaofanya kazi ya mikono tu, mara kwa mara hufanya kazi kupita kiasi bila kuwa na muda wa kupumzika; huku kundi la wasomi linatumikisha ubongo kupita kiasi, na kuteseka kwa kukosa afua na nguvu za mwili ambazo kazi za mikono humletea mtu. Ikiwa wale wanaotumia ubongo wangeshiriki mzigo wa tabaka la wafanyakazi wanaotumia nguvu za mwili kwa kiasi fulani, na hivyo kuimarisha misuli, basi wale wanaotumika kwa kazi za mikono wangeweza kufanya kazi pungufu kidogo, na kutoa sehemu ya muda wao kwa utamaduni wa akili na ukuaji wa maadili. Wale walio na mazoea ya kukaa na kusoma wanapaswa kuchukua kazi za kimwili/mikono, hata kama hawana haja ya kufanya kazi kwa sababu hali yao ya kifedha iko sawa. Afya inapaswa kuwa kichocheo tosha, cha kuwaongoza kuunganisha kazi za kimwili na za kiakili. {FEsw 41.3}

Utamaduni wa kimaadili, kiakili, na wa kimwili unapaswa kuunganishwa ili kuwa na wanaume na wanawake waliokuzwa vizuri, na wenye usawa. Baadhi wana sifa ya kutumia nguvu kubwa ya kiakili kuliko wengine, huku wengine wakiwa na mwelekeo wa kupenda na kufurahia kazi za kimwili. Makundi haya yote mawili yatafute kuboresha pale yanapopungukiwa, hivyo wanaweza kumtolea Mungu dhabihu yenye maana nafsi yote ikiwa kamili, dhabihu iliyo hai, takatifu na inayokubalika Kwake, ambayo ndiyo dhabihu na huduma yao yenye maana. Mazoea na desturi za jamii ya mitindo haipaswi kupima mwendo wao wa kiutendaji. Mtume Paulo aliyevuviwa anaongeza, “Wala msifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu.” {FEsw 42.1}

Bongo za wanaume wanaofikiria zinatatumikishwa sana. Wanatumia mara kwa mara nguvu zao za kiakili kwa upotevu; wakati kuna kundi lingine ambalo Lengo lao kuu la maisha ni kazi ya kimwili. Kundi hili la pili halishughulishi akili. Misuli yao

inatumika, huku akili zao zinaporwa nguvu za kiakili; kama vile akili za watu wenye kufikiri zinavyofanya kazi, huku miili yao ikinyimwa nguvu kwa kupuuza kwao kufanya mazoezi ya misuli. Wale ambao wako radhi kujitolea maisha yao kwa kazi ya kimwili, na kuwaacha wengine wawe wanafikiri kwa ajili yao (kwa niaba yao), wakati wanatekeleza yale ambayo akili za wengine zimepanga bila ya kutumia akili zao wenyewe, watakuwa na nguvu ya misuli, lakini akili dhaifu. Ushawishi wao kwa wema ni mdogo kulinganisha na ambavyo ingekuwa kama wangetumia akili zao pamoja na misuli yao. Kundi hili huanguka kwa urahisi zaidi likishambuliwa na ugonjwa, kwa sababu mfumo unapewa nishati na nguvu ya umeme ya ubongo kudhibiti na kuyapinga magonjwa. {FEsw 42.2}

Wanaume ambao wana nguvu nzuri za kimwili wanapaswa kujielimisha kufikiri na kutenda, na kutotegemea wengine kuwa akili yao. Ni kosa maarufu na linalopendwa na kundi kubwa kuchukulia kazi kama jambo la kudhalilisha. Kwa hiyo vijana wanahangaika sana kujielimisha kuwa walimu, makarani, wafanyabiashara, wanasheria, na kuwa na nafasi yoyote ambayo haihitaji kazi ya kimwili/mikono. Wasichana huchukulia kazi za nyumbani kuwa za kudhalilisha. Na ingawa mazoezi ya mwili yanahitajika kufanya kazi ya nyumbani, ikiwa sio makali sana, husaidia katika kukuza afya, ila wao watatafuta elimu ambayo itawafaa kuwa walimu au makarani, au watajifunza kazi fulani ambayo itawafungia ndani kwenye ajira ya kukaa tu. Mashavu yao yanaonyesha kutonawiri, na kukosa afya (rangi ya ngozi inapauka na kuonyesha damu haitembei vizuri-'pale'), na maradhi yanawashika; kwa sababu wameunyang'anya mwili mazoezi, na tabia zao kwa ujumla hupotoshwa. Yote haya ni kwa sababu ni ya mtindo! Wanafurahia maisha ya urembo na laini, ambayo ni unyonge na ya kuoza. {FEsw 43.1}

Ni kweli, kuna kisingizio kwa wasichana kutochagua kazi za nyumbani kuwa ajira yao, kwa sababu wale wanaojiri wasichana wa jikoni kwa ujumla. huwatendea kama watumwa. Mara nyingi waajiri wao hawawaheshimu, na kuwachukulia kana kwamba hawakustahili kuwa washirika wa familia zao. Hawawapi upendeleo kama wanaowapa washonaji, katibu muhtasi, na mwalimu wa muziki. Lakini hakuna ajira iliyo muhimu zaidi kuliko kazi ya nyumbani. Kupika vizuri, kuweka chakula chenye afya mezani kwa njia ya kuvutia mtu ale, inahitaji akili na uzoefu. Yule anayeandaa chakula cha kuwekwa ndani ya matumbo yetu, chakula ambacho kitageuzwa kuwa damu na kulisha mfumo wa mwili, anachukua nafasi muhimu zaidi na iliyoinuliwa. Nafasi ya karani/mnakili yule anayechema kwa mashine, mtengeneza mavazi, au mwalimu wa muziki haiwezi kufanana kwa umuhimu na nafasi ile ya mpishi. {FEsw 43.2}

Kinachoendelea ni taarifa ya kile ambacho kinaweza kufanywa na mfumo sahihi wa elimu. Muda ni mfupi sana sasa kutimiza yale ambayo yangeweza kufanyika katika vizazi vilivyopita; lakini tunaweza kufanya mengi, hata katika siku hizi za mwisho, kurekebisha maovu yaliyopo ndani elimu ya vijana. Na kwa sababu muda

ni mfupi, tunapaswa kuwa dhati na wenye bidii, na kufanya kazi kwa usongo/ari katika kuwapa vijana elimu hiyo ambayo inaendana na imani yetu. Sisi ni wanamatengenezo. Tunatamamani kwamba watoto wetu wasome kwa manufaa bora kabisa. Ili kufanya hili, kazi inapaswa iwape kile kitachohitaji misuli kuwa na mazoezi. Kila siku, kazi iliyopangwa kwa utaratibu inapaswa kujumuishwa kama sehemu ya elimu ya vijana, hata katika kipindi hiki cha mwisho. Mengi sasa yanaweza kufikiwa kwa kuunganisha kazi na shule. Kwa kufuata mpango huu, wanafunzi watatambua kunyumbulishwa kwa Roho na nguvu ya mawazo, na wataweza kukamilisha kazi nyingi za kiakili kwa wakati fulani kuliko ambayo wangeweza kwa kusoma peke yao. Na wanaweza kutoka shule bila ya miili yao kuharibiwa, na kwa nguvu na ujasiri wa kudumu kushika nafasi yoyote ambayo majaliwa ya Mungu yataweza kuwaweka. {FEsw 44.1}

Kwa sababu muda ni mfupi, tunapaswa kufanya kazi kwa uadilifu na kwa nguvu maradufu. Watoto wetu wanaweza kamwe wasiingie chuoni, lakini wanaweza kupata elimu katika matawi haya muhimu ambapo wanaweza kuigeuza elimu hiyo wanayoipata katika matumizi ya vitendo, na ambayo itatoa ukuaji wa akili, na kufanya nguvu zake kutumika. Vijana wengi sana ambao wamepitia kozi za chuo hawajapata elimu ya kweli na halisi ambayo wanaweza kuitumia kwa vitendo. Wanaweza kuwa na jina la kuwa na elimu ya chuo kikuu (wanaweza kujulikana wana shahada), lakini kwa kweli ni majinga yaliyoelimika tu (au wamesoma ila hawakuelimika). {FEsw 44.2}

Kuna vijana wengi ambao Mungu angekubali huduma zao, lau wangejiweka wakfu Kwake bila ya kusita au kujibakizabakiza. Ikiwa wangetumia nguvu hizo za akili katika utumishi wa Mungu ambazo sasa wanazitumia katika kujihudumia wenyewe na katika kupata mali, basi wangepanya kazi kwa dhati/unyofu, kwa ustahimilivu, kwa kufanikiwa katika shamba la mizabibu la Mungu. Wengi wa vijana wetu wanapaswa kuelekeza usikivu wao kwenye kusoma Maandiko, ili Mungu awatumie katika kazi Yake. Lakini hawana akili katika maarifa ya kiroho kama katika mambo ya kitambo; kwa hiyo wanashindwa kufanya kazi ya Mungu ambayo wangeweza kuifanya na kukubalika. Ni wachache tu waliopo kuwaonya wenye dhambi na kuleta Roho kwa Kristo, wakati kulipaswa kuwa na wengi. Vijana wetu kwa ujumla ni wenye hekima katika mambo ya kidunia, lakini si wenye akili kuhusu mambo ya ufalme wa Mungu. Wanaweza kugeuza akili zao katika njia ya kimbingu, njia ya Bwana, na kutembea katika Nuru, kuendelea kutoka kiwango kimoja cha Nuru na nguvu hadi nyingine, mpaka watapoweza kuwageuza wenye dhambi kwa Kristo, na kuwaelekeza wasioamini na waliokata tamaa katika njia yenye Nuru ielekeayo Mbinguni. Na vita vitakapokwisha, wapate kukaribishwa kwenye furaha ya Bwana wao. {FEsw 44.3}

Vijana hawapaswi kuingia katika kazi ya kueleza Maandiko na kufundisha juu ya unabii, wakati hawana ujuzi wa zile Kweli muhimu za Biblia wanazojaribu kuelezea

wengine. Wanaweza kuwa na mapungufu katika matawi ya elimu ya kawaida, na kwa hivyo kushindwa kufanya mema ambayo wangepanya endapo walipata faida za shule nzuri. Ujinga hautuongezei unyenyekevu au hali ya kiroho ya/kwa mtu yeyote anayedai kuwa mfuasi wa Kristo. Kweli za Neno la Mungu zinaweza kuthaminiwa na kupendwa vyema zaidi na Mkristo anayetumia ubongo wake vizuri. Kristo anaweza kutukuzwa vyema zaidi na wale wanaomtumikia kwa utashi wao. Lengo kuu la elimu ni kutuwezesha kutumia nguvu ambazo Mungu ametupatia kwa namna itakayowakilisha dini ya Biblia kwa ubora zaidi na kuendeleza Utukufu wa Mungu. {FEsw 45.1}

Tuna deni kwa Yeye aliyefanya sisi tuwepo (aliyefanya uwepo wetu, aliyetuumba), na kwa talanta zote ambazo zimekabidhiwa kwetu; na ni wajibu tunaowiwa na Muumba wetu katika kukuza na kuboresha talanta alizoziweka amana kwetu. Elimu itatia nidhamu akili na nia, itakuza nguvu zake, na kuzielekeza kwa ufahamu, ili tuweze kufaidika katika kupeleka mbele Utukufu wa Mungu. Tunahitaji shule ambayo wale ambao ndiyo wanaingia katika huduma wanaweza kufundishwa angalau matawi ya kawaida ya elimu, na ambapo wanaweza pia kujifunza kikamilifu zaidi Ukweli wa Neno la Mungu kwa wakati huu. Kuhusiana na shule hizi, mihadhara inapaswa kutolewa juu ya unabii. Wale ambao kweli wana uwezo mzuri kama vile Mungu atavyowakubali kufanya kazi katika shamba Lake la mizabibu, wangepaidika sana kwa maelekezo ya miezi michache tu ya shule kama hiyo. — *Shuhuda kwa Kanisa 3:131-160, 1872.* {FEsw 45.2}

Kwa marejeleo ya Ziada

Life of Christ {12 Articles}, The Youth's Instructor, March 1, 1872 to March 3, 1874, Dangers and Duties of Youth, Testimonies for the Church 3:221-227 {1872}, Appeal to the Youth, Idem., 362-380 {1875}.

Sura ya 2

KRISTO MWALIMU

Akili ya mwanadamu ina uwezo wa ukuaji wa juu zaidi (Yaweza kukuzwa). Maisha yaliyotolewa wakfu kwa Mungu sio maisha ya ujinga. Wengi wanazungumza dhidi ya elimu kwa sababu Yesu alichagua wavuvi wasio na elimu kuihubiri injili Yake. Wanadai kwamba Yeye alionyesha upendeleo kwa wasio na elimu. Watu wengi wasomi na wenye heshima waliyaamini mafundisho Yake. Kama hawa wangetii usadikisho wa dhamiri zao bila woga, hakika wangelimfuata. Uwezo wao ungekubaliwa, na wangetumika katika huduma ya Kristo, kama wangeutoa. Lakini hawakuwa na nguvu ya kimaadili kumkiri Kristo mbele ya makuhani waliokunja uso na watawala wenye wivu, na kuhatarisha hadhi yao wakiungana pamoja na Yule Mgalilaya mnyenyekevu. {FEsw 47.1}

Yeye anayeijua mioyo ya wote, alilielewa hili. Ikiwa wenye elimu na waungwana wasingefanya kazi waliyostahili kufanya, Kristo angechagua watu ambao wangekuwa watiifu na waaminifu katika kufanya mapenzi Yake. Aliwachagua watu wanyenyekevu na kuwaunganisha na Yeye Mwenyewe, ili aweze kuwaelimisha kuiendeleza kazi kubwa duniani wakati atakapoiacha. {FEsw 47.2}

Kristo alikuwa Nuru ya ulimwengu. Alikuwa chemchemi ya Maarifa yote. Alikuwa tayari kuwastahilisha wavuvi (kuwapa sifa) ambao hawajaelimika kupokea agizo kuu ambalo angewapa. Mafunzo ya Ukweli waliyopewa watu hawa wa hali ya chini yalikuwa ya maana kubwa. Walipaswa kuupindua ulimwengu. Ilionekana jambo rahisi kwa Yesu kuwaunganisha watu hawa wanyenyekevu na Yeye Mwenyewe; lakini lilikuwa tukio lenye tija ya matokeo makubwa. Maneno yao na matendo yao yalikuwa ya kuleta mapinduzi duniani. {FEsw 47.3}

Yesu hakuidharau elimu. Utamaduni wa juu wa akili (uelimishaji wa juu wa akili), ikiwa umetakaswa kwa njia ya upendo na hofu ya Mungu, hupokea ukubali Wake kamili. Watu waliochaguliwa na Kristo walikuwa pamoja Naye miaka mitatu, chini ya mvuto unaotakasa wa Mkuu wa Mbinguni. Kristo ni Mwalimu Mkuu kuliko wote ambao ulimwengu umewahi kujua. {FEsw 47.4}

Mungu atawakubali vijana kwa talanta zao, na utajiri wa mvuto wao, ikiwa watajiweka wakfu Kwake. Wanaweza kufikia kiwango cha juu zaidi cha ukuu wa kiakili; na ikiwa wamesawazishwa na kanuni za kidini/kiroho wanaweza kuendeleza kazi ambayo Kristo alikuja kutoka Mbinguni kuitimiza, na kwa kufanya hivyo wanakuwa watenda kazi pamoja na Bwana. {FEsw 48.1}

Wanafunzi katika Chuo chetu wana fursa za muhimu, sio tu ya kupata maarifa ya sayansi, lakini pia ya kujifunza jinsi kukuza na kutekeleza fadhila zitakazowapa ulinganifu wa tabia. Ni mawakala wanaowajibika wa maadili ya Mungu. Karama ya

mali, cheo, na akili hutolewa na Mungu kama amana kwa mwanadamu kwa uboreshaji kupitia busara yake. Amana hizi za aina mbalimbali, Yeye amezisambaza kwa kadiri ya uwezo unaojulikana wa waja Wake, kwa kila mmoja kazi yake. {FEsw 48.2}

Mpaji anatarajia mrejesho unaolingana na karama. Karama ya baraka inayoonekana nyenyekevu au ndogo, si ya kudharauliwa au kuachwa bila kutendewa kazi. Kijito kidogo hakiwezi kusema, sitatiririka kwenye mkondo wangu mwembamba kwa sababu mimi si mto mkubwa. Mabuu ya nyasi hayakatai kukua kwa sababu yenyewe sio msitu. Mshumaa haukatai kutoa mwanga wake mdogo kwa sababu sio nyota. Mwezi na nyota hazikatai kuangaza kwa sababu hazina mwanga mkali wa jua. Kila mtu anayo duru yake ya kipekee na shughuli yake ya maisha ambayo mwingine hana. Wale wanaotumia zaidi fursa walizopewa na Mungu watamrudishia Mpaji, katika uboreshaji wao, riba inayolingana na mtaji waliokabidhiwa. {FEsw 48.3}

Bwana hatoi thawabu kutokana na ukubwa wa kazi ilivyofanywa. Yeye hazingatii ukubwa wa kazi sawa na uadilifu ambao kazi hiyo ilifanywa nayo. Watumishi wema na waaminifu ndio hupewa thawabu. Kama tunakuza nguvu ambazo Mungu ametupa hapa duniani, tutaongezeka katika maarifa na utambuzi, na kuwezesha kufahamu thamani ya maisha ya umilele. Wale ambao wametumia vibaya fursa walizopewa na Mungu katika maisha haya, na wameridhika na ujinga wao, wakiruhusu akili zao kushughulishwa kabisa na mambo ya thamani ndogo kwao wenyewe au kwa wengine, hawa hawatatambua wajibu wao binafsi, na kushinda mielekeo miovu, na kuimarishwa kwa maisha ya juu yanayoleta hali ya usafi wa moyo, ubora wa juu na maisha matakatiifu zaidi. {FEsw 48.4}

Vijana wanapaswa kuwa wanafunzi kwa ulimwengu ujao. Ustahimilivu katika kupata maarifa, wakitawaliwa na hofu na upendo wa Mungu, kutawaongezea uwezo wa wema katika maisha haya, na wale ambao wametumia vyema fursa walizojaliwa kukifikia kilele cha mafanikio hapa, watachukua uwezo huu muhimu pamoja hadi katika maisha yajayo. Wametafuta na kupata kile kisichoweza kuharibika. Uwezo wa kuthamini Utukufu ambao “jicho halijapata Kuona, wala sikio kusikia,” utakuwa sawa na mafanikio yaliyofikiwa katika ukuzaji wa vitivo vyao katika maisha haya. {FEsw 49.1}

Wale ambao watakaoumimina nje ya mioyo yao ubatili na takataka kwa Neema ya Mungu wanaweza kutakasa nyua za nia, na kuzifanya hazina ya ujuzi, usafi na Ukweli. Na daima itakuwa ikifikia nje ya mipaka finyu ya mawazo ya kidunia, na kuingia katika ukuu wa Yule Asiye na ukomo. Haki na rehema za Mungu zitafunuliwa katika mitazamo ya maadili. Tabia ya huzuni ya dhambi, pamoja na matokeo yake, itatambulika. Tabia ya Mungu, upendo Wake uliodhihirishwa kwa kumtoa Mwanawe ili afe kwa ajili ya ulimwengu, na uzuri wa utakatifu, ni mada kutafakari zilizotukuka. Hizi zitaimarisha akili, na kumleta mtu katika ushirika wa

karibu na Yule Mmoja Asiye na ukomo. — *The Review and Herald, Juni 21, 1877.*
{FEsw 49.2}

Kwa rejea za Ziada

Signs of the Times, February 7, 1878

Signs of the Times, February 14, 1878

Battle Creek college.

WITO KWA WANAFUNZI WETU

Tumekuwa na hofu nyingi kwamba wanafunzi wanaohudhuria Chuo cha Battle Creek watashindwa kupokea faida zote wanazoweza, kwa njia ya utamaduni wa kidini, kutoka kwa familia zinazowapa vyumba vya kukaa. Familia zingine hazifurahii mvuto mzuri wa dini ya Kristo, ingawa wanajiita Wakristo. Ushawishi ambao tabaka hili la watu hushinikiza juu ya wanafunzi ni wa kuchukiza zaidi kuliko wale wasiojifanya kuwa watauwa. Watu hawa wasio na dini, wasiowajibika na wanaofuata desturi bila dini ya moyoni, wanaweza kujitokeza mbele ya ulimwengu kama majani ya mtini yanayodanganya, huku, kama mtini usiozaa, yakiwa yamepungukiwa kabisa na kile ambacho Mwokozi wetu ndicho Yeye anachokithamini peke yake, –matunda kwa Utukufu Wake. Kazi iliyofanywa moyoni kwa neema ya Mungu, wao hawajui chochote kuihusu. Watu hawa wana ushawishi wenye msukumo ambao ni hatari kwa wote wanaoshirikiana nao. Kunapaswa kuwe na kamati za kuona kwamba nyumba zinazotolewa kwa ajili ya wanafunzi si za watu wenye dini za mapokeo au desturi tu, zisiwe za wale ambao hawana mzigo kwa Roho za vijana wapendwa watakaoishi majumbani mwao. {FEsw 50.1}

Mengi sana yanaweza kufanywa kwa wale vijana ambao wamenyimwa, mvuto laini na wa kutiisha majumbani mwao. Roho inayodhihirishwa na huonyesha kwamba lugha ya moyoni inasema, Je “Mimi ni mlinzi wa ndugu yangu?” Sina mzigo wala wajibu kando na familia yangu mwenyewe. Sina mzigo maalum au maslahi kwa wanafunzi ambao wanaishi ndani ya vyumba nyumbani mwangu.” Ningewauliza hawa watu kama wana mizigo na kuhisi jukumu kwa watoto wao wenyewe. Ninaumia kuona wasiwasi kidogo kwa upande wa baadhi ya wazazi kwamba mivuto yote inayowazunguka watoto wao inapaswa kuwa mizuri kwa malezi ya tabia ya Kikristo; ila wale walio na mizigo ya nafsi za wapendwa wao wasiwekee mipaka maslahi hayo kwa ubinafsi kwa familia zao wenyewe. Yesu ni kielelezo chetu katika mambo yote; lakini hajatupa mfano wa ubinafsi au uchoyo kama unaodhihirishwa na wengi wanaodai kuwa wafuasi Wake. Tukikaa ndani ya Kristo, na upendo Wake ukakaa ndani yetu, tutawapenda wale ambao Kristo alikufa kwa ajili yao; kwa maana aliwaamuru wafuasi Wake kupendana kama Yeye alivyowapenda wao. Je, sisi tunaokiri Jina Lake tunatii agizo hili? Ikiwa tutashindwa katika jambo hii tutashindwa katika mengine pia. Ikiwa Kristo angezingatia faida Yake Mwenyewe, kuvaa Kwake na, na raha Yake, ulimwengu ungeachwa uangamie katika dhambi na ufisadi wake. {FEsw 50.2}

Kutojali kwa ajabu kuhusiana na wokovu wa Roho kunaonekana kumilikiwa na wengi wanaojiita Wakristo. Wenye dhambi wanaweza kuwa wanaangamia pande zote kuwazunguka, nao hawana mzigo maalum katika suala hili. Je, Kristo

atawaambia hawa wasiojali, “Vema, mtumwa mwema na mwaminifu, ingia katika furaha ya Bwana wako”? Furaha ya Kristo hujumuisha kuona Roho zikikombolewa kupitia kafara Yake aliyoifanya kwa ajili yao. {FEsw 51.1}

Vijana wa kiume na wa kike ambao hawako chini ya ushawishi wa nyumbani wanahitaji mtu wa kuwaangalia, na kudhihirisha kuwajali; na wanaofanya haya huenda wakasaidia mapungufu mengi, na kwa hakika hufanya kazi kwa ajili ya Mungu na wokovu wa Roho kama mhudumu katika mimbari. Kazi hii ya ukarimu usio na ubinafsi katika kufanya kazi na vijana ndiyo ile ambayo Mungu anaihitaji kutoka kwa kila mmoja wetu. Mkristo mwenye uzoefu anapaswa kufanya kazi kwa dhati na bidii ya kiasi gani ili kuzuia kukua kwa mazoea ambayo yanaharibu tabia, nayo yanakuwa magumu kufutika. Hebu wafuasi wa Kristo wafanye Neno la Mungu kuwa la kuvutia kwa vijana. Hebu tabia zenu wenyewe ziwe zilizolainishwa na kutiishwa na uzuri wa utakatifu, ziwe mahubiri ya kila siku, na ya kila saa kwa vijana. Usionyeshe Roho ya kunung'unika; bali wavute kwa utakatifu wa maisha na utii kwa Mungu. Baadhi ya maprofesa, kwa ugwadu wao kama ndimu, huwafukuza vijana. Mioyo ya vijana sasa ni kama nta au zege mbichi ambayo inaweka alama ya kudumu mtu akipita hapo, na unaweza kuwaongoza wapendezwe na tabia ya Kikristo; lakini katika miaka michache ijayo nta au simenti inaweza kuwa ngumu kama jiwe (na usifanye tofauti katika maisha yao). {FEsw 51.2}

Ninatoa wito kwa wale wanaojiita Wakristo wa Battle Creek kama kanisa, na kama mtu mmoja-mmoja, chukueni wajibu mliopewa na Mungu. Tembeeni na Mungu ninyi wenyewe; na kuwa na ushawishi wenye msukumo juu ya vijana ambao utawalinda dhidi ya kuanguka chini ya majaribu mengi na mbalimbali yaliyofanywa kuwavuta vijana wa kizazi hiki. Shetani huanza na wale wanaojiita watu wa Mungu. Wanaonekana wamelala kwa hatari za vijana, na uharibifu unaowatishia/unaowakabili. Shetani huonyesha kwa furaha ushindi wake alioupata juu ya vijana; na wale wanaodai kuwa askari wa msalaba wanamruhusu kuchukua wahanga wake kutoka chini ya juu ya dari, na kuonekana kupatana ajabu. {FEsw 51.3}

Kesi za wengi zinatazamwa kuwa hazina tumaini na wale ambao hawakunyoosha mkono wa kusaidia kuwaokoa. Baadhi ya hawa wangeweza kuwa wameokolewa; na hata sasa, ikiwa nia sahihi itadhihirika kwao, wangeweza kufikiwa. Ni nini kati yetu ambacho hatujakipokea? Sisi tu wadeni kwa Kristo kwa kila uwezo, na kila neema, kila wazo jema, na kila tendo linalofaa. Sisi wenyewe ndani yetu hatuna kitu cha kujigamba nacho. Kwa kujishusha na unyenyekevu, hebu na tuiname chini ya msalaba; na acheni maneno na matendo yetu yote yawe yale tu yatakayowaleta wengine kwa Kristo, na siyo kuwakimbiza mbali zaidi kutoka Kwake. {FEsw 52.1}

Ninawaagiza ninyi manoishi katika kituo kikuu cha kazi. Hamwezi kuwa wazembe, watu wa mapokeo yasiyo na kicho au hofu ya Mungu, mkijishughulikia

nafsi zenu wenyewe tu. Mashahidi wengi wanakutazama, na wengi wanafuata mwenendo wako. Maisha yako yasiyo ya kidini sio tu huweka muhuri hukumu yako mwenyewe, lakini huwaangamiza wengine pia. Ninyi mnaoishi mahali ambapo masilahi mazito kama hayo yanapaswa kuhifadhiwa, mnapaswa kuwa watu wenye utayari wakati wote, walinzi waaminifu, kamwe msisinzie. Nukta moja bila kuchukua tahadhari iliyotumiwa kwa kujiendekeza na anasa binafsi au katika kujifurahisha yaweza kumpa adui faida ambayo miaka ya kazi ngumu haiwezi kuiondoa. Wale wanaochagua Battle Creek kuwa makazi yao wanapaswa wawe wanaume na wanawake wenye imani na maombi, wakweli kwa mstakabali wa wale walio karibu nao. Hakuna usalama ila tu wanapotembea na Mungu. {FESw 52.2}

Kutakuwa na utofauti wa tabia miongoni mwa vijana watakaohudhuria Chuo cha Battle Creek. Wamefunzwa na kuelimishwa kwa aina tofauti tofauti. Wengi wameachwa kufuata mkunjo wa akili zao wenyewe zisizo na uzoefu. Wazazi wamefikiri kwamba wanawapenda watoto wao, lakini kumbe wamejidhihirisha kuwa adui zao wabaya zaidi. Wameuacha uovu uendeleo bila kuzuiwa. Wamewaruhusu watoto wao kutunza dhambi, ambayo ni kama kumfuga, kumlea, kumlinda na kumbembeleza nyoka, ambaye hatamuuma tu mwathirika anayemtunza huyo nyoka, bali wote ambao hushikamana naye. {FESw 52.3}

Baadhi ya watoto hawa wanaodekezwa ni miongoni mwa wanafunzi wanaohudhuria Chuo chetu. Walimu, na wote wana shauku na wanafunzi hawa wangewasaidia, wana kazi isiyotamanika au kufurahisha katika kutafuta kusaidia hili kundi la vijana 'wasiofugwa' (wasiolelewa) vyema au kutiishwa. Hawakuwatii wazazi wao nyumbani, na hawana wazo la kuwawatii wakuu shuleni au katika nyumba walimopanga. Ni Imani iliyoje, subira, neema, na hekima inahitajika ili kukabiliana na hawa vijana waliopuuzwa na kudekeshwa, na wa kuhurumiwa sana. Wazazi waliodanganywa wanaweza hata kusimama upande wa watoto na kupinga nidhamu ya shule na majumbani walimopanga. Wangewazuia wengine kutoka katika kutekeleza wajibu ambao Mungu anataka kutoka kwao, na ambao wao wamepuuzia kwa kiasi kikubwa. Ni hekima gani kutoka kwa Mungu inahitajika ili kutenda kwa haki na kupenda rehema chini ya hali hizi zenye kujaribu. Ni vigumu jinsi gani kusawazisha mwelekeo sahihi akili ambazo zimepotoshwa na huu usimamizi mbaya. Ingawa wengine wameachiwa huru kufanya wanavyotaka, wengine wamebanwa na kutawaliwa kupita kiasi; na wakati wanapokuwa mbali na mikono iliyo macho ambayo ilishikilia hatamu za udhibiti kwa ukali, ikiacha upendo na huruma nje, wamehisi kwamba hawataambiwa kitu au kuamriwa na yeyote. Wanadharau/wanachukia wazo la kuzuiwa au kuwekewa mipaka. {FESWsw 53.1}

Je, haiwapasi wale ambao wana kazi ngumu ya kuwaelimisha hawa vijana na kufinyanga tabia zao, wakumbukwe kwa maombi ya uaminifu ya watoto wa Mungu? Utunzaji, mizigo, na mahusiano mazito ya wajibu lazima yaanguke kwenye fungu la mwalimu ambaye dhamiri yake inafanya kazi vyema na mcha Mungu, na vilevile

kwa baba na mama waliobeba mizigo katika Israeli ambao wanaishi katika Battle Creek. Wakristo wote wanyoofu, wanaothamini nafsi ambazo Kristo alizifia, watajitahidi kwa dhati kufanya yote yaliyo ndani ya uwezo wao kurekebisha hata yale makosa yaliyopuuzwa na wazazi wao waliowazaa. Walimu watahisi kwamba wana jukumu lililokabidhiwa mabegani mwao la kuwawasilisha wanafunzi wao mbele ya ulimwengu na mbele za Mungu wakiwa na tabia zenye ulinganifu na akili zilizosawazishwa vyema. Lakini walimu hawawezi kubeba mzigo huu wote peke yao, na haipaswi kutarajiwa kwamba wao peke yao wanawajibika kwa tabia njema na maadili yaliyotukuka ya wanafunzi wao. Kila familia ambayo hutoa vyumba kwa ajili yao inapaswa kuwa na sheria ambazo lazima wazifuate. Itakuwa si kuwafanyia wao au wazazi wao wema kuwaruhusu kuunda tabia zisizo na sheria au mipaka na kuvunja au kuharibu samani/fanicha. Kama wana Roho za uchangamfu na nguvu nyingi zilizohifadhiwa mwilini za ujana, hebu basi na wafanye kwa nguvu kazi za mikono, mpaka uchovu uwaandame kukubali kupumzika vyumbani mwao. {FEsw

53.2}

Vyumba vya baadhi ya wanafunzi mwaka jana vilikuwa na kumbukumbu za tetesi mbaya. Ikiwa wanafunzi ni wakorofi au wajeuri, vyumba vyao mara nyingi huweka ukweli huu wazi. Michezo isiyo na kujali na ya ovyo, vicheko vya kelele, na kuwa macho saa za usiku wa manane havipaswi kuvumiliwa na wale wanaowakodishia vyumba. Ikiwa wanaruhusu tabia hizi kwa wanafunzi, wanafanya makosa makubwa, na kujifanya wenyewe, kwa kiwango kikubwa, kuwajibika kwa utovu huu wa nidhamu. Vyumba vya wanafunzi vinapaswa kutembelewa mara kwa mara, kuona kama vinafaa kwa afya na faraja, na kuhakikisha kama wote wanaishi kwa kufuata sheria za shule. Mapungufu yoyote yanapaswa kuweka wazi, na kwa uaminifu wanafunzi wanapaswa kufanyiwa kazi ili kuacha hivi vitabia. Ikiwa wao hawatatii na hawatadhibitiwa, basi ni bora warudi majumbani mwao, na ni bora shule iachane nao. Chuo chetu kisiharibike kwa ajili ya wanafunzi wachache wasiotii sheria. Vyuo vyetu katika nchi yetu ni mahali ambapo vijana wako katika hatari ya kuwa na maadili yenye uovu na upotofu kupitia ushirika huu mwovu.

{FEsw 54.1}

Mahusiano ya wanafunzi wetu ni jambo muhimu, na hayapaswi kupuuziwa. Wengi wanaokuja katika Chuo chetu ni wale wanaokiri kuwa Wakristo. Maslahi maalum yanapaswa kuonyeshwa katika hawa, na wanapaswa kutiwa moyo katika juhudi zao za kuishi maisha ya kikristo. Wanapaswa kulindwa kadiri inavyowezekana, kutokana na majaribu yanayowakuta vijana kwa njia yoyote wanayoweza kugeukia. Kwa wale ambao wamekuwa na uzoefu wa miaka mingi, majaribu ambayo yanawashinda vijana hawa yanaweza kuonekana kuwa mepesi na yasio na maana kiasi kwamba wataondoa huruma zao kutoka kwa wale wanaojaribiwa. Hili ni kosa. Maisha na uzoefu wao wenyewe wa awali unaweza kuwa ulikuwa wenye ubaya mkubwa zaidi kuliko ule wa vijana wanaowashutumu au kuwakosoa madhaifu yao {FEsw 54.2}

Wengi wanaodai kuwa wafuasi wa Kristo ni wadhaifu katika nguvu za maadili. Hawajawahi kuwa mashujaa wa msalaba, na wanavutiwa kirahisi kutoka katika utii wao kwa Mungu na anasa za ubinafsi, maburudisho au starehe. Watu hawa wanapaswa kusaidiwa. Hawapaswi kuachwa kupata nafasi katika kuchagua marafiki zao au wale ambao wataishi nao chumba kimoja (roommate). Wale wanaompenda na kumcha Mungu wanapaswa kubeba mzigo wa kesi hizi katika nafsi zao, na wanapaswa kusonga kwa busara katika kubadilisha wenzi au mahusiano yasiyofaa. Vijana Wakristo ambao wana mwelekeo wa kushawishiwa na washirika wasio na dini wanapaswa kuwa na ushirika na wale ambao watasaidia kuimarisha hatima nzuri na mielekeo ya kidini. Kijana mwenye mwenendo mzuri, mwenye mwelekeo wa kidini (mionjo ya kiroho), na hata anayekiri mambo ya kidini/kiroho, anaweza kupoteza mvuto wake wa kidini kwa kushirikiana na mtu ambaye huzungumza kwa wepesi juu ya mambo matakatifu na ya kidini, na hata kuyadhihaki, na ambaye hana kicho na dhamira yenye umakini. Chachu kidogo inaweza kuchachusha donge zima. Wengine ni dhaifu katika imani; lakini ikiwa wamewekwa na wenzi sahihi vyumbani mwao, wale ambao ushawishi una nguvu kwa ajili ya haki, wanaweza kusawazishwa katika mwelekeo ufao, na kupata uzoefu wa kidini/kiroho wenye thamani, na kufanikiwa katika kujennga tabia ya Kikristo. {FEsw 55.1}

Ningependa kwamba kaka na dada zetu wangechunga Roho kama wale wanaopaswa kutoa hesabu. Akili yangu imejizoeza kwa kina juu ya jambo hili. Napenda kuwasihi wale wanaomkiri Kristo, umuhimu wa kuzivaa silaha zote; na kufanya kazi kwa vijana wetu wanaohudhuria Chuo cha Battle Creek. Huenda wasihitaji mahubiri na mihadhara mirefu na kupigiwa marufuku kama wanavyohitaji upendo na umakini wa kweli kutoka kwenu. Hebu na wajue kwa matendo yako kwamba unawapenda na kuzijali nafsi zao. Ikiwa ungedhihirisha nusu ya kujali kwako mambo ya dunia na ya muda mfupi kwa vijana wachanga wanaokuja sasa Battle Creek, wale ambao wametupwa katika mikono ya kanisa, unaweza kuwafunga kwako kwa vifungo vikali vya huruma; na mvuto wako juu yao ungekuwa nguvu kwa ajili wema. — *The Review and Herald, FEswbruayi 21, 1878.*

{FEsw 55.2}

Kwa marejeleo ya Ziada

Joseph in Egypt, Signs of the Times, January 8, 1880-February 5, 1880

Cultivation of the Voice, The Review and Herald, February 5, 1880

Early Life and Call of Moses, Signs of the Times, February 4, 1880- March 4, 1880 Our College Test, Testimonies for the Church, 4: 418-429

College Students, Idem, 4: 430-437

Improvement of Talents, Idem, 4: 519-522

Warning and Admonition, Idem, 4: 537-544

Moral and Intellectual Culture, Idem, 4: 545-549

Influence of Associates, Idem, 4: 587-591

Simplicity in Dress, Idem, 4: 628-648

Proper Education, Idem, 4: 648-653

Literary Societies, The Review and Herald, January 4, 1881

Bible Study, The Review and Herald, January 11, 1881

The Life of Daniel, The Review and Herald, January 25, 1881-February 15, 1881

Sura ya 4

MASHAURI JUU YA ELIMU

Hakuna kazi iliyowahi kufanywa na mwanadamu inayohitaji uangalifu na ustadi zaidi kuliko mafunzo na elimu sahihi ya vijana na watoto. Hakuna mivuto yenye athari zenye nguvu kali kama ile inayotuzunguka katika miaka yetu ya awali. Mwenye hekima asema, “Mlee mtoto katika njia impasayo; naye hataiacha hata atakapokuwa mzee.” Asili ya mwanadamu ni ya mgawanyiko wa namna tatu, na mafunzo yaliyoamriwa na Sulemani yanatambua uendelezaji sahihi wa nguvu za kimwili, kiakili na kimaadili. Ili kufanya kazi hii kwa usahihi, wazazi na walimu lazima wao wenyewe kuielewa “njia impasayo mtoto kuiendea.” Hii inakumbatia zaidi ya ujuzi wa vitabu au mafunzo ya shuleni. Inahusu tabia ya kiasi, upendano wa kindugu, utauwa; ya kutekeleza wajibu wetu kwetu wenyewe, kwa jirani zetu, na kwa Mungu. {FEsw 57.1}

Mafunzo ya watoto lazima yafanywe kwa kanuni tofauti na ile inayoongoza mafunzo ya wanyama wasio na akili. Mnyama analazimishwa kuwa tu na desturi ya kujisalimisha kumtii bwana wake; lakini mtoto lazima afundishwe kujidhibiti. Nia lazima ifunzwe kutii maagizo ya akili na dhamiri. Mtoto anaweza kunidhamishwa kuwa sawa na mnyama, bila mapenzi yake mwenyewe, utu au upekee wake kupotea katika ule wa mwalimu wake. Mafunzo kama haya sio ya busara, na athari zake za mabalaa. Watoto wakielimishwa kwa namna hiyo watakuwa na mapungufu katika uimara na uamuzi. Hawafundishwi kutenda kutokana na kanuni; nguvu za akili hazijaimarishwa kwa kutumiwa. Kadri iwezekanavyo, kila mtoto anapaswa kufundishwa kujitegemea. Kwa kushughulisha katika vitivo mbalimbali, atajifunza ni wapi alipo na nguvu zaidi, na wapi ana mapungufu. Mwalimu mwenye busara ataweka umakini maalum kwa ukuaji wa vitabia vilivyo dhaifu, ili mtoto aweze kuunda tabia linganifu, yenye uwiano (balansi) na njema. {FEsw 57.2}

Katika baadhi ya shule na familia, watoto wanaonekana kuwa wamefunzwa vizuri, wawapo chini ya nidhamu ya muda, lakini wakati mfumo ambao

umewashikilia kwa kuweka sheria unapovunjwa, wanaonekana hawana uwezo wa kufikiri, kutenda, au kuamua kwa ajili yao wenyewe. Kama wangefundishwa kuzoeza na kutekeleza uamuzi wao wenyewe kwa haraka na kadiri inavyowezekana, uovu ungeondolewa. Lakini wamedhibitiwa kwa muda mrefu na wazazi au walimu kwa kuwategemea kabisa. Yeye anayetafuta kuwa na utu au upekee wa wanafunzi wake kuunganishwa katika wake, ili akili, uamuzi, na dhamiri iwe chini ya udhibiti wake, hufanya wajibu usio na msingi na wa kutisha. Wale wanaowafundisha wanafunzi wao kuhisi kwamba uwezo upo ndani yao wenyewe kuwa wanaume na wanawake wenye heshima na manufaa, watakuwa na mafanikio ya kudumu zaidi. Huenda kazi yao isionekane kuwa na manufaa zaidi watazamaji wasioweka umakini, na kazi yao inaweza isithaminiwe sana kama ile ya mwalimu ambaye hubeba udhibiti kamili, lakini maisha ya baadaye ya wanafunzi hawa yataonyesha matokeo ya mpango bora wa elimu. {FEsw 57.3}

Wazazi na walimu wote wako katika hatari ya kuamrisha na kulazimisha sana (madikteta), wakati wanashindwa kuwa vya kutosha katika uhusiano wa kijamii na watoto wao au wanafunzi wao. Wanazingatia sana kujihifadhi, yaani wanakosa moyo wa kirafiki au ukaribu, na kutumia mamlaka yao kwa ubaridi, bila namna ya huruma, ambayo hushindwa kuwaleta watoto karibu nao, na badala yake huwafanya watake kutoroka, kisha wanakuwa hawa wanakuwa ujasiri, kujiamini na mapenzi. Kama mara nyingi wangekusanya watoto kando yao, na wakaonesha kupendezwa na kazi zao, na hata katika michezo yao, wangepata upendo na ujasiri wa watoto hawa wadogo, na somo heshima na utii lingejifunzwa kwa urahisi zaidi; Kwani upendo ndiye mwalimu bora zaidi. Matamanio kama hayo yakioneshwa kwa vijana yatavana matokeo yayo hayo. Moyo wa mtoto ni wa haraka kuitikia mvuto wa huruma. {FEsw 58.1}

Isisahauliwe kamwe kwamba mwalimu lazima awe vile anavyotamani wanafunzi wake wawe. Kwa hivyo, kanuni na mazoea yake yanapaswa kuzingatiwa kuwa muhimu zaidi kuliko hata sifa zake za kitaaluma Anapaswa kuwa mtu yule anayemcha Mungu, na anayeuhisi wajibu wa kazi yake. Anapaswa kuelewa umuhimu wa mafunzo ya kimwili, kiakili, na kimaadili na anapaswa kuzingatia ipasavyo kila moja. Yeye ambaye atawadhibiti wanafunzi wake lazima kwanza ajidhibiti yeye mwenyewe. Ili kuupata upendo wao, ni lazima aonyeshe kwa mwonekano, maneno na matendo kwamba moyo wake umejazwa na upendo kwao. Wakati huo huo, uthabiti na uamuzi ni muhimu katika kazi ya kuunda tabia sahihi, na kukuza tabia njema. {FEsw 58.2}

Mafunzo ya kimwili yanapaswa kuchukua nafasi muhimu katika kila mfumo wa elimu. Ni wajibu wa wazazi na walimu kuufahamu mfumo wa mwili wa binadamu na kanuni zinazouendesha, na kadiri inavyowezekana, kuwapatia watoto wao na wanafunzi baraka kubwa zaidi ya zote za kidunia, “akili timamu yenye busara katika mwili timamu.” Mamia ya watoto hufa kila mwaka, na wengine wengi huachwa

kuburuta maisha ya unyonge na huzuni, labda kwa ajili ya dhambi, au kwa sababu ya ujinga au uzembe wa wazazi na walimu. {FEsw 59.1}

Mama wengi hutumia saa na hata siku nzima katika kazi zisizohitajika kwa ajili ya kujionesha tu, na bado hawana muda wa kupata taarifa muhimu ili kuhifadhi afya ya watoto wake. Anapeleka miili yao kwa daktari, na Roho zao kwa mhudumu, ili apate kuendelea bila kusumbuliwa katika ibada yake ya mitindo. Ili kuelewa mfumo wa ajabu wa umbo la binadamu, kuelewa utegemezi wa kiungo kimoja juu ya kingine, kwa hatua ya afya ya vyote, ni kazi ambayo yeye hana haja nayo. Kuhusu ushawishi wa pande zote za akili na mwili, anajua kidogo sana. Akili yenyewe, ni zawadi na amana ya ajabu sana tuliyojaliwa ambayo huunganisha mwenye ukomo na asiye na ukomo, yeye haielewi. {FEsw 59.2}

Kwa vizazi na vizazi, mfumo wa elimu maarufu, kwa Watoto hasa, imekuwa ni uharibifu kwa afya, na hata kwa maisha yenyewe. Masaa matano hadi sita kwa siku watoto wadogo wamekuwa katika vyumba vya shule ambavyo havina hewa ya kutosha wala ukubwa wa kutosha kwa ajili ya makazi ya afya ya wanafunzi. Hewa ya vyumba hivyo punde inakuwa sumu kwenye mapafu ambayo huivuta. Na hapa hawa wadogo, na miili yao iliyo na utendaji mwingi na inayotaka kurukaruka, yaani isiyotulia, na akili zilizo na shughuli nyingi na zisizotulia, zimeachwa bila kushughulishwa wakati wa siku zenye mwanga mrefu wakati wa kiangazi*, wakati ulimwengu wa nje huwaita kukusanya afya na furaha pamoja ndege na maua. Watoto wengi wadogo wanashikilia afya kwa udogo tu katika maisha yao. Kufungiwa shuleni huwafanya kuwa na wasiwasi na wagonjwa. Miili yao inadumaa na hudhoofishwa kwa Ukosefu kwa ukosefu wa mazoezi na uchovu wa hali ya mfumo wa neva. Ikiwa taa ya uzima itazimika, wazazi na walimu wako mbali na kushuku kwamba wao wenyewe walikuwa na lolote kuhusiana na kuzizima cheche muhimu za maisha. Msiba wa kusikitisha unaonekana kama matokeo ya majaliwa ya Mpaji, wakati ukweli ni kwamba, kwa ujinga wao usio na udhuru na kupuuza sheria za maumbile na asili (nature) vimeharibu maisha ya watoto hawa. Mungu aliwaumba waishi katika kufurahia afya na nguvu, kukuza tabia safi, bora, takatifu, na ya kupendeza katika maisha haya na kisha kumtukuza Mungu milele katika maisha yajayo Mbinguni. {FEsw 59.3}

*(jua linaweza kuwaka kwa masaa 18 mpaka 24 sehemu nyingine kwa siku wakati wa miezi mitatu ya kiangazi hivyo watoto wasikae ndani siku nzima)

Ni nani anaweza kupima maisha ambayo yameharibiwa kwa kukuza akili kwa kupuuza nguvu za kimwili? Njia iliyochukuliwa na wazazi na walimu wasio na hekima katika kuchochea akili ya vijana ni kuwasifia kwa kutia chumvi au kuwatia hofu, na hivi vimethibitika kuwa vibaya kwa wanafunzi wengi walioonyesha matumaini. Badala ya kuwatia moyo kwa kila aina ya motisha iwezekanayo, mwalimu mwenye busara atazuia akili inayofanya kazi sana ishughulike na mazoezi au kazi za mikono mpaka mfumo wa mwili umekuwa na nguvu za kutosha

kuhimili juhudi za kiakili (wafanye kazi muda mwingi badala ya kukaa kwenye masomo). {FEsw 60.1}

Ili vijana wawe na afya na uchangamfu, ambavyo hutegemea ukuaji wa kawaida wa mwili na akili, umakini lazima utolewe kwa udhibiti sahihi wa kupanga saa za masomo ya kitabuni, kazi za mikono na burudani. Wale ambao wamejifungia kwa kusoma kwa kupuuzia mazoezi ya mwili, wanadhuru afya wanapofanya hivyo. Mzunguko wa damu au mitoki (lymph) hauwi na usawa, ubongo huwa na damu nyingi na mwili kidogo sana (hasa sehemu zilizo mbali na moyo, kama miguu, mikono-extremities). Masomo yao yanapaswa kuzuiliwa kwa idadi sahihi ya masaa (wasiwe na vitabu saa yote), na kisha muda unapaswa kutolewa kwa kazi za mikono katika hewa ya wazi. {FEsw 60.2}

Hebu Watoto wadogo waruhusiwe kukimbia na kucheza nje, kufurahia hewa safi, na mwanga wa jua unaotoa uhai. Hebu msingi wa mfumo mwema wa afya ya mwili uwekwe katika maisha ya awali. Wazazi wanapaswa kuwa walimu pekee wa watoto wao, hadi wawe na miaka minane au umri wa miaka kumi. Hebu mama awe na kujali kudogo sana kuhusiana na mambo ya bandia, hebu akatae kutoa nguvu zake kwa utumwa wa maonyesho ya mtindo, na kupata muda wa kusitawisha ndani yake na watoto wake upendo wa mambo mazuri ya asili. Hebu na awaelekeze kwenye Utukufu ulioenea huko Mbinguni, kwa maumbo mazuri elfu yanayopamba nchi, kisha awaambie Kuhusu Yeye aliyewaviumba vyote. Hivyo kuweza kuongoza akili zao changa kwa Muumba, na kuamsha mioyoni mwao heshima na upendo kwa Mpaji wa kila baraka. Mashamba na vilima ndivyo Chumba cha kutazama asilia, yaani Uumbaji wa Mungu- hivi ndiyo vinapaswa kuwa chumba cha darasa la watoto wadogo. Hazina za Uumbaji zinapaswa kuwa kitabu chao cha kiada. Na hilo litafanya Masomo yanayotiwa chapa katika akili zao kutotasahaulika upesi. {FEsw 60.3}

Kazi za Mungu katika asili zina mafunzo ya hekima na karama za uponyaji kwa wote. Taswira zinazobadilika kila wakati ya misimu inayojirudia daima huonyesha ishara mpya za Utukufu Wake, nguvu Zake, na upendo Wake. Ilikuwa vizuri kwa wanafunzi wakubwa, wakati wanafanya kazi ili kupata sanaa na elimu ya watu, pia kutafuta zaidi hekima ya Mungu, —kujifunza zaidi sheria za kimbingu, za asili na za kimaadili. Katika Utiifu kwa haya kuna maisha na furaha katika dunia hii na katika ulimwengu ujao wa milele yaani Paradiso. — *The Review and Herald, January 10, 1882.* {FEsw 61.1}

Kwa marejeleo ya Ziada

The Review and Herald, February 28, 1882, Should Christians Dance?

Testimonies for the Church, 5: 319-323 Parental Responsibility Training of Children, Idem, 5: 323-331 Business and Religion, Idem, 5: 422-429.

Sura ya 5

KUTEMBELEA MJI WA COLLEGE CITY AMBAPO KUNA CHUO KIKUBWA

Wiki chache, tangu nilipotembelea Jiji la College City ulio jimbo la California, kuzungumza, kwa mwaliko, juu ya suala la kuwa na kiasi. Kanisa lilikuwa limejitoa kwa hafla hiyo, na kulikuwa na mahudhurio mazuri. Watu wa mahali hapa tayari wamechukua msimamo wa kusifika juu ya kanuni za kuwa na kiasi. Kwa kweli, ilikuwa ni kwa sababu ya sharti hili ndio chuo kikaanzishwa hapa. Ardhi ambayo majengo la chuo yanasimama, na eneo kubwa kuzunguka, ilitolewa kwa Kanisa la Kikristo kwa madhumuni ya kielimu, kwa masharti kwamba hakuna baa au klabu cha pombe kinachopaswa kufunguliwa ndani ya maili tatu kutoka chuoni. Mkataba huu unaonekana kutunzwa kwa uaminifu. Tunaweza kujisikia kuwa vijana walikuwa salama zaidi kuhudhuria shule katika mji kama huo kuliko pale ambapo kuna baa zimefunguliwa mchana na usiku kwenye kila kona ya mtaa. {FEsw 62.1}

Sheria za chuo hiki zinalinda kabisa ushirika wa vijana wanaume na wanawake vijana wakati wa muhula wa masomo shuleni. Ni wakati tu sheria hizi zinaposimamishwa kwa muda, kama ilivyo wakati mwingine, kwamba wanaume wanaruhusiwa kuchangamana, au kuwasindikiza wanawake kwenda na kutoka katika mikusanyiko ya umma. Chuo chetu huko Battle Creek kina kanuni sawa na hizi, ingawa sio kali sana. Sheria kama hizi ni za lazima kwa usalama na kuwalinda vijana dhidi ya hatari za uchumba wa mapema na ndoa zisizo za busara. Vijana hupelekwa shuleni na wazazi wao ili kupata elimu, si kutongozana na kufanya mapenzi na watu wa jinsia tofauti (siku hizi mengi zaidi yamechipuka kama ushoga, ila haya yote ni uovu), vijana wasiopevuka vyema wasijiingize kwenye mahaba}. Uzuri wa jumuiya, kama yalivyo matakwa ya juu zaidi kwa wanafunzi, hudai

kwamba wasijaribu kuchagua mwenzi wa maisha wakati tabia yao bado haijaendelezwa, uamuzi wao haujakomaa, na wakiwa bado wakati huo huo hawana uangalizi na mwongozo wa wazazi. {FEsw 62.2}

Ni kwa sababu mafunzo ya nyumbani yana kasoro ndivyo maana vijana hawako tayari kunyenyekea kwa mamlaka husika. Mimi ni mama; Najua yale ambayo ninazungumza, ninaposema kwamba vijana na watoto sio tu kwamba wapo salama wakiwa na wigo unaofaa, lakini pia wana furaha zaidi kwa kuwa kwao chini ya udhibiti ufaao kuliko kufuata mielekeo yao wenyewe. Wazazi, wana na binti zenu hawaangaliwi vizuri. Hawapaswi kamwe kuruhusiwa kwenda na kurudi watakavyo wao, bila wewe kujua na kwa idhini yako. Uhuru usio na mipaka unaotolewa kwa watoto katika kizazi hiki umethibitisha uharibifu wa maelfu. Ni wangapi wanaruhusiwa kuwa mitaani nyakati za usiku, na wazazi wanaridhika na kutojua marafiki/wenzi wa watoto wao. Mara nyingi sana, marafiki huchaguliwa ambao mvuto wao huelekea tu kuwadhoofisha na kuwakatisha tamaa kimaadili. {FEsw 62.3}

Katika kivuli cha giza, wavulana hukusanyika katika vikundi ili kujifunza masomo yao ya kwanza katika kucheza kadi, kamari, kuvuta sigara na kunywa mvinyo au bia. Vijana wa wazazi wa kidini hujitosa kwenye baa kwa ajili ya kula chaza usiku, au anasa zingine wanazojifurahisha nazo (kama hiyo za gharama na uchafuzi wa mwili), na hivyo kujiweka wenyewe katika njia ya majaribu. Mazingira ya hoteli hizi yamejaa matusi, makufuru na uchafu. Hakuna mtu anayeweza kubaki kwa muda mrefu ndani yake bila kuharibikiwa tabia kwa kuingia kwenye ufisadi. Ni kwa ushirika wa namna hiyo vijana ambao wameonyesha matumaini huingia kwenye uzembe. ulevi na uhalifu. Uovu huu unapoanza tu, unapaswa kuzuiliwa dhidi yake. Wazazi, isipokuwa unajua kuwa mazingira yao ni ya kipekee, usiruhusu watoto wako kwenda mitaani usiku ili kushiriki katika michezo ya nje, au kukutana na wavulana wengine kwa maburudisho. Ikiwa kanuni hii itatekelezwa kwa uthabiti, kuitii kwake kutakuwa mazoea, na hamu ya kutenda uovu itakoma hivi karibuni. {FEsw 63.1}

Wale wanaotafuta kuwakinga vijana dhidi ya majaribu na kuwatayarisha kwa maisha yenye manufaa, wanajishughulisha na kazi njema. Tunafurahi kuona katika taasisi yoyote ya kujifunza utambuzi wa umuhimu wa kudhibiti na kufunza nidhamu ipasayo kwa vijana. Hebu Jitihada za wakufunzi hao wote zipewe taji ya mafanikio. — *The Signs ya Times, March 2, 1882.* {FEsw 63.2}

Sura ya 6

NYUMBANI NA SHULENI

Kizazi hiki cha sasa kinapenda sana kujigamba kwamba kamwe hakujawahi kutokea watu wenye miundo mbiu na vitivo vya kukusanya maarifa na watu kujilimbikizia nyenzo kubwa sana za kukusanya maarifa, au kudhihirisha shauku kubwa katika elimu kama sasa. Hata hivyo licha ya hayo maendeleo ya kusifiwa, kuna Roho ya ukaidi (kutotii), uzembe na uharibifu usiyo na mfano ambayo inainua mapembe yake, katika kizazi hiki; kuzorota kiakili na kimaadili kumesheheni karibia kote. Elimu maarufu inayopenda na wengi haitibu uovu. Ulegevu wa kinidhamu katika taasisi nyingi za elimu umekaribia kuharibu manufaa yao, na kwa namna fulani kuwaletea laana badala ya baraka. Uhalisia huu umeonekana na upingamizi, na juhudi za dhati zimefanywa ili kurekebisha kasoro katika mfumo wetu wa elimu. Kuna hitaji la dharura kwenye shule ambazo vijana wanaweza kufundishwa kuwa na tabia ya kujitawala, elimu ya kivitendo kwa yale wanayojifunza, na kujitegemea, kuheshimu wakubwa na uchaji kwa Mungu. Kwa mafunzo kama haya, tunaweza kutumaini kuona vijana wakitayarishwa kumheshimu Muumba wao na kuwabariki binadamu wenzao. {FEsw 64.1}

Ilikuwa ni kwa ajili ya makusudi haya Chuo chetu chetu cha Battle Creek kilianzishwa. Lakini wale wanaojitahidi kutimiza kazi hii, hujikuta wanapigwa kikumbo na magumu mengi ya kutisha. Uovu ambao huwa na mengine wote, na ambayo mara nyingi huzikabili juhudi za wakufunzi bora, hupatikana katika nidhamu ya nyumbani. Wazazi hawaoni umuhimu wa kukinga watoto wao dhidi ya majaribu yaliyopambwa ya wakati huu. Hawajishughulishi kuwadhibiti ipasavyo, na kwa hivyo hawatambui ipasavyo thamani yake. {FEsw 64.2}

Baba na mama wengi hukosea kwa kushindwa kuunga mkono juhudi ya mwalimu mwaminifu. Vijana na watoto, kwa ajili ya upungufu wao katika ufahamu na maamuzi yasiyopevuka, sio kila wakati wanaweza kuelewa mikakati na mbinu

zote za mwalimu. Hata hivyo wanapoleta taarifa nyumbani za kile kinachosemwa na kufanywa shuleni, wazazi hukijadili hicho katika familia, na mwenendo au msimamo wa mwalimu hukosolewa bila kujizuia. Hapa watoto hujifunza masomo ambayo si rahisi kuyaondoa kichwani. Kila wanapowekwa kwenye kizuizi wasichokizoea, au kuhitajika kujishughulisha na kujifunza kwa bidii, husihi huruma za wazazi wao wasio na maamuzi yenye busara waendekeze hoja zao. Hivyo Roho ya kutotulia, machafuko na kutoridhika inaungwa mkono, shule kwa ujumla inakabiliwa na hali ya kukatishwa tamaa, na mzigo wa mwalimu unafanywa kuwa mzito zaidi. Lakini upotevu mkubwa zaidi hudumu katika maisha ya waathirika wa usimamizi mbovu wa wazazi (Watoto). Kasoro za tabia ambazo zingesahihishwa wa mafunzo sahihi zinaachwa kukomaa miaka inavyokwenda, na pengine kudhuru na hata kuharibu manufaa ya mhusika. {FEsw 64.3}

Kwa kawaida. kanuni ambayo imegunduliwa mahali pengi, ni kwamba wale wanafunzi ambao wapo tayari kufanya ulalamishi juu ya nidhamu ya shule, ni wale ambao wamepokea elimu ya juu juu tu. Wakiwa hawajafundishwa kufanya vitu kwa ukamilifu na umakini, huchukulia jambo hilo kwa kutolipenda. Wazazi wamepuuza kutoa mafunzo yao kwa watoto wa kiume na wa kike katika utendaji wa uaminifu wa kazi za nyumbani. Watoto wanaruhusiwa kutumia saa zao katika kucheza, wakati baba na mama wanahenyeka bila kupumzika. Ni vijana wachache wanaohisi kuwa ni wajibu wao kubeba sehemu ya mzigo wa familia. Hawajafundishwa kwamba kuendekeza uchu wa kula, au kutafuta raha na starehe, sio kipaumbele au lengo la maisha haya. {FEsw 65.1}

Mduara wa familia ni shule ambayo mtoto hupokea mafunzo yake ya awali na ya kudumu zaidi. Kwa hivyo wazazi wanapaswa sana kuwa nyumbani. Kwa kanuni na kielelezo, wanapaswa kuwafundisha watoto wao kumpenda na kumcha Mungu; wawafundishe kutumia akili zao, kuwa na mahusiano na ikiwezekana urafiki na jamii (social), wenye upendo/mapenzi, wenye kukuza tabia za kujishughulisha na kazi au stadi, wachumi, na wenye kujikana nafsi. Kwa kutoa kwa watoto wao upendo, huruma, na faraja nyumbani, wazazi wanaweza kutoa mazingira salama na hilo litawavuta kutoka kwenye wingi wa majaribu ya ulimwengu huu. {FEsw 65.2}

“Hakuna muda,” baba husema, “sina muda wa kutoa mafunzo hayo kwa watoto wangu, hakuna muda wa kuchangamana nao na [kufurahia kukaa nao](#) nyumbani.” Basi usingelipaswa kujitwika jukumu la kuwa na familia. Kwa kuwazuilia wakati ulio haki yao, unawanyima elimu ambayo wanapaswa kupokea kutoka mikononi mwako. Ikiwa una watoto, una kazi ya kufanya, kwa kushirikiana na mama yao, katika ujenzi wa tabia zao. Wale wanaohisi kuwa wana wito muhimu sana wa kufanya kazi kwa ajili ya kuboresha jumuiya, wakati watoto wao wenyewe hukua bila nidhamu, wanapaswa kujiuliza iwapo hawajakosea wajibu wao. Nyumba zao wenyewe ndiyo eneo la kwanza la umishonari ambamo wazazi wanatakiwa kufanya kazi. Wale ambao huacha bustani ya nyumbani ikimea miiba, magugu na

michongoma, huku wakidhihirisha shauku kubwa katika kulima kiwanja cha jirani yao, wanalipuuza Neno la Mungu. {FEsw 65.3}

Narudia, ni ukosefu wa upendo na ucha Mungu, na kupuuza nidhamu sahihi nyumbani, ndiyo huleta ugumu sana shuleni na vyuoni. Kuna hali ya ubaridi wa kutisha na kukosa shauku miongoni mwa wanaojiita Wakristo. Hawana hisia, ni wasio na upendo, wasiosamehe. Tabia hizi zenye uovu, ziliendekezwa nyumbani kwanza, kisha hushinikiza ushawishi wake mbaya katika mahusiano yote kwenye maisha ya kila siku. Ikiwa Roho ya wema na adabu ingeinuliwa na kuthaminiwa na wazazi na watoto, basi ingeonekana pia katika mahusiano ya mwalimu na mwanafunzi. Kristo anapaswa kuwa mgeni wa heshima katika familia, na uwepo Wake usiwe wa kiasi kidogo katika chumba cha darasa. Hebu Nguvu hiyo ya Mungu ya kuongoa iweze kulainisha na kutiisha mioyo ya wazazi na watoto, walimu na wanafunzi, na kuwageuza kuwa mfano wa Kristo. {FEsw 66.1}

Akina baba na akina mama wanapaswa kujifunza kwa umakini na kwa maombi tabia za watoto wao. Wanapaswa kutafuta kudhibiti na kuzuia zile sifa ambazo ni maarufu sana, na kutia moyo zingine ambazo zinaweza kuwa na upungufu, na hivyo kuleta ukuaji wenye usawa/uwiano. Hili siyo jambo jepesi. Huenda baba asione kuwa ni dhambi kubwa kupuuza mafunzo ya watoto wake; lakini ndivyo Mungu anavyoliona jambo hilo. Wazazi wakristo wanahitaji uongofu kamili juu ya jambo hili. Hatia inajilimbikiza juu yao, na matokeo ya matendo yao hutoka kwa watoto wao hadi kwa watoto wa watoto wao. Ugonjwa wa akili isiyo usawa (balansi), hasira ya haraka, kukerwa kirahisi, husuda, au wivu; hutoa ushuhuda wa malezi yaliyopuuzwa na mzazi. Mienendo hii yenye uovu wa tabia huleta huzuni kubwa kwa wanaoimiliki. Ni wangapi wanashindwa kupokea kutoka kwa marafiki upendo ambao wangeweza kuwa nao, ikiwa wangukuwa wanapendeka kwa kuwa na mioyo ya kirafiki, nidhamu na mapenzi kwa watu. Ni wangapi wanaleta chokocho au shida popote wanapokwenda, na katika chochote wanachoshiriki! {FEsw 66.2}

Watoto wana madai ambayo wazazi wao wanapaswa kuyatambua na kuyaheshimu. Wana haki ya kupata elimu na mafunzo yatakayowafanya kuheshimiwa, kuwa watu wenye manufaa, na wapendwa katika jamii hapa duniani, na kuwapa maadili bora kwa ajili ya jamii safi na takatifu kule Mbinguni. Vijana wanapaswa kufundishwa kwamba ustawi wao wote wa sasa na wa wakati ujao unategemea kwa kiwango kikubwa tabia wanayoiunda utotoni na ujanani. Wanapaswa kuzoezwa mapema kujisalimisha, kujinyima, na kujali furaha ya wengine. Wanapaswa kufundishwa kudhibiti hasira ya haraka, kuzuia neno la ghadhabu, wapate kuonyesha wema usiobadilika-badilika, adabu, na kutawala nafsi. Baba na mama wanapaswa kufanya utafiti wao wa maisha ili watoto wao wakaribie ukamilifu katika tabia kadri iwezekanavyo kwa juhudi za kibinadamu, pamoja na msaada wa kimbingu, wataweza kukakamilisha. Kazi hii, pamoja na

umuhimu wake wote na wajibu wameikubali, kwa kuwa ni wao ndio wamewaleta watoto hawa duniani. {FEsw 67.1}

Wazazi lazima waone kwamba mioyo na maisha yao wenyewe vinatawaliwa kwa maagizo ya Bwana, ikiwa watawalea watoto wao katika malezi na mawaidha ya Bwana. Hawana mamlaka ya kufadhaisha, kukasirikakasirika, kukemea na kukejeli. Hawajapewa mamlaka na Mungu ya kuonyesha hasira au wasiwasi mbele za watoto wao kwa kuwagombeza, kuwafyolea, kutoa matusi au kuwadhihaki. Wazazi hawapasi kuwachokoza watoto wao kwa kejeli kwa kuzizungumza tabia zao mbaya ambazo wao wenyewe wamewarithisha watoto wao (pia wasiwakejeli watoto na kuwaambia ni wabaya au kuhusu tabia mbovu maana unaweza pia kuwa unabii wa kuwafanya kuziishi hizo tabia). Aina hii ya malezi au ufunzaji wa adabu haitibu uovu. Wazazi leteni kanuni za Neno Lake Mungu Mungu ili kuonya, kufundisha, kusahihisha na kukemea watoto wapotovu. Waonyesheni “Bwana asema hivi” pale unapowaambia matakwa yako. Karipio linalokuja kama Neno la Mungu lina ufanisi zaidi kuliko lile linalotoka kwa ukali, na sauti yenye hasira kutoka kwenye midomo ya wazazi. {FEsw 67.1}

Popote inapoonekana ni muhimu kukataa matakwa au kupinga mapenzi ya mtoto, anapaswa kuvutiwa sana na wazo hilo kwamba hili halifanywi kwa ajili ya kuwaridhisha wazazi tu, au kuifurahisha mamlaka ya kiholela, lakini kwa manufaa yake mwenyewe. Anapaswa kufundishwa kwamba kila kosa ambalo halijarekebisha litaleta huzuni kwake mwenyewe, na kumchukiza Mungu. Chini ya nidhamu kama hiyo, watoto watapata furaha yao kubwa zaidi katika kusalimisha mapenzi yao wenyewe kwa mapenzi ya Baba yao wa Mbinguni. {FEsw 67.2}

Baadhi ya wazazi na baadhi ya walimu vilevile, wanaonekana kusahau kwamba wao wenyewe waliwahi kuwa Watoto wanatunza hadhi zao kwa kukunja nyuso zao na kuwafanya watoto wasiwakaribie, wanakuwa wana ubaridi, na hawana huruma. Popote wanapokutana na vijana, nyumbani, katika shule ya kutwa, shule ya Sabato, au kanisani, wanadumisha hali ile ile ya mamlaka, na nyuso zao huvaa kauli nzito yenye kukaripia, na huwa hazina tabasamu. Furaha ya kitoto na burudani yao au upotovu, miili ya watoto isiyotulia na yenye shughuli, maisha ya utotoni au ujana, hayapati udhuru machoni pao. {FEsw 68.1}

Makosa madogo madogo yanachukuliwa kuwa dhambi kubwa. Nidhamu kama hiyo si ya Kristo. Watoto waliofunzwa hivyo huwaogopa wazazi au walimu wao, lakini hawawapendi; hawana ujasiri wa kuwaambia uzoefu wao wa kitoto. Baadhi ya sifa za thamani zaidi za akili na moyo hupozwa hadi kufa, kama mmea mchanga kabla ya mlipuko wa theluji wakati wa majira ya baridi. {FESWsw 68.2}

Tabasamuni wazazi, walimu tabasamuni. Ikiwa moyo wako una huzuni, hebu usiruhusu uso wako kufichua jambo hilo. Hebu jua liangaze kutoka moyo wa upendo na shukrani itie Nuru uso wako. Achana na uadhi yako ya kutokunjika

kama chuma, badilika kutokana na mahitaji ya watoto, na wafanye wakupende. Lazima ujipatie/ushinde upendo wao, kama ungetaka kuwaambukiza na joto la Ukweli wa kidini juu ya mioyo yao. {FEsw 68.3}

Yesu aliwapenda watoto. Alikumbuka kwamba aliwahi kuwa mtoto, na uso Wake mkarimu ukayashinda mapenzi ya watoto wadogo. Walipenda kucheza karibu Naye, na kuupapasa uso ule wa upendo kwa mikono yao isiyo na hatia. Wakati akina mama wa Kiebrania walipoleta watoto wao wachanga kubarikiwa na Mwokozi Mpendwa wanafunzi waliiona shughuli hiyo ni ya umuhimu mdogo sana kukatiza mafundisho Yake. Lakini Yesu aliisoma shauku ya dhati ya mioyo ya akina mama hao, na kuwaangalia Wanafunzi Wake, kwa kusema, “Waacheneni watoto wadogo waje Kwangu, wala msiwazuie; kwa maana ufalme wa Mbinguni ni wao.” {FEsw 68.4}

Wazazi, mnayo kazi ya kuwafanyia watoto wenu ambayo hakuna mwingine anaweza kuifanya. Huwezi kuuhamisha wajibu wako kwa mwingine. Wajibu wa baba kwa watoto wake hauwezi kuhamishiwa kwa mama. Kama mama anatimiza wajibu wake mwenyewe, basi ana mzigo tosha wa kubeba. Ni kwa kufanya kazi kwa pamoja tu, ndiyo baba na mama wanaweza kukamilisha kazi ambayo Mungu ameiweka mikononi mwao. {FEsw 69.1}

Wakati ambao hutolewa katika kupata mali, unakuwa umetumiwa vibaya zaidi kuliko ule muda uliopotezwa kwa wazazi na watoto, wakati muda ungetumiwa kwa uboreshaji wa ubongo na wa maadili hupuuzwa. Hazina za duniani lazima zitapita; lakini ubora wa tabia, thamani ya maadili, itadumu milele. Ikiwa kazi ya wazazi itafanyika vyema, itashuhudia katika umilele juu ya hekima na uaminifu wao. Wale wanaozishughulisha pochi zao kwa bidii na werevu wao ili kuzipatia familia zao mavazi ya gharama na chakula cha mapochopocho na vitafunio vya gharama, au kudumu katika kuwaepusha watoto wasijue stadi zenye manufaa, watalipwa tu kwa kiburi, wivu, husuda, ukaidi, kukosa adabu, kukosa utii na kutoheshimiwa na watoto wao walioharibiwa. {FEsw 69.2}

Vijana wanahitaji kuwa na kizuizi thabiti kilichojengwa tangu utoto wao kati yao na dunia, ili ushawishi wake unaoharibu usipate kuwaathiri. Wazazi lazima wawe na uangalifu unaoongezeka, kwamba wao watoto wasipotee kwa Mungu. Ikiwa ingezingatiwa kuwa muhimu vijana wawe na tabia nzuri na tabia ya kupendeza kama wanavyoiga mitindo ya ulimwengu katika mavazi na adabu, na mwenendo, basi tungeona mamia ambapo kuna mmoja tu leo anayekuja juu ya jukwaa la maisha makamilifu yaliyoandaliwa kutoa ushawishi unaonekana bora wenye kutukuka juu ya jamii. {FEw 69.3}

Kazi ya wazazi ya elimu, mafundisho, na nidhamu ni msingi na kipaumbele cha ya kazi nyingine yoyote. Juhudi za walimu bora mara nyingi, lazima zizae matunda kidogo sana ikiwa baba na mama watashindwa kufanya sehemu yao kwa uaminifu.

Neno la Mungu lazima liwe mwongozo wao daima. Hatujitahidi kuwasilisha njia mpya ya wajibu au majukumu mapya. Tunaweka mbele ya mafundisho yote Neno hilo kwalo kazi yetu inapaswa kuhukumiwa/kutathminiwa kwalo, na tunajiuliza, Je! hiki ndicho kiwango ambacho sisi kama wazazi Wakristo tunajitahidi kukifuata na kukifikia? — *The Review and Herald, March 21, 1882.* {FEsw 69.4}

Kwa Marejeleo ya Ziada

Signs of the Times, April 27, 1882 The Teacher and His Work,

Signs of the Times, May 4, 1882, Labor as a Blessing, Signs of the Times, May 4, 1882, „ Our School at Healdsburg

Signs of the Times, May 25, 1882, Home Training — Its Importance and Results, The Review and Herald, June 13, 1882. Home Discipline,

Sura ya 7

Umuhimu wa Mafunzo ya Kimwili

Kipindi cha sasa ni cha shauku isiyo na kifani na kisichoweza kulinganishwa na kingine chochote katika elimu. Ueneaji mpana wa maarifa kupitia wakala wa vyombo vya habari, umeweka mbinu za ukuzaji wa utamaduni binafsi wa kiakili kwenye uwezo wa wote, na kuamsha hamu ya jumla ya kukuza akili. {FEsw 71.1}

Wakati tunakiri kwa shukrani kuongezeka kwa vifaa, miundo mbinu na nyenzo zetu (pengine hata maarifa ya sayansi na teknolojia), hatupaswi kufumbia macho kasoro za mfumo wa sasa wa elimu. Katika juhudi za kutaka kujipatia utamaduni wa kiakili, mafunzo ya kimwili pamoja na ya kimaadili yamepuuzwa. Vijana wengi hutoka katika taasisi za elimu wenye maadili duni, na nguvu dhaifu za kimwili; bila ujuzi wa maisha ya vitendo, na nguvu kidogo za kutekeleza majukumu yake. {FEsw 71.2}

Nilivyoona maovu haya, nimeuliza, Je, ni lazima vijana na mabinti zetu wadhoofike kimaadili na kimwili, ili kupata elimu shuleni? Haipaswi kuwa hivyo; si lazima, kama walimu na wanafunzi watakuwa wakweli kwa sheria za asili, ambazo pia ni sheria za Mungu. Nguvu zote za akili na mwili zinapaswa kushughulishwa, ili kijana awe hodari; mwanaume na mwanawake mwenye usawa. {FEsw 71.3}

Wanafunzi wengi wana haraka sana kumaliza masomo yao kiasi kwamba si wakamilifu katika jambo lolote wanalofanya (wanalipua lipua mambo). Wachache

huwa na ujasiri wa kutosha na kujitawala kutenda kutokana na kanuni. Wanafunzi wengi hushindwa kuelewa lengo la kweli la elimu, na hivyo hushindwa kuchukua jukumu katika njia hiyo ili kufikia kusudi hili. Wanajituma kwa masomo ya hisabati au lugha, huku wakipuuza kujifunza yale yaliyo muhimu zaidi kwa furaha na mafanikio yao katika maisha. Wengi ambao wanaweza kuchunguza vilindi vya dunia na mwanajiolelezi, au kupita mbingu pamoja na mnajimu, hawaoneshi kupendezwa au kuwa na shauku hata kidogo na utendaji wa ajabu wa miili yao wenyewe. Wengine wanaweza kusema kuna mifupa mingapi katika kiwiliwili cha binadamu, na kwa usahihi kuelezea kila kiungo cha mwili, na bado ni wajinga wa sheria za afya, na tiba za magonjwa, kana kwamba maisha yanadhibitiwa imani ya bahati nasibu tu, badala ya kanuni za uhakika na zisizobadilika. {FEsw 71.4}

Afya ya kimwili imelala kwenye msingi wa matarajio, matamano na matumaini ya mwanafunzi. Kwa hivyo umuhimu wa kwanza ni kupata ujuzi wa sheria hizo ambazo afya inalindwa na kuhifadhiwa. Kila kijana anapaswa kujifunza jinsi ya kudhibiti mazoea ya lishe yake, —nini cha kula, wakati gani wa kula, na jinsi gani ya kula. Anapaswa kujifunza ni masaa mangapi ya kusoma, na muda gani wa kutumia kwa mazoezi ya viungo. Mwili wa mwanadamu unaweza kulinganishwa na mashine nzuri iliyotengenezwa au iliyowekwa au kurekebishwa vizuri, ambayo inahitaji utunzaji ili kuiweka katika mpangilio mzuri. Sehemu moja haipaswi kuwa chini ya matumizi ya mara kwa mara na kulika au kuchoshwa na hivyo kuwa katika shinikizo, huku sehemu nyingine ikiwa na kutu kutokana na kutotumika. Wakati akili inashughulishwa, misuli pia inapaswa kuwa na uwiano wake wa mazoezi. {FEsw 72.1}

Udhibiti sahihi wa tabia yake ya kula, kulala, kusoma, na mazoezi, ni wajibu ambao kila mwanafunzi anawiwa kwake mwenyewe binafsi, na kwa jamii, na kwa Mungu. Elimu ambayo itawafanya vijana kuwa mbaraka kwa ulimwengu, ni ile inayowawezesha kuwa wanaume na wanawake wakweli, bora na adhimu. Mwanafunzi yule ambaye anasoma sana, analala kidogo, na kufanya mazoezi kidogo, na kula bila mpangilio na ubora usiofaa au duni wa chakula, hupata mafunzo ya akili kwa gharama ya afya na maadili, ya kiroho, na, inaweza kuwa, ya maisha. {FEsw 72.2}

Wale walio wadogo au vijana, kwa asili hutamani shughuli, na ikiwa hawatapata wigo halali wa nguvu zao za kujifunga baada ya kufungiwa kwenye chumba cha darasa, wanakosa utulivu na kukosa subira ya udhibiti, na hivyo kuongozwa kujihusisha na michezo isiyo na adabu, yenye jeuri, isiyo na uungwana, na inayofedhehesha shule nyingi na vyuo, na hata kutumbukia katika matukio ya zinaa na ulevi halisi. Vijana wengi walioziacha nyumba zao bila hatia, wameharibiwa kwa kuchangamana kwao shuleni na marafiki. {FEsw 72.3}

Kila taasisi ya elimu inapaswa kutoa fursa kwa ajili ya kujifunza na kupata mazoezi ya kilimo na ufundi wa mashine (mekanika au uinjini wa aina Fulani).

Walimu mahiri wanapaswa kuajiriwa kuwafundisha vijana katika sekta mbalimbali za shughuli za viwanda, na vile vile katika matawi kadhaa za masomo. Wakati sehemu ya kila siku hutolewa kwa uboreshaji wa akili, hebu sehemu nyingine tajwa itolewe kwa kazi ya mikono/kimwili, na wakati unaofaa wa zoezi la ibada na kujifunza Maandiko. {FEsw 72.4}

Mafunzo haya yatahimiza tabia za kujitegemea, uimara, na maamuzi. Wahitimu wa taasisi kama hizo wangekuwa tayari kushiriki kwa mafanikio katika majukumu ya vitendo ya maisha. Wangekuwa na ujasiri na ustahimilivu wa kushinda vikwazo, na uimara wa kanuni ambao hautajisalimisha kwenye ushawishi mbaya. {FEsw 73.1}

Kama ingetokea vijana wana nafasi ya kupata elimu ya upande mmoja tu, ni ipi ambayo ni ya umuhimu mkubwa zaidi basi, usomi wa sayansi, pamoja na hasara zote kwa afya na maadili au mafunzo ya kina katika majukumu ya vitendo, yenye maadili mema na bora na ukuaji mzuri wa kimwili? Bila kusita tunasema hiyo ya pili. Lakini kwa juhudi zinazofaa mara nyingi zote mbili zinaweza kufanywa (kama kuna kuchagua kazi za mikono tu au kazi za masomo tu, ni bora uchague kazi za mikono tu, ila vyote viwili unaweza kufanya, ila kamwe usiache kazi za mikono, kwa sababu wewe ni msomi). {FEsw 73.21}

Wale wanaochanganya kazi muhimu na masomo hawana haja ya mazoezi ya viungo ya sarakasi (gymnastic-kama yale ya halaiki). Na kazi inayofanywa katika hewa ya wazi ina manufaa mara kumi zaidi kwa afya kuliko kazi ya ndani. Fundi na mkulima, wote wana mazoezi ya viungo, lakini mkulima ndiye mwenye afya bora kati ya hao wawili. Hana upungufu wa hewa ya asili ya kuisimua na itiayo nguvu na ukijumlisha na jua vyote, hivyo vitakidhi kikamilifu mahitaji ya mfumo wa mwili. Mkatuaji ardhi hupata katika kazi yake mijongeo ya mwili yote ambayo ingetendwa katika ukumbi wa mazoezi (gymn). Chumba chake cha mazoezi ni uwanja wa wazi. Anga la mbingu ndilo paa lake, ardhi ngumu ndiyo sakafu yake. Hapa analima kwa plau, anakatua na jembe, hupanda na kuvuna. Mwangalie basi katika "kuvuna majani ya ngombe-(haying)" anakata majani na anayareki, anayanyanyua na kuyarusha juu ili kuyachambua ili hewa ipite ndani yake, anayasawazisha na kuyaangusha, anayainua na kuyabeba, anayarusha juu, na kuyabiringisha ili yawe kwenye shepu inayotakiwa na kisha huyafunga kwenye tita. Mijongeo hii mbalimbali huifanya mifupa, viungo, misuli, mishipa na neva za fahamu ya mwili zitende kazi. Mazoezi yake yenye nguvu na ya harakaharaka, husababisha upumuaji kamili, wa kina, wenye nguvu, ambao kupanua mapafu na kutakasa/kusafisha damu, hiyo hupeleka joto kwenye mkondo wa maisha kulifunga kupitia kwenye mishipa ya ateri na vena. Mkulima mwenye kiasi, yaani anayejithibiti katika mazoea yake yote, kwa kawaida hufurahia afya. Kazi yake ni ya kupendeza. Ana hamu nzuri ya kula. Analala vizuri, na anaweza kuwa na furaha. {FEsw 73.41}

Tofauti na hali ya mkulima na ile ya mwanafunzi ambaye hupuuza mazoezi ya

mwili. Anakaa kwenye chumba kilichofungwa, akiinama juu ya dawati au meza yake, kifua chake kimejikaza na kusinyaa, mapafu yake yamejaa. Hawezi kuwa na uvutaji wa hewa ili iingie ndani kwa ukamilifu, na kina. Ubongo wake umelemewa na jukumu kubwa, huku mwili wake ukiwa haufanyi kazi wa kujongea kana kwamba hana matumizi maalum nao. Damu yake hutembea kwa udhaifu na polepole katika mfumo. Miguu yake ni ya baridi, kichwa chake cha moto. Mtu kama huyo anawezaje kuwa na afya? {FEsw 74.11}

Hebu mwanafunzi afanye mazoezi ya kila siku yatakayomfanya apumue kwa kina na kwa ukamilifu, akichukua ndani ya mapafu yake hewa safi ya kuchangamsha na yenye nguvu ya Mbinguni, naye atakuwa kiumbe kipya. Sio kusoma kwa bidii ndiko hugaribu afya za wanafunzi, kwa kiasi kikubwa, bali ni kutojali kwao sheria za asili. {FEsw 74.21}

Katika taasisi za mafunzo au elimu, walimu wenye uzoefu wanapaswa kuajiriwa ili kuwafundisha mabinti wadogo katika maajabu na siri za jikoni. Ujuzi wa kazi za nyumbani una thamani isiyokadirika kwa kila mwanamke. Kuna familia zisizo na idadi ambazo furaha yao imevunjwa kwa kutokuwa na ufanisi kwa mke na mama. Sio muhimu sana kwamba binti zetu wajifunze upakaji rangi, kazi ya kupendeza kama kutarizi, kushona vitambaa, muziki, au hata kutafuta cube root kwenye mahesabu au sanaa za kuongea au kuuliza maswali kwa umbuji, kama vile wao kujifunza jinsi ya kukata, kutengeneza, na kurekebisha mavazi yao wenyewe, au kuandaa chakula kwa namna nzuri, bila ya kukoboa au kusindika na kukifanya kiwe na ladha tamu. Wakati msichana mdogo anapofikisha umri wa miaka tisa au kumi, anapaswa kuchukua sehemu yake ya kawaida katika kazi za nyumbani, na kadri awezavyo anapoendelea kujifunza, yeye anapaswa kuwajibishwa kwa jinsi anavyojifanyia kazi zake. Huyo alikuwa ni baba mwenye busara, ambaye, alipoulizwa alikusudia nini kufanya kwa mabinti zake, akajibu, “Ninakusudia kuwaweka chini ya mama yao bora, ili wajifunze sanaa ya kutumia muda, na kufaa kuwa wake na mama, viongozi wa familia, na wenye manufaa kwa jamii.” {FEsw 74.31}

Kufua nguo kwa mtindo wa zamani kwenye ubao wa kusugulia, kufagia, kutoa vumbi, na aina ya majukumu mengine ya jikoni na bustanini, vitakuwa mazoezi muhimu kwa mabinti wadogo (wanawake vijana). Kazi muhimu za mikono kama hizi zitachukua nafasi ya mchezo wa kulenga mbao na kuzipiga kama mchezo wa gololi nyumbani (croquet), kulenga shabaha na mishale (archery), kucheza, na matumbuizo mengine ambayo hayamfai mtu yeyote. {FEsw 74.41}

Wadada wengi, waliosoma vizuri, wamehitimu kwa maksi kubwa za heshima darasani kwenye taasisi fulani za elimu, kwa aibu hawajui majukumu ya shughuli za maisha. Wana ukame wa sifa muhimu kwa ajili ya uangalizi sahihi wa familia, na hivyo kutojua umuhimu wa furaha ya familia. Wanaweza kuzungumza juu ya duru ya kuinuliwa ya mwanamke, na ya haki zake, lakini

wenyewe huanguka chini kabisa ya viwango vya kweli vya mwanamke. Ni haki ya kila binti wa Hawa kuwa ujuzi kamili wa kazi za nyumbani, na kupata mafunzo katika kila idara ya kazi za nyumbani. Kila binti (mdada kijana) anapaswa kuelimishwa sana kiasi kwamba akiitwa kushika nafasi ya mke na mama, anaweza kuongoza kama malkia katika milki yake. Anapaswa kuwa na uwezo kamili kuwaongoza na kuwaelekeza watoto wake na kuwaelekeza watumishi wake, au ikibidi, kuhudumia kwa mikono yake mwenyewe mahitaji ya nyumba yake. Ni haki yake kuelewa utaratibu wa mwili wa binadamu unavyofanya kazi na kanuni za usafi, masuala ya chakula na mavazi, kazi na burudani, na mengine mengi ambayo yanahusu ustawi wa nyumba yake. Ni haki yake kupata elimu kama hiyo ya njia bora zaidi za kutibu magonjwa ili aweze kutunza watoto wake katika ugonjwa, badala ya kuacha hazina zake za thamani mikononi mwa wauguzi asiowajua na matabibu. {FEsw 75.11}

Fikra kwamba kutojua kazi ni sifa ya maana kwa mwanaume muungwana au mdada wa kweli, ni kinyume na mpango wa Mungu katika uumbaji wa mwanadamu. Kuwa goigoi ni dhambi, na ujinga wa majukumu ya kawaida ni matokeo ya upumbavu, ambao baada ya maisha haya hivi vitavuna mazao tosha na kuleta majuto ya uchungu. {FEsw 75.21}

Wale wanaofanya kanuni yao ya maisha kuwa kumtumikia na kumheshimu Mungu watalitilia maanani na kulizingatia agizo la mtume, “Mlapo, au mnywapo, au mfanyalo jambo lo lote, fanyeni yote kwa Utukufu wa Mungu.” Wanafunzi kama hao watahifadhi uadilifu wao mbele ya majaribu, na watamaliza na kutoka shule wakiwa wenye akili iliyokuzwa vizuri, na yenye afya ya mwili na afya ya kiroho. – *The Signs of the Times, June 29, 1882.* {FEsw 75.31} *The Signs of the Times, September 28, 1882*

Kwa marejeleo ya Ziada

The Review and Herald, July 11, 1882, The Primal Object of Education.

UADILIFU WA DANIELI KATIKA JARIBU (ALIPOTAHINIWA)

Nabii Danieli alikuwa mtu wa kuheshimika na aliyejulikana sana. Alikuwa mfano ang'avu wa vile wanadamu wanavyoweza kuwa wakiunganishwa na hekima ya Mungu. Maelezo mafupi ya maisha ya mtu huyu mtakatifu wa Mungu yamesalia kwenye kumbukumbu kwa ajili ya kuwatia moyo wale ambao baadaye wataitwa kustahimili mitihani na majaribu. {FEsw 77.11}

Wakati wana wa Israeli, Mfalme wao, wakuu, na makuhani, walipochukuliwa utumwani, wanne kati ya idadi yao walichaguliwa kutumika katika nyuaywa Mfalme wa Babeli. Mmoja wao alikuwa Danieli, ambaye mapema alitoa ahadi ya uwezo wa ajabu uliokuzwa katika miaka ya baadaye. Vijana hawa wote walikuwa wazawa wa kifalme, na wanaelezwa kama "vijana wasio na mawaa, wazuri wa uso, wajuzi wa hekima, werevu kwa sababu ya maarifa yao, wenye kufahamu elimu (sayansi na mengine); na wale waliokuwa na uwezo ndani yao."Kupokea vipaji vya hali ya juu vya mateka hawa vijana, Mfalme Nebukadneza aliazimia kuwatayarisha kujaza nyadhifa muhimu katika ufalme wake. Ili wakastahili kabisa maisha yao mahakamani au nyuani mwa Mfalme, kulingana na desturi za Mashariki, walipaswa kufundishwa lugha ya Wakaldayo, na kufanyiwa hivyo kwa muda wa miaka mitatu kwa mafunzo kamili ya kimwili na ya kiakili. {FEsw 77.21}

Vijana katika shule hii ya mafunzo hawakukubaliwa tu kuwa katika nyumba ya kifalme, lakini iliamriwa kwamba wanapaswa kula nyama, na kinywaji cha divai, vitokavyo katika meza ya Mfalme. Katika Haya yote Mfalme alizingatia kuwa hakuwa tu akitoa heshima ya ukuu au kubwa juu yao, lakini kuwaandalia maendeleo yaliyo bora zaidi kimwili na kiakili ambayo yanaweza kupatikana. {FEsw 77.31}

Miongoni mwa aina ya vyakula (kwenye butfet) vilivyowekwa mbele ya Mfalme kulikuwa na nyama ya nguruwe na vyakula vingine vilitangazwa si vya kuliwa kwa vile vilikuwa najisi kwa sheria ya Musa, na ambavyo Waebraia walikuwa wamekatazwa waziwazi kula. Hapa ni pale Daniel aliletwa kwenye mtihani mzito. Je, azingatie mafundisho ya baba zake katika habari ya vyakula na vinywaji, na kumkosea Mfalme; na pengine kupoteza si cheo chake tu bali hata maisha yake pia? Au anapaswa kupuuza amri ya Bwana, na kuhifadhi kibali/kukubaliwa kwake na Mfalme, na hivyo kupata faida kubwa za kiakili na zaidi kusifiwa kwa udanganyifu na kujipendezekeza kwa matarajio ya kidunia? {FEsw 77.41}

Daniel hakusita kwa muda mrefu. Aliamua kusimama kidete katika uadilifu wake, akiacha matokeo yawe vile yatakavyokuwa. "Aliazimu moyoni mwake ya kuwa hatajitia unajisi kwa chakula cha Mfalme, wala kwa divai aliyokunywa." {FEsw 78.11}

Kuna wengi kati ya wanaodai kuwa Wakristo leo ambao wameamua kuwa Danieli alikuwa amezidi kwa kuwa na umaalumu sana au kujali mambo madogomadogo kiasi hicho, na wangemwona mwenye ufinyu wa mawazo na shabiki wa dini au hata pengine mtu mwenye ubaguzi. Wanadai kuwa suala la kula na kunywa ni la athari kidogo sana kuhitaji msimamo huo, –msimamo ule ambao unahusisha kujitoa mhanga kwa kuacha kila faida ya kidunia. Lakini wale wanaofikiri hivyo siku ya hukumu wataona kuwa waligeuka kutoka katika matakwa ya Mungu yaliyo wazi, na kuweka maoni yao wenyewe kama kiwango cha mema na mabaya. Watatambua kuwa kile kilichoonekana kutokuwa na umuhimu, Mungu hakukizingatia hivyo. Maelekezo yake yanapaswa kutiiwa kwa kicho kitakatifu. Wale wanaokubali na kutii moja katika maagizo Yake kwa sababu ni rahisi kufanya hivyo au haiwagharimu chochote, wakati wanakataa mengine kwa sababu kuzingatia kwake kungehitaji kujitoa dhabihu, hushusha kiwango cha haki, na kwa kielelezo chao huwaongoza wengine kutochukulia kwa uzito sheria takatifu ya Mungu. “Bwana asema hivi” inapaswa kuwa sheria/kanuni yetu katika mambo yote.

{FEsw 78.21}

Danieli alipatwa na majaribu makali zaidi yanayoweza kumkabili kijana wa siku hizi; lakini alikuwa mwaminifu kwa mafundisho ya kidini aliyopokea katika maisha yake ya awali. Alikuwa amezungukwa na mvuto uliohesabiwa kupotosha wale ambao wangeweza kuyumba kati ya kanuni na mielekeo; lakini Neno la Mungu linamtambulisha kama mwenye tabia isiyo na dosari. Daniel hakuthubutu kutegemea nguvu zake za kimaadili. Maombi yalikuwa kwake hitaji la lazima. Alimfanya Mungu kuwa nguvu yake, na kumcha Mungu kukawa daima mbele yake katika shughuli zote za maisha yake. **{FEsw 78.31}**.

Danieli alikuwa na neema ya upole wa kweli. Alikuwa mkweli, imara, mwungana bora na mtakatifu. Alitafuta kuishi kwa amani na watu wote, huku akiwa kama mwerezi mrefu usiopinda popote pale kanuni ilipohusika. Katika kila kitu ambacho hakikukinzana na uaminifu wake kwa Mungu, alikuwa mwenye heshima na mtiifu kwa wale waliokuwa na mamlaka juu yake; lakini alikuwa na uelewa wa juu sana wa madai ya Mungu kiasi kwamba sheria za watawala wa kidunia ziliwekwa chini (zilipewa upili). Asingeshawishiwa au kupindishwa na mawazo yoyote ya ubinafsi ili kukwepa wajibu wake. **{FEsw 78.41}**

Tabia ya Danieli inawasilishwa kwa ulimwengu kama mfano wa kushangaza wa kile ambacho neema ya Mungu inaweza kufanya kwa wanadamu walioanguka kwa asili na kuharibiwa na dhambi. Kumbukumbu ya maisha yake adhimu, ya kujikana nafsi hutia shime ubinadamu wetu wa kawaida. Kutoka kwake tunaweza kukusanya nguvu ya kustahimili majaribu, na kwa uthabiti, na katika neema ya upole, kusimamia haki chini ya majaribu makali zaidi. **{FEsw 79.11}**.

Danieli angeweza kupata kisingizio chenye kusadikika cha kuondoka kwake kutoka katika umakini mkali wa kuwa na kiasi (katika kula na mengineyo); lakini

kukubaliwa na Mungu kulikuwa bora zaidi kwake kuliko upendeleo wa mwenye nguvu zaidi duniani—bora hata zaidi kuliko maisha yenyewe. Kwa kuwa kwa mwenendo wake wa adabu alipata kibali na Ashpenazi, mkuu wa matowashi, msimamizi wa vijana wa Kiebrania, Danieli aliomba kibali kwamba wasile nyama ya Mfalme au kunywa mvinyo yake. Ashpenazi aliogopa kwamba kama angetii ombi hili, angeweza kusababisha hasira ya Mfalme, na hivyo kuhatarisha maisha yake mwenyewe. Kama wengi katika siku ya leo, alidhani kwamba chakula hiki cha kawaida kingewasababishia vijana hawa kuhafifika rangi (kutonawiri) na kuwa na mwonekano wa ugonjwa, na kuwa na upungufu wa nguvu za misuli, wakati chakula cha anasa/lakshari kutoka kwa meza ya Mfalme kingewafanya kuwa wekundu* na wazuri, na ingekuza nguvu za kimwili na za kiakili.* (damu inatembea vizuri, afya na kunawiri) {FEsw 79.21}

Danieli aliomba kwamba jambo hilo liamuliwe kwa kuwajaribu kwa siku kumi, vijana wa Kiebrania katika kipindi hiki kifupi waliruhusiwa kula chakula rahisi*, wakati wenzao wakila vyakula vitamu vya Mfalme au (mapochopocho ya ikulu). Hatimaye ombi hilo lilikubaliwa, na ndipo Daniel akahisi kuhakikishiwa ushindi wa hoja/kesi yake. Ingawa alikuwa kijana, alikuwa ameona madhara ya mvinyo na maisha ya anasa juu ya afya ya kimwili na kiakili. * (Vyakula rahisi ni vile ambavyo si vya maigizo, bali alivyotoa Mungu kwetu navyo ni vitano- nafaka isiyokobolewa, jamii ya maharage, jamii ya karanga, matunda na mbogamboga, bila mikaango na madoido mengi mengi ya upishi!) {FEsw 79.31}

Mwisho wa siku kumi matokeo yalionekana kuwa kinyume na matarajio ya Ashpenazi. Sio tu katika mwonekano binafsi, bali pia katika nguvu za kimwili na nguvu za akili, wale ambao walikuwa wenye kiasi katika mazoea yao walionyesha ukuu wao kuliko wenzao waliokuwa na uchu wa kula. Kama matokeo ya jaribio hili, Danieli na wenzake waliruhusiwa kuendelea na chakula chao cha kawaida wakati wote wa mafunzo yao kwa ajili ya majukumu ya kifalme. {FEsw 80.11}

Bwana aliukubali uthabiti na kujinyima (kujikana nafsi) kwa vijana hawa wa Kiebrania, na baraka Zake zilikaa nao. "Mungu aliwapa maarifa na ujuzi katika elimu na hekima; Danieli naye alikuwa na ufahamu katika maono yote, na ndoto. "Wakati wa kumalizika muda wa miaka mitatu ya mafunzo, wakati uwezo wao na ujuzi wao vilipopimwa na Mfalme, "miongoni mwao wote hawakuonekana waliokuwa kama Danieli, na Hanania, na Mishaeli, na Azaria; kwa hiyo wakasimama mbele ya Mfalme. Na katika kila jambo la hekima na ufahamu alilowauliza Mfalme, akawaona kuwa walifaa mara kumi zaidi ya waganga na wachawi waliokuwa katika ufalme wake. " {FEsw 80.21}

Maisha ya Danieli ni kielelezo kilichovuviwa cha kile kinachojumuisha tabia iliyotakaswa. Inatoa somo kwa wote, na haswa kwa vijana. Utiifu thabiti wa sheria ya Mungu ni muhimu kwa afya ya mwili na akili. Ili kufikia kiwango cha juu zaidi cha maadili na kiakili, ni muhimu kutafuta hekima na nguvu kutoka kwa Mungu, na

kuwa na kiasi katika mazoea yote ya maisha. Katika uzoefu wa Danieli na wenzake tuna mfano wa ushindi wa kanuni juu ya majaribu ya kuendekeza uchu wa kula. Inatuonyesha kuwa kupitia kanuni za kidini vijana wanaweza kuzishinda tamaa za mwili, na kubaki wakweli kwa matakwa ya Mungu, *ingawa itawagharimu wao sadaka kubwa.* {FEsw 80.31}.

Ingekuwaje basi kama Danieli na wenzake wangepanya maridhiano pamoja na wale maofisa wa kipagani, na wangepitoa kwa shinikizo la kula na kunywa kama ilivyokuwa desturi ya Wababeli? Tukio hilo moja la kuziacha kanuni lingedhoofisha ufahamu wao wa haki (kweli) na chuki yao kwa uovu. Kuendekeza uchu wa chakula kungehusisha kutoa kafara ya nguvu za kimwili, usafi wa akili, na nguvu za kiroho. Hatua moja isiyo sahihi (dhambi) ingeongoza zingine, mpaka, muunganiko wao na mbingu ungekatwa, wangepagiliwa mblai na majaribu. {FEsw 80.41}.

Mungu amesema, “Wale wanaoniheshimu Mimi, Nami nitawaheshimu.” Wakati Daniel alipomng'ang'ania Mungu wake kwa tumaini lisiloyumba, Roho ya uwezo wa kiunabii ilikuja juu yake. Huku akielekezwa na mwanadamu katika majukumu ya maisha ya mahakama, yeye alifundishwa na Mungu Mwenyewe kusoma mafumbo na siri za siku zijazo, na hivyo kuyawasilisha kwa vizazi vijavyo, kupitia alama na mifano, mambo ya ajabu na kushangamza ambayo yangetokea wakati wa siku za mwisho.— *The Signs of the Times, September 28, 1882.* {FEsw 81.11}.

Kwa Marejeleo ya Ziada

Signs of the Times, December 14, 1882, Holiday Gifts

The Review and Herald, July 17, 1883, Young Men as Missionary Workers

Signs of the Times, March 13, 1884, Science and Revelation

Signs of the Times, March 2, 1884, Science and the Bible in Education

Signs of the Times, April 10, 1884 The Training of Children

Signs of the Times, April 17, 1884. Important Duties in Home Life.

Sura ya 9

UMUHIMU WA ELIMU.

Kusudi la kweli la elimu linapaswa kuzingatiwa kwa uangalifu. Mungu amemkabidhi kila mmoja uwezo na nguvu, ili ziweze kurudishwa Kwake zikiwa zimekuzwa na kuboreshwa. Karama Zake zote zimetolewa ili zitumike kwa kiwango cha juu zaidi. Yeye Anamhitaji kila mmoja wetu kukuza uwezo wake, na kufikia uwezo wa juu kabisa wa manufaa, ili tufanye kazi nzuri na bora kwa ajili ya Mungu, na kuwabariki wanadamu. Kila talanta tuliyo nayo, iwe ya uwezo wa kiakili, pesa, au ushawishi, ni ya Mungu, ili kwamba tuseme pamoja na Daudi (kama kiitikio), “vitu vyote vyatoka Kwako, na katika mali Yako tumekutolea. {FEsw 82.11}.

Wapendwa vijana, ni nini lengo na madhumuni ya maisha yenu? Je, una nia ya kupata elimu ili uweze kuwa na jina na cheo duniani? Je, una mawazo ambayo huthubutu kumwambia mtu, kwamba siku moja unaweza kusimama juu ya kilele cha ukuu wa kiakili; hivyo unaweza kukaa katika mabaraza ya kujadili na kutunga sheria, na kusaidia kutunga sheria kwa taifa? Hakuna baya katika matamano haya. Kila mmoja wenu anaweza kuweka alama ya umashuhuri wake. Usiridhike na mafanikio yoyote ya kawaida au wastani tu (au mbilikimo). Lenga juu, na usikwepe maumivu yoyote kufikia kiwango cha juu. {FEsw 82.21}.

Kumcha Bwana ndiko msingi wa ukuu wote wa Kweli. Uadilifu, uadilifu usioyumba, ndiyo kanuni unayohitaji kuibeba katika mahusiano yote ya maisha. Ichukue dini yako katika maisha yako ya shule, ndani ya bweni lako, katika shughuli zako zote. Swali muhimu kwako sasa ni, jinsi ya kuchagua na kukamilisha masomo yako huku ukiendelea kudumisha uimara na usafi wa tabia ya Kikristo isiyochafuliwa, inayoshikilia madai na manufaa yote ya kitambo au ya dunia chini ya madai ya juu ya Injili ya Kristo. Jenga tabia yako kama vile ungejenga nyumba thabiti, iliyo na fanicha bora. Kwa njia hiyo hiyo, fanya tabia yako kuwa imara na yenye manufaa. Ili kwamba ujihusishe na jamii na maisha yatakayokupa kujibu kusudi la Mungu katika uumbaji wako. Kama wanafunzi wa Kristo, hamjazuiliwa kujihusisha na shughuli za kitambo; lakini mnapaswa kubeba dini yenu pamoja nanyi. Haijalishi shughuli yoyote ambayo unaweza kujihusisha nayo mwenyewe, kamwe [usiendekeze wazo kwamba huwezi kutengeneza mafanikio yake bila kudhabihu kanuni.](#) {FEsw 82.31}.

Ukisawazishwa na kanuni za kidini, unaweza kupanda juu hadi kufikia urefu wowote unaoupenda. Tutafurahi kukuona wewe ukiinuka kwenye ubora wa hali ya juu juu ambako Mungu amepanga ufikie. Yesu anawapenda vijana wa thamani; na Yeye hafurahishwi kuwaona wanakua na vipaji visivyokuzwa na kuendelezwa. Wanaweza kuwa wanaume wenye nguvu, wenye kanuni thabiti, wanaofaa kukabidhiwa majukumu ya hali ya juu, na kwa ajili hiyo wanaweza kuushughulika

kihalali kila mshipa wa fahamu – (kila neva) . {FEsw 83.11}.

Lakini kamwe usifanye uhalifu mkubwa kiasi cha kuipotosha nguvu uliyopewa na Mungu kwa shetani na kuharibu wengine. Kuna watu wenye vipawa wanaotumia uwezo wao kueneza uharibifu ua mapooza ya maadili na ufisadi; lakini yote hiyo ni kupanda mbegu ambayo itazaa mavuno ambayo hawatajivunia kuyavuna. Ni jambo la kutisha kutumia uwezo tuliopewa na Mungu katika hali kama hiyo ya njia ya kutawanya uharibibu au mapooza na ole badala ya baraka katika jumuiya. Ni jambo pia la kutisha kukunja talanta tuliyokabidhiwa kwenye lesa, na kuificha duniani; kwa maana huku ni kutupilia mbali taji ya uzima. Mungu anadai utumishi wetu. Kila mtu ana wajibu wa kuubeba; na tunaweza kutimiza utume mkuu wa maisha pale tu majukumu haya yanapokubaliwa kikamilifu, na kwa uaminifu na kwa dhamira yenye utambuzi kutekelezwa. {FEsw 83.21}

Anasema mtu mwenye hekima, “Mkumbuke Muumba wako siku za ujana wako.” Lakini usifikiri kwamba dini itakufanya wewe uwe na huzuni, giza au hofu na kisha kukufungia njia yako ya mafanikio. Dini ya Kristo haihafifishi, haifyeki au kudhoofisha hata moja ya nguvu. Kamwe haikuondolei wewe uwezo kwa ajili ya kufurahia starehe yenye furaha ya kweli; haijawekwa ili kupunguza matamania yako katika maisha, au kukufanya kutojali madai ya marafiki na jamii. Haifuniki masha katika nguo za magunia; haionyeshwi kwa miguno na kuugua kwa maumivu au huzuni. Hapana, hapana; wale wanaomtanguliza Mungu katika kila jambo na kumfanya kuwa wa kwanza, wa mwisho na bora zaidi, ndio watu wenye furaha zaidi ulimwenguni. Tabasamu na mwanga wa jua haukomi nyusoni mwao. Dini haimfanyi mpokeaji kuwa mbaya, jeuri, rafu, wa hovy, asiye nadhifu, na asiye na adabu au uungwana; bali kinyume chake, humwinua na kumtukuza, husafisha ladha yake, hutakasa uamuzi wake, na kumfanya kufaa kwa jamii ya malaika wa Mbinguni na kwa makazi ambayo Yesu ameenda kuyatayarisha. {FEsw 83.31}.

Kamwe tusipoteze machoni mwetu kamwe ukweli kwamba Yesu ni chemchemi ya furaha. Hafurahii mateso au huzuni za wanadamu, bali anapenda awaone wakiwa na furaha. Wakristo wana vyanzo vingi vya furaha kwenye uwezo wao, nao wanaweza kusema kwa usahihi usio na shaka, starehe zipi ni halali na za haki. Wanaweza wakafurahia burudani kama hazitaweza kupotelewa na akili au kuidhalilisha nafsi, zile ambazo hazitawavunja moyo, na kuwaachia huzuni baada ya ushawishi wenye kuharibu hadhi yao au kuzuia njia za wao kuwa watu wenye manufaa. Kama wanaweza kumchukua Yesu pamoja nao kwenye maburudisho kokote, na kudumisha Roho ya maombi, basi wao wako salama kabisa. {FEsw 84.11}.

Mwandishi **Zaburi** anasema: “Kufafanusha Maneno yako kwatia Nuru; huwapa ufahamu mjinga.” Kama nguvu ya kutoa elimu Biblia haina mpinzani. Hakuna kazi za kisayansi ambazo zimetengenezwa vizuri kukuza akili kama tafakuri ya Kweli kuu na muhimu na masomo ya vitendo ya Biblia. Hakuna kitabu kingine ambacho

kimewahi kuchapishwa ambacho kimehesabiwa kuwa chema kutoa nguvu ya kiakili. Watu wakubwa wenye akili nyingi (genius), ikiwa hawaongozwi na Neno la Mungu katika utafiti wao, wanachanganyikiwa na kufadhaishwa; hawawezi kumfahamu Muumba wala kazi Zake. Lakini wakiweka akili katika kuushika na kuupima Ukweli wa milele, wakauita Ukweli uje kwa juhudi kwa kuvinjari vito vya Ukweli katika mgodi tajiri wa Neno la Mungu, basi akili zao hazitawahi kuwa duni na kudhoofika, na kuachwa kujikita katika mambo ya kawaida. {FEsw 84.21}.

Biblia ndiyo historia yenye mafundisho na mapana zaidi ambayo yamewahi kutolewa kwa ulimwengu. Kurasa Zake takatifu ndizo pekee zina habari halisi za uumbaji (ndipo mahali pekee tunajua kwa uhakika jinsi ulimwengu wetu na sisi tulipotoka). Humu tunaona nguvu zilizoitanda mbingu, na kuiweka misingi ya mbingu nchi.” Humu tuna historia ya Kweli ya jamii ya wanadamu, ambayo haijaathiriwa na ubaguzi au kiburi cha kibinadamu. {FEsw 84.3}.

Katika Neno la Mungu tunapata somo la fikra za ndani kabisa; Ukweli wake huamsha matarajio na matamania ya hali ya juu zaidi. Humu tunashiriki ushirika wa pamoja na wazee na manabii, na kuisikiliza sauti ya Yeye Aishiye Milele kama azungumzavyo na watu. Humu tunasugua bongo zetu kwa muda mrefu kuhusu kile malaika wanachokitafakari kwa mshangao, —Mwana wa Mungu, alivyojinyenyekeza na kuwa mbadala wetu na mdhamini, kukabiliana na mamlaka ya giza, na kupata ushindi kwa niaba yetu. {FEsw 85.11}.

Vijana wetu wana Biblia ya thamani; na ikiwa mipango yao yote na makusudi yanajaribiwa na Maandiko Matakatifu, wataongozwa kwenye njia salama. Hapa tunaweza kujifunza kile ambacho Mungu anatarajia kutoka kwa viumbe walioumbwa kwa mfano Wake. Hapa tunaweza kujifunza jinsi ya kuboresha Maisha ya sasa, na jinsi ya kupata maisha ya baadaye. Hakuna kitabu kingine kinachoweza kutosheleza maswali ya akili, na matamania ya moyo. Na kwa kuzingatia mafundisho ya Neno la Mungu, wanadamu wanaweza kuinuka kutoka kwenye vilindi vya chini kabisa vya ujinga, uharibifu na udhalilishaji na kufanywa wana wa Mungu, washirika au wenzi wa malaika wasio na dhambi. {FEsw 85.21}

Kadiri akili inavyodumu juu ya mada hizi, ndivyo itakavyoonekana kwamba kanuni zile zile hupitia mada za asili na za kiroho. Kuna upatanifu kati ya asili na Ukristo; kwa kuwa vyote viwili vina Muumbaji mmoja. Kitabu cha asili na kitabu cha Mafunuo ya Mungu vinaonyesha utendaji kazi wa nia ile ile ya kimbingu. Kuna masomo ya kujifunza katika asili; na kuna masomo, ya kina, ya dhati, na masomo muhimu sana, ya kujifunza kutoka katika kitabu cha Mungu. {FEsw 85.31}

Marafiki vijana, hofu ya Bwana ndio msingi wa maendeleo yote; ni mwanzo wa hekima. Baba yako wa Mbinguni ana madai juu yako; kwa kuwa bila wewe kuomba au kustahili kwa upande wako anakupa fadhila tele za riziki na Majaliwa Yake; na zaidi ya hii, amewapa mbingu zote katika Karama ile Moja, ile ya Mwanawe

mpendwa. Kwa kushukuru kwa karama hii isiyo na kikomo, anadai juu yako utii wa hiari. Kama mlivyonunuliwa kwa thamani, hata kwa damu ya thamani ya Mwana wa Mungu, Anahitaji kwamba utumie ipasavyo majaliwa na fursa unazozifurahia. Uwezo wako wa kiakili na kimaadili ni karama za Mungu, talanta zimewekwa kwako kama amana kwa ajili uboreshaji wenye busara, na wewe hauna uhuru wa kuziacha hizo zibungae hapo kwa kukosa kukuzwa vizuri, au zipate ulema na kuwa mbilikimo kwa kutotumiwa. {FEsw 85.41}

Ni juu yako kuamua ikiwa kama majukumu mazito yaliyo juu yako yataweza kutendwa kwa uaminifu, ikiwa juhudi zako zitaelekezwa vyema na kwa ubora zaidi. Tunaishi katika hatari za siku za mwisho. Mbingu zote zina shauku katika tabia unazojenga. Kila majaliwa na karama imetolewa kwa ajili yenu, ili mpate kuwa washirika wa tabia ya Uungu, mkiepukana na uharibifu uliomo duniani kwa sababu ya tamaa. Mu hajaachwa peke yake ili kuzishinda nguvu za uovu kwa juhudi zake za unyonge. Msaada uko karibu, na utatolewa kwa kila nafsi ambayo kwa hakika inahitaji. Malaika wa Mungu, wanaopanda na kushuka kwenye ngazi ile aliyoiona Yakobo katika maono, watasaidia kila nafsi ambayo inataka kupanda hata mpaka Mbinguni juu. Wanawalinda watu wa Mungu, na kuangalia jinsi kila hatua inavyopigwa. Wale wanaopanda njia yenye kung'aa watatunukiwa; wataingia katika furaha ya Bwana wao. {FEsw 86.11}

Umuhimu wa Elimu.

Kwa Danieli, kumcha Bwana ilikuwa mwanzo wa hekima. Aliwekwa katika nafasi ambayo majaribu yalikuwa na nguvu. Katika nyua za Mfalme, uharibifu ulikuwa kila upande; kujifurahisha nafsi, kuridhisha uchu wa chakula, kutokuwa na kiasi na ulafi, vilikuwa ni jambo kawaida kila siku. Danieli angeweza kujiunga katika mazoea yenye kudhoofisha, na yenye kupotosha ya watumishi, au angeweza kupinga ushawishi unaoelekea kuzimu. Yeye alichagua la pili. Aliazmia moyoni mwake kwamba hatapotoshwa na anasa za dhambi ambazo angekutana nazo, aliacha matokeo yawe vile ambavyo yangukuwa. Hakutaka hata kujitia unajisi kwa chakula cha Mfalme, au kwa divai aliyokunywa. Bwana alipendezwa na mwenendo ambao Danieli alifuata. Alipendwa sana na kuheshimiwa na mbingu; na kwake Mungu wa hekima alitoa ujuzi katika elimu ya Wakaldayo, na ufahamu katika maono yote na ndoto. {FEsw 86.21}

Iwapo wanafunzi wanaohudhuria vyo vyetu wangukuwa imara, na kudumisha uadilifu, ikiwa hawatashirikiana na wale wanaoenenda katika njia za dhambi, wala wasivutiwe na ushirika wao, kama Danieli, wao wangefurahia neema ya Mungu. Ikiwa wangetupilia mbali matumbuizo au burudani zisizo na faida na kuendekeza uchu ya kula, akili zao zingekuwa safi kwa ajili ya kutafuta maarifa. Na hivyo wangepata nguvu ya uadilifu ambayo ingewawezesha kubaki bila kutikiswa watakaposhambuliwa na majaribu. Ni mapambano ya kudumu kuwa macho kila wakati kupinga uovu; ila inalipa kupata ushindi mmoja baada ya mwingine juu ya nafsi na nguvu za giza. Na ikiwa vijana wamethibitishwa na kupimwa, kama ilivyokuwa kwa Danieli, ni heshima gani wanaweza kuleta kwa Mungu kwa kushikamana kwao kwa uthabiti kwenye Ukweli. {FEsw 87.11}

Tabia isiyo na doa ni ya thamani kama dhahabu ya Ofiri. Bila uadilifu safi, usiochafuliwa, hakuna awezaye kusimama kwa ukuu wowote wa kuheshimika. Lakini matamano Matakatiifu na kupenda haki hakurithishwi. Tabia haiwezi kununuliwa; lazima iundwe kwa juhudi thabiti za kupinga majaribu. Uundaji wa tabia sahihi ni kazi ya maisha yote, na ni chimbuko la tafakari ya maombi iliyunganishwa na kusudi kuu. Ubora wa tabia ulio nao lazima uwe matokeo ya juhudi yako binafsi. Marafiki wanaweza kukutia moyo, lakini hawawezi kukufanyia kazi. Kutamani, kuugua, kuota, shauku kamwe hazikufanyi kuwa mkuu au mwema. Lazima upande juu. Jifunge viuno vya akili yako, na uende kufanya kazi kwa nguvu zote za nguvu za nia yako. Ni uboreshaji wa busara wa fursa zenu, kukuza talanta zenu mlizopewa na Mungu, ambako kutawafanya ninyi kuwa wanaume na wanawake wanaokubaliwa na Mungu, na kuwa baraka kwa jamii. Hebu kiwango chako kiwe cha juu, na kwa nguvu isiyoweza kuepukika, tumia vyema talanta zako na fursa, na songa mbele, ukisukuma gurudumu hadi mwisho. {FEsw 87.21}

Je, vijana wetu watazingatia kwamba wana vita vya kupigana? Shetani na majeshi yake yamejipanga juu yao, wala hawana uzoefu kama wale waliokomaa walioupata. {FEsw 88.11}

Shetani ana chuki ya kutisha kwa Kristo, na wale aliowanunua kwa damu yake, naye hutenda kazi kwa madanganyo yote ya udhalimu. Hutafuta kwa kila namna kuwaandikisha vijana chini ya bendera yake; na anawatumia kama mawakala wake kupendekeza mashaka ya Biblia. Wakati mbegu moja ya mashaka inapopandwa, Shetani huikuza hadi ikatoa mavuno mengi. Anapoweza kumtingisha kijana mmoja kuhusiana na Maandiko, huyo mtu mmoja hataacha kufanya kazi mpaka akili zingine zitakapokuwa zimetiba chachu na mashaka kama hayo. {FEsw 88.21}

Wale wanaoendekeza mashaka watajigamba kuhusu uhuru wao akili; lakini wako mbali kiasi cha kutosha kuwa na uhuru wa Kweli. Akili zao zimejaa hofu ya kiutumwa, kwamba asije akatokea mtu dhaifu na wa juu juu kama wao wenyewe na kisha akawadhihaki. Huu ni udhaifu, na utumwa wa kidhalimu kabisa. Uhuru wa Kweli hupatikana katika utumishi wa Mungu. Utumishi Wake hautaweka juu yako kizuizi ambacho hakitaongeza furaha yako. Katika kuyazingatia mapenzi Yake, utapata amani, kuridhika moyo, na furaha kwamba huwezi kamwe kuwa nayo katika njia ya uovu na dhambi. Kisha jifunze vyema asili ya uhuru unaoutamani. Je, ni uhuru wa wana wa Mungu, wa kuwa huru katika Kristo Yesu? au unaita ubinafsi na tamaa kuwa ndio uhuru? Uhuru kama huo unaambatana na majuto mazito zaidi; ni utumwa wa kikatili zaidi. {FEsw 88.31}

Uhuru wa Kweli wa akili sio ukaidi. Huwaongoza vijana kuunda maoni yao juu ya Neno la Mungu bila kujali kile ambacho wengine wanaweza kusema au kufanya. Ikiwa ni katika makundi ya makafiri, wasiomwamini Mungu, au mafedhuli, huwaongoza kukiri na kutetea imani yao katika ile Kweli takatifu za injili dhidi ya kukusolewa, kuhojiwa, na kutaniwa na washirika wao wasiomcha Mungu. Kama wapo pamoja na hao wanaofikiri kuwa ni jambo jema kudhihirisha makosa ya wale wanaojiita Wakristo, na kisha kuidhihaki dini, maadili, na wema, uhuru wa kweli wa akili utawaongoza kwa adabu lakini kwa ujasiri kuonyesha dhihaka hiyo ni mbadala duni kwa hoja yenye Ukweli. Itawawezesha kutazama mbele zaidi ya mkosoaji na kumwona yule anayemshawishi kutenda vile, yaani adui wa Mungu na mwanadamu, na hivyo kumpinga mbele ya wakala wake. {FEsw 88.41}

Simameni kwa ajili ya Yesu, marafiki vijana, na wakati wa hitaji lako Yesu atasimama kwa ajili yako. "Mtawatambua kwa matunda yao." Ama Mungu au Shetani hutawala akili; na maisha huonesha wazi bila kukosea kuwa ni nguvu gani unayoitii. Kila mmoja ana mvuto ama kwa wema au kwa uovu. Je, ushawishi wako uko upande wa Kristo au ule wa Shetani? Wale wanaogeuka kutoka kwenye uovu hujiweka katika nguvu ya mwenye Uweza wote kwa ajili yao. Angahewa inayowazunguka si ya duniani. Kwa nguvu ya kimya ya maisha yenye mpangilio mzuri na mazungumzo ya kimbingu, wanaweza kumwasilisha Yesu kwa ulimwengu.

Wanaweza kuakisi Nuru ya Mbinguni, na kuzileta Roho kwa Kristo. {FEsw 89.11}

Ninafurahi kwamba tuna taasisi ambazo vijana wetu wanaweza kutengwa na athari za ufisadi zilizoenea sana katika shule za siku hizi. Ndugu na dada zetu wanapaswa kushukuru kwa majaliwa ya Mungu kuwa vyuo vyetu vimeanzishwa, na wanapaswa kuwa tayari kuvitegemeza kwa mali zao. Kila mvuto unapaswa kutolewa ili kuwaelimisha vijana na kuyainua maadili yao. Wanapaswa kufundishwa kuwa na ujasiri wa kimaadili kupinga wimbi la uchafuzi wa maadili katika zama hizi mbovu. Kwa kuzishikilia kwa nguvu za kimbangu, wanaweza kusimama katika jamii ili wakiumba na kutengeneza, badala ya wao kuumbwa kwa mtindo wa ulimwengu. {FEsw 89.2}

Hakuwezi kuwa na kazi muhimu zaidi kuliko elimu sahihi ya vijana wetu. Ni lazima tuwalinde, tukipigana na Shetani, ili asiye akawaondoa mikononi mwetu. Vijana wanapokuja vyuoni mwetu, wasifanywe kuhisi kuwa wameingia kwa watu wasiowajua, wasiojali Roho zao. Kunapaswa kuwa na akina baba na akina mama katika Israeli watakaozilinda Roho zao kama wale ambao lazima watatoa hesabu. Ndugu na dada, msijitenge na vijana wapendwa na kuwa na ubaridi, kana kwamba hamna wasiwasi wowote au kuwajibika kwa ajili yao. Ninyi ambao kwa muda mrefu mnakiri kuwa Wakristo mna kazi ya kufanya ili kuwaongoza kwa subira na upole katika njia sahihi. Mnapaswa kuwaonyesha kwamba mnawapenda kwa sababu wao ni washiriki wachanga zaidi wa familia ya Bwana, ambao wamenunuliwa kwa damu Yake.

Mustakabali wa jamii utatokana na vijana wa leo. Shetani anafanya jitihada za dhati usongo na kudumu ili kuvuruga/kuharibu/kuchafua mawazo na kupotosha tabia ya kila kijana; je sisi tulio na uzoefu zaidi tubaki tumesimama kama watazamaji tu tukibungaa na kisha tumuangalie akifanikisha madhumuni yake bila pingamizi/kizuizi? Hebu basi na tusimame katika nafasi zetu kama askari muhimu walio na utayari kushughulikia vijana hawa, na kwa msaada wa Mungu, tuwarejeshe watoke kwenye shimo la uharibifu. Katika ule mfano, wakati watu wamelala, adui aliwafunga mitego; wakati ninyi ndugu na dada zangu hamjashtukia kazi yake (mmejiziuka), huyo anakusanya jeshi vijana chini ya bango lake, na anatamba, kwani kwa kuwatumia, wao, anafanya na kuendeleza vita dhidi ya Mungu. . {FEsw 90.11}

Walimu katika shule zetu wana jukumu zito la kubeba. Wanapaswa wawe katika maneno na tabia kile wanachotamani wanafunzi wao wawe, wawe wanaume kwa wanawake wamchao Mungu na kutenda haki. Ikiwa wao wanafahamu njia wao wenyewe, wanaweza kuwaelekeza vijana kutembea ndani yake. Hawatawaelimisha tu katika sayansi, lakini watawafundisha kuwa na uhuru wa kimaadili, kumtumikia Yesu, na kuichukua mizigo katika kusudi Lake. {FEsw 90.21}

Walimu, fursa zenu ni zipi? Ni upendeleo ulioje kwenu wa kuunda akili na tabia

za vijana chini ya usimamizi wenu! Itakuwa furaha iliyoje kwenu kukutana nao kando ya kiti cha enzi kikubwa cheupe, na kujua kwamba mlifanya mliloweza ili kuwafanya kufaa kwa ajili ya umilele na kutokufa! Ikiwa kazi yenu itastahiki kipimo cha ile siku kuu, ni kwa jinsi gani kama muziki mtamu zaidi itasikika sikioni mwako ile baraka ya Bwana, "Vema, mtumwa mwema na mwaminifu; ingia katika raha ya Bwana wako." {FEsw 90.31}

Katika shamba kubwa la mavuno kuna kazi nyingi kwa wote, na wale wanaopuuza kufanya wawezalo, watapatikana na hatia mbele za Mungu. Hebu tufanye kazi kwa wakati na kwa umilele. Tufanye kazi kwa ajili ya vijana kwa uwezo wote ambao Mungu ametupa, Naye atabariki juhudi zetu zilizoelekezwa vyema. Mwokozi wetu anatamani kuwaokoa vijana. Angefurahi kuwaona wakizunguka kiti Chake cha enzi wakiwa wamevikwa mavazi yasiyo na mawaa ya haki Yake. Anangojea kuweka juu ya vichwa vyao taji ya uzima, na kusikia sauti zao za furaha wakijiunga katika kutoa heshima na Utukufu na ukuu kwa Mungu na Mwana-Kondoo katika wimbo wa ushindi ambao utatoa mwangwi wa kujirudiarudia katika nyua zote za Mbinguni. — *The Review and Herald, Agosti 19, 26, 1884.* {FEsw 91.11}

HATARI YA KUSOMA HADITHI ZA KUBUNI NA VITABU VYA KIKAFIRI -{FICTION, NOVELS}

Kila Mkristo, awe mkubwa au mdogo, atashambuliwa na majaribu; na usalama wetu pekee ni katika kujifunza kwa uangalifu wajibu wetu, na kisha kuufanya kwa gharama yoyote kwetu wenyewe. Kila kitu kimefanywa ili kuupata wokovu wetu, na hatuna budi kuwa tayari tu bali pia shauku ya kujifunza mapenzi ya Mungu, na kufanya mambo yote kwa Utukufu wake. Hii ni kazi ya maisha ya Mkristo. Hatajaribu kuona ni kwa kina cha chini kiasi gani, yeye anaweza kujitosa katika njia ya kutojali na kutoamini/ukafiri, na bado akaitwa au (akawa) mtoto wa Mungu; lakini atasoma ili kuona jinsi anavyoweza kuiga kwa ukaribu maisha na tabia ya Kristo. {FEsw 92.1}

Rafiki vijana, ujuzi wa Biblia utakusaidia kupinga majaribu. Ikiwa umekuwa na tabia ya kusoma vitabu vya hadithi/hekaya, Je, utatilia umakini kwa kujiuliza kama ni sawa kwako kutumia wakati na vitabu hivi ambavyo huchukua muda wako tu na kukufurahisha, lakini havikupi nguvu ya kiakili au kimaadili? Ikiwa unavisoma, na kujua kuwa huunda hamu mbaya ya riwaya za kuisimua, ikiwa zitakuongoza kutoipenda Biblia, na kuitupilia mbali, ikiwa vinakuhusisha katika giza na kukurudisha nyuma kutoka kwa Mungu, - ikiwa huu ndio mvuto vilivyo navyo juu yako, acha! Hapo hapo ulipo. Usifuate mwenendo huu wa kusoma mpaka mawazo yako yameharibika, na unakuwa hufai kwa ajili ya kujifunza Biblia, na kwa wajibu wa matendo ya maisha halisi. {FEsw 92.2}

Kazi rahisi za hadithi za kubuni hazifaidiki. Hazitoi ujuzi wa Kweli; hazivutii kusudi kubwa na jema; haziwashi katika moyo hamu ya dhati ya usafi; haziichochei nafsi kwa ajili ya njia ya haki. Kinyume chake, huchukua muda ambao unapaswa kutolewa kwa majukumu ya shughuli za maisha na kwa utumishi wa Mungu, muda ambao unapaswa kutolewa kwa ajili ya maombi, kuwatembelea wagonjwa, kuwatunza wahitaji, na kujielimisha kwa ajili ya maisha yenye manufaa. Unapoanza kusoma kitabu cha hadithi, ni mara ngapi mawazo yanasimka na kudanganywa kutumbukia katika dhambi. Unawaasi wazazi wako, na kuleta usumbufu ndani ya familia kwa kupuuza majukumu rahisi yaliyoelekezwa juu yako. Na mbaya zaidi kuliko hii, maombi yamesahauliwa, na Biblia inasomwa bila kujali au kupuuzwa kabisa. {FEsw 92.3}

Kuna kundi lingine la vitabu ambalo unapaswa kuliepuka, machapisho ya waandishi makafiri kama vile Paine na Ingersoll. Haya mara nyingi husisitizwa juu yako kwa kukuchokoza na dhihaka kwamba wewe siyo shujaa, na u mwoga wa kuyasoma. Waambieni kwa ukweli wazi maadui hawa ambao wangewajaribu ninyi—kwani hakika ni maadui haswa, haijalishi wao wanaweza kujidai kuwa

marafiki zenu kwa namna nzuri namna gani—kwamba mtamtii Mungu, na kuichukua Biblia kuwa mwongozo wako. Waambie kwamba una hofu ya kusoma vitabu hivi; kwamba imani yako katika Neno la Mungu sasa ni dhaifu bado, nawe unaitaka iongezeke na kuimarishwa badala ya kupungua; na kwamba unakataa kuwa na uhusiano wa karibu na baba wa uongo. {FEsw 93.1}

Nawaonya nyinyi kusimama imara, na kamwe msifanye kitendo kibaya, bora kabisa kuitwa mwoga kulikoni kutenda dhambi. Usiruhusu dhihaka, vitisho, maneno ya dharau, kukushawishi kukiuka dhamiri yako hata kidogo, na hivyo kufungua mlango ambapo Shetani anaweza kuingia na kuidhibiti akili. {FEsw 93.2}

Msijiruhusu wenyewe kufungua vifuniko vya kitabu ambacho kinatia shaka. Kuna mvuto wa kuzimu yaani Jehanamu katika fasihi ya Shetani. Ni betri yenye nguvu ambayo kwayo inaruararua imani rahisi ya kidini. Kamwe usijisikie kuwa una nguvu za kutosha kusoma vitabu vya kikafiri; kwani vina sumu kama ya kansa. Haviwezi kukufanyia lolote jema, na hakika vitakudhuru. Katika kuvisoma, unavuta mvuke unaonuka wa kuzimu/Jehanamu. Vitabu hivi vitakuwa katika nafsi yako kama kijito cha maji kilichoharibika (chenye ufisadi), kikichafua akili, na kuiweka katika msitu ulioshonana na unaofanya watu wapotee na mashaka, na pia kuifanya akili kuwa ya kidunia na ya tamaa za kimwili. Vitabu hivi vimeandikwa na watu ambao Shetani huwatumia kama mawakala wake; na kwa njia hii anapanga kuichanganya akili, kuyaondoa mapenzi kutoka kwa Mungu, na kumwibia Muumba wako heshima na shukrani ambayo kazi zake zinaidai. {FEsw 93.3}

Akili inahitaji kufundishwa na kuzoezwa, na matamania yake kudhibitiwa na kusalimishwa chini ya mapenzi ya Mungu. {FEsw 94.1}

Badala ya kuwa kufanywa kuwa mbilikimo na kulemazwa kwa kujilisha maovu ya takataka ambazo Shetani hutoa, inapaswa kuwa na chakula bora, ambacho itakipa nguvu na uimara. {FEsw 94.2}

Kijana Mkristo, una kila kitu cha kujifunza. Unapaswa uwe mwanafunzi mwenye kupendezwa na/wa Biblia; lazima utafute, ukilinganisha Andiko kwa Andiko. Ikiwa ungemfanyia Bwana wako wema na huduma inayokubalika, ungejua anachohitaji. Neno Lake ni mwongozo wa uhakika; ikiwa linasomwa kwa uangalifu/umakini, kutakuwa hakuna hatari ya kuangukia chini ya nguvu za majaribu yanayowazunguka vijana, na kuwaminya. — *The Youth's Instructor, September 10, 1884.* {FEsw 94.3}

Kwa marejeleo ya ziada

The True Object of Education, Signs of the Times, September 18, 1884

The Benefits of Industry, Signs of the Times, October 9, 1884

Science Falsely So—Called, Signs of the Times, November 6, 1884, November 13,

Sura ya 11

SHULE ZA WAEBRANIA WA KALE

Taasisi za jamii ya wanadamu hupata mifano yake bora katika Neno la Mungu. Kwa zile zenye kuelimisha (kutoa mafunzo), hasa, maagizo na vielelezo havikosekani. Masomo yenye faida kubwa, hata katika hiki kizazi cha maendeleo ya elimu, yanaweza kupatikana katika historia ya watu wa Mungu wa kale. {FEsw 95.1}

Bwana alijiwekea Mwenyewe elimu na mafundisho ya Israeli. Uangalizi Wake haukuzingatia mambo yao ya kidini tu. Bali kila ambacho kiliathiri ustawi wao wa kiakili au kimwili, kilikuwa pia kitu cha umakini kwa mbingu, na kikaja kwao kama jambo la sheria ya Kimbingu. {FEsw 95.2}

Mungu aliwaamuru Waebrania kuwafundisha watoto wao matakwa Yake, na kuwafahamisha utendaji Wake wote kwao (na kuhusiana Kwake nao). Nyumbani na shuleni vilikuwa kitu kimoja. Badala ya midomo ya yule wasiyemjuai, mioyo yenye upendo ya baba na mama ilipaswa kutoa mafundisho kwa watoto wao. Makusudi, na Maoni ya Mungu yalihusishwa katika matukio yote ya maisha ya kila siku katika makazi ya nyumbani. Matendo makuu ya Mungu katika ukombozi wa watu Wake yalisimuliwa kwa ufasaha/umbuji na kicho na hofu ya Mungu. Kweli kuu za majaliwa ya Mungu na za maisha yajayo zilisitizwa juu ya akili vijana. Akili ikazoezwa kwa kulelewa na Ukweli, wema, na uzuri. {FEsw 95.3}

Kwa matumizi ya mifano na vielelezo mafunzo yaliyotolewa yalioneshwa, na hivyo kudumishwa kwa uthabiti zaidi kwenye kumbukumbu zao. Kupitia hizi taswira za uhuishaji, mtoto, karibu tangu utoto, alianzishwa kujua siri kuu, hekima, na matumaini ya baba zake, na kuongozwa katika njia ya kufikiri na kuhisi na kutazamia, iliyokuwa juu zaidi ya vitu vinavyoonekana na vya kupita, kwa vile visivyoonekana na vya milele. {FEsw 95.4}

Kutokana na elimu hii vijana wengi wa Israeli walitoka wakiwa na nguvu katika mwili na akili, wepesi wa kuona na wenye nguvu ya kutenda, moyo ulio tayari kama udongo mzuri kwa ajili ya ukuaji wa mbegu ya thamani, akili iliyofunzwa kumwona Mungu katika Maneno ya ufunuo na matukio ya asili. Nyota za Mbinguni, miti na maua ya kondeni, Milima mirefu, vijito vya maji vinavyobubujika, vyote vilizungumza naye, na sauti za manabii, zilizosikika katika nchi yote, vilipata mwitikio katika moyo wake. {FEsw 96.1}

Hayo ndiyo yalikuwa mafunzo ya Musa katika nyumba ya kibanda cha hali ya

chini Gosheni; ya Samweli, kwa Hana mwaminifu; ya Daudi, katika mlima wa uliokuwa Bethlehemu; ya Danieli, kabla ya matukio ya uhamisho yaliyomtenga na nyumba ya baba zake. Hayo, pia, yalikuwa maisha ya Kristo mwanzoni mwa miaka yake ya awali, katika nyumba duni ya Nazareti; ni mafunzo kama hayo ambayo mtoto Timotheo alijifunza kutoka kwa midomo ya mama yake Yunike, na bibi yake Loisi, zile Kweli za Maandiko Matakatifu. {FEsw 96.1}

Majaliwa na mikakati zaidi ilifanywa kwa ajili ya mafundisho ya vijana na watoto, kwa kuanzishwa kwa “Shule ya Manabii.” Ikiwa kijana alikuwa na matamania kupata ujuzi bora zaidi wa Maandiko, kuchunguza kwa undani zaidi mafumbo ya ufalme wa Mungu, na kutafuta hekima kutoka juu, ili apate kuwa mwalimu katika Israeli, shule hii ilikuwa imefunguliwa ajili yake. {FEsw 96.2}

Kupitia kwa Samweli shule za manabii zilianzishwa kutumika kama wigo/kizuizi dhidi ya upotofu uliosheheni kutokana na mwenendo wenye uovu wa wana wa Eli, na kukuza ustawi wa watu kimaadili na kiroho. Shule hizi zilithibitisha kuwa baraka kubwa kwa Israeli, wakiikuza ile haki iinuayo taifa, na kuwapatia watu waliostahili kutenda katika kumcha Mungu, kama viongozi na washauri. Katika kutimiza jambo hili, Samweli alikusanya makundi ya vijana ambao walikuwa wacha Mungu, wenye akili na juhudi za kujifunza. Hawa waliitwa wana wa manabii. Walimu walikuwa sio tu wale wenye ujuzi wa Ukweli wa kimbingu, bali wale ambao waliufurahia ushirika na Mungu, na walikuwa wamepokea majaliwa maalum ya Roho Wake. Walifurahia heshima na imani ya watu, vyote viwili, kwa ajili ya kujifunza na ucha Mungu. {FEsw 96.3}

Katika siku za Samweli kulikuwa na shule mbili kati ya hizi, moja huko Rama, nyumba ya nabii, na ya pili huko Kiriath-yearimu, ambapo Sanduku la Agano baadaye lilikuwa. Mbili ziliongezwa siku za Eliya, huko Yeriko na Betheli, na nyingine zikasimikwa baadaye huko Samaria na Gilgali. {FEsw 96.4}

Wanafunzi wa shule hizi walijikimu kimaisha kwa kazi za mikono yao wenyewe kama wakulima na mafundi. Katika Israeli hili halikuwa la ajabu au la kudhalilisha; ilizingatiwa kuwa ni uhalifu kuruhusu watoto kukua katika ujinga kama hawakuweza kujua kufanya kazi zenye kuleta manufaa. Katika kutii amri ya Mungu, kila mtoto alifundishwa stadi fulani, hata kama alipaswa kuelimishwa kwa ajili ya ofisi takatifu. Walimu wengi wa kidini walijisaidia kimaisha wenyewe kwa kazi za mikono. Hata baadaye sana katika wakati wa Kristo, hili halikuonwa kuwa ni kitu chenye kudhalilisha kwamba Paulo na Akila walipata riziki kwa kazi yao ya kutengeneza mahema. {FEsw 97.1}

Masomo makuu yalikuwa ya sheria ya Mungu pamoja na maagizo aliyopewa Musa, historia takatifu, muziki mtakatifu, na ushairi. Lilikuwa lengo kuu la masomo yote kujifunza mapenzi ya Mungu na majukumu ya watu Wake. Katika kumbukumbu za historia takatifu zilifuatiliwa nyayo za Yehova. Kutoka kwa

matukio ya zamani yalitolewa masomo ya kufundishia siku zijazo. Ukweli mkuu uliowekwa kwa mifano na vivuli vya sheria ya Musa uliletwa mbele yao, na imani ilishika kipaumbele kikuu katika mfumo huo wote, Mwana-Kondoo wa

Lugha ya Kiebrania ilikuzwa kama lugha takatifu zaidi katika dunia. Roho ya uchaji Mungu ilithaminiwa. Si tu wanafunzi walifundishwa wajibu wa maombi, lakini walifundishwa jinsi ya kuomba, jinsi ya kumwendea Muumba wao, jinsi ya kuishi kwa imani Kwake, na jinsi ya kuelewa na kutii mafundisho ya Roho wake. Akili zilizotakaswa zilitoa katika nyumba ya hazina ya Mungu mambo mapya na ya kale.

{FEsw 97.4}

Sanaa ya nyimbo takatifu na sauti ilikuzwa kwa bidii. Hakuna nyimbo za kijinga au za kipuuzi zilizofanana na zile za kwenye nyumba za dansi, zilizosikika, wala wimbo usio na heshima au umakini ambao ungemtukuza mwanadamu na kukengeusha umakini wake kutoka kwa Mungu; bali ni Zaburi takatifu za sifa kwa Bwana Muumba, zikilitukuza Jina Lake na kusimulia matendo Yake ya ajabu. Hivyo muziki ulifanywa kutumika kwa kusudi takatifu, kuinua mawazo kwenda kwenye kile kilichokua safi na adhimu na chenye kuinua, na kuamsha katika nafsi uchaji na shukrani kwa Mungu. {FEsw 98.1}

Kuna tofauti kubwa kiasi gani kati ya shule za nyakati za zamani, chini ya usimamizi wa Mungu Mwenyewe, na taasisi zetu za kisasa za kujifunza. Hata kutoka shule za theolojia wanafunzi wengi huhitimu na ujuzi mdogo wa Mungu na Ukweli wa kidini kuliko wakati walipokuwa wakiingia. Shule chache zitapatikana ambazo hazitawaliwi kwa kanuni, semi na desturi za ulimwengu. Kuna shule chache ambazo upendo wa mzazi Mkristo kwa watoto wake hautakabiliwa na uchungu wa kukatisha tamaa akiwaweka humo. {FEsw 98.2}

Ni nini huhusisha ubora wa hali ya juu wa mifumo yetu ya elimu? Je, ni katika fasihi ya kitambo wanayosema ni bora na ambayo imejazwa ndani ya vichwa vya wana wetu? Je, ni katika kufanikiwa kwa mapambo ya elimu ambayo binti zetu hupata kwa kutoa afya au nguvu za kiakili kama sadaka? Je, ni jambo la kweli kwamba mafundisho ya kisasa kwa ujumla yametenganishwa na Neno la Kweli, na injili ya wokovu wetu? Je, ubora mkuu wa elimu maarufu inayopendwa na wengi unajumuisha kutazama maeneo ya matawi binafsi, kando ya uchunguzi wa kina unaohusisha uchunguzaji wa Maandiko, na ujuzi wa Mungu na wa maisha yajayo? Je, inahusisha kuingiza akilini mwa vijana dhana za uhuru, maadili, na haki za ukafiri? Je, ni salama kuwakabidhi vijana wetu chini ya uangalizi wa wale viongozi vipofu wanaosoma Maandiko matakatifu kwa shauku ndogo sana kuliko wanavyodhihirisha shauku yao kwa waandishi wa kale wa Ugiriki na Rumi? {FEsw 98.3}

“Elimu,” asema mwandishi, “inazidi kuwa mfumo wa kuwatongoza watu” Kuna

ukosefu wa kuhuzunisha wa kujizuia na nidhamu yenye busara. Hisia za uchungu zaidi, tamaa zisizoweza kudhibitiwa, zinaenziwa na mwenendo wa walimu wasio na hekima na wasiomcha Mungu. Akili ya vijana zinasisimuliwa kirahisi, na kunywa katika uasi kama maji. {FEsw 98.4}

Ujinga uliopo wa Neno la Mungu, miongoni mwa watu wanaokiri kuwa Wakristo, ni wa kutisha. Vijana katika shule zetu za umma wamenyang'anywa baraka za vitu vitakatifu. Mazungumzo ya juujuu, hisia na mihemko tu isiyo na maana, hupita katika mafundisho ya maadili ya kidini; lakini hukosa sifa muhimu za utauwa halisi. Haki na rehema ya Mungu, uzuri wa utakatifu, na malipo ya hakika ya kutenda haki, tabia kutisha ya dhambi, na uhakika wa adhabu; havijaingizwa kwenye akili za vijana. {FEsw 99.1}

Kuwa na mashaka juu ya imani na ukafiri, vilivyojificha ndani ya kile kinachopendeza, au kama vidokezo vya uovu, mara nyingi sana hujipenyeza kwenye vitabu vya shule. Katika baadhi ya matukio, kanuni mbovu zaidi zimepandikizwa na kukuzwa na walimu. Marafiki waovu wanawafundisha vijana masomo ya uhalifu, kuzurura, ulevi na uasherati ambao ukiutafakari unachukiza sana. Shule zetu nyingi za umma ni vitanda vinavyozaa uovu. {FEsw 99.1}

Je, vijana wetu wanaweza kulindwa vipi dhidi ya mivuto hii michafu? Lazima kuwe na shule zilizoanzishwa kwa kanuni, na kudhibitiwa na maagizo ya Neno la Mungu. Roho nyingine lazima iwe katika shule zetu, kuhuisha na kutakasa kila nyanja ya elimu. Ushirikiano wa Kimbingu lazima utafutwe kwa bidii. Na hatutautafuta bure. Ahadi za Neno la Mungu ni zetu. Tunaweza kutarajia uwepo wa mwalimu wa kimbingu. Tunaweza kumwona Roho wa Bwana akisambaa kama katika shule za manabii, na kila kitu kushiriki utakaso wa kimbingu. Sayansi itakuwa basi, kama ilivyokuwa kwa Danieli, wakala au msaidizi wa kidini; na kila juhudi, ya kwanza hadi ya mwisho, itakuwa ikielekea wokovu wa mwanadamu, nafsi, mwili, na Roho, na Utukufu wa Mungu kupitia kwa Kristo. — *The Signs of the Times, Agosti 13, 1885.* {FEsw 99.2}

Kwa marejeleo ya ziada

Christian Courtesy, The Review and Herald, September 1, 1885

The Teacher and His Work, The Review and Herald, September 22, 1885

UCHUMBA NA NDOA

Katika siku hizi za hatari na ufigadi, vijana wanaingizwa katika mitihani na majaribu mengi. Wengi wanasafiri kwa meli katika bandari iliyo ya hatari. Wanahitaji rubani; lakini wanadharau/wanasonya kukubali msaada unaohitajika sana, wanaona kuwa wao wana uwezo wa kuongoza mtumbwi wao wenyewe, na hawatambui kwamba wanakaribia kugonga mwamba uliofichwa ambao unaweza kuwasababisha kuvunja merikebu yao ya imani na furaha yao pia. Wanagubikwa na mahaba ya udanganyifu kwenye suala la uchumba na ndoa, na mzigo wao mkuu ni kuwa na njia yao wenyewe. Katika hili, ambapo ndiyo kipindi muhimu zaidi cha maisha yao, wanahitaji mshauri asiyekosea, na mwongozo usio na dosari. Haya mawili watayapata katika Neno la Mungu. Isipokuwa ni wanafunzi wenye bidii wa Neno hilo, watafanya makosa makubwa, ambayo yatawaharibia furaha yao na ile ya wengine, kwa maisha ya sasa na yajayo. {FEsw 100.1}

Kuna tabia ya watu wengi kuwa na msukumo na ukaidi. Hawajatii shauri la hekima la Neno la Mungu; hawajapambana na nafsi, na kuupata ushindi wa thamani; na kiburi chenye nia isiyopinda kimewatoa katika njia ya wajibu na utiifu. Yaangalieni maisha yenu ya zamani, marafiki vijana, na mfikirie kwa uaminifu mwenendo wenu katika Nuru ya Neno la Mungu. Je! mmependa kujali kwa uangalifu wajibu wenu kwa wazazi wenu ambao Biblia inauamuru? Je, umemtendea wema na kumpenda mama ambaye amekutunza tangu utotoni? Je, Umezingatia matamano yake, au umeleta uchungu na huzuni moyoni mwake kwa kutekeleza tamaa na mipango yako mwenyewe? Je, Ukweli unaodai umeutakasa moyo wako, umeilainisha na kuitiisha nia yako? Ikiwa sivyo, unayo ya kazi karibu nawe ya kufanya ili kurekebisha makosa yaliyopita. {FEsw 100.2}

Biblia inawasilisha kiwango kamili cha tabia. Kitabu hiki kitakatifu, kilichovuviwa na Mungu, na kilichoandikwa na wanadamu watakatifu, ni mwongozo kamili katika hali zote za maisha. Kinaweka waziwazi majukumu ya vijana na watu wazima. Kikifanywa kuwa mwongozo wa maisha, mafundisho yake yataiongoza Roho kuelekea juu. Itainua akili, itaboresha tabia, na kutoa amani na furaha moyoni. Lakini vijana wengi wamechagua kuwa washauri na viongozi wao wenyewe, na wamechukua kesi zao kwenye mikono yao wenyewe. Hawa wana haja ya kujifunza kwa karibu zaidi mafundisho ya Biblia. Katika kurasa Zake watapata wazi wajibu wao kwa wazazi na ndugu zao katika Imani. Amri ya tano inasomeka hivi: “Waheshimu baba yako na mama yako, siku zako zipate kuwa nyingi katika nchi upewayo na Bwana, Mungu wako.” Tena twasoma, “Enyi watoto, watiini wazazi wenu katika Bwana, maana hii ndiyo haki.” Moja ya ishara kwamba tunaishi katika siku za mwisho ni kwamba Watoto

hawawatii wazazi, wasio na shukrani, na wasio watakatifu. Neno la Mungu limejaa maagizo, mashauri na nasaha zinazoamrisha na kufundisha heshima kwa wazazi. Linasisitiza kwenye akili za vijana wajibu mtakatifu wa kuwapenda na kuwatunza *wazazi wao* ambao wamewaongoza katika uchanga, utoto na ujana hadi kuwa wanaume na wanawake, wale ambao sasa wako katika kiwango kikubwa katika kuwategemea kwa amani na furaha. Biblia haitoi sauti inayosita au isiyoeleweka juu ya jambo hili; walakini, mafundisho Yake yamekuwa yakipuuzwa sana. {FEsw 100.3}

Vijana wana masomo mengi ya kujifunza, na moja la muhimu zaidi ni kujifunza kujijua wao wenyewe. Wanapaswa kuwa na mawazo sahihi ya wajibu na majukumu yao kwa wazazi wao, na wanapaswa daima kujifunza katika shule ya Kristo kuwa wapole na wanyenyekevu wa moyo. Wakati wanapaswa kuwapenda na kuwaheshimu wazazi wao, pia wanapaswa kuheshimu maamuzi ya watu wenye uzoefu ambao wameunganishwa nao kanisani. Kijana anayefurahia ushirika na kuwa na urafiki na msichana bali hajulikani kwa wazazi wake msichana, yeye hafanyi sehemu ya uungwana wa Kikristo kwake au kwa wazazi wake. Kupitia mawasiliano na msichana na kukutana naye kwa siri anaweza kupata kuwa na ushawishi juu ya akili yake; lakini kwa kufanya hivyo anashindwa kudhihirisha uungwana na uadilifu wa nafsi ambao kila mtoto wa Mungu ataumiliki. Ili kutimiza malengo yao, wanatenda sehemu ambayo ni ya udanganyifu na iliyo wazi na kulingana na kiwango cha Biblia, na kuthibitisha kuwa si wakweli kwa wale wanaowapenda na kujaribu kuwa walinzi waaminifu juu yao. Ndoa zilizofungwa chini ya ushawishi kama huo haziko kulingana na Neno la Mungu. Yule ambaye angemwondoa binti kutoka katika wajibu, ambaye angeyachanganya mawazo yake ya amri za Mungu zilizo wazi na chanya kuhusu kuwatii na kuwaheshimu wazazi wake, si mtu ambaye angekuwa mwaminifu kwa majukumu ya ndoa. {FEsw 101.1}

Swali linaulizwa, "Jinsi gani kijana aisafishe njia yake?" na jibu linatolewa, "Kwa kutii, akilifuata Neno Lako." Kijana anayeifanya Biblia kuwa mwongozo wake, yabidi asikosee njia ya wajibu na ya usalama. Kitabu hicho kilichobarikiwa kitamfundisha kuuhiifadhi uadilifu wa tabia yake, kuwa mkweli, na kutofanya udanganyifu. "Usiibe" iliandikwa na chanda cha Mungu juu ya mbao za mawe; Lakini, bado ni kwa siri kiasi gani wizi wa mapenzi unafanywa na kutolewa udhuru. Uchumba wa udanganyifu huendelezwa, mawasiliano ya faragha hutunzwa mpaka mapenzi ya mtu asiye na ujuzi na asiyejua mambo yanaweza kukua, na kwa kiasi fulani anaondolewa kutoka kwa wazazi wake na kuwekwa kwa yule ambaye anaonyesha kwa njia ile ile anayofuata kuwa hastahili upendo wake. Biblia inakosoa kila aina ya kutokuwa na uaminifu, na kudai haki itendeke katika hali zote. Yeye aifanyaye Biblia kuwa kiongozi wa ujana wake, na Nuru ya njia yake; atatii mafundisho yake katika mambo yote. Hatakiuka yodi moja au nukta ya sheria ili kutimiza jambo lolote, hata

kama ni lazima kujitoa dhabihu kubwa katika katika matokeo. Ikiwa anaiamini Biblia, anajua kwamba baraka ya Mungu haitakuwa juu yake ikiwa ataondoka kutoka katika njia kali ya uadilifu na maadili yaliyo bora. Ingawa anaweza kuonekana kwa wakati fulani kufanikiwa, hakika atavuna matunda ya matendo yake. {FEsw 102.1}

Laana ya Mungu iko juu ya miunganiko mingi mibaya, isiyofaa ambayo inaundwa katika kipindi hiki cha ulimwengu. Ikiwa Biblia ingeacha mambo haya katika mwanga usio wazi, wenye utusitusi, usio na uhakika, basi bila shaka wengi wa vijana wa siku hizi wanaofuatana ili kuanzisha mahusiano baina yao, wangekuwa na udhuru zaidi. Lakini matakwa ya Biblia siyo maagizo yaliyo nusu; yanadai usafi kamili wa mawazo, wa maneno, na wa vitendo. Tunamshukuru Mungu kwamba Neno Lake ni Nuru kwenye miguu yetu, na kwamba hakuna haja ya kukosea njia ya wajibu. Vijana wanapaswa wafanye shughuli kuzifuata kurasa zake na kuzingatia mashauri yake; kwani makosa ya huzuni yanafanywa kila mara kwa kuachana na maagizo Yake. {FEsw 102.2}

Kama kuna jambo lolote ambalo linapaswa kuzingatiwa kwa akili za utulivu na uamuzi usio na huruma, ni suala la ndoa. Kama kuna wakati Biblia ilihitajika kama mshauri, basi ni kabla ya kuchukua ile hatua inayowaunganisha watu maishani mwao. Lakini hisia inayotawala katika jambo hili ni kwamba hisia zinapaswa ziwe mwongozo; na katika hali nyingi sana hisia za mihemko ya mahaba huchukua usukani, na kuelekeza kwenye uharibifu fulani. Ni hapa ambapo vijana huonyesha akili ndogo kuliko jambo lingine lolote; ni hapa ambapo wanakataa watu kusemezana nao. Swala la ndoa linaonekana kuwa na nguvu ya kuwaroga wao. Hawajisalimishi kwa Mungu. Hisia zao zimefungwa, na husonga mbele kwa usiri, kana kwamba wanaogopa mipango yao itaingiliwa na mtu fulani. {FEsw 103.1}

Njia hii ya kisirisiri ambayo uchumba na ndoa huendeshwa, ndiyo sababu ya kiasi kikubwa cha masaibu na huzuni, ambayo kiwango chake kamili kinajulikana kwa Mungu pekee. Juu ya mwamba huu maelfu wamevunja meli za Roho zao. Wale wanaojiita Wakristo wenye maadili, ambao maisha yao yamewekewa alama ya uadilifu, na wanaoonekana kuwa wenye busara kwa kila jambo lingine, hufanya makosa ya kutisha hapa. Wanadhihirisha utashi uliodhamiriwa ambao hauwezi kubadilika. Wanavutiwa sana na hisia ya kibinadamu na misukumo kiasi kwamba hawana hamu ya kuichunguza Biblia na kuwa katika uhusiano wa karibu na Mungu. Shetani anajua ni vipengele gani anayopaswa kushughulika nayo, na anatamba kwa hekima yake ya jehanamu/kuzimu iliyo na mbinu za udanganyifu mbalimbali wa kunasa Roho kwa uharibifu wao. Anaangalia kila hatua ambayo inachukuliwa, na kutoa mapendekezo mengi, na mara nyingi mapendekezo haya yanafuatwa badala ya shauri la Neno la Mungu. Wavu huu laini uliofumwa, wenye hatari umetayarishwa kwa ustadi ili kuwanasa makinda na wasio na tahadhari. Mara nyingi anaweza kujificha chini ya vazi la Nuru; lakini wale ambao wanakuwa waathirika wake,

wanajichoma wenyewe kwa huzuni nyingi. Kama matokeo, tunaona majeruhi ya uharibifu wa wanadamu kila mahali. {FEsw 103.2}

Ni lini vijana wetu watakuwa na hekima? Muda gani aina hii ya kazi itaendelea? Je! watoto watashauriana tu na matamania na mielekeo yao wenyewe bila kujali ushauri na uamuzi wa wazazi wao? Baadhi wanaonekana kutokuwa na mawazo juu ya matakwa au matamania ya wazazi wao, wala kuzingatia uamuzi wao uliokomaa. Ubinafsi umefunga mlango wa mioyo yao ili wasiwe na mapenzi kwa wazazi wao kama watoto. Akili za vijana zinahitaji kuamshwa kuhusiana na jambo hili. Amri ya tano ni amri pekee ambayo imeambatanishwa na ahadi, lakini inaangaliwa kirahisi, na hata kupuuzwa kwa njia inayoonekana chanya kwa madai ya kumjali rafiki wa kiume au kike wanayehusiana naye kimahaba. Kudharau upendo wa mama, kutoheshimu uangelizi wa baba ni dhambi zinazosimama zikiwa zimeandikwa dhidi ya vijana wengi. {FEsw 104.1}

Kama kuna moja ya makosa makubwa yanayohusiana na jambo hili na ni sheria waliyoweka, ni kwamba vijana hawa wasio na uzoefu wa mapenzi, lazima wasisumbuliwe; kwamba lazima kusiwe na kuingiliwa katika uzoefu wao wa kimahaba/kimapenzi. Kama kuna somo ambalo lilihitaji kutazamwa kwa kila upande, ni hili. Msaada wa uzoefu wa wengine, na utulivu, upimaji wa makini wa jambo katika pande zote, ni wenye umuhimu chanya. Ni jambo ambalo linachukuliwa kirahisi mno na watu wengi. Mfanyeni Mwenyezi Mungu na wazazi wenu wamchao Mungu kwenye washauri yenu, marafiki vijana. Ombeni juu ya jambo hilo. Pimeni kila hisia, na mhemko na tazameni kila ukuaji wa tabia ndani ya yule mnayefikiria kuunganisha naye hatima ya maisha yenu. Hatua mnayokaribia kuichukua ni moja ya hatua muhimu zaidi katika maisha yenu, na haipaswi kuchukuliwa kwa haraka. Ingawa mnaweza kupenda, msipende kwa upofu. {FEsw 104.2}

Chunguzeni kwa makini ili kuona kama maisha yenu ya ndoa yatakuwa ya furaha, au ya kutokupatana na huzuni. Hebu swali hili lije moyoni mwako, Je! Umoja huu utanisaidia kuelekea Mbinguni? Je! atakuongezea upendo wangu kwa Mungu? Je! Itaongeza duru ya manufaa yangu katika maisha haya? Kama tafakari hizi hazina kizuizi, basi, katika kicho kwa Mungu songa mbele. Lakini hata kama uchumba umeingiwa bila uelewa kamili wa tabia ya yule unayekusudia kuungana naye, basi usifikirie kwamba uchumba unalifanya hilo liwe hitaji chanya kwako kujitwika nadhiri ya ndoa, na kujihusisha maishani na mtu ambaye huwezi kumpenda na kumheshimu. Kuwa makini sana jinsi unavyoingia katika uchumba wa masharti; lakini ni bora, bora zaidi, kuvunja uchumba kabla ya ndoa, kuliko kutengana baadaye kwa talaka kama wengi wanavyofanya. {FEsw 104.3}

Upendo wa kweli ni mmea unaohitaji kukuzwa. Hebu kila mwanamke ambaye anayetamani kuwa na unyumba wenye raha na amani, yule apendaye kuepuka taabu za baadaye na huzuni, ajiulize maswali haya kabla hajatoa ukubali wake wa

mapenzi, Je, mpenzi wangu anaye mama? Tabia ya mama yake ikoje? Je, anautambua wajibu wake kwa mamaye? Je, anazingatia haja na furaha yake? Ikiwa hamjali na kumheshimu mama yake, Je! Ni kweli atadhihirisha heshima na upendo, wema na usikivu kwa mke wake? Je! Wakati shani ya harusi itakapokwisha, atadumu kunipenda? Je, atakuwa mvumilivu kwa makosa yangu, au atakuwa mkosoaji, mkali, na dikteta? Mapenzi ya kweli yatapuza makosa mengi; upendo hautayaona. {FEsw 105.1}

Kwa kawaida vijana wanaamini sana mihemko na misukumo. Hawapaswi kujitoa kwa urahisi mno kwa hiyo, wala kutekwa kirahisi sana na kutwaliwa moyo kwa mapenzi ya nje. Uchumba, kama unavyofanywa katika zama hizi, ni mpango wa udanganyifu na unafiki, ambao adui wa Roho ana mengi ya kufanya kuliko Bwana. Busara nzuri ya kawaida au akili ya kuzaliwa, inahitajika hapa kuliko popote; lakini ukweli ni kwamba, ina kidogo cha kufanya katika suala hilo la uchumba. {FEsw 105.2}

Kama watoto wangefahamiana zaidi na wazazi wao, ikiwa wangewatumainia, na kuwatwika furaha na huzuni zao wangejiokoa na kutoka kwenye huzuni nyingi za baadaye. Wakati wanafadhaika kujua ni njia gani iliyo sawa, hebu walianike jambo hilo wazi kama wanavyolijua mbele ya wazazi wao, na kuwaomba ushauri. Je! ni akina nani wanaoweza kwa uzuri sana kutaja hatari zao kama wazazi wale wanaomcha Mungu? Ni nani anayeweza kuelewa tabia zao za kipekee vizuri na mahesabu yake kama wazazi wao? Watoto ambao ni Wakristo watastahi juu ya kila baraka za duniani upendo na kibali cha wazazi wao wanaomcha Mungu. Wazazi wanaweza kuwahurumia watoto, na kuwaombea na kuomba pamoja nao ili Mungu awalinde na kuwaongoza. Zaidi ya yote watawaelekeza kwa Rafiki na Mshauri wao asiyeshindwa kamwe, ambaye anaguswa na hisia za madhaifu yao. Yeye aliyejaribiwa katika mambo yote kama sisi, lakini bila kutenda dhambi, anajua jinsi ya kuwasaidia hao wanaojaribiwa, na wanaomjia kwa imani. — *The Review and Herald, January 26, 1886.* {FEsw 105.3}

Kwa Marejeleo ya ziada

Home Education, The Youth's Instructor, April 21, 1886

Christian Recreation, The Review and Herald, May 25, 1886.

UMUHIMU WA MAFUNZO KATIKA KAZI YA MUNGU.

Kazi ya mtendakazi anayefanya kazi za nguvu na za mikono sio ndogo au isiyo ya muhimu. Ikiwa anajitoa mwenyewe kwa aina yoyote ya kazi, shughuli yake ya kwanza ni kujiangalia yeye mwenyewe, na baadaye, Mafundisho ya imani. Anapaswa kuuchunguza moyo wake mwenyewe na kuiondoa dhambi; ndipo anapaswa kukifuata kile Kielelezo, Kristo Yesu, daima mbele yake kama mfano wake. Hatakiwi kujisikia yuko huru kuunda njia yake kama appendavyo kwa mwelekeo wake mwenyewe. Yeye ni mali ya Yesu. Amechagua wito wa juu zaidi, na kutoka katika kazi hiyo, maisha yake yote ya baadaye lazima yawe na rangi na umbo la huo utume. Ameingia katika shule ya Kristo, na huko apaswa apate maarifa ya Kristo na utume Wake, na ile kazi anayopaswa kuifanya. Nguvu zake zote lazima ziletwe chini ya udhibiti wa Mwalimu mkuu. Kila kitivo cha akili, kila kiungo cha mwili, lazima kiwekwe katika hali ya afya kadri iwezekanavyo; ili kazi ya Mungu isiwe na alama za upungufu wa tabia yake. {FEsw 107.1}

Kabla ya mtu kuwa tayari kuwa mwalimu wa ile Kweli kwa wale walio gizani, lazima kwanza awe tayari kuwa mwanafunzi. Lazima awe tayari kushauriwa. Hawezi kuweka mguu wake juu ya ngazi ya tatu, ya nne, au ya tano ya maendeleo kabla hajaanza ngazi ya kwanza au hatua ya kwanza. Wengi wanahisi kwamba wanafaa kwa kazi hiyo, wakati wao hawajui chochote kuhusu hiyo kazi. Kama hawa wanaruhusiwa kuanza kufanya kazi kwa kujiamini, watashindwa kupokea maarifa yale ambayo ni fursa yao kuyapata, na watajipatia bahati mbaya ya kuhangaika na matatizo mengi ambayo watakuwa hawajajiandaa kwayo. {FEsw 107.2}

Sasa, kwa kila mtendakazi kuna fursa ya kujiboresha, na anapaswa kufanya kila jitihada kuelekea lengo hilo. Wakati wowote juhudi maalum zinapopaswa kufanywa katika mahali muhimu, mfumo mzuri uliopangwa vema wa kazi unapaswa kuanzishwa, ili wale wanaotaka kuwa wainjilisti wa vitabu na wauza vitabu, na wale ambao tayari wamefanyia mazoezi ya kufundisha Biblia katika familia, waweze kupokea maelekezo yanayohitajika. Wale walio watenda kazi wanapaswa pia kuwa wanafunzi, na wakati mhudumu anafanya kazi katika Neno na mafundisho, wao hawapaswi kuzurura hovyoyote na kuwa wavivu, kana kwamba hakuna kitu katika hotuba wanachopaswa kusikia. Hawapaswi kumchukulia mzungumzaji kama msemaji tu, bali kama mjumbe kutoka kwa Mungu kwa wanadamu. Mielekeo kibinafsi na chuki zisiruhusiwe kuwaathiri wakati wa kusikiliza. Kama wote wangeiga mfano wa Kornelio, na kusema, “Basi sasa sisi sote tupo hapa mbele za Mungu, kuyasikia yote uliyoamriwa na Mungu,” wangepaidika sana kwa mahubiri wanayoyasikia. {FEsw 107.3}

Wanapaswa kuunganishwa na shule zetu za mafunzo ya utume kwa wale

ambao wanataka kuingia mashambani kama watendakazi. Wanapaswa kuhisi kwamba lazima wawe kama wanagenzi wa kujifunza kazi ya kufanya kazi ya uongoaji wa Roho. Kazi katika shule hizi inapaswa kuwa tofauti tofauti. Usomaji wa Biblia unapaswa kufanywa kuwa na umuhimu wa kwanza, na wakati huo huo kuwe na mfumo wa mafunzo ya akili na adabu/tabia ili wajifunze kuwafikia watu kwa njia iliyo bora zaidi. Wote wanapaswa kujifunza jinsi ya kufanya kazi kwa busara, uungwana na kwa adabu, na kwa Roho wa Kristo. Hawapaswi kamwe kuacha kuwa wanafunzi, bali wanapaswa kuendelea kuuchimba Ukweli na kwa njia bora za kufanya kazi, kama ambavyo wangechimba dhahabu iliyofukiwa. {FEsw 108.1}

Hebu wote wanaoanza kazi waamue kwamba hawatapumzika hadi wamekuwa watendakazi wa daraja la kwanza. Ili kufanya hivi, akili zao zisiruhusiwe kupeperuka kutokana na hali na kufuata mihemko, bali ni lazima kufungwa kwa uhakika kwenye kusudi, wakifanya kazi wawezavyo kuufahamu Ukweli katika namna yake yote. {FEsw 108.2}

Watu wenye uwezo wamefanya kazi kwa hasara kubwa kwa sababu akili yao haikuwa na nidhamu ya kazi hiyo. Kwa Kuona hitaji la watendakazi, waliingia kwenye nafasi, na ingawa wanaweza kuwa wameitimiza vizuri sana, katika hali nyingi hata 1/10 haikuweza kutimizwa wanapokamilisha, jambo ambalo lisingekuwa hivyo kama wangukuwa na mafunzo sahihi mwanzoni. {FEsw 108.3}

Wengi wanaofikiria kujitoa kwa ajili ya utumishi wa Mungu, hawahisi hitaji la mafunzo yoyote maalum. Lakini wale wanaohisi hivyo ndio hasa wanaohitaji zoezi gumu la mafundisho. Ni wakati ambao wana ujuzi mdogo wa wao wenyewe na wa kazi ndio wanajihisi kuwa na uwezo na sifa zote kuifanya. Wanapojua zaidi, ndipo wanahisi ujinga wao na upungufu wao. Wanapoitoa mioyo yao kwa ajili ya uchunguzi wa karibu, ndipo wataona mengi ndani yao yaliyo tofauti na tabia ya Kristo, ndipo watapaza sauti, “Ni nani anayefaa kwa mambo haya?” na kwa unyenyekevu mkubwa watakazana kila siku kujiweka karibu na uhusiano na Kristo. Kwa kuisulubisha nafsi, wanaiweka miguu yao katika njia ambayo Kristo anaweza kuwaongoza. {FEsw 109.1}

Kuna hatari kwamba mtendazi asiye na uzoefu, wakati akitafuta kufaa mwenyewe kwa ajili ya kazi, atajisikia imara kujiweka penye aina yoyote ya nafasi, ambapo pepo mbalimbali za Mafundisho ya imani zitavuma juu yake. Hili hawezi kulifanya bila hatari ya upotevu wa nafsi yake. Majaribu na mitihani vikija juu yake, Bwana atatoa nguvu ya kuyashinda; lakini wakati mtu anapojiweka mwenyewe katika njia ya majaribu, mara nyingi hutokea kwamba Shetani kupitia mawakala wake huendeleza mihemko na hisia zake kwa namna hiyo ya kutatanisha na kutotuliza akili. Kwa ushirika na Mungu na kuchunguza sana Maandiko, mtendakazi anapaswa kujiimarisha mwenyewe kabisa kabla hajaingia mara kwa mara katika kazi ya kufundisha wengine. Yohana, mwanafunzi mpendwa, aliamishwa hadi

Patmo ya upweke, ili aweze kutengwa na fujo zote, na hata kutoka kwa kazi aliyoipenda, ili Bwana apate kuzungumza naye na kufungua mbele yake matukio ya kufunga historia ya dunia hii. Palikuwa ni nyikani ambapo Yohana Mbatizaji alijifunza ujumbe ambao alipaswa kuubeba, kuandaa njia kwa Yeye ajaye. {FEsw 109.2}

Lakini zaidi ya yote inapaswa kusesitizwa kwa watu binafsi ambao wameamua kuwa watumishi wa Mungu, kwamba lazima wawe watu walioongoka. Moyo lazima uwe safi. Utauwa ni wa muhimu kwa maisha haya na yale yatakayokuja. Mtu asiye na nguvu, na tabia njema hakika hatakuwa mwenye heshima kwa ajili ya ile Kweli. Kijana anayefikiria kufanya kazi pamoja na Mungu anapaswa kuwa safi moyoni. Katika midomo yake, katika kinywa chake, hakupaswi kuwa na hila. Mawazo yanapaswa kuwa safi. Utakatifu wa maisha na tabia ni jambo adimu, lakini hili kwa mtendakazi ni lazima awe nalo ama sivyo hawezi kujifunga nira pamoja na Kristo. Kristo anasema, “Bila Mimi ninyi hamwezi kufanya neno lo lote.” Kama wale wanaokusudia kufanya kazi kwa mema ya wengine na kwa wokovu wa wanadamu wenzao watategemea hekima yao wenyewe, watashindwa. Ikiwa wataendekeza maoni ya unyenyekevu wao wenyewe, basi ni sahili vya kutosha kumwamini Mungu na kutarajia msaada Wake. “Usizitegemee akili zako wenyewe. Katika njia zako zote umkiri Yeye, Naye atayanyoosha mapito yako.” Ndipo tunayo fursa ya kuongozwa na Mshauri Mwenye hekima, na ufahamu utaongezeka kutolewa kwa mtafutaji wa dhati haswa wa ile Kweli, na maarifa. {FEsw 109.3}

Sababu ya kwa nini hatuna watu tena wenye upana na ujuzi mwingi, ni kwa sababu wanaitumainia hekima yao wenyewe yenye kikomo na kutafuta kuweka umbo lao wenyewe juu ya kazi, mahali pa kuwa na umbo la Mungu. Hawasali kwa bidii na kuendeleza mawasiliano ya karibu kati ya na Mungu na Roho zao, ili waweze kuitambua sauti Yake. Wajumbe wa Nuru watakuja kuwasaidia wale wanaohisi kuwa wao ni udhaifu, bila uangalizi ya ulinzi wa Mbinguni. Neno la Mungu lazima lichunguzwe zaidi, na kuletwa katika maisha na tabia, iliyotengenezwa kwa kiwango cha haki ya Mungu, kile alichokiweka katika Neno Lake. Ndipo akili itapanukaa na kuimarika, na kuwa na utakatifu kwa kushika mambo ambayo ni ya milele. Ingawa ulimwengu haujali na una ubaridi katika ujumbe wa onyo na rehema unaotolewa kwao katika Biblia, watu wa Mungu, wanaona mwisho uko karibu, wanapaswa kuwa imara zaidi na kujitoa zaidi, na kufanya kazi kwa bidii zaidi, ili wapate kuzitangaza sifa Zake Yeye aliyewaita kutoka gizani waingie katika Nuru Yake ya ajabu. {FEsw 110.1}

Maarifa yana nguvu, ama kwa wema au kwa ubaya. Dini ya Biblia ndio kinga pekee kwa wanadamu. Umakini mwingi huelekezwa kwa vijana katika kipindi hiki, ili waingie mahali kwa uzuri, kudansi, na kupiga vyombo vya muziki. Lakini elimu hii imewanyimwa, kumjua Mungu na kuyajua madai Yake. Elimu ambayo ni ya kudumu hadi katika umilele, iko karibu kabisa kupuuzwa kwamba ni ya kizamani na

isiyohitajika. Kuelimisha watoto kubeba kazi ya kujenga tabia kwa ajili ya mema yao ya sasa, amani na furaha yake ya sasa, na kuiongoza miguu yao katika njia iliyowekwa kwa waliokombolewa na Bwana ili kuenenda kwayo, hiyo huonekana kuwa jambo la kawaida na, kwamba, sio la muhimu. Ili watoto wako waingie malango ya mji wa Mungu kama washindi, lazima waelimishwe kumcha Mungu na kuzishika amri Zake katika maisha ya sasa. Ni hawa ambao Yesu ametamka wana baraka: “Heri wazishikao amri Zake, wawe na haki ya kuuendea huo mti wa uzima, na kuingia mjini kwa milango Yake.” {FEsw 111.1}

Baraka imetamkwa juu ya wale wanaoendana na mapenzi ya Mungu yaliyofunuliwa katika Neno Lake. Biblia ni wakala mkuu mikononi mwa Mwandishi Wake ili kuimarisha akili. Inafungua bustani ya akili kulimwa na Mkulima wa Mbinguni. Ni kwa sababu kuna umakini mdogo sana unaowekwa kwa kile ambacho Mungu anasema na kwa kile ambacho Mungu anataka, ndio maana kuna wachache sana ambao wana mzigo wowote wa kufanya kazi ya umishonari, hivyo ni wachache sana ambao wamekuwa wakipita chini ya utendaji wenye jitihada, wakitoa katika utumishi kila nguvu ili kuzoezwa na kuimarishwa kufanya huduma ya juu zaidi kwa ajili ya Mungu. {FEsw 111.2}

Juhudi dhaifu sana zinafanywa kuunganisha shule zetu na za watu wa mataifa mbalimbali ambao wanataka kuunganishwa pamoja nao, ili wapate elimu na kufaa kwa kazi hiyo bora takatifu sana, iliyoinuliwa sana, na inayofika mbali kwa mvuto wake. Siku za ujinga Mungu alizona. Lakini Nuru iliyoongezeka inaangaza; Nuru na fursa za kuelewa Ukweli wa Biblia ni nyingi, ikiwa watendakazi watafungua tu macho ya ufahamu wao. Ukweli lazima uenee. Utume wa kigeni na wa nyumbani unahitaji wakristo kamili kushiriki katika kazi za kimishonari. Misheni katika miji yetu ya ndani na nje ya nchi inawataka watu waliojazwa na Roho wa Kristo, ambao watafanya kazi kama Kristo alivyofanya kazi. — *The Review and Herald, Juni 14, 1887.* {FEsw 111.3}

ELIMU SAHIHI KWA VIJANA

Malaika wa tatu anawasilishwa akiwa anaruka katikati ya mbingu, kuonyesha kwamba ujumbe unapaswa kuenea kotekote katika marefu na mapana ya dunia. Ni ujumbe mzito na adhimu zaidi kuwahi kutolewa kwa wanadamu, na wote wanaoungana na kazi wanapaswa kwanza kuhisi hitaji lao la elimu, na mchakato kamili wa mafunzo kwa ajili ya kazi, kwa kuzingatia manufaa yao ya baadaye; na kunapaswa kuwepo mikakati iliyopangwa na juhudi zilizopitishwa kwa ajili ya uboreshaji wa kundi hilo ambalo linatarajia kuunganishwa na matawi yoyote ya kazi. Kazi ya utumishi haiwezi na haipaswi kukabidhiwa kwa wavulana, na pia kazi ya kutoa mafundisho ya Biblia isikabidhiwe kwa wasichana wasio na uzoefu, eti kwa sababu wanatoa huduma zao, na wako tayari kuchukua nafasi za majukumu,ila wana upungufu wa uzoefu wa kidini, pia hawana elimu na mafunzo ya kina. Lazima wathibitishwe ili kuona kama watastahimili jaribu; na isipokuwa kuna uendelezaji imara, uangalifu wa kanuni ya kuwa vile ambavyo Mungu angetaka wawe, hawataweza kuwasilisha kwa usahihi mambo na kazi yetu kwa wakati huu. Kuna lazima kuwa pamoja na dada zetu wanaohusika katika kazi katika kila misheni, wenye uzoefu wa kina, uliopatikana kutoka kwa wale ambao wamepata uzoefu, na wanaofahamu namna na njia za kufanya kazi. Shughuli za umishenari daima huaibishwa kwa ukosefu wa watendakazi wa kundi sahihi la akili, na ibada na uchaMungu ambao watawasilisha kwa usahihi imani yetu. {FEsw 113.1}

Kuna idadi ya ambao wanapaswa kuwa wamisionari ambao kamwe hawajaingia shambani, kwa sababu wale waliunganishwa nao kanisani au katika vyuo vyetu, hawajauhisi mzigo wa kufanya kazi nao, kuweka mbele yao madai ambayo Mungu anayo juu ya nguvu zote, wala hawawaombe na hawaombi pamoja nao; na kipindi cha matukio ambayo huamua mipango na mwendo wa maisha hupita, imani yao inakandamizwa; mivuto mingine na vishawishi vinawavuta, pamoja na majaribu ya kutafuta vyeo vya kidunia wanavyotamani, wanadhani, vitaleta pesa, na kuwapeleka

na mkondo wa dunia. Vijana hawa wangeweza kuokolewa kwa ajili ya huduma kupitia mikakati iliyopangwa vizuri. Kama makanisa katika sehemu mbalimbali yanafanya wajibu wao, Mungu atafanya kazi pamoja na juhudi zao kwa Roho Wake, na atawapa watu waaminifu kwa ajili ya huduma. {FEsw 113.2}

Shule zetu zinapaswa kuwa za kuelimisha na shule za mafunzo; na ikiwa wanaume na wanawake wanapomaliza shule wakiwa wamestahiki kwa ajili ya huduma ya umishonari, lazima watakuwa wameweka juu yao ukubwa wa kazi, na huo utauwa wa vitendo lazima uletwe katika uzoefu wao wa kila siku, ili kufaa kwa ajili ya mahali popote pa manufaa ulimwenguni kwetu, ama kanisani, ama katika shamba kuu la maadili la Mungu, linalohitaji/linalotoa mwito sasa kwa watendakazi

katika nchi za kigeni. {FEsw 114.1}in

Vijana lazima waguswe moyo na wazo kwamba wanaaminika. Wana hisia ya heshima au (kusimama kwa uadilifu), na wanataka kuheshimiwa, na hivyo ni haki yao. Ikiwa wanafunzi wanapata hisia kwamba hawawezi kutoka au kuingia, kuketi mezani, au kuwa popote, hata katika vyumba vyao; isipokuwa wamelindwa, jicho la kukosoa liko kwao na kuwaripoti, kutakuwa na ushawishi wa kukatisha tamaa, na mara zote hakutakuwa na furaha ndani yake. Uelewa huu wa uangalizi unaoendelea ni zaidi ya uangalizi wa wazazi, na mbaya zaidi; kwa wazazi wenye busara wanaweza, kwa busara, mara nyingi kutambua kwa undani waone akili isiyotulia inavyofanya kazi chini ya matamanio ya ujana, au chini ya nguvu za majaribu, na kuweka mipango yao ya kufanya kazi ili kukabiliana na maovu. Lakini uangalizi huu wa mara kwa mara si wa asili, na huleta maovu ambayo inataka kuyaepuka. Afya ya ujana inahitaji mazoezi, uchangamfu, angahewa ya furaha, ya kupendeza inayowazunguka kwa ajili ya maendeleo na kukua kwa afya ya kimwili na tabia linganifu. {FEsw 114.1}

Neno la Mungu lazima lifunguliwe kwa vijana, lakini vijana hawapaswi kuruhusiwa kuwa na nafasi ya kufanya hivi. Wale ambao lazima wawe na jicho juu yao mara kwa mara ili kuhakikisha tabia zao ni nzuri, watahitaji kutazamwa katika nafasi yoyote ambapo wanaweza kuwa. Kwa hivyo uumbaji wa tabia katika ujana unaotakana na mfumo huo wa mafunzo, ni wa kuharibu kabisa. Kusudieni kulenga kwenye nidhamu ya kiakili na kujenga hisia za maadili mema (haki) na tabia. {FEsw 114.2}

Masomo kwa ujumla yanapaswa kuwa machache na yaliyochaguliwa vizuri, na wale ambao huhudhuria vyo vyetu wanapaswa kuwa na mafunzo tofauti na yale ya shule za kawaida za siku hizi. Wawe Wamendishwa kwa ujumla Kanuni za Kikristo, ikiwa wana wazazi wenye hekima na wanaomcha Mungu. Neno la Mungu limeheshimiwa katika nyumba zao, na mafundisho Yake yamekuwa sheria ya nyumbani. Wamelelewa katika malezi na maonyo na maagizo ya injili, na wanapokuja shuleni, elimu na mafunzo haya haya yanapaswa kuendelea. Maagizo ya ulimwengu na kawaida zake, mila na desturi za ulimwengu, si mafundisho wanayoyahitaji; bali wanapaswa kuona kwamba walimu mashuleni wanajali Roho zao, kwamba wanafanya uamuzi kwa ajili ya hali yao njema kiroho, na dini ndiyo iwe kanuni kuu inayofunzwa; kwani kumpenda na kumcha Mungu ndio mwanzo wa hekima. Vijana walioondolewa katika mazingira au angahewa la nyumbani, kutoka katika utawala wa nyumbani na malezi ya wazazi, ikiwa wataachiwa wao wenyewe kupendekeza na kuchagua marafiki zao, watakutana na hali tete au migogoro ya dharura katika historia yao isiyopendelea uchaMungu au kanuni. {FEsw 115.1}

Kisha, popote shule inapoanzishwa, kuwe na mioyo yenye jotojoto

ya ukarimu na kupendezwa na vijana wetu. Baba na mama wenye wenye huruma zenye jotojoto wanahitajika, na wenye mawaidha mema, na uzuri wote unaowezekana kuletwa katika maisha ya kidini. Iwapo wapo wanaorefusha shughuli za kidini hadi kuchosha wanaacha hisia kwenye akili ya vijana, ambazo zitahusisha dini na yale yote ambayo ni makavu, yasiyo ya kijamii au kirafiki, na yasiyopendeza. Na vijana hawa hawawezi kiwango chao kuwa cha juu zaidi, lakini kanuni dhaifu na zenye viwango vya chini huharibu wale ambao wangelifundishwa ipasavyo, watakuwa si baraka tu kwa kazi, lakini pia kwa kanisa lote na kwa ulimwengu. Kujitoa kwa bidii na ari, na uchaMungu wa matendo ni muhimu kwa mwalimu. Ibada ya asubuhi na jioni katika kanisa, na Mikutano ya Sabato, inaweza kuwa, bila uangalizi wa kila mara na isipokuwa iwe inahuishwa na kupewa uwezo na Roho wa Mungu, inakuwa yenye urasmi sana, feki/bandia, mikavu, isiyo na urafiki au jotojoto na mchanganyiko mchungu na kisha kwa vijana, inakuwa mzigo mzito zaidi, ulio na mvuto kidogo katika mlolongo wa ratiba zote za shule. Mikutano yetu ya kijamii {social} inapaswa kusimamiwa kwa mipango na vifaa vya kuifanya sio tu ya kupendeza kwa vipindi bali pia yenye mvuto wa kupendeza. {FEsw 115.2}

Hebu wale wenye uwezo wa kuwafundisha vijana wajielimishe wenyewe katika shule ya Kristo, na wajifunze masomo ya kuwasilisha kwa vijana. Kujitoa wakfu kwa dhati, na kwa kina, kunakotoka moyoni kunahitajika. Upungufu au ufinyu wowote unapaswa kuepukwa. Hebu walimu waondokane na hadhi yao ya juu na kuwa kitu kimoja na watoto katika mazoezi yao na burudani, bila kuondoa hisia la jukumu kwamba ni wewe ndiye unawaangalia, na sio kuzungukazunguka ukionyesha hadhi yako kwa kifahari, kana kwamba u mtu aliyevaa sare za askari akiwalinda. Uwepo wako unaumba kitu katika tabia na mwenendo wao. Umoja wako na wao husababisha moyo wako kudunda kwa mapenzi mapya. Vijana wanahitaji huruma, mapenzi na upendo, vinginevyo watakunja moyo. Roho ya "Sijali mtu yeyote kwani hakuna mtu anayenijali" zitawatawala, na ingawa wanakiri kuwa wafuasi wa Kristo, wana shetani anayewajaribu katika njia yao, na wako katika hatari ya kukatishwa tamaa, kuwa vuguvugu, na kurudi nyuma kutoka kwa Mungu. Ndipo wengine wanaona kuwa ni wajibu wao kuwalaumu, na kuwatendea kwa ubaridi pasipo urafiki, kana kwamba vijana hawa ni wabaya kuliko walivyo kihalisia, lakini wachache, na pengine hakuna kabisa, wanaohisi wana wajibu binafsi na jitihada maalum ya kufanya katika kuwasaidia na matengenezo, na kuwaondolea hisia mbaya ambazo zimejengwa juu yao. {FEsw 116.1}

Wajibu wa mwalimu ni mzito na mtakatifu, lakini hakuna sehemu ya kazi ambayo ni muhimu zaidi kuliko kuwatunza vijana kwa huruma, kujali, na kwa maombi ya upendo, ili wahisi kwamba tuna urafiki nao. Kwanza pata ujasiri wao yaani wakuamimi, na kisha unaweza kuwaongoza, kuwadhibiti, na kuwalea/kuwafundisha kwa urahisi. Kanuni takatifu za Ukristo wetu

lazima ziletwe katika maisha yetu. Wokovu wa wanafunzi wetu ni maslahi ya juu zaidi yaliyokabidhiwa kwa mwalimu anayemcha Mungu. Yeye ni mtendakazi wa Kristo, na juhudi zake maalum na zilizoazimiwa zinapaswa kuokoa Roho kutoka katika upotevu na kuzileta kwa Yesu Kristo. Mungu adai hili mikononi mwa walimu. Kila mmoja anapaswa kuishi maisha ya uchaMungu, ya wakfu, ya usafi, na ya juhudi kubwa katika utekelezaji wa kila wajibu. Ikiwa moyo unawaka moto kwa upendo wa Mungu, kutakuwa na upendo safi, ambao ni wa muhimu; maombi yatakuwa ya bidii, na maonyo ya uaminifu yatatolewa. Puuzia haya, na Roho zilizo chini ya usimamizi wako zitakuwa hatarini. Itakuwa afadhali au bora kutumia muda kidogo katika hotuba ndefu, au katika kusoma, na kushughulikia majukumu haya yaliyopuuzwa. {FEsw 116.2}

Baada ya juhudi zote hizi, walimu watatambua kwamba chini ya usimamizi wao baadhi watakuza tabia zisizo za kanuni. Kama matokeo, wamelegea katika maadili, mara nyingi, wakiwa wenye ukatili na malezi ya wazazi yaliyopuuzwa. Na walimu waliofanya kila wawezalo wanaweza wakashindwa kuwaleta vijana hawa katika maisha ya usafi na utakatifu; na baada ya ustahimilivu katika nidhamu, kazi ya upendo, na maombi ya bidii, watakunja moyo na wale ambao waliwategemea sana. Na zaidi ya hayo, lawama za wazazi zitawafikia wao kwa sababu hawakuwa na uwezo wa kupinga ushawishi wa mfano wao wenyewe na mafunzo yasiyo ya busara. Mwalimu atakatishwa tamaa baada ya kutekeleza wajibu wake. Lakini lazima afanye kazi, akimwamini Mungu kufanya kazi pamoja naye, akisimama kwenye wadhifa wake kiume/dede, na kufanya kazi kwa imani. Wengine wataokolewa kwa ajili ya Mungu, na mvuto wao waliookolewa utainuliwa na kuwaokoa wengine. Hebu mchungaji, mwalimu wa shule ya Sabato, na walimu katika vyuo vyetu waunganishe moyo na Roho na kukusudia katika kazi ya kuokoa vijana wetu kutoka kwenye maanguko

Wengi wamehisi, "Ni vema tu, kwani haijalishi kama hatuweki umakini sana kuhusu kujielimisha kikamilifu," na basi kiwango cha chini cha maarifa kinaweza kukubaliwa. Na sasa wakati wanaume wanaofaa au kustahili wanatakiwa kujaza nafasi mbalimbali za amana, huwa adimu; wakati wanawake wanapotafutwa wenye akili zilizosawazishwa vizuri, wasio na elimu duni, bali wenye elimu inayofaa au kustahili kwa nafasi yoyote ya utumishi na amana, wanakuwa hawapatikani kwa urahisi. Kinastahili kufanywa hata kile ambacho ni kidogo, kinafaa kufanywa vyema. Ingawa dini inapaswa kuwa kipengele cha kuenea katika kila shule, haitasabisha kupungua kwa ufanisi katika kujipatia elimu. Ingawa hali ya kidini yapasa kuenea shuleni, ikieneza mvuto wake, itawafanya wote ambao ni Wakristo wa kweli wahisi hitaji lao la ndani zaidi la maarifa kamili, ili waweze kutumia vyema vitivo ambavyo Mungu amewapa. Huku wakikua katika neema na katika kumjua Bwana wetu Yesu Kristo, wataugua kwa hisia za kutokukamilika kwao, na watatafuta daima kupanua nguvu zao za akili, ili wapate kuwa Wakristo wenye akili. {FEsw 117.2}

Bwana Yesu anadharauliwa, na kuvunjiwa heshima na mawazo au miundo duni kwa upande wetu. Yeye ambaye hahisi madai ya sheria ya Mungu, na hupuuza kushika kila kanuni, huikiuka sheria yote. Yeye ambaye ameridhika kwa kiasi fulani kufikia kiwango cha haki, na hashindi kila adui wa kiroho, hatakutana na mipango ya Kristo. Anaudunisha mpango mzima wa maisha yake ya kidini, na kudhoofisha tabia yake ya kidini, na chini ya nguvu ya majaribu kasoro zake za tabia hupata ukuu, na uovu hushinda. Tunahitaji kuwa na subira na kuazimia kufikia kiwango cha juu iwezekanavyo. Tabia na mawazo yaliyodumishwa awali lazima yashindwe katika kesi nyingi, kabla hatujaweza kufanya maendeleo katika maisha ya kidini. Mkristo mwaminifu atazaa matunda mengi; yeye ni mtendakazi; hatatenda kwa uvivu, lakini atavaa silaha zote kupigana vita vya Mungu. Kazi muhimu ni kushinda ladha, uchu wa kula, tamaa, nia, shauku, misukumo,

kufikia kiwango kikubwa cha maadili ya haki. Kazi lazima ianzie moyoni. Huo lazima uwe safi, kulingana na mapenzi ya Kristo, la sivyotamaa ya mwili inayojiinua, au tabia fulani au kasoro fulani, itakuwa nguvu ya kuharibu. Mungu hata kubali chochote pungufu ya moyo wote. {FEsw 118.1}

Mungu anataka walimu katika shule zetu kuwa na ufanisi. Kama wameendelea katika ufahamu wa kiroho, watahisi kwamba ni muhimu wasiwe na upungufu katika maarifa ya sayansi. Ucha Mungu na uzoefu wa kidini ndio msingi wa elimu ya Kweli. Lakini mtu yeyote asijisikie kwamba bidii kwenye mambo ya kidini pekee yatosha kwenye umuhimu wa uelimishaji. Wakati hawahitaji uchaMungu kidogo, pia wanahitaji elimu kamili ya sayansi. Hili itawafanya sio tu kuwa Wakristo wazuri, wa vitendo, bali litawawezesha kuwaelimisha vijana, na wakati huo huo wao watakuwa na hekima ya Mbinguni kuwaongoza kwenye chemchemi ya maji ya uzima. Ni Mkristo analenga kufikia viwango vya juu zaidi kwa kusudi la kuwatendea wengine mema. Maarifa yakiambatana na na tabia kama ya Kristo itamfanya mtu kuwa Nuru kweli kwa ulimwengu. Mungu hufanya kazi pamoja na juhudi za wanadamu. Wote ambao hufanya bidii yote ya kutimiza wito na kuchaguliwa kwao kuwa hakika, watahisi kwamba ujuzi wa juu juu hautawafaa kwa nafasi zenye manufaa. Elimu iliyosawazishwa na uzoefu thabiti wa kidini, inamfaa mtoto wa Mungu kufanya kazi yake aliyoiwekewa kwa uthabiti, kwa uimara, na kwa ufahamu. Kama mtu anajifunza kwa Yesu na kuhusu Yeye, Mwalimu mkuu kuliko wote ambao ulimwengu umewahi kumjua, hatakuwa tu na tabia ya Kikristo yenye ulinganifu, bali pia na akili iliyofundishwa kufanya kazi kwa ufanisi. Akili ambazo ni nyepesi kupambanua zitaenda katika kina cha chini. {FEsw 119.1}

Mungu hataki sisi tutosheke akili yenye uvivu na isiyo na nidhamu, mawazo butu, na kumbukumbu legelege. Anataka kila mwalimu kuwa na ufanisi, wala asijisikie kuridhika na kiwango fulani cha mafanikio tu, bali kuhisi haja yake ya bidii ya kudumu katika kupata maarifa. Miili na Roho zetu ni mali ya Mungu, kwa kuwa amezinunua. Ametupa talanta, na amefanya iwezekanavyo kwetu kupata zaidi, ili

tuweze kujisaidia sisi wenyewe na wengine kuendelea mwelekeo wa njia ya uzima. Ni kazi ya kila mtu kuendeleza na kuziimarisha karama ambazo Mungu amemkopesha, na kufanya kazi ya bidii zaidi, kwa vitendo, katika mambo ya kitambo yaani ya dunia na ya kidini yaani ya kiroho au ya Mbinguni. Ikiwa wote watalitambua hili, ni tofauti gani kubwa tunapaswa kuiona katika shule zetu, katika makanisa yetu, na katika misheni zetu! Lakini idadi kubwa huridhika kwa ujuzi mdogo, mafanikio kidogo, alimradi yameingia kwenye rekodi ya kukubalika; na umuhimu wa kuwa watu kama Danieli na Musa, watu wenye ushawishi, wanaume ambao tabia zao zimekuwa na mapatano kwa kufanya kazi kwao kuwabariki binadamu na kumtukuza Mungu, lakini uzoefu kama huo ni wachache wamekuwa nao, na matokeo yake ni kwamba, ni wachache tu waliokuwa na utayari wa hitaji kubwa la nyakati hizi. {FEsw 119.2}

Mungu hawapuuzi watu wajinga yaani wasiojua kitu, lakini ikiwa wameunganishwa pamoja na Kristo, ikiwa wametakaswa kupitia ukweli, watakuwa wakikusanya maarifa mara kwa mara. Kwa kutumia kila nguvu kumtukuza Mungu, watakuwa na nguvu zaidi ya kumtukuza. Lakini wale walio tayari kubaki katika njia nyembamba kwa sababu Mungu alijishusha kuwakubali wakati walipokuwa huko, ni wapumbavu sana; na bado kuna mamia na maelfu ambao wanafanya jambo hili. Mungu amewapa mwili hai, na huu unahitaji utumike kila siku ili akili iweze kufikia mafanikio ya juu na juu zaidi. Ni aibu kwamba wengi huhusisha ujinga na unyenyekevu, na kwamba pamoja na sifa zote Mungu ametupa kwa ajili ya elimu, idadi kubwa bado wako tayari kubaki katika nafasi hiyo hiyo ya chini waliyokuwa nayo wakati ukweli ulipowafikia kwa mara ya kwanza. Hawakui kiakili; hawajafaa zaidi na kutayarishwa kufanya matendo makuu na mema kuliko waliposikia Ukweli mara ya kwanza. {FEsw 120.1}

Wengi walio waalimu wa ile Kweli huacha kuwa wanafunzi, huacha kuchimba, na kuchimba daima ile Kweli kama hazina iliyofichwa. Akili zao hufikia kiwango cha kawaida, cha chini; lakini hawatafuti kuwa watu wa mvuto, —si kwa ajili ya matamano ya ukuu wenye ubinafsi, bali kwa ajili ya Kristo, ili wapate kudhihirisha nguvu ya Ukweli juu ya akili. Sio dhambi kuthamini talanta ya elimu, ikiwa haijaabudiwa; lakini hakuna mtu anayepasa kutia juhudi katika kujikweza ili kuitukuza nafsi. Inapokuwa hivyo, kunakuwa na ukosefu wa hekima itokayo juu, ambayo kwanza ni safi; tena ni ya amani, yenye kusihi, iliyojaa upendo na matunda mema. {FEsw 120.2}

Misheni zilizoanzishwa katika miji yetu, ikiwa zitaendeshwa na watu ambao wana uwezo wa kusimamia kwa busara misheni kama hizo, zitakuwa taa zinazomulika kwa uthabiti, ikiangaza katikati ya giza la maadili. Ufunguzi wa

Maandiko kwa njia za usomaji wa Biblia ni sehemu muhimu ya kazi iliyunganishwa na misheni hizi; lakini watendakazi hawawezi kuishika kazi hii isipokuwa wamejiandaa kwayo. Wengi wanapaswa kufundishwa na kuzoezwa shuleni kabla hata hawajua jinsi ya kujifunza ili kuleta akili na mawazo yao chini udhibiti wa nia, na jinsi ya kutumia kwa hekima nguvu zao za kiakili. {FEsw 121.1}

Kuna mengi ya kujifunza kwetu kama watu kabla hatujastahili kushiriki katika kazi kubwa ya kuandaa watu kusimama katika siku kuu ya Bwana. Shule zetu za Sabato ambazo ni za kufundisha watoto na vijana ni za juu juu sana. Wasimamizi wa haya wanapaswa kuchimba kwa kukatua chini zaidi (ili mbegu ipandwe vyema). Wanahitaji kuweka mawazo zaidi na juhudi zaidi juu ya kazi wanayofanya. Wanapaswa kuwa wanafunzi kamilifu na wa kina zaidi wa Biblia, na kuwa na uzoefu wa kina wa kidini/kiroho, ili kujua jinsi ya kuendesha shule za Sabato kwa kulingana na agizo la Bwana, na jinsi ya kuwaongoza watoto na vijana kwa Mwokozi wao. Hii ni moja ya aina ya kazi ambayo imedhoofika kwa kukosa wanaume na wanawake wenye uwezo, hekima na utambuzi wanaohisi uwajibikaji wao kwa Mungu kutumia nguvu zao, si kujionyesha wenyewe, si kujitukuza wenyewe kwa ubatili, bali kufanya mema. {FEsw 121.2}

Jinsi gani amri hii ilivyo kubwa na pana, “Basi enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa Jina la Baba, na la Mwana, na wa Roho Mtakatifu: mkiwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, Mimi Nipo pamoja nanyi siku zote; hata ukamilifu wa dahari!” Ni heshima iliyoje wanadamu waliyotunukiwa hapa, na bado idadi kubwa jinsi gani hukumbatia ufuko wa bahari bila ya kutaka kwenda kwenye vilindi samaki walipo! Ni wachache jinsi gani wataingia kilindini, na kushusha nyavu zao ili kuvua samaki, wakishindana na changamoto zote za dhoruba! Sasa, ikiwa hili likifanywa, ikiwa wanadamu ni watenda kazi pamoja na Mungu, ikiwa wanadamu ni watenda kazi walioitwa kutenda katika misheni kwenye majiji, na kukutana na makundi yote ya akili, kunapaswa kuwa na matayarisho ya pekee kwa ajili ya kazi ya aina hii. — *Review and Herald, Juni 21, 1887.* {FEsw 121.3}

Kwa marejeleo ya Ziada

Divine Wisdom, The Review and Herald, April 17, 1888

THAMANI YA KUJIFUNZA BIBLIA

“Kila Andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuaadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa katika matendo mema.” Neno la Mungu ni kama nyumba ya hazina yenye kila kitu ambacho ni muhimu ili kumkamilisha mtu wa Mungu. Hatuithamini Biblia kama tunavyopaswa. Hatuna makadirio sahihi ya utajiri wa hazina yake, wala hatutambui umuhimu mkubwa uliopo wa kuyachunguza Maandiko. Watu hupuuza kujifunza Neno la Mungu, ili kufuata mambo ya kidunia, au kujishughulisha katika raha za kitambo. Mambo madogo madogo yanafanywa kuwa kisingizio cha kutojua Maandiko Matakatifu yaliyotolewa kwa uvuvio na Mungu. Lakini kitu chochote chenye namna ya kidunia ni bora kiachwe, kuliko huku kujifunza kuliko muhimu sana, ambako hutufanya tuwe na hekima hadi uzima wa milele. {FESW 123.1}

Moyo wangu unaumia ninapowaona watu—hata wale wanaodai kuwa wanatazamia ujio wa Kristo—wakitoa muda wao na talanta zao kwa ajili vitabu ambavyo viko kwenye mzunguko, na ambavyo havina chochote kuhusu zile Kweli hizo maalum za wakati wetu, -vitabu vya masimulizi, vitabu vya wasifu (biografia), vitabu vya nadharia na dhana na ubunifu wa watu. Ulimwengu umejaa vitabu hivyo; vinaweza kuwa mahali popote; lakini wafuasi wa Kristo wanaweza kujihusisha katika kazi ya kawaida isiyo na ladha wala maadili wakati kuna hitaji la kilio cha ile Kweli ya Mungu kila kona? Sio utume wetu kusambaza kazi kama hizo. Kuna maelfu ya wengine wa kufanya hivi, ambao bado hawana maarifa ya kitu chochote kiicho bora. Tuna utume wa uhakika, na hatupaswi kuuacha na kugeukia maswala ya kando, tukitumia watu na mali kuwavuta watu kuelekea vitabu vya watu ambavyo havina uhusiano wowote na Ukweli wa sasa. {FESW 123.2}

Je, unaomba kwa ajili ya maendeleo ya ile Kweli? Basi ifanyie kazi pia, na uonyeshe kwamba maombi yako yanapanda kutoka katika moyo wa kweli na wa dhati. Mungu hafanyi miujiza mahali ambapo ametoa njia na uwezo ambao kwayo kazi inaweza kukamilika. Tumia muda wako na talanta katika huduma Yake, na hataacha kufanya kazi na juhudi zako. Ikiwa mkulima anashindwa kulima na kupanda, Mungu hafanyi muujiza wa kutengua matokeo ya kupuuzia kwake. Wakati wa mavuno huyakuta mashamba yake yakiwa tasa—hakuna miganda ya kuvunwa, hakuna nafaka za kuvuna. Mungu alitoa mbegu na udongo, jua na mvua; na kama mkulima angetumia mali zilizokuwa mkononi mwake, angepokea kulingana na kupanda kwake na kazi yake. {FESW 123.3}

Kuna sheria kuu zinazotawala ulimwengu wa asili, na kwa mambo ya kiroho yananatawaliwa na kanuni sawa; njia zinazoleta matokeo ni lazima zitumike,

endapo matokeo yanayohitajika yatapatikana. Wale ambao hawafanyi juhudi zilizoamuliwa, hawafanyi kazi kwa kupatana na sheria za Mungu. Hawatumii majaliwa ya Baba wa Mbinguni, na hawawezi kutarajia chochote ila faida chache tu. Roho Mtakatifu hatawalazimisha wanadamu kuchukua hatua fulani. Sisi ni watu ambao tumepewa utashi na uhuru wa kuchagua; na ikiwa tumepewa ushahidi wa kutosha kuwa kama wajibu wetu, basi imebakia kwetu kuamua njia na mwenendo wetu. {FEsw 124.1}

Ninyi ambao mnaongojea kizembe kwamba Mungu atafanya muujiza fulani wa ajabu wa kuuangazia ulimwengu kuhusiana na Ukweli, Ninataka kuwauliza ikiwa mmetumia njia ambazo Mungu ametoa kwa ajili ya kuendeleza kazi Yake? Ninyi mnaoomba kwa ajili ya Nuru ya ile Kweli kutoka Mbinguni, je, mmejifunza Maandiko? Je, mmetamani “maziwa yasiyoghoshiwa ya Neno,” ili mpate kukua kwayo? Je, mmejisalimisha kwa amri Zake/Yake iliyofunuliwa? “Tenda/Fanya,” na “usitende/Usifanye,” ni matakwa ya uhakika, na hakuna nafasi ya uvivu katika maisha ya Kikristo. Ninyi mnaoombolezea upungufu wenu wa kiroho, je, mnatafuta kujua na kufanya mapenzi ya Mungu? Je! mnajitahidi kuingia katika mlango ulio mwembamba? Kuna kazi, kazi ya bidii, ya kufanywa kwa ajili ya Bwana. Maovu yanayoshutumiwa katika Neno la Mungu, lazima tuyaache/tuyashinde. Lazima mtu mmoja mmoja apigane dhidi ya ulimwengu, tamaa za mwili na shetani. Neno la Mungu linaitwa “upanga wa Roho,” nawe unapaswa kuwa stadi katika matumizi yake, ikiwa unataka kutengeneza njia yako kupitia katika majeshi ya upinzani na giza. {FEsw 124.2}

Jingatue kwa nguvu kutoka kwenye ushirika wenye kuumiza. Hesabu gharama ya kumfuata Yesu, na uilipie hiyo, ukiwa na kusudi la kujitakasa na uchafu wote wa mwili na Roho. Uzima wa milele una thamani yako yote, na Yesu amesema, “Yeyote aliye miongoni mwenu asiyeacha vyote alivyo navyo, hawezi kuwa mfuasi Wangu.” Yeye ambaye hafanyi chochote, lakini anangoja kulazimishwa na mawakala Fulani wa miujiza, atasubiri katika uchovu na giza. Mungu amelitoa Neno Lake. Mungu anazungumza kwa lugha isiyotatanisha na nafsi yako. Je, lile Neno la kinywa Chake halitoshi kukuonyesha wewe wajibu wako, na kukuhimiza utimilifu ndani yako? {FEsw 125.1}

Wale wanaochunguza Maandiko kwa unyenyekevu na maombi, ili kujua na kufanya mapenzi ya Mungu, hawatakuwa na shaka ya wajibu wao kwa Mungu. Kwa maana “mtu akipenda kufanya mapenzi Yake, atayajua mafundisho.” Kama utajua siri ya utauwa, lazima utafuata Neno la wazi la Ukweli, —kuhisi au kutokuwa na hisia, hisia au kutokuwa na hisia. Utii lazima utolewe kutoka katika ufahamu wa kanuni, na haki lazima ifuatwe katika hali zote. Hii ndiyo tabia iliyochaguliwa na Mungu kwa wokovu. Mtihani wa Mkristo wa kweli umetolewa katika Neno la Mungu. Yesu anasema, “Mkinipenda, mtazishika amri zangu.” “Yeye aliye na amri Zangu, na kuzishika, yeye ndiye anipendaye, Naye anipendaye atapendwa na Baba Yangu,

Nami nitampenda, na kujidhihirisha kwake.... Mtu akinipenda atayashika Maneno Yangu: na Baba Yangu atampenda, Nasi tutakuja kwake, na kufanya makao kwake. Yeye asiyenipenda hayashiki Maneno Yangu, na Neno hilo mnalolisikia si Langu, bali ni la Baba aliyenipeleka.” {FEsw 125.2}

Hapa kuna masharti ambayo kila nafsi itachaguliwa kwa ajili ya uzima wa milele. Utiifu wako kwa amri za Mungu utathibitisha haki yako ya urithi pamoja na watakatifu katika Nuru. Mungu amechagua ubora fulani wa tabia; na kila mtu ambaye, kupitia neema ya Kristo, atafikia kiwango cha mahitaji yake, ataingia katika ufalme wa Utukufu. Wote ambao wangeweza kufikia kiwango hiki cha tabia, itawabidi kutumia njia ambazo Mungu ametoa katika mwisho huu. Ikiwa utarithi pumziko lililosalia kwa watoto wa Mungu, lazima uwe mtendakazi pamoja na Mungu. Mmechaguliwa kuvaa nira ya Kristo, —kubeba mzigo Wake, na kuinua msalaba Wake. Unapaswa kuwa na bidii “kufanya wito wako na uteule wako kuwa wa uhakika.” Myachunguze Maandiko, na hutaona kwamba mwana au binti wa Adamu aliyechaguliwa kuokolewa kwa kutotii sheria ya Mungu. Ulimwengu unaibatilisha sheria ya Mungu; bali Wakristo wamechaguliwa kutakaswa kwa njia ya kuitii ile Kweli. Wamechaguliwa kubeba msalaba, kama watavaa ile taji. {FEsw 125.3}

Biblia ndiyo kanuni pekee ya imani na mafundisho. Na kuna hakuna kitu kinachohesabiwa zaidi kutia nguvu akili, na kuimarisha akili, kuliko kujifunza Neno la Mungu. Hakuna kitabu kingine chenye uwezo wa kuinua mawazo, kutoa nguvu kwa ufahamu, kama Ukweli mpana, na wenye kutia moyo wa Biblia. Kama Neno la Mungu lingesomwa kama inavyopaswa kuwa, watu wangukuwa na upana wa akili, uungwana wa tabia, na uthabiti wa kusudi, jambo ambalo halionekani sana katika nyakati hizi. Maelfu ya wanaume wanaohudumu kwenye mimbari wanakosa sifa muhimu za akili na tabia, kwa sababu hawajishughulishi wao wenyewe katika kujifunza Maandiko. Wanaridhika na ujuzi wa juu juu wa zile kweli ambazo zimejaa kina kirefu cha maana; na wanapendelea kuendelea, wakipoteza mengi katika kila njia, kuliko kutafuta kwa bidii hazina iliyofichwa. {FEsw 126.1}

Utafutaji wa ile Kweli utampa thawabu mtafutaji katika kila upande, na kila ugunduzi utafungua nyanja tajiri katika uchunguzi wake. Watu hubadilishwa kulingana na kile wanachofikiria. Ikiwa mawazo na mambo ya kawaida yatazingatiwa, mtu huyo atakuwa wa kawaida. Ikiwa anapuuzia sana kupata chochote isipokuwa ufahamu wa juu juu wa ukweli wa Mungu, hatapokea utajiri wa baraka ambazo Mungu angefurahi kumpa. Ni sheria ya akili, kwamba itapunguza au kupanuka kulingana na vipimo vya mambo ambayo inahusiana nayo. Nguvu za akili hakika zitasinyaa, na kupoteza uwezo wake wa kufahamu maana za kina za Neno la Mungu, isipokuwa zimewekwa kwa nguvu na kwa bidi katika kazi ya kuutafuta Ukweli. Akili itapanuka, ikiwa itatumika katika kufuatilia uhusiano wa masomo ya Biblia, ikilinganisha maandiko na maandiko, na mambo ya kiroho

pamoja na ya kiroho. Nenda chini ya uso wa ardhi; hazina za utajiri wa mawazo humgonja mwanafunzi stadi na mwenye bidii. {FEsw 126.2}

Wale wanaofundisha ule ujumbe mzito zaidi kuwahi kutolewa kwa ulimwengu, wanapaswa kuiadabisha akili ili kuuelewa umuhimu wake. Dhima ya ukombozi itahitaji umakini zaidi wa kujifunza, na kina chake hakitachunguzwa kikamilifu. Huna haja ya kuogopa kwamba utamaliza mada hii ya ajabu. Kunywa ndani ya kisima cha wokovu. Nenda kwenye chemchemi kwa ajili yako, ili ujazwe burudisho, ili Yesu awe ndani yako chemchemi ya maji yanayobubujika kwa uzima wa milele. Ukweli wa Biblia na dini ya Biblia pekee ndiyo zitastahimili wa jaribu la hukumu. Hatupaswi kupotosha Neno la Mungu kuendana na urahisi wetu, na maslahi ya kidunia, bali tuulize kwa uaminifu, “Unataka nifanye nini?” “Ninyi si mali yenu wenyewe, kwa maana ninyi mmenunuliwa kwa thamani.” Na ni kwa gharama gani! Si “kwa vitu viharibikavyo, kama fedha na dhahabu, ... bali kwa damu ya thamani ya Kristo.” Wakati mwanadamu alipopotea, Mwana wa Mungu alisema, nitamkomboa, nitakuwa mdhamini wake na mbadala wake. Aliweka kando mavazi Yake ya kifalme, akauvisha Uungu Wake na ubinadamu, akashuka kutoka kwenye kiti cha enzi cha kifalme, ili aweze kufikia kina cha ole na majaribu ya mwanadamu, kuinua juu asili zetu zilizoanguka, na kufanya iwezekane kwetu kuwa washindi, wana wa Mungu, warithi wa ufalme wa milele. Je, basi tutaruhusu mambo yoyote ya dunia kutugeuza kutoka kwenye njia ya haki? Je! hatutapinga kila fundisho na nadharia, na kulipima au kulijaribu kwa Neno la Mungu? {FEsw 127.1}

Hatupaswi kuruhusu hoja zozote za wanadamu zituzuie tuache kuchunguza kikamilifu zile Kweli za Biblia. Maoni na desturi za wanadamu havipaswi kupokelewa kama mamlaka ya Bwana. Mungu amefunua katika Neno Lake ni nini wajibu wote wa mwanadamu, na hatupaswi kuyumbishwa kutoka kwenye kiwango kikuu cha uadilifu. Alimtuma Mwanawe wa pekee awe kielelezo chetu, na akatuamuru tumsikie na kumfuata. Hatupaswi kushawishiwa kutoka kwa ile Kweli kama ilivyo ndani ya Yesu, kwa sababu watu wakuu na wanaodai kuwa wema huhimiza maoni yao juu ya Maneno ya wazi ya Neno la Mungu. {FEsw 128.1}

Kazi ya Kristo ni kuwavuta watu kutoka kwenye uongo na upotovu hadi kwenye ule Ukweli halisi. “Yeye anifuataye hatakwenda gizani, bali atakuwa na Nuru ya uzima.” Hakuna hatari ya kuingia katika makosa tunapofuata nyayo za “Nuru ya ulimwengu.” Tunapaswa kuzitenda kazi za Kristo. Ni lazima tushiriki moyo na Roho katika huduma Yake; lazima tuchunguze Neno la uzima, na kuliwasilisha kwa wengine. Ni lazima tuwaelimishe watu watambue umuhimu wa mafundisho Yake, na hatari ya kukengeuka kutoka katika amri Zake zilizo wazi. {FEsw 128.2}

Wayahudi waliongozwa kwenye upotofu na uharibifu, na kumkataa Bwana wa Utukufu, kwa sababu hawakujua Maandiko wala uweza wa Mungu. Kazi kubwa iko mbele yetu, —kuwaongoza watu kulichukulia Neno la Mungu kama kanuni ya maisha yao, kutopatana na mila na desturi bali kuenenda katika amri zote na

maagizo yote ya Mungu. — *The Review and Herald, Julai 17, 1888.* {FEsw 128.3}

KITABU CHA VITABU

Usomaji wa Biblia hutoa nguvu kwa akili. Anasema Mwandishi wa Zaburi, “Kufafanusha Maneno Yako kwatia Nuru; humtia ufahamu mjinga.” Swali limeulizwa mara nyingi kwangu, “Je, Biblia inapaswa kuwa kitabu muhimu katika shule zetu?” Ni kitabu chenye thamani, kitabu cha ajabu. Ni hazina iliyo na vito vya thamani. Ni historia ambayo inatufunulia kuhusu karne zilizopita. Bila Biblia tungeachwa kwenye dhana zisizo sahihi au zenye Ukweli nusunusu na hekaya kuhusiana na matukio ya zama zilizopita. Kati ya vitabu vyote vilivyofurika duniani humu, hata viwe vya thamani sana, **Biblia ni Kitabu cha vitabu**, na kinastahili umakini mwingi na usomaji wa kina. Hakitoi tu historia ya uumbaji ya ulimwengu huu, bali maelezo ya ulimwengu ujao. Ina mafundisho kuhusu maajabu ya ulimwengu (mbingu na nchi, na malimwengu yote), na inafunua katika ufahamu wetu Muumba wa mbingu na nchi. Inafunua mfumo rahisi na kamili wa teolojia na falsafa. Wale ambao ni wanafunzi wa kina, wa Neno, na wanaoliweka Neno hilo la Mungu kwa ukaribu, na kuyatii maelekezo Yake sahili, na kuzipenda Kweli Zake zilizo wazi, wataimarika na kuboreshwa akilini na katika tabia. Hakika majaliwa ya Mungu yanapasa kuamsha katika kila moyo shukrani ya dhati kabisa; kwa maana ni ufunuo wa Mungu kwa mwanadamu. {FEsw 129.1}

Ikiwa Kweli za Biblia zitafumwa katika maisha ya vitendo, zitainua akili kutoka katika hali yake ya kidunia na unyonge. Wale ambao wanaoyafahamu Maandiko Matakatifu, watapatikana kuwa ni wanaume na wanawake ambao wana ushawishi unaoiua. Katika kutafuta Ukweli wa Mbinguni uliofunuliwa, Roho wa Mungu ataletwa katika uhusiano wa karibu na mchunguzaji mnyoofu wa Maandiko. Ufahamu wa mapenzi ya Mungu yaliyofunuliwa, huikuza akili, huipanua, huiinua, na huijaza nguvu mpya, kwa kuleta uwezo wake katika kupatana na Kweli za ajabu na kushangaza. Kama ujifunzaji wa Maandiko utafanywa kuwa ni jambo la pili katika kuzingatwa, kutakuwa na hasara kubwa. Biblia imekuwa kwa muda mrefu ikiwekwa kando na shule zetu, na Shetani akapata shamba la kutosha, ambalo ndani yake alifanya kazi kwa kasi ya ajabu, na akakusanya mavuno kama appendavyo. {FEsw 129.2}

Kawaida Uelewa wa mtu, huendana na kiwango cha mambo ambayo hujizoeza nayo. Ikiwa wote wangepanya Biblia kuwa somo lao, tungeona watu waliokuzwa kwa hali ya ubora na walioendelezwa zaidi na wenye uwezo wa kufikiria kwa undani zaidi, wakionyesha kiwango kikubwa cha akili, kuliko ambavyo bidii zaidi katika kusoma tu sayansi na historia za ulimwengu inavyoweza kuwafanya. Biblia humpa mtafutaji wa kweli, nidhamu ya juu ya kiakili, na anatoka katika kutafakari mambo ya Bwana huku vitivo vyake vikiwa vimetajirishwa; Nafsi imenyenyekwa, na

Mungu Mwenyezi na Ukweli Wake uliofunuliwa umeinuliwa. Ni kwa sababu watu hawazifahamu historia za thamani za Biblia, ndio maana kuna kuinuliwa sana kwa mwanadamu, na kicho na heshima ndogo sana hutolewa kwa Mungu. Biblia ina ubora wa chakula ambacho Mkristo anakihitaji ili apate kuwa na nguvu katika Roho na akili. Kuchunguza vitabu vyote vya falsafa na sayansi hakuwezi kufanya katika akili na maadili kile ambacho Biblia inaweza kufanya, ikiwa imesomwa na kutekelezwa kwa vitendo. Kupitia kujifunza Biblia, mazungumzo yanafanyika na wazee na manabii. Ukweli umevikwa lugha iliyoinuliwa, ambayo hutoa nguvu ya kuvutia juu ya akili; fikra huinuliwa kutoka katika vitu vya kidunia, na kuletwa kutafakari Utukufu wa maisha ya umilele. Hekima gani ya mwanadamu inaweza kulinganishwa na ukuu wa ufunuo wa Mungu? Mwanadamu mwenye ukomo, ambaye hamjui Mungu, anaweza kutafuta kupunguza thamani ya Maandiko, na anaweza kuuzika Ukweli chini ya ujuzi unaodhaniwa kuwa (yumkini) ni sayansi.

{FEsw 130.1}

Wale wanaojivunia hekima zaidi ya mafundisho ya Neno la Mungu, wanahitaji kunywa kwa kina zaidi katika chemchemi ya maarifa, ili waweze kuujua ujinga wao halisi. Kuna hekima ya kujivunia ya wanadamu, ambayo ni upumbavu mbele za Mungu. "Mtu asijidanganye mwenyewe, Kama mtu akijiona kuwa mwenye hekima miongoni mwenu katika dunia hii, na awe mpumbavu, ili apate kuwa mwenye hekima. Maana hekima ya dunia hii ni upuuzi mbele za Mungu. Kwa maana imeandikwa, Yeye Ndiye awanasaye wenye hekima katika hila yao." Wale ambao wana hekima hii tu, wanahitaji kuwa wajinga kwa kipimo chao wenyewe. Ujinga mkubwa ambao sasa unalaani jamii ya wanadamu unahusiana na mashiko/madai ya sheria ya Mungu; na ujinga huu ni matokeo ya kupuuzia kujifunza Maneno ya Mungu. Ni mkakati uliodhamiriwa wa Shetani kushughulisha na kuivuta akili, ili Kitabu hivi Kikuu cha Mwongozo cha Mungu kisiwe Kitabu cha vitabu, na ili mdhambi asiongozwe kutoka katika njia ya uasi kuiendea njia ya utii. {FEsw 130.2}

Biblia haijainuliwa hadi mahali Pake inapostahili kuwa, na jambo ambalo ni la umuhimu usio na kipimo kwa Roho za watu. Katika kuchunguza kurasa zake, tunapita katika matukio makuu na ya umilele. Tunamwona Yesu, Mwana wa Mungu, akija katika ulimwengu wetu, na kushiriki katika pambano kuu la siri ya ajabu ambapo nguvu za giza zinaumbuliwa kwa kufichuliwa. Tazama ni ajabu jinsi gani, tena jinsi ilivyo ya kushangaza, kwamba Mungu asiye na mwisho angekubali kuteswa kwa Mwana Wake Mpendwa! Hebu kila mwanafunzi wa Maandiko atafakari kwa umakini na muda, Ukweli huu mkuu, naye hatatoka katika tafakuri kama hiyo bila kuinuliwa, kutakaswa, na kukuzwa. {FEsw 131.1}

Biblia ni kitabu kinachofungua kanuni za haki na Kweli. Ina kila kinachohitajika kwa ajili ya kuokoa Roho, na wakati huo huo inafaa kuimarisha na kunidhamisha akili. Ikiwa itatumika kama kitabu cha kiada katika shule zetu, kutakuwa na ufanisi zaidi kuliko kitabu kingine chochote duniani, katika kuongoza kwa hekima mambo

ya maisha haya, vilevile katika kuisaidia nafsi kupanda ngazi ya kukua na kuendelea hadi kufikia Mbinguni. Mungu anatumia kama viumbe wenye akili, Naye ametupa Neno Lake kama taa ya miguu yetu na mwangaza wa njia yetu. “Kufafanusha Neno Lake kwatia nuru; kwampa ufahamu mjinga.” Sio kusoma tu Neno ndiko kutatimiza matokeo ambayo yamepangwa na Mbingu, bali Ukweli uliofunuliwa katika Neno la Mungu lazima upate kuingia ndani ya moyo, ikiwa mema yaliyokusudiwa yanapatikana. {FEsw 131.2}

Wale waliosoma zaidi katika sayansi sio mara zote ndio vyombo vyenye ufanisi zaidi kwa ajili ya kutumiwa na Mungu. Kuna wengi ambao wanajikuta wamewekwa kando, na kisha wale ambao wamekuwa na bahati ndogo ya kupata maarifa ya vitabu, wakichukua nafasi zao, kwa sababu hawa wengine wana ujuzi wa mambo ya vitendo ambayo ni muhimu kwa matumizi ya maisha ya kila siku (practical life); wakati wale wanaojiona kuwa wamejifunza, mara nyingi huacha kuwa wanafunzi au kuendelea kujifunza, wakijiona wamejitoshela, na wako juu ya kufunzwa na mtu, hata na Yesu Mwenyewe; ambaye alikuwa Mwalimu mkuu kuliko wote ambao ulimwengu umewahi kujua. Wale ambao wamekuwa na kutanuka, ambao vitivo vyao vya kufikiri vimeboreshwa kwa kuyachunguza kwa kina Maandiko, wapate kujua mapenzi Yake Mungu, watakuja katika nafasi za manufaa; kwa maana Neno la Mungu limepata mlango wa kuingia katika maisha na tabia zao. Hakika hilo litafanya kazi yake ya kipekee, hata kuvitenganisha viungo na mafuta, na kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo. Neno la Mungu linapaswa kuwa lishe ambayo kwayo Mkristo lazima astawi kwa nguvu katika Roho na akili yake, ili apate kupigana kwa ajili ya Ukweli na haki. {FEsw 132.1}

Kwa nini vijana wetu, na hata wale wa miaka ya ukomavu, wanaongozwa kirahisi katika majaribu na dhambi? Ni kwa sababu Neno la Mungu halisomwi na kutafakariwa inavyopaswa. Kama lingethaminiwa na kupendwa, basi kungekuwa na uaminifu wa kimaadili wa ndani ya moyo, nguvu ya Roho, ambayo ingepinga majaribu ya Shetani ya kufanya maovu. Uimara/uthabiti na, nia yenye uamuzi sahihi haviletwi katika maisha na tabia kwa sababu mafundisho matakatifu ya Mungu hayajifunzwi, na kuwa somo la kutafakari. Hakuna juhudi iliyowekwa kwamba kunapaswa kuwepo na kuunganishwa kwa nia na mawazo safi, matakatifu na kuigeuza kutoka katika kile kilicho ni najisi na ambacho si cha kweli. Hakuna uchaguzi wa mahali palipo bora, kuketi miguuni pa Yesu, kama vile Mariamu, kujifunza zaidi masomo matakatifu ya Mwalimu wa kimbungu, ili yawekwe ndani moyo, na kutendwa katika maisha ya kila siku. Kutafakari mambo matakatifu kutaiinua, kutaifafanua na kuiboresha akili, na kuendeleza/kukuza wanawake na wanaume Wakristo. {FEsw 132.2}

Mungu hatamkubali hata mmoja wetu ambaye anadharau uwezo au nguvu zake kwa tamaa mbaya zinazopunguza thamani, kwa udhalilishaji wa kidunia, kwa mawazo, au neno, au tendo. Mbinguni ni mahali safi na patakatifu, ambapo hakuna

awezaye kuingia isipokuwa amesafishwa; amekuwa wa kiroho, amesafishwa, na kutakaswa. Kuna kazi ya kufanya kwa ajili yetu wenyewe, na tutakuwa na uwezo wa kuifanya kwa kuchota nguvu kutoka kwa Yesu tu. Tunapaswa kuifanya Biblia kuwa somo letu la juu ya kila kitabu kingine; tunapaswa kuipenda, na kuitii kama sauti ya Mungu. Tunapaswa kuona na kuelewa makatazo na matakwa Yake, "fanya" na "usifanye," na kutambua maana ya Kweli ya Neno la Mungu. {FEsw 133.1}

Neno la Mungu linapofanywa kuwa mshauri wetu, na tunapotafuta Maandiko kwa ajili ya Nuru, malaika wa Mbinguni wanakaribia ili kuvutia au kushawishi akili, na kuangaza ufahamu, ili iweze kusemwa hakika, "Kufafanuliwa kwa Maneno Yako kwatia Nuru; humpa ufahamu mjinga." Sio jambo la kushangaza kwamba hakuna nia ya Mbinguni zaidi inayoonyeshwa miongoni mwa vijana wanaodai kuwa wakristo, wakati kuna umakini mdogo sana unaotolewa kwa Neno la Mungu. Mashauri ya Mungu hayazingatiwi; mawaidha Yake hayazingatiwi; neema na hekima ya Mbinguni havitafutwi, ili dhambi zilizopita ziepukwe, na kila doa la ufiisadi lisafishwe kutoka katika tabia. Maombi ya Daudi yalikuwa, "Unifahamisha njia ya mausia Yako; ndipo nitayasimulia matendo Yako ya ajabu. {FEsw 133.2}

Ikiwa akili za vijana wetu, na vile vile za watu wazima zaidi, zिलielekezwa vema wanapochangamana pamoja, mazungumzo yao yatakuwa juu ya mada zilizotukuka. Wakati akili ni safi, na mawazo yalioinuliwa na Kweli ya Mungu, Maneno yatakuwa ya namna au tabia ile ile, "ni kama machungwa katika vyano vya fedha." Lakini kwa uelewa wa sasa, na mazoea ya sasa, na kiwango cha chini ambacho hata Wakristo wanaridhika kukifikia, mazungumzo ni ya kawaida sana na hayana faida kwani ni hafifu tu. Ni ya "chini, ya udunia, na ya duniani," na si manukato ya Kweli, au ya Mbinguni, na hayapandi juu, hata kwa kipimo/kiwango cha wale watu wenye tamaduni au elimu bora zaidi za kiulimwengu. Wakati Kristo na mbingu vitakuwka ndizo mada za kutafakari, mazungumzo yatatoa Ushahidi wa ukweli huu. Maneno yatajazwa na neema, na mzungumzaji ataonesha kuwa amekuwa akipata elimu katika shule ya Mwalimu wa Kimbingu. Mwandishi wa Zaburi Anasema, "nimeichagua njia ya uaminifu; na kuziweka hukumu Zako mbele yangu." Hakika Alilithamini Neno la Mungu. Hilo lilipata Kuingia katika ufahamu wake, sio kwa kupuuzwa, bali kutekelezwa katika maisha yake. {FEsw 133.3}

Isipokuwa Neno takatifu limethaminiwa na kupendwa, halitatiiwa kama kitabu cha kiada chenye uhakika na salama na cha thamani. Kila dhambi inayosumbua lazima iwekwe mbali. Vita lazima ipiganwe dhidi yake hadi ishindwe. Bwana atafanya kazi kwa juhudi zako. Kama yule mwenye ukomo, mwanadamu mwenye dhambi hufanyia kazi wokovu wake wenyewe kwa kuogopa na kutetemeka, ni Mungu atendaye kazi ndani yake; kutaka na kutenda mapenzi Yake mema. Lakini Mungu hatafanya kazi bila ushirikiano wa mwanadamu. Ni lazima yeye mwenyewe atumie uwezo wake kwa ukamilifu kabisa; lazima ajiweke kama mwanafunzi anayefaa, aliye tayari katika shule ya Kristo (aliye na sifa, anayestahili); na

anaipokubali neema inayotolewa bure kwake, uwepo wa Kristo katika mawazo na moyo humpa uamuzi wenye kusudi katika kuweka kando kila uzito wa dhambi, ili moyo uweze kujazwa na utimilifu wote wa Mungu, na upendo Wake. {FEsw 134.1}

Wanafunzi wa shule zetu wanapaswa kuzingatia kwamba kupitia kuiwaziawazia dhambi, matokeo ya hakika yamefuata, na uwezo wa vitivo vyao walivyopewa na Mungu umedhoofika na haufai kwa maendeleo ya maadili, kwa sababu umetumika visivyo au vibaya. Wapo wengi wanaokubali hili kama ile Kweli. Wametunza kiburi na majivuno na kujidanganya wenyewe kuhusu thamani yao, mpaka hizi chembechembe mbaya za tabia zimekuwa nguvu inayotawala, na inayodhibiti matamania na mielekeo yao. Ingawa wamekuwa na mfano wa utauwa, nao wamefanya matendo mengi ya kujihesabia haki yao wenyewe, hakuja na mabadiliko ya kweli ya moyo. Hawajaileta mitindo yao ya maisha na kuipatanisha na kipimo dhahiri na cha karibu na kiwango kikuu cha haki, yaani, ile sheria ya Mungu. Iwapo wangelinganisha maisha yao kwa uangalifu na kina na kiwango hiki, wangeweza kuhisi kwamba walikuwa na upungufu, wenye ugonjwa wa dhambi, na walihitaji tabibu. Wanaweza tu kuelewa kina ambacho wameanguka, kwa kutazama Dhabihu isiyo na kikomo ambayo imetolewa na Yesu Kristo, ili kuwainua kutoka katika unyonge wao. {FEsw 134.2}

Ni wachache tu walio na ufahamu halisi wa jinsi dhambi inavyotisha na kuleta huzuni, na ambao wanafahamu uharibifu mkuu ambao umetokana na uvunjaji wa sheria ya Mungu. Kwa kuchunguza mpango wa ajabu wa ukombozi wa kumrudisha mwenye dhambi katika sura ya maadili ya Mungu, tunaona kwamba njia pekee ya ukombozi wa mwanadamu ilifanywa kwa kujitoa kafara, na kujishusha kusiko na kifani na upendo wa Mwana wa Mungu. Yeye peke Yake Ndiye alikuwa na nguvu ya kupigana vita na Adui mkuu wa Mungu na wanadamu, na kama mbadala wetu na mdhamini wetu, amewapa uwezo wale wanaomshika YEYE kwa imani, kuwa washindi katika Jina Lake, na kwa njia ya sifa na haki Yake. {FEsw 135.1}

Tunaweza kuona katika msalaba wa Kalvari kwamba ni gharama kuu ya kiasi gani imemgharimu Mwana Mungu kuleta wokovu kwa jamii iliyoanguka. Kama dhabihu kwa niaba ya mwanadamu ilivyokuwa kamili, ndivyo ambavyo urejeshwaji wa mwanadamu kutoka katika unajisi wa dhambi unavyopaswa kuwa kamili. Sheria ya Mungu imetolewa kwetu, ili tuwe na kanuni za kutawala mwenendo wetu. Hakuna tendo la uovu ambalo sheria itasamehe; hakuna tendo la udhalimu ambalo litaepuka hukumu Yake. Maisha ya Kristo ni ukamilifu ulio kamili kwa kila agizo la sheria hii. Anasema, "Nimezishika amri za Baba Yangu." Ujuzi wa sheria unamhukumu mwenye dhambi, na kupondaponda tumaini kutoka kifuni mwake asipomwona Yesu kama mbadala wake na mdhamini wake, aliye tayari kumsamehe kosa lake, na kumsamehe dhambi yake. Wakati ambapo, kwa njia ya imani katika Yesu Kristo, mwanadamu anapofanya kwa kadiri ya uwezo wake wote, na kutafuta kuishika njia ya Bwana kwa kutii amri kumi, ukamilifu ya Kristo

unahesabiwa kufunika uasi wa mwenye kutubu na kutii. {FEsw 135.2}

Kutakuwa na juhudi zitakazofanywa kwa upande wa marafiki wengi katika nyanja za elimu kuikwanya/kuitaliki dini kutoka kwenye sayansi, katika shule zetu. Hao watapitia maumivu au gharama tele ili tu wawape elimu ya kiulimwengu; ila hawataichanganya na elimu ya kile Mungu alichofunua kwamba ndiyo kinachojenga ukamilifu wa tabia. Na bado mafunzo katika Ukweli wa Mungu hukuza akili, na kutoa maarifa ya matawi ya elimu ya kidunia pia (jiografia, hesabu, lugha, sayansi nk); kwani msingi wa elimu ya Kweli ni katika kumcha Bwana. Anasema mwandishi wa Zaburi, “Kumcha Bwana ni mwanzo wa hekima.” Maneno ya Mungu yaliyo hai na historia Yake, yanafunua udanganyifu wa baba wa uongo. Ni nani kati ya vijana wetu anaweza kuichuja ile Kweli, na akailinganisha na ule upotofu, isipokuwa awe anayafahamu Maandiko? Usahili wa utauwa wa ile Kweli lazima uletwe katika elimu ya vijana wetu, ikiwa kama wanataka kuwa na maarifa ya kimbingu ili waweze kuepuka uharibifu ulioko duniani kupitia tamaa za mwili. Wale ambao ni wafuasi wa Kweli wa Kristo, hawatamtumikia Mungu ikiwa tu ni kwa mujibu wa mwelekeo wao, lakini, vile vile, inapohusisha kujikana nafsi na kuubeba msalaba. Shauri la dhati lililotolewa na mtume Paulo kwa Timotheo, ili kwamba asishindwe katika kutekeleza wajibu wake, linapaswa kuwekwa mbele ya vijana wa siku hizi: “Mtu awaye yote asiudharau ujana wako; bali uwe kielelezo kwao waaminio, katika usemi, na mwenendo, na katika upendo, na imani, na usafi.” Dhambi zinazotusumbua au zinazotuzinga kwa wepesi lazima zipiganwe na zishindwe. Chembechembe vitabia vya dhambi zinazochukiza kwenye haiba zetu zinapaswa kupingwa, ziwe zile ambazo tumezirithi au zile ambazo tumezikuza wenyewe, zote hizo zinapaswa kuwekwa kando, na kulinganishwa na kanuni kuu ya haki; na katika Nuru inayoakisiwa kutoka katika Neno la Mungu, zinapaswa kupingwa kwa uthabiti na kushindwa, kwa nguvu za Kristo. “Tafuteni kwa bidii kuwa amani na watu wote, na huo utakatifu, ambao hapana mtu atakayemwona Bwana asipokuwa nao.” {FEsw 135.3}

Siku kwa siku, na saa kwa saa, lazima kuwe na mchakato wenye nguvu tele wa kujikana nafsi na utakaso unaoendelea ndani; na kisha matendo ya nje yatashuhudia kwamba Yesu anakaa moyoni kwa imani. Utakaso haufungi njia za Rohoni kwa ajili maarifa, bali huja kupanua akili, na kuitia msukumo ili iweze kuitafuta ile Kweli, kama vile hazina iliyofichwa; na ujuzi wa mapenzi ya Mungu huendeleza kazi ya utakaso. Kuna mbingu jamani, na Tazama!, ni kwa bidii jinsi gani tunapaswa kujitahidi kuifikia hiyo. Ninawasihi ninyi wanafunzi wa shule zetu na vyuo, kumwamini Yesu kama Mwokozi wako. Mwaminini kwamba Yuko tayari kuwasaidia kwa neema Yake, mnapomjia kwa unyoofu. Lazima mvipige vile vita vizuri vya imani. Lazima muwe wapiganaji mieleka kwa ajili ya taji ya uzima. Jitahidini, kwani mkono wa Shetani uko juu yenu kuwanyangua, na kama hamtajinasua kwake, mtapooza na kuangamia. Adui yuko mkono wa kulia, na upande wa kushoto, mbele yenu na nyuma yenu; nanyi mnapaswa

kumkanyagakanyaga chini ya miguu yenu. Jitahidini, kwani ipo taji la kushinda/ushindi. Jitahidini, kwani msiposhinda taji, mnapoteza kila kitu katika maisha haya na katika maisha yajayo. Jitahidini, lakini hebu iwe katika nguvu za Mwokozi wenu aliyefufuka. {FEsw 136.1}

Je, wanafunzi wa shule zetu watajifunza, na kujitahidi kunakili maisha na tabia Yake Yeye aliyeshuka kutoka Mbinguni ili kuwaonesha kile wanachopaswa kuwa, ikiwa wataingia katika ufalme wa Mungu? Nimewaleta ujumbe wa kuja kwa karibu kwa Mwana wa Mungu katika mawingu ya Mbinguni kwa nguvu na Utukufu mkuu. Sijawasilisha mbele yenu wakati wowote maalum, lakini nimerudia kwenu agizo la Kristo Mwenyewe, la kukesha kwa maombi, “Maana katika saa msiyodhani, Mwana wa Adamu Yuaja.” Onyo lingekuwa likitoa mwangwi wa sauti kubwa hadi nyakati zetu, “Tazama, Naja upesi; na ujira Wangu u pamoja Nami, kumlipa kila mtu kama kazi yake ilivyo. Mimi ni Alfa na Omega, Mwanzo na Mwisho, wa Kwanza na wa Mwisho. Heri wale wazishikao amri Zake, ili wawe na haki ya kuundea huo mti wa uzima, na kuingia mjini kwa malango yake.”— *The Review and Herald, August 21, 1888.* {FEsw 137.1}

Kwa marejeleo ya ziada

The Work of Reform, Signs of the Times, June 3, 1889

Proper Education, The Review and Herald, July 14, 1889

Home Training, Signs of the Times, July 22, 1889

Religion and Scientific Education, Testimonies for the Church, 5: 501-504

The Education of Our Children, Idem, 5: 505-507

Dangers to the Young, Idem, 5: 508-516

Suitable Reading for Our Children, Idem, 5: 516-520

Advice to the Young, Idem, 5: 520-529

Needs of Our Institutions, Idem, 5: 549-554

Our Institution at Battle Creek, Testimonies for the Church, 5: 555- 567

Education of Workers, Testimonies for the Church, 5: 580-586

Sura ya 17

WAJIBU WA MZAZI

Mungu ameruhusu Nuru ya matengenezo ya afya kuangaza juu yetu katika siku hizi za mwisho, ili kwa kuenenda Nuruni tuweze kuepuka hatari nyingi ambazo zitatukabili (tutaanikwa kwazo). Shetani anafanya kazi kwa uwezo mkubwa kuwaongoza watu kujiingiza katika uchu wa kula, kuridhisha mielekeo ya nafsi, na kutumia siku zao katika upumbavu wa dhambi za kutotilia umakini. Analeta mivuto katika maisha ya starehe za ubinafsi na anasa za tamaa za mwili kama ngono na zinginezo. **Kutokuwa na kiasi kunapora nishati ya akili na mwili. Yeye** ambaye anayetekewa na haya amejiweka mwenyewe katika uwanja na udhibiti wa Shetani, ambapo atajaribiwa na kuudhika, na hatimaye kutawaliwa kwa anasa na adui wa haki yote. Wazazi wanapaswa kuvutwa na wajibu wao wa kuwapeleka watoto wao ulimwenguni wakiwa wana tabia zilizokuzwa vizuri, - watoto ambao watakuwa na uwezo wa kimaadili kuyapinga majaribu, na ambao maisha yao yatakuwa ni heshima kwa Mungu na baraka kwa wanadamu wenzao. Wale wanaoingia katika maisha ya utendaji au kazi, wakiwa na kanuni thabiti, wataandaliwa kusimama bila kuchafuliwa katikati ya maadili yenye uchafuzi katika zama hizi za uovu. Hebu akina mama waboreshe kila fursa ya kuwaelimisha watoto wao ili wawe na manufaa. **{FEsw 139.1}**

Kazi ya mama ni takatifu na ya muhimu. Anapaswa awafundishe watoto wake, toka wakiwa wachanga, tabia za kujikana nafsi {kujinyima} na kujizuia (kutawala nafsi). Muda wake, kwa namna maalum, ni wa watoto wake. Lakini ikiwa atashughulishwa zaidi na upumbavu wa zama hizi za uovu, ikiwa jumuiya, mavazi, na maburudisho vinachukua umakini wake, watoto wake watashindwa kuelimishwa ipasavyo. **{FEsw 139.2}**

Akina mama wengi wanaochukia hali ya kukosa kiasi iliyopo kila mahali, hawachunguzi kwa kina ili waone sababu. Mara nyingi sana inaweza kushuhudiwa kuwa ilianzia kwenye meza ya nyumbani (chakula wanachokula). Akina mama

wengi, hata kati ya wale ambao wanaodai kuwa Wakristo, kila siku huwapa watu wa nyumbani mwao chakula tajiri (kilichokobolewa na kusindikwa, chenye kalori nyingi kama siagi, mafuta, karanga, maziwa, keki nk) na chakula kilichokolezwa viungo sana (hukasirisha tumbo), ambacho huleta majaribu ya hamu ya kula na kuhimiza ulafi, yaani ulaji wa chakula kingi na kilichokolezwa ambacho hujaribu tamaa ya kula na kuhimiza ulaji wa kupita kiasi. Katika baadhi ya familia, chakula cha nyama ni sehemu kuu ya chakula, na kwa sababu hiyo, damu hujazwa na viini vya saratani na maradhi makali kama uvimbe au mafundo kwenye mwili. Kisha wakati mateso na magonjwa yanapowaandama, Mungu hulaumiwa kwa yale ambayo ni matokeo ya mwenendo mbaya. Narudia kusema: Kutokuwa na kiasi huanzia mezani, na, kwa walio wengi, uchu wa kula huendekezwa hadi inakuwa asili ya pili (mwenendo.)

{FEsw 139.3}

Yeyote anayekula sana, au chakula kisicho na afya, anadhoofisha nguvu za makelele ya sauti zinazopinga uchu wa chakula na tamaa zingine za mwili. Wazazi wengi, ili kuepuka kazi ya kuwaelimisha Watoto wao kwa Subira tabia ya kujinyima au kujikana nafsi, huwaendekeza kula na kunywa muda wowote wanaotaka. Shauku ya kukidhi ladha na kuridhisha nafsi, haipungui kulingana ongezeko la umri; na hawa vijana waliondekezwa, wanapokua, hutawaliwa na misukumo, na kuwa watumwa wa uchu wa kula. Wanapochukua nafasi zao katika jamii, na kuanza Maisha yao wenyewe, hawana uwezo wa kupinga majaribu. Katika ulafi, matumizi ya tumbaku, ulafi na ulevi, tunaona matokeo mabaya ya elimu potofu na kufurahisha nafsi. {FEsw 140.1} F{

Tunaposikia maombolezo ya kusikitisha ya wanaume na wanawake Wakristo juu ya maovu ya kutisha ya kutokuwa na kiasi, maswali huibuka mara moja: Nani wamewaelimisha vijana? Nani ambao wamekuza ndani yao hizi hamu za kula? Nani ambao wamepuuza jukumu zito la kuunda tabia zao kwa manufaa katika maisha haya, na ya jamii ya malaika wa Mbinguni yajayo? {FEsw 140.2}

Wazazi na watoto wanapokutana na kumbukumbu yao ya mwisho, ni tukio gani litakalowasilishwa! Maelfu ya watoto ambao wamekuwa watumwa wa uchu wa kula na maovu yenye kufedhehesha, ambao maisha yao yameharibika kimaadili na kuwa magofu; watasimama uso kwa uso na wazazi waliowafanya wawe vile walivyo. Ni nani isipokuwa wazazi wanapaswa kubeba jukumu hili la kutisha? Je! Ni Bwana aliwafanya vijana hawa kuwa wafisadi? —La, hapana! Nani, basi, amefanya kazi hii ya kutisha? Je! Si dhambi za wazazi zilizopitishwa kwa watoto katika uchu na tamaa za mwili potovu? na haikuwa kazi iliyokamilishwa na wale waliopuuza kuwafundisha kulingana na mfano ambao Mungu ametoa? Kwa hakika kama waishivyo, wazazi wote watapita katika uhakiki mbele za Mungu. {FEsw 140.3}

Shetani yuko tayari kufanya kazi yake; hatapuuza kuwasilisha vivutio ambavyo watoto hawana nia au nguvu ya kimaadili kuvipinga. Niliona kwamba, kupitia

majaribu yake, anaanzisha kila wakati mitindo inayobadilika, na karamu za kuvutia na maburudisho, ambayo akina mama wanaweza kuongozwa kutumia muda wao kwa mambo ya hovy au kipumbavu, badala ya kutoa elimu na mafunzo kwa watoto wao. Vijana wetu wanahitaji akina mama ambao watawafundisha kutoka utotoni, kudhibiti hamu, kupinga uchu wa kula, na kushinda ubinafsi. Wanahitaji mstari juu ya mstari, amri juu ya amri, huku kidogo na huku kidogo. {FEsw

141.1} F{

Waebrania walifundishwa jinsi ya kuwazoeza watoto wao ili waepuke ibada ya sanamu na uovu wa mataifa “Kwa hiyo yawekeneni Maneno Yangu mioyoni mwenu na Rohoni mwenu, yafungeni yawe dalili juu ya mikono yenu, nayo yatakuwa kama utepe katikati ya macho yenu. Nayo wafunzeni vijana wenu, kuyazungumza uketipo katika nyumba yako, na utembeapo njiani, ulalapo, na uondokapo.” {FEsw

141.2} F{ aaff

Mwanamke anapaswa kujaza nafasi ambayo Mungu alipanga awali kwa ajili yake, kama mume wake. Ulimwengu unahitaji akina mama ambao ni akina mama si kwa jina tu, bali kwa kila maana ya neno. Tunanaweza kusema kwa uwazi kwamba majukumu tofauti ya mwanamke ni matakatifu zaidi, kuliko ya mwanaume. Hebu mwanamke atambue utakatifu ya kazi yake, na kwa nguvu na hofu ya Mungu kuuchukua utume wa maisha yake. Hebu awafundishe watoto wake kwa manufaa katika ulimwengu huu, na nyumbani katika ulimwengu ujao ulio bora. {FEsw

141.3}

Nafasi ya mwanamke katika familia yake ni takatifu zaidi kuliko ile ya Mfalme katika kiti chake cha enzi. Kazi yake kubwa ni kufanya maisha yake kuwa kielelezo kwa namna ile ambayo angetamani watoto wake waige. Na kwa amri na mfano, ni kwa kuzijaza akili zao kwa maarifa yenye manufaa, na kuwaongoza kwenye kazi ya kujitoa kwa ajili ya manufaa ya wengine. Kichocheo kikubwa kwa mama anayetaabika, aliyelemewa kinapaswa kuwa katika kila mtoto wake aliyefunzwa ipasavyo, na aliye na mapambo ya ndani, pambo la Roho ya upole na utulivu, ataangaza katika nyua za Bwana. {FEsw 141.4} F{ aaff

Ninawasihi akina mama Wakristo kutambua wajibu wao, na kuishi, si ili kujipendeza wenyewe, bali kumtukua Mungu. Kristo hakujipendeza Mwenyewe, bali alichukua juu Yake namna ya mtumwa. Aliacha mbingu za kifalme, na kuuvika Uungu Wake kwa ubinadamu, ili kwa mfano Wake aweze kutufundisha jinsi tunavyoweza kuinuliwa kuwa na nafasi wa wana na binti katika familia ya kifalme, watoto wa Mfalme wa Mbinguni. Lakini ni masharti gani ambayo tunaweza kuipata baraka hii kubwa? “Tokeni kati yao, na mkajitenge nao; asema Bwana, wala msiguse kitu kilicho najisi; Nami niwatapokea na nitakuwa Baba kwenu, nanyi mtakuwa Kwangu wana na binti.” {FEsw 142.1} F{ aaff

Kristo alijinyenyekeza kutoka katika nafasi ya Mmoja aliye sawa na Mungu hadi

kuwa mtumishi. Nyumba Yake ilikuwa Nazareti, mahali palipofahamika kwa uovu wake. Wazazi wake walikuwa miongoni mwa watu maskini sana. Kazi yake ilikuwa ya useremala, na Alifanya kazi kwa mikono Yake kufanya Sehemu Yake katika kuitunza familia. Kwa miaka thelathini alikuwa chini ya Wazazi Wake. Maisha ya Kristo yanaonyesha wajibu wetu wa kuwa na bidii katika kazi, na kuwajali wale waliokabidhiwa katika uangalizi wetu. {FEsw 142.2}

Katika mafundisho Yake kwa wanafunzi Wake, Yesu aliwafundisha kwamba ufalme wake si ufalme wa kidunia, ambapo wote wanajitahidi kujipatia nafasi ya juu; bali aliwapa mafunzo katika unyenyekevu na kujitoa kwa manufaa ya wengine. Unyenyekevu Wake haukujumuisha makadirio ya chini ya tabia na sifa Zake Mwenyewe, bali katika kujifananisha na wanadamu walioanguka, ili kuwainua pamoja Naye katika maisha ya juu. Hata hivyo ni wachache kiasi gani wanaona chochote cha kuvutia katika unyenyekevu wa Kristo! Walimwengu daima wanajitahidi kujiinua wenyewe mmoja juu ya mwingine; lakini Yesu, Mwana wa Mungu, alijinyenyekeza ili kumwinua mwanadamu. Mwanafunzi wa Kweli wa Kristo atafuata mfano Wake. Laiti akina mama wa kizazi hiki wangehisi utakatifu wa utume wao, si kujaribu kushindana na majirani zao matajiri katika muonekano, bali kutafuta kumheshimu Mungu kwa utendaji wa uaminifu wa wajibu. Ikiwa kanuni sahihi kuhusiana na kiasi zingepandikizwa katika vijana ambao wanapaswa kuunda na kuumba jamii, kungekuwa na hitaji kidogo la pambano juu ya kutalawala nafsi au kiasi. Uimara wa tabia, kudhibiti maadili, vingeshinda, na kwa nguvu za Yesu majaribu ya siku hizi za mwisho yangepingwa. {FEsw 142.3}

Ni jambo gumu sana kuachana na tabia ambazo zimeendekezwa Maisha yote. Pepo la kutokuwa na kiasi lina nguvu, na halishindwi kwa urahisi. Lakini ikiwa wazazi wanaanza vita dhidi yake kwenye mazungumzo ya familia wanapoota moto, katika familia zao wenyewe, katika kanuni wanazowafundisha watoto wao tangu wakiwa wachanga sana, basi wanaweza kutumaini mafanikio. Itawalipa, akina mama, kutumia masaa ya thamani ambayo mmepewa na Mungu katika kutengeneza tabia za watoto wenu, na katika kuwafundisha kuzingatia kabisa kanuni za kiasi katika kula na kunywa. {FEsw 143.1}

Amana takatifu imewekwa kwa wazazi, kulinda mwili na mfumo wa maadili ya watoto wao, ili mfumo wa neva uweze kuwa na uwiano mzuri, na nafsi isihatarishwe. Akina baba na akina mama wanapaswa kuelewa sheria za maisha, ili wasiweze kwa ujinga, kuruhusu mielekeo mibaya isitawi kwa watoto wao. Lishe huathiri afya ya mwili na maadili. Kwa uangalifu kiasi gani, basi, akina mama wanapaswa kujifunza ili kuweka mezani vyakula rahisi zaidi, vya afya, ili viungo vya mmeng'enyo wa chakula visifanywe kuwa dhaifu, mishipa ya neva ikakosa kuwa na uwiano, au mafundisho wanayowapa watoto wao kupingwa. {FEsw 143.2} F

Shetani anaona kwamba hawezi kuwa na nguvu kubwa sana juu ya akili wakati uchu wa kula unapodhibitiwa kama wakati unapoendekezwa, na daima hufanya

kazi ili kuwaongoza watu katika kuudekeshwa. Kupitia ya ushawishi wa chakula kisicho na afya, dhamiri inataabishwa na kufanywa isiweze kufikiri inavyopaswa, akili hutiwa giza, na unyeti wake kufanya maamuzi bora huharibiwa. Lakini hatia ya mkosaji haipungui kwa sababu dhamiri imeharibiwa hadi ikawa haina uwezo wa kufikiri kabisa tena. {FEsw 143.3} F

Kwa kuwa hali ya akili yenye afya inategemea hali ya kawaida ya nguvu muhimu, ni uangalifu gani unapaswa kuchukuliwa ili vichocheo (nikotini-kahawa, colacola, redbull) au dawa zenye kileo au zenye kuleta uraibu visitumiwe kamwe (narcotics)! Bila bado tunaona kwamba idadi kubwa ya hao wanaodai kuwa Wakristo wanatumia tumbaku. Wanachukia ubaya wa kutokuwa na kiasi; na ijapokuwa wao wanazungumza dhidi ya matumizi ya vileo, watu hao hao wanatema mate ya ugoro ambayo ni tumbako. Lazima kuwe na mabadiliko ya hisia kuhusiana na matumizi ya tumbaku kabla ya mizizi ya uovu haijafikiwa. Tunaisukuma mada hii hadi mwisho. Chai na kahawa hukuza uchu wa vichocheo vikali zaidi. Na kisha tunakaribia zaidi nyumbani, kwa maandalizi ya chakula, na kuuliza, Je, kutawala nafsi na kiasi hutekelezwa katika mambo yote? Je, matengenezo ambayo ni muhimu kwa afya na furaha hufanyika hapa? {FEsw 144.1}

Kila Mkristo wa kweli atakuwa na udhibiti wa hamu yake kula na tamaa zake za mwili. Isipokuwa yuko huru kutoka katika utumwa wa uchu wa kula, hawezi kuwa, mtumishi mkweli na mtiifu wa Kristo. Kuendekeza uchu wa kula na tamaa huhafifisha matokeo ya ile Kweli ndani ya moyo. Haiwezekani kwa Roho na nguvu ya Ukweli kutakasa mtu, nafsi, mwili na Roho, ikiwa anadhibitiwa na tamaa za kimwili. {FEsw 144.2} — *Christian Temperance and Bible Hygiene, 75-80, 1890.*

ELIMU NA AFYA

Kwa vizazi vingi mfumo uliopo wa elimu umekuwa na uharibifu kwa afya, na hata kwa maisha yenyewe. Wazazi na walimu wengi wanashindwa kuelewa kwamba katika miaka ya awali ya mtoto tahadhari na umakini mkubwa zaidi inahitaji kuweka kwenye mfumo wa mwili, ili hali nzuri ya kimwili na ubongo iweze kulindwa. Imekuwa desturi kuhimiza upelekaji wa watoto shule wakiwa watoto wachanga bado, wanaohitaji uangalizi wa mama. Katika hali nyingi, watoto wadogo wanasongamana katika vyumba vya shule visivyo na mzunguko wa hewa unaofaa au unaotosha, ambapo wanakaa katika mkao usiofaa kwa uvutaji pumzi, na juu ya madawati yaliyotengenezwa vibaya, na matokeo yake, miili ya vijana na watoto huharibika kwa kupata ulema. Watoto wadogo, ambao viungo vyao na misuli yao haina nguvu, na akili zao hazijakua kikamilifu, hufungiwa ndani kwa muda mrefu, kwa maumivu yao. Wengi kwa kuanzia wana nguvu kidogo tu za kushikilia maisha, na kufungiwa shuleni siku hadi siku huwafanya kuwa na wasiwasi, na kuwa wagonjwa. Miili yao iko duni kwa sababu ya hali ya uchovu ya mfumo wa neva. Hata hivyo taa ya uzima inapozimika, wazazi na walimu huwagundui kwamba walihusika kwa njia yoyote katika kuzizima cheche muhimu za uzima. Wakiwa wamesimama kando ya kaburi la mtoto wao, wazazi wanaoteseka kwa huzuni hutazama kufiwa kwao kama matokeo ya majaliwa maalum ya Mungu, wakati ilikuwa ni mwendo wao wenyewe usio na udhuru, wa kijinga ulioharibu maisha ya mtoto. Katika hali kama hizo, kuhamisha hatia ya kifo cha mtoto wao kwa Mungu, ni harufu/ladha ya kufuru. Mungu anataka watoto wadogo waishi, na wapate elimu ifaayo, ili wapate kukuza tabia nzuri, na kisha wakamtukuze katika dunia hii, na kumsifu katika ulimwengu ulio bora zaidi. {FEsw 145.1}

Wazazi na walimu walio na jukumu la kuwafunza hawa watoto, ni wachache kiasi gani kati yao wanaotambua wajibu wao mbele za Mungu kufahamu mfumo wa kimwili, ili wapate kujua jinsi ya kuhifadhi maisha na afya ya wale ambao wamewekwa katika uangalizi wao. Maelfu ya watoto wanakufa kwa sababu ya ujinga wa hao wanaowahudumia. {FEsw 145.2}

Watoto wengi wameharibiwa maishani, na wengine wamekufa, kama matokeo ya utendaji wa dhuluma wa wazazi na walimu, katika kuilazimisha akili changa huku wakipuuza asili ya mwili. Watoto walikuwa wachanga sana kuwa kwenye chumba cha shule. Akili zao zilitindikiwa na masomo badala ya kuachwa bila ya kuwa na msongo. Watoto wadogo wanapaswa kuachwa huru kama wana-kondoo kukimbia nje. Wanapaswa kupewa fursa bora zaidi ili kuweka msingi wa mfumo mzuri. {FEsw 146.1}

Vijana ambao wanawekwa shuleni, wakiwa wamefungiwa kwa ajili ya kuweka

umakini kwenye masomo, hawawezi kuwa na afya njema. Juhudi za kiakili bila usawia wa mazoezi ya kimwili, huweka uwiano usiofaa wa damu kwenye ubongo, na hivyo mzunguko unakosa usawa. Ubongo huwa na damu nyingi, wakati miguu, na mikono huwa na damu kidogo sana. Saa za kusoma na burudani zinapaswa kudhibitiwa kwa uangalifu, na sehemu ya muda unapaswa kutumika katika kazi ya kimwili/mikono. Wakati tabia za wanafunzi katika kula na kunywa, kuvaa na kulala ni kwa mujibu wa sheria ya mwili; wanaweza kupata elimu bila kutoa mhanga afya zao. Somo lazima lirudiwe mara nyingi, na kushinikizwa nyumbani katika dhamiri, kwamba elimu itakuwa na thamani ndogo ikiwa hakuna nguvu ya kimwili ya kutumia baada ya kuipata. {FEsw 146.2}

Wanafunzi hawapaswi kuruhusiwa kuchukua masomo mengi kiasi kwamba hawatakuwa na wakati wa mazoezi ya mwili. Afya haiwezi kuhifadhiwa isipokuwa sehemu fulani ya kila siku inatolewa kwa shughuli za misuli katika hewa ya wazi. Saa zilizotajwa zinapaswa kutolewa kwa kazi ya mikono ya aina fulani, kitu chochote kitakachofanya sehemu zote za mwili kufanya kazi. Sawazisha ujazo wa nguvu za kiakili na za kimwili, na akili ya mwanafunzi itaburudishwa. Ikiwa ni mgonjwa, mazoezi ya mwili mara nyingi yatasaidia mfumo kurejesha hali yake ya kawaida. Wanafunzi wanapotoka chuoni, wanapaswa kuwa na afya bora zaidi na ufahamu bora wa sheria za maisha kuliko wakati walipoingia chuoni. Afya inapaswa kulindwa kwa utakatifu kama tabia. {FEsw 146.3}

Wanafunzi wengi hawajui ukweli kwamba lishe ina ushawishi mkubwa juu ya afya. Wengine hawajawahi kufanya juhudi zilizowekwa ili kudhibiti uchu wa kula, au kufuata sheria zinazofaa kuhusu lishe. Wanakula kupita kiasi, hata kwenye milo yao, na wengine hula katikati ya milo wakati jaribu hili linapowasilishwa kwao. Ikiwa wale ambao wanaodai kuwa Wakristo wanataka kujibu maswali yanayowatatiza, kwa nini akili zao ni butu sana, kwa nini matamanio yao ya kidini/kiroho ni dhaifu sana, hawahitaji, mara nyingi, kwenda mbali zaidi ya meza zao; hapa kuna sababu ya kutosha, ikiwa hakutakuwa na nyingine. {FEsw 147.1}

Wengi hujitenga na Mungu kwa kuendekeza tamaa yao tamaa ya kula. Yeye aonaye anguko la shomoro, anayehesabu nywele za kichwa, huitia alama dhambi ya wale wanaojiingiza katika uchu wa chakula kwa gharama ya kudhoofisha nguvu za kimwili, kudhoofisha akili, na kufisha mitazamo ya maadili. {FEsw 147.2}

Walimu wenyewe wanapaswa kuzingatia ipasavyo sheria za afya, ili waweze kuhifadhi nguvu zao wenyewe katika hali bora inavyowezekana, na kwa mfano na vile vile kwa kanuni, waweze kutoa ushawishi sahihi kwa wanafunzi wao. Mwalimu ambaye nguvu zake za kimwili tayari zimedhoofishwa na ugonjwa au kufanya kazi kupita kiasi, anapaswa kuzingatia sheria za maisha. Anapaswa kuchukua muda kwa ajili ya kupumzika. Hapaswi kuchukua jukumu la nje ya kazi yake ya shule, ambayo itamchosha, kimwili au kiakili, hadi mfumo wa neva zake kutokuwa na usawa; kwa maana katika hali hii atakuwa hafai kushughulika na akili, na hawezi

kujifanyia uadilifu yeye mwenyewe au hata kwa wanafunzi wake. {FEsw 147.3}

Taasisi zetu za elimu zinapaswa kupewa kila fursa ya kufundishia kuhusu utaratibu wa mfumo wa binadamu. Wanafunzi wanapaswa kufundishwa jinsi ya kupumua, jinsi ya kusoma na kuzungumza ili kwamba mkazo usitokee kwenye koo na kwenye mapafu, bali juu ya misuli ya tumbo. Walimu wanahitaji kujielimisha katika mwelekeo huu. Wanafunzi wetu wanapaswa kuwa na mafunzo ya kina, ili waweze kuingia kwenye ya utendaji wenye bidii na maarifa ya akili kwenye makazi ambayo Mungu amewapa {mwili wao}. Wafundishe kwamba wanapaswa kujifunza kadri waishivyo. Na unapowafundisha, kumbuka pia watafundisha wengine. Fundisho lako litakuwa likirudiwa kwa manufaa ya wengi zaidi kuliko kuketi mbele yako siku baada ya siku. {FEsw 147.4} – *Christian Temperance and Bible hygiene, 81-84, 1890.*

ELIMU YA NYUMBANI

Kazi ya mama ni muhimu sana. Kwenye shughuli za masumbufu ya nyumbani na majukumu yenye mitihani katika maisha ya kila siku, anapaswa kujitahidi kushinikiza ushawishi ambao utabariki na kuinua nyumba yake. Kwa watoto waliowekwa chini ya utunzaji wake, kila mama ana jukumu takatifu kutoka kwa Baba wa Mbinguni; na ni fursa yake, kwa njia ya neema ya Kristo, kuziunda/kuzifinyanga tabia zao kufuatana na kielelezo cha kimbingu, kuweka ushawishi juu ya maisha yao ambao utawavuta kwa Mungu na Mbinguni. Ikiwa akina mama daima wangelitambua wajibu wao, na kulifanya liwe kusudi lao la kwanza, na utume wao muhimu zaidi, kuwafanya watoto wao kufaa kwa majukumu ya maisha haya na kwa heshima ya siku zijazo za maisha ya milele, tusingeona taabu ambayo sasa iko katika nyumba nyingi katika nchi yetu. Kazi ya mama ni ile inayohitaji kukuzwa katika maisha yake yeye mwenyewe, ili apate kuwaongoza watoto wake kwa ajili ya mafanikio ya juu na ya juu zaidi. Lakini Shetani anaweka mipango yake ya kuzinasa Roho za wazazi na watoto. Akina mama wanavutwa kutoka katika majukumu ya nyumbani na mafunzo makini ya watoto wao, kwa ajili ya kutumikia nafsi na ulimwengu. Ubatili, mitindo, na mambo yenye umuhimu mdogo huruhusiwa kuchukua umakini wao, na elimu ya kimwili na kimaadili ya watoto wa thamani hupuuza. {FEsw 149.1}

Ikiwa anafanya mila na desturi za ulimwengu kuwa kigezo chake, mama atakuwa hafai kwa majukumu yake kwa sehemu yake. Iwapo mitindo imemgeuza kuwa mtumwa, itadhoofisha nguvu zake za uvumilivu, na kuyafanya maisha kuwa mzigo badala ya baraka. Kupitia udhaifu wa kimwili anaweza kushindwa kufahamu thamani ya fursa ambazo ni zake, na familia yake inaweza kuachwa ikue bila faida ya mawazo yake, maombi yake, na maelekezo yake ya bidii. Ikiwa akina mama wangezingatia upendeleo wa ajabu ambao Mwenyezi Mungu amewapa pekee, wasingegeuzwa kirahisi hivyo kutoka katika majukumu yao matakatifu kwenda katika mambo madogo madogo ya ulimwengu. {FEsw 149.2}

Kazi ya mama huanza na mtoto mchanga mikononi mwake. Nimeona mara nyingi kichanga akijitupa, na kujigaragaza na kupiga kelele, kama mapenzi yake yamepingwa kwa njia yoyote. Huu ni wakati wa kukemea Roho mbaya. Adui atajaribu kudhibiti akili za watoto wetu, lakini, je, tutamruhusu kuwafinyanga kulingana na mapenzi yake? Hawa watoto wadogo hawawezi kutambua ni Roho gani inayosukuma na kuwashawishi, na ni wajibu wa wazazi kutumia maamuzi na busara zao. Tabia zao lazima zitazamwe kwa makini. Mielekeo yao mibaya inapaswa kuzuiwa, na akili kuchochewa katika kupendelea haki. Mtoto anapaswa kutiwa moyo katika kila jitihada ili kujitawala nafsi. {FEsw 150.1}

Utaratibu unapaswa kuwa ni sheria katika tabia zote za watoto. Akina mama hufanya makosa makubwa kwa kuwaruhusu watoto kula katikati ya milo. Tumbo huharibika kwa mazoea haya, na msingi unawekwa kwa ajili ya mateso ya baadaye. Kutotulia au kukasirishwa kwao kunaweza kusababishwa na chakula kisichofaa, yaani kile ambacho bado hakijameng'enywa; lakini mama anahisi kwamba hawezi kuchukua muda wake ili kuchunguza juu ya jambo hilo na kurekebisha usimamizi wake mbaya. Wala hawezi kuchukua muda ili kutuliza wasiwasi na kukosa subira kwao. Huwapa hawa wadogo wanaoteseka kipande cha keki au kitu kitafunio kingine cha kupendeza ili kuwanyamazisha, lakini hii huongeza tu uovu. Baadhi ya akina mama, katika mahangaiko, na wasiwasi wao wa kufanya kazi kubwa kupita kiasi, wanafanya mambo kwa haraka na wasiwasi wa moyo, kiasi kwamba wanakuwa na hasira kuliko watoto, na kwa kuwakemea na hata kupatwa hasira kali au kuwapiga makofi ili kujaribu kuwatia hofu watoto ili watulie. {FEsw 150.2}

Akina mama mara nyingi hulalamika juu ya afya dhaifu ya watoto wao, na kumwona daktari, wakati, ikiwa wangetumia busara ya kawaida kidogo tu, wangeona kwamba shida inasababishwa na makosa katika chakula. {FEsw 150.2}

Tunaishi katika zama za ulafi, na mazoea ambayo kwayo vijana wameelimishwa, hata na Waadventista wengi wa Sabato wapo kinyume na sheria za asili. Niliketi wakati fulani mezani na watoto kadhaa waliokuwa chini ya miaka kumi na miwili. Nyama ilipakuliwa kwa wingi, na kisha msichana maridadi na mwenye neva zenye wasiwasi akaomba matango yaliyowekewa siki (pickles*). Chupa ya achari, iliyokuwa na viungo ambavyo vimekaangwa na haradali na vyenye harufu kali, ilikabidhiwa kwake, naye akajihudumia mwenyewe kwa uhuru. Mtoto huyu alijulikana kwa tabia yake ya wasiwasi wa neva, na hasira zinazoamka kwa urahisi, na vitoweo hivi vya vikali kwa ugwadu na pilipili ndivyo vilizalisha ile hali. Kijana mkubwa alifikiri hawezi kula chakula bila nyama, na alionyesha kutoridhika kabisa, na hata kukosa heshima, alipokosa kupewa hiyo nyama. Mama yake alikuwa amemwendekiza katika matamania yake hadi akawa mdogo punde kuliko mtumwa wa viungo vyake. Kijana huyo hakupewa kazi, na alitumia sehemu kubwa zaidi ya muda wake katika kusoma kile ambacho hakikuwa na maana au kibaya zaidi kuliko kutokuwa na maana. Alilalamika daima juu ya maumivu ya kichwa, na hakuwa anafurahishwa kwa chakula rahisi (hakupenda ladha ya chakula sahili cha mimea na kisicho na viungo vya kukasirisha tumbo). {FEsw 150.3}

Wazazi wanapaswa kutoa kazi kwa watoto wao. Hakuna kitu kitachokuwa chanzo cha uhakika kwa uovu kuliko uvivu. Kazi ya kimwili ambayo huleta uchovu wa kiafya kwa misuli, italeti hamu ya kula chakula rahisi, kizuri, na vijana ambao wametumika ipasavyo hawatainuka kutoka mezani wakinung'unika kwa sababu hawaoni mbele yao sahani ya nyama na karamu za vyakula mbalimbali ili kujaribu hamu yake ya chakula. {FEsw 151.1}

Yesu, Mwana wa Mungu, katika kufanya kazi kwa mikono Yake katika kazi ya

useremala, alitoa mfano kwa vijana wote. Hebu wanaodharau kuchukua majukumu ya kawaida ya maisha wakumbuke kuwa Yesu alikubali kuwa chini ya wazazi wake, na akatenda sehemu Yake katika kuleta riziki ya familia. Anasa chache zilionekana kwenye meza ya Yusufu na Mariamu, kwani walikuwa miongoni mwa watu maskini na wa hali ya chini. {FEsw 151.1}

Wazazi wanapaswa kuwa mfano kwa watoto wao katika matumizi ya pesa. Wapo wale ambao mara tu wanapopata pesa, huzitumia kwa ajili ya chakula cha anasa, au kwa ajili ya mapambo ya mavazi yasiyo ya lazima, na wakati upatikanaji wa fedha unapopungua, wanahisi uhitaji wa kile walichokifanyia ubaradhifu. Ikiwa wana mapato mengi, wanatumia kila pesa senti yao; ikiwa ndogo, haitoshi kwa tabia za ubadhirifu walionao, na wanakopa ili kukidhi mahitaji. Wanakusanya kutoka kwa chanzo chochote kinachowezekana ili kukidhi mahitaji yao ya mapambo au vitu visivyo vya lazima. Wanakuwa si waaminifu na wasio wakweli, na kumbukumbu inayosimama dhidi yao katika vitabu vya Mbinguni ni ile ambayo hawatapenda kuitazama siku ya hukumu. Tamaa ya jicho lazima ishibishwe/iridhishwe, na tamaa ya kula iendekezwe, nao hujiweka wenyewe kuwa masikini kwa tabia zao zisizo na hekima na zenye ufujaji, wakati wangeweza kujifunza kuishi kulingana na uwezo wao. Ubadhirifu ni miongoni mwa dhambi ambazo zinawazinga vijana kwa wepesi. Wanadharau tabia za kiuchumi, kwa hofu ya kufikiriwa kuwa ni wabahili, wakatili na wachungu. Je, Yesu, Mkuu wa Mbinguni, ambaye amewapa mfano wa uvumilivu na uchumi, atasema nini kwao? {FEsw 151.3}

Sio lazima kutaja kila kitu hapa kuhusu vile uchumi unavyoweza kufanywa katika kila jambo mahususi. Wale ambao mioyo yao imesalimishwa kwa Mungu, na wanaolichukulia Neno Lake kama kiongozi wao, watajua jinsi ya kutenda wao wenyewe katika majukumu yote ya maisha. Watajifunza juu ya Yesu, ambaye ni mpole na mnyenyekevu wa moyo; na katika kukuza upole wa Kristo watafunga mlango dhidi ya majaribu yasiyohesabika. {FEsw 152.1}

Hawatakuwa wakijifunza jinsi ya kuendekeza ulafi wa chakula na matamano ya kujionyesha, wakati wengi hawawezi hata kuondoa njaa kutoka malangoni mwa nyumba zao. Kiasi kikubwa kinachotumiwa kila siku katika mambo yasiyo ya lazima, kwa wazo kuwa, "Ni senti tano tu," "Ni kiasi kidogo tu," inaonekana kuwa kidogo sana; lakini zidisha hivi vidogo kwa siku za mwaka, na kadiri miaka inavyosonga, ndivyo mlolongo wa takwimu utakavyoonekana wa ajabu. {FEsw 152.2}

Bwana amependezwa kuwasilisha mbele yangu maovu ambayo hutokana na tabia ya ubadhirifu, ili nipate kuwaonya wazazi kuwafundisha watoto wao uchumi mkali. Wafundishe kwamba pesa zilizotumika kwa ajili yale ambayo hawayahitaji, inapotoshwa kutoka kwenye matumizi yake sahihi. Yule ambaye sio mwaminifu katika lililo dogo, hatakuwa mwaminifu katika lililo kubwa. Ikiwa watu hawana

uaminifu kwa mali ya dunia, hawawezi kuaminiwa utajiri wa milele. Weka mlinzi juu ya uchu wa kula (ulafi wa chakula); wafundishe watoto wako kwa mfano na pia kwa maagizo kutumia lishe rahisi/sahili. Wafundishe kuwa wenye bidii, si tu kuwa na shughuli nyingi, bali kufanya kazi yenye manufaa. Tafuta kuamsha hisia za maadili. Wafundishe kwamba Mungu ana madai juu yao, hata tangu miaka ya mapema ya utoto wao. Waambie kwamba kuna ufidadi wa kimaadili unaopaswa kukabiliwa katika kila upande, kwamba wanahitaji kuja kwa Yesu na kujitoa Kwake, mwili na Roho, na kwamba ndani Yake watapata nguvu za kupinga kila jaribu. Wakumbushe kwamba hawakuumbwa ili wajipendeze wao wenyewe tu, bali wawe mawakala wa Bwana kwa makusudi matakatifu na bora zaidi. Wafundishe, wakati majaribu yanapowasukuma katika njia za kuendekeza nafsi, wakati Shetani anatafuta kuwafanya wasimwone Mungu, wamtazame Yesu, wakiomba, “Bwana, uniokoe, nisije nikatekewa.” Malaika watakusanyika kando yao kama jibu la maombi yao, na kuwaongoza kwenye njia zilizo salama. {FEsw 152.3}

Kristo aliwaombea wanafunzi Wake, si kwamba waondoke katika ulimwenguni huu, bali walindwe na yule mwovu, ili waweze kuzuiwa kujisalimisha au kuanguka katika majaribu ambayo wangekutana nayo kila pande. Haya ni maombi ambayo yanapaswa kutolewa na kila baba na mama. Lakini je, wangemsihi Mungu kwa ajili ya watoto wao, na kisha kuwaacha wafanye wapendavyo? Je! watakuza uchu wa kula mpaka uwatawale, na kisha kutarajia kuwadhibiti watoto? —La; kiasi na kujitawala vinapaswa kufundishwa kutoka utotoni hadi utu uzima. Juu ya mama kunapaswa kuwa na wajibu wa kazi hii kwa kiasi kikubwa. Mshikamano wa kidunia ulio wa kipekee zaidi ni ule uliopo kati ya mama na mtoto wake. Mtoto anavutiwa kwa urahisi zaidi na maisha na mfano wa mama kuliko wa baba, kwa sababu ya muunganiko huu ulio imara wenye nguvu na wa kipekee. Bado wajibu wa mama ni mzito, na unapaswa kuwa na msaada wa mara kwa mara wa baba. {FEsw 153.1}

Kutokuwa na kiasi katika kula na kunywa, kutokuwa na kiasi katika kazi, kutokuwa na kiasi katika karibu kila kitu, kuko kila upande. Wale ambao hufanya bidii kubwa kukamilisha kazi nyingi kwa wakati mmoja, na kuendelea kufanya kazi wakati busara yao inapowaambia wanapaswa kupumzika, hawapati faida yoyote. Wanaishi kwa mtaji wa kukopa. Wanatumia nguvu muhimu ambayo watahitaji wakati ujao. Na wakati nishati waliyoitumia kwa uzembe itakapohitajika, wanashindwa kwa kuikosa. Nguvu za mwili zimeisha, nguvu za akili zinashindwa. Wanatambua kuwa wamepata hasara, lakini hawajui ni nini. Wakati wao wa kuihitaji umefika, lakini rasilimali za kimwili wao zimechoka. Kila anayekiuka sheria za afya lazima wakati fulani awe mgonjwa kwa kiwango kikubwa au kidogo. Mungu ametupa nguvu ya kiakili, ambayo itahitajika katika vipindi tofauti vya maisha yetu. Ikiwa tutamaliza nguvu hii bila kujali kwa kuitumikisha, wakati fulani tutakuwa wenye hasara. Manufaa yetu yatapunguzwa, kama si maisha yetu yenyewe kuharibiwa. {FEsw 153.2}

Kama kanuni, kazi ya siku haipaswi kufanywa kwa muda mrefu hadi jioni. Ikiwa saa zote za siku zimetumiwa vizuri, kazi kusogezwa hadi jioni ni kupitiliza sana, na mfumo uliolemewa utateseka kutokana na mzigo uliowekwa juu yake. Nimeonyeshwa kwamba wale wanaofanya hivi, mara nyingi hupoteza zaidi ya wanaavyopata/kupata, kwani nguvu zao zinatindikiwa, na wanafanya kazi kwa msisimko wa neva. Huenda wasitambue madhara yoyote papo hapo, lakini hakika wanadidimiza mifumo ya miili yao. {FEsw 154.1}

Hebu wazazi watoe muda wa jioni kwa ajili ya familia zao. Waachane na mifadhaiko na taabu za mchana. Mume na baba angefaidi mengi ikiwa angeweka sheria ya kutoharibu furaha ya familia yake kwa kuleta matatizo ya kibarua chake nyumbani ili kuwahangaisha na kuwapa wasiwasi. Anaweza kuhitaji ushauri wa mke wake katika mambo magumu, na wote wawili wanaweza kupata ahueni katika mashaka yao kwa kutafuta hekima ya Mungu wakiwa na umoja; lakini kuweka akili idumu kila wakati kuhusu shughuli au kibarua, hudhuru afya ya akili na mwili. {FEsw 154.2}

Hebu mida ya jioni iitumike kwa furaha kwa kadri iwezekanavyo. Hebu nyumba iwe mahali ambapo uchangamfu, adabu, kuheshimiana na upendo vinakuwepo. Hili litapafanya kuwa mahali pa kuvutia kwa watoto. Ikiwa wazazi wataendelea kukopa matatizo, kukasirika-kasirika na kutafutatafuta makosa, watoto hushiriki Roho ile ile ya kutoridhika na ugomvi, na nyumbani panakuwa ndio mahali pa huzuni na kukosa faraja zaidi duniani. Watoto hupata raha yao zaidi kwa wapita njia, kwa marafiki wasiojali au wa hovyoyote, au mitaani, kuliko nyumbani. Haya yote yanaweza kuepukwa ikiwa kiasi katika mambo yote kingezingatiwa, na uvumilivu ungekuzwa. Kujitawala kwa kila sehemu ya wanafamilia kutapafanya nyumbani kuwa sawa na paradiso. Fanya vyumba vya nyuma yako viwe vya furaha kadri iwezekanavyo. Hebu watoto wapaone nyumbani mahali pa kuvutia zaidi duniani. Wawekee juu yao mvuto ambao hawataweza kuupata kwa marafiki wa mitaani, wala wasiyafikirie maeneo yenye maovu isipokuwa kwa hofu. Ikiwa maisha ya nyumbani ndivyo yanavyopaswa kuwa, tabia zilizoundwa zitakuwa ni ulinzi mkali dhidi ya mashambulizi ya majaribu wakati vijana watakapoyaacha makao ya nyumbani kwa ajili ya ulimwengu. {FEsw 154.3}

Je, tunajenga nyumba zetu kwa ajili furaha ya familia, au tu kwa ajili ya maonesho? Je, tunawaandalia watoto wetu vyumba vya kupendeza, vyenye mwanga wa jua, au tunaviweka kuwa vyenye giza na kufungwa, tukivihifadhi kwa ajili ya wageni ambao hawatutegemei kwa ajili ya furaha yao? Hakuna kazi adhimu ambayo tunaweza kuifanya, hakuna faida kubwa zaidi ambayo tunaweza kuitoa kwa jamii, kuliko kuwapa watoto wetu elimu ifaayo, tukiwasisitizia, kwa kanuni na mfano, kanuni muhimu kwamba usafi wa maisha na unyofu wa nia utawastahilisha vyema zaidi kutenda sehemu yao katika ulimwengu. {FEsw 155.1}

Tabia zetu za bandia/feki hutunyima fursa nyingi na kufurahia maisha, na

kutufanya tusiwe wa manufaa. Maisha ya fasheni au mitindo ni magumu, ni maisha yasiyo na shukrani (hayakidhi). Ni mara ngapi muda, pesa, na afya hutolewa kafara, subira hujaribiwa sana, na kutawala nafsi hupotea, kwa ajili tu ya kujionesha. Ikiwa wazazi wangeshikilia maisha rahisi/sahili, bila ya kuendekeza gharama kwa ajili ya kujifurahisha kwa ubatili, na kufuata mitindo/fasheni tu za maisha haya; kama wao wangedumisha uhuru uliotukuka katika haki na kutenda yale yaliyo mema, bila kusukumwa na ushawishi wa wale ambao, huku wakimkiri Kristo, wanakataa kuinua msalaba wa kujinyima au kujikana nafsi, wangetoa kwa mfano huu tu kwa watoto elimu yenye thamani kubwa. Watoto wangekuwa wanaume na wanawake wenye thamani ya kimaadili, na, kwa zamu yao, watoto hao wangekuwa na ujasiri kusimama kwa ushujaa kwa ajili ya haki, hata dhidi ya mitindo ya kisasa na maoni maarufu, yale yanayopendwa na wengi. {FEsw 155.2}

Kila tendo la wazazi linaeleza juu ya mustakabali wa maisha ya mbele ya watoto. Kwa kutumia muda na pesa kwa mapambo ya nje na kujiendekeza kwa tamaa potovu, wanakuza ubatili, ubinafsi, na tamaa kwa watoto. Akina mama wanalalamika kulemewa sana kwa huduma na kazi kiasi cha kukosa muda kuwafundisha wao wadogo kwa subira, na kuwahurumia katika masikitiko yao na majaribu. Mioyo michanga hutamani huruma na kujali, na ikiwa wataikosa na wasiipate kutoka kwa wazazi wao, wataitafuta kutoka kwa vyanzo ambavyo vinaweza kuhatarisha akili na maadili. Nimesikia akina mama wanaowanyima watoto wao furaha isiyo na hatia, kwa kukosa muda na mawazo, huku vidole vyao viko kwenye shughuli nyingi (za kutarizi) na macho yaliyochoka yakiwa yanajishughulisha kwa umakini kwenye kipande cha kitambaa kisicho na maana, cha mapambo au nakshi tu, kitu ambacho kinaweza kutumika tu kukuza ubatili na ubadhirifu kwa watoto. "Kadri tawi linavyopindishwa, ndivyo mti unavyoinama." (samaki mkunje angali mbichi) Kari watoto wanavyokaribia utu uzima, masomo haya yanazaa matunda katika kiburi na upotovu wa maadili. Wazazi huchukia makosa ya watoto, lakini ni wapofu kuona ukweli kwamba wanavuna tu mavuno kutoka kwenye mbegu zao wenyewe walizopanda. {FEsw 156.1}

Wazazi Wakristo, jitwikeneni mzigo wa maisha yenu, na mfikirie kwa unyoofu juu ya majukumu matakatifu yaliyo juu yenu. Lifanyeni Neno la Mungu kuwa kipimo chenu, badala ya kufuata mitindo na desturi za dunia, tamaa ya macho, na kiburi cha uzima. Furaha ya baadaye ya familia zenu na ustawi wa jamii hutegemea sana elimu ya kimwili na kimaadili ambayo watoto wenu hupokea katika miaka ya kwanza ya maisha yao. Ikiwa ladha na tabia zao ni rahisi kwa vitu vyote kama inavyopaswa kuwa, ikiwa mavazi ni safi, bila mapambo ya ziada, akina mama watapata muda wa kuwafurahisha watoto wao, na kuwafundisha utii wa upendo. {FEsw 156.2}

Usiwapeleke watoto wako wadogo shuleni mapema sana. Mama anapaswa kuwa mwangalifu jinsi anavyoamini kufinyangwa/kuundwa kwa akili ya mtoto wake

na mikono ya watu wengine. Wazazi wanapaswa kuwa walimu bora wa watoto wao mpaka wafikie umri wa miaka minane au kumi. Chumba chao cha shule kinapaswa kuwa nje, kwenye hewa wazi, katikati ya maua na ndege, na kitabu chao cha kiada kiwe hazina ya asili. Kwa haraka kadri akili zao zinavyoweza kufahamu, ndivyo wazazi wanapaswa kufungua mbele yao kitabu kikuu cha Mungu cha asili (uumbaji). Haya masomo, yanayotolewa katikati ya mazingira kama hayo, hayatasahaulika hivi karibuni. Maumivu na juhudi kubwa inapaswa kuchukuliwa ili kuandaa udongo wa moyo ili mpanzi apande mbegu njema. Ikiwa nusu ya wakati na kazi ambayo sasa ni mbaya zaidi kuliko kuipoteza katika kufuata mitindo ya ulimwengu, ingetolewa katika kukuza akili za watoto, kwa malezi ya tabia sahihi, mabadiliko makubwa yangeonekana katika familia. {FEsw 156.3}

Muda si mrefu nilisikia mama mmoja akisema kwamba anapenda kuona nyumba iliyojengwa vizuri, kwamba kasoro katika mpangilio na kutolingana kwa nakshi za mbao katika kuimalizia kunamuumiza. Silaumu ladha nzuri katika suala hili, lakini nilipomsikiliza, nilijuta kwamba uzuri huu unaweza kuwa haujawekwa katika mbinu zake zake mama huyu katika kuwasimamia watoto wake. Haya ndiyo yalikuwa majengo ambayo aliwajibikia nayo kwa uundaji wake {tabia za watoto};na bado njia zao mbaya, rafu, zenye jeuri, na zisizo na adabu, mihemko mibaya, ubinafsi, na mapenzi yasiyodhibitiwa, yalionekana kuleta uchungu kwa wengine. Tabia mbaya zilizoundwa vibaya, vipande visivyolingana vya utu wao wa tabia, kwa hakika walikuwa navyo, lakini bado mama alikuwa kipofu kwa yote. Mpangilio wa nyumba yake ulikuwa wenye umuhimu zaidi kwake kuliko ulinganifu wa tabia za watoto wake. {FEsw 157.1}

Usafi na utaratibu ni wajibu wa Kikristo, lakini hata hivi vinaweza kuchukuliwa kwa kupitiliza sana, na kufanywa kuwa vya muhimu kwa kupitiliza, wakati mambo yenye umuhimu mkubwa zaidi yakipuuzwa. Wale wanaopuza maslahi ya watoto kwa mambo haya hutoa zaka ya mnanaa na jira; huku wakipuza mambo makuu ya sheria, yaani, haki, rehema, na upendo wa Mungu. {FEsw 157.2}

Wale watoto ambao wanadekeshwa au kuendekezwa zaidi, wanakuwa watu wenye nia zao wenyewe, na shauku, zisizopendeza. Afadhali wazazi wangeweza kutambua kwa busara, kwamba, mafunzo ya mapema kwayo hutegemea furaha ya wote wawili, wazazi na watoto. Ni akina nani hawa wadogo, ambao wamekabidhiwa kwa ajili ya uangalizi wetu? Hao ndio washiriki wachanga zaidi wa familia ya Bwana. “Chukua mwana huyu, binti huyu,” Anasema, “nitunzie hao, na wafanye kufaa ‘ili wang’arishwe kwa ajili ya jumba la kifalme,’ ili wapate kung’aa katika nyua za Bwana.” Kazi ya thamani! Kazi ya Muhimu! Hata hivyo tunaona akina mama wakiugua kwa matamanio uwanja mpana zaidi wa kazi, kwa kazi fulani ya kufanya kwenye umishionari wa mbali. Laiti wangeweza kwenda Afrika au India, wangehisi kwamba walikuwa wanafanya jambo fulani la umuhimu mkubwa zaidi. Lakini kutekeleza majukumu madogo ya kila siku ya maisha, na kuyaendeleza kwa

uaminifu, kwa ustahimilivu, kunaonekana kwao kuwa ni jambo lisilo la maana. Kwa nini hili? Je, si kwa sababu mara nyingi kazi ya mama haithaminiwi sana? Ana masumbufu elfu na mizigo ambayo baba ni kwa nadra sana anakuwa na ujuzi wowote nayo. Mara nyingi sana anarudi nyumbani akiwa na matatizo yake na fadhaa za shughuli na kuiwekea familia kivuli cha huzuni, na ikiwa hapati kila kitu kama vile akili yake ingependa pale nyumbani, basi anaongea hisia zake kwa kukosa subira na kutafuta makosa. Anaweza kujivunia yale aliyofanikiwa kutimiza kwa siku nzima, lakini kazi ya mama, kwa akili yake, ni ya kiwango kidogo, au ni ya kutothaminiwa au ya hali ya chini. Kwake masumbufu yake yanaonekana kuwa madogo. Yeye ni kupika tu chakula, kuangalia wa watoto, wakati mwingine kuishughulikia familia kubwa, na kuweka nyumba katika utaratibu. Amejaribu siku nzima kuweka mambo ya nyumbani kwenda vizuri. Amejitahidi, ingawa amechoka na amefadhaishwa, kuongea kwa upole na kwa furaha, na kuwafundisha watoto na kuwaweka katika njia iliyo sawa. Yote haya yamegharimu juhudi, na uvumilivu mwingi kwa upande wake. Hawezi, kwa upande wake, kujivunia kile alichokifanya. Na inaonekana kwake kana kwamba hajafanya lolote au kufanikisha lolote. Lakini siyo hivyo. Ingawa matokeo ya kazi yake hayaonekani, malaika wa Mungu wanamwangalia mama mlezi aliyetindikiwa, wakiona mizigo anayoibeba siku hadi siku. Huenda jina lake lisionekane kamwe kwenye kumbukumbu za kihistoria, au kupokea heshima na pongezi ya ulimwengu, kama ilivyo kwa mume na baba; lakini amehifadhiwa katika katika kitabu cha umilele cha Mungu. Anafanya awezavyo, na nafasi yake mbele ya Mungu, na nafasi yake imetukuka zaidi kuliko ile ya Mfalme katika kiti chake cha enzi; maana anashughulikia tabia, anazijenga akili. {FEsw 157.3}

Akina mama wa siku hizi wanatengeneza jamii ya baadaye. Ni muhimu kiasi gani basi, kwamba watoto wao walelewe kiasi kwamba wataweza kupinga majaribu watakayokutana nayo kila upande katika maisha ya baadae! {FEsw 159.1}

Vyovyote wito wake na mashaka yake yawezavyo kuwa, hebu baba achukue katika nyumba yake sura ile ile ya tabasamu na sauti ya kupendeza ambayo siku nzima amekuwa akiwasalimia wageni na watu baki asiowajua. Hebu mke ahisi kwamba anaweza kuegemea mapenzi makubwa ya mume wake, –kwamba mikono yake itamtia nguvu na kumtegemeza katika taabu zake zote na masumbufu, kwamba ushawishi wake utamdumisha, na mzigo wake utapotea nusu ya uzito wake. Je! watoto si wake kama walivyo kwake? {FEsw 159.2}

Hebu baba atafute kurahisisha kazi ya mama. Katika muda ule ambao angeutoa kufurahia starehe za binafsi, hebu atafute kufahamiana na watoto wake—ashirikiane nao katika michezo yao, na katika kazi zao. Hebu awaelekeze kwenye maua mazuri, miti mirefu, ambayo kwa majani yake wanaweza kufuatilia kazi na upendo wa Mungu. Anapaswa kuwafundisha kwamba Mungu aliyeumba haya mambo yote hupenda uzuri na mema/wema. Kristo aliwaelekeza wanafunzi

wake kwenye maua ya kondeni na ndege wa angani, akiwaonesha jinsi Mungu anavyowajali, na akawasilisha hili kama ushahidi kwamba Yeye atamjali mwanadamu, ambaye ana ubora wa juu kuliko ndege na maua. Waambie watoto kwamba hata muda mwingi ungepotezwa kiasi gani kwa ajili ya kujaribu kujionesha, mwonekano wetu hauwezi kamwe kulinganishwa, kwa neema na uzuri, na ule urahisi wa maua ya kondeni. Hivyo akili zao zinaweza zielekezwe kutoka kwenye yale ya bandia na kwenda kwenye asili. Wanaweza kujifunza kwamba Mungu amewapa vitu hivi vyote vizuri ili kufurahia, na anachotaka kutoka kwao ni kumpa Yeye mapenzi bora na matakatifu ya moyo. {FEsw 159.3}

Wazazi wanapaswa kutafuta kuamsha kwa watoto wao shauku ya kujifunza fiziolojia. Vijana wanahitaji kufundishwa kuhusiana na miili yao wenyewe. Kuna wachache tu kati ya vijana ambao wana ujuzi wowote wa uhakika juu ya siri na mafumbo ya maisha. Ujifunzaji wa mfumo wa ajabu wa mwili wa binadamu, uhusiano na utegemezi wake wote wa sehemu zake tata, ni jambo moja ambalo akina mama wengi huchukulia uzito mdogo, na wanakuwa hawana matamania hayo. Hawaelewi ushawishi wa mwili juu ya akili, au wa akili juu ya mwili. Wanajishughulisha kwa vitu visivyo na maana, na kisha kudai kwamba hawana muda wa kupata ujuzi wanaohitaji ili kutunza ipasavyo afya ya watoto wao. Wanaona watapata usumbufu mdogo wakiwapeleka watoto kwa madaktari kuliko kujifunza kuhusu afya. Maelfu ya watoto hufa kwa kutojua sheria za uzima wao. {FEsw 159.4}

Iwapo wazazi wenyewe wangepata maarifa juu ya mada hii na kuhisi umuhimu wa kuyaweka katika matumizi ya vitendo, tungepaswa kuona hali bora ya mambo. Wafundishe watoto wako kufikiri juu ya sababu na athari. Waonyeshe kwamba ikiwa watakiuka sheria za uzima wa miili yao, ni lazima walipie faini au adhabu kwa kupata mateso. Kama huoni mabadiliko ya haraka kama unavyotaka, usikate tamaa, bali fundisha kwa subira, na endelea hadi ushindi upatikane. Endelea kuwafundisha kuhusu miili yao wenyewe, na jinsi ya kuitunza miili yao. Uzembe au kutojali kuhusiana na afya ya mwili huelekea kwenye njia ya kutojali maadili. {FEsw 160.1}

Usipuuzie kuwafundisha watoto wako jinsi ya kutayarisha chakula cha afya. Katika kuwapa masomo haya ya fiziolojia na upishi mzuri, unawapa hatua za kwanza katika baadhi ya mambo muhimu zaidi ya matawi ya elimu, na kufundisha kanuni ambazo ni vipengele vinavyohitajika na vyenye maana katika elimu ya dini. {FEsw 160.2}

Masomo yote ambayo nimeyazungumza katika makala hii yanahitajika. Yakizingatiwa ipasavyo, yatakuwa kama ngome itakayowahifadhi watoto wetu kutokana na maovu ambayo yanafurika duniani. Tunahitaji kujitawala nafsi na kiasi kwenye meza zetu. Tunahitaji nyumba ambazo mwanga wa jua tuliopewa na Mungu na hewa safi ya Mbinguni vinakaribishwa. Tunahitaji mvuto wenye uchangamfu na furaha katika nyumba zetu. Ni lazima tusitawishe mazoea yenye

manufaa kwa watoto wetu, na lazima tuwaelekeze katika mambo ya Mungu. Inagharimu kitu kufanya haya yote. Inagharimu maombi na machozi, na subira inayoandamana na maagizo yanayorudiwa mara kwa mara. Wakati mwingine akili zetu zinachanganyikiwa na kufikia kikomo katika kujua nini cha kufanya; lakini tunaweza kuwapeleka watoto kwa Mungu katika maombi yetu, tukiomba waepushwe na uovu, tukisihi, “Sasa, Bwana, fanya Kazi yako; ilainishe na kuitiisha mioyo ya watoto wetu,” na Yeye atatusikia. Mungu husikiliza maombi ya wanaolia, akina mama waliochoka na wenye huzuni. Kristo alipokuwa duniani, akina mama wenye mizigo walileta watoto wao Kwake; walifikiri kwamba kama angeweka mikono Yake juu yao, wangukuwa na ujasiri bora zaidi wa kuwalea katika njia iwapasayo. Mwokozi alijua kwa nini akina mama hawa walimjia pamoja na watoto wao, na akawakemea wanafunzi, ambao walitaka kuwazuia, akisema, “Waacheni watoto wadogo waje Kwangu; wala msiwazuie; kwa maana ufalme wa Mungu ni wao.” Yesu anawapenda wale walio wadogo, Naye anatazama kuona jinsi wazazi wanavyofanya kazi yao. {FEsw 160.3}

Uovu unazidi kila upande, na ikiwa watoto wataokolewa, ni lazima bidii ya kudumu ifanyike. Kristo alisema, “Mimi najiweka wakfu, ili na hao watakaswe.” Alitaka wanafunzi Wake kutakaswa, Naye akajiweka Mwenyewe kama kielelezo cha utakaso, ili waweze kumfuata. Itakuwaje basi kama baba na mama watauchukua msimamo huu huu, wakisema, “Nataka watoto wangu wawe na kanuni thabiti, nami nitawapa mfano wa hili katika maisha yangu”? Hebu mama asifikiri kuna kafara au kujitoa mhanga kukubwa sana, kama akijitoa kwa ajili ya wokovu wa familia yake. Kumbuka, Yesu alitoa maisha Yake kwa kusudi la kukuokoa wewe na watu wako dhidi ya uharibifu. Utakuwa na msaada na huruma yake katika kazi hii iliyobarikiwa, na atakuwa mtenda kazi pamoja na Mungu. {FEsw 161.1}

Katika jambo lingine lolote tunaloweza kushindwa, tusishindwe basi katika malezi, hebu na tuwe wakamilifu katika kazi kwa ajili ya watoto wetu. Ikiwa watatoka kwenye mafunzo ya nyumbani, wasafi na wema, ikiwa wanajaza nafasi ndogo na ya chini kabisa katika mpango mkuu wa Mungu wa mema kwa ulimwengu, kazi yetu ya maisha haiwezi kamwe kuitwa iliyoshindwa/iliyoFEswli. {FEsw 161.2} - *Christian Temperance and Bible Hygiene* 60-72, 1890.

WALEVI WA AKILI

Je! watoto wetu watasoma/wasome nini? ni swali zito, na linadai jibu zito. Ninatatizika kuona, katika familia za Kikristo, majarida na magazeti yenye hadithi zinazoendelezwa ambazo haziachi msisitizo wa mema au wema katika akili. Nimewatazama wale ambao hamu yao kwa ajili tamthiliya imekuzwa. Wamepata fursa ya kusikiliza zile Kweli za Neno la Mungu, na nguzo na sababu ya imani yetu; lakini wamekua na kupevuka katika umri na mapungufu ya ucha Mungu wa kweli. Vijana hawa wapendwa wanahitaji sana kuweka katika ujenzi wa tabia zao malighafi/nyenzo bora zaidi-- upendo na hofu ya Mungu na maarifa ya Kristo. Lakini wengi hawana akili ya kuuelewa ule Ukweli kama ulivyo ndani ya Yesu. Akili zimefanyiwa karamu ya kulishwa hadithi za kuisimua. Wanaishi katika ulimwengu usio halisi, na hawafai kwa majukumu ya utendaji ya maisha haya. Nimeona watoto wanaruhusiwa kukua kwa njia hii. Iwe nyumbani au nje ya nchi, wanakosa utulivu au wana ndoto, na hawawezi kuzungumzia hata masomo au mada za kawaida zinapoletwa kwenye mjadala, hujihusisha na mambo ya kawaida. Akili bora zaidi, zilizobadilishwa kwa mambo ya juu zaidi, zimeshushwa hadhi hadi kutafakari mambo madogo au mabaya zaidi kuliko mambo madogo-madogo, mpaka wale wanaozimiliki wameridhika na mada kama hizi, na ni shida sana kwao kuwa na uwezo wa kufikia chochote cha juu zaidi. Mawazo ya kidini na mazungumzo yamekuwa ya kuchukiza au yenye ladha mbaya. Chakula cha akili ambacho kinafurahiwa, kinachafua au kina maambukizo kwa athari zake, na husababisha mawazo machafu na yenye tamaa mbaya za mwili. Nimejisikia huruma ya dhati kwa Roho hizi kwani nimezingatia jinsi gani hupoteza kwa kupuuza fursa za kupata ujuzi wa Kristo, ambaye katika Yeye tumaini letu la uzima wa milele ndiyo Kiini chake (limekita Kwake). Ni muda wa thamani kiasi gani unapotea, ambao wangeweza kuwa wanajifunza Kielelezo cha wema wa Kweli. {FEsw 162.1}

Binafsi nimefahamiana na baadhi ya waliopoteza afya yao ya akili kutokana na mazoea mabaya ya kusoma. Wanapitia maisha yenye fikra gonjwa, yakikuza kila malalamiko madogo. Mambo ambayo mtu mwenye akili timamu, mwenye busara hangeweza kuyaona, huwa majaribu kwao yasiyostahimilika, na vikwazo visivyoweza kushindwa(hufeli na hivyo vikwazo). Kwao, maisha ni kivuli cha kudumu. {FEsw 163.1}

Wale ambao wamejiingiza katika tabia ya kukimbilia katika njia ya hadithi za kuisimua, wanalemaza nguvu zao za kiakili, na kuwafanya wao wenyewe kutofaa kuwa na mawazo bora yenye nguvu na utafiti wenye nguvu. Kuna wanaume na wanawake sasa walio katika kuzorota kwa maisha ambao hawajawahi kupona kutokana na madhara ya kusoma bila kutawala nafsi (wanasoma kila kitu bila

kujitawala, na vingine ni uozo au sumu). Tabia, iliyoundwa katika umri wa mapema, imeongezeka pamoja na ukuaji wao na kuimarishwa pamoja na nguvu zao; na juhudi zao za kuishinda, ingawa wamedhamiria kuacha, juhudi zao zimekuwa na mafanikio kidogo. Wengi hawajawahi kurejesha nguvu zao za awali za akili. Majaribio yote ya kuwa Wakristo wa vitendo huishia kwenye matamania bila utendaji. Hawawezi kuwa kama Kristo hakika, na huendelea kulisha akili katika aina hii ya fasihi. Wala hakuna athari ya kimwili ambayo si mbaya sana. Mfumo wa neva hulemewa bila sababu na shauku hii ya kusoma. Katika baadhi ya hali, vijana, na hata wale waliokomaa, wamepatwa na matatizo na kupooza si kutokana na sababu nyingine bali katika kusoma kupita kiasi. Akili iliwekwa chini ya msisimko wa kudumu, mpaka mashine maridadi ya ubongo ikadhoofika kiasi kwamba haikuweza kutenda, na kupooza yakawa ndiyo matokeo yake. {FEsw 163.1}

Wakati hamu ya hadithi za kuisimua, na kushtua hisia zinapokuzwa, nguvu ya maadili inapotoshwa, na akili haitosheki isipokuwa inalishwa mara kwa mara na chakula hiki kichafu ambacho ni kama takataka isiyofaa. Nimeona wasichana, waliojiita wafuasi wa Kristo, ambao kwa kweli hawakuwa na furaha isipokuwa kama wamekuwa na riwaya mpya au gazeti la hadithi mkononi. Akili ilikuwa na hamu kali ya kuisimuliwa kama mlevi anavyotamani kileo. Hawa vijana hawakuonesha Roho ya kujitoa wakfu au ibada; hawakuwa na Nuru ya Mbinguni iliyotolewa kwa marafiki zao, ili kuwaongoza kwenye chemchemi ya elimu. Hawana uzoefu wa kina, wa kidini au mambo ya kiroho. Kama aina hii ya usomaji isingekuwa mbele yao kila mara, kungeweza kuwa na tumaini fulani la matengenezo kwao; lakini waliutamani usomaji huo na kuupata. {FEsw 163.2}

Ninaumia kuona vijana wa kiume na wa kike wakiharibu manufaa yao katika maisha haya, na kushindwa kupata uzoefu ambao utaweza kuwatayarisha kwa ajili ya uzima wa milele katika jamii ya Mbinguni. Tunaweza tusipate jina linalofaa zaidi kwao kuliko "walevi wa kiakili." au "watu ambao akili zao zimesumishwa" {FEsw 164.1}

Tabia zisizo na kutawala nafsi (kiasi) za kusoma huwa na ushawishi mbaya wa ubongo kwa hakika kama vile ilivyo kutokuwa na kiasi katika kula na kunywa. {FEsw 164.2}

Njia bora ya kuzuia ukuaji wa uovu ni kuushughulisha tena huo udongo wa akili (akili yabidi ipaliliwe au kushughulikiwa vyema tena). Uangalifu mkubwa na wa kudumu unahitajika katika kukuza akili na kupanda humo mbegu zenye thamani za ile Kweli ya Biblia. Bwana, kwa rehema Zake kuu, ametufunulia katika Maandiko Matakatiifu kanuni za maisha matakatiifu. Hutuambia dhambi za kuepuka; Hutuelezea mpango wa wokovu, na kutuonyesha njia ya kwenda Mbinguni. Amewavuvia watu watakatiifu kuandika, kwa faida yetu, maagizo kuhusu hatari

zinazoizinga njia, na jinsi ya kuziepuka. Wale ambao hutii agizo Lake la kuyachunguza Maandiko hawatakuwa wajinga kwa mambo haya. Katikati ya hatari za siku za mwisho, kila mshiriki wa Kanisa anapaswa kuelewa sababu za tumaini na imani yake, — sababu ambazo si ngumu kuzielewa. Yapo mambo tosha ya kuijaza akili, ikiwa tunataka kukua katika neema na katika ujuzi ya Bwana wetu Yesu Kristo. {FEsw 164.3}

Sisi ni tuna mwisho/kikomo, lakini tunapaswa kuwa na ufahamu wa asiye na mwisho. Akili lazima iletwe katika mazoezi ya kumtafakari Mungu, na mpango Wake wa ajabu kwa wokovu wetu. Hivyo nafsi itainuliwa juu ya dunia na mahali pa kawaida, na kudumishwa juu ya kile ambacho ni cha Utukufu na cha milele. Wazo kwamba tuko katika ulimwengu wa Mungu, katika uwepo wa Muumba mkuu wa ulimwengu wote, aliyemfanya mwanadamu kwa mfano Wake Mwenyewe, litaongoza akili katika nyanja pana, zilizotukuka kwa kutafakari. Wazo kwamba jicho la Mungu linatuangalia, kwamba anatupenda, na alitujali sana hata akamtoa Mwanawe mpendwa kwa ajili ya kutukombo, ili tusiangamie kwa jinsi ya kutisha, ni kuu mno; na yule anayefungua moyo wake kwa kukubali na kutafakari mada kama hii, kamwe hatatosheka na mambo madogo, ya yenye masomo kuisisimua. {FEsw 164.4}

Ikiwa Biblia ingesomwa jinsi inavyopaswa kuwa, wanadamu wangekuwa na nguvu katika akili. Mada bora zinazoshughulikiwa katika Neno la Mungu, usahili wa Utukufu wa matamshi yake, mada adhimu ambazo huwasilishwa akilini, hukuza uwezo ndani ya mwanadamu ambao vinginevyo hauwezi kukuzwa. Katika Biblia, uwanja usio na mipaka umefunuliwa kwa ajili ya akili/fikra za mwanadamu. Mwanafunzi atatoka katika tafakuri ya mada zake kuu, kutokana na kuhusishwa na taswira zake za juu, zikiwa na usafi wa moyo zaidi na kuinuliwa katika mawazo na hisia kuliko kama angetumia muda huo katika kusoma kazi yoyote ya asili ya kibinadamu tu, bila kusema chochote juu ya hizo tabia za kijinga-jinga. Akili za vijana hushindwa kufikia ubora wa maendeleo yake wanapopuuza chanzo cha juu kabisa cha hekima yao, —Neno la Mungu. Sababu za kwa nini tuna watu wachache wenye akili nzuri, yenye utulivu, uthabiti na thamani, ni kwa kuwa hakuna kumcha Mungu, kumpenda Mungu, na kanuni za dini hazitekelezwi katika maisha kama inavyopaswa kuwa. {FEsw 165.1}

Mungu angetaka tujinufaishe wenyewe kwa kila njia ya kukuza na kuimarisha uwezo wetu wa kiakili. Tuliumbwa kwa ajili ya maisha ya hali ya juu zaidi kuliko maisha ya sasa. Wakati huu ni ule wa matayarisho ya maisha yajayo, ya umilele. Kunaweza kupatikana wapi mada kuu za kutafakari, mada ya kuvutia zaidi kuliko kweli tukufu zinazofunuliwa katika Biblia? Kweli hizi zitafanya kazi kubwa kwa mwanadamu, ikiwa atafuata tu yale zinayoyafundisha. Lakini ni kwa jinsi gani Biblia husomwa kidogo! Kila kitu kisicho na umuhimu hutundikwa hapo badala ya mada zake. Ikiwa Biblia ingesomwa zaidi, ikiwa Kweli zake zingeeleweka vyema,

tungepata Nuru zaidi na kuwa watu wenye akili. Malaika kutoka ulimwengu wa Nuru husimama kando ya upande wa mtafutaji wa ile Kweli mwenye bidii, ili kuivuta na kuimulika akili yake. Aliye gizani katika juu ya ufahamu anaweza kupata Nuru kupitia kwa kuyatambua Maandiko. — *Christian Temperance and Bible Hygeine, 123-26 {1890}. {FEsw 165.2}*

Kwa Marejeleo ya Ziada

The Literal Week, Patriarchs and Prophets, 111-116

The Schools of the Prophets, Patriarchs and Prophets, 592-602

Teach by Precept and Example, The Review and Herald, March 31, 1891

The Mother's Work, The Review and Herald, September 15, 1891

A Knowledge of God, Steps to Christ, 89-96

VITABU KATIKA SHULE ZETU

Katika kazi ya kuelimisha vijana katika shule zetu, itakuwa jambo gumu kuhifadhi ushawishi wa Roho Mtakatifu wa Mungu na katika wakati huo huo tukishikilia kanuni potofu yaani zenye makosa. Nuru inayomulika juu ya walio na macho ya kuona, haiwawezi kuchanganywa na giza la uzushi na makosa linayopatikana katika vitabu vingi vya kiada vilivyopendekezwa kwa wanafunzi katika vyuo vyetu. Walimu na wanafunzi wamefikiria kwamba ili kupata elimu, ilikuwa ni lazima kusoma machapisho ya waandishi wanaofundisha ukafiri, kwa sababu ya kazi zao zenye baadhi ya vito angavu ya mawazo. Lakini ni nani alikuwa mwanzilishi wa vito hivi vya mawazo? —Ilikuwa ni Mungu na Mungu pekee; kwani Yeye ndiye chanzo cha Nuru yote. Je, vitu vyote hivi vya muhimu kwa afya na ukuaji wa asili ya kiroho na kimaadili havipatikani katika kurasa za Maandiko Mtakatifu? Je! Kristo si kiongozi wetu aliye hai? Na si sisi je, hatukui ndani Yeye hadi kufukia kimo kamili cha wanaume na wanawake? Je, chemchemi chafu inaweza kutoa maji matamu? Kwa nini tutangetange kuzama katika mrundikano wa makosa yaliyomo katika kazi za wapagani na makafiri, kwa ajili ya kupata faida chache za kweli chache tu za kiakili, wakati ule Ukweli wote uko upande wetu? {FEsw 167.2}

Mwanadamu hawezi kutimiza lolote jema bila Mungu. Yeye Ndiye chanzo cha kila mionzi ya Nuru inayopenya katika giza la ulimwengu. Kila chenye thamani kinatoka kwa Mungu, na ni Chake. Kuna sababu kwamba mawakala wa adui wakati mwingine huonyesha hekima ya ajabu. Shetani mwenyewe alielimishwa na kuadibishwa katika nyua za Mbinguni, na anao ujuzi wa mema na mabaya vilevile. Huchanganya vitu vya thamani pamoja na vitu vibaya, na hii ndiyo humpa uwezo kuwadanganya wana wa watu. Lakini kwa sababu Shetani ameiba jezi/sare ya Mbinguni ili apate kuwashawishi na ile mamlaka aliyoinyakua, je, wale ambao wamekaa gizani na kuiona Nuru kuu, watageuka kutoka kwenye Nuru ili kuiendea giza? Je, wale waliozijua hazina za Maneno ya Mungu, watapendekeza kwa wanafunzi wetu kusoma vitabu vinavyoeleza hisia za kipagani au za kikafiri, ili waweze kuwa na akili? Shetani ana mawakala wake, walioelimika katika mbinu zake, wakiongozwa na Roho yake, na wakichukuliwa kwa kazi yake; lakini je, tutashirikiana nao? Je, sisi kama Wakristo, tunapendekeza kazi za mawakala wake kama zenye thamani, hata kufaa katika kupata elimu? {FEsw 167.2}

Bwana Mwenyewe amekusudia kwamba shule zianzishwe miongoni mwetu ili elimu ya Kweli ipatikane. Hakuna mwalimu katika shule zetu anayepaswa kupendekeza wazo kwamba, ili kuwa na nidhamu sahihi ya fani fulani, eti ni muhimu kujifunza vitabu vinavyoeleza upagani na hisia za kikafiri. Wanafunzi ambao wameelimishwa hivyo, hawana uwezo wa kuwa waelimishaji katika zamu

yao; maana wamejaa hila za udanganyifu wa adui. Kujifunza kazi ambazo kwa njia yoyote hueleza hisia za kikafiri ni kama kushika makaa meusi; kwa sababu mtu hawezi kukosa kunajisika akilini anapofikiri katika mwelekeo wa mashaka (skepticism). Je, katika kuviendea vyanzo hivyo ili kupata elimu, hatugeuki mbali kutoka katika theluji ya Lebanoni ili kunywa maji machafu ya bondeni? {FEsw 168.1}

Watu wanaokengeuka kutoka katika elimu ya Mungu, wameweka akili zao chini ya udhibiti wa bwana wao, Shetani, naye huwazoeza kuwa watumishi wake. Kadiri machapisho yanaonyesha maoni ya kikafiri unavyopungua kuletwa mbele ya vijana, ni bora zaidi. Malaika waovu huwa macho kila wakati ili wapate kuinua mbele ya nia za vijana yale yatakayowadhuru, na ikiwa vitabu vinavyoeleza hisia za kikafiri na za kipagani vinasomwa, hawa mawakala wa uovu wasioonekana hutafuta kuwajaza wale wanaosoma kuwa na Roho ya kuuliza kwa mashakamashaka na kutoamini. Wale wanaokunywa kutoka katika mifereji hii iliyochafuliwa hawana kiu ya maji ya uzima; kwani wameridhika na mabirika ya kidunia yaliyopasuka (viriba vilivyopasukapasuka). Wao wanafikiri wanazo hazina za elimu, wanapokuwa wanajirundikia tele hazina hizo kwa pupa, na kumbe ni kuni, nyasi na mabua, tu ambayo hayana faida masikini, hayastahili kabisa kuhifadhiwa kwenye ghala zao. Thamani ya utu wao, wazo lao kwamba maarifa ya juujuu ya mambo ni elimu, huwafanya wajigambe na kuridhika, wakati wao ni, kama walivyokuwa Mafarisayo, wasiojua Maandiko na nguvu za Mungu. {FEsw 168.2}

Laiti vijana wetu wangejiwekea hazina ya maarifa yasiyoweza kuharibika, ili waweze kubeba pamoja nao katika siku zijazo, maisha ya umilele, maarifa ambayo yanawakilishwa kama dhahabu na fedha na mawe ya thamani! Kundi la walimu na wanafunzi wanaojiona wenye hekima, hawajui lolote kama inavyowapasa kujua. Wanahitaji kujifunza upole na unyenyekevu katika shule ya Kristo, ili wapate kuthamini sana kile ambacho Mbingu inakiona kuwa bora. Wale wanaopokea elimu yenye thamani, ambayo itakuwa ya kudumu kama umilele, hawangatiwi wala kuchukuliwa kama watu bora zaidi wenye elimu duniani. Lakini Maandiko hudai kuwa “kumcha Bwana ndiyo chanzo cha hekima.” Aina hii ya maarifa iko chini ya kiwango katika makadirio ya ulimwengu, na hata hivyo ni muhimu kwa kila kijana kuwa na hekima katika Maandiko, ikiwa atakuwa na uzima wa milele. Mtume anasema, “Kila Andiko lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa ili apate kutenda kila tendo jema.” Hili ni pana vya kutosha. Wote na watafute kufahamu, kwa kadiri ya ukamilifu wa nguvu zao, maana ya Neno la Mungu. Usomaji wa juujuu tu ya Neno lililovuviwa utakuwa na faida kidogo; kwani kila Andiko lililoko katika kurasa takatifu linahitaji kutafakariwa kwa uangalifu. Ni kweli kwamba baadhi ya aya hazihitaji umakini wa dhati kama zilivyo zingine; kwa kuwa maana zake zi dhahiri zaidi. Lakini mwanafunzi wa Neno la Mungu anapaswa kutafuta kuelewa maana ya aya moja hadi nyingine mpaka mtiririko wa ile Kweli utakapofunuliwa kwenye akili yake.

Kama hazina za madini ya thamani zilivyofichwa chini ya uso wa dunia; ndivyo utajiri wa kiroho ulivyofichwa katika aya za Maandiko Matakاتفu, nayo inahitajika juhudi za kiakili na umakini wa maombi ili kugundua maana iliyojificha ya Neno la Mungu. Hebu kila mwanafunzi anayethamini hazina ya Mbinguni atumie nguvu zake za akili na kiroho, na kuzama ndani ya mgodi wa ile Kweli, ili apate dhahabu ya Mbinguni,— Busara ile itakayomfanya awe na hekima hadi kuokolewa. {FEsw 169.1}

Ikiwa nusu ya juhudi inayooneshwa katika kutafuta kufahamu mawazo angavu ya makafiri, ingeoneshwa katika kusoma mpango wa wokovu, maelfu ambao sasa wako gizani, wangependezwa na hekima, usafi, na majaliwa ya Mungu yaliyotukuka kwa niaba yetu; wangeinuliwa mbali na ubinafsi wao wenyewe na hata kufikia maajabu ya upendo na unyenyekevu wa kujishusha kwa Mungu na hata kumtoa Mwanawe wa pekee kwa ajili ya jamii iliyoanguka. Inakuwaje wengi wanatosheka kunywa kwenye vijito vichafu na vinavyotiririka kwenye bonde la matopetope, wakati wangeweza kuburudisha Roho zao kwenye vijito hai vya milimani? Nabii anauliza, “Je, mtu ataacha theluji ya Lebanoni katika jabali la kondeni? Au je! Maji ya baridi yashukayo toka mbali yatakauka?” Mungu anajibu, “Watu wangu wamenisahau Mimi, nao wamefukizia ubatili uvumba, na wamewakaza katika njia zao kutoka njia za kale, katika mapito ya zamani ili wapite katika njia za kando, katika njia isiyotengenezwa.” {FEsw 170.1}

Ni jambo la kusikitisha kwamba watu ambao wamekabidhiwa uwezo mzuri wa kutumika katika utumishi wa Mungu, wamefanyia ukahaba nguvu zao katika utumishi wa uovu, na kuweka talanta zao miguuni pa adui. Wamejiweka katika utumwa wa kutisha zaidi kwa mkuu wa uovu, huku wakiikataa huduma ya Kristo kama inayofedhehesha na isiyopendeza. Waliitazama kazi ya mfuasi wa Kristo kama kazi iliyo chini ya matamano yao ya ukuu, iliyohitaji kushuka chini kutoka katika ukuu wao, aina ya utumwa, ambao ungeshusha nguvu zao, na kupunguza mduara wa ushawishi wao. Yule ambaye alifanya dhabihu isiyo na kikomo ili waweze kuwekwa huru kutoka katika utumwa wa uovu, aliwekwa kando kuwa asiyefaa kwa juhudi zao bora na huduma zilizotukuka zaidi. {FEsw 170.2}

Watu hawa wamepokea talanta zao kutoka kwa Mungu, na kila kito cha mawazo ambacho walikuwa wamehesabiwa kuwa wanastahili kuzingatiwa kama wasomi na wanafikra, si uwezo wao, bali ni wa Mungu Mwenye hekima yote, ambaye hawakumkiri. Kupitia mila, mapokeo, na kupitia elimu ya uwongo, watu hawa wanainuliwa kama waelimishaji wa ulimwengu; lakini katika kuwaendea wanafunzi wako katika hatari ya kuukubali maovu; kwa maana ushirikina, mawazo potofu, na makosa yamechanganywa na sehemu za falsafa na mafundisho ya Kweli. Mchanganyiko au mkorogo huu hutengeneza dawa ambayo ni sumu kwa Roho, yenye uharibifu wa Imani katika Mungu wa Kweli yote. Wale ambao wana kiu ya maarifa wasiende kwenye chemchemi hizi zilizochafuliwa; kwa maana wamealikwa kuja kwenye chemchemi ya uzima na kunywa bure. Kupitia kutafuta Neno la Mungu,

wanaweza kupata hazina iliyofichwa ya Ukweli ambayo imezikwa kwa muda mrefu chini ya takataka za makosa, mapokeo ya wanadamu, na maoni ya watu. {FEsw 170.3}

Biblia ni mwelimishaji/mwalimu mkuu; maana haiwezekani kwa maombi kusoma kurasa zake takatifu bila kuwa na nidhamu ya akili, iliyokuzwa, iliyosafishwa, na kutakaswa. "Bwana asema hivi, mwenye hekima asijisifu kwa sababu ya hekima yake, wala mwenye nguvu asijisifu kwa nguvu wake, wala tajiri asijisifu kwa sababu ya utajiri wake, bali na ajisifuye na ajisifu kwa sababu hii, ya kwamba ananifahamu Mimi na kunijua; ya kuwa Mimi ni BWANA, nitendaye wema, na hukumu, na haki katika nchi; maana Mimi napendezwa na mambo hayo, asema BWANA. Tazama, siku zinakuja, asema BWANA, nitakapowaadhibu wote waliotahiriwa katika hali yao ya kutotahiriwa." {FEsw 171.1}

Wale wanaodai kuwa Wakristo, wanaodai kuuamini Ukweli, na bado hunywa kwenye chemchemi zilizochafuliwa za ukafiri, na kwa kanuni na mfano huwavuta wengine mbali na, maji ya baridi ya theluji ya Lebanoni, ni wapumbavu, ingawa wanajidai kuwa wenye hekima. "Enyi nyumba ya Israeli lisikieni nNeno awaambialo BWANA. BWANA asema hivi, Msijifunze njia ya mataifa, wala msishangae kwa sababu ya ishara za Mbinguni; maana mataifa hushangaa kwa sababu ya ishara hizo.... Bali BWANA Ndiye Mungu wa Kweli, Ndiye Mungu aliye hai, Mfalme wa milele; mbele za ghadhabu Yake nchi yatetemeka, wala mataifa hawawezi kustahimili hasira Yake. Mtawaambia hivi, Miungu hiyo isiyofanya mbingu na nchi; hiyo itaangamia katika nchi, nayo itatoweka chini ya mbingu. Ameiumba dunia kwa uweza wake, Ameuthibitisha ulimwengu kwa hekima Yake, na kwa ufahamu Wake amezitandika mbingu. Atoapo sauti Yake, pana mshindo wa maji Mbinguni, Naye hupandisha mvuke/mawingu toka ncha za nchi; Hufanyia mvua umeme, huutoa upepo katika hazina zake. Kila mtu amekuwa mjinga katika ujuzi wake: kila mfua dhahabu amefedheheshwa na sanamu yake ya kuchonga: maana sanamu yake ya kuyeyuka ni uongo, wala hamna pumzi ndani yake. Ni ubatili tu, na kazi za udanganyifu; wakati wa kujiliwa kwao watapotea. Yeye, fungu la Yakobo siye kama hawa, maana Ndiye aliyeviumba vitu vyote; na Israeli ni kabila ya urithi Wake: BWANA wa majeshi ndilo Jina Lake." {FEsw 171.2}

"BWANA asema hivi; Amelaaniwa mtu yule amtegemeaye mwanadamu, amfanyaye mwanadamu kuwa kinga yake, na moyoni mwake amemwacha Bwana. Maana atakuwa kama fukra nyikani, hataona yatakapotokea mema; bali atakaa jangwani palipo ukame; katika nchi ya chumvi isiyokaliwa na watu. Amebarikiwa mtu yule anayemtegemea BWANA, ambaye Bwana ni tumaini lake. Maana atakuwa kama mti uliopandwa kando ya maji, uenezao mizizi yake karibu na mto; hautaona hofu wakati wa hari ujapo, bali jani lake litakuwa bichi; wala hautahangaika mwaka wa uchache wa mvua, wala hautaacha kuzaa matunda.... Ee Bwana, Tumaini la Israeli, wote wakuachao watatahayarika. Wao watakaojitenga nami wataandikwa

katika mchanga, kwa sababu wamemwacha Bwana, kisima cha maji yaliyo hai. Uniponye, Ee Bwana, nami nitaponyeka; uniokoe, nami nitaokoka; kwa maana Wewe Ndiwe uliye sifa zangu.” {FEsw 172.1}

Hebu waumini wa ile Kweli kwa wakati huu, wajiepushe na waandishi wanaofundisha ukafiri. Usiruhusu kazi za wakosoaji zionekane katika sheflu za maktaba yako, ambapo watoto wako wanaweza kuzifikia. Hebu wale walioonja Neno jema la Mungu, na nguvu za ulimwengu ujao, wasione tena kuwa ni sifa muhimu ya elimu njema kuwa na ujuzi wa maandiko ya wale wanaokanusha uwepo wa Mungu, na kuwa na dharau juu ya Neno Lake takatifu. Usitoe nafasi kwa mawakala wa Shetani, kwa kuwa hakuna kitu cha kufanya kuthibitisha matendo yao; kitu kilicho safi hakiwezi kutoka katika kitu kichafu. {FEsw 172.2} -*Review and Herald, November 10, 1891.*

Sura ya 22

MWALIMU WA UKWELI NDIYE MWELIMISHAJI PEKEE ALIYE SALAMA

Kuna makundi mawili ya waelimishaji au walimu duniani. Kundi moja ni wale ambao Mungu huwafanya mikondo ya Nuru, na kundi lingine ni wale ambao Shetani anawatumia kama mawakala wake, ambao ni wenye hekima katika kutenda maovu. Kundi moja hutafakari tabia ya Mungu, na kuongezeka katika kumjua Yesu, ambaye Mungu alimtuma ulimwenguni. Hili kundi linakuwa limejitoa kabisa kwa yale mambo yaletayo Nuru ya Mbinguni, hekima ya Mbinguni, kwa ajili ya kuiinua nafsi. Kila uwezo wao wa asili huletwa chini ya Mungu, na mawazo yao huwa chini ya utumwa kwa Kristo. Kundi lingine liko kwenye muunganiko na mkuu wa giza, ambaye yuko macho sikuzote ili apate nafasi ya kuwafundisha wengine maarifa ya uovu. Ikiwa nafasi itatolewa kwa ajili yake, hatakawia kuzisukuma njia zake katika moyo na akili. {FEsw 174.1}

Kuna haja kubwa ya kuinua kiwango cha haki katika shule zetu, kutoa mafundisho kulingana na utaratibu wa Mungu. Kristo angeingia katika taasisi zetu za elimu ya vijana, angewasafisha kama alivyolisafisha hekalu, akiondoa vitu vingi vyenye ushawishi unaonajisi. Vitabu vingi ambavyo vijana husoma vingetupiliwa mbali, na badala yake, kwenye hiyo sehemu vingejazwa vingine ambavyo vingeweza kuwaingizia maarifa makubwa, na kujaza hisia ambazo zinaweza kuwa hazina moyoni, katika kanuni ambazo zingeweza kutawala mwenendo. Je! ni kusudi la Bwana kwamba kanuni za uongo, hoja za uongo, na hila za Shetani ziwekwe mbele ya akili za vijana na watoto wetu? Je, mivuto ya kipagani na kikafiri iwasilishwe kwa wanafunzi wetu kama nyongeza muhimu kwenye hazina yao ya maarifa? Kazi za mtu mwenye akili zenye mashaka sana ni kazi za akili iliyolevywa kwa utumishi wa adui, na, je, wale ambao wanadai kuwa wanamatengenezo, wanaotafuta kuwaongoza watoto na vijana katika Njia ya Kweli, katika njia iliyotupwa nje, watafikiri kuwa Mungu atapendezwa kwa wao kuwasilisha kwa vijana yale ambayo yatapotosha tabia yake, yakimweka katika Nuru ya uongo mbele za vijana? Je! mivuto ya wasioamini, maneno ya watu waliopotea, yatetwe kama yanastahili umakini wa mwanafunzi, kwa sababu ni machapisho ya watu ambao ulimwengu unawasifu kama walio na fikra bora? Je! watu wanaodai kumwamini Mungu, wakusanye kutoka kwa hawa waandishi wasiotakaswa, maneno na hisia zao, na kuziweka hazina kama vito vya thamani vya kuhifadhiwa katikati ya utajiri wa akili? — Hebu Mungu aepushe mbali. {FEsw 174.2}

Bwana amewajalia watu hawa ambao ulimwengu unawasifu, karama za kiakili zisizo na kifani; amewajalia akili kubwa; lakini hawakuzitumia kwa Utukufu wa

Mungu. Walijitenga Naye kama vile Shetani alivyojitenga; lakini huku wakijitenga kutoka Kwake, bado walihifadhi vito vingi vya thamani vya fikra ambazo alikuwa amewapa, na hivi wakaviweka katika mfumo wa makosa ili kutoa mng'aro kwa hisia zao za kibinadamu, kuyafanya maneno yaliyovuviwa na mkuu wa uovu kuvutia. Ni kweli kwamba katika maandishi ya wapagani na makafiri kunapatikana fikra za juu za kitabia, ambazo zina mvuto kwenye akili. Lakini kuna sababu ya hili. Je, Shetani hakuwa mbeba Nuru, mshiriki wa Utukufu wa Mungu Mbinguni, na alifuata baada ya Yesu katika nguvu na ukuu? Kwa Maneno ya msukumo, anafafanuliwa kuwa mmoja anayekitia muhuri kipimo "aliyejaa hekima, na ukamilifu, na uzuri." Nabii anasema, "Ulikuwa ndani ya Adeni, bustani ya Mungu; kila jiwe la thamani lilikuwa kifuniko chako.... Wewe ulikuwa kerubi mwenye kutiwa mafuta afunikaye; Nami nalikuweka hata ukawa juu ya mlima mtakatifu wa Mungu; umetembea huko na huko chini kati ya mawe ya moto. Ulikuwa mkamilifu katika njia zako tangu siku ile ulipoumbwa, hata uovu ulipoonekana ndani yake.... Moyo wako uliinuka kwa sababu ya uzuri wako, umeiharibu hekima yako kwa sababu ya mwangaza wako, nimekutupa chini, nimekulaza mbele ya wafalme, wapate kukutazama. Kwa wingi wa maovu yako, katika uovu wa uchuuzi wako, Umepatia unajisi patakatifu pako; basi nimetokeza moto kutoka ndani yako, nao umekuteketeza, Nami nimekufanya kuwa majivu juu ya nchi, machoni pa watu wote wakutazamao. Wote wakujuao kati ya kabila za watu watakustaajabia; umekuwa kitu cha kutisha, wala hutakuwapo tena hata milele." {FEsw 175.1}

Ukuu na nguvu ambazo Muumba alimjalia Lusifa ameupotosha; na bado, unapofaa kusudi lake, anaweza kuwapa watu hisia zinazopotosha na kuvutia kwa njia mbaya. Kila kitu katika asili hutoka kwa Mungu; lakini Shetani anaweza kuwavuvia mawakala wake fikra ambazo zinaonekana kuwa za juu na za heshima. Je, hakuja kwa Kristo na nukuu za Maandiko alipokusudia kumshinda na kumtupa kwa majaribu yake ya ajabu? Hivi ndivyo ambavyo huwajia mwanadamu, kama malaika wa Nuru akiyaficha majaribu yake, au akiyafanya ya kutatanisha, chini ya mwonekano wa wema, na kuwafanya watu wamwamini yeye kuwa rafiki kuliko adui wa binadamu. Ni kwa njia hii kwamba amedanganya na kuwapotosha jamii ya binadamu, -kuwadanganya kwa majaribu nyeti yenye hila zisizokuwa rahisi kutambulika, na kuwapotosha kwa madanganyo mabaya ambayo yanaonekana kuwavutia. {FEsw 176.1}

Shetani amemhusisha Mungu na maovu yote ambayo mtu huyarithi. Amemwakilisha Mungu kama **yule** anayefurahia mateso ya Viumbe wake, ambaye ni wa kulipiza kisasi na asiye na msimamo. Ni Shetani ambaye alianzisha fundisho la mateso ya milele kama adhabu kwa ajili ya dhambi, kwa sababu kwa njia hii angeweza kuwaongoza watu katika ukafiri na uasi, kuvuruga Roho, na kuangusha akili ya mwanadamu. {FEsw 176.2}

Mbingu, ilipoangalia chini, na kuona udanganyifu ambao kwao watu huongozwa,

alijua kwamba Mwalimu wa kimbingu lazima aje duniani. Wanadamu katika ujinga na giza la maadili lazima wawe na Nuru, Nuru ya kiroho; kwani ulimwengu haukumjua Mungu, na lazima afunuliwe katika fahamu wao. Kweli alitazama chini kutoka Mbinguni na hakuona mwonekano Wake sura yake; kwa maana mawingu mazito ya giza la maadili na utusitusi uliifunika ulimwengu, na Bwana Yesu pekee Ndiye aliyeweza kuyaondoa mawingu; Maana alikuwa Nuru ya ulimwengu. Kwa uwepo wake angeweza kuondoa kivuli cha utusitusi ambacho Shetani alikiweka kati ya mwanadamu na Mungu. Giza liliifunika dunia, na giza kuu likawafunika watu. Kupitia uwasilishaji mbaya wa adui, wengi walidanganywa sana hata wakamwabudu Mungu wa uwongo, aliyejivika vazi lenye sifa za tabia ya kishetani.

{FEsw 176.3}

Mwalimu kutoka Mbinguni, si mtu mdogo kuliko Mwana wa Mungu, alikuja duniani kuifunua tabia ya Baba kwa wanadamu, kwamba wapate kumwabudu katika Roho na Kweli. Kristo alifunua kwa wanadamu Ukweli kwamba kufuata kwa ushupavu zaidi sherehe na taratibu au mapokeo kusingewaokoa; kwa maana ufalme wa Mungu ulikuwa wa kiroho katika asili yake. Kristo alikuja ulimwenguni ili kuupanda Ukweli. Alishikilia funguo zote za hazina za hekima, na aliweza kufungua milango ya sayansi, na kufichua hazina za maarifa ambazo hazijagunduliwa, kama zilihitajika kwa ajili ya wokovu. Aliwasilisha kwa wanadamu kile ambacho kilikuwa kinyume kabisa cha alichowasilisha adui kuhusiana na tabia ya Mungu, na alikazia juu ya wanadamu upendo wa Baba, ambaye “aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.” Alisisitiza juu ya watu umuhimu wa sala, toba, maungamo, na kutupiliwa mbali kwa dhambi. Aliwafundisha uaminifu, uvumilivu, rehema, na huruma, akiwaamrisha kuwapenda sio wale tu wanaowapenda, bali na wale waliowachukia, ambao waliwatendea vibaya. Katika hili alikuwa akiwafunulia tabia ya Baba, ambaye ni mvumilivu, Mwenye rehema, na Mwenye neema, si mwepesi wa hasira, amejaa wema tele na kweli. Wale walioyakubali mafundisho Yake walikuwa chini ya ulinzi wa malaika waliopewa kazi ya kuwatia nguvu, kuwaangaza, ili ile ule ukweli uwafanye upya na kuitakasa Roho. **{FEsw 177.1}**

Kristo hutangaza utume aliokuwa nao kwa kuja kKake duniani. Yeye anasema katika sala Yake ya mwisho ya hadhara, “Baba Mwenye haki, ulimwengu haukukujua, lakini Mimi nalikujua, na hao wamejua kuwa Ndiwe uliyenituma. Nami niliwajulisha Jina Lako, tena nitawajulisha hilo; ili pendo lile ulilonipenda Mimi liwe ndani yao, Nami Niwe ndani yao.” Musa alipomwomba Bwana amwonyeshe Utukufu Wake, Bwana alisema, “Nitapitisha wema Wangu wote mbele yako.” “BWANA akapita mbele yake, akatangaza, BWANA, BWANA, Mungu mwingi wa huruma, Mwenye fadhili, si mwepesi wa hasira, mwingi wa rehema na Kweli, Mwenye kuwaonea huruma elfu elfu, Mwenye kusamehe maovu na makosa na dhambi, wala si Mwenye kumhesabia mtu mwovu kuwa hana hatia kamwe... Musa akafanya haraka, akainamisha kichwa chake hata nchi, akasujudu.” Tunapofahamu

tabia ya Mungu kama Musa, sisi pia tutaharakisha kusujudu kwa ibada na sifa. Yesu hakutafakari chochote kile, zaidi ya “Pendo lile ulilonipenda Mimi” linapaswa kuwa katika mioyo ya watoto Wake, ili waweza kuwapa wengine ujuzi wa Mungu. {FEsw 177.2}

Huu ni uhakikisho ulioje, kwamba upendo wa Mungu ukae ndani ya mioyo ya wote wanaomwamini! Tazama ni wokovu wa thamani jinsi gani uliotolewa; kwa maana aweza kuwaokoa kabisa wote wamjiao Mungu kwa njia ya Yeye. Kwa mshangao tunadai, Mambo haya yawezaje kuwa? Lakini Yesu hataridhika na chochote kidogo kuliko hiki. Wale ambao ni washiriki wa mateso yake hapa, kuFEswdheheshwa Kwake, wakivumilia kwa ajili ya jina lake, wanapaswa kuwa na upendo wa Mungu juu yao kama ulivyokuwa juu ya Mwana. Mtu anayejua, amesema, “Baba Mwenyewe awapenda ninyi.” Mwenye ujuzi wa uzoefu wa urefu, na upana, na kimo, na kina cha upendo huo, ametangaza kwetu Ukweli huu wa ajabu. Upendo huu ni wetu kwa njia ya imani katika Mwana wa Mungu, kwa hiyo muunganiko na Kristo unamaanisha kila kitu kwetu. Sisi tuwe umoja Naye kama vile Yeye alivyo umoja na Baba, na kisha tu wapendwao na Mungu asiye na mwisho kama viungo vya mwili wa Kristo, kama matawi ya Mzabibu ulio hai. Tunapaswa kushikamana na sehemu kuu ya shina, na kupokea lishe kutoka kwenye Mzabibu. Kristo Ndiye Mkuu aliyetukuzwa, na upendo wa kimbingu unaotiririka kutoka moyoni mwa Mungu, hukaa ndani Kristo, na huwasilishwa kwa wale ambao wameunganishwa Naye. Upendo huu wa kimbingu unaoingia ndani ya nafsi huichochea kwa shukrani, huiweka huru kutoka katika udhaifu wake wa kiroho, kutoka kwenye kiburi, ubatili, na ubinafsi, na kutoka kwa yote ambayo yangeharibu tabia ya Kikristo. {FEsw 178.1}

Tazameni, mtazameni Yesu na muishi! Hamwezi ila kupendezwa na mvuto usio na kifani wa Mwana wa Mungu. Kristo alikuwa Mungu aliyedhihirishwa katika mwili, ile siri iliyofichwa tangu milele, na katika kumkubali kwetu au kumkataa Mwokozi wa ulimwengu tunahusika katika faida za milele. {FEsw 179.1}

Ili kumwokoia mkosaji wa sheria ya Mungu, Kristo, Yule aliye sawa na Baba, alikuja kuiishi mbingu mbele za watu, ili wajifunze kujua ni nini maana ya kuwa na mbingu moyoni. Alionyesha kile mtu anachopaswa kuwa ili kustahili neema ya thamani ya maisha ambayo hupimwa kwa uzima wa Mungu. {FEsw 179.2}

Maisha ya Kristo yalikuwa maisha yenye ujumbe wa kimbingu wa upendo wa Mungu, na alitamani sana kuwapa wengine upendo huu kipimo cha kutosha. Huruma ikang'aa kutoka katika uso Wake, na mwenendo Wake ulikuwa na sifa ya neema, unyenyekevu, Ukweli, na upendo. Kila mshiriki wa kanisa lake linalopambana vita na Shetani, lazima adhihirishe sifa zile zile, ikiwa angejiunga na lile kanisa lililopata ushindi ambalo linaingia Mbinguni*. Upendo wa Kristo ni mpana sana, umejaa Utukufu kiasi kwamba kwa kulinganishwa nayo, kila kitu ambacho wanadamu hukithamini kuwa kikuu, hupungua na kuwa duni. Tunapopata

kuutazama, tunashangaa, Tazama jinsi kina cha utajiri wa upendo ambao Mungu aliutoa kwa wanadamu katika zawadi ya Mwanawe wa pekee! {FEsw 179.3}

Tunapotafuta lugha ifaayo ya kuelezea upendo wa Mungu, tunapata maneno dhaifu sana, dhaifu sana, mbali sana kwa mada, na tunaweka kalamu yetu chini na kusema, “Hapana, hauwezi kuelezeka.” Tunaweza tu kufanya kama yule mwanafunzi mpendwa, na kusema, “Tazameni, ni pendo la namna gani alilotupa Baba; ili tuitwe wana wa Mungu.” Katika kujaribu kueleza upendo huu, tunahisi kwamba sisi ni kama watoto wachanga tunaotamka maneno ya kwanza kwa kithembe. Kimya tunaweza kuabudu; maana ukimya katika jambo hili ndio ufasaha pekee. Upendo huu umepita lugha zote kuuelezea. Ni fumbo na siri ya Mungu katika mwili, Mungu katika Kristo, na Uungu katika ubinadamu. Kristo alishuka chini kwa unyenyekevu usio na kifani, kwamba katika kuinuliwa Kwake kitini pa enzi pa Mungu, ili pia awainue wale wanaomwamini, ili waketi pamoja Naye katika kiti chake cha enzi. Wote wanaomtazama Yesu kwa Imani kwamba majeraha na michubuko ambayo dhambi imetenda, itapona ndani yake, watafanywa kuwa wazima. {FEsw 179.4}

Wimbo wa ukombozi ni mada muhimu, na ni wale tu walio na nia ya kiroho wanaweza kutambua kina na umuhimu wake. Ni usalama wetu, maisha yetu, furaha yetu, kukaa katika kweli za mpango wa wokovu. Imani na maombi ni muhimu ili tupate kuona mambo ya kina ya Mungu. Akili zetu zimefungwa sana na mawazo finyu, kiasi kwamba tunapata ila maoni finyu ya uzoefu ambao ni fursa yetu kuwa nao. Ni kidogo jinsi gani tunaelewa kile kilichomaanishwa na ombi la mtume, anaposema, “awajalieni, kwa kadiri ya utajiri wa Utukufu wake, kufanywa imara kwa nguvu, kwa kazi ya Roho Wake katika utu wa ndani; Kristo akae mioyoni mwenu kwa imani mkiwa na shina na msingi katika upendo; ili mpate kufahamu pamoja na watakatifu wote jinsi ulivyo upana, na urefu, na kimo, na kina; na kuujua upendo wa Kristo, upitao ufahamu ulivyo mwingi, mpate kutimilika kwa ukamilifu wote wa Mungu. Basi atukuzwe Yeye awezaye kufanya mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyaombayo au tuyawazayo, kwa kadiri ya nguvu itendayo kazi ndani yetu; naam, atukuzwe katika kanisa na katika Kristo Yesu hata vizazi vyote vyamilele na milele. Amina.” {FEsw 180.2}— *The Review and Herald, November 17, 1891*

****Kanisa linalopigana vita ni hali yetu ya sasa kama kanisa. Tunapigana vita vizuri vya imani, na kudai ushindi wa Kristo kwa niaba yetu. Ushindi wa kanisa ni pale tunapomwona Yesu na akitupa thawabu yetu. Ndipo kanisa litamshinda Shetani kwa sababu ataangamizwa pamoja na malaika Zake waovu wote.***

HAZINA ZA KUHIFADHI AKILI.

Yesu aliiona jamii ya wanadamu, ikiwa katika ujinga, walioasi kutoka kwa Mungu, wakisimama chini ya adhabu ya sheria iliyovunjwa; na alikuja kuleta ukombozi, kutoa msamaha kamili, uliotiwa sahihi na Mkuu wa Mbinguni. Kama mwanadamu atakubali msamaha huu, anaweza kuokolewa; kama ataukataa, atapotea. Hekima ya Mungu pekee ndiyo inayoweza kufunua siri za mpango wa wokovu. Hekima ya wanadamu inaweza kuwa au isiwe ya thamani, kama uzoefu utakavyohibitisha, lakini hekima ya Mungu ni ya lazima; na bado wengi wanaodai kuwa wenye hekima wana hiari kuwa wajinga wa mambo ya uzima wa milele. Kosa kile unachoweza katika aina ya mafanikio ya kibinadamu, lakini lazima uwe na imani katika msamaha unaoletwa kwako kwa gharama isiyo na kikomo, au hekima yote iliyopatikana duniani, itaangamia pamoja nawe. {FEsw 181.1}

Kama Jua la Haki lingeweza kuondoa miale yake ya Nuru kutoka ulimwenguni, tungeachwa katika giza la usiku wa milele. Yesu alizungumza namna ambavyo mwanadamu hajakata kunena. Alitoa kwa wanadamu hazina yote ya Mbinguni katika hekima na maarifa. Ni Nuru inayomuangazia kila mtu amjiaye ulimwenguni. Kila aina ya Kweli ilikuwa dhahiri Kwake. Hakuja kutamka hisia na maoni yasiyo na uhakika; bali kusema tu Ukweli uliowekwa juu ya kanuni za milele. Basi kwa nini myachukulie maneno ya wanadamu yasiyo imara kuwa hekima iliyotukuka? wakati hekima kuu na ya hakika iko kwa kwa ajili yako? Watu huchukua maandishi ya wanasayansi, wanaoitwa kwa uwongo, na kutafuta kuyafanya yapatane na maandiko ya Biblia. Lakini pale ambapo hakuna makubaliano hapawezi kuwa na mapatano. Kristo anatangaza, "Hakuna mtu anayeweza kuwatumikia mabwana wawili." Hakika matakwa yao yatagongana. Tena na tena watu wamejaribu kuweka Biblia na maandishi ya watu kwa misingi ya kupatana; lakini jaribio limeonekana kushindwa; kwani hatuwezi kumtumikia Mungu na mali.

Tuko ulimwenguni, lakini hatupaswi kuwa wa ulimwengu. Yesu anasihi kwamba wale aliowafia, wasipoteze thawabu yao ya umilele kwa kuendekeza matamania yao juu ya mambo ya ulimwengu huu unaopotea, na hivyo kujikosesha wenyewe dhidi ya furaha isiyo na kikomo. Kwa akili nyepesi tunalazimika kukiri kwamba mambo ya Mbinguni ni bora kuliko vitu vya dunia, na bado moyo uliopotoka wa mwanadamu humpeleka kutanguliza mambo ya dunia. Maoni ya watu wakuu, nadharia za sayansi, zinazojulikana kwa uwongo, zimchanganywa na Kweli za Maandiko Matakatifu. {FEsw 181.2}

Lakini moyo ambao umejitoa kwa Mungu, hupenda Ukweli wa Neno la Mungu; kwa maana kwa njia ya Kweli Roho hufanywa upya. Akili ya kimwili haioni radhi katika kulitafakari Neno la Mungu, bali yeye ambaye amefanywa upya katika Roho

ya nia yake, huona tunu na mvuto mpya katika Maneno haya ya historia iliyo hai; kwa kuwa uzuri wa kimbingu na Nuru ya Mbinguni inaonekana kuangaza katika kila kitu kifungu. Kile ambacho kwa nia ya mwili ni jangwa lisilo na watu, kwa akili ya kiroho ni nchi ya vijito vilivyo hai. Kile ambacho kwa moyo usiofanywa upya kilionekana ni tasa, kwa walioongoka nafsi huwa bustani ya Mungu, iliyofunikwa na vichaka vyenye harufu nzuri na maua yanayochanua. {FEsw 182.2}

Biblia imewekwa kando, huku maneno ya watu wakuu, kama waitawavyo, yamechukuliwa mbadala Wake. Bwana na atusamehe kwa kidogo tulichoweka juu ya neno lake. Ingawa hazina zisizo na kifani zimo katika Biblia, na ni kama mgodi uliojaa ya madini ya thamani, haithaminiwi, haichunguzwi, na utajiri Wake haugunduliwi. Rehema na kweli na upendo ni vya thamani zaidi ya uwezo wetu wa kutambua; hakika hatuwezi kuwa na kiwango kikubwa sana cha hizi hazina, na ni katika Neno la Mungu tunapata jinsi tunavyoweza kuwa wamiliki wa utajiri huu wa Mbinguni, na bado kwa nini ni Neno la Mungu halipendezwi na wengi wanaojiita Wakristo? Je! Ni kwa sababu Neno la Mungu si Roho wala si uzima? Je, Yesu ameweka juu yetu kazi isiyopendeza, anapotuamuru “kuyachunguza Maandiko”? Yesu anasema, “Maneno niwaambiayo ninyi ni Roho na ni uzima.” Lakini mambo ya Rohoni hutambulikana kwa jinsi ya Rohoni, na sababu ya kutokuwa na matamania nayo, ni kukosa Roho ya Mungu. Moyo unapoletwa katika upatanifu na Neno, uzima mpya utatiririka ndani yako, Nuru mpya itaangaza katika kila mstari wa Neno, na itakuwa sauti ya Mungu katika nafsi yako. Kwa njia hii utakuwa na mtazamo wa Mbinguni, na kujua mahali unapokwenda, na utaweza kutumia vyema fursa zako leo. {FEsw 182.3}

Tunapaswa kumwomba Bwana afungue ufahamu wetu, ili tuweze kuufahamu Ukweli wa Bwana. Tukinyenyekeza mioyo yetu mbele za Mungu, tukiupepete nje ubatili na kiburi na ubinafsi, kwa neema tuliyopewa kwa wingi; ikiwa tunatamani kwa dhati na kuamini bila kusitasita, miale angavu ya Jua la Haki itamulika akili zetu, na kuuangazia ufahamu wetu wenye giza. Yesu Ndiye Nuru inayomulikia kila mtu amjiaye ulimwenguni. Yeye Ndiye Nuru ya ulimwengu, na anatusihi tuje Kwake, na tujifunze kutoka Kwake. Yesu Ndiye Mwalimu mkuu. Angeweza kufungua kwenye sayansi yale ambayo ingeweka uvumbuzi wa watu wakuu chini kama wadogo kabisa; lakini huu haukuwa utume Wake au kazi Yake. Alikuwa kutafuta na kuokoa kile kilichopotea, na Hakuweza kujiruhusu Mwenyewe kugeuzwa kutoka kwenye lengo Lake hata moja. Hakuruhusu chochote kumkengeusha. Kazi hii imekabidhiwa kwenye mikono yetu. Je, tutafanya hivyo? {FEsw 183.1}

Katika siku za Kristo walimu imara waliwafundisha watu katika mapokeo ya mababa, katika hadithi za kitoto, zilizochanganyikana na maoni ya watu wale ambao walidhaniwa ni mamlaka ya juu. Bado mtu wa chini au wa juu hakuweza kutambua miale yoyote ya Nuru katika mafundisho yao. Ni ajabu kwamba makutano walifuata nyayo za Bwana, na kumpa heshima walipokuwa wakisikiliza

Maneno Yake! Alifichua zile Kweli zilizokuwa zimezikwa chini ya takataka za uwongo, na akawaweka huru kutokana na mashaka na mila za watu, na akawaishi wasimame imara daima. Aliiokoa Kweli kutoka katika giza lake, na kuiweka katika mfumo wake sahihi, kuangaza katika mng'ao wake wa asili. Alihutubia watu kwa Jina Lake Mwenyewe; kwa kuwa mamlaka yalikuwa yamo ndani Yake Mwenyewe, na kwa nini watu, wanaodai kuwa wafuasi Wake, wasinene kwa mamlaka kuhusu masuala yale ambayo ameyapa Nuru? Kwa nini kuchukua vyanzo duni vya mafundisho wakati Kristo Ndiye Mwalimu mkuu anayejua mambo yote? Kwa nini tuwasilishe waandishi duni katika usikivu wa wanafunzi, wakati Yeye ambaye Maneno Yake ni Roho na uzima anapokaribisha, “Njoo, ... na ujifunze Kwangu”?

{FEsw 183.2}

Je, hatutakiwi kupendezwa sana na mafundisho ya Kristo? Je, hatutavutiwa na Nuru mpya na tukufu ya Ukweli wa Mbinguni? Nuru hii iko juu ya kila kitu ambacho mwanadamu anaweza kuwasilisha. Tunaweza kupokea Nuru tu tunapokuja msalabani na kujisalimisha wenyewe kama madhabahu ya sadaka. Hapa udhaifu wa mwanadamu unadhihirika; hapa Nguvu Zake zinafunuliwa. Hapa watu wanaona kuna nguvu ndani ya Kristo kuwaokoa kabisa wote wamjiao Mungu kwa Yeye.

{FEsw 184.1}

Je! hatutakuwa watendaji wa maneno ya Yeye ambaye anajua kila kitu? Je, hatutaifanya Biblia kuwa mtu wa shauri letu katika elimu na mafunzo ya vijana wetu? Neno la Mungu ni msingi wa maarifa yote ya Kweli, na Kristo anafundisha kile ambacho wanadamu wanapaswa kufanya ili kuokolewa. Hadi sasa mipango ya adui imefanywa katika kuwaletea wanafunzi wetu vitabu kama vile ambavyo vimefundisha makosa tu, na kuwasilisha hekaya ambazo zimejaribu na kuamsha tamaa zao za kimwili. Je, tumlete katika shule zetu mpanzi wa magugu? Je, tutaruhusu watu ambao wanaitwa wakuu, na bado ambao wamefundishwa na adui wa Ukweli wote, kuwa na elimu ya vijana wetu? Au tutachukua Neno la Mungu kama mwongozo wetu, na kufanya shule zetu ziendeshwe zaidi kwa kufuata utaratibu wa shule za kale za manabii? **{FEsw 184.2}**

Kama Biblia ingesomwa, ingechunguzwa na kutiiwa; kama tungekuwa na Roho ya Kristo, tungepaswa kufanya juhudi thabiti kuwa watenda kazi pamoja na Mungu. Tunapaswa kufahamu vyema thamani ya nafsi; kwani kila nafsi iliyoongoka kwa Mungu maana yake ni chombo kilichowekwa wakfu kwa matumizi matakatifu, akiba ya Ukweli, mbebaji wa Nuru kwa wengine. Mungu anatarajia mengi kutoka shule kuliko ambayo sasa yametolewa. Kristo amesema, “Msikitendee kazi chakula chenye kuharibika, bali chakula kidumucho hata uzima wa milele; ambacho Mwana wa Adamu atawapa; kwa sababu Huyu Ndiye aliyetiwa muhuri na Baba, yaani, Mungu.” **{FEsw 184.3}**

Kisha tutaelewa kwa usahihi mafundisho ya Neno la Mungu, na kuthamini Ukweli kama hazina ya thamani zaidi ambayo tunaweza kutumia kuhifadhi akili.

Tutakuwa na chemchemi za maji daima ya uzima. Tutaomba kama mwandishi wa - Zaburi, "Unifumbue macho yangu, niyatazame maajabu yatokayo katika sheria Yako," na tutajua kama Yeye kwamba "hukumu za BWANA ni Kweli na zina haki kabisa. Ni za kutamanika kuliko dhahabu, naam, kuliko wingi wa dhahabu safi, nazo ni tamu kuliko asali, kuliko sega la asali. Tena mtumishi wako huonywa kwazo, katika kuzishika kuna thawabu nyingi." {FEsw 185.1}— *The Review and Herald, November 24, 1891.*

SAYANSI YA WOKOVU NI YA KWANZA KATIKA SAYANSI ZOTE.

Shule zilizoanzishwa miongoni mwetu ni masuala ya uwajibikaji mkubwa; maana maslahi muhimu yanahusika. Kwa namna maalum shule zetu ni tamasha la maonyesho ambayo hutazamwa na malaika na wanadamu. Maarifa ya sayansi ya kila aina ni nguvu, na ni katika kusudi la Mungu sayansi ya hali ya juu itafundishwa katika shule zetu kama maandalizi ya kazi ambayo itatangulia matukio ya mwisho wa historia ya dunia. Ukweli unapaswa kwenda kwenye mipaka ya mbali zaidi ya dunia, kupitia mawakala waliofunzwa kwa kazi. Lakini ingawa ujuzi wa sayansi ni nguvu, ujuzi ambao Yesu alikuja kuupa ulimwengu ulikuwa ujuzi wa injili. Nuru ya Ukweli ilikuwa imulike miale angavu katika miisho ya dunia, na kuukubali au kuukataa ujumbe wa Mungu kulihusisha hatima ya milele ya Roho za watu. {FEsw 186.1}

Mpango wa wokovu ulikuwa na nafasi yake katika mashauri ya Yeye Asiye na mwisho tangu milele. Injili ni ufunuo wa upendo wa Mungu kwa wanadamu, na humaanisha kila kitu ambacho ni muhimu kwa furaha na ustawi wa wanadamu. Kazi ya Mungu duniani haipimiki kwa umuhimu wake, na ni lengo maalum la Shetani kuiminyia ili watu wasiweze kuiona au kuitia akili mwao, ili aweze kufanya madanganyifu yake katika kazi ya kuharibu wale ambao Kristo alikufa kwa ajili yao. Ni kusudi lake kuyafanya yale yaliyovumbuliwa na mwanadamu yainuliwe juu ya hekima ya Mungu. Wakati akili imezama katika dhana na nadharia za watu na kisha wakaiondoa hekima ya Mungu, watu huwekwa kwenye ibada ya sanamu. Sayansi, kama waitavyo wanadamu, ambayo ni sayansi ya uwongo, imeinuliwa juu ya Mungu, asili juu Muumba Wake, na Je, Mungu anawezaje kuitazama hekima hiyo? {FEsw 186.2}

Katika Biblia wajibu wote wa mwanadamu umefafanuliwa. Sulemani anasema, "Mche Mungu, nawe uzishike amri Zake; maana kwa jumla ndiyo impasayo mtu." Mapenzi ya Mungu yanafunuliwa katika Neno Lake lililoandikwa, na haya ndiyo maarifa ya muhimu. Hekima ya kibinadamu, kufahamu lugha za mataifa mbalimbali, ni msaada katika kazi ya umishonari. Ufahamu wa desturi za watu, kuelewa mahali na nyakati za matukio, ni maarifa ya vitendo; kwani inasaidia katika kutengeneza hekima na mada za Biblia kwa uwazi, katika kuleta nguvu ya masomo ya Kristo; lakini sio lazima kujua mambo haya. Msafiri anaweza kupata njia iliyotengenezwa ya waliokombolewa kuiendea, na hakutakuwa na udhuru wowote kwa yeyote anayeangamia kwa kutoelewa Maandiko. {FEsw 186.3}

Katika Biblia kila kanuni muhimu imetangazwa, kila wajibu umefanywa wazi, kila jukumu limewekwa wazi. Wajibu wote wa mwanadamu umefupishwa na Mwokozi. Husema, "Mpende Bwana wako Mungu kwa moyo wako wote, na kwa Roho yako

yote, na kwa akili zako zote.... mpende jirani yako kama nafsi yako." Katika Neno mpango wa wokovu umeelezwa waziwazi. Zawadi ya uzima wa milele imeahidiwa kwa sharti la imani iokoayo katika Kristo. Nguvu ya ivutayo ya Roho Mtakatifu imeoneshwa kama wakala katika kazi ya wokovu wa mwanadamu. Ujira wa waaminifu, adhabu ya waovu, yote yamewekwa nje kwa mistari ya wazi. Biblia ina sayansi ya wokovu kwa wote wale watakaosikia na kuyatenda Maneno ya Kristo. {FEsw 187.1}

Mtume anasema, "Kila Andiko, lenye pumzi ya Mungu, na lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema." Biblia hujifafanua yenyewe. Fungu moja litathibitisha kuwa ufunguo ambao utafungua mafungu mengine, na kwa njia hii Nuru itaangaza juu ya maana iliyofichika ya Neno. Kwa kulinganisha mafungu tofauti yanayoshughulikia mada moja, kutazama maana zake kila upande, maana ya Kweli ya Maandiko itakuwa dhahiri. {FEsw 187.2}

Wengi wanafikiri kwamba ni lazima wachunguze Fafanuzi za Maandiko Matakatifu ili kuelewa maana ya neno la Mungu, na tusingechukua msimamo kuwa fafanuzi hazifai kusomwa; lakini itahitaji utambuzi mgumu kugundua Ukweli wa Mungu ndani ya wingi wa maneno ya wanadamu. Ni kidogo kiasi gani kimefanywa na kanisa kama kundi linalodai kuiamini Biblia, kukusanyika vito vilivyotawanyika vya Neno la Mungu katika mnyororo mmoja mkamilifu wa Ukweli! Vito vya Ukweli haviko juu ya uso wa nchi, kama wengi wanavyodhani. Akili kuu katika muungano wa uovu daima iko kazini kuuweka Ukweli nje ya ufahamu, na kuleta katika mtazamo kamili maoni ya watu wakuu. Adui anafanya yote awezayo ili kuificha Nuru ya Mbinguni kupitia taratibu na mchakato wa elimu; kwa maana hataki watu waisikie sauti ya Bwana, ikisema, Njia ni hii, ifuateni. {FEsw 187.3}

Vito vya Ukweli vimetawanyika kwenye uwanja wa mafunuo; lakini vimezikwa chini ya mapokeo ya wanadamu, chini ya maneno na amri za wanadamu, na hekima kutoka Mbinguni imepuuzwa kivitendo; kwa maana Shetani amefaulu kufanya ulimwengu uamini kwamba maneno na mafanikio ya wanadamu ni ya maana makubwa. Bwana Mungu, Muumba wa malimwengu, kwa gharama isiyo na kipimo aimetoa injili kwa ulimwengu. Kupitia wakala huyu wa Mungu, furaha, chemchemi za kuburudisha za faraja ya Mbinguni na faraja ya kudumu zimefunguliwa kwa ajili ya wale watakaokuja kwenye chemchemi ya uzima. Kuna mifereji ya Ukweli ambayo bado haijagunduliwa; lakini mambo ya kiroho kutambulika kiroho. Akili zilizojaa uovu haziwezi kuthamini thamani ya zile Kweli kama ilivyo ndani ya Yesu. Uovu unapotunzwa, watu hawaoni ulazima wa kufanya juhudi kwa bidii, kwa maombi na kutafakari, kuelewa kile ambacho ni lazima kukijua au kuipoteza mbingu. Kwa muda mrefu wamekuwa chini ya kivuli cha adui, na huona Ukweli kama wanadamu wanavyotazama vitu kupitia kwenye kioo chenye moshi na

kisicho kamili; maana vitu vyote ni giza na vimepotoka machoni pao. Maono yao ya kiroho ni dhaifu na hayaaminiki; kwa maana wanakitazama kivuli, na kujiepusha na Nuru. {FEsw 188.1}

Lakini wale wanaodai kumwamini Yesu, wanapaswa kudumu Nuruni. Wanapaswa kuomba kila siku kwa ajili ya Nuru ya Roho Mtakatifu iangaze kwenye kurasa za kitabu kitakatifu, ili wawezeshwe kufahamu mambo ya Roho wa Mungu. Lazima tuwe na tumaini kamilifu kwa Neno la Mungu, kama sivyo tutapotea. Maneno ya watu, hata yawe wakuu kiasi gani, hayawezi kutufanya wakamilifu, kwa kutufanya kufaa kwa matendo yote njema. "Mungu amewachagua tangu mwanzo mpate wokovu katika kutakaswa na Roho na kuamani ile Kweli." Katika Andiko hili mawakala wawili katika wokovu wa mwanadamu wamefunuliwa, —Nguvu ya Mungu, imani yenye nguvu, iliyo hai ya wale ambao humfuata Kristo. Ni kwa njia ya utakaso wa Roho na imani ya ile Kweli, ndipo tunakuwa watenda kazi pamoja na Mungu. Mungu anasubiri ushirikiano na kanisa Lake. Haundi ili kuongeza kipengele kipya cha ufanisi katika Neno Lake; Amefanya kazi Yake kuu katika kutoa msukumo Wake kwa ulimwengu. Damu ya Yesu, Roho Mtakatifu, na Neno la Mungu, ni vyetu. Lengo la utoaji huu wote wa Mbinguni liko mbele yetu, - Roho ambazo Kristo alikufa kwa ajili yake, - na hutegemea sisi kuzishika ahadi ambazo Mungu ametoa, na kuwa watenda kazi pamoja Naye; kwani wakala wa Kimungu na wa kibinadamu lazima washirikiane katika kazi hii. {FEsw 188.2}

Sababu ambayo watu wengi wanaojiita Wakristo hawana uzoefu sahihi, unaoeleweka vizuri, ni kuwa hawafikirii kuwa ni fursa yao kuelewa kile ambacho Mungu amekisema kupitia Neno Lake. Baada ya ufufuo wa Yesu, wawili wa wanafunzi Wake walikuwa wakisafiri kuelekea Emau, na Yesu akajiunga nao. Lakini hawakumtambua Bwana wao, na wakafikiri alikuwa mgeni au mtu baki, ingawa "akaanza kutoka Musa na manabii wote, akawaeleza katika maandiko yote mambo yanayomhusu Yeye Mwenyewe. Wakakaribia kile kijiji walicholuwa wakienda: Naye alifanya kama anataka kuendelea mbele. Wakamshawishi kwa bidii, wakisema, Kaa pamoja nasi; kwa kuwa kumekuchwa, na mchana unakwisha. Akaingia ndani kukaa nao. Ikawa alipokuwa ameketi nao chakulani, Alitwaa mkate, akaubariki, akaumega, akawapa. Yakafumbuliwa macho yao, wakamtambua; kisha akatoweka mbele yao. Wakaambiana, Je! Mioyo yetu haikuwaka ndani yetu, hapo alipokuwa akisema nasi njiani, na kutufunulia Maandiko? ... Ndipo akawafunulia akili zao wapate kuelewa na Maandiko." Hii ndiyo kazi ambayo tunaweza kumtazamia Kristo atufanyie; kwa kuwa yale Bwana aliyofunua, ni kwa ajili yetu na watoto wetu milele. {FEsw 189.1}

Yesu alijua kwamba chochote kilichotolewa ambacho hakikuwa na upatanifu na kile Alichokuja duniani kukifunua, kilikuwa cha uwongo na cha udanganyifu. Lakini Alisema, "Kila aliye wa Kweli huisikia sauti Yangu." Akiwa alimesimama katika mashauri ya Mungu, akiwa amekaa katika vilele vya milele vya Patakatifu, vipengele vyote vya kweli vilikuwa ndani Yake, na ni Vyake; kwani Alikuwa mmoja na Mungu.

“Amin, amin, nakuambia, lile tulijualo twalinena, na lile tuliloliona twalishuhudia; wala ushuhuda wetu hamwukubali. Ikiwa nimewaambia mambo ya duniani, wala hamsadiki, mtasadiki wapi niwaambiapo mambo ya Mbinguni? Wala hakuna mtu aliyepaa Mbinguni, ila Yeye aliyeshuka kutoka Mbinguni yaani Mwana wa Adamu.” “Kila Neno la Mungu limehakikishwa: Yeye ni ngao yao wamwaminio. Usiongeze Neno kwa Maneno Yake, asije akakulaumu, ukaonekana u mwongo.” {FEsw 190.1}— *The Review and Herald, December 1, 1891.*

TABIA YA KIKRISTO IDHIHIRISHWE KWA MFANO KWA WALIMU NA WANAFUNZI

Kwa Jjina la Bwana wangu, nawasihi vijana wa kiume na wa kike wanaodai kuwa wana na binti za Mungu, kulitii Neno la Mungu. Natoa wito kwa walimu katika shule zetu kuwa mfano sahihi kwa wale wanaochangamana nao. Wale ambao wangestahili kuzifinyanga tabia za vijana, lazima wawe wanafunzi katika shule ya Kristo, ili wawe wapole na wanyenyekevu wa moyo, kama ilivyokuwa kwa Kielelezo cha Bwana. Katika mavazi, katika tabia, katika njia zao zote, wanapaswa kuonesha tabia ya Kikristo, ikifunua Ukweli kwamba wako chini ya kanuni za nidhamu za hekima ya Mwalimu mkuu. Kijana wa Kikristo anapaswa kuwa na unyofu wa moyo na bidii, akifunzwa kubeba majukumu kwa moyo wa ushujaa na mkono wa hiari. Anapaswa kuwa tayari kukutana na majaribu ya Maisha kwa uvumilivu na ujasiri. Anapaswa kutafuta kuunda tabia inayoendana na mfano wa Mmoja aliye wa Kiungu, akifuata kanuni za thamani, akijithibitisha mwenyewe katika tabia ambazo zitamwezesha kushinda taji la mshindi. {FEsw 191.1}

Katika maisha ya shule vijana wanaweza kupanda mbegu ambazo zitazaa mavuno, si ya miiba, bali ya nafaka za thamani kwa ajili ya ghala ya Mbinguni. Hakuna wakati mzuri zaidi kuliko wakati unaotumika shuleni ambapo kukiri nguvu ya neema ya wokovu ya Kristo, kutawaliwa na kanuni za sheria ya Mungu, na ni kwa ajili ya maslahi ya mwanafunzi kuishi maisha ya ucha Mungu. Utukufu mkuu wa maisha unatokana na uhusiano pamoja na Kristo. Hakuna mtu anayeishi kwa ajili yake mwenyewe. Maisha yenu yameunganishwa na wengine wote katika mtandao wa ubinadamu wote, na mnapaswa kuwa watenda kazi pamoja na Mungu kwa ajili ya wokovu wa wale wanaoangamia katika upotovu na ole. Mnapaswa kuwa vyombo vya kuwavuta wote wale mnaoshirikiana nao kwa maisha bora, ili kuelekeza akili zao kwa Yesu. {FEsw 191.2}

Yohana anaandika hivi: “Nimewaandikia ninyi, vijana, kwa sababu mna nguvu, na Neno la Mungu linakaa ndani yenu, nanyi mmemshida yule mwovu. Na Paulo anamhimiza Tito kuwaonya vijana wawe na “akili na kiasi.” Inua nafsi yako kuwa kama alivyokuwa Danieli, mtumishi mwaminifu/mwadilifu na thabiti wa Bwana wa majeshi. Tafakari vizuri njia ya miguu yako; kwa maana unasimama katika ardhi takatifu, na Malaika ya Mungu wako kando yako. Ni sawa kwamba mnapaswa kuhisi kwamba ni lazima kupanda hadi ngazi ya juu kabisa ya ngazi ya elimu. Falsafa na historia ni masomo muhimu; lakini kujitoa kwako mhanga kwa muda na pesa hakutafaa kitu, ikiwa hutumii mafanikio yako kwa ajili ya heshima ya Mungu na wema kwa wanadamu. Isipokuwa ujuzi wa sayansi ni ngazi ya kufikia malengo ya juu zaidi, haitakuwa na faida yoyote. Elimu ambayo haitoi maarifa ya

kudumu kama umilele, haina maana. Isipokuwa umeiweka mbingu na maisha yajayo, ya umilele mbele yako, mafanikio yako hayana thamani ya kudumu. Lakini ikiwa Yesu ni mwalimu wako, si kwa siku moja tu ya juma, lakini kila siku, kila saa, unaweza kuwa na tabasamu Lake juu yako katika harakati za kupata elimu. {FEsw 191.3}

Danieli daima aliweka mbele yake Utukufu wa Mungu, nawe pia unapaswa kusema, Bwana, nataka maarifa, wala si kwa ajili ya kujitukuza nafsi; bali kutimiza matarajio ya Yesu, nipate kukamilisha tabia ya nia na hekima ya Kikristo, kupitia neema aliyonipa. Je, wanafunzi watakuwa waaminifu kwa kanuni kama alivyokuwa Danieli? {FEsw 192.1}

Katika siku zijazo kutakuwa na haja kubwa zaidi ya wanaume na wanawake wenye sifa za kielimu kuliko ilivyokuwa hapo awali; kwa kuwa mashamba yanafunguka kwa upana mbele yetu, na ni meupe tayari kwa ajili ya kuvunwa. Katika haya mashamba mwaweza kuwa watenda kazi pamoja na Mungu. Lakini ikiwa ninyi ni wapenda anasa kuliko kumpenda Mungu, ikiwa mmejawa na moyo usio na umakini, na futuhi, nanyi mkaruhusu fursa za dhahabu kupita bila kupata ujuzi, bila kuziweka mbao imara katika jengo lenu la tabia, mtakuwa duni na walemavu katika aina yoyote ya kazi mtakayoweza kufanya. {FEsw 192.2}

Wakati elimu bora ni ya faida kubwa ikiwa imeunganishwa na kujitoa mhanga kwa yule aliye nayo, bado wale ambao hawana fursa hiyo ya kupata mafanikio ya juu ya elimu hawana haja ya kufikiria kuwa hawawezi kuendelea katika maisha ya kiakili na kiroho. Ikiwa watafaidika zaidi na ujuzi walio nao, ikiwa watatafuta kukusanya kitu katika hazina yao kila siku, na watashinda upotovu wote wa hasira kupitia kusitawisha kwa bidii tabia kama za Kristo, Mungu atawafungulia mifereji ya hekima, na inaweza kusemwa juu yao kama ilivyosemwa zamani, kuhusu watoto wa Kiebrania, Mungu aliwapa hekima na ufahamu. {FEsw 192.3}

Si kweli kwamba vijana wenye akili kubwa sikuzote hupata mafanikio makubwa zaidi. Ni mara ngapi watu wenye vipaji na elimu wamewekwa katika nafasi za kuaminiwa, na wamethibitisha kushindwa. Pambo lao lilikuwa na muonekano wa dhahabu, lakini ilipojaribiwa, ilionekana kuwa chuma kisicho na thamani na takataka. Walishindwa katika kazi yao kwa kukosa uaminifu. Hawakuwa wachapakazi na wastahimilivu, na hawakwenda katika kiini cha mambo. Hawakuwa tayari kuanza chini ya ngazi, na kwa subira ya taabu, wakipanda pande zote ngazi kwa ngazi mpaka wamefika kileleni. Walitembea kwenye cheche (miale ang'avu ya fikra) ya kujiwashia wao wenyewe. Hawakutegemea hekima ambayo ni Mungu pekee awezaye kuitoa. Kushindwa kwao hakukuwa kwa sababu hawakupata nafasi, bali kwa sababu hawakuwa na akili timamu. Hawakuhisi kuwa faida zao za kielimu zilikuwa za thamani kwao, na kwa hivyo hawakusonga mbele kama ambavyo wangeweza kusonga mbele katika elimu ya dini na sayansi. Akili na tabia zao hazikusawazishwa kwa kanuni za juu za haki. {FEsw 193.1}

Hebu Vijana wetu na wawe na kiasi, wakizitafakari njia za miguu yao. Hebu waiepuke dhambi kwa sababu inaharibu kwa mielekeo yake na haimpendezi Mungu. Hebu watambue ni uwezekano gani ulio ndani mwao, na wamtafute Mungu kwa ajili ya neema katika njia njia za haki. Na watafute ushauri na maongozi ya Bwana, ili watumie maisha yao kwa ajili ya Utukufu Wake duniani. {FEsw 193.2}

Katika kupata elimu, mafanikio hayapaswi kuchukuliwa kama suala la bahati nasibu au hatima; ni kutoka kwa Mungu Yule aliyesoma moyo wa Danieli, ambaye alitazama kwa furaha usafi wa nia yake, azimio lake la kusudi la kumheshimu Bwana. Danieli hakutembea katika miale ya kutengeneza yeye mwenyewe, bali alimfanya Bwana kuwa hekima yake. Falsafa ya kimbingu ilifanywa kuwa msingi wa elimu yake. Yeye alikaribisha shauri la Bwana. Laiti wanafunzi wote wangekuwa kama alivyokuwa Danieli; lakini wengi hawaoni umuhimu wa kujisalimisha katika nidhamu ya Bwana. {FEsw 193.3}

Laiti wote wangetambua kuwa bila Kristo hawawezi kufanya lolote! Wale wasiokusanya pamoja Naye hutawanya mbali. Mawazo yao na vitendo vyao havitakuwa na tabia sahihi, na mvuto wao utakuwa wa uharibifu wa mema. Matendo yetu yana athari mbili; kwani yanaathiri wengine na sisi wenyewe. Mvuto huu utakuwa ama baraka au laana kwa wale tunaoshirikiana nao. Ni kidogo jinsi gani tunauthamini Ukweli huu. Matendo hufanya mazoea, na mazoea, tabia, na tusipochunga tabia zetu, hatutakuwa na sifa za kuungana pamoja na wakala wa Mbinguni katika kazi ya wokovu, wala kuwa tayari kuingia katika makao ya Mbinguni ambayo Yesu amekwenda kuyaandaa; kwani hakuna mtu atayekuwepo pale, isipokuwa wale waliosalimisha nia yao na njia zao katika mapenzi na njia za Mungu. Yeye ambaye tabia yake imethibitishwa, ambaye alistahimili majaribu, ambaye ni mshiriki wa asili ya Uungu, atakuwa kati ya wale ambao Kristo anawataja kuwa wamebarikiwa. {FEsw 194.1}

Bila Kristo hatuwezi kufanya lolote. Kanuni safi za uadilifu, uzuri, na wema zote vinatoka kwa Mungu. Dhamiri ya uwajibikaji, ya huruma kama ya Kristo, upendo kwa Roho zingine na upendo kwa nafsi yako, kwa sababu wewe ni wa Mungu, na umenunuliwa kwa damu ya thamani ya Kristo, itakufanya kuwa mtenda kazi pamoja na Mungu, na kukujaalia kuwa na mvuto na nguvu ya ivutayo. Lazima uiheshimu imani yako mwenyewe ili ufaulu kuitambulisha kwa wengine. Kwa mfano pamoja na kanuni, lazima uonyeshe kwamba unaiheshimu imani yako, ukisema kwa heshima mambo matakatifu. Usiruhusu kamwe usemi wa futuhi na wa kuudhi kutoka katika midomo yako unapoyanukuu Maandiko. Unapoichukua Biblia mikononi mwako, kumbuka kwamba uko kwenye ardhi takatifu. Malaika wako karibu nawe, na endapo macho yako yangefunguliwa, ungewaona. Mwenendo wako uwe ule utakaoacha mvuto juu ya kila nafsi mnayoshirikiana nayo kwani mazingira safi na matakatifu yanakuzunguka. Neno moja la ubatili au la kutofikiri vyema, kicheko kimoja kidogo, kinaweza kuelekeza Roho katika mwelekeo mbaya. Mambo

ya kutisha ni matokeo ya kutokuwa na uhusiano wa kudumu na Mungu. {FEsw 194.2}

Jiepusheni na maovu yote. Dhambi za kawaida, ingawa hazina maana zinaweza kuzingatiwa, zitaharibu hisia zako za maadili, na kuzima hisia ya ndani ya Roho wa Mungu. Tabia ya mawazo huacha chapa yake juu ya nafsi, na mazungumzo yote duni huchafua akili. Matendo yote maovu yanawaangamiza wale wanaoyafanya. Mungu anaweza na atamsamehe mwenye dhambi anayetubu, lakini ingawa amesamehewa, Roho yake inakuwa imeshaharibiwa; uwezo wa mawazo yaliyoinuliwa iwezekanavyo kwa wasio na hatia nayo yameharibika. Wakati wote Roho hubeba makovu. Ndipo na tutafute imani ile itendayo kazi kwa upendo na kuusafisha moyo; ili tuweze kuwakilisha tabia ya Kristo kwa ulimwengu. {FEsw 195.1} – *The Review and Herald, December 8, 1891.*

ULIMWENGU KWA HEKIMA HAUKUMJUA MUNGU

Ukweli wa Mungu hauna kikomo, unaweza kupanuka bila kipimo, na kadiri tunavyoutafakari, ndivyo Utukufu wake unavyoonekana. Ukweli umefunuliwa mbele yetu, na bado Maneno ya Paulo kwa wale Wagalatia yanatumika kwetu. Anasema: “Enyi Wagalatia msio na akili! Ni nani aliyewaloga, ninyi ambao Yesu Kristo aliwekwa wazi mbele ya macho yenu ya kuwa amesulubiwa? Nataka kujifunza Neno hili moja kwenu, Je, mlimpokea Roho kwa matendo ya sheria, au kwa kusikia kunakotokana na imani? Je, mmekuwa wajinga namna hii? Baada ya kuanza katika Roho, mnataka kukamilishwa katika mwili? Mmepatikana na mateso makubwa namna hii bure? ikiwa ni bure kweli.” {FEsw 196.1}

“Bila Mimi,” Kristo asema, “hamwezi kufanya neno lo lote.” Wale wanaojizatiti kuendeleza kazi kwa nguvu zao wenyewe bila shaka watashindwa. Elimu peke yake haitamfanya mtu kufaa kwa katika nafasi ya kazi, haitamwezesha mtu kupata maarifa ya Mungu. Sikia kile Paulo anachopaswa kufanya sema juu ya jambo hili: “Maana Kristo hakunituma ili nibatize, bali nihubiri Habari Njema wala si kwa hekima ya maneno, msalaba wa Kristo usije ukabatilika. Kwa sababu Neno la msalaba kwao wanaopotea ni upuuzi; bali kwetu sisi tunaookolewa ni nguvu ya Mungu. Kwa kuwa imeandikwa, Nitaiharibu hekima yao wenye hekima, na akili zao wenye akili nitazikataa. Yu wapi mwenye hekima? Yu wapi mwandishi? Yu wapi mleta hoja wa zamani hizi? Je! Mungu hakuifanya hekima ya ulimwengu hii kuwa ni upumbavu? Kwa maana katika hekima ya Mungu, dunia isipopata kumjua Mungu kwa hekima Yake, Mungu alipenda kuwaokoa waaminio kwa upuzi wa lile Neno lililohubiriwa.” {FEsw 196.2}

Kupitia nyakati za giza zilizofuatana, katika usiku wa giza la upagani, Mungu aliwaruhusu wanadamu kujaribu majaribio ya kumtafuta Mungu kwa hekima yao wenyewe, wasidhihirishe kutoweza kwao kwa kuridhika kwake, bali watu wenyewe wapate kuona kwamba hawakuweza kupata maarifa ya Mungu na ya Yesu Kristo Mwanawe, ila kupitia ufunuo wa neno lake kwa Roho Mtakatifu. Kristo alipokuja ulimwengu, jaribio lilikuwa limefanywa kikamilifu, na matokeo yakawa dhahiri kwamba ulimwengu kwa hekima haukumjua Mungu. Hata kanisani Mungu ameruhusu watu wajaribu hekima yao wenyewe katika jambo hili, lakini wakati shida inapokuja kupitia udhaifu wa mwanadamu, Mungu ameinuka sana kuwatetea watu wake. Wakati kanisa lilipokuwa likishuka, wakati mitihani na ukandamizaji ulipowafikia watu wake Alizidi kuwainua zaidi kwa ukombozi wa ishara. Walimu wasio waaminifu walipokuja kati ya watu, udhaifu ulifuata, na imani ya watu wa Mungu ilionekana kupungua; lakini Mungu aliinuka na kutakasa eneo lake, na waliojaribiwa na wa Kweli waliinuliwa. {FEsw 196.3}

Kuna nyakati ambapo uasi huingia, wakati ucha Mungu unapoachwa nje ya mioyo na wale ambao walipaswa kushika hatua pamoja na Kiongozi wao wa Kiungu. Watu wa Mungu wanajitenga na chanzo cha nguvu zao, na kiburi, ubatili, ubadhirifu, na maonyesho kufuata. Kuna sanamu ndani na nje; lakini Mungu humtuma Mfariji kama Mwenye kukemea dhambi, ili watu Wake waonywe kwa uasi wao na kukemewa kwa kurudi nyuma kwao. Wakati upendo Wake wa thamani utakapodhihirishwa kwa shukrani na kuthaminiwa, Bwana atamimina zeri ya faraja na mafuta ya shangwe. {FEsw 197.1}

Watu wanapoongozwa kutambua kwamba uwezo wao ni mdogo sana, na wanasadiki kwamba hekima yao ni upumbavu tu ndipo wanapomgeukia Bwana na kumtafuta kwa moyo wao wote; ili wampate. {FEsw 197.2}

Imeoneshwa kwangu kuwa kila kanisa miongoni mwetu linahitaji utendaji wa kina wa Roho wa Mungu. Laiti tungewaelekeza watu kwenye msalaba wa Kalvari. Tungewaambia wamtazame Yule ambaye dhambi zao zilimumiza. Tungewaonesha wamtazame Mkombozi wa ulimwengu anayeteseka kwa adhabu ya ukiukwaji wao wa sheria ya Mungu. Hukumu ni kwamba “Roho itendayo dhambi ndiyo itakayokufa.” Lakini juu msalabani mwenye dhambi humwona Mwana-pekee wa Baba, akifa badala yake, na kumpa uhai mpotovu. Akili zote katika dunia na mbingu zinaitwa kuutazama upendo wa namna gani Baba ametupatia ili tuitwe wana wa Mungu. Kila mwenye dhambi anaweza kutazama na kuishi. Usichunguze tukio la Kalvari kwa akili isiyojali, na yenye mashaka. Je, inaweza kuwa kwamba Malaika hututazama, wapokeaji wa upendo wa Mungu, na kutuona tukiwa baridi, tusiojali, tusiovutiwa, wakati mbingu kwa mshangao inapotazama kazi ya ajabu ya ukombozi kuuokoa ulimwengu ulioanguka, na hutamani kuangalia katika siri kuu ya upendo na ole wa Kalvari? Malaika kwa kustaajabu na kushangaa hutazama wale ambao wokovu wao mkuu sana umetolewa, na kustaajabia kwamba upendo wa Mungu haujawaamsha, na kuwaongoza kutoa nyimbo za shukrani na kuabudu. Lakini matokeo ambayo mbingu zote huyatazama hayaonekani miongoni mwa wale wanaodai kuwa wafuasi wa Kristo. Ni jinsi gani tunakuwa tayari kuzungumza maneno ya kupendeza ya marafiki na jamaa zetu, na bado ni jinsi tulivyo wazito kusema juu ya Yeye ambaye upendo Wake hauna kifani katika Kristo Aliyesulubiwa katikati yenu. {FEsw 197.3}

Upendo wa Baba yetu wa Mbinguni katika karama ya Mwana Wake wa pekee kwa ulimwengu, inatosha kuamsha kila Roho, kuyeyusha kila ugumu, moyo usio na upendo katika majuto na huruma; na je, bado viumbe wa Mbinguni watawaona wale ambao Kristo alikufa kwa ajili yao, wakiwa hawana hisia na upendo Wake, wagumu wa moyo, na bila mwitikio wa shukrani na upendo kwa Mpaji wa vitu vyote vyema? Mambo yasiyo na umuhimu yatayofyonza nguvu zote za mtu, na upendo wa Mungu ukose mwitikio? Je, Jua la Haki litang’aa bure? Kwa mtazamo wa Alichokifanya Mungu, madai Yake yanaweza kuwa bure juu yako? Je, mioyo yetu inaweza

kuguswa, inaweza kuvutiwa na upendo wa Bwana? Je, tuko tayari kuwa vyombo viteule? Je! jicho la Mungu haliko juu yetu, na hakuamuru kutuletea ujumbe Wake wa Nuru? Tunahitaji ongezeko la imani. Lazima tusubiri, lazima tukeshe, lazima tuombe, lazima tufanye kazi, tukisihi kwamba Roho Mtakatifu aweze kumwagwa kwa wingi, ili tuwe Nuru katika ulimwengu. {FEsw 198.1}

Yesu aliutazama ulimwengu katika hali yake ya kuanguka kwa huruma isiyo na kikomo. Aliuchukua ubinadamu juu Yake ili aweze kuugusa na kuuinua ubinadamu. Alikuwa kutafuta na kuokoa kile kilichopotea. Alikifikia kina kirefu cha taabu na ole wa mwanadamu, kumchukua mwanadamu kama alivyomkuta, amechafuliwa na ufisadi, amedhalilishwa kwa uovu, mpotovu wa dhambi, na akiwa ameungana na Shetani katika uasi, na kumwinua aketi kwenye kiti Chake cha enzi. Lakini iliandikwa juu Yake kwamba “Yeye hatashindwa wala kuvunjika moyo,” na akatoka katika njia ya kujikana na kujinyima, akitupa mfano wa kuzifuata nyayo Zake. Tunapaswa kufanya kazi kama Yesu, tukiondoka katika anasa zetu wenyewe, tukiepuka kununuliwa aukurubuniwa na Shetani, tukidharau, na kuuchukua ubinafsi, ili tupate kutafuta na kuokoa kile kilichopotea, kuleta Roho kutoka gizani kuja kwenye Nuru, hadi kwenye Nuru ya jua ya upendo wa Mungu. Tumeagizwa kwenda na kuihubiri injili kwa kila kiumbe. Tunapaswa kuwapelekea waliopotea habari kuwa Kristo anaweza kusamehe dhambi, anaweza kuifanya upya asili, anaweza kuifunika nafsi katika mavazi ya haki Yake, kumleta mdhambi katika nia ya haki yake, na kumfundisha na kumfanya kufaa kuwa mtenda kazi pamoja Mungu. {FEsw 199.1}

Roho iliyoongoka inaishi ndani ya Kristo. Giza lake limepita, na Nuru mpya na ya Mbinguni inaangaza ndani ya nafsi yake. “Yeye Aishindaye nafsi ana hekima.” “Na walio na hekima watang’aa kama mwanga wa jua; nao wawaongozao wengi kutenda haki kama nyota milele na milele.” Kile kinachofanywa kupitia ushirikiano wa watu na Mungu ni kazi ambayo haitaharibika kamwe, bali hudumu zama za milele zote. Yeye amfanyaye Mungu kuwa hekima yake, ambaye hukua hata kufikia kimo kamili cha mtu katika Kristo Yesu, atasimama mbele ya wafalme, mbele ya wanaoitwa watu wakuu wa ulimwengu, na kutangaza sifa za Yeye aliyemwita kutoka gizani kuingia katika Nuru Yake ya ajabu. Sayansi na fasihi haziwezi kuleta katika akili iliyotiwa giza ya wanadamu Nuru ambayo injili takatifu ya Mwana wa Mungu inaweza kuleta. Mwana wa Mungu peke yake Ndiye anayeweza kufanya kazi kuu ya kuiangazia nafsi. Kumbe ndiyo maana Paulo alipigia kelele akisema, “Kwa maana sionei haya Injili ya Kristo; kwa kuwa ni uweza wa Mungu uletao wokovu kwa kila aaminiye.” Injili ya Kristo inakuwa utu katika hao wanaoamini, na kuwafanya barua zilizo hai, zinazojulikana na kusomwa na watu wote. Kwa njia hii chachu ya utauwa hupita katika makutano. Mawakala wa Mbinguni wana uwezo wa kutambua mambo ya Kweli ya ukuu katika tabia; kwa maana ni wema pekee ndio unaohesabika kuwa ni ufanisi pamoja na Mungu. {FEsw 199.2}

“Bila Mimi,” Kristo asema, “hamuwezi kufanya neno lo lote.” Imani yetu, kielelezo

chetu, lazima vitazamwe na kukumbatiwa kama vitu vitakatifu zaidi kuliko ilivyokuwa katika nyakati zilizopita. Neno la Mungu lazima lichunguzwe kuliko hapo kabla; kwa kuwa ni sadaka ya thamani ambayo imetupasa kutoa kwa wanadamu, ili wapate kujifunza njia ya amani, wapate ule uzima, unaopimwa na maisha ya Mungu (milele). Hekima ya mwanadamu iliyotukuka sana miongoni mwa wanadamu inazama katika kutokuwa na maana mbele ya hekima ile inayoonesha njia iliyotolewa kwa ajili ya waliokombolewa na Bwana kuitembea. Biblia pekee ndiyo inatuwezesha kutofautisha njia ya uzima na njia pana ambayo huongoza kwenye uharibifu na kifo. {FEsw 200.1}— *The Review and Herald, December 15, 1891.*

UHUSIANO WA ELIMU KATIKA KAZI YA MUNGU

“Hamsemi ninyi, bado miezi minne, ndipo yaja mavuno? Tazama, Mimi nawaambieni, Inueni macho yenu, myatazame mashamba; ya kuwa yamekwisha kuwa meupe tayari kwa mavuno. Naye avunaye hupokea mshahara, na kukusanya matunda kwa uzima wa milele, ili yeye apandaye na yeye avunaye wapate kufurahi pamoja.” {FEsw 201.1}

Kuna uhaba mkubwa wa watenda kazi waliojaliwa Roho ya kweli ya umishionari kwenda kwenye mashamba ya umishionari, walio tayari kuangaza Nuru ya Ukweli katikati ya giza la maadili la ulimwengu. Maadui wa Mungu kila siku wanapanga njama kwa ajili ya kuugandamiza Ukweli, na kuziteka Roho za watu. Wanatafuta kuiinua Sabato ya uongo, na kwa kuwaharakisha watu katika makosa, huongeza giza linaloifunika dunia, na giza kuu linalowafunika watu. Katika wakati kama huu, wale waijuao Kweli, je, watakaa bila kutenda kazi, na kuruhusu nguvu za giza kutawala? Je! Wale wanaouamini ule Ukweli wa wakati huu hawapaswi kuwa macho kabisa, huku wakikeshwa, na kufanya kazi kwa nguvu kulingana na kiwango cha imani wanayoikiri? Je, wale wanaoujua ule Ukweli wa Mungu hawatoa kila dhabihu ili kuzileta Roho kwa Kristo, ili kuitii sheria ya Mungu? Mchana umeendelea sana, usiku umekaribia, na ni muhimu kufanya kazi wakati kungali ni mchana; kwani usiku waja ambapo hakuna mtu atakayeweza kufanya kazi. Katika wakati kama huu, tunapaswa kuwa na lengo hili katika mtazamo wetu, - kutumia kila mali ambayo Mungu ametupa ambayo kwayo Kweli inaweza kupandwa ndani ya mioyo ya watu. Ni kwa kusudi hili kwamba Neno la Mungu lilitumwa kwa ulimwengu, ili liweze kutawala/kudhibiti maisha, na kubadilisha tabia. Ni wajibu wa kila mkristo kujitahidi kadiri ya uwezo Wake kuueneza ujuzi wa Kweli. Kristo aliwaagiza wanafunzi Wake kwenda katika ulimwengu wote na kuhubiri injili kwa mataifa yote. {FEsw 201.2}

Pamoja na kazi kuu mbele yetu ya kuuangaza ulimwengu, sisi ambao tunauamini Ukweli tunapaswa kuhisi umuhimu wa elimu ya kamilifu na ya kina katika aina ya vitendo vya maarifa, na hasa hitaji letu la elimu katika Kweli za Maandiko. Upotovu wa kila tabia sasa umeinuliwa kama Ukweli, na ni wajibu wetu kutafuta kwa bidii Neno takatifu, ili tupate kujua Ukweli, na kuweza kwa hekima, na akili kuuwasilisha kwa wengine. Tutaitwa kutangaza sababu za imani yetu. Itabidi tusimame mbele ya mahakimu kujibu utii wetu kwa sheria ya Mungu. Bwana ametuita tutoke ulimwenguni ili tuwe mashahidi wa Ukweli Wake; na kote katika nyadhifa zetu yote, vijana wa kiume na wa kike wanapaswa kufunzwa majukumu ya manufaa na yenye mvuto. Wana bahati ya kuwa wamishionari kwa ajili ya Mungu; lakini hawawezi kukosa uzoefu katika elimu na katika maarifa ya Neno la Mungu,

na kuitendea haki kazi hiyo takatifu ambayo wameitiwa. Katika kila nchi hitaji la elimu miongoni mwa wafanyakazi wetu linaonekana kuleta maumivu. Tunatambua kwamba elimu si lazima tu kwa utimizaji ipasavyo wa majukumu ya maisha ya nyumbani, lakini ni muhimu kwa mafanikio katika matawi yote yenye manufaa. {FEsw 202.1}

Kwa kuzingatia hitaji la elimu kwa kazi ya Mungu, na kwa ajili ya utimilifu wa mafanikio wa majukumu mbalimbali ya maisha, ni jinsi gani tunapaswa kushukuru kwamba shule iko karibu kufunguliwa huko Melbourne chini ya uongozi wa waumini wenye bidii katika Ukweli wa wakati huu. Kwa ajili ya mafanikio ya mradi huu mpya, kwa faida itakayowaleeteni ninyi na watoto wenu, hebu ndugu na dada zetu wote sasa wawe na juhudi kwa moyo wote kushirikiana na wale ambao wamekuja kuubeba mzigo wa kazi. Walimu wamekuja kwenu kutoka Amerika katika hofu na upendo wa Mungu, si bila kujitolea, ili kuwasaidia katika juhudi zenu ili kuinua kiwango cha Ukweli miongoni mwa watu. Wanatamani kuwaelimisha vijana kulielewa neno la Mungu, ili watoto wenu wapate kuwa na uwezo wa kuyafungua Maandiko kwa wengine. Sasa inabaki kwa wale ambao tayari wameangaziwa na Ukweli katika makoloni haya, kushirikiana na juhudi za ndugu zao wa Marekani, wakijua kwamba katika Kristo ubaguzi wa rangi zote, tofauti zote za kitaifa, zimewekwa kando, na sisi sote ni ndugu, tuna ojishughulisha na kazi ya kupeleka mbele ufalme wa Mkombozi. Sisi sote ni wamoja katika Kristo, na tunapaswa kuungana kwa dhati katika jitihada za kuelimisha na kufundisha jeshi la vijana wa kiume na na wa kike kwa namna ambayo watakuwa thabiti, Wakristo sawia, wenye uwezo wa kuelewa na kuyaeleza Maandiko. Usafi, imani, bidii, na uthabiti wa tabia katika wale wanaokwenda kwa ajili ya kazi ya Bwana, inapaswa kuwa dhahiri ili wengine waweze kuyaona matendo yao mema, na kuongozwa kumtukuza Baba yetu aliye Mbinguni. Kama kukiri kwetu imani kutadumishwa na uchaji wa moyo, itakuwa njia ya wema; kwayo Roho zitashawishiwa kupatana na masharti ya wokovu. Mungu anakusudia kuwa neema Yake idhihirishwe kwa anayeamini, ili kwa njia ya tabia kama ya Kristo kwa washiriki, kanisa linaweza kuwa Nuru ya ulimwengu. {FEsw 202.2}

Hebu wazazi wafanye kila linalowezekana kuwapeleka watoto wao kwenye shule ambayo itafunguliwa hivi karibuni huko Melbourne; kwani kwa njia hii, washiriki wa familia yako mwenyewe wanaweza kustahilishwa na Bwana kuwa watenda kazi katika kazi Yake. Kuna fursa nyingi kwa wamishonari katika Australia, New Zealand, na visiwa vya bahari. Na haitawezekana kujipatia au kusambaza watendakazi kutoka Amerika kujaza nafasi hizi nyingi. Watendakazi lazima waelimishwe katika maeneo haya, wanaoweza kufanya kazi, na kwenda nje kama wabeba Nuru kwenye maeneo ya giza ya nchi hizi. Sio wengi wanaoweza kwenda Amerika kupata elimu; na hata kama wangeweza kwenda, huenda isiwe bora kwao, au kwa maendeleo ya kazi. Bwana angependa kuwa na shule zilizoanzishwa katika nchi hii ili kuelimisha wafanyakazi, kutoa tabia ya kazi ya Ukweli wa sasa katika

nyanja hizi mpya, na kuamsha shauku kwa wasioamini. Angetaka muwe na kituo cha elimu katika nchi yenu, ambapo wanafunzi wenye wito wanaweza kuelimishwa katika nyanja za vitendo, na katika Kweli za Biblia, ili waweze kuwa tayari kufanya kazi katika nchi hizi, kuokoa Roho kutoka katika utumwa wa Shetani. Walimu wanaweza kuja kutoka Amerika, mpaka hapo kazi itakapokuwa imeimarika kwa hakika, na kwa njia hii ushirika huo mpya wa muungano unaweza kuundwa kati ya Amerika na Australia, New Zealand, na visiwa vya bahari. {FEsw 203.1}

Kuna vijana katika nchi hizi ambao Mungu kwa neema amewapa uwezo wa kiakili; lakini ili kufanya kazi yao bora, uwezo/nguvu zao lazima zielekezwe ipasavyo. Wanapaswa kutumia vipaji walivyopewa na Mungu kwa ajili ya kupata dhamana ya juu, kuwa watendakazi ambao hawana haja ya kuwa kutahayari (kujipatia aibu), wakiligawanya Neno la Kweli, kwa hekima kwa ajili ya wokovu. Kipaji/Karama hii inahitaji kukuzwa, na kwa kuwa shule iko karibu kuanzishwa hapa, hakika si busara kuwapeleka wanafunzi kwa gharama kubwa sana Amerika. Kazi inatakiwa kufanywa hapa. Huu ni uwanja wa umishionari, na kila mtu ambaye anafikiriwa kuwa anastahili elimu ambayo shule zetu za Marekani zinaweza kutoa, anapaswa kupata elimu hapa kwa msingi wa kazi zao za baadaye. Wale ambao wana uwezo wanaweza kufunzwa hapa ili waweze kuweka maarifa yao katika matumizi ya vitendo haraka iwezekanavyo, na kuwa mawakala katika mikono ya Bwana kwa ajili ya kueneza Nuru na ile Kweli. {FEsw 204.1}

Lakini kama hakuna majukumu haya yaliyowekwa juu yenu, kusingekuwapo na mashamba ya wamishionari kuingia, bado ingehitajika watoto wenu kupaswa kuelimishwa. Shughuli yoyote ambayo wazazi wanaweza kuifikiria yafaa kwa watoto wao, iwe walitaka wawe watengenezaji au waundaji vitu, wakulima, mafundi mafundi au makanika, au kufuata wito fulani wa kitaaluma, watapata faida kubwa kutokana na nidhamu ya elimu. Watoto wenu wanapaswa kupata fursa ya kusoma Biblia shuleni. Wanahitaji kutengenezwa kabisa juu ya sababu za imani yetu, kuyaelewa Maandiko kwa ajili yao wenyewe. Kupitia kuzielewa Kweli za Biblia, watakuwa bora zaidi kufaa kujaza nafasi za kuaminika. Wataimarika dhidi ya majaribu yatakayowakumba katika mkono wa kuume na wa kushoto. Lakini ikiwa wameelekezwa kikamilifu na kujitoa wakfu, wanaweza kuitwa, kama Danieli, kutimiza majukumu muhimu. Danieli alikuwa mtawala mwaminifu katika nyua za Babeli; kwa maana alimcha, alimpenda, na alimwamini Mungu; na wakati wa majaribu na hatari alihifadhiwa kwa uwezo wa Mungu. Tunasoma kwamba Mungu alimpa Danieli hekima, na akamjalia ufahamu. {FEsw 204.2}

Wale wanaopata maarifa ya mapenzi ya Mungu, na kuyatenda mafundisho ya Neno Lake, ataonekana kuwa mwaminifu katika nafasi yoyote ile ya kuaminiwa wanayoweza kuwekwa. Wazazi, zingatieni hili, na wekeni watoto wenu ambapo watafundishwa katika kanuni za Ukweli, ambapo kila juhudi itafanywa kuwasaidia kudumisha ucha Mungu wao, ikiwa wameongoka, au ikiwa hawajaongoka, ili

kuwashawishi kuwa watoto wa Mungu, na hivyo kuwafanya kufaa kwenda kuwavuta wengine kuja kwenye Ukweli.

Hebu wale walio na upendo wa Ukweli mioyoni mwao, wakadirie thamani ya nafsi ambayo Kristo ameifia, katika Nuru unayoakisiwa kutoka katika msalaba wa Kalvari. Kuna wengi wanaohisi kusukumwa na Roho ya Mungu ili kwenda katika shamba la mizabibu la Bwana. Wanatamani kutafuta na kuokoa kile kilichopotea. Lakini kwa sababu ya kukosa maarifa na nidhamu, hawana sifa ya kwenda katika kazi ya kuwainua na kuwaimarisha wanadamu wenzao. Wale wanaowafundisha wengine, lazima na wenyewe wafundishwe. Wanahitaji kujifunza jinsi ya kushughulika na akili za binadamu. Wanapaswa kuwa watenda kazi pamoja na Kristo, wakiboresha kila fursa ya kuwapa wanadamu ujuzi wa Mungu. Ili kuwa mawakala kwa ajili ya Mungu katika kazi ya kuinua akili za watu kutoka katika mambo ya kidunia na kimwili kuwa ya kiroho na ya kimbingu, watendakazi lazima waelimishwe na kufunzwa. Kwa wao wenyewe kuwa wanafunzi, wataweza kuelewa vizuri jinsi ya kuwafundisha wengine. Lazima wapate nidhamu ya kiakili, kwa kuzoesha na kutumia uwezo wao waliopewa na Mungu, kuleta moyo wote na akili katika kazi ya kupata maarifa. Kwa kuutazama Utukufu wa Mungu mbele yao, ni lazima waweke nguvu zao zote katika kufanya kazi, kujifunza yote wawezayo, na kuwa na akili, ili waweze kutoa maarifa kwa wengine. {FEsw 205.1}

Kuna kazi kubwa ya kufanywa katika nchi hizi; na upendo ya Kristo, na upendo kwa ajili ya Roho alizozifia, unapaswa kutusukuma kuweka kila juhudi katika uwezo wetu kutafuta na kuokoa kile kilichopotea. Hebu kila mtu na asimame kama askari mwaminifu wa Kristo mfanye kazi kwa ajili ya na pamoja na ndugu zenu, ili kazi ipate kufaulu mikononi mwenu. Hebu kila mtu aliyejiandikisha katika kazi hii inayohitajika sana akumbuke kuwa shule imeanzishwa si kwa manufaa yetu sisi tu wenyewe na watoto wetu; bali maarifa ya Ukweli yaweze kutolewa, na Roho zinazoangamia kuokolewa katika ufalme wa milele. Hebu kila mtu aishike kazi hii, akidhamiria kutoshindwa wala kuvunjika moyo, na Bwana atafanya maajabu kati yetu. Ikiwa katika wakati huu tunashindwa kufanya juhudi madhubuti za kupanua na kuiinua kazi, na kurudi nyuma kwa sababu mambo hayasimamiwi ipasavyo kulingana na mawazo yetu, Bwana hakika atatupita, na kuchagua mawakala wengine ambao wataishikilia kazi Yake katika njia Yake, na kufuata uongozi wa Roho Wake. Laiti kila mtu angefanya wajibu wake, ili ushawishi wetu uweze kuunganishwa kuiendeleza kazi ya Mungu! {FEsw 205.2}

Jicho la Mungu liko juu ya maeneo haya; kwa maana hapa angeweka Kiwango Chake na kuiinua bendera Yake. Hapa kwenye ardhi hii ya kimishionari, angeona Roho zikivutwa na kutwaliwa kwa Yesu Kristo. Angekuwa na kila anayekiri kuwa Mkristo mmishionari wa Kwenye, aliye tayari kusonga mbele katika mstari, akifanya kazi yake binafsi mahali pake, na wote wakijiunga katika jitihada zilizo katika utaratibu mzuri. Angekuwa na watu wanaosahau mawazo yao wenyewe na chuki,

ambayo kuleta tu giza na mashaka juu ya nafsi zao, na wafanye kazi kwa ajili ya hao walio tayari kuangamia. Angependa watambue kwamba hakuna mtu anaishi kwa ajili yake mwenyewe. Ni kwa kutozingatia na kuwa na juhudi zisizo za ubinafsi kwa ajili ya wengine, ndio wengi wamekuwa duni na vilema katika uzoefu wao wa kidini. Baadhi ya walio nyuma wangeweza kuwa wameendelea sana katika kumjua Mungu, kama hawangejitenga kutoka kwa ndugu zao, kujitenga na ushirika na waumini ambao hawakufanya kazi kulingana na mawazo yao finyu. Laiti, kama wazuiaji hawa wangeweza kuacha mtazamo wao wenyewe na maslahi yao wenyewe katika wokovu wa Roho, tofauti zao ndogo ndogo zingesahaulika, na utengano na ndugu zao haungeweza kuwepo. Kama wanalikuja pamoja, hawangalisema juu ya mambo ambayo kwayo wanaona upinzani, lakini wangezuia vinywa vyao kama kwa lijamu, na wangemtafuta Bwana katika maombi ya dhati ili Roho Wake Mtakatifu apate kukaa juu yao, ili wawe na mzigo kwa nafsi ambazo Kristo alizifia, wangepundua kuwa giza lao lingekimbia, na Nuru na tumaini vingekuwa katika nafsi zao. Ubinafsi ungetoweka, na wangeweza kufundishika kama watoto. Ukaidi ungeyeyuka katika kuutafakari upendo wa Mungu, na mioyo yao ingewaka, ikiguswa na kaa litokalo kwenye madhabahu. Huzuni ingefukuzwa, na furaha ichukue mahali pake; kwani upendo usio na kikomo na wema wa Mungu vingekuwa dhima ya ushuhuda wao. {FEsw 206.1}

Wale ambao watakuwa washindi lazima wavutwe kutoka kwao wenyewe; na kitu pekee kitakachokamilisha kazi hii kuu, ni kupendezwa sana na wokovu wa wengine. Hii haimaanishi kwamba unapaswa kuwaongoa watu kwa njia yako, au kuwashurutisha kuona mambo kwa mtazamo sawa na wewe; bali wewe ni kutafuta kuuwasilisha Ukweli kama ulivyo ndani ya Yesu, na kujitahidi kuwa baraka kwa wengine, nawe utapata baraka lete toka kwa Mungu. Ukweli kwamba umefanya na unafanya kitu ili kupanua mipaka ya ufalme wa Mungu katika kuokoa Roho maskini kutoka katika nira ya Shetani ya ushirikina na makosa, vitaufurahisha moyo wako, na kupanua mawazo na mipango yako. Unapotambua shauku yako na ile ya Kristo, utataka kwa ajili ya Mungu talanta yako ya uwezo, mvuto, na mali. Baadhi yenu mtaona kuwa ni fursa kwenu kuacha nyumba zenu ili muweze kufanya kazi katika visiwa vya bahari, na kuokoa Roho za watu kutoka katika utumwa wa dhambi na makosa. Mnapopata uzoefu mpya na wa kina zaidi, mtajifunza ni nini kuomba katika Roho Mtakatifu; na wale ambao walioasi kutoka kwa Mungu watarejeshwa, na kutakuwa na shauku zaidi iliyodhihirishwa kujifunza juu ya Yesu kuwa mpole na mnyenyekevu wa moyo, kuliko kubainisha makosa na mapungufu ya ndugu zenu; kwani kwa imani mnamkubali Kristo kama Mwokozi wenu binafsi. Na hamtakuja kwenye mkutano kusema mashaka na hofu zenu. Mtakuwa na -jambo bora la kuzungumzia; kwa maana mioyo yenu itakuwa mikunjufu, mkiwa nayo amani ya Kristo, ipitayo ufahamu. Huu ndio uzoefu ambao Mungu angetaka muulewe katika nchi hii. {FEsw 207.1}

Lakini ili kufikia uzoefu huu, hatua za uhakika lazima zichukuliwe. Mbinu na

mipango ambayo kwayo kazi inapaswa kufanywa lazima iendane na utaratibu wa Bwana, si kulingana na mawazo yenu binafsi, na matokeo yatakuwa ni zaidi ya kufidia gharama inayotumika. Juhudi za kimishonari zitakuwa za jumla zaidi, na mfano wa mtendakazi mmoja mwenye bidii, anayefanya kazi katika mwelekeo sahihi, utaathiri wengine, na wao pia watatoka ili kuihubiri injili. Roho ya umishonari itapita kutoka nyumba hadi nyumba, na ndugu watapata jambo la kuzungumzia lenye maslahi zaidi kuliko malalamiko yao. Watakuwa na nia ya kuonyesha vito vya Kweli vilivyomo katika Biblia, na makanisa yataanzishwa, nyumba za mikutano zitajengwa, na wengi watakuja kwa ajili ya msaada wa Bwana. Ndugu wataunganishwa katika vifungo vya upendo, na watatambua umoja wao na Wakristo wenye uzoefu katika sehemu zote za ulimwengu, kuwa wao ni wamoja katika mipango yao, wamoja katika lengo la kusudi lao. Hatua ya mapema inayochukuliwa na wale walio viongozi wa kazi itahisiwa na walio katika nchi hii na katika nchi zote, na wale walio katika nchi za kigeni nchi wataitikia juhudi zilizofanywa katika kiini cha kazi kumfuata Kiongozi wetu mkuu; na hivyo, kupitia uongoaji wa Roho kwa ajili ya Ukweli, wingi wa sifa utapanda hadi kwa Yeye aketiye juu ya kiti cha enzi. {FEsw 208.1}

Kazi ya umishonari katika Australia na New Zealand bado iko katika uchanga wake; lakini kazi hiyo hiyo lazima imalizike huko Australia, New Zealand, Afrika, India, Uchina, na visiwa vya bahari, kama ilivyomalizika katika eneo la nyumbani (Marekani). Katika ishara ifaayo ya malaika anayeruka katikati ya mbingu huwakilishwa kazi ya watu wa Mungu. Katika kazi hii nguvu za Mbinguni hushirikiana na mawakala wa kibinadamu katika kuufikisha ujumbe wa mwisho kwa wenyeji wa dunia. Lakini mipango na kazi ya wanadamu haiko sambamba na kazi ya majaliwa ya Mungu; wakati baadhi katika nchi hizi zinazodai kuuamini Ukweli hutangaza kwa mtazamo wao, "Hatutaki njia Yako, Ee Bwana, bali njia yetu wenyewe," wako wengi wanaomsihi Mungu ili wapate kuelewa ni nini Ukweli. Mahali pa siri wanalia na kuomba ili wapate Nuru katika Maandiko; na Mungu wa Mbinguni amewagiza malaika Zake kushirikiana na mawakala wa kibinadamu katika kuendeleza mpango Wake mkubwa, ili wote wanaoitamani Nuru wapate kuutazama Utukufu wa Mungu. Tunapaswa kufuata kule ambapo majaliwa ya Mungu hufungua njia; na kadri tunavyoendelea, tutaona kuwa Mbingu zimetangulia mbele yetu, zikitanua uwanja wa kazi zaidi ya uwiano wa uwezo na mali zetu ziwezavyo kutoa. Uhitaji mkubwa wa uwanja ulio wazi mbele yetu, unapaswa kuita kwa wote ambao Mungu amewakabidhi talanta za mali au uwezo, ili waweze kujitolea wao wenyewe na vyote walivyo navyo kwa Mungu. Tunapaswa kuwa kama mawakili waaminifu, si kwa mali zetu tu, bali wa neema tuliyopewa, ili Roho nyingi ziletwe chini ya bendera yenye damu ya Mfalme Immanuel. Madhumuni na miisho ya kufikiwa na wamisionari waliowekwa wakfu ni mapana sana. Uwanja kwa kazi ya umishonari haizuiliwi na tabaka au utaifa. Uwanja ni ulimwengu, na Nuru ya Ukweli inapaswa kwenda katika sehemu zote zenye giza duniani katika muda mfupi

zaidi kuliko wengi wanavyofikiri. {FEsw 208.2}

Mungu anakusudia kuweka katika kazi mawakala katika nchi yako mwenyewe kusaidia katika kazi hii kuu ya kuuangazia ulimwengu. Anakusudia kukutumia wewe na watoto wako kama askari ili kushiriki katika vita hivi vikali dhidi ya nguvu za giza, na hakika usipuuze baraka za Mungu, na kuichukulia kirahisi fursa iliyotanuliwa kwako! Angetaka mshiriki katika pambano, mkijitahidi pamoja kwa Utukufu wake, si kutafuta ukuu, si kujitahidi kujiinua kwa kuwashusha wengine thamani. Angekujalia Roho ya umishionari wa kweli, ambayo huinua, kutakasa, na kuinua chochote inachogusa, kuwafanya wasafi na wazuri na watakatifu wote wanaokuja kwa hiari chini ya mvuto wake; kwa maana kila wakala anayeshirikiana na nguvu za Mbinguni atavikwa uwezo utokao juu, na kuiwasilisha tabia ya Kristo. Roho ya umishionari hutuwezesha kuthamini kikamilifu zaidi Maneno ya maombi ya Bwana, anapotuelekeza ombeni, “Ufalme Wako uje. Mapenzi Yako yatimizwe hapa duniani kama huko Mbinguni.” Roho ya umishionari hupanua mawazo yetu, na kutuleta tuwe na umoja na wote wenye ufahamu wa kupanua mvuto wa Roho Mtakatifu. {FEsw 209.1}

Mungu angeyatawanya mawingu yaliyojikusanya katika Roho kwenye makoloni haya, na kuwaunganisha ndugu zetu wote katika Kristo Yesu. Tungefungwa katika kamba za ushirika wa Kikristo, zilizojazwa upendo kwa Roho ambazo Kristo alizifia. Kristo alisema, “Hii ndiyo amri Yangu, pendaneni, kama Mimi nilivyowapenda ninyi.” Angetaka tuwe na umoja wa moyo na mipango ya kufanya kazi kubwa tuliyopewa. Ndugu wanapaswa kusimama bega kwa bega, kuunganisha maombi yao kwenye kiti cha neema, ili waweze kuusogeza mkono wa Muweza wa yote. Mbingu na dunia ndipo zitakapounganishwa kwa karibu kazi, na kutakuwa na furaha na shangwe mbele za malaika wa Mungu, wakati kondoo waliopotea wanapopatikana na kurejeshwa. {FEsw 210.1}

Roho Mtakatifu, anayeyeyusha na kuutiisha moyo wa mwanadamu atawaongoza watu kufanya kazi za Kristo. Watatii agizo la “viuzeni mlivyo navyo, mtoe sadaka; jifanyieni mifuko isiyochakaa, akiba isiyopungua katika mbingu.” Kristo alijitoa Mwenyewe kwa ajili yetu, na wafuasi Wake wanatakiwa kujitoa wenyewe, pamoja na talanta zao za mali na uwezo wao Kwake. Nini cha zaidi Bwana amfanyie mwanadamu kuliko alivyofanya? Na sisi je, tusimpe vyote tuliyo navyo na vile tulivyo, tukifanya mazoezi ya kujitoa, na kujinyima? Ikiwa sisi ni wanafunzi wa Kristo, itafanywa dhahiri kwa ulimwengu kupitia upendo wetu kwa wale aliowafia. {FEsw 210.2}

Ilikuwa ni kwa njia ya Roho ya upendo ndipo injili ililetwa kwako, na kwa watu wote wanaomjua Mungu. Hatutakiwi tu kuwastaajabia watu ambao Mungu amewatumia, kutamani kama tungelikuwa nao hao sasa, bali kujitoa sisi wenyewe kutumiwa na Mungu kama mawakala Wake wa kibinadamu. Alikuwa ni Roho Wake ambaye aliongoza juhudi zao, na Yeye anaweza kuwapa watenda kazi wake leo

ujasiri uleule, bidii, juhudi, na kujitolea. Yesu Ndiye aliyewapa watu hawa neema, nguvu, uhodari, na ustahimilivu, Naye Yuko tayari kufanya hivyo kwa kila mtu ambaye atakuwa mmishionari wa Kweli. {FEsw 211.1}

Mungu ameanza kufanya kazi katika nchi hii, na kanisa lazima liungane na akili na nguvu za Mbinguni, kudhihirisha shughuli takatifu, na kwa kutumia uwezo wao kuwa na ufanisi zaidi kuokoa Roho na kumtukuza Mungu. Sisi ambao tumeiona Nuru ya Kweli, tunaitwa kusaidia katika maendeleo yake, kuamsha wajibu mkubwa wa kazi ya umishionari ukamilike katika mipaka yetu; na ni wajibu wa kila nafsi kushirikiana na wale ambao wangeendeleza kazi hiyo. Hebu Kila mmoja na atafute kuvuta kamba zilizo sawa pamoja na Kristo. Hebu tufiche njia zetu katika njia za Mungu, ili tofauti zote zikome, ili tabia ya Kristo iweze kuwakilishwa katika wema, uvumilivu, kujinyima, upole, unyenyekevu, na upendo. Hebu wote wajiunge kwa moyo wote kufanya kile kinachowezekana kwa uwezo wao kusaidia shule ambayo sasa itaanzishwa; kwa kuwa mikononi mwa Mungu inaweza kuwa njia ya kuwaelimisha watendakazi kuangazia Nuru ya Ukweli kwa watu. Nani atakuwa kwenye upande wa Bwana? Nani sasa ataona kazi ya kufanywa, na kuifanya?

{FEsw 211.2}— *Supplement to The Bible Echo, September 1, 1892*

Sura ya 28

HAJA YA WATENDAKAZI WALIOFUNZWA

Nimekuwa nikipendezwa sana na uzoefu wa hivi karibuni wa Mzee Daniells, ambaye, akiwa njiani kutoka Melbourne kwenda Adelaide, alisimama katika mji uitwao Nhill, ili kuwatembelea baadhi ya vijana ambao wamekuwa wakituma oda zao kwenye ofisi yetu ya *Echo* kwa ajili ya magazeti na vitabu vyetu. Alimpata hapa kijana mmoja kwa jina Hansen, Mdenmark, ambaye alipata nafasi Echo kwenye maktaba ya umma, na kuwa msomaji anayevutiwa wa magazeti. Masomo ya Ukweli yaliyowasilishwa katika safu zake ulipata nafasi katika moyo wake, na akaanza kuzungumza kwa rafiki zake hotelini alikokuwa akihudumu. Mtu huyu, Bw. Williams, pia naye akapendezwa, nao wakatuma oda za machapisho mengine, nao wakawa wanachama wa kudumu wa machapisho yetu. Mzee Daniells akawakuta watu wenye shauku ya ujuzi bora wa Ukweli. Juu ya meza ya Bw. Williams kulipatikana "Masomo juu ya Danieli na Ufunuo," na vitabu vingine kadhaa vilivyochapishwa na watu wetu. Walimwona ila mmoja tu mtu ambaye alikuwa wa imani yetu. Wakanunua kutoka kwa Mzee Daniells nakala tatu za "Hatua za Ushindi," ili kila mmoja wao awe na nakala moja na kisha nyingine wampe mhudumu. Mzee Daniells alifurahishwa na ziara yake, na kutiwa moyo na mazungumzo yake na waulizaji hawa juu ya Ukweli. {FEsw 212.1}

Watu hawa walikuwa wamejifunza Ukweli kutoka kwenye kurasa zilizochapishwa na Biblia, na walikuwa wamekubali mafundisho yote makuu ya imani (doctrines) kadiri walivyoweza kuyaelewa bila msaada wa mhubiri aliye hai. Kazi kubwa inaendelea kimya kimya kupitia usambazaji wa machapisho yetu; lakini ni kiasi gani yale yaliyo mazuri na yenye manufaa yangeweza kufanywa ikiwa baadhi ya ndugu na dada zetu kutoka Marekani wangekuja kwenye makoloni haya, kama wakulima matunda, wakulima, au wachuuzi/ wafanyabiashara, na katika kicho na upendo wa Mungu, wangetafuta kuvuta Roho kwa ajili Ukweli. Kama kuna familia kama hizo ambazo zingejiweka wakfu kwa Mungu, Angewatumia kama mawakala Wake. Watumishi/wachungaji wana nafasi zao na kazi zao, lakini kuna alama ambazo watumishi hawawezi kuwafikia, ambazo zinaweza kufikiwa na

familia zinazoweza kutembelea watu na kusesitiza juu yao Ukweli wa siku hizi za mwisho. Katika mahusiano yao ya nyumbani au ya kibiashara wanaweza kukutana na tabaka ambalo halifikiwi na watumishi au wachungaji, na wangeweza kuwafungulia hazina za Ukweli, na kuwapa ujuzi wa wokovu. Kuna machache sana yaliyofanywa katika aina hii ya kazi ya umishionari; kwa maana shamba ni kubwa, na watendakazi wengi wanaweza kufanya kazi kwa mafanikio katika aina hii ya juhudi. Ikiwa wale waliopata ujuzi wa Ukweli wangetambua umuhimu wa kusoma Maandiko kwa ajili yao wenyewe, kama wangeuhisi uzito wa wajibu uliopo juu yao, kama mawakili waaminifu wa neema ya Mungu, basi wangelipeleka Nuru kwa wengi walioketi gizani, na ni mavuno ya Roho ya namna gani yangekusanywa kwa ajili ya Bwana. Kama kila mmoja angetambua uwajibikaji wake kwa Mungu, kwa mvuto wake binafsi, asingekuwa kwa namna yoyote kuwa mzururaji, bali kuutumia uwezo wake, na kuelimisha kila uwezo ili amtumikie Yeye aliyemnunua kwa damu Yake Mwenyewe. {FEsw 212.2}

Hasa vijana, wanapaswa kuhisi kwamba lazima wafundishe akili zao, na kuchukua kila nafasi kuwa na akili, ili waweze kutoa utumishi unaokubalika kwa Yeye ambaye ametoa uhai Wake wenye thamani kwa ajili yao. Wala mtu asifanye makosa ya kujichukulia mwenyewe kuwa mwenye elimu ya kutosha kiasi cha kutokuwa na haja tena ya kujifunza vitabu au asili/uumbaji. Hebu kila mtu aboreshe kila fursa ambayo katika majaliwa ya Mungu amependelewa, kupata yote yawezekanayo katika mafunuo ya Mungu au sayansi. Tunapaswa kujifunza kuweka makadirio sahihi juu ya nguvu ambazo Mungu ametupatia. Ikiwa kijana anapaswa kuanza chini kabisa ya ngazi, hapaswi kukata tamaa, bali kudhamiria kupanda pande zote, ngazi kwa ngazi hadi atakaposikia sauti ya Kristo akisema, “Mwanangu, njoo juu zaidi. Vema mtumwa mwema na mwaminifu; umekuwa mwaminifu kwa machache, nitakuweka juu ya mengi; ingia katika furaha ya Bwana wako.” {FEsw 213.1}

Tunapaswa kulinganisha tabia zetu na kiwango kile kisichokosea cha sheria ya Mungu. Ili kufanya hivyo, ni lazima tuchunguze Maandiko, tukipima mafanikio yetu kwa Neno la Mungu. Kupitia neema ya Kristo, mafanikio ya juu zaidi katika tabia yanawezekana; kwani kila Roho/nafsi inayokuja chini ya ushawishi wa kufinyangwa wa Roho wa Mungu, inaweza kubadilishwa nia, akili na moyo. Ili kuelewa hali yako, ni muhimu kujifunza Biblia, na kukesha katika maombi. Mtume anasema, “Jijaribuni wenyewe kwamba mmekuwa katika imani; jithibitisheni wenyewe. Au hamjijui wenyewe, kwamba Yesu Kristo Yu ndani yenu? Isipokuwa mmekataliwa. Hebu wale waliopo katika ujinga wasibaki katika ujinga. Hawawezi kubaki katika ujinga, na kuifikia nia ya Mungu. Wanapaswa kutazama msalaba wa Kalvari, na kupima nafsi kwa thamani ya sadaka iliyotolewa. Yesu anasema kwa Waumini wote, “Ninyi ni mashahidi Wangu.” “Ninyi ni watenda kazi pamoja na Mungu.” Hii ikiwa ni Kweli, ni kwa jinsi gani kila mmoja anapaswa kujitahidi kutumia kila nguvu kuboresha kila fursa ya kuwa na ufanisi ili asiwe “mvivu katika kazi; mwenye bidii katika Roho;

akimtumikia Bwana.” {FEsw 214.1}

Kila talanta ambayo imetolewa kwa watu inapaswa kutumiwa ili iweze kuongezeka thamani yake, na uboreshaji wote lazima urudishwe kwa Mungu. Kama mna kasoro katika tabia, katika sauti, na katika elimu, sio lazima kila wakati kubaki katika hali hii. Lazima daima mpambane kufikia kiwango cha juu zaidi katika elimu na katika uzoefu wa kidini/kiroho, ili mpate kuwa walimu wa mambo mema. Mkiwa watumishi wa Mfalme mkuu, mnapaswa kutambua binafsi mko chini ya wajibu wa kujiboresha kwa kuchunguza, kutazama, kusoma, na kwa ushirika na Mungu. Neno la Mungu linaweza kukufanya kuwa na hekima, kukuongoza na kukufanyakamili katika Kristo. Mwokozi Mwenye heri alikuwa kielelezo kisicho na dosari kwa wafuasi Wake wote kuiga. Ni fursa kwa mtoto wa Mungu kuelewa mambo ya kiroho, kuwa na uwezo wa kusimamia kwa busara kile ambacho kimekabidhiwa katika uwajibikaji wake. Mungu hatoi njia ambayo kwayo mtu yeyote anaweza kuwa na udhuru kwa kuifanya kazi bila utaratibu; na bado kazi kubwa ya aina hii ikatolewa kwake na wale wanaofanya kazi katika kazi Yake, lakini haikubaliki Kwake. {FEsw 214.2}

Vijana wa kiume na wa kike, kama watu mlionunuliwa kwa gharama isiyo na kikomo, mmejithahidi kujionyesha kuwa mmekubaliwa na Mungu, watendakazi wasio na sababu ya kutahayari? Je, mmeleta kwa Mungu karama ya thamani ya sauti zenu, na kuweka juhudi kubwa za kusema kwa Ukweli, kwa uwazi, na kwa urahisi? Hata ikiwa namna yako ya usemi ikiwa sio kamili kiasi gani, unaweza kurekebisha makosa yako, na kukataa kuruhusu kuwa na sauti ya puani, au kuzungumza kwa kukoroma, kwa njia isiyoeleweka. Ikiwa matamshi yako ni tofauti na yanaeleweka, manufaa yako yataongezeka sana. Basi usiache tabia moja mbovu ya kuzungumza kutosahihishwa. Omba kuhusu jambo hilo, na ushirikiane na Roho Mtakatifu anayefanya kazi kwa ajili ya ukamilifu wako. Bwana, aliyemuumba mwanadamu mkamilifu hapo mwanzo, atakusaidia kukuza mwili wako na nguvu za kiakili, na ufae kubeba mizigo na majukumu katika kusudi la Mungu. {FEsw 215.1}

Kuna maelfu leoambao hawafai kwa kazi ya huduma, ambao hawawezi kuchukua nafasi ya amana takatifu, na wamepotea katika kusudi la kazi ya Mungu, kwa sababu wameshindwa kuthamini talanta walizopewa na Mungu, na hawajakuza nguvu zao za akili na mwili, ili waweze kubeba nafasi za uaminifu katika kazi ya Bwana. Mtu mmoja mmoja tuko hapa kama wale wajaribiwao, wapewao mtihani, na Bwana anataribu na kuthibitisha uaminifu wetu Kwake. {FEsw 215.2}

Angetutumia kama mawakala kuwasilisha Nuru ya Neno Lake kwa ulimwengu. Ikiwa tuliboresha Nuru tuliyopewa na Mungu kwa tukieneza kwa wengine, tutakuwa na Nuru iliyoongezeka; kwa kila “aliye na kitu atapewa, naye atakuwa na tele; bali yule asiye na kitu atanyang’anywa hata alichochacho.” Iko katika uchaguzi wetu wenyewe kuhusu kile tutakachofanya na Nuru ambayo Mungu ametupa. Tunaweza

kutembea ndani yake, au kukataa kufuata Nyayo za Kristo, na hivyo kuizima Nuru yetu. {FEsw 215.3}

Kwa kuzingatia Nuru ambayo Mungu ametoa, ni jambo la ajabu sana hakuna vijana wengi wa kiume na wa kike wanaouliza, "Bwana! unataka nifanye nini?" Ni kosa la kufisha kufikiria kwamba isipokuwa kijana ameamua kujitoa katika huduma, hakuna juhudi maalum inayohitajika ili kumfanya kufaa kwa kazi ya Mungu. Haijalishi wito wako ulioitiwa, ni muhimu kukuza uwezo wako kwa kusoma kwa bidii. Vijana wa kiume na wa kike wanapaswa kuhimizwa kuthamini fursa za baraka zilizotolewa na Mbinguni kuwa na nidhamu nzuri na werevu. Wanapaswa kuchukua fursa za shule ambazo zimeanzishwa kwa madhumuni ya kutoa maarifa bora zaidi. Ni dhambi kuwa kulemaa kwa uvivu na kusita katika kupata maarifa. Muda ni mfupi, na hivyo kwa sababu Bwana yu karibu kuja kufunga matukio ya historia ya dunia, kuna umuhimu mkubwa zaidi wa kukuza fursa zilizopo. {FEsw 216.1}

Vijana wa kiume na wa kike wanapaswa kwenda katika shule zetu, katika mkondo ambapo maarifa na nidhamu vinaweza kupatikana. Wanapaswa kuweka wakfu uwezo wao kwa Mungu, kuwa wanafunzi wa Biblia wenye bidii, ili wapate kuimarishwa dhidi ya mafundisho potovu, wala wasichukuliwe na kosa la waovu; maana ni kwa kuichunguza Biblia kwa bidii ndipo tunapata ujuzi wa ni nini iliyo Kweli. Kwa kuutumia Ukweli tunayojua tayari, Nuru iongezekayo itatuangazia kutoka katika Maandiko Matakatifu. Tunaposalimisha nia zetu katika mapenzi ya Mungu, tunaponyenyekeza mioyo yetu mbele Zake, tutatamani sana kuwa watenda kazi pamoja Naye, tukitoka kwenda kuokoa wale wanaoangamia. Wale ambao wamejiweka wakfu kwa Mungu Kweli hawataingia kazini kwa kuchochewa na nia ile ile inayowaongoza watu katika kujishughulisha na mambo ya kidunia, kwa ajili ya kujipatia riziki tu, bali wataingia kazini bila kuruhusu mazingatio ya kidunia wawadhibiti, wakitambua kwamba kazi ya Mungu ni takatifu. {FEsw 216.2}

Ulimwengu unapaswa kuonywa, na hakuna mtu anayepaswa kutulia kwa kuridhika kwa maarifa ya Ukweli wa juu juu. Huwezi kujua ni kwa majukumu gani unaweza kuitwa. Hujui ni wapi unaweza kuitwa ili kutoa ushuhuda wako wa Ukweli. Wengi watalazimika kusimama katika mahakama za kisheria; wengine watalazimika kusimama mbele ya wafalme na mbele ya wasomi wa dunia, kuitetea imani yao. Wale ambao wana ufahamu wa juu juu tu wa ukweli hawataweza kwa uwazi kufafanua Maandiko, na kutoa sababu mahususi za imani yao. Watachanganyikiwa, na hawatakuwa watendakazi wasiohitaji kutahayari. Hebu hata hebu asifikirie kuwa hana haja ya kusoma, kwa sababu hatakiwi kuhubiri katika kibweta takatifu. Hujui nini Mungu anaweza kuhitaji kwako. Ni ukweli wa kusikitisha kwamba maendeleo ya kazi yanakabiliwa na upungufu wa watendakazi wenye elimu ambao wamejiweka wenyewe katika nafasi za uaminifu. Bwana atawakubali maelfu kufanya kazi katika shamba Lake kuu la mavuno, lakini wengi wameshindwa kufaa wenyewe kwa kazi hiyo. Lakini kila mtu ambaye ameunga

mkono kazi hiyo ya Kristo, aliyejitoa nafsi yake kuwa askari katika jeshi la Bwana, anapaswa kujiweka mahali ambapo anaweza kuwa na mazoezi ya uaminifu. Dini imekuwa na maana kidogo sana kwa wale wanaodai kuwa wafuai wa Kristo; kwani sio mapenzi ya Mungu kwamba mtu ye yote abaki mjinga wakati hekima na maarifa vimewekwa katika namna ya kufikika. {FEsw 217.1}

Ni wachache kiasi gani wamestahili katika sayansi ya kuokoa Roho! Ni wachache kiasi gani wanaoelewa kazi inayopaswa kufanywa katika kulijenga kanisa, katika kuwatangazia Nuru wale wanaoketi gizani! Lakini Mungu amempa kila mtu kazi yake. Tunapaswa kufanya kazi za wokovu wetu wenyewe kwa kuogopa na kutetemeka; kwa maana Mungu Ndiye atendaye kazi ndani yetu, kunia na kutenda kwa mapenzi Yake mema. Katika kazi ya wokovu kuna ushirikiano wa wakala wa kibinadamu na wa kimbingu. Kuna mengi yamesemwa kuhusu uzembe wa juhudi za binadamu, ila Bwana hafanyi lolote kwa ajili ya wokovu wa nafsi bila ushirikiano na watendakazi wa kibinadamu. Neno la Mungu liko wazi na dhahiri juu ya hili, na bado wakati wengi wanategemea ushirikiano wetu na mawakala wa kimbingu, watu hujiendesha kana kwamba wanaweza kumudu kuweka kando madai ya Mungu, na kuacha mambo ya umuhimu wa milele kusubiri urahisi wao au pale wanapopenda. Wanatenda kana kwamba wanaweza husimamia mambo ya kiroho ili kujiridhisha wenyewe, na huweka maslahi ya umilele katika kutii mambo ya kidunia na ya kitambo. Lakini ni jinsi gani ilivyo vibaya kushughulikia hayo kwa kiburi hivyo, yaani kwa yale ambayo ni muhimu zaidi, na ya kupotea kwa urahisi zaidi. {FEsw 217.2}

Wako wapi wale ambao wangekuwa watenda kazi wenye hekima pamoja na Mungu? Mtume anasema, "Ninyi ni shamba la Mungu, ninyi ni jengo la Mungu." Lakini je, watu watamini ili waweze kuwa na uwezo chini ya shinikizo la changamoto kuingia katika nafasi fulani muhimu, wakati wanapuuza kujizoeza na kujitia adabu kwa kazi hiyo? Je, Watafikiri kwamba wanaweza kuwa vyombo vilivyong'arishwa mikononi ya Mungu kwa ajili ya wokovu wa Roho ambazo Kristo alizifia, huku wao wakipuuza kutumia fursa zilizowekwa upande wao wapate kufaa kwa ajili ya kazi? "Kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama, bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa Roho. Kwa sababu hiyo twaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kushindana siku ya uovu, na mkiisha kuyatimiza yote kusimama." Kila mmoja anahitaji kuendeleza fursa na uwezo wake aliopewa na Mungu, ili kila mmoja wetu awe , mtenda kazi pamoja Mungu. {FEsw 218.1}

Mungu anaendelea kufanya kazi kwa ajili yetu ili tuweze kutoka kuwa nyuma kuhusiana na karama. Ametupa nguvu zetu za kimwili, kiakili, na kimaadili, na tukizikuza jinsi tunavyopaswa, tutaweza kukutana na nguvu za giza na kuzishinda. Yesu amebainisha njia ya uzima, ameidhihirisha Nuru ya Kweli, amemtoa Roho Mtakatifu, na kutujalia kwa wingi kila kitu cha muhimu kwa ukamilifu wetu. Lakini

faida hizi hazithaminiwi, na tunapuuzia mapendeleo na fursa zetu, na kushindwa kushirikiana na mawakala wa kimbingu, na hivyo kushindwa kuwa watendakazi bora, werevu, na wenye akili kwa ajili ya Mungu. Wale ambao njia yao wenyewe inaonekana kuwa ya kuvutia zaidi kuliko njia ya Bwana, hawawezi kutumika katika utumishi Wake kwani wangewakilisha vibaya tabia ya Kristo, na kuongoza Roho za watu mbali na huduma inayokubalika kwa Mungu. {FEsw 218.2}

Wale wanaofanya kazi kwa Bwana lazima wawe na nidhamu nzuri, ili waweze kusimama kama walinzi waaminifu. Lazima wawe wanaume na wanawake ambao watatekeleza mipango ya Mungu kwa ukuzaji wa hekima akili za wale wanaokuja chini ya mvuto wao. Lazima waungane na mawakala wote wanaotaka kutimiza mapenzi ya Mungu katika kuuokoa ulimwengu uliopotea. Kristo amejitoa Mwenyewe, Yeye Mwenye haki kwa ajili ya wasio haki, amekufa juu ya msalaba wa Kalvari, na amekabidhi kwa mawakala wa kibinadamu kazi ya kukamilisha kipimo kikubwa cha upendo unaokoa; kwa maana mwanadamu hushirikiana na Mungu katika juhudi zake za kuokoa wanaoangamia. Katika majukumu yaliyopuuzwa ya kanisa tunatazama kuchelewesha utimilifu wa kusudi la Mungu; lakini ikiwa watu wakashindwa kukamilisha kazi yao, ingekuwa bora kama wasingezaliwa. Uovu mkubwa utafuata kwa kupuuzia kushirikiana na Mungu; kwani uzima wa milele utapotea. Mafanikio yetu kama watahiniwa wa Mbinguni yatapatikana kutegemea bidii yetu katika kutimiza masharti ambayo kwayo uzima wa milele umetolewa. Tunapaswa kupokea na kutii Neno la Mungu, hatuwezi kuwa goigoi, na kuelea kwa mkumbo. Ni lazima tuwe na wanafunzi wenye wa Neno la Mungu. Ni lazima tujizoeze na kujielimisha kama askari wazuri wa Kristo. Ni lazima tuiendeleze kazi, kuwa watendakazi pamoja na Mungu. {FEsw 219.1}— *The Review and Herald, February 14, 1893.*

Sura ya 29

KWA WALIMU NA WANAFUNZI

Kwa Walimu na Wanafunzi katika Chuo chetu cha Battle Creek, na katika Taasisi Zetu Zote za Elimu.

Katika majira ya usiku ujumbe ulitolewa kwangu kuwapa ninyi wa Battle Creek, na kwenye shule zetu zote. Wakati ni maelekezo ya Mungu kwamba nguvu za kimwili zifunzwe kama zilivyo za akili, bado mazoezi ya kimwili yanapaswa kuwa katika upatanifu kamili sambamba na mafundisho yaliyotolewa na Yesu Kristo kwa wanafunzi Wake. Kile kinachotolewa kwa ulimwengu kinapaswa kuonekana katika maisha ya Wakristo, ili katika elimu ya shule zetu na katika kujizoeza na kujifunza kwa kibinafsi akili za Mbinguni (Malaika) zisije zikarekodi katika vitabu kwamba wanafunzi na walimu ni wale ambao “wanapenda anasa kuliko kumpenda Mungu.” Hii ndio kumbukumbu inayowekwa kwa wengi sasa hivi. “Wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu.” Hivyo Shetani na malaika zake huweka mitego yao iliyojificha kwa ajili ya nafsi zenu, naye hufanya kazi kwa namna fulani juu ya walimu na wanafunzi kuwashawishi kushiriki katika mazoezi na burudani ambazo huwafyonza ubongo sana, lakini ambazo zina tabia kuimarisha nguvu za tamaa za chini, na kujenga uchu na tamaa ambazo zitaongoza, na kuzuia zaidi kwa hakika utendaji na kazi ya Roho Mtakatifu wa Mungu juu ya moyo wa mwanadamu. {FEsw 220.1}

Roho Mtakatifu anawaambia ninyi nini? Nguvu yake ilikuwa ni ipi na mvuto wake juu ya mioyo yenu wakati wa Mkutano Kuu wa Konferensi kuu, na Mikutano mikuu katika majimbo mengine? Je, mmechukua umakini maalum ninyi wenyewe? Je,

walimu mashuleni waliona kwamba lazima wawe na umakini? Ikiwa Mungu amewateua kuwa waelimishaji wa vijana, wao pia ni “waangalizi wa kundi.” Hawako katika kazi ya shule kuvumbua mipango ya mazoezi na michezo ya kuelimisha wapiganaji masumbwi hodari; hawako hapo kushusha chini vitu vitakatifu kwa kiwango sawa na mambo ya kawaida. {FEsw 220.2}

Nilikuwa nikizungumza na walimu katika jumbe za maonyo. Walimu wote wanahitaji mazoezi, mabadiliko ya utumishi. Mungu ameelekeza kuwa hii inapaswa kuwa ya manufaa, kazi ya vitendo; lakini mmegeuka kando na mpango wa Mungu, kufuata uvumbuzi wa wanadamu, na hivyo kuharibu maisha ya kiroho. Sio yodi wala nukta ya ushawishi wa baadaye, wa elimu ya namna hiyo utawasaidia mbeleni katika kukabiliana na mapambano makali ya siku hizi za mwisho. Walimu na wanafunzi wetu ni elimu ya aina gani wanayoipokea? Je, Mungu amebuni na kupanga aina hii ya shughuli/zoezi kwa ajili yenu, au ni imeletwa na uvumbuzi wa kibinadamu na mawazo ya kibinadamu? Akili imeandaliwa vipi kwa kufikiri na kutafakari, na fikra za umakini, na maombi ya dhati, ya toba, yanayotoka katika mioyo iliyotiishwa na Roho Mtakatifu wa Mungu? “Kama ilivyokuwa siku za Nuhu, ndivyo itakavyokuwa pia katika siku za Mwana wa Adamu.” “Bwana akaona ya kuwa maovu ya mwanadamu ni makubwa duniani, na kwamba kila kusudi analowaza moyoni mwake ni baya tu sikuzote.” {FEsw 220.3}

Bwana alifungua mbele yangu ulazima wa kuanzisha shule huko Battle Creek ambayo haipaswi kufuata namna ya shule yoyote iliyopo. Tulipaswa kuwa na walimu ambao wangeweka Roho zao katika upendo na kumcha Mungu. Walimu walipaswa kujielimisha katika mambo ya kiroho, ili kuwatayarisha watu kusimama katika dhiki inayotaribu mbele yetu; lakini kumekuwa na ukiukwaji wa mpango wa Mungu kwa namna nyingi. Burudani zimefanya zaidi kuipinga kazi ya Roho Mtakatifu kuliko chochote kingine, na Bwana amehuzunishwa. {FEsw 221.1}

“Jiosheni, jitakaseni; ondoeni uovu wa matendo yenu usiwe mbele za macho Yangu; acheni kutenda mabaya [lakini msitulia hapa; songeni mbele katika kuifuata Nuru ya ulimwengu]; jifunzeni kutenda mema; takeni hukumu na haki, wasaidieni walioonewa, mpatieni yatima haki yake, mteteeni mjane. Haya njoni, tusemezane, asema BWANA; Dhambi zenu zijapokuwa nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kama theluji; zijapokuwa nyekundu kama bendera, zitakuwa kama sufu.” Hapa kuna eneo lako ambapo ni pa kutumia akili yako na kukupa mabadiliko ya mazoezi. “Kama mkikubali na kutii mtakula mema ya nchi.” {FEsw 221.2}

Mji huu uliokuwa mwaminifu umekuwaje kahaba! Yeye aliyejaa hukumu ya haki; haki ilikaa ndani yake; bali sasa wauaji. fedha yako imekuwa takataka, divai yako imechanganywa na maji; Wakuu wako ni waasi; na rafiki za wevi; kila mtu hupenda rushwa, hufuata malipo, Hawampatii yatima haki yake, wala maneno ya mjane hayawawasilii.” {FEsw 222.1}

“Enyi wa nyumba ya Israeli, njoni, twende katika Nuru ya Bwana.” “Mwacheni mwanadamu ambaye pumzi yake i katika mianzi ya pua yake; kwa maana hudhaniwaje kuwa ni kitu?” “Msiwatumainie wakuu, wala binadamu ambaye hakuna wokovu kwake. Pumzi yake hutoka, hukurudia udongo wake; siku hiyo mawazo yake yapotea. Heri ambaye Mungu wa Yakobo ni msaada wake, na tumaini lake ni kwa Bwana, Mungu wake.” “Enyi watu Wangu, wakuongozao wakukosesha, waiharibu njia ya mapito yako.” {FEsw 222.2}

Nimepata woga kwa ajili ya Battle Creek. Walimu ni wakali kabisa katika kuwafikia na kuwashutumu na kuwaadhibu wale wanafunzi ambao huzikiuka sheria ndogo, wala sio kwa kusudi lolote baya, bali kwa kutojali; au changamoto zinazotokea ambazo haiifanyi kuwa dhambi kwao kukiuka sheria ambazo zimetengenezwa, na ambazo hazipaswi kushikiliwa kwa kutobadilika ikiwa zimekiukwa, na bado mtu mwenye kosa hilo dogo anatendewa kana kwamba amefanya dhambi ya kutisha. Sasa nataka mzingatie, walimu, mliposimama, nanyi jishughulikieni na kutamka hukumu dhidi yenu wenyewe; kwani hamjakiuka sheria tu, bali pia mmekuwa wakali sana, wakali sana kwa wanafunzi; na zaidi ya hili, kuna mgogoro kati yenu na Mungu. Hamjafanya njia zenu kuwa nyoofu katika miguu yenu, vilema wasije wakageuka njia. Mmetoka kwenye njia salama. Nasema “walimu”; mimi sijataja jina la mtu. Ninaacha hilo katika dhamiri zenu wenyewe kulielewa. Bwana, Mungu wa Israeli, ametenda kati yenu tena na tena. Mmekuwa na udhihirisho mkubwa wa nyayo za Aliye Mkuu. Lakini kipindi cha Nuru kuu, cha ufunuo wa ajabu wa Roho na uweza wa Mungu, ndicho kipindi cha hatari kubwa, ili Nuru isije ikatumiwa. Je, mtazingatia [Yeremia 17:5-10; 18:12-15](#)? Kwa kuwa hakika mtakuja chini ya maonyo ya Mungu. Nuru imekuwa ikimulika katika miale iliyo angavu na thabiti juu yenu. Nuru hii imefanya nini kwenu? Kristo, Mchungaji Mkuu, anatazama kwa uchungu na kuchukizwa, na kuuliza, Liko wapi lile kundi lako dogo ulilopewa, kundi lile nzuri? “Kwa hiyo nakutaka uikumbuke siku hii ya leo, kwamba mimi ni safi na damu ya watu wote. Kwa kuwa sikujizuia kuwatangazia ninyi mashauri yote ya Mungu. Chukueni tahadhari basi kwa ajili yenu wenyewe, na kwa kundi lote, ambalo Roho Wake Mtakatifu amewaweka ninyi kuwa waangalizi Wake, mpate kulilisha kanisa la Mungu, ambalo Amelinunua kwa damu Yake Mwenyewe.” “Lichungeni (lilisheni) kundi la Mungu lililo kwenu na kulisimamia, si kwa kulazimishwa; bali kwa hiari kama Mungu atakavyo; si kwa Kutaka fedha ya aibu, bali kwa nia na moyo.” {FEsw 222.3}

Wale walimu ambao hawana uzoefu wa endelevu wa kidini/kiroho, ambao hawajifunzi masomo ya kila siku katika shule ya Kristo, ili waweze kuwa vielelezo kwa kundi, bali wanakubali ujira wao kama ndiyo kiini au jambo kuu, hawafai kwa nafasi makini na takatifu waliyonayo. Kwa maana andiko hili linafaa kwa shule zetu zote zilizoanzishwa kama Mungu alivyopanga zipasavyo kuwa, kufuata utaratibu au mfano wa shule za manabii, zikitoa daraja la juu la maarifa— zisizochanganya taka na chuma cha fedha baada ya kutakaswa, na divai na maji, ambavyo huwakilisha

kanuni za thamani. Fikra za uwongo na mazoea yasiyofaa yanatia chachu yaliyo safi, na kuharibu yale yapasayo daima kutunzwa kwa usafi, na kutazamwa na ulimwengu, na malaika, na wanadamu, kama taasisi ya Bwana—shule ambapo elimu ya kumpenda na kumcha Mungu inafanywa kuwa kwa kwanza (nambari moja). “Na uzima wa milele ndio huu, wakujue Wewe, Mungu wa pekee wa Kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma.” “Wala si kama wajifanyao mabwana juu ya urithi wa Mungu, bali wa kujifanya vielelezo kwa lile kundi.” {FEsw 223.1}

Hebu walimu wanaodai kuwa Wakristo wajifunze kila siku ndani shule ya Kristo masomo Yake. “Jitieni nira Yangu, mjifunze Kwangu; kwa kuwa Mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo, nanyi mtapata raha nafsi mwenu.” Niwauliza, Je, kila mwalimu shuleni anaivaa nira ya Kristo, au hutengeneza nira zake mwenyewe ili kuziweka juu ya shingo za wengine, nira ambazo wao wenyewe hawatazivaa, zenye ncha kali ;zinazoumiza, na hili, pia, huku wanajibeba kilegevu sana kwenda kwa Mungu, wakijikosesha kila siku kwa mambo madogo na makubwa, na kuweka iwe dhahiri kwa maneno, katika Roho, na katika matendo, kwamba wao si mfano sahihi kwa wanafunzi, na hawana uelewa kwamba wako chini ya nidhamu ya Mwalimu mkuu zaidi ambaye ulimwengu umewahi kumjua? Kuna haja ya kuwa na namna ya juu zaidi, takatifu zaidi shuleni huko Battle Creek, na kwenye shule zingine ambazo zimechukua namna yao kutoka kwake. Mila na desturi za shule ya Battle Creek husambaa kwenye makanisa yote, na mapigo ya moyo ya shule hiyo yanaonekana katika kundi zima la waumini. {FEsw 223.2}

Si utaratibu wa Mungu kwamba maelfu ya dola zitatumika katika upanuzi na kuongezewa katika taasisi ya Battle Creek. Kuna mengi miundo mbiu mingi sana hapo sasa. Chukueni mali hizo za ziada na kuanzisha kazi katika sehemu zinazoteseka za maeneo mengine, ili kuweka tabia katika kazi. Nimesema Neno la Mungu juu ya jambo hili. Kuna hoja wengi hawazioni, ambazo sina uhuru wa kuziweka wazi mbele yenu sasa; lakini nawaambieni kwa Jina la Bwana, mtafanya kosa katika kuongeza jengo juu ya jengo; kwani hurundikana katika Battle Creek majukumu ambayo kwa pamoja ni mengi sana katika eneo moja. Kama majukumu haya yangepiganywa na kuwekwa katika maeneo mengine, itakuwa bora zaidi kuliko kusongamana sana katika Battle Creek, huyaibia meneno mengine yenye uhitaji wa faida za Mungu ambazo wangenufaika nazo. {FEsw 224.1}

Kuna mabwana wakubwa wengi sana mashuleni wanaopenda kuutawala urithi wa Mungu. Kuna machache sana ya Kristo na mengi sana ya nafsi. Lakini wale walio chini ya uongozi wa Roho wa Mungu, walio chini ya utawala wa Kristo ni vielelezo kwa kundi; na wakati Mchungaji Mkuu atakapotokea, watapokea taji ya Utukufu isiyoharibika. {FEsw 224.2}

“Vivyo hivyo ninyi vijana, watiini wazee. Naam, ninyi nyote jifungeni unyenyekevu; mpate kuhudumiana, kwa sababu Mungu huwapinga wenye kiburi, lakini huwapa wanyenyekevu neema. Basi nyenyekeeni chini ya mkono wa Mungu ulio hodari, ili

awakweze kwa wakati Wake.” Kujiinua kwenu kote kuna matokeo ya asili, na huwafanya kuwa na tabia ambayo Mungu haitathibitisha. “Bila Mimi,” asema Kristo, “hamuwezi kufanya neno lo lote.” Fanya Kazi na fundisha, fanya kazi katika mistari ya Kristo, na ndipo hamtafanya kazi kwa uwezo wenu dhaifu, ila mtakuwa na ushirikiano na Uungu, pamoja na uwezo wa kibinadamu aliopewa na Mungu. “Huku mkimtwika Yeye fadhaa zenu zote, kwa maana hujishughulisha sana kwa mambo yenu. Mwe na kiasi, na kukesha” (sio kwa kucheza mpira wa miguu na kwa kujielimisha katika mambo ya michezo isiyofaa ambayo inaweza kumfanya kila Mkristo kuona soni usoni/haya) “Mwe na kiasi, na kukesha; kwa kuwa mshitaki wenu Ibilisi, kama simba angurumaye, huzunguka-zunguka, akitafuta mtu ammeze.” Ndio, yuko kando ya michezo yenu akitazama burudani zenu, akikamata kila nafsi ambayo haina ulinzi dhidi yake, akipanda mbegu zake katika akili za mwanadamu, na kudhibiti akili za mwanadamu. Kwa ajili ya Kristo sitisheni katika Chuo cha Battle Creek, na fikirini matokeo ya baadaye ndani ya moyo na tabia na kanuni, ya hizi burudani zilizoigwa kwa kufuata mtindo wa shule zingine. Mmekuwa mkiendelea kwa kasi katika njia za Mataifa, na sio kufuata mfano wa Yesu Kristo. Shetani yuko kwenye mazingira ya shule; yupo katika kila shughuli katika chumba shuleni. Wanafunzi ambao wamekuwa na akili za kusioniwa sana katika michezo yao, hawako katika hali bora ya kupokea mafundisho, mashauri, makaripio, ya zaidi muhimu kwao katika maisha haya na kwa maisha ya umilele yajayo. {FEsw 225.1}

Maandiko yanasema hivi kuhusu Danieli na wenzake: “Basi kwa habari za hao vijana wanne, Mungu aliwapa maarifa na ujuzi katika elimu na hekima; Danieli naye alikuwa na ufahamu katika maono yote na ndoto.” Je, ni kwa namna gani mnajiweka wenyewe kushirikiana na Mungu? “Mkaribieni Mungu, Naye atawakaribia ninyi.” “Mpingeni shetani, naye atawakimbia.” Hebu lishe ijifunzwe kwa uangalifu; siyo yenye afya. Vyakula kadhaa vidogo vidogo vilivyotengenezwa kwa vitu vitamu baada ya mlo (kitindamlo-kekink) ambavyo vina madhara badala ya kusaidia na afya, na kutoka katika Nuru niliyopewa, lazima kuwe na mabadiliko ya makusudi katika maandalizi ya chakula. Kunapaswa kuwa na mpishi mwenye ujuzi kamili, ambaye atatoa ugavi wa chakula cha kutosha kwa wanafunzi wenye njaa. Elimu katika mstari wa aina hii kuhusu vile vitu vilivyoandaliwa mezani, sio sahihi, sio yenye afya, au sio ya kuridhisha, na matengenezo yaliyoazimiwa ni muhimu. Wanafunzi hawa ni urithi wa Mungu, na kanuni bora na zenye afya zinapaswa kuletwa katika shule ya bweni kuhusu lishe. Vyakula laini, vya supu/michuzi na vyakula vya majimaji, au matumizi huru ya nyama, sio bora sana katika kujenga misuli yenye afya, katika viungo vya mmeng’enywa wa chakula, au akili nzuri. Tazama jinsi tunavyojifunza, kwa taratibu mno! Na katika taasisi zetu zote duniani shule ni muhimu zaidi! Hapa swala la lishe ni la kujifunza; sio uchu au ulafi wa mtu, au ladha, au dhana au hoja inayopaswa kufuatwa; bali kuna haja ya matengenezo makubwa; kwani madhara ya maisha yote hakika yatakuwa matokeo ya namna ya sasa ya kupika. Katika nafasi zote muhimu katika chuo hicho, ya kwanza ni ya yule

aliyeajiriwa kuelekeza na kuongoza katika utayarishaji wa vitu vya kuwekwa mbele ya wanafunzi wenye njaa; kwa maana kazi hii ikipuuzwa, akili haitakuwa tayari kufanya kazi yake, kwa sababu tumbo limetendewa isivyofaa na hivyo haliwezi kufanya kazi yake ipasavyo. Akili zenye nguvu zinahitajika. Akili ya mwanadamu lazima ipate kupanuka na kuwa na nguvu na utimamu wenye makini sana na kushughulishwa. Ni lazima itumikishwe kwa kufanya kazi ngumu, au itakuwa dhaifu na isiyofaa. Nguvu ya ubongo inahitajika kufikiri kwa bidii na unyofu zaidi; ni lazima iwe kweli kutumika kutatua changamoto ngumu na kuzishinda, vinginevyo akili itapungua nguvu na uwezo wa kufikiri. Akili lazima ibuni, ifanye ugunduzi, ifanye kazi, na kushindana au kuwa na mieleka, ili kutoa ugumu na nguvu kwa akili; na ikiwa viungo vya mwili haviwekwi katika hali ya afya zaidi kwa chakula cha kutosha na chenye lishe, ubongo hautapata sehemu yake ya lishe ili kufanya kazi. Danieli alifahamu jambo hili, akajipatia chakula rahisi, kisicho na viungo, sahili, chenye lishe bora, na kukataa anasa za meza ya Mfalme (luxury foods). Vyakula vitamu vya kitindamlo (desserts kama keki, maandazi nk) ambavyo huchukua muda mwingi kuandaa, vingi, vina madhara kwa afya. Vyakula vikavu na vigumu vinavyohitaji kutafunwa vitakuwa bora zaidi kuliko vya kuchemsha, laini au vyakula vya majimaji. Ninakita hapa kwa kuonyesha kuwa ni jambo muhimu. Nitatuma onyo langu kwenye Chuo cha Battle Creek, kutoka hapo kwenda kwenye taasisi zetu zote za elimu. Jifunzeni juu ya masomo haya, na muwaruhusu wanafunzi kupata elimu sahihi katika maandalizi ya vyakula vya afya, visivyokobolewa wala kusindika, vyenye ladha, vikavu, vyakula vinavyoimarisha mfumo. Hawana sasa, na hawakupata katika siku za nyuma, aina sahihi ya mafunzo na elimu juu ya chakula chenye afya zaidi cha kutengeneza mishipa yenye afya na misuli, na kutoa ustawi katika ubongo na nguvu za neva. {FEsw 225.2}

Akili inapaswa kuwekwa sawa kabisa kwa kazi mpya, ya bidii, na kazi hiyo ifanywe kwa moyo wote. Hili linapaswa kufanywaje? Nguvu ya Roho Mtakatifu ni lazima itakase mawazo na kuisafisha Roho kwa kutoka kwenye unajisi wake wa maadili. Tabia za unajisi sio tu kwamba zinainajisi nafsi, bali zinainajisi akili. Kumbukumbu huumizwa, ikiwekwa kwenye madhabahu ya mazoea mabaya, yenye kuumiza. “Maana yeye apandaye kwa mwili wake, katika mwili wake atavuna uharibifu; bali yeye apandaye kwa Roho, katika Roho atavuna uzima wa milele.” Wakati walimu na wanafunzi watakapoweka wakfu nafsi, mwili na Roho kwa Mungu, na kutakasa mawazo yao kwa kutii sheria za Mungu, wataendelea kupokea majaliwa mapya ya nguvu za kimwili na kiakili. Ndipo kutakuwa na shauku ya moyo kumtafuta Mungu, na maombi ya dhati kwa ajili ya utambuzi thabiti wa kupambanua. Ofisi na kazi ya Roho Mtakatifu si kwa ajili ya wao kumtumia, kama wengi wanavyofikiri, bali kwa ajili ya Roho Mtakatifu kutumia, kufinyanga, kutengeneza, na kutakasa kila nguvu. Utoaji wa akili kwa mazoea ya tamaa za mwili huvuruga ubongo na mishipa ya fahamu, na ingawa wanadai kuwa na dini, kwa sasa na kamwe hawatakuwa mawakala ambao Mungu anaweza kuwatumia; kwani

Yeye huyadharau mazoea ya uchafu, ambayo huharibu nguvu muhimu za neva (mishipa ya ya fahamu). Dhambi hii ya uchafu hupunguza nguvu za kimwili na uwezo wa kiakili, ili kila kitu kama utumikishwaji wa akili baada ya muda mfupi iwe ya kukera. Kumbukumbu inafaa; na, tazama ni dhabihu ya kuchukiza jinsi gani huwasilishwa kwa Mungu! {FEsw 227.1}

Ndipo ninapotazama matukio yaliyoonyeshwa mbele yangu; ninapozingatia shule zilizoanzishwa katika sehemu tofauti, na kuziona zikianguka chini sana ya shule za manabii, ninahuzunika kupita kawaida. Zoezi la kimwili liliwekewa alama na Mungu wa hekima. Masaa kadhaa kila siku yanapaswa kutolewa kwa elimu muhimu katika aina ya kazi ambayo itasaidia wanafunzi katika kujifunza majukumu ya maisha ya vitendo, ambayo ni muhimu kwa vijana wetu wote. Lakini hili limekataliwa, na burudani zimeanzishwa, ambazo hutoa mazoezi tu, bila kuwa na baraka yoyote maalum katika kufanya matendo mema na ya haki, ambayo ni elimu na mafunzo muhimu. {FEsw 228.1}

Wanafunzi, kila mmoja, anahitaji elimu ya kina zaidi ya majukumu ya vitendo. Muda unaotumika katika mazoezi ya mwili, ambayo, hatua kwa hatua, huongoza katika kupita kiasi, kwa kiwango katika michezo na matumizi ya akili, yapasa kutumika katika namna ya Kristo, na baraka za Mungu zikae juu yao kwa kufanya hivyo. Wote wanapaswa kutoka shuleni wakiwa na ufanisi kielimu, ili wakati watakapoachwa katika rasilimali zao wenyewe, wawe na maarifa wanayoweza kuyatumia ambayo ni muhimu kwa maisha ya vitendo. Kutafuta kwa wingi katika uvumbuzi kwa kutumia uwezo aliopewa na Mungu kwa kutofanya chochote kizuri, hakuna unachoweza kwenda nacho katika maisha yajayo, hakuna kumbukumbu ya matendo mema, ya matendo ya rehema, yaliyoandikwa katika kitabu cha Mbinguni, — “Amepimwa katika mizani na kuonekana amepungua.” {FEsw 228.2}

Kujifunza kwa bidii ni muhimu, na kufanya kazi kwa bidii. Kucheza sio muhimu. Ushawishi umekuwa ukiongezeka miongoni mwa wanafunzi **katika masomo kujitoa kwa burudani, kwa nguvu za kuvutia, ya uchawi**, kwa mivuto inayopinga ile Kweli juu ya akili ya mwanadamu na tabia. Akili iliyosawazishwa vizuri haipatikani kwa kutoa nguvu za kimwili kwenye burudani. Kazi ya kimwili inayojumuisha kuitumikisha akili kwa manufaa, ni nidhamu katika maisha ya vitendo, yakipendezeshwa kila wakati kwa kutafakari yale yanayostahili na kuelimisha akili na mwili kufaa kufanya kazi ya Mungu aliyoibuni watu kuifanya katika namna mbalimbali. Vijana wakamilifu zaidi huelewa jinsi ya kutekeleza majukumu ya maisha ya vitendo, nia makini zaidi na afya njema zaidi siku baada ya siku vitakuwa shangwe yao katika kutumiwa kwa ajili ya wengine. {FEsw 228.}

Wanachoweza kufanya kwa ajili ya Yesu ni kuwa na bidii, kuwa na shauku inayowaka kuonyesha shukrani zao kwa Mungu katika utekelezaji wa bidii zaidi wa kila wajibu uliowekwa juu yao, ili, kwa uaminifu wao kwa Mungu, wanaweza kuwa na mwitikio kwa ile zawadi kuu na ya ajabu ya Mungu Mwana pekee wa Mungu, ili

kwa imani katika Yeye wasije wakapotea, bali wawe na uzima wa milele. {FEsw 230.1}

Kuna haja ya kila mmoja katika kila shule na katika kila taasisi, kuwa, kama alivyokuwa Danieli, katika uhusiano wa karibu sana na Chanzo cha hekima yote, ili maombi yake yamwezeshe kufika kiwango cha juu zaidi cha majukumu yake katika kila eneo, ili aweze kutimiza mahitaji yake ya kielimu sio tu chini ya walimu wenye uwezo, bali pia chini ya usimamizi wa mawakala wa Mbinguni, akijua kwamba Yeye Aonaye yote, Jicho lisiloweza kusinzia liko juu yake. Upendo na hofu ya Mungu vilikuwa mbele ya Danieli, naye alielimisha na kuzoeza nguvu zake zote kuitikia kadiri inavyowezekana kwa ule utunzaji wenye upendo wa Mwalimu Mkuu, kufahamu juu ya wema wake kwa Mungu. Vijana wanne wa Kiebrania hawangeruhusu nia za ubinafsi na kupenda burudani kuchukua nyakati za thamani za maisha haya. Walifanya kazi kwa moyo wa kupenda na akili iliyo tayari. Hiki si kiwango cha juu kuliko kila Mkristo anavyoweza kufikia. Mungu anataka kwa kila mwanazuoni Mkristo zaidi ya alivyopewa. Ninyi ni “tamasha kwa dunia, na kwa malaika, na kwa wanadamu.” {FEsw 230.2}— *Special Testimonies on Education, Oktoba, 1893.*

Sura ya 30

ELIMU BORA NA MADHUMUNI YAKE

Elimu bora inayoweza kutolewa kwa watoto na vijana ni ile ambayo ina uhusiano wa karibu zaidi na wakati ujao, yaani uzima wa milele. Aina hii ya elimu inapaswa kutolewa na wazazi wacha Mungu, na walimu waliojitoa, na kanisa, ili kwamba vijana nao wapate kuwa wamishonari wenye bidii kwa ajili ya maeneo ya nyumbani au ya ugenini. Wanapaswa kufundishwa kwa bidii katika kweli za Biblia, ili waweza kuwa nguzo katika kanisa, mabingwa na hodari wa ile Kweli, wenye mizizi na msingi katika imani. Wanapaswa kujua wanachokiamini na kuwa na uzoefu wa namna hiyo katika mambo ya kimbingu kiasi kwamba hawatakuwa wasaliti wa amana takatifu. {FEsw 231.1}

Vijana wanapaswa kuelimishwa kwa kanuni na vielelezo kwamba ni mawakala wa Mungu, wajumbe wa rehema, walio tayari kwa kila Neno na kazi njema, ili wawe baraka kwa wale walio tayari kuangamia. Tuko katika uhitaji mkubwa wa uwezo wa elimu, na vipaji viliyokabidhiwa kwa vijana wetu vinapaswa kuwekwa wakfu kwa utumishi wa Mungu, na kutumika katika kazi Yake. Kunapaswa kuwepo na wanaume na wanawake ambao wana sifa za kufanya kazi makanisani na kuwafundisha vijana wetu kwa kazi mistari maalum ya kazi, ili Roho ziletwe

kumwona Yesu. Shule zilizoanzishwa nasi zinapaswa kuzingatia lengo hili, na siyo kwa utaratibu wa shule za madhehebu zilizoanzishwa na makanisa mengine, au kulingana na utaratibu wa seminari na vyuo vya kidunia. Zinapaswa kuwa za hali ya juu kabisa, ambapo hakuna aina ya ukafiri utakuwepo, au kukubaliwa. Wanafunzi wanatakiwa waelimishwe katika Ukristo wa vitendo, na Biblia lazima izingatiwe kama kitabu cha juu zaidi, na muhimu zaidi. {FEsw 231.2}

Kuna hitaji kubwa katika sehemu zote za ulimwengu la walimu wa Kikristo na kwa wamisionari wa tiba. Katika sehemu zote za kazi zote mbili ndani na nje ya nchi, kuna milango wazi kwa wale wanaoweza kufanya mema kwa mwili na Roho, wakionesha Nuru ya thamani ya Ukweli. Upuuziaji wa awali katika mwelekeo huu lazima usiendelezwe. Nuru kubwa inaangaza kwenye njia yetu kuliko katika njia za wengine, na bado maendeleo yetu katika ana hili yamekuwa mbali kabisa kinyume na Nuru tuliyonayo. Wengi wa vijana wetu wa kiume na wa kike wa kutumainiwa zaidi wametoa uwezo wao bora zaidi kwenye madhabahu ya sanamu, na wamejitoea wenyewe kama dhabihu kwa mkuu wa uovu. Laiti kama vijana katika shule zetu, mmoja na wote, wamejitoea kwa jitihada za thamani za Roho wa Bwana, wapate kujua ishara za majaliwa Yake na wamngojee Mungu ili wapate kumjua na kutenda mapenzi Yake! Kwa njia hii wangemfungulia Yesu mlango wa moyo. {FEsw 231.3}

Katika kujitoea kwetu kwa Mungu, tunavuna faida kubwa; kwa maana ikiwa tuna udhaifu wa tabia, kama sote tulivyo, tunaungana wenyewe na Yeye aliye na uwezo wa kuokoa. Ujinga wetu utaunganishwa na hekima isiyo na kikomo, udhaifu wetu na uwezo udumuo, na, kama Yakobo, kila mmoja wetu anakuwa mtawala pamoja na Mungu. Kwa kuunganishwa na Bwana, Mungu wa Israeli, tutakuwa na nguvu kutoka juu ambayo itatuwezesha kuwa washindi; na kwa ugawaji wa upendo wa kimbingu, tutapata kuifikia mioyo ya wanadamu. Tutakuwa tumejizatiti kwa mikono yetu inayotetemeka juu ya kiti cha enzi cha Yule Asiye na mwisho, na tutasema, "Sikuachi usiponibariki." Uhakika umetolewa kuwa atatubariki na kutufanya kuwa mbaraka; na hii ndiyo Nuru yetu, furaha yetu, na ushindi wetu. Vijana watakapoelewa ni nini ulio upendeleo na upendo wa Mungu moyoni, wataanza kutambua thamani ya upendeleo wao wa kununuliwa kwa damu, na wataweka wakfu uwezo wao kwa Mungu, na kujitahidi kwa nguvu zote walizopewa na Mungu kukuza talanta zao kuzitumia katika utumishi wa Bwana. {FEsw 232.1}

Usalama pekee kwa vijana wetu katika zama hizi za dhambi na uhalifu ni kuwa na uhusiano hai na Mungu. Lazima wajifunze jinsi ya kumtafuta Mungu, ili wajazwe na Roho Wake Mtakatifu, na kutenda kana kwamba wanaotambua kwamba jeshi lote la Mbinguni linawatazama kwa shauku njema, tayari kuwahudumia katika hatari na wakati wa mahitaji. Vijana wanapaswa kuzuiwa kwa maonyo na mafundisho dhidi ya majaribu. Wanapaswa kufundishwa ni mambo gani ya kutia moyo ambayo yapo kwenye Neno la Mungu kwa ajili yao. Wanapaswa kuwekewa mbele yao hatari ya kuchukua hatua kwenye njia za uovu. Hebu na waelimishwe

kuwa na kicho kwa historia na mashauri ambayo Mungu ametoa katika Maneno Yake matakatifu. Wanapaswa kuelekezwa hivyo kwa wazi ili waweke azimio lao dhidi ya uovu, na kuamua kwamba hawataingia katika njia yoyote ambayo hawatatarajia Yesu kuandamana na wao, na baraka zake kukaa juu yao. Wanapaswa kufundishwa dini ya vitendo, dini ya maisha ya kila siku ambayo itawatakasa katika kila uhusiano wa maisha, katika nyumba zao, katika biashara, na kanisani, na katika jamii. Lazima wawe na elimu kiasi kwamba watatambua kuwa ni jambo la hatari kuchezea fursa zao, bali kwamba Mungu anawatarajia kwa uchaji na kwa bidii kutafuta baraka zake kila siku. Baraka ya Mungu ni zawadi ya thamani, na zinapaswa kuhesabiwa kuwa za thamani ambayo hazitasalimishwa kwa gharama yoyote. Baraka ya Mungu hutajirisha, nayo haongezi huzuni. {FEsw 232.2}

Moyo wangu umesukwasukwa sana ninaposoma habari za matumizi mabaya ya uwezo mkuu katika utumishi wa Shetani. Katika idara za serikali, katika nafasi za uwajibikaji wa juu, katika dhamana rasmi, watu hujaribiwa na yule mwovu; na rushwa na uhalifu, ubadhirifu, ujambazi, na unyang'anyi huwa ndio matokeo. Kuna mashimo mabaya ya ufisadi, yanayomwaga juu ya ulimwengu wetu mivuto ya sumu inayoharibu jamii. Kila mahali Shetani ametega mitego yake ili apate kuwamata watu wa walio na elimu, wenye karama nzuri za asili, watu walio uwezo wa kuwa watenda kazi pamoja na Mungu, washirika wa malaika, wenyeji wa Mbinguni, ili apate kuwafunga kwenye gari lake kama watumwa wake. Japo Yesu amewakomboa kutoka katika utumwa wa adui, na wanakataa kuwa huru, na hawatakuwa wana wa Mungu, warithi wa Mungu, warithio pamoja na Yesu Kristo urithi wa milele. Wanaishi kana kwamba dunia, pesa, cheo, nyumba, na ardhi vilikuwa ndilo kusudi kuu la kuumbwa kwao. Kupitia rehema za Mungu maisha yao yanarefushwa; lakini je, hili si jambo la kusikitisha kuona watu wenye uwezo wa juu wakiishi kwenye hali ya chini sana? {FEsw 233.1}

Fidia imelipwa, na inawezekana kwa wote kuja kwa Mungu, na kupitia maisha ya utii ili kuufikia uzima wa milele. Basi ni huzuni iliyoje kwamba watu wanageuka kutoka katika urithi usio na kikomo, na kuishi kwa ajili ya kujitosheleza kiburi, kwa ubinafsi na kujionyesha, na kwa kujitiisha chini ya utawala wa Shetani, wanapoteza mbaraka ambao wanaweza kuwa nao katika maisha haya na yajayo. Wanaweza kuingia katika majumba ya Mbinguni, na kushirikiana kwa masharti ya uhuru na usawa na Kristo na malaika wa Mbinguni, na wakuu wa Mungu; na bado, cha kushangaza, kama inavyoweza kuonekana, wao wanageuka kutoka katika vivutio vya Mbinguni. Muumba wa ulimwengu wote anapendekeza kuwapenda wale ambao huamini katika Mwanawe wa pekee kama Mwokozi wao binafsi, kama yeye Alivyompenda Mwanawe. Hata hapa na sasa neema Yake inatolewa juu yetu kwa kiwango hiki cha ajabu. Amewapa wanadamu karama ya Nuru na Mkuu wa mbingu, na pamoja Naye amejawajalia hazina zote za Mbinguni. Kama vile alivyotuahidi kwa ajili ya uzima ujao, Yeye pia hutukabidhi karama za kifalme katika maisha haya, na

kama raia wa neema Yake, angetaka tufurahie kila kitu kitakachokuza, kitakachopanua, na kuinua tabia zetu ili kuwa bora zaidi. Ni mpango Wake kutufanya kufaa kwa ajili ya nyua za Mbinguni juu. {FEsw 234.1}

Lakini Shetani anapigania Roho za watu, na kutupa kivuli chake cha jehanamu katika njia yao, ili wasione Nuru. Hawaruhusu wapate taswira ya heshima ya siku zijazo, Utukufu wa milele, uliowekwa kwa ajili ya hao watakaokaa Mbinguni, au kuwa na ladha ya uzoefu ambao unatoa ladha ya mbele ya furaha ya Mbinguni. Lakini kwa vivutio vya Mbinguni vilivyowekwa mbele ya akili kuivuvia tumaini, kuamsha nia, kuchochea juhudi, jinsi gani tunaweza kugeuka kutoka katika matumaini, na kuchagua dhambi na ujira wake, ambao ni kifo? {FEsw 234.2}

Wale wanaomkubali Kristo kama Mwokozi wao wanayo ahadi ya Mungu ya maisha ya sasa na yale yajayo. Wakala wa kibinadamu hadaiwi sehemu ya uwezo wake wa kumtumikia Shetani; bali utii wake wote ni kwa sababu ya Mungu asiye na mwisho na wa milele. Mwanafunzi wa chini kabisa wa Kristo anaweza kuwa mkazi wa Mbinguni, mrithi wa Mungu wa urithi usioharibika, na usiokoma. Laiti kama kila mtu angeweza kufanya uchaguzi wa zawadi ya Mbinguni, kuwa mrithi wa Mungu wa urithi huo ambao jina lake ni salama kutoka kwa mharibifu yeyote, ulimwengu usio na mwisho! Tazama! Usiuchague ulmwengu, bali chagua urithi ulio bora! Songa mbele, himiza njia yako kuelekea alama kwa ajili ya thawabu ya mwito wako mkuu katika Kristo Yesu. Kwa ajili ya Kristo, hebu lengo la elimu yako liundwe kwa vivutio vya ulimwengu ulio bora zaidi. {FEsw 234.3} — *The Review and Herald, November 21, 1893.*

Sura ya 31

KRISTO KAMA MWALIMU.

Kwa kusudi Lake lenye hekima Bwana hufunua zile Kweli za mifano, alama na ishara. Kupitia matumizi ya tamathali za semi makaripio ya wazi yalitolewa kwa washitaki na maadui Zake, na hawakuweza kupata katika Maneno Yake nafasi ya kumhukumu. Yeye, Katika mafumbo na malinganisho aliipata njia bora ya kuwasilisha Ukweli wa kimbingu. Kwa lugha rahisi, kwa kutumia mifano, alama na vielelezo vilivyotolewa kutoka katika ulimwengu wa asili, Aliufunua Ukweli wa kiroho kwa wasikilizaji Wake, na kutoa maelezo kwa kanuni za thamani ambazo zingepita kando ya akili zao, na wala hakuacha alama yoyote, aliunganisha maneno Yake na matukio ya kisisimua ya maisha, uzoefu, au asili. Kwa njia hii aliipata mapenzi yao manyofu, naye akaamsha uchunguzi, na Alipokwisha kuupata usikivu wao kikamilifu, aliwavuta kwa makusudi katika shuhuda za kweli. Kwa njia hii

aliweza kutengeneza msukumo wa kutosha juu ya moyo ili kwamba baadaye wasikilizaji Wake wangeweza kutazama jambo ambalo aliunganisha somo Lake nalo, na kukumbuka Maneno ya Mwalimu wa kimbingu. {FEsw 236.1}

Mafundisho ya Yesu yalikuwa ya mpangilio tofauti kabisa na yale ya waandishi wenye elimu. Walijidai kuwa wafafanuaaji wa sheria, zote mbili, zilizoandikwa na za jadi. Lakini sauti rasmi ya maagizo yao ingeonyesha kwamba hawakuona chochote katika mafundisho matakatiifu Maneno ambayo yalikuwa na nguvu muhimu. Hawakuwasilisha chochote kipya, hawakusema maneno yaliyofikia hitaji hali la nafsi. Hawakutoa chakula cha kondoo na wana-kondoo wenye njaa. Kawaida yao ilikuwa kukaa juu ya mistari inayotatanisha, migumu, isiyo na isiyo na umuhimu zaidi ya sheria, na matokeo ya mawazo yao yalikuwa maneno ya kipuuzi, ambayo wasomi wala watu wa kawaida hawakuweza kuyafahamu na kuyaelewa. {FEsw 236.2}

Kristo alikuja kuifunua ile Kweli ya kimbingu/Bwana kwa ulimwengu. Alifundisha kama Mwenye mamlaka. Alizungumza namna mbavyo mwanadamu hajapata kunena. Kwake hakukuwa na kusitasita, wala kivuli cha mashaka katika matamshi Yake. Alizungumza kama mtu aliyeelewa kila sehemu ya somo Lake. Angeweza kufungua siri ambazo wazee wa kale na manabii walikuwa na matamanio kuona, ambazo udadisi wa mwanadamu umekuwa ukitamani sana kuzifahamu. Lakini wakati watu hawakuweza kutambua zile Kweli rahisi zaidi, Kweli zilizosemwa wazi, wangewezaje kuelewa siri ambazo zilifichwa kutoka katika macho ya mwanadamu wenye ukomo? Yesu hakudharau kurudia zile Kweli za zamani, Ukweli unaojulikana; kwa maana Yeye Ndiye aliyekuwa mwanzilishi wa Kweli hizi. Alikuwa Ndiye Utukufu wa hekalu. Kweli ambazo zilikuwa zimepotea machoni, ambazo zilikuwa zimepotoshwa, zilizokuwa zimetafsiriwa vibaya, na kutengwa kutoka katika nafasi yake safi, alizitenga na ushirika wa upotovu; na akiwaonyesha kama vito vya thamani katika mng'ao wake, aliziweka upya katika mpangilio wake ufao, na akaziamuru zisimame imara milele. Ilikuwa kazi ya namna gani hii! Ilikuwa ya namna ambayo hapana mwanadamu mwenye kikomo angeweza kuielewa au kuifanya. Mkono wa Mungu pekee ndio ungeweza kuuchukua Ukweli ambao, kutokana na kuhusiana kwake na upotovu, ulikuwa unatumika kwa kusudi la adui wa Mungu na wa mwanadamu, na kuuweka mahali ambapo ungeweza kumukuza Mungu, na kuwa wokovu wa wanadamu. Kazi ya Kristo ilikuwa kutoa tena kwa ulimwengu Ukweli katika upya wake wa asili na uzuri. Aliyawakilisha mambo ya kiroho na ya Mbinguni, kwa vitu ya asili na uzoefu. Aliipa nafsi yenye njaa mana safi, aliwasilisha ufalme mpya ambao ungesimamishwa kati ya wanadamu. {FEsw 236.1}

Marabi wa Kiyahudi waliwasilisha matakwa ya sheria kama kuvaa duru ya ushuru. Walifanya vile Shetani anavyofanya katika siku zetu, —kuiwasilisha sheria mbele ya watu kama amri baridi, sheria na tamaduni ngumu. Ushirikina uliizika Nuru, Utukufu, heshima, na madai ya milele ya sheria ya Mungu. Walijidai kusema

na watu mahali pa Mungu. Baada ya kosa la Adamu, Bwana hakuzungumza tena moja kwa moja na mtu; jamii ya wanadamu ilitolewa mikononi mwa Kristo, na mawasiliano yote yalikuja kwa ulimwengu kupitia Yeye. Ilikuwa ni Kristo ambaye aliinena torati katika mlima Sinai, na alijua mzigo wake wote wa maagizo, Utukufu na ukuu wa sheria ya Mbinguni. Katika mahubiri Yake mlimani, Kristo aliifafanua sheria, na kutafuta kuweka ndani mawazo ya wasikilizaji Wake madai ya milele ya maagizo ya Yehova. Maagizo Yake yalikuja kama ufunuo mpya kwa watu; na waalimu wa sheria, na waandishi na Mafarisayo, na hali kadhalika watu wa kawaida, walishangazwa na mafundisho Yake. Maneno ya Kristo hayakuwa mapya, na bado yalitoka na nguvu ya ufunuo; kwani aliuwasilisha Ukweli katika Nuru yake ifaayo, na sio katika Nuru ambayo walimu walikuwa wameiweka mbele ya watu. Hakuonesha kuzingatia mapokeo na amri za wanadamu, bali akawaonyesha macho ya akili zao kutazama mambo ya ajabu kutoka ndani ya sheria ya Mungu, ambayo ni msingi wa kiti Chake cha enzi kutoka mwanzo wa ulimwengu; na kadri mbingu na nchi zidumupo, katika enzi zisizokoma za milele, Sheria itakuwa kiwango kikuu cha uadilifu, utakatifu na cha haki na wema. {FEsw 237.1}

Mfumo wa Kiyahudi ulikuwa injili kwa/katika vielelezo, uwasilishaji wa awali wa Ukristo ambao ulipaswa kuendelezwa kwa haraka kadri akili za watu ambavyo zingeweza kufahamu Nuru ya kiroho. Shetani daima hutafuta kuuficha Ukweli ulio wazi, na Kristo hutafuta kila wakati kufungua akili kufahamu kila Ukweli muhimu unaohusu wokovu wa mwanadamu aliyeanguka. Hadi leo bado kuna vipengele vya Ukweli ambavyo vinaonekana kwa uhafifu sana, miunganiko isiyoeleweka, na mambo ya ndani kabisa ya sheria ya Mungu ambayo hayajaeleweka. Kuna upana usiopimika, utakatifu, na Utukufu katika sheria ya Mungu; na bado ulimwengu wa kidini umeiweka kando sheria hii, kama walivyofanya Wayahudi kuyatukuza mapokeo na maagizo ya wanadamu. Kabla ya siku za Kristo, wanadamu waliuliza, "Kweli ni nini?" Giza liliifunika nchi, na giza kuu kwa watu. Hata Yudea ilifunikwa na giza, ingawa sauti ya Mungu ilinena nao katika Maneno Yake. Ukweli wa Mungu ulikuwa umenyamazishwa na ushirikina na mapokeo ya wale wanaojiita wafasiri wake, na ugomvi, wivu, na chuki na ikawagawanya wale wanaodai kuwa wana wa Mungu. Ndipo kukawa na Mwalimu alitumwa kutoka kwa Mungu, Yeye aliyekuwa Njia, Kweli, na Uzima. Yesu aliwasilisha Ukweli ulio safi, na utajiri wa Mbinguni ili kuangaza katikati giza la kimaadili na utusitusi wa dunia. Mungu akasema, "Na iwe Nuru ya Rohoni," na Nuru ya Utukufu wa Mungu ikafunuliwa katika uso wa Yesu Kristo. {FEsw 238.1}

Kristo alidhihirishwa kama Mwokozi wa wanadamu. Watu hawakupaswa kutegemea matendo yao wenyewe, haki yao wenyewe, au kwao wenyewe kwa vyovyote vile, bali katika Mwana-Kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi za ulimwengu. Ndani Yake Mtetezi na Baba alifunuliwa. Kupitia Kwake mwaliko ulitolewa, "Njooi, na tusemezane, asema Bwana; dhambi zenu zijapokuwa nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kama theluji; zijapokuwa nyekundu kama bendera,

zitakuwa nyeupe kama sufu.” Mwaliko huu unakuja na kutoa sauti kwetu leo. Tusiruhusu kiburi, au kujiinua, au kujiona kuwa mwadilifu kumweka mtu yeyote asiungame dhambi zake, ili apate kudai ahadi: “Yeye afichaye dhambi zake hatafanikiwa; bali yeye aziungamaye na kuziacha atapata rehema.” Usimzuilie au kumficha Mungu chochote, na msiache kuungama makosa yenu mbele ya ndugu yanapokuwa yanakuwa na uhusiano nao. “Ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi, na kuombeana, mpate kuponywa.” Dhambi nyingi zimesalia bila kuungamwa, nazo zitakabiliwa katika siku ya hukumu; ni bora kabisa kuziona dhambi zenu sasa, na kuziungama, na kuziweka mbali, wakati ile Dhabihu ya upatanisho inasihi kwa niaba yako. Usichukie kujifunza mapenzi ya Mungu juu ya somo hili. Afya ya nafsi yako, umoja wako na ndugu, unaweza kutegemea mwenendo unaofuata katika mambo haya. Basi, nyenyekeeni chini ya mkono wa Mungu ulio hodari, Naye atawakweza kwa wakati Wake, “huku mkimtwika Yeye fadhaa zenu zote; kwa maana Yeye hujishughulisha sana kwa mambo yenu.” {FEsw 239.1}

Ni Ukweli wa kusikitisha kwamba moyo unaokosea hautaki kukosolewa, au kujinyenyekeza/kujidhili kwa kuziungama dhambi. Wengine huona makosa yao, lakini hufikiri kwamba kuungama kutapunguza hadhi au cheo chao, wanapuuzia makosa yao, na wanajikinga na nidhamu ambayo maungamo yangeipa nafsi. Wazo la upotovu wao ulio wazi utabaki kuwa wa kuumiza furaha zao na kuabisha mienendo yao; kwani kwa kupita kando ya njia ya maungamo, wanashindwa kuwa vielelezo aminifu kwa watu. Wanaona makosa ya wengine; lakini wanawezaje kuwa na ujasiri wa kutoa ushauri, “Ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi, na kuombeana, ili mpate kuponywa,” wakati wameshindwa kufuata agizo hili katika maisha yao wenyewe? Watumishi au watu watajifunzaje Ukweli ambao wanauweka kando, na kuusahau ikiwezekana, kwa sababu haupendezi kwao na; kwa sababu hausifii kiburi chao kwa udanganyifu, bali hukemea na kutoa maumivu kwao? Wachungaji na watu, ikiwa wataokolewa hata kidogo, lazima waokolewe siku kwa siku siku, saa kwa saa. Ni lazima wawe na njaa na kiu ya haki ya Kristo, Nuru ya Roho Mtakatifu. Washiriki wa kanisa, - wale waliowekwa katika vyeo vya uaminifu, –lazima wabatizwe kwa Roho wa Mungu, ama sivyo hawatastahiki nyadhifa wanazozikubali.

{FEsw 239.2}

Mtu anaweza kuwa na maarifa ya Maandiko ambayo hayamfanyi mwenye hekima hata apate wokovu, ingawa aweza kushinda wapinzani wake katika mabishano (debate) ya hadharani. Ikiwa hana shauku nafsini kumtafuta Mungu; ikiwa hatachunguza moyo wake mwenyewe kama mshumaa uliowashwa, akiogopa kwamba ubaya wowote unaweza kukaa hapo; ikiwa hana shauku ya kujibu maombi ya Kristo, kwa wanafunzi wawe kitu kimoja kama Yeye alivyo mmoja na Baba, ili ulimwengu uweze kuamini kwamba Yesu Ndiye Kristo, –anajidanganya bure nwenyewe kuwa yeye ni Mkristo. Ujuzi wake, ulianza kwa matamanio ya ukuu, unabebwa kwa kiburi; lakini nafsi yake imepungukiwa upole na upendo wa Kristo. Yeye si mtu mwenye hekima machoni pa Mungu. Anaweza kuwa na busara ya

kumshinda mpinzani; lakini kuwa mwenye hekima hadi wokovu, lazima ategemee wakala wa Mtakatifu Roho. Na “tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi.” Hakuna talanta, ufasaha, wala kujifunza Maandiko kwa ubinafsi, kutakoleta upendo kwa Mungu au kufanana na sura ya Kristo. Hakuna ila uwezo wa kimbingu ndio unaoweza kutengeneza upya moyo na tabia ya mwanadamu, na kuijaza nafsi kwa upendo wa Kristo, ambao utajidhihirisha katika upendo kwa wale ambao aliwafia. {FEsw 240.1} – *The Review and Herald, November 28, 1893.*

Sura ya 32

ELIMU MUHIMU SANA KWA WATENDA KAZI WA INJILI

Kuna watendakazi Wa Kikristo ambao hawajapata elimu ya chuo kwa sababu haikuwezekana wao kuyapata manufaa haya; lakini Mungu ametoa ushahidi kwamba amewachagua. Amewaagiza waende na kufanya kazi katika shamba Lake la mizabibu. Amewafanya kuwa watenda kazi pamoja na Yeye Mwenyewe. Wana Roho ya kufundishika; wanahisi tegemeo lao kwa Mungu, na Roho Mtakatifu Yuko pamoja nao kusaidia udhaifu wao. Atahuisha na kutia nguvu akili, atawelekeza mawazo yao, na kuwasaidia katika uwasilishaji wa Ukweli. Mtendakazi anaposimama mbele ya watu kuyashikilia maneno ya uzima, kunasikika katika

sauti yake mwangwi wa sauti ya Kristo. {FEsw 242.1}

Ni dhahiri kwamba anatembea na Mungu; kwamba amekuwa na Yesu na kujifunza kutoka Kwake. Ameleta Ukweli ndani ya Patakatifu pa nafsi; kwake ni uhalisi ulio hai, na anawasilisha Ukweli ndani yake kwa udhihirisho wa Roho na wa nguvu. Watu huisikia sauti ya shangwe. Mungu huzungumza na mioyo yao kupitia mtu aliyewekwa wakfu kwa utumishi Wake. Mtenda kazi anapomwinua Yesu kwa njia ya Roho, yeye huwa na ufasaha wa kweli. Ni mwaminifu na mkweli, na hupendwa na wale anaowafanyia kazi. {FEsw 242.2}

Ni dhambi iliyoje itakayomkalia mtu yeyote ambaye angesikiliza mwanadamu wa kama huyu na kumkosoa tu, kutafuta makosa ya sarufi mbaya, au unyambulishaji wa matamshi usio sahihi, na kushikilia makosa haya hadi kumdhihaki. Mafarisayo walimdhihaki Kristo; walikosoa usahili wa lugha Yake, ambao ulikuwa wazi kiasi kwamba mtoto, mzee, na watu wa kawaida walimsikia kwa furaha, na walivutiwa na Maneno Yake. Masadukayo pia walimdhihaki kwa sababu mazungumzo Yake yalikuwa tofauti kabisa na maneno ya watawala na waandishi wao. Walimu hao wa Kiyahudi walizungumza kwa sauti ya isiyopendeza, isiyo na mkazo, na inayofanana wakati wote {inaboeshia, monotony}, na maandiko yaliyo wazi na ya thamani zaidi yalifanywa kutovutia na yasiyoeleweka, yaliyozikwa chini ya tamaduni nyingi sana na hadithi walizojifunza ambazo zilisemwa na marabi, watu walipungukiwa zaidi na ujuzi wa Maandiko baada ya kuwasikiliza. Kulikuwa na Roho nyingi zenye njaa kwa ajili ya Mkate wa Uzima, na Yesu aliwalisha kwa Ukweli safi na rahisi. Katika mafundisho Yake alichukua mifano kutoka kwa vitu vya asili/uumbaji na shughuli za kawaida za maisha, na ambazo walikuwa wanazifahamu. Hivyo Ukweli ukawa uhalisia ulio hai; matukio ya asili na mambo ya maisha ya kila siku yalikuwa milele yakirudia kwao mafundisho ya thamani ya Mwokozi. Tabia ya Kristo ya Ufundishaji ilikuwa ni kile anachotaka watumishi Wake wakifuate. {FEsw 242.3}

Mzungumzaji ambaye hana elimu kamili anaweza wakati mwingine kuanguka katika makosa ya sarufi au matamshi; anaweza asitumie maneno fasaha zaidi au taswira nzuri zaidi, lakini ikiwa yeye mwenyewe amekula Mkate wa Uzima; ikiwa amekunywa Chemchemi ya Uzima, anaweza kulisha Roho zenye njaa; anaweza kutoa Maji ya Uzima kwake yeye aliye na kiu. Kasoro zake zitasamehewa na kusahaulika. Wasikilizaji wake hawatachoka wala kuchukizwa, bali watamshukuru Mungu kwa ujumbe wa neema uliowafikia kupitia mtumishi Wake. {FEsw 243.1}

Ikiwa mtenndakazi amejijweka wakfu kikamilifu kwa Mungu na ana bidii katika maombi ya nguvu na hekima ya Mbinguni, neema ya Kristo itakuwa mwalimu wake, naye atashinda mapungufu makubwa na kuwa mwenye akili zaidi na zaidi katika mambo ya Mungu. Lakini hebu mtu yeyote asichukue haki kutoka katika hili kuwa mvivu, kupoteza wakati na fursa, na kupuuza mafunzo ambayo ni muhimu kwake ili kuwa na ufanisi. Bwana hafurahishwi hata kidogo na wale walio na fursa za kupata maarifa lakini wanaojiteteta kwa kupuuza kuendeleza fursa zote ambazo Ameweka

ndani ya uwezo wao ili wapate kuwa watendakazi wenye akili, waliohitimu vyema ambao hataaibishwa nao. {FEsw 243.2}

Zaidi ya watu wengine wote duniani, mtu ambaye akili yake imeangazwa kwa kufunuliwa kwa Neno la Mungu katika ufahamu wake, atahisi kwamba lazima ajitoe kwa bidii zaidi katika kusoma Neno la Mungu, na kusoma kwa bidii sayansi, kwani tumaini na wito wake ni mkuu kuliko mwingine wowote. Kadri mwanadamu anavyokuwa karibu na Chanzo cha maarifa na hekima yote, ndivyo anavyoweza kufaidika zaidi kiakili na kiroho kupitia uhusiano wake na Mungu. Ujuzi wa Mungu ni elimu muhimu, na maarifa haya kila mtendakazi wa kweli atafanya juhudi daima kujifunza ili kuyapata. {FEsw 243.3}—*Christian Education, 143 1893.*

Sura ya 33

WANAFUNZI KUAMUA HATIMA YAO YA MILELE

Hebu wanafunzi wakumbuke kwamba ili kuunda tabia itakayosimama katika hukumu, ni jambo kubwa sana. Ninyi wenyewe mnawajibika kwa aina ya tabia mnazozijenga. Hakuna proFEswa katika taasisi ya elimu anayeweza kutengeneza tabia yako. Ninyi wenyewe mnaamua hatima yenu ya milele. Inahitajika kutafakari tabia ambazo zinastahili kuigwa. Tunakuelekeza kwa Yusufu akiwa Misri, na kwa Danieli huko Babeli. Vijana hawa walijaribiwa na wakathibitishwa; na kwa sababu walisimama kidete juu ya kanuni, wakawa watu wawakilishi, na vielelezo vya

uadilifu. Napenda kusema kwa vijana katika taasisi zetu za elimu, iwe mnadai kuamini au la, kwamba sasa mko katika kipindi cha rehema, na rehema ya pili gaitakuwepo kwa hata mmoja wenu. Hii ndiyo fursa pekee mtakayokuwa nayo ya kuhimili jarib na kumthibitisha Mungu. {FEsw 245.1}

Kwa shauku kubwa zaidi malaika wa Mungu katika nyua za Mbinguni wanaangalia maendeleo ya tabia; na kutoka katika kumbukumbu za vitabu vya Mbinguni, matendo yanapimwa, na thamani ya maadili hupimwa. Kila siku kumbukumbu ya maisha yako inapitishwa mbele za Mungu, kama ilivyo, iwe ni njema au mbaya. Unapungukiwa katika uchaji na wema wa nafsi, na hakuna mtu anayeweza kukupa tabia unayohitaji. Njia pekee unayoweza kufikia kiwango cha thamani ya maadili ambayo kwayo utapimwa, ni kumtegemea Kristo, na kushirikiana Naye kwa uthabiti, kwa bidii, na kwa nia thabiti. {FEsw 245.2}

Wale wanaofanya hivi hawatakuwa katika kazi zao na Roho ya wepesi, ya upuuzi, na ya kupenda anasa. Watazingatia kwamba si kwa gharama ndogo kwa wazazi wao au kwao wenyewe, wamekuja shuleni ili kupata maarifa bora ya sayansi, na kupata ufahamu mpana zaidi wa Agano la Kale na Agano Jipya. Ngingezungumza nanyi kama wenye akili timamu, na ambao mna ufahamu wenye akili wa fursa na na wajibu wenu. Je! haitakuwa bora kwenu kushirikiana na walimu, ili mpate kufikia kiwango cha juu sana ambacho inawezekana ninyi kukifikia? Muda ni wa thamani zaidi kwenu kuliko dhahabu, na mnapaswa kuutumia kila muda wa thamani. Mnapaswa kufikiria ni upi ya tuakuwa mvuto wenu kwa wengine. Ikiwa mwanafunzi mmoja ni mzembe, na kujiingiza katika kupenda kulikopindukia juu ya anasa, anapaswa ajiweke chini ya udhibiti wa kanuni, asije akawa a wakala wa kufanya kazi ya Shetani, kupinga, kwa ushawishi wake mbaya, kazi ambayo walimu wanajaribu kuifanya, na kuharibu yale ambayo wakala wa kimbangu hutafuta kuyatimiza kupitia mawakala wa kibinadamu. Anaweza kuharibu mpango wa Mungu, na kushindwa kumkubali Kristo na kuwa kweli mwana wa Mungu. {FEsw 245.3}

Wajibu kati ya walimu na wanafunzi ni wa pande zote. Walimu wanapaswa kufanya juhudi kwa bidii ili nafsi zao wenyewe zipate kutakaswa kwa neema ya Kristo, na wafanye kazi katika njia ya Kristo kwa ajili ya wokovu wa wanafunzi wao. Kwa upande mwingine, wanafunzi hawapaswi kufuata njia ambayo itafanya iwe vigumu na kujaribu kwa walimu wao, na kuleta juu yao majaribu magumu kupinga. Wanafunzi hawapaswi, kwa mwenendo mbaya, kususha kiwango cha msimamo wa juu na sifa ya shule, na kutoa sababu ya habari hiyo kwenda nje kati ya waumini na wasioamini, kwamba shu le za Waadventista wa Sabato, ingawa zinadaiwa kuanzishwa kwa ajili ya kutoa elimu bora kwa wale wanaohudhuria, si bora kuliko shule za kawaida duniani kote. Hii siyo tabia wala sifa ambayo Mungu angetaka shule zetu kuzibeba; na wale ambao wametoa mvuto ambao Mungu amewakabidhi, kwa kutoa tabia au sifa kama hizo shuleni, wametoa katika mwelekeo mbaya. Wale

ambao wameonyesha kutoheshimu sheria, na ambao wametaka kuharibu mamlaka, hata kama ni waumini au makafiri wameandikwa katika Vitabu vya Mbinguni kuwa ni wale ambao hawawezi kuaminiwa kama washirika wa familia ya kifalme, watoto wa Mfalme wa Mbinguni. Walimu wanaobeba mzigo wa kazi ile wanayopaswa, watakuwa na wajibu, uangalizi, na mzigo wa kutosha, bila kuwa na mzigo wa ziada wa uasi wenu. Watafhamini kila juhudi zinazofanywa kwa upande wa wanafunzi kushirikiana nao katika kazi. {FEsw 246.1}

Mwanafunzi asiyejali, asiyejiheshimu, asiyejithamini, asiye na mwelekeo mzuri, na ambaye hajitahidi kufanya kwa ubora kwa sehemu yake, anajiumiza sana. Anaamua kile kitachokuwa ni uelekeo wa tabia yake, na kuwashawishi wengine kuacha ukweli na unyoofu, ambao, kama si kwa ushawishi wake mbaya, wangekuthubutu kuwa wakweli na watakatifu. Mwanafunzi mmoja anayehisi uwajibikaji wake kuwa mwaminifu katika kuwasaidia wakufunzi wake, atajisaidia zaidi kuliko anavyowasaidia wengine wote. Mbingu hutazama chini kwa shauku wanafunzi wanaojitahidi kutenda haki, na kuwa na kusudi thabiti la kuwa wa kweli kwa Mungu. Watapata msaada kutoka kwa Mungu. Juu ya Danieli na wenzake waliosimama imara kama mwamba wa ukweli, imeandikwa, “Basi, kwa habari za hao vijana wanne, Mungu aliwapa maarifa na ujuzi katika elimu na hekima: ... na katika kila jambo la hekima na ufahamu alilowauliza Mfalme, akawaona kuwa walifaa mara kumi zaidi ya waganga na wachawi waliokuwa katika ufalme wake.” {FEsw 247.1}

Ikiwa hamna nia ya kuboresha fursa na majaliwa yenu, kwa nini mnatumia, katika kuhudhuria shule, pesa ambazo wazazi wenu wamehangaika kuipata? Wamewapeleka mbali na paa la nyumbani, kwa matumaini makubwa kwamba mtaelimika na kufaidika na ugeni wenu chuoni. Wamewafuata kwa barua pamoja na maombi, na kila mstari mliouandika umesomwa kwa shauku. Wamemshukuru Mungu kwa kila dalili kuwa mngefanikisha maisha yenu ya Kikristo, na wamelia kwa kufurahishwa na dalili za maendeleo yenu katika sayansi na maarifa ya kiroho. Tazama nataka kuwasihi msifanye chochote ambacho ni chenye shaka. Fikiria jinsi wazazi wenu wataavyoyachukulia matendo yenu, na acheni kufanya lolote ambalo litatia miiba mito yao. Msiwe wazembe, wazito, na waovu. Matendo yenu hayaishii kwenu wenyewe; yanaonyesha faida au hasara kwa shule, kulingana na kama ni mazuri au mabaya. Mkifanya ubaya Mnamhuzunisha Yesu Kristo, aliyewanunua kwa gharama ya damu yake mwenyewe, mnaumiza nafsi ya mkuu wenu, mnaijeruhi mioyo ya walimu wenu, na kujeruhi na kuharibu nafsi zenu. Mnatia doa kumbukumbu zenu, ambazo kwazo mtaabika. Je, italipa? Daima ni bora na salama kutenda haki kwa sababu ni sawa. Je, kwa sasa hamwezi kufikiri kwa umakini? Fikra sahihi zipo kwenye msingi wa kutenda kwa usahihi. Wekeni akili zenu kuamini kuwa mtakidhi matarajio ya wazazi wenu waliyonayo kwenu, ya kwamba mtakuwa na juhudi za uaminifu ili kuwa bora, kwamba mtaona pesa walizotumia hazijatumika vibaya. Kuweni na madhumuni madhubuti ya kushirikiana na juhudi

zinazofanywa na wazazi na walimu, na kufikia kiwango cha juu cha maarifa na tabia. Azimieni kutowakatisha tamaa hao wanaowapenda kiasi cha kutosha kuwaamini. Ni uanaume kutenda haki, na Yesu atawasaidia kutenda mema, mkitafuta kuyafanya kwa sababu ni haki. {FEsw 247.2}

Wale wanaovutiwa juu yenu wana matumaini ya kupendeza kwenu, kuwa mtakuwa watu wenye manufaa, ambao mtajazwa na maadili ya thamani na uadilifu usioyumba. Kwa vijana ambao wametoka New Zealand hadi Amerika, mengi yamefanyika; nami nitawaambia hawa wanafunzi, Wekeni malengo ya juu, na kisha mfuata hatua kwa hatua kukifikia kiwango, ingawa inaweza kuwa kwa juhudi za maumivu, kwa kujinyima na kujitolea. Kristo atakuwa msaada unaopatikana kwenu kila wakati wa haja, kama mkimwita, ili muwe kama Danieli, ambaye hakuna majaribu yaliyoweza kumharibu. Msiwakatishe tamaa wazazi wenu na marafiki zenu; lakini zaidi ya yote msimkatishe tamaa yule aliyewapenda kiasi cha kutoa maisha yake mwenyewe ili kufuta dhambi zenu na kuwa kwenu Mwokozi binafsi. Yesu alisema, “Bila Mimi ninyi hamwezi kufanya neno lo lote.” Wekeni hili akilini. Ikiwa mmefanya makosa, mnaweza kupata ushindi kwa kuyatambua makosa haya, na kwa kuyaona kama minara ya onyo, ili kuwawezesha kuepuka matokeo yake. Sina haja kuwaambia kwamba hili litageuza kushindwa kwenu kuwa ushindi, kumkatisha tamaa adui, na kumheshimu Mkombozi wenu, ambaye ninyi ni mali Yake. {FEsw 248.1}

Tunasikitika kweli kwamba udhaifu wowote wa tabia unapaswa kuwa uliharibu rekodi ya zamani, kwa sababu tunajua ni Ushahidi kwamba hamkukeshwa katika maombi. Tunasikitika kuwa makosa yamefanywa kwa sababu wamewatwika walimu mizigo ambayo hawakupaswa kuibeba. Walimu wana asili yao wenyewe ya udhaifu wa tabia ya kushindana nao, na wana uwezo wa kusonga bila busara chini ya mkazo wa majaribu. Wanaweza kufikiria wanafanya haki wakati wanatekeleza nidhamu kali, lakini wanaweza kuwa wanafanya makosa katika hali wanayoshughulika nayo. Ingekuwa bora zaidi kwa wanafunzi na walimu, kama wanafunzi wangejiweka ktika heshima yao, na kutenda kutokana na nia safi na adhimu, ili mwenendo wao wenyewe wa kutenda uwe wa kuwatambulisha kwa wale ambao ni walimu na wakufunzi wao. Ikiwa kwa kila njia inayowezekana na katika kila hali, wangefanya kuwatendea wale walio katika nafasi za uongozi, na kubeba wajibu, kama vile wao wenyewe wangependa kutendewa, ni amani na mafanikio gani yangekuwa shuleni. {FEsw 249.1}

Kwa nini wanafunzi wajihusishe na yule muasi mkuu, kuwa mawakala wake katika kuwajaribu wengine, na kupitia wengine na kusababisha anguko la wengi? Kila binadamu ana majaribu binafsi, ya kipekee yake mwenyewe, na hakuna mtu aliye huru dhidi ya majaribu. Kama walimu ni wanafunzi wa Kristo, na wanajishughulisha na kazi katika njia iliyokubaliwa na Mungu, bila shaka Shetani atawashambulia kwa majaribu yake. Ikiwa mdanganyifu mkuu anaweza kuchochea

mambo mabaya ya tabia katika wanafunzi, na kupitia kwao kuleta mashaka na kukata tamaa kwa walimu, amefanikiwa kupata kusudi lake. Ikiwa chini ya jaribu mwalimu anaonyesha udhaifu, kwa namna yoyote ile, basi ushawishi wake umeharibiwa; lakini anayejihibitisha kuwa wakala wa adui mkuu wa Roho, lazima atatoa hesabu kwa Mungu kwa sehemu aliyotenda katika kumfanya mwalimu ajikwae. Hebu wanafunzi wazingatie kwa makini aina hii ya jambo, na hebu afadhali wasome jinsi ya kuwatia moyo na kuwaimarisha walimu wao, kuliko namna ya kuleta kukatisha tamaa na majaribu juu yao. Kwa kufanya hivyo, hawatakuwa wakipanda magugu yatakayochipuka katikati ya ngano. “Msidanganyike; Mungu hadhihakiwi; kwa kuwa cho chote apandacho mtu, ndicho atakachovuna. Maana yeye apandaye kwa mwili wake katika mwili wake atavuna uharibifu; bali yeye apandaye kwa Roho, katika Roho atavuna uzima wa milele. Tena tusichoke katika kutenda mema; maana tutavuna kwa wakati wake tusipozimia Roho. Kwa hiyo kadri tupatavyo nafasi, na tuwatendee watu wote mema, na hasa wale jamaa ya waaminio.” **Wagalatia 6:7-10. {FEsw 249.2}**

Wanafunzi watajaribiwa kufanya mambo ya kupinga sheria yaani, uasi, ikiwa ni kwa ajili tu ya kujifurahisha wenyewe na kuwa na kile wanachokiita “raha/fun.” Ikiwa watapenda kujiweka juu ya heshima yao, na kuzingatia Ukweli kwamba katika kufanya mambo haya hawambariki mtu yeyote, hawamfaidi mtu yeyote, bali yanawahusisha wengine pamoja na wao wenyewe katika ugumu, watakuwa na uwezekano mkubwa wa kuchukua njia ya ushujaa {kiume} na ya heshima, na kuyaweka mapenzi yao upande wa mapenzi ya Kristo. Watafanya kazi katika mistari/nyanja ya Kristo, na kuwasaidia walimu wao kubeba mizigo yao, ambayo Shetani angewavunja moyo zaidi kwa kutumia akili zisizofikiri kwa hila zisizo na maana (kuwachezea walimu kwa kupanga vioja). Watatafuta kutengeneza mazingira katika shule, ambayo, badala ya kuwa ya huzuni na ya kudhoofisha nguvu za maadili, yatakuwa ya afya na ya kuisisimua. Kwa kufanya hivyo, wanafunzi watakuwa wametumia dhamira zao kutenda sehemu yao kwa upande wa lile kusudi la Kristo, na hawajatoa hata nukta moja ya mvuto au uwezo wao kwa adui mkuu wa yote yaliyo mema. Ni Kwa kiasi gani cha kuridhika zaidi wanafunzi wanaweza kukumbuka mpango huu wa utendaji, kuliko hatua ya mwenendo ambapo wanaidhinisha mipango ya siri ya kudharau na kutoheshimu mamlaka. Watakuwa na sababu za kumsifu Mungu kwa kuwa wameyapinga mayowe ya kelele za mielekeo y atamaa za mwili; na wameweka mvuto wao upande wa utaratibu, bidii, na Utiifu. Hebu kila mwanafunzi akumbuke kwamba iko katika uwezo wake kusaidia, na si kuzuia, kusudi la elimu. **{FEsw 250.1}**

Wanafunzi katika taasisi zetu za elimu wanaweza kuunda tabia kulingana na mfano wa kimbingu/Bwana, au kudhalilisha nguvu zao walizopewa na Mungu, na kujishusha chini zaodo, wala wao hawatakuwa na mtu kulaumu bali wao wenyewe wakijishushia hadhi. Kila kitu ambacho Mungu angeweza kufanya kimefanywa kwa ajili ya mwanadamu. Kila hitaji limetazamwa; kila shida, kila dharura, imezingatiwa.

Mahali palipopindapinda pamenyooshwa, mahali pagumu pamelainishwa, na kwa hiyo hakuna atakayekuwa na udhuru siku ya hukumu, ikiwa emeonesha kutokuamini na kupinga utendaji wa Roho Mtakatifu. {FEsw 251.1}

Yesu Kristo amejitoa kama dhabihu kamili kwa ajili ya kila mwana na binti aliyeanguka wa Adamu. Tazama ni unyonge ulioje alioubeba!! Jinsi gani alishuka, hatua baada ya hatua, kwenda chini na chini katika njia ya unyonge, lakini hakuidhalilisha nafsi Yake kwa uchafu hata mmoja wa doa la dhambi! Aliteseka kwa haya yote, ili akuinue, akusafishe, akutakase, na kukuheshimisha, na akuweke kama mrithi pamoja Naye juu ya kiti Chake cha enzi. Utaufanyaje wito na uteule wako uwe wa hakika? Njia ya wokovu ni ipi? Kristo anasema, “Mimi Ndimi njia, Kweli, na uzima.” Hata kama wewe ni mwenye dhambi, hata uwe na hatia kiasi gani, wewe umeitwa, umechaguliwa. “Mkaribieni Mungu, Naye atawakaribia ninyi.” Hakuna hata mmoja atakayelazimishwa kinyume na mapenzi Yake kuja kwa Yesu Kristo. Mkuu wa Mbinguni, Mwana pekee wa Mungu wa Kweli na Aliye Hai, alikufungulia njia ya kuja Kwake, kwa kutoa maisha Yake kama dhabihu kwenye msalaba wa Kalvari. Lakini ingawa Aliteseka kwa haya yote kwa ajili yako, Yeye ni mtakatifu sana, Msafi wa moyo sana, na ni Mwenye haki sana, kuutazama uovu. Lakini hata hili halihitaji kukuweka mbali Naye; kwani anasema, “Sikuja kuwaita wenye haki, bali wenye dhambi, wapate kutubu.” Hebu zile Roho zinazoangamia zije Kwake kama zilivyo, bila kusita, na kusihi damu ya upatanisho ya Kristo, na watapata kibali kwa Mungu akaaye katika Utukufu katikati ya makerubi juu ya kiti cha rehema. Damu ya Yesu ni pasipoti isiyoweza kushindwa, ambayo kwayo maombi yako yote yanaweza kupata kibali katika kiti cha cha Mungu. {FEsw 251.2}

— *“Christian Education” {Supplement}, 1893.*

URASIMU, NA SIO TARATIBU, ULIO WA UOVU

Uovu hautokei kwa sababu ya kuweka utaratibu wa mambo au uundaji wa mfumo, bali kwa sababu ya kuufanya mfumo{organization} kuwa kila kitu, na uwepo wa utauwa wa muda tu. Wakati umbo na utendaji vinapochukua nafasi ya kwanza, na kazi ngumu hufanywa ili kuendeleza na kazi inayopaswa kufanywa kwa urahisi/usahili, uovu utatokea, na kidogo sana ndicho kitakachofanikishwa kulingana na juhudi zilizowekwa. Lengo la kuunda mfumo wa utaratibu ni kinyume cha hili; na kwa kuuvuruga, itakuwa ni kama kubomoa kile tulichokijenga. Matokeo mabaya yameonekana, katika kazi ya shule ya Sabato na katika jumuiya ya kimishionari, kwa sababu ya kutumia nguvu nyingi huku uzoefu muhimu ukipotea. Katika maboresho mengi yaliyofikiriwa ambayo yamekuwepo, uundaji wa mwanadamu umewekwa kwenye kazi. Katika shule ya Sabato, wanaume na wanawake wamekubaliwa kama maafisa na walimu, ambao hawakuwa na nia ya kiroho, na hawana shauku hai katika kazi iliyowekwa kwao; lakini mambo yanaweza kuwekwa sawa tu kwa msaada wa Roho Mtakatifu. Uovu huo huo umekuwepo kwa miaka kama ilivyo sasa katika makanisa yetu. Taratibu zenye ubaridi na kavu kavu au urasimu, kiburi, na kupenda maonyesho vimechukua mahali pa uchaMungu wa kweli na utauwa mnyenyekevu. Tungeweza kuona mpangilio tofauti wa mambo idadi kubwa itajitoa kikamilifu kwa Mungu, na kisha wangetoa talanta zao kwa Kazi ya shule ya Sabato, wakiendelea katika maarifa, na kujielimisha wao wenyewe ili waweze kuwafundisha wengine kwa njia iliyo bora ya kutumia katika kazi; lakini si kwa watendakazi kutafuta mbinu ambazo wanaweza kufanya maonesho, wakitumia muda katika maigizo ya maonesho na muziki, kwani haya hayamfaidishi yoyote. Haifai kitu kuwazoeza watoto kutoa hotuba katika matukio maalum. Wanapaswa kuletwa kwa Kristo, na badala ya kutumia muda, pesa, na bidii kufanya maonesho, hebu juhudi zote ziwe za kukusanya miganda ya mavuno. {FEsw 253.1}

Wengi wameonekana kufikiri kwamba yote yaliyokuwa muhimu katika kazi ya shule ya Sabato ilikuwa kuandaa shule, na kuwanoa wasomi ili kwamba watende kulingana na mfumo wa maadhimisho na maonesho; na kwamba kama watu wangeweza kupatikana kama walimu, shule ya Sabato ingejiendesha yenyewe. Walimu mara nyingi wanatafutwa ambao hawawezi kuongoza Roho kwa Kristo kwa sababu hawamwoni kuwa wa thamani kwa nafsi zao wenyewe; lakini wale wote wasioithamini nafsi ili watafanye kazi kama Kristo, watatawanya kutoka kwa Kristo. “Yeye ambaye [zingatia Maneno haya] hakusanyi pamoja Nami, hutawanya.” Ikiwa walimu hawana mzigo wa kuwaongoza watu kwa Yesu, watakuwa wasiojali Ukweli; watakuwa wazembe, na mazingira ambayo yanazungukaa nafsi zao yatafanya kazi ya kutawanya mbali na Kristo. Na kwa vipengele kama hivyo katika shule ya Sabato, kutakuwa na mgongano wa kudumu na shida; kwani wakati walimu wanajihusisha

na kazi ile wasiyopendezwa nayo, wanafunzi watashiriki Roho hiyo hiyo. {FEsw 254.1}

Lakini ingawa shida hizi zipo, Je, zitaondolewa kwa kuukomesha mfumo? Nina hakika kuwa Bwana ameleta mfumo ambao umekamilika, na Ukweli kwamba vipopengele vya kukatisha tamaa katika kazi haipaswi kufikiriwa vya kutosha kuwa sababu ya kutokuwa na mfumo. Nuru ya kutosha ilitolewa kwetu kuhusiana na mfumo wa ya makanisa, na bado tulikuwa na vita ngumu kupigana katika ukamilifu wa mfumo; lakini ushindi ulipatikana hatimaye, na sasa je, kanisa litakosa kuwa na mfumo kwa sababu ya kutojali, kuwa na utaratibu baridi na mkavu, na kiburi? Je, turudi nyuma kwenye machafuko au kutokuwa na utaratibu kwa sababu washiriki wa kanisa ambao hajawekwa wakfu wameweka juu ya kazi umbo la mwanadamu, na kutafuta kulifanya kanisa kukidhi viwango vyenye umaarufu sana? {FEsw 254.2}

Ni kweli kwamba usahili wa utauwa wa kweli kwa kiwango kikubwa umepotea kanisani, na wengi wa wale wanaokiri kuwa wafuasi wa Kristo wamepofushwa kiasi kwamba wanafikiri faida ndiyo utauwa, nao wanatoa nguvu zao katika mambo ya kitambo. Hawatambui kwamba uwezo wao wote wa kiakili umenunuliwa na Kristo, na kwamba wanapaswa kutoa Kwake matokeo yaliyo bora zaidi ya mawazo yao, ili kusudi Lake liendeleo mbele. Lakini badala ya kutoa mawazo yao, yaliyo wazi ili kuendeleza kazi, kuimarisha na kulibariki kanisa, wanatoa uwezo wao wote kwa maendeleo ya maslahi yao binafsi. Hawakusanyi pamoja na Kristo, bali wanatawanya kutoka Kwake kwa maneno na vitendo vyao. Wanazingira nafsi zao kwa mazingira ambayo ni mabaya kwa mionjo ya kiroho. Wanadai kuwa wafuasi wa Kristo, lakini hawamjui kwa uzoefu wa maarifa. Hawaiiishi dini. Hawatafuti kuwa Wakristo kwa njia sawa na ambayo wangejifunza biashara. Wanadai kuuamini Ukweli wa hali ya juu; lakini ni dhahiri kwamba wameuweka katika ua wa nje; kwa maana hauna nguvu ya utakaso juu ya maisha na tabia. Hawatambui ni kiasi gani uko hatarini; wokovu wa nafsi zao na za wengine. Hawatambui kwamba ili wawe harufu ya uzima iletayo uzima ni lazima wawe chini ya nidhamu na mafunzo ya kiroho, kujifunza katika shule ya Kristo. Bila nidhamu hii ya kiroho, wanakuwa wasiofaa, wajinga, na wasio na maendeleo, na wasioona ulazima wa mafunzo ya kiroho na maarifa ambayo yangewawezesha kushika nyadhifa za ushawishi na manufaa. Ikiwa hawakujiweka wakfu kwa Mungu kikamilifu, kuwa wanafunzi katika shule Yake, watafanya kazi ya kubahatisha, isiyo na utaratibu, yenye vurugu na ambayo itasababisha kuumia kwa kanisa. {FEsw 254.3}

Lakini kwa sababu ya mivuto hii isiyowekwa wakfu, tutachukua hatua za kurudi nyuma, na kubomoa njia zile ambazo zimetugharimu mengi kuzijenga, na kutangaza kuwa mifumo yote ya utaratibu yote ni makosa? Tusithubutu kufanya hivi. Kuna mambo mengi yanayohitaji kurekebisha; ila kuna baadhi ya mambo yenye umuhimu mdogo nayo hutuzwa mno, wakati mambo mengine yaliyo na umuhimu mkubwa hupuuuzwa, na kuonekana kama si ya muhimu. Akili za watu

zinahitaji mafunzo ya vitabu/kitaaluma na kiroho ambayo yanaweza kuendelezwa kwa usawa; kwani bila mafunzo ya vitabu/kitaaluma, watu hawawezi kujaza nafasi mbalimbali za amana zilizokubalika. {FEsw 255.1}

Kitabu kikuu cha kuelimishia ni Biblia, na bado husomwa kidogo au hakifanyiwi mazoezi. Laiti kila mtu angetafuta kujitengeneza mwenyewe kwa yote anayoweza, kuboresha fursa zake kwa ubora wake, akikusudia kutumia kila uwezo ambao Mungu amempa, si ili tu kuendeleza mambo yake ya kitambo, bali kuendeleza maslahi ya kiroho. Laiti wote wangepata kutafuta kwa bidii kujua Ukweli ni upi, kujifunza kwa bidii ili wapate kuwa na lugha sahihi na sauti zilizokuzwa vyema, wapate kuwasilisha ile Kweli katika namna iliyotukuka, bora na uzuri unaoinua. Mtu asiwaze kwamba atateleza katika baadhi ya nyadhifa au vyeo vyenye manufaa. Ikiwa wanadamu wangetaka kujizoesha kazi kwa ajili ya Mungu, hebu wanyumbulishe nguvu zao, na kuzielekeza akili zao kwa unyofu katika utumiaji. Ni Shetani ndiye anayeweza kuwaweka watu katika ujinga, kutokuwa na ufanisi na uzembe, ili waweze kuendelea kwa njia ya upande mmoja ambao wanaweza kamwe wasiweze kuusahihisha. Angetaka watu wakuze aina moja ya kitivo kwa kuiacha kingine au kutoitumia seti nyingine, ili akili ipoteze nguvu zake, na wakati kunapokuwa na uhitaji wa kweli, wasiweze kuamka katika dharura. Mungu anataka wanadamu wafanye wawezavyo, na huku Shetani akivuta akili kuelekea upande mmoja, Yesu anaivuta katika upande mwingine. {FEsw 256.1}

Ukweli unapopokelewa moyoni, huanza kazi ya kumsafisha na kumtakasa mpokeaji. Yeye anayeuthamini Ukweli, hatahisi kwamba hana haja tena ya kuelimishwa, bali atatambua anapotekeleza Ukweli katika maisha yake ya vitendo, kuwa yuko katika uhitaji wa Nuru daima ili apate kuongezeka katika ujuzi. Kadri anavyoleta Ukweli katika maisha yake, atahisi ujinga wake halisi, na kutambua umuhimu wa kuwa na elimu ya kina zaidi, ili aweze kuelewa jinsi ya kuutumia uwezo wake kwa ubora zaidi. {FEsw 256.2}

Kuna upungufu wa uwezo wa kielimu miongoni mwetu, na hatuna watu ambao wamefunzwa vya kutosha kutenda haki kwa kazi ya kusimamia shule zetu za Sabato na makanisa. Wengi wanaojua Ukweli, bado hawaelewi kwa njia ipi wangeweza kusimamia wenyewe katika uwasilishaji wake. Hawajaandaliwa kuiwasilisha kwa njia ambayo tabia Yake takatifu, ya adhama itakuwa wazi kwa watu. Badala ya nidhamu ndogo, wanahitaji mafunzo ya kina zaidi. Haiwezekani mtu kuona mbele atakavyoitwa. Anaweza kuwekwa katika hali ambamo atahitaji utambuzi wa haraka na hoja zenye uwiano mzuri, na kwa hiyo ni kwa ajili ya heshima ya Kristo kwamba watenda kazi walioelimika vyema wazidishwe kati yetu; watakuwa na uwezo mzuri zaidi wa kuwasilisha Ukweli kwa njia iliyo wazi na njia yenye akili, na Ukweli unapaswa kuonyeshwa kwa njia ambayo itakuwa huru iwezekanavyo kutokana na kasoro. {FEsw 256.3}

Elimu ya Kweli, wakati akili iko chini ya ushawishi wa udhibiti wa Roho Mtakatifu,

ni ya umuhimu mkubwa, na kila mtu anapaswa ajifunze kuthamini kwa usahihi uwezo ambao Mungu ametoa; na kwa mazoezi ya maarifa anayopata, anaweza, kwa ushawishi ya tabia yake mwenyewe, kuwaonyesha wengine thamani wa kupata mafunzo kwa ajili ya utumishi wa Kristo, na kuwaongoza kuufuata mfano Wake. Kuna mengi duniani ya kufanywa, na siyo faida kuweka wasio na uzoefu kufanyia kazi mambo yale ambayo ni ya umuhimu wa juu. Kutojali, ugoigoi, kukosa shauku, kutokuwa makini, kutochangamka ambako kumedhihirika kuhusiana na elimu ni kwa ajabu, lakini hilo humpendeza Shetani. Mungu angependa tuamke kutoka katika kutojali kwetu, na kutoruhusu tena nguvu zetu za kiakili kukimbia kwenye pipa la takataka, na kuharibika kwa kukosa maadili na kisha kujaa ujinga. Watu wanapaswa kuthamini talanta walizokabidhiwa, na kutumia fursa zilizo katika uwezo wao. Hebu nguvu za akili zifungwe kwa kazi, na kwa kujitahidi kwa nguvu kuacha akili ikuzwe na kuendelezwa. {FEsw 257.1}

Kuna haja zaidi sasa kuliko hapo awali kwamba vijana wetu kiume na wa kike watakuwa wamehitimu kiakili kwa kazi. Shule zetu ya Sabato si tu zinahitaji watendakazi wa kiakili, bali wa kiroho, na akili hupokea nguvu na ufanisi wake kwa nidhamu kamili. Kwa usomaji wa juujuu, akili polepole hupoteza toni yake, na kuzorota katika ujinga, na kukosa uwezo wa juhudi zozote za kuitumia. Lakini elimu inawatayarisha watu kujua na kufanya aina ya kazi ambayo lazima wakati huu ifanyike. Nidhamu kamili, chini ya mwalimu mwenye busara, ni ya thamani zaidi kuliko uwezo wa asili na majaliwa, ambapo hakuna nidhamu. {FEsw 257.2}

Bwana amedhihirisha kuthamini Kwake wanadamu, katika kumtoa Mwana Wake wa pekee ili kumkomboa. Shetani pia ameonesha uthamini wake kwa uwezo uliofunzwa vyema na kutakaswa, kwa mbinu za kijanja ambazo kwazo hutafuta kugeuza akili na moyo wa mtu kama huyo kutoka katika utumishi wa Mungu, ili apate kumwongoza kujiunga katika safu za uasi. Kama malaika wa Nuru, anakuja kwa kisingizio cha kuwavuta watu katika utumishi wake; maana anajua kuwa mwanamume au mwanamke aliyeelimika, wakati hayuko chini ya udhibiti wa Roho wa Mungu, anaweza kuwa na faida kubwa kwake. Atamkimbiza mwanafunzi kwa majaribu makali ya aina tofauti, akitafuta kumshawishi ajivunie mafanikio yake, na kufikiria kuwa yeye ni mkuu, ili ajitumainie mwenyewe, na kutembea katika cheche za moto wake aliouwasha mwenyewe {Nuru yake}. Hivyo anaongozwa kutenganisha nafsi yake na Mungu, chanzo cha Nuru yote na maarifa, na ili apate kujikweza, aungane na Shetani; mwanzilishi wa dhambi zote. {FEsw 258.1}

Kumcha Bwana ni mwanzo wa hekima yote; na pale Mungu anapokuwa hategemewi, matokeo ya elimu ni kukuza tu kutomcha Mungu. Sababu ya kanisa kuwa dhaifu na lisilofaa ni kwamba kuna upungufu wa neema ya Kristo kati ya wale wanaokiri Ukweli wa siku hizi za mwisho. Ikiwa Bwana amewahi kunena kwangu mimi, kuna dhambi karibu kwa kila tabia inayopendwa na wengi wanaodai kuwa watoto wa Mungu; na isipokuwa wamejitenga mbali na Shetani na kushikamana na

haki Yesu wetu, ole wa Mungu itakuwa juu ya wale ambao wamekuwa na Nuru kuu, na bado wamechagua kutembea gizani. “Ndipo akaanza kuikemea miji ile ambamo ndani yake ilifanyika miujiza, kwa sababu haikutubu: Ole wako! Korazini; ole wako, Bethsaida; kwa kuwa kama miujiza iliyofanyika kwenu, ingelifanyika katika Tiro na Sidoni, wangelitubu zamani kwa kuvaa magunia na majivu. Walakini nawaambieni, Itakuwa rahisi zaidi Tiro na Sidoni kustahimili adhabu zao siku ya hukumu kuliko ninyi. Na wewe, Kapernaumu, je, utakuzwa mpaka Mbinguni; utashushwa hata kuzimu; kwa sababu kama mijuziza iliyofanyika kwako, ingalifanyika katika Sodoma, ungalikuwepo mji huo hata leo. Walakini nawaambieni, itakuwa rahisi nchi ya Sodoma kustahimili adhabu siku ya hukumu kuliko wewe.” {FEsw 258.2}

Ni jambo la kutisha kuwa na Nuru kubwa na baraka, kuwa na fursa nyingi na upendeleo, na bado visitumike kutuokoa. Wale ambao hawatumii kwa kujiokoa fursa zao, watahukumiwa kwa fursa ambazo Mungu amewapa; lakini wale wanaotembea katika Nuru watakuwa wameongezeka katika Nuru. Wale ambao wana Nuru ya ile Kweli, na bado wameshindwa kutembea katika Nuru, wako chini ya hukumu sawa na Korazini na Bethsaida. Je, maonyo haya hayatazingatiwa nasi? Je! maonyo haya hayana uzito kwetu? Katika siku za hivi karibuni itaonekana wale ambao wamekuwa wakitembea kwa unyenyekevu na Mungu, na ambao wamekuwa wakitii amri Zake. Wale ambao wamekuwa wakitembea katika cheche zao wenyewe watalala chini kwa huzuni. Itaonekana kuwa wao wamefanya kosa kubwa sana. Hebu na tuamke! Nuru sasa inaangaza; hebu madirisha ya akili na moyo yafunguliwe kuikaribisha miale iliyotumwa ya Mbinguni. Je, Yesu atasema juu ya wale wanaodai kuutii Ukweli, na bado wanaoshindwa kutembea katika Nuru Yake, “Na Neno la nabii wa Isaya linatimia kwao, likisema, Kusikia mtasikia wala hamtaelewa; kutazama mtatazama, wala hamtaona; Maana mioyo ya watu hawa imekuwa mizito, na kwa masikio yao hawasikii vema na macho yao wameyafumba; wasije wakaona kwa macho yao, wakasikia kwa masikio yao, wakaelewa kwa moyoni yao, na wakaongoka, nikawaponya”? {FEsw 259.1} – [Christian Education, 140 1893](#).

* Anachojaribu kusema hapo ni kuwa kuna hatari pia ya kutaka kufanya vitu kwa utaratibu kwa kuweka sheria nyingi ambazo zaweza kuchelewesha kazi ama isifanyike kabisa (formality). MFANO KUSEMA UTARATIBU WETU WA KUFUNDISHA LESONI NI LAZIMA MTU AWE MSHIRIKI, AYEHUDHURIA DARASALA LA WALIMU, N.K ni Jambo zuri ila, Jem ikitokea mtu wa namna hiyo hayupo itakuwaje?

KWA WAALIMU

Kila mtu anayehusika katika kuelimisha darasa la wanafunzi ambalo lina vijana wadogo, anapaswa kuzingatia kwamba watoto hawa wanaathiriwa, na huhisi hisia za angahewa, liwe la kupendeza au lisilo la kupendeza. {FEsw 260.1}

Ikiwa mwalimu ameunganishwa na Mungu, ikiwa ana Kristo anayekaa ndani moyo wake, Roho anayoionesha huhisiwa na watoto. Wakati mwalimu anapoonisha kutokuwa na subira au hasira kwa mtoto, kosa haliwezi kuwa kwa mtoto nusu kama vile lilivyo kwa mwalimu. Walimu huchoka kwa kazi zao, kisha kitu kidogo watoto wanachosema au kukifanya kisipopatana na hisia zao, je wataruhusu Roho ya Shetani iingie ndani yao, na kuwaongoza kuwa na hisia kwa watoto ambazo ni mbaya sana na zisizokubalika au kupendeza, kwa wao kukosa busara na hekima kutoka kwa Mungu? Kusiwe na mwalimu atakayeajiriwa, isipokuwa kuna ushahidi kwa kumjaribu na kumthibitisha, kuwa yeye anampenda, na ana hofu ya kumkosea Mungu. Kama walimu wanafundishwa na Mungu, ikiwa katika masomo yao wanajifunza kila siku katika mistari ya shule ya Kristo, watafanya kazi katika mistari ya Kristo. Watashinda na kujitwalia Roho pamoja na Kristo; kwani kila mtoto na kijana ni wa thamani. {FEsw 260.2}

Kila mwalimu anamhitaji Kristo kukaa moyoni mwake kwa imani, na kuwa na Roho ya Kweli, ya kujikana nafsi, ya kujitolea kwa ajili ya Kristo. Mmoja anaweza kuwa na elimu na maarifa ya kutosha katika sayansi ya kufundisha; lakini je amethibitishwa kwamba ana busara na hekima za kushughulikia akili za binadamu? Ikiwa waalimu hawana upendo wa Kristo ukikaa moyoni, hawafai kuunganishwa na watoto, na kubeba majukumu mazito yaliyowekwa katika kuwaelimisha watoto na vijana hawa. Wanakosa elimu na mafunzo ya juu ndani yao, na hawajui jinsi ya kushughulika na akili za kibinadamu. Wana Roho ya unyonge wao wenyewe, mioyo ya asili ambayo haitaki kutiishwa, na inajitahidi kutawala, na wanataka kuzikanyaga chini akili laini za plastiki zinazoweza kuathiriwa kirahisi (nyeti) na tabia za watoto kwa uangalizi kama huo, basi hilo litasaidia kuacha makovu na michubuko kwenye akili za watoto, ambayo haitaweza kuisha. {FEsw 260.3}

Ikiwa mwalimu hawezi kufanywa kujisikia wajibu na uangalifu anaopaswa kudhihirisha katika kushughulika na akili za wanadamu, elimu yake kwa namna fulani ina kasoro kubwa mno. Katika maisha ya nyumbani mafunzo yamekuwa na madhara katika tabia, na ni jambo la kuhuzunisha kuzalisha tena tabia hii mbovu katika usimamizi wa watoto wale ambao wamewekwa chini ya uangalizi wake. Tunasimama mbele za Mungu kwa kupimwa na kujaribiwa ili kuona kama tunaweza kuaminiwa kibinafsi na kisha kuwa sehemu ya familia itakayohusisha waliokombolewa Mbinguni. "Nikawaona wafu, wakubwa kwa wadogo,

wamesimama mbele ya hicho kiti chaenzi; na vitabu vikafunguliwa, na kitabu kingine kikafunguliwa, ambacho ni cha uzima; na hao wafu wakahukumiwa katika mambo hayo yaliyoandikwa katika vile vitabu, sawasawa na matendo yao.” {FEsw 261.1}

Hapa kunawasilishwa kiti cha enzi kikubwa cheupe na Yeye aketiye juu yake ambaye mbingu na nchi zilikimbia mbele Yake. Hebu kila mwalimu azingatie kuwa anafanya kazi yake machoni pa ulimwengu wa Mbinguni. Kila mtoto ambaye mwalimu huletwa kukutana Naye amenunuliwa kwa damu ya Mwana -pekee wa Mungu, na Yeye ambaye amekufa kwa ajili ya watoto hawa angetaka watendewe kama mali Yake Mwenyewe. Hakikisha kwamba katika kuchangamana/kuhusiana kwenu, walimu, na kila moja ya hawa watoto kunakuwa kwa tabia ile ambayo haitawaibisha mtakapokutana nayo katika siku ile kuu ya hukumu, wakati kila neno na tendo litapoletwa upya mbele za Mungu, na mzigo wa matokeo yake kuwekwa wazi mbele yako binafsi. “Mmenunuliwa kwa thamani,”—Tazama ni gharama ya kiasi gani imetolewa kwetu!, umilele pekee ndio utakaofunua siri hiyo! {FEsw 261.2}

Bwana Yesu Kristo ana huruma isiyo na kikomo kwa wale ambao Amewanunua kwa gharama ya mateso Yake Mwenyewe katika mwili Wake, ili kwamba wasiangamie pamoja na Ibilisi na malaika zake, bali aweze kuwadai kama wateule Wake. Wao ni malimbuko ya upendo Wake, mali Yake Mwenyewe; na Anawatazama kwa hali ya upendo usiotamkika, na harufu ya haki Yake Mwenyewe huwapa wapendwa Wake wanaomwamini Yeye. Inahitaji busara na hekima na upendo wa kibinadamu, na upendo uliotakaswa kwa wana-kondoo wa thamani wa kundi, kuwaongoza kuona na kuthamini fursa zao katika kujitoa wenyewe hadi kwa uongozi mwororo wa wachungaji waaminifu. Watoto wa Mungu watatumia upole wa Yesu Kristo. {FEsw 261.3}

Walimu, Yesu Yuko shuleni kwenu kila siku. Moyo Wake wa upendo mkuu usio na kikomo hutolewa, sio tu kwa watoto wenye tabia bora tu, ambao wana mazingira mazuri zaidi, bali kwa watoto ambao huwa na tabia za urithi zenye kuchukiza. Hata wazazi hawajaelewa ni kiasi gani wanawajibika kwa sifa za tabia zilizokuzwa kwa watoto wao, na hawajapata huruma na hekima ya kushughulika na watoto hawa maskini, ambao wamewafanya wao kuwa hivi. Wanashindwa kufuatilia nyuma sababu ya maendeleo haya ya kukatisha tamaa ambayo ni jaribu au mtihani kwao. Lakini Yesu anawatazama hawa watoto kwa huruma na kwa upendo, kwa kuwa anaona, Anaelewa tangu chanzo hadi athari. {FEsw 262.1}

Mwalimu anaweza kuwafunga watoto hawa kwenye moyo wake kwa upendo wa Kristo kukaa katika hekalu la nafsi kama harufu nzuri, harufu ya uzima. Walimu wanaweza, kwa neema ya Kristo aliyowapa, kuwa wakala hai wa kibinadamu—kuwa

watenda kazi pamoja na Mungu—kuangaza, kuinua, kutia moyo, na kusaidia kuitakasa nafsi dhidi ya unajisi wake wa kimaadili; na sura ya Mungu itafunuliwa katika nafsi ya mtoto, na tabia itabadilishwa kwa neema ya Kristo. {FEsw 262.2}

Injili ni nguvu na hekima ya Mungu, ikiwa itawakilishwa kwa usahihi na wale wanaodai kuwa Wakristo. Kristo Aliyesulubiwa kwa ajili ya dhambi zetu lazima anyenyekeze kila Roho mbele za Mungu kwa; makusudi Yake Mwenyewe. Kristo aliyefufuka kutoka kwa wafu, na kupaa juu, Mwombezi wetu aliye hai mbele za Mungu, ni sayansi ya wokovu ambayo tunahitaji kujifunza na kuwafundisha watoto na vijana. Kristo alisema, “Najiweka wakfu Mwenyewe, ili na hao watakaswe.” Hii ndiyo kazi ambayo daima humshughulisha kila mwalimu. Ni lazima kusiwe na kazi hovyovy au holela katika jambo hili, kwani hata kazi ya kuelimisha watoto katika shule za kutwa inahitaji sana neema ya Kristo na kujinyenyekeza. Wale ambao kwa asili wana hasira, hukasirika kwa haraka, na wamendekezai tabia ya ukosoaji, ya kufikiria maovu, wanapaswa kutafuta aina nyingine ya kazi ambayo haitazalisha yoyote ya tabia zao zisizopendeza kwa watoto na vijana, kwa kuwa wamegharimu mbingu na dunia mno. Mbinguhuona kwa mtoto, mwanaume au mwanamke asiyeendelezwa, mwenye uwezo na mamlaka ambayo, ikiwa yataongozwa kwa usahihi na kukuzwa na hekima ya Mbinguni, watakuwa mawakala wa kibinadamu ambao kupitia kwao nguvu ya kimbingu inaweza kushirikiana nao ili kuwa watendakazi pamoja na Mungu. Maneno makali, na (magombezo) makaripio ya mara kwa mara humdhuru mtoto, lakini usiyarekebishe kamwe. Zuia neno hilo dogo mdomoni mwako; weka Roho yako chini ya nidhamu ya Yesu Kristo; ndipo utajifunza jinsi gani ya kuwahurumia wale walioletwa chini ya mvuto wako. Usioneshe kukosa uvumilivu na ukali wa kupindukia, kwa maana kama watoto hawa wangukuwa wakamilifu, basi wasingehitaji kuja shule ili kupata manufaa ya shule. Watoto wanapaswa kutendewa kwa subira, upole, na kwa upendo ili kuinua ngazi ya maendeleo na ufanisi, kwa kupanda ngazi hatua kwa hatua katika kuyapata maarifa. {FEsw 262.3}

Ni wakala atendaye kazi kila siku ambaye anaweza kutekeleza, imani itendayo kazi kwa upendo, na kuitakasa Roho ya mwelimishaji. Je! mapenzi ya Mungu yaliyofunuliwa yamewekwa kama mamlaka yako ya juu zaidi? Ikiwa Kristo Yumo ndani, tumaini la Utukufu, ndipo ile Kweli ya Mungu itatenda dhidi ya tabia yako ya asili, ili wakala Wake wa kubadilisha Afunuliwe katika tabia iliyobadilika, nawe kwa mvuto wako hutaonesha moyo wa hasira isiyotakaswa, ukigeuza ule Ukweli wa Mungu kuwa uongo mbele ya mwanafunzi wako yeyote; wala katika uwasilishaji wako wa hasira ya ubinafsi, isiyo na subira, isiyo ya Kikristo katika kushughulika na akili yoyote ya kibinadamu, ukionesha kwamba neema ya Kristo haitoshi kwako kila wakati na kila mahali. Kwa hivyo utaonyesha kuwa mamlaka ya Mungu juu yenu si kwa jina tu bali katika uhalisia na Ukweli. Lazima kuwe na utengano kutoka kwa yote ambayo ni ya kupingwa na kuchukizwa au yasiyo ya Kikristo, hata kama yatakuwa magumu kiasi gani kwa muumini wa Kweli. {FEsw 263.1}

Jiulizeni, walimu, ninyi mnaofanya kazi zenu si kwa muda tu bali kwa umilele, Je, upendo wa Kristo unausukuma moyo wangu na Roho yangu, katika kushughulika na nafsi za thamani ambazo kwa ajili yao Yesu ameyatoa Maisha Yake? Chini ya msukumo wa nidhamu Yake, je, tabia za zamani, zisizopatana na mapenzi ya Mungu, huondoka na mbadala Wake kuchukua nafasi yake? "Nami nitawapa moyo mpya." Je, mambo yote yamekuwa mapya kupitia uongofu wako kwa Bwana Yesu Kristo? Katika maneno na kwa bidii sana Je, unapanda mbegu katika hii mioyo michanga ambayo wewe unaweza kumwomba Bwana ainyweshe, ili iweze, kwa kuhesabiwa katika Haki Yake, kuiva na kuwa mavuno mengi? Jiulizeni, Je, mimi kwa maneno yangu mwenyewe yasiyotakaswa na kukosa subira na kutaka hekima ile itokayo juu, Je, nitawathibitishia vijana hawa katika nafsi zao Roho potovu, kwa sababu wanaona kuwa mwalimu wao ana Roho tofauti na Kristo? Ikiwa watakufa katika dhambi zao, je, sitawajibika kwa nafsi zao? Nafsi inayompenda Yesu, inayothamini nguvu ya wokovu ya neema Yake, itahisi kusogea karibu na Kristo, hata kutamani kufanya kazi katika upande Wake. Haiwezi, au kuthubutu, kumruhusu Shetani atawale Roho yake na harufu zenye sumu kuizunguka nafsi yake. Kila kitu ambacho kitaharibu kitarundikwa upande mmoja ili kuharibu ushawishi wake, kwa sababu kinapinga mapenzi ya Mungu na kuhatarisha Roho za kondoo hawa wenye thamani na wana-kondoo; naye anatakiwa kulinda hizo Roho kama yule ambaye atatoa hesabu yake. Popote ambapo Mungu ametuweka, kwa majaliwa Yake, atatuhiadhi; kama siku zetu zitakavyokuwa ndivyo na nguvu zetu zitakavyokuwa. {FEsw 264.1}

Yeyote atakayeacha hisia zake za asili na misukumo yake ziende kokote na kuwa dhaifu na asiyeaminika, kwani yeye huwa mfereji ambao Shetani anaweza kuwasiliana ili kuchafua na kupotosha nafsi nyingi, na fitina hizi zisizo takatifu ambazo humdhibiti mtu huyo humkosesha hofu au dhamira njema, na aibu na machafuko huwa matokeo ya hakika. Roho wa Yesu Kristo daima ana nguvu ya kufanya upya, kurejesha nguvu juu ya nafsi ambayo imejisikia dhaifu na kumkimbilia Yeye asiyebadilika ambaye anaweza kutoa neema na uwezo wa kupinga kila uovu. Mkombozi wetu ana ufahamu mpana wa ubinadamu (kwa uumbaji na kwa kuwa binadamu). Moyo Wake huguswa daima na kukosa msaada kulikotambuliwa kwa mtoto mdogo ambaye anakabiliwa na mabaya au anatendewa ubaya kwa jeuri; kwa maana aliwapenda watoto. Kilio cha unyonge zaidi cha mateso ya mwanadamu hakitafika katika sikio Lake bure. Na kila anayebeba jukumu la kufundisha vijana atakutana na mioyo yenye ukaidi mzito, tabia ngumu, za kuchosha, zisizo na hekima na zenye upotofu wa kushangaza, na kazi yake ni kushirikiana na Mungu katika kurudisha sura ya maadili ya Mungu ndani ya kila mtoto. Yesu, Yesu wa thamani, —chemchemi yote ya upendo ilikuwa ndani ya Nafsi yake. Wanaowafundisha watoto wanapaswa kuwa wanaume na wanawake wa kanuni. {FEsw 264.2}

Maisha ya kidini ya watu wengi wanaodai kuwa Wakristo ni yale yanayoonesha

kuwa wao si Wakristo. Daima humwakilisha Kristo vibaya, wakiipotosha tabia Yake au kuieleza kwa udanganyifu. Hawahisi umuhimu wa mabadiliko haya ya tabia, na kwamba lazima wafananishwe na sura Yake ya Uungu; na wakati fulani wataonesha muonekano wa uongo wa Ukristo kwa ulimwengu, ambao utafanya kazi ya kuangamiza nafsi za walio wanaohusiana nao kwa sababu wao wenyewe, huku wakidai kuwa Wakristo, hawako chini ya udhibiti wa Yesu Kristo. Mielekeo yao ya kurithi na hulka zilizokuzwa za tabia hutunzwa kama sifa za thamani huku wakishughulika kwa jinsi ya kufisha katika ushawishi wao juu ya akili za wengine. Kwa maneno laini, na rahisi, wanatembea katika cheche za Nuru yao wenyewe. Wana dini iliyoelekezwa na, ya kudhibitiwa na, mazingira. Kama kila kitu hutokea kuwasukuma katika njia inayowapendeza, na huko hakuna hali za kuudhi zinazoweka wazi tabia zao zisizostahili, zisizo kama za Kikristo, watajishusha na kupendezwa; na watavutiwa sana. Wakati kunapokuwa na mambo yanayotokea katika familia au kwa kuchangamana na wengine ambayo huharibu amani yao na kutibua hasira zao, kama wakimwekea Mungu kila jambo na kudumisha haja zao wakiomba fadhila Zake kabla ya kujujihusisha na kazi zao za kila siku kama walimu, na wakijua nguvu na neema na upendo wa Kristo ukao ndani ya mioyo yao kabla ya kuingia katika kazi zao, malaika wa Mungu wataenda pamoja nao darasani. Lakini wakiingia darasani wakiwa wameudhika, na Roho ya hasira, mazingira ya maadili yanayozunguka nafsi huacha mvuto wake kwa watoto walio chini ya huduma na uangalizi wao, na mahali pa kufaa kuwafundisha watoto, wanahitaji mtu wa kuwafundisha masomo ya Yesu Kristo. {FEsw 265.1}

Hebu kila mwalimu anayekubali jukumu la kuelimisha watoto na vijana, ajichunguze, na asome kwa umakini tangu chanzo hadi athari. Je, ile Kweli ya Mungu umeimiliki nafsi yangu? Imefanya hekima itokayo kwa Yesu Kristo, ambayo kwanza ni “safi, tena ni ya amani, ya upole, tayari kusikiliza maneno ya watu, imejaa rehema na matunda mema, haina fitina, haina unafiki” imekuwa katika tabia yangu? Nikiwa nimesimama katika nafasi ya uwajibikaji wa ualimu, je, ninathamini kanuni kwamba “tunda la haki hupandwa katika amani na wale wafanyao amani”? Ukweli haupaswi kuhifadhiwa, na kutekelezwa pale tunapojisikia kufanya hivyo, bali wakati wote na katika mahali pote. {FEsw 266.1}

Akili zilizosawazishwa vizuri na tabia linganifu zinahitajika kama walimu katika kila mstari. Msiitoe kazi hii mikononi mwa vijana wa kike na wa kiume ambao hawajui jinsi ya kukabiliana nao akili za binadamu. Wanajua kidogo sana nguvu ya neema ya kutawala mioyo na tabia zao wenyewe ambapo wayatupe mafunzo ya zamani na kisha wajifunze masomo mapya kabisa katika uzoefu wa Kikristo. Hawajawahi kujifunza kuweka nafsi na tabia zao chini ya nidhamu ya Yesu Kristo, na kuleta hata yale mawazo yao kuwa mateka wa Yesu Kristo. Kuna kila aina ya tabia za kushughulikia watoto na vijana. Akili zao ni kama simenti mpya, inaacha kila alama. Kitu chochote kama vile harara, maonyesho ya hisia kwa upande wa mwalimu kinaweza kukatisha ushawishi wa wema juu ya wanafunzi ambao

amepewa kwa 'jina la kuwaelimisha'. Na je, elimu hii itakuwa ya wema wa sasa na ujao wa milele kwa watoto na vijana? Kuna ushawishi sahihi kutekelezwa juu yao kwa manufaa yao ya kiroho. Maelekezo yanapaswa kutolewa mara kwa mara ili kuwatia moyo watoto katika kutengeneza tabia sahihi katika maneno, sauti, na tabia. {FEsw 266.2}

Wengi wa watoto hao hawajapata mafunzo yafaayo nyumbani. Wametelekezwa kwa huzuni. Wengine wameachwa wafanye kama wapendavyo; wengine wamepatikana na makosa na kukatishwa tamaa. Lakini kupendeza kudogo na uchangamfu kumeonyeshwa kwao, na maneno machache ya kuwakubali yamesemwa kwao. Tabia mbovu za wazazi zimerithiwa, na nidhamu iliyotolewa na tabia hizi zenye kasoro zimekuwa za kuchukiza katika kuunda tabia. Mbao imara hazijaletwa kwenye ujenzi wa tabia zao. Hakuna kazi muhimu zaidi ambayo inaweza kufanyika kuliko kuelimisha na kuwafunza vijana na watoto hawa. Walimu wanaofanya kazi katika sehemu hii ya shamba la mizabibu la Bwana wanahitaji kujifunza kwanza jinsi ya kujimiliki, kutunza hasira zao na hisia zao chini ya udhibiti, chini ya Roho Mtakatifu wa Mungu. Wanapaswa kutoa ushahidi wa kutokuwa na uzoefu wa upande mmoja, bali akili iliyosawazishwa (balansi) vizuri, na tabia linganifu ili waweze kuaminiwa kwa sababu wao ni Wakristo waangalifu, wenyewe chini ya Mwalimu mkuu, ambaye amesema, "Jifunzeni Kwangu, kwa maana Mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo, nanyi mtapata raha nafsini mwenu." Ndipo kwa kujifunza katika shule ya Kristo kila siku, wao wanaweza kuwafunza watoto na vijana. {FEsw 267.1}

Wanaojiboresha, au wanaokuza utamaduni wao wenyewe, wanaojielimisha wenyewe, na wenye kujidhibiti nafsi, chini ya nidhamu katika shule ya Kristo, wakiwa na uhusiano hai na Mwalimu mkuu, watakuwa na ujuzi wa akili yenye dini ya vitendo; na kuweka nafsi zao wenyewe katika upendo wa Mungu, watajua jinsi ya kuwa na neema ya saburi na ustahimilivu kama wa Kristo. Uvumilivu, upendo, ustahimilivu, na huruma vinahitajika katika kazi. Watatambua kwamba wana uwanja muhimu sana katika eneo la Bwana la shamba la mizabibu la kulima. Ni lazima wainue mioyo yao kwa Mungu katika maombi ya dhati, Uwe kielelezo changu, kisha kwa kumtazama Yesu watafanya kazi ya Yesu Kristo. Yesu alisema, "Mwana hawezi kutenda Neno Mwenyewe, ila lile ambalo amwona Baba analitenda." Hivyo na wana na binti za Mungu; wanamtazama kwa uthabiti na kwa kufundishika Yesu, bila kufanya chochote kwa njia yao wenyewe na kwa mapenzi na furaha yao wenyewe; bali yale waliyo nayo, katika mafundisho ya Kristo, wamemwona Yeye, Kielelezo chao, anachofanya, nao wanakifanya pia. Kwa hivyo wanawakilisha kwa wanafunzi kwa maelekezo yao wakati wote na katika kila matukio tabia ya Yesu Kristo. Wanapata miale angavu ya Jua la Haki na kuakisi miale hii ya thamani juu ya watoto na vijana ambao wanawafundisha. Uundaji wa tabia sahihi ni kuuacha

msukumo wake kwenye akili na tabia za watoto, ili wapate kutenda njia iliyo sawa. Ina maana kubwa kuwaleta hawa watoto chini ya ushawishi wa moja kwa moja wa Roho wa Mungu, kuwafunza na na kuwaadisha katika malezi na maonyo ya Bwana. Malezi ya tabia sahihi, maonyesho ya Roho sahihi, huhitaji juhudi za dhati katika Jina na nguvu za Yesu. Mkufunzi lazima avumilie, akitoa mstari juu ya mstari, amri juu ya amri, hapa kidogo na pale kidogo, katika uvumilivu wote na subira, huruma na upendo, akiwafunga watoto hawa kwa moyo Wake kwa upendo wa Kristo unaofunuliwa ndani Yake Mwenyewe. {FEsw 267.2}

Ukweli huu unaweza kwa maana ya juu zaidi kutendwa, na kuonyeshwa mfano mbele ya watoto. “Awezaye kuwachukuliaa kwa upole wao wasiojua na kupotea; kwa kuwa Yeye Mwenyewe Yu katika hali ya udhaifu. Na kwa sababu hiyo imempasa, kama kwa ajili ya watu, vivyo hivyo kwa ajili ya nafsi Yake Mwenyewe, kutoa dhabihu kwa ajili ya dhambi.” {FEsw 268.1}

Hebu walimu wazingatie hili, na kamwe wasilisahau wanapochochewa kuwa na hisia zao dhidi ya watoto na vijana kwa tabia yoyote mbaya; wakumbuke kuwa Malaika wa Mungu huwatazama kwa huzuni; kwa maana watoto wakikosea na kufanya vibaya, basi ni muhimu zaidi kwa wale waliowekwa juu yao kama walimu wanapaswa kuwa na uwezo wa kuwafundisha kwa maagizo na mfano. Kwa hali yoyote hawapaswi kupoteza kutawala nafsi, kudhihirisha kutokuwa na subira na ukali, na ukosefu wa huruma na upendo; kwani hawa watoto ni mali ya Yesu Kristo, na walimu lazima wawe waangalifu sana na wamchao Mungu kwa habari ya Roho wanayoionesha na maneno wanayotamka, kwa maana watoto watakamata Roho iliyodhihirishwa, iwe ni nzuri au ni mbaya. Ni jukumu zito na takatifu. {FEsw 268.2}

Kuna haja ya kuwa na walimu wanaofikiria, wanaojali udhaifu wao wenyewe na mapungufu na dhambi zao, na ambao hawatawakandamiza na kuwakatisha tamaa watoto na vijana. Kuna haja ya kusali sana, kuwa na imani nyingi, na saburi nyingi, na ujasiri; vitu ambavyo Bwana Yuko tayari kuvitoa. Kwani Mungu huona kila jaribu, na mvuto wa wa ajabu unaweza kutolewa na walimu, ikiwa watayaishi masomo ambayo Kristo amewapa. Lakini je, walimu hawa watazingatia njia zao mbaya, kwamba wanafanya juhudi dhaifu sana za kujifunza katika shule ya Kristo na kutenda upole na unyenyekevu wa moyo kama wa Kristo? Walimu wanapaswa wao wenyewe kuwa na utiifu kwa Yesu Kristo, na kuyatenda maneno yake daima, ili wapate kuwa kielelezo cha tabia ya Yesu Kristo kwa wanafunzi. Hebu Nuru yenu na iangaze katika mema katika kukesha na kuwatunza wana-kondoo wa kundi kwa uaminifu; kwa saburi, kwa upole, na upendo wa Yesu katika mioyo yenu. {FEsw 269.1}

Kuwaweka vijana wa kiume na wa kike katika eneo hilo, ambao hawajakuza upendo wa kina, wa dhati kwa Mungu na kwa Roho ambazo ajili yake ambaye Kristo alikufa, ni kufanya kosa ambalo litasababisha kupoteza nafsi nyingi za thamani. Mwalimu anahitaji kujihusisha na ushawishi wa Roho wa Mungu. Mtu

ambaye atakuwa na papara na amekasirika, asiwe mwalimu. Walimu lazima wazingatie kuwa wanashughulika na watoto, si wanaume na wanawake. Wao ni watoto ambao wana kila kitu cha kujifunza, na ni ngumu zaidi kwa wengine kujifunza kuliko wengine. Msomi asiye na akili duni anahitaji mengi zaidi ya kutia moyo kuliko anavyopokea. Ikiwa walimu watawekwa juu ya hizi akili mbalimbali, ambao kwa asili hupenda kuagiza na kuamuru na kujitukuza wenyewe katika mamlaka yao, ambao watashughulikia kwa upendeleo/ubaguzi, na kuwa na wanafunzi ambao ni 'wapendwa wao/favorties' ambao watawaonesha upendeleo, wakati wengine hutendewa kwa ukali na ujeuri, watatengeneza hali ya kuchanganyikiwa, machafuko na kutotii. Walimu ambao hawajabarikiwa na tabia zenye uzoefu wa kupendeza na uliosawazishwa wanaweza kuwekwa kubeba jukumu la watoto na vijana, lakini kosa kubwa hufanywa kwa wale ambao wanaowaelekeza. Wazazi lazima wafikie hatua ya kuona jambo hili kwa Nuru tofauti. Ni lazima wajisikie kuwa ni wajibu wao kushirikiana na mwalimu, kuhimiza nidhamu ya hekima, na kumwomba sana yeye anayewafundisha watoto wao. Hautawasaidia watoto kwa kuwafadhaisha, kuwakemea, au kuwakatisha tamaa; wala hamtatenda sehemu nzuri katika kuwasaidia kuasi, na kuwafanya wasiotii, wasio na fadhili na wasiopenda kwa sababu ya Roho mnayooendeleza. Ikiwa nyinyi ni Wakristo kweli, mtaambatana na Kristo aishiye, na Roho Yake Yeye aliyetoa uhai Wake kwa wenye dhambi; na hekima ya Mungu itawafundisha katika kila jambo la dharura namna ya kufuata. {FEsw 269.2}

Watoto wanahitaji kuwa na kanuni thabiti, imara na kanuni hai ya haki ikifanywa juu yao na kutendwa mbele yao. Hakikisha unaacha Nuru ya Kweli iangaze mbele ya wanafunzi wako. Nuru ya mbingu inahitajikaa. Kamwe usiruhusu ulimwengu kuwa na maoni kuwa Roho yako na ladha na matamania yako sio ya juu na ya utaratibu safi kuliko ya walimwengu. Ikiwa wewe katika vitendo vyako unaacha hisia hii kwao, unaacha Nuru ya uongo, ya udanganyifu iwaongoze kwenye uharibifu. Baragumu lazima itoe sauti fulani. Kuna mstari mpana, wa wazi na wa kina uliowekwa na Mungu wa milele kati ya wenye haki na wasio haki, wacha Mungu na wasiomcha Mungu; kati ya wale wanaotii amri za Mungu na wale wasiziotii. {FEsw 270.1}

Ngazi ambayo Yakobo aliiona katika maono ya usiku, msingi wake Umesimama juu ya ardhi, na kilele kikifika mpaka mbingu za juu; Mungu Mwenyewe juu ya ngazi, na Utukufu wake ukiangaza kwa kila hatua ya ngazi; malaika wakipanda na kushuka juu ya ngazi hii ya Nuru inayoangaza, ni ishara ya mawasiliano ya mara kwa mara yaliyowekwa kati ya ulimwengu huu na ulimwengu wa Roho. Mungu anatimiza Mapenzi Yake kupitia utendaji wa malaika wa Mbinguni daima wakishirikiana na ubinadamu. Ngazi hii inaonyesha njia ya moja kwa moja na muhimu ya mawasiliano na wakazi wa dunia hii. Ngazi iliwakilisha kwa Yakobo Mkombozi wa ulimwengu, anayeunganisha dunia na Mbinguni pamoja. Kila mtu ambaye ameona ushahidi na Nuru ya Ukweli na kuukubali ule Ukweli, akikiri imani

yake katika Yesu Kristo, ni mmishonari kwa maana ya juu kabisa ya neno hili. Ni mpokeaji wa hazina za Mbinguni, na ni wajibu wake kuwapa, kueneza hiyo ambayo ameipokea. {FEsw 270.2}

Kisha kwa wale wanaokubaliwa kuwa walimu katika shule zetu kumefunguliwa shamba kwa ajili ya kazi na kulima, kwa ajili ya kupanda mbegu na kwa ajili ya kuvuna nafaka iliyoiva. Ni nini kinaweza kuridhisha zaidi kuliko kuwa watenda kazi pamoja na Mungu katika kuelimisha na kuwafundisha watoto na vijana kumpenda Mungu na kushika amri Zake? Waongoze watoto unaowafundisha katika shule ya kutwa na shule ya Sabato kwa Yesu. Ni nini kinachoweza kukupa furaha kubwa kuliko kuona watoto na vijana wakimfuata Kristo, Mchungaji mkuu, anayetoa wito, na kondoo na wana-kondoo huisikia sauti Yake na kumfuata? Ni Nini inaweza kueneza Nuru na uchangamfu zaidi kupitia nafsi yenye nia, mtendakzzi aliyojitolea kuliko kujua kwamba kazi yake ya subira ya kudumu si ya bure katika Bwana, na kuwaona wanafunzi wake wakiwa na Nuru ya furaha ndani ya nafsi zao kwa sababu Kristo amewasamehe dhambi zao? Nini kinaweza kumridhisha zaidi mtenda kazi pamoja na Mungu, kuliko kuona watoto na vijana wanaupokea mvuto wa Roho wa Mungu katika heshima na ubora wa Kweli wa tabia na katika kurejesha sura ya kimaadili ya Mungu—Watoto wanaotafuta amani inayotoka kwa Mfalme wa amani? Je ile, Kweli ya Mungu ni utumwa? Ndiyo, kwa maana nyingine inaweza kuonekana hivyo; kwani unazifunga nafsi zilizo tayari kufungwa - yaani kujisalimisha kwa Yesu Kristo, wakiinamisha mioyo yao kwa upole wa Yesu Kristo. Lo! ina maana kubwa aaidi ya akili zenye kikomo zivyoweza kuelewa, kumwasilisha katika kila juhudi ya umishonari Yesu Kristo na Yeye Aliyesulubiwa. “Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu, Alichubuliwa kwa maovu yetu: adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake, na kwa kupigwa Kwake sisi tumepona.” “Yeye asiyejua dhambi alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yetu; ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika Yeye.” Huu unapaswa uwe mzigo wa kazi yetu. Ikiwa yoyote anadhani ana uwezo wa kufundisha katika shule ya Sabato au ya kutwa elimu ya sayansi, anahitaji kwanza kujifunza hofu ya Bwana, ambayo ni mwanzo wa hekima, ili apate kuwafundisha hii sayansi ya juu kuliko zote. {FEsw 271.1}

“Na uzima wa milele ndio huu, wakujue Wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma.” “Maneno uliyonipa nimewapa wao; na wakayapokea nao, wakajua hakika ya kuwa nalitoka Kwako, wakasadiki ya kwamba Ndiwe uliyenituma.” Hapa kuna kazi iliyowekwa mbele yetu, kuwa wawakilishi wa Kristo, kama Yeye katika ulimwengu wetu alivyokuwa mwakilishi wa Baba. Tunapaswa kufundisha Maneno tuliyopewa katika mafundisho ya Kristo. “Maneno uliyonipa nimewapa wao.” Tuna kazi yetu, na kila mwalimu wa vijana wa uwezo wowote anapaswa kupokea kwa moyo mwema na mnyofu kile ambacho Mungu amefunua na kuandika katika Neno Lake takatifu katika mafundisho ya Kristo, kwa upole kuyakubali Maneno ya uzima. Tuko katika siku ya mfano ya Upatanisho/Atonement, na sio tu kwamba tunapaswa kunyenyekeza mioyo yetu mbele za Mungu na

kuungama dhambi zetu bali tunapaswa, kwa vipaji vyetu vyote vya kuelimisha, tutafute kuwaelekeza wale tunaokutana nao, na kuwapa kwa kanuni na mfano kumjua Mungu na Yesu Kristo ambaye Amemtuma. {FEsw 272.1}

Lo! natamani sana kwamba Bwana wa Mbinguni angefungua macho ya wengi ambayo sasa ni vipofu, wapate kujiona kama Mungu anavyowaona, na kuwapa utambuzi wa kazi inayopaswa kufanywa katika mashamba ya kazi. Lakini sina tumaini kama maoni yote nitakayotoa yatafaa, isipokuwa Bwana amezungumza na nafsi na kuandika madai Yake juu ya bamba za moyo. Je, kila wakala aliye hai wa kibinadamu hatakuwa na utambuzi wa juu na uliotukuka kuhusu maana ya kuwa na uwanja mkubwa na muhimu wa kazi ya umishonari wa nyumbani uliowekwa kwake, bila ulazima wa kwenda nchi za mbali? Na ijapolkuwa baadhi lazima watangaze ujumbe wa rehema kwa wale walio mbali, kuna wengi wanaopaswa kutangaza ujumbe kwa wale walio karibu nao. Shule zetu zinapaswa za kuelimisha ili kuwaandaa vijana kufaaa kuwa wamisionari kwa maagizo na mfano. Hebu anayeigiza katika uwezo wa mwalimu daima akumbuke kuwa vijana na watoto hawa wamenunuliwa kwa damu ya Mwana wa Mungu. Lazima waongozwe kumwamini Kristo kama Mwokozi wao binafsi. Jina la kila Muumini anuwai limechorwa kwenye vitanga vya mikono Yake. Mchungaji Mkuu hutazama chini kutoka Patakatifu pa Mbinguni kondoo wa malisho Yake. “Huwaita kondoo Wake kwa majina, na kuwaongoza.” “Kama mtu akitenda dhambi, tunaye Mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo mwenye haki.” Tazama, Ukweli wa thamani, uliobarikiwa! Hashughulikii jambo moja kwa kutojali. {FEsw 272.2}

Mfano Wake wa kuvutia wa mchungaji mwema unawakilisha jukumu la kila mhudumu na kila Mkristo ambaye amekubali cheo cha kuwa mwalimu wa watoto na vijana na mwalimu wa wazee kwa vijana, katika kuwafunulia Maandiko. Ikiwa mmoja atapotoka kutoka zizini, **hafuatwi kwa maneno makali na kwa mjeledi**, bali na mwaliko unaoshinda wa kurudi. Tisini na tisa ambao hawakuwa wamepotea hawakuhitaji huruma, na upendo wa mchungaji. Bali mchungaji anawafuata kondoo na wana-kondoo waliomsababishia wasiwasi mkubwa na kuteka huruma Yake. Mchungaji mpendwa, asiyejali maslahi yake mwenyewe namwaminifu anawaacha kondoo wengine wote, na moyo wake wote na nafsi yake yote na nguvu zake zote hutumika kumtafuta huyo mmoja aliyepotea. Na kisha humsifu Mungu-mchungaji anarudi pamoja na kondoo, akiwa amembeba mikononi mwake, akishangilia kwa kila hatua; anasema, “Furahini pamoja Nami; kwa kuwa nimempata kondoo wangu aliyepotea. Ninashukuru sana katika mfano huu, kondoo anapatikana. Na hii ndilo somo ambalo mchungaji anapaswa kujifunza—mafanikio katika kuwaleta kondoo na kuwarejesha. {FEsw 273.1}

Hakuna taswira iliyotolewa katika fikira zetu kuhusu mchungaji mwenye maumivu akirudi bila kondoo. Na Bwana Yesu anatangaza furaha ya mchungaji na furaha Yake katika kupata kondoo huleta furaha na shangwe Mbinguni miongoni

mwa malaika. Hekima ya Mungu, nguvu Zake na upendo Wake, havina kifani. Ni uhakikisho wa kimbingu kwamba hakuna hata mmoja wa kondoo na wana-kondoo wanaopotea ambaye ni kupuuzwa, na hakuna aliyeachwa bila msaada. Mnyororo wa dhahabu - rehema na huruma ya uweza wa Bwana—hupitishwa kwa kila moja ya Roho hizi zilizo hatarini. Je, basi, kwanini wakala wa kibinadamu asishirikiane na Mungu? Je, hatakuwa ametenda dhambi, mwenye kushindwa, mwenye kasoro katika tabia mwenyewe, bila kujali tabia ya hiyo nafsi iliyo tayari kuangamia (haijalishi tabia ya kondoo aliyepotea, yeye anapaswa kuitafuta)? Kristo amemuunganisha huyu na kiti Chake cha enzi cha milele kwa kuutoa uhai Wake Mwenyewe. {FEsw 274.1}

Maelezo ya Zekaria juu ya Yoshua, kuhani Mkuu, ni yenye kudokeza uwakilishi wa mwenye dhambi ambaye Kristo anampatanisha ili aweze kuletwa kwenye toba. Shetani amesimama mkono wa kuume wa Mwombezi, akipinga kazi ya Kristo, na kusihi mtu huyo ni mali yake, kwa kuwa amemchagua kuwa mtawala wake. Lakini Mlinzi wa mwanadamu, Mrejeshaji, Mwenye nguvu kuliko aliye hodari, husikia madai ya Shetani, na kumjibu: "Bwana na akukemee Ewe Shetani; naam, BWANA aliyechagua Yerusalemu, na akukemee; je, hiki si kinga kilichotolewa motoni? Basi Yoshua alikuwa amevaa nguo na chafu sana naye alikuwa akisimama mbele ya malaika. Naye huyo akajibu akawaambia wale waliosimama mbele yake, akisema, Mvueni nguo hizi zenye uchafu. Kisha akamwambia yeye, Tazama, **Nimekuondolea** uovu wako, nami nitakuvika mavazi ya thamani nyingi. Nikasema, Na wampige kilemba kizuri juu yake kichwa chake. Basi wakampiga kilemba kizuri juu ya kichwa chake, wakamvika mavazi naye malaika wa BWANA akasimama karibu." {FEsw 274.2}

Kumbuka, kila mwalimu anayechukua jukumu la kushughulika na akili za wanadamu, kwamba kila mtu ambaye ana mwelekeo wa kukosea na hujaribiwa kwa urahisi, huyo ndiye mboni ya jicho Lake Kristo au muhusika pekee ambaye Kristo ni mtetezi kwake. Wenye afya hawahitaji tabibu, bali walio hawawezi. Mwombezi Mwenye huruma anasihi, na je wadhambi, wenye ukomo, wale wanaume na wanawake wataipiga teke au kuisukumilia mbali nafsi hii moja? {FEsw 275.1}

Je, mwanamume au mwanamke yeyote atakuwa asiyejali nafsi hizo ambao Kristo anasihi katika nyua za Mbinguni? Je, wewe katika kwa matendo yako, utawaiga Mafarisayo, ambao walikuwa hawana huruma, na Shetani, ambaye ni mshitaki na mwenye kuharibu? Lo! Je, mnaweza kunyenyekeza nafsi zenu mbele za Mungu, na kuruhusu mshipa huo mkali wa fahamnu na chuma ngumu kutiishwa na kuvunjika? {FEsw 275.2}

Ondoka mbali na sauti ya Shetani na kutenda mapenzi yake huyo, nawe usimame upande wa Yesu, ukiwa na sifa Zake Yeye, Mwenye shauku, huruma na uelewa mwororo, ambao unaweza kuwafanya kesi za wenye dhiki, na wanaoteseka kuwa zake mwenyewe. Mtu ambaye amesamehewa sana atapenda sana. Yesu ni

mwombezi Mwenye huruma, Mwenye rehema na kuhani mkuu mwaminifu. Yeye, Mkuu wa Mbinguni Mfalme wa Utukufu anapomtaazama mwanadamu mwenye kikomo, na aliye chini ya majaribu ya Shetani, Mwenyewe kwasababu akiwa duniani anazihisi nguvu za hila za Shetani. Na “Hivyo ilimpasa Yeye kufananishwa na ndugu Zake katika mambo yote [kuuvika Uungu Wake na ubinadamu], apate kuwa Kuhani Mkuu Mwenye rehema, mwaminifu katika mambo ya Mungu, ili afanye suluhu kwa dhambi za watu. Na kwa kuwa mwenyewe aliteswa alipojaribiwa, aweza kuwasaidia wao wanaojaribiwa.” {FEsw 275.3}

Kisha nawaomba, ndugu zangu, jizoezeni kufanya kazi kwa namna ambayo Kristo alifanya kazi. Kamwe msivae vazi la ukali na kulaani na kushutumu na kuwafukuza kutoka zizini hao walio maskini, wanadamu waliojaribiwa; bali kama watenda kazi pamoja na Mungu, waponyeni wanaougua kiroho. Hili utalifanya ikiwa una nia ya Kristo. “Kwa kuwa hamna kuhani mkuu asiyeweza kuchukuliana nasi katika mambo yetu ya udhaifu; bali Yeye alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote, bila kufanya dhambi.” “Je, wewe hukujua? hukusikia? Yeye Mungu wa milele, Bwana, Muumba miisho ya dunia, hazimii wala haichoki? Akili Zake hazichunguziki.” {FEsw 275.4}—Christian Education, 161 {1893}.

Sura ya 36

KUSIMAMISHWA SHULE KWA WANAFUNZI (SUSPENSION)

Jambo moja nataka muelewe, kwamba sikubaliani na kufukuzwa kwa wanafunzi shuleni, isipokuwa upotovu wa kibinadamu na uasherati mkubwa uliifanye iwe lazima, ili wengine wasiharibiwe. Kumekuwa na hitilafu katika kuwafukuza wanafunzi kutoka shuleni kama ilivyokuwa kwa___ na kwa_, na kesi nyinginezo, ambazo zimekuwa uovu mkubwa, na Roho zilizotendewa hivyo zimefungua mbele yao hatua ambayo imewaweka katika safu ya adui kama maadui wenye silaha na waliotayarishwa. Tena, kuhusu kutengeneza hadharani makosa ya wanafunzi shuleni, -nimeletwa katika kuona na kusikia baadhi ya maonyesho haya, na kisha kuonyeshwa ushawishi na mfichuo huo baada ya hilo, na umekuwa na madhara kwa kila hali, na hakuna ushawishi wa manufaa kwa shule. Kama wale waliohusika katika mambo haya walikuwa na Roho na hekima ya Kristo, wangekuwa nayo tiba na njia ya kuona na kurekebisha matatizo yaliyopo kama Mfano wa Yesu Kristo. Kamwe haimsaidii mwanafunzi kudhalilishwa mbele ya shule nzima. Inajenga jeraha ambalo linaumiza/linafisha. Haiponyi chochote, haitibu chochote. Kuna wanafunzi waliokatishwa masomo. Wako katika hatua hii wamesukumwa kwenye uwanja wa vita wa Shetani kukabiliana nao enzi na mamlaka bila silaha wala ulinzi, ili kuwa mawindo rahisi ya hila za Shetani. Acha niseme neno nawe kwa jina ya Bwana. Wakati kuna njia sahihi inachukuliwa katika kesi ambapo wanafunzi wanaonekana kupotoshwa kwa urahisi, hakutakuwa na ulazima wowote wa

kusimamishwa au kufukuzwa. Ipo njia iliyo sawa, na Roho wa Bwana lazima ashughulike na wakala wa kibinadamu la sivyo kutakuwa makosa ya kutisha yatakayofanywa. Kama kuna kazi nzuri zaidi ambayo imewahi kufanywa na wakala wa kibinadamu, ni ile ya kushughulika na akili za wanadamu. Walimu wanapaswa kuzingatia kwamba hawashughulikii na malaika, bali wanadamu wenye tamaa za kimwili kama wao wenyewe. Wahusika hawajaundwa wakifana kama mapacha au kutoka kwenye mkungu mmoja. Kuna kila awamu ya tabia inayopokelewa na watoto kama urithi. Kasoro na fadhila katika sifa za tabia zinafichuliwa hivyo. Hebu kila mwalimu azingatie hili. Ulemavu wa kurithi na uliokuzwa wa tabia ya binadamu, kama vile ulivyo uzuri wa tabia, lazima mwalimu atakutana nazo, na neema nyingi yapawa kukuzwa kwenye haiba ya mwalimu ili kujua jinsi ya kukabiliana na waliokosea kwa faida yao sasa na wema wa milele. Msukumo, uchoyo, kutokuwa na subira, kiburi, ubinafsi, na umimi, ikiwa vitatunzwa, vitafanya kiasi kikubwa cha uovu ambao unaweza kuisukuma Roho juu ya uwanja wa vita vya Shetani bila hekima ya kuiongoza merikebu ya kiroho, naye atakuwa katika hatari ya kurushwa huku na huko kwenye mchezo wa majaribu ya Shetani hadi kuvunjikiwa meli yake ya imani. Kila mwalimu ana tabia zake za kipekee anazopaswa kuziangalia ili Shetani asije akamtumia kama wakala wake wa kuharibu Roho, kwa ajili ya tabia yake mwenyewe isiyowekwa wakfu. Usalama pekee kwa walimu ni kujifunza kila siku katika shule ya Kristo, upole Wake, unyenyekevu wa moyo, ndipo nafsi itafichwa ndani ya Kristo; na kwa upole ataivaa nira ya Kristo, na kuzingatia kwamba yuko hapo kushughulika na urithi wake. Lazima niseme kwako kwamba nimeonyeshwa kuwa njia bora hazijachukuliwa kila wakati katika kushughulikia makosa na madhaifu ya wanafunzi, na matokeo yake ni kwamba Roho zimehatarishwa na zingine zimepotea. Hasira zenye uovu kwa walimu, harakati zisizo za busara, kujilinda nafsi, vimefanya kazi mbaya. Hakuna namna ya uovu, kwenye udunia au ulevi, ambao utafanyakazi mbaya zaidi juu ya mhusika, na kuhuzunisha nafsi, na kuiweka katika kufundisha maovu yashindayo mema, kuliko tamaa za mwili za kibinadamu zisizo chini ya udhibiti wa Roho wa Mungu. Hasira, kuguswa, kuchochewa, havilipi kamwe. Ni wana wapotevu wangapi wanaowekwa nje ya ufalme wa Mungu kwa tabia isiyopendeza au mbaya ya wale wanaodai kuwa wao ni Wakristo. Wivu, husuda, kiburi, na hisia zisizofaa, kujihesabia haki, hasira za upesi, kufikiri mabaya, ukali, ubaridi, kutokuwa na huruma, hizi ni sifa za Shetani. Walimu watakutana na vitabia hivi ndani kwa wanafunzi. Ni jambo la kutisha kuwa na tabia hizi na kushughulika nazo; lakini katika kutafuta kufukuza maovu haya, mtenda kazi amechafua moyo wake ndani kwa tabia hizo hizo mbaya (tabia za mtoto mwalimu ni sawa), nazo zimeharibu nafsi ya yule mwanafunzi ambaye mwalimu anashughulika naye. {FEsw 277.1}

Kwa kweli hakuna mahali Mbinguni penye nafasi ya tabia hizi. Mtu mwenye tabia kama hiyo ataifanya mbingu kuwa mahali pa masikitiko, kwa sababu yeye mwenyewe hana furaha. “Msipozaliwa mara ya pili,” Kristo alisema, “ninyi hawezi

kuingia katika ufalme wa Mbinguni.” Ili kuingia Mbinguni, Kristo lazima aumbwe ndani ya mtu kwa tabia, na tumaini la Utukufu, na kisha yeye achukue tabia hiyo Mbinguni pamoja naye. Bwana Yesu pekee Ndiye anayeweza kuumba na kubadilisha tabia. Kwa kupungukiwa ustahimilivu, utu wema, uvumilivu, ubinafsi na upendo, mfichuo wa sifa hutoa kimulimuli kwa dunia bila hata hiari ya mtu wakati ambapo amejisahau kuwa kwenye lindo lake, na maneno yasiyo ya Kikristo, na tabia ya kutofanana na Kristo inalipuka kama bomu nyakati fulani hadi kuangamiza nafsi. "upendo Haufurahii uovu." Tia alama hapo. Mtume alimaanisha pale ambapo kuna kusitawishwa kwa upendo wa Kweli kwa ajili Yake kwa zile nafsi za thamani, hali hiyo itaonyeshwa kwa wale wanaohitaji zaidi hiyo subira ambayo ina uvumilivu na fadhili, na upendo hautakuwa tayari kukuza hata kidogo kosa la mtu au kuelekeza kosa katika makosa makubwa ambayo hayawezi kusamehewa, na hautachukua makosa ya wengine kuwa mtaji. Upendo kwa Roho ambazo Kristo alikufa kwazo hautachukua yale makosa ambayo yamefanyika kwa ajili ya uelewa mbaya au ujinga na kisha kuuweka udhaifu huo hadharani mbele ya shule nzima. Unafikiri kwa jinsi gani Yesu ameangalia shughuli kama hizo? Angekuwa hapa sasa angaliwaambia wale wanaofanya mambo haya, “Ninyi hamjui Maandiko wala uweza Wake Mungu.” Kwa maana katika Maandiko nimeonyeshwa kwa uwazi jinsi ya kukabiliana na mkosaji. Uvumilivu, kutafakari kwa fadhili, na “Jifikirie nafsi yako usije ukajaribiwa wewe mwenyewe,” ndiyo maneno ambayo yangekutana na moyo mgumu, usiojisalimisha na wenye ukaidi. Upendo wa Yesu utafunika wingi wa dhambi, ili wasimnyatie mkosaji ili kumrarua wala wasianikwe kwenye kujiundia hisia za kila mstari na tabia zilizo kwenye kifua cha mwanadamu yule ambaye makosa na maovu yake wanayaanika wazi, na kwa yule wanayemshughulikia hivyo. Mara nyingi sana anasukumwa na kujitakia tamaa au kutindikiwa. Akili yake sasa haiwezi kufikiwa na uponyaji tena. Sasa kazi inayopaswa kutendeka ni kuwa na neema ya Kristo katika nafsi ambayo haitawahi kuwa na hatia ya kufichua makosa ya mtu mwingine, isipokuwa kuna hitaji chanya. Fanya mazoezi katika mstari wa Kristo. Shahidi wa Kweli anazungumza katika [Ufunuo 21:5](#). Fanya mazoezi ya upendo. Hakuna kitu katika Ukristo ambacho kinamsukuma kwa ukorofi usiotabirika. ([Ufu 12:5](#). Na Yeye aketiye juu ya kile kiti cha enzi akasema, Tazama, nayafanya yote kuwa mapya. Akaniambia, Andika ya kwamba Maneno hayo ni amini na Kweli.) **{FEsw 279.1}**

Endapo mtu hatatumia mkono wake, basi huo mkono unakuwa dhaifu na wenye upungufu kwenyenguvu ya misuli. Isipokuwa Mkristo afanye mazoezi yake ya kiroho kwa nguvu, basi hatapata nguvu za tabia, hatakuwa na nguvu ya tabia njema za maadili. Upendo ni mmea wa thamani sana na ni lazima upaliliwe na kujaliwa iwapo utastawi. mmea wa thamani wa upendo unapaswa kutendewa kwa upole (kufanyiwa mazoezi), na hivyo watakuwa mashujaa, hodari na matajiri katika kuzaa matunda, wakitoa harufu njema ya tabia kwa mhusika mzima. Tabia kama ya Kristo si ya ubinafsi, uchoyo, isiyo na fadhila au upole, na haitaumiza Roho za wale

wanaotaabika na majaribu ya Shetani. Itaingia katika hisia za wale ambao wanajaribiwa kwamba mitihani na kisha majaribu yatadhibitiwa na kisha kuleta dhahabu kuonekana katika maisha yao, na pia kuteketeza takataka wakati wa kusafisha hiyo dhahabu kabulini. Haya ndiyo mazoezi ambayo Mungu ameweka kwa wote. Katika shule hii ya Kristo, wote wanaweza kujifunza masomo yao ya kila siku, walimu na wanafunzi, kuwa na subira, unyenyekevu, mkarimu, ubora na uungwana. Ninyi nyote mtalazimika kumtafuta Mungu kwa dhati na bidii zaidi, na kwa maombi yaliyochanganyikana na imani iliyo hai, na mkono wa Mungu unaofinyangwa tabia utaweza kuleta sura Yake Mwenyewe katika mwenendo wako. Majaribu yatakuja, lakini siyo ya kukuletea kushindwa. Lakini kupitia njia ya neema inayopatikana katika kufungua moyo wako unaposikia sauti ya Yesu akibisha mlango, tabia ya Kikristo na uzoefu huo utaongezeka kwa kukua kwa uzuri zaidi, na ukifanana na mbingu. Hebu tukumbuke kwamba tunashughulika na nafsi ambazo Kristo amezinunua kwa gharama za Kwake zisizo na ukomo. Jamani, waambieni wakosefu Mungu anawapenda, Mungu alikufa kwa ajili yako. Lieni juu yao, ombeni pamoja nao. Mwageni machozi juu yao, lakini usifanye kuwakasirikia. Wao ni mali iliyonunuliwa na Kristo. Hebu kila mtu atafute tabia ambayo itadhihirisha upendo katika matendo yake yote. “Yeyote atakayemkosesha mmojawapo wa wadogo hawa waniaminio, ingekuwa afadhali kwake jiwe la kusagia lifungiwe shingoni mwake. na kwamba angezama katika vilindi vya bahari.” Ilikuwa bora zaidi kutoishi kuliko kuishi siku baada ya siku bila upendo huo wa Kristo amefunua katika tabia Yake, na amewausia watoto Wake. Kristo alisema, “Mpendane kama Mimi nilivyowapenda ninyi.” Tunaishi katika ulimwengu mgumu, usio na hisia, usio na hisani. Shetani na vibaraka wake wanajaribu kila ustadi ili kuzidanganya Roho ambazo Kristo ametoa maisha Yake ya thamani kwa ajili yao. Kila anayempenda Mungu kwa unyofu na Ukweli, atazipenda Roho ambazo Kristo alizifia. Ikiwa tunataka kufanya mema kwa Roho, mafanikio, na kuthamini kwetu Roho hizi kutakuwa sawa na imani yao kwetu, na thamani yao kwetu. Heshima inayoonyeshwa kwa Roho ya mwanadamu inayohangaika ndiyo njia ya uhakika kupitia Yesu Kristo ya kurejesha heshima na kujithamini kwa mtu huyo aliyepoteza utu wake. Mawazo yetu ya kile atakachokuwa mbeleni, yanaweza kuwa msaada ambao sisi wenyewe hatuwezi kuthamini kikamilifu. Kila saa tunahitaji neema tele ya Mungu, nasi tutakuwa na tajiriba, na uzoefu wa vitendo, kwani Mungu ni upendo. Yeye anayekaa katika upendo, hukaa ndani ya Mungu. Wape upendo wale wanaohitaji zaidi. Wale wenye maafa au shida zaidi, wale ambao wana kutokubalika na tabia zisizopendeza au kuchukiza, wanahitaji upendo wetu, upole wetu, huruma yetu. Wale wanaojaribu uvumilivu wetu wanahitaji upendo zaidi. Tunapita duniani mara moja tu; jambo lolote jema tunaloweza kulifanya, tunapaswa kulifanya kwa dhati na bidii zaidi, bila ya kuchoka, tukiwa na Roho ile ile kama inavyosemwa na Kristo katika kazi Yake. Naye hatashindwa wala hatakatishwa tamaa. Wale watu welio na tabia ujeuri, ukali, ukaidi, chuki, kuzira, hasira za

kirahisi na wenye mudimudi (moodymood) ndio wanaohitaji msaada zaidi. Hawa wanawezaje kusaidiwa basi? Ni kwa ule upendo tu uliojizoesha katika kushughulika nao, ambao Kristo alimfunulia mwanadamu aliyeanguka. Unaweza kusema watendee, kama wanavyostahili. Je, kama Kristo angetutendea jinsi tunavyostahili, Je, ingekuwaje? Yeye, asiyestahili, alitendewa kama sisi tunavyostahili. Bado sisi tunatendewa na Kristo kwa neema na upendo jinsi tusivyostahili bali kama Yeye alivyostahili. Ukiwatendea watu wa tabia tete kama unavyodhani ndivyo wanastahili hawa, basi wewe utakatilia mbali uzi wa matumaini yao ya mwisho, na kuharibu ushawishi wako na kisha uiharibu hiyo Roho. Je, kuna faida kweli ya kufanya hivi? Hapana, nasema hapana, mara mia hapana. Zifunge Roho hizi zinazohitaji msaada wako, karibu nawe, kwa upendo wote unaoweza kuzipa, upendo wenye huruma, na sikitiko, unaofurika kama ule wa Kristo, nawe utaokoa Roho kutoka kwenye mauti na kuficha wingi wa dhambi. Je, halitakuwa jambo bora zaidi kwetu kuanza mchakato huu upendo? {FEsw 280.1}

Uwe mwangalifu kwa kile unachofanya katika mstari wa kuwasimamisha wanafunzi shule (kuwaambia warudi nyumbani kwa muda kama adhabu-suspension). Hili ni jambo zito. Adhabu hii itolewe tu kwa kosa lile ambalo ni kubwa sana kuhitaji nidhamu hii. Kisha hali zote zinazohusiana na kesi hiyo zinapaswa kuzingatiwa kwa uangalifu. Wanafunzi wa mbali na wa karibu, waliotumwa na wazazi wao kutoka nyumbani, maelfu na maelfu ya maili kwa umbali na kunyimwa faida za nyumbani, na ikiwa watafukuzwa na kurudi nyumbani, watanyimwa faida za shule. Gharama zote zinazotumika katika shughuli hii ya kusafiri n.k zinashughulikiwa na wale ambao walikuwa na matumaini na ujasiri kwamba pesa zao hazitawekezwa bure bure hivi tu. Mwanafunzi anaingia, au anaanguka, katika majaribu, naye anapaswa kuadhibiwa kwa kosa lake. Anahisi kabisa kwamba rekodi yake imeharibiwa, na kwamba amewaangusha wale ambao wamemwamini katika kukuza tabia yake chini ya ushawishi wa mafunzo yake katika maisha yake ya kielimu, ambayo yatampa faida kutokana na yale yote ambayo yamewekezwa kwa niaba yake. Lakini sasa anasimamishwa shule kwa mwenendo wake wa kipumbavu. Je, Atafanya nini? Ujasiri wake uko kwenye hali ya chini kabisa, ujasiri na hata uanaume/utu wake hauthaminiwi. Anaingia gharama na familia yake, na wakati wa thamani hupotea. Ni nani aliye mpole na mkarimu, na ambaye anahisi mzigo wa Roho hizi? Hatuoni ajabu kwamba Shetani huchukua faida ya hali hii iliyojitokeza. Vijana hawa wanasukumwa kwenye uwanja wa vita wa Shetani na hisia mbaya sana za moyo wa mwanadamu huitwa katika zoezi na kuimarishwa na kisha kuthibitishwa. Naziweka kesi hizi kama zilivyokuwa zimewasilishwa kwangu. Natamani wote wangeliona hili kama lilivyo katika pembe zake zote. Kisha kungelikuwa na mabadiliko makubwa katika sheria nyingi na mbinu za kushughulika na akili za mwanadamu. Kungekuwa matabibu zaidi wa kuponya Roho za wanadamu, wanaoelewa jinsi ya kuchukuliana na akili za binadamu. Kungekuwa na kutoa msamaha kwingi zaidi, huruma na upendo kwa

vitendo, kutokatisha wanafunzi tamaa, na kutoraura-rarua ushawishi unaotumiwa. Kama Kristo angeshughulika hivi na wanawe na binti Zake wote wanaojifunza Kwake, kama wakala wa kibinadamu unavyofanya, kama walimu wanavyowa shughulikia wale walio chini ya usimamizi wao; kwamba wakati sheria ya Bwana, kipimo Chake, na maagizo yake yamepuuzwa nasi, sisi kama wakosefu hufukuzwa au kusimamishwa, Naye awafukuze wakosefu kutoka kwenye ushawishi wake wa kuokoa, kuinua, kuelimisha, na kumwacha yule mkosefu kuchagua njia na mwenendo wake mwenyewe bila Msaada Wake Bwana, Je, itakuwaje basi kwa nafsi zetu? Msamaha Wake wa daima, hufunga maslahi ya nafsi zetu pamoja na Yeye Mwenyewe. Oh! Ninapoutafakari upendo mkuu wa Yesu, ninatekewa {ninachanganyikiwa}. Nira ya Kristo ni laini na mzigo Wake ni mwepesi. Tunapoingia kikamilifu zaidi kwenye upendo wa Yesu kwa vitendo, tutaona matokeo tofauti kabisa katika maendeleo yetu wenyewe kama Wakristo, na katika kuunda tabia ya wale walioletwa katika mahusiano nasi. Shughuli ngumu zaidi kwa watu binafsi ni kuacha kile ambacho mtu anadhani ni haki yake. Upendo hautafuti mambo yake. Upendo uliozaliwa Mbinguni hugusa ndani zaidi, na siyo juu juu tu. Upendo hautakabari na haujivuni. Upendo ukiimarishwa kwa neema ya Kristo, haufanyi mambo yasiyofaa, na wala haukosi adabu. Yeye akaaye katika upendo, anakaa ndani ya Mungu. Mungu ni upendo. Sote tunahitaji upendo, utu wema, kujaliwa, upole, huruma na ustahimilivu. Fukuza kutoka nafsi yako kila mabaki ya ubinafsi au kulinda hadhi yako (kutetea ubinafsi). {FEsw 282.1}

Wakati tumaini lote liliondolewa kutoka kwa Adamu na Hawa katika matokeo ya uasi na dhambi, wakati haki ilipodai kifo cha mwenye dhambi, Kristo alijitoa Mwenyewe kuwa dhabihu kwa ajili ya dhambi ya ulimwengu. Ulimwengu ulikuwa chini ya hukumu. **Kristo alifanyika kuwa mbadala na mdhamini wa mwanadamu.** Angetoa uhai Wake kwa ajili ya ulimwengu, ambao uliwakilishwa kama kondoo mmoja aliyepotea kutoka kwenye zizi, ambaye hatia moyoni, pamoja na kutokuwa na msaada lilikuwa shitaka dhidi yake, lililosimama njiani na kumzuia asirudi nyumbani. "Bali Mungu alionyesha pendo Lake Yeye Mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi." "Sisi sote kama kondoo tumepotea; tumegeuka kila mtu kwa njia yake mwenyewe; na Bwana ameweka juu Yake maovu yetu sote." Kila mwana na binti wa Mungu, aliyedumu ndani ya Kristo Mwokozi atamwiga kwa kutenda kama Kristo. Kila nafsi isiyo ndani ya Mwokozi itadhihirisha katika kutofanana na Kristo katika tabia. Upendo hautakuwa ukithaminiwa au kupendwa, wala kuwekwa katika mazoezi kwa vitendo. "Tumuinue Mwokozi aliyefufuka," kwa maneno yetu, katika mazungumzo yetu, na katika kushughulika kwetu na wakosefu. {FEsw 283.1}

Kutokana na mzigo ambao umevingirwa juu yangu, najua kwamba wengi ambao wanahudumu katika shule zetu, wao wenyewe wanahitaji kujifunza katika shule ya Kristo. Ukuu wa Kristo upole Wake, kushughulika kwake na wakosaji, huruma na upendo Wake. Mpaka wawe wameyeyuka kama dhahabu na takataka katika

taNuru la moto inapotengwa na kutolewa, walimu hao au wahusika hao watafanya kazi kwa malengo tofauti, yanayokinzana. Mimi nilihuzunika sana moyoni mwangu kwa matokeo mabaya yaliyohusu na kushughulika bila hekima, matokeo mazito zaidi kuliko wengi walivyo tayari kukubali kwenye dhamiri zao au kwa Mungu. Ubinafsi ni mkubwa sana katika mioyo ya wengi, huu ubinafsi unajitahidi kupata umahiri. Kuna wale wanaodai kuwa wafuasi wa Yesu Kristo ambao nafsi zao hazijawai kufa. Hawajawahi kuanguka kwenye mwamba na kuvunjwawunjwa. Mpaka hili litokee, hao wataishi kwa ajili ya nafsi zao tu. Na ikiwa watakufa jinsi walivyo, watakuwa wamechelewa sana kurekebisha makosa yao na kuhesabiwa haki. Nazipenda nafsi zao. Yesu anazipenda nafsi zao na atazifanyia kazi njema, ikiwa watajinyenyekeza chini ya Mkono Wake wenye nguvu, kwa kutubu na kuongoka, wakijisalimisha kila siku kwa Mungu. Yapaswa kujisalimisha daima, kujisalimisha kila siku. Lazima tuwe wanaume na wanawake wenye utayari wakati wote, daima tuwe kwenye kituo chetu cha ulinzi, na kuangalia jinsi ya kuboresha kila fursa katika kutenda mema, na mema tu kwa ajili ya nafsi ambazo kwa ajili ya hizo, Kristo ametoa maisha Yake ili kuwafanya kuwa Wake. Mwenyewe. Wakati mawakala wa kibinadamu wanashughulikia Roho hizi kwa ukali mwingi wanauhuzunisha moyo wa Kristo, na kumweka kwenye aibu ya wazi, kwa maana wanaiwakilisha vibaya tabia ya Kristo, katika tabia zao mwenyewe. Alisema mmoja, “Na unyenyekevu wako mwenyewe utanifanya kuwa mkuu..” Ninaomba kwa Baba yetu wa Mbinguni kwamba wote waliounganishwa pamoja na shule zetu waweze kuwa ndani ya Kristo kama vile tawi linavyounganishwa na Mzabibu Hai. {FEsw 284.1} —Barua ya 50, 1893.

Sura ya 37

KWA WANAFUNZI WA CHUO CHA BATTLE CREEK

Nina shauku kubwa sana katika taasisi ya elimu huko Battle Creek. Kwa miaka mingi mimi na mume wangu tulihusika sana na zoezi la kuanzisha shule ambayo vijana na watoto wetu wanapaswa kupata faida za tabia bora kuliko zile zinazopatikana katika shule za kawaida za umma, au katika vyuo vya ulimwengu. Mungu alionyesha wazi wazi jinsi tabia ya ushawishi na mafundisho ambayo shule inapaswa kudumisha, ili kwamba kazi muhimu ambayo shule iliundwa inaweza kukamilika. Kwa vile maarifa ya Bwana na hofu ya Mungu ndiyo Chanzo cha hekima,

ilikuwa ni lazima kwamba mafunzo ya Biblia yachukue nafasi kuu katika matawi mbalimbali ya elimu ya kisayansi. Kiwango cha shule kilipaswa kuwa cha hali ya juu utaratibu wa juu, na kanuni za muhimu katika ucha Mungu (utauwa) zilipaswa kuwekwa mbele ya wanafunzi kama kipengele muhimu sana katika mchakato wa elimu. “Na huu ndio uzima wa milele, wapate kujua Wewe, Mungu wa pekee wa Kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma.” Vijana walipaswa kufundishwa kuhusu nyakati ambazo tunaishi, na kufahamishwa yale yatakayotokea kabla ya kufungwa kwa historia ya ulimwengu. {FEsw 285.1}

Sababu moja kwa nini ilikuwa ni lazima kuanzisha taasisi zetu wenyewe ilikuwa kwamba wazazi hawakuweza kukabiliana na ushawishi wa mafundisho ambayo watoto wao walikuwa wakipokea hadharani shule, na kosa lililofundishwa huko lilikuwa likiongoza vijana kwenye uwongo njia. Hakuna ushawishi mkubwa zaidi ungeweza kuletwa juu ya akili ya vijana na watoto kuliko wale waliokuwa wakiwafunza katika kanuni za sayansi. Kwa sababu hii ilikuwa dhahiri kwamba shule lazima ianzishwe, ambamo watoto wetu wanapaswa kufundishwa njia ya Kweli. Katika shule zetu ilielezwa kuwa vijana wanapaswa kufundishwa katika kanuni za kiasi za Biblia, na kila ushawishi ulipaswa kuletwa juu yao ambao ungeelekea kuwasaidia waachane na upumbavu wa zama hizi mbovu, ambazo zilikuwa zikifanya haraka kuleta ulimwengu wa Sodoma ya pili. {FEsw 285.2}

Katika taasisi zetu za elimu kulikuwa na mvuto ambao ungepinga ushawishi wa ulimwengu katika mambo yafuatayo: kutia moyo kujiingiza katika hamu ya kula, kuendekeza kufurahisha hisia na nafsi, kiburi, tamaa za mwili, upendo kwa mavazi na maonyesho, kupenda kusifiwa, kutia chumvi na kutoa sifa za udanganyifu, na magomvi na mashindano kwa ajili ya vizawadi na heshima kama fidia ya kufanya masomo vizuri. Haya yote yasingepaswa kuhamasishwa kwenye shule zetu. Isingewezekana kuepuka mambo haya, kama watoto wangeenda kwenye shule za umma, ambapo ingepelekea kuwasiliana na yale ambayo yangechafua maadili yao kila siku. Ulimwenguni kote kumekuwa na upuuzaji mkubwa wa mafunzo ya nyumbani na kisha watoto walipoenda shule za umma, walipokea mafunzo waliyoyakuta huko, nao kwa sehemu kubwa, wakawa wabaradhifu wa rasilimali, na wakazama katika maovu. {FEsw 286.1}

Kazi ambayo sisi kama watu tulipaswa kufanya katika jambo hili, ilikuwa kuanzisha shule, na kufanya kazi ambayo Yesu Kristo aliongoza kutoka kwenye ile nguzo ya wingu, ambayo ilikuwa imeelekezwa kama kazi ya watu Wake, —kufundisha na kuwaelimisha watoto na vijana wetu kuzingatia amri ya Mungu. Kupuuzua waziwazi kwa sheria ya Mungu kulikofanywa na ulimwengu, kulikuwa kunachafua maadili ya wale waliodai kuwa wanatunza sheria ya Mungu. Lakini tunaitwa kufuata mfano wa Ibrahimu. Juu yake Bwana amesema, “Mimi namjua, ya kwamba atamjua Waamuru watoto wake na nyumba yake baada yake, nao watawaamuru ishike njia ya Bwana, ili kutenda haki na hukumu.” {FEsw 286.2}

Ibrahimu alilazimika kuiacha nchi yake na nyumba ya baba yake, na kukaa katika nchi ngeni, ili kuanzisha kwa ufanishi na mafanikio mapya utaratibu wa mambo katika nyumba yake. Majaliwa na utunzaji wa Mungu daima ulikuwa ukimfungulia yeye mbinu mpya na mpangilio wa mambo kila siku, na uendeleu wa mambo haya ulipaswa kufanywa kutoka kwa kizazi kwa kizazi, ili kuhifadhi katika ulimwengu ujuzi wa Mungu wa Kweli, wa sheria na amri Zake. Hii inaweza kufanyika tu kwa kusitawisha dini ya nyumbani. Lakini haikuwezekana kwa Ibrahimu kufanya hivi huku akiwa amezungukwa marafiki na jamaa zake waliokuwa waabudu sanamu. Ilikuwa ni lazima kwa amri ya Mungu atoke peke yake na kwenda, na kuisikiliza sauti ya Kristo, Kiongozi wa wana wa Israeli. Yesu alikuweco juu ya dunia ili kuwafundisha na kuwaelimisha wateule wa Mungu. Abrahamu aliamua kutii sheria ya Mungu, na Bwana alijua kwamba yeye asingeisaliti amana takatifu kwa upande wake, na wala asingejisalimisha kwa kiongozi mwingine yeyote kuliko Yeye ambaye alihisi kuwa chini ya wajibu wa kumtii. Alitambua kwamba aliwajibika kutoa mafundisho ya nyumba yake na watoto wake, naye akawaamuru baada yake watende haki, maamuzi na hukumu. Katika kuwafundisha sheria za Mungu, aliwafundisha kwamba Bwana Ndiye hakimumu wetu, mpaji sheria na Mfalme wetu, na kwamba wazazi na watoto wapaswa kutawaliwa/kuongozwa Naye; kwamba kwa upande wa wazazi pasiwepe ukandamizaji, na kwa upande wa watoto kusiwepe na uasi. {FEsw 286.3}

Bwana akamwamuru Musa kwenda kuzungumza na Farao, akimtaka awaruhusu Israeli kuondoka Misri. Kwa miaka mia nne walikuwa wameishi Misri, na walikuwa watumwa wa Wamisri. Walikuwa wamepotoshwa na ibada ya sanamu, na wakati ukafika ambapo Mungu aliwaita watoke Misri, ili wazitii sheria Zake na kuitunza Sabato Yake, ambayo aliweka katika Edeni. Alitamka zile Amri Kumi kwao kwa uzuri wa kutisha na kushangaza kutoka mlima Sinai, ili waweze kuelewa tabia takatifu na ya kudumu ya sheria za Mungu, na hivyo kujenga misingi ya vizazi vingi, kwa kuwafundisha watoto wao madai yenye mashiko ya maagizo haya matakatifu ya Mungu. {FEsw 287.1}

Hii ndiyo kazi ambayo tunaitwa kufanya. Kutoka kwenye mimbari za makanisa maarufu na yanayopendwa, siku ya kwanza ya juma ndiyo inatangazwa kuwa Sabato ya Bwana; lakini Mungu ametupa Nuru, akituonyesha kwamba Amri ya nne ya dekalojia ina **mashiko** mazito kama yalivyo maagizo mengine tisa ya Kanuni/amri hizi za Mungu. Ni kazi yetu kuweka wazi kwa watoto wetu kwamba siku ya kwanza ya juma si Sabato ya kweli, na kwamba kuendelea kuadhimishwa kwake baada ya Nuru ya kweli ya ile Sabato ya kweli kutujia, ni ibada ya sanamu, na ukinzani wa wazi wa sheria ya Mungu. Katika kuwapa maelekezo kuhusiana na madai ya sheria ya Yehova, ni lazima tuwatenganishe watoto wetu na ushirikiano na mivuto ya ulimwengu, na kuweka mbele yao Maandiko ya ile Kweli, kuwafundisha kanuni juu ya kanuni, na amri juu ya amri, ili wasikose uaminifu kwa Mungu. {FEsw 287.2}

Waprotestanti wameikubali Sabato ya uwongo/feki, yule mtoto wa upapa, na wameiinua hiyo siku, juu ya ile siku takatifu ya Mungu, iliyotakaswa; na taasisi zetu za elimu zimeanzishwa kwa ajili ya kuelezea lengo la kupinga ushawishi wa wale ambao hawafuati Neno la Mungu. Hizi ni sababu za kutosha kuonyesha umuhimu wa kuwa na taasisi zetu za elimu; kwa maana inatupasa kufundisha ile Kweli kuliko uongo na kazi za kubuni (fiction). Shule ni ya kuongezea mafunzo ya nyumbani, na kote, yaani, nyumbani na shuleni, unyenyekevu wa mavazi, chakula, na burudani/maburudisho lazima udumishwe. Mazingira lazima yaundwe, ambayo hayatakuwa mabaya kwa maadili. Mstari juu ya mstari, amri juu ya amri, watoto wetu na kaya zetu lazima waelimishwe kuishika njia ya Bwana, kusimama imara kwa ajili ya Kweli na haki. Ni lazima tudumishe msimamo dhidi ya kila aina ya hila na ujanja unaoshangaza katika enzi hii ya uharibifu, wakati makosa yamefichwa kwa kupambwa, na kuchanganyikana naile Kweli kiasi kwamba haiwezekani kwa wale ambao hawajui tofauti zinazofanywa na Maandiko kati ya mapokeo ya wanadamu na Neno la Mungu, ili kutofautisha Ukweli kutoka kwa makosa. Imesemwa kwa wazi kwamba katika enzi hii “si Roho anena waziwazi ya kwamba nyakati za mwisho wengine watajitenga na imani, wakisikiliza Roho zidanganyazo, na mafundisho ya mashetani.” {FEsw 288.1}

Ukweli unapoletwa katika maisha ya kila siku ya vitendo, kiwango kinapaswa kuinuliwa juu zaidi na zaidi, ili kukidhi matakwa ya Biblia. Hii itahitaji upinzani dhidi ya mitindo, mila, desturi, utendaji na kanuni za ulimwengu. Athari za kidunia, kama mawimbi ya maji baharini, hupiga dhidi ya wafuasi wa Kristo ili kufagilia mbali kanuni za upole na neema ya Kristo, ya ile Kweli; lakini wanapaswa kusimama imara kama mwamba wa kanuni. Ili jambo hili lifanyike, kutahitajika kuwa na ujasiri wa kimaadil, na wale ambao Roho zao hazijaelekezwa kwenye Mwamba wa milele, watazolewa na mkondo wa dunia. Tunaweza kusimama imara tu, kama maisha yetu yamefichwa pamoja na Kristo katika Mungu. Uhuru wa kimaadili utakuwa umekamilika/mkamilifu wakati wa kupinga ulimwengu. Kwa kupatana kabisa na mapenzi ya Mungu, tutawekwa juu ya ardhi nzuri, na tutaona ulazima wa kutengana na mila, desturi na mazoea ya ulimwengu huu. Hatupaswi kuinua kiwango chetu juu kidogo tu kulinganisha na kiwango cha ulimwengu; bali tunapaswa kutengeneza mstari ulio wazi kabisa wa mpaka unaonekana dhahiri. {FEsw 288.2}

Wamo wengi kanisani ambao mioyoni mwao ni wa ulimwengu, lakini Mwenyezi Mungu anawaita wale wanaodai kuwa wameamini ule Ukweli wa hali ya juu na endelevu. kupanda juu ya mtazamo wa sasa wa makanisa maarufu na yanayopendwa ya siku hizi. Kuko wapi kujikana nafsi, kuko wapi kubeba msalaba ambako Kristo alisema kunapaswa kuwatambulisha wafuasi Wake? Sababu yetu ya kuwa na ushawishi mdogo kwa jamaa na washirika wasioamini ni kwa kuwa tumedhihirisha tofauti ndogo iliyoazimiwa katika tabia/mazoea kulinganisha na zile mazoea/tabia za dunia. Wazazi wanahitaji kuamka, na kutakasa Roho zao kwa kuishi na kutenda ile Kweli katika maisha yao ya nyumbani. Tunapofikia kiwango

ambacho Bwana angetaka tufikie, walimwengu watawachukulia Waadventista Wasabato kama watu wasio wa kawaida, walioteuliwa, na wenye msimamo mkali. "Sisi ni tumefanywa kuwa tamasha kwa ulimwengu, na kwa malaika, na kwa wanadamu." {FEsw 289.1}

Tuko chini ya agano zito, na takatifu kwa Mungu katika kulea watoto wetu, sio kwa kuiweka mikono yao mikononi mwa ulimwengu, bali kumpenda na kumcha Mungu, na kuzishika amri Zake. Tunapaswa kuwaelekeza kufanya kazi kwa akili katika mistari ya Kristo, ili kuwasilisha tabia ya Kikristo iliyotukuka, iliyoinuliwa kwa wale ambao wanashirikiana pamoja nao. Hii ndiyo sababu shule zetu zilianzishwa, ili vijana na watoto wapate elimu kiasi cha kuweza kushinikiza ushawishi wao kwa ajili ya Mungu duniani. Je basi, shule zetu zigeuzwe tena na kuwa za ulimwengu, na kisha kufuata desturi na mitindo yake? "Kwa hiyo, ndugu zangu, nawasihi kwa rehema Zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu na inayompendeza Mungu, hii ndiyo ibada yenu yenye maana." {FEsw 289.2}

Wakati wale ambao wamefikia miaka ya ujana na utu uzima, hawaoni tofauti kati ya shule zetu na vyo vya ulimwengu, na hawana upendeleo juu ya ile shule wanayohudhuria, ingawa makosa yanafundishwa kwa amri, kanuni na mfano katika shule za ulimwengu, sisi tuna haja ya kuchunguza kwa karibu sababu zinazosababisha hitimisho kama hilo. Taasisi zetu za elimu zinaweza kupindishwa na kufuatisha elimu ya kidunia. Hatua kwa hatua wanaweza kusonga mbele kuelekea kwenye ulimwengu; bali wao ni wafungwa matumaini (Zek 9:2), na Mungu atawarekebisha na kuwaangazia, na kuwarejesha kwenye msimamo wao mnyoofu akiwatofautisha na ulimwengu. Naangalia kwa shauku kubwa, tukitarajia kuona shule zetu zikiwa zimejazwa kwa Roho ya dini ya Kweli na isiyo na mawaa. Wakati wanafunzi wakijazwa hivyo na Roho Mtakatifu wa Mungu, wataona kwamba kuna kazi kubwa ya kufanywa katika mistari ambayo Kristo alifanya kazi, na muda ambao wameupanga na kuutoa kwa maburudisho/burudani utatolewa kwa kufanya kazi ya umishonari wenye dhati na bidii. Watajitahidi kufanya wema kwa wote wanaowazunguka, wataziinua Roho ambazo zimeinama chini kwa kukata tamaa, na kuwaangazia wale ambao wako katika giza la upotovu. Watamvaa Bwana Yesu Kristo, na wala hawataufanya mwili wao kuwa kituo cha kutimiza kutimiza tamaa zake. {FEsw 290.1} — The Review and Herald, Januari 9, 1894.

Sura ya 38

WANAFUNZI WANAHTAJIKA KUWA WATENDAKAZI PAMOJA NA MUNGU

Yesu alikufa kwa ajili ya wanadamu, na katika kutoa maisha Yake aliinua ubinadamu katika kiwango cha thamani ya maadili na Mungu. Mwana wa Mungu asiye na ukomo, akauvisha Uungu Wake ubinadamu, na kujisalimisha kwa kifo cha

msalabani, ili apate kuwa ngazi ya kukanyagia ambayo kwayo wanadamu wanaweza kukutana na Mungu. Yeye aliwezesha uwezekano wa mwanadamu kuwa mshiriki wa tabia ya Uungu, ili kuepuka ule uharibifu uliopo duniani wa tamaa zake za mwili. Kristo anaendelea kufanya kazi ili kumwinua mwanadamu, na Anaitaka kila nafsi aliyoikomboa kutoka katika taabu, na huzuni isiyo na matumaini, watashirikiana Naye katika kazi kubwa ya kuokoa waliopotea. Hatupaswi kuweka mitego na kutengeneza mipango ya siri ya kuvuta Roho kwenda kwenye majaribu.

{FEsw 291.1}

Lo, laiti kila mmoja angeweza kuona jambo hili kama linavyowasilishwa mbele yangu katika fani zake zote, ni haraka kiasi gani wangemwacha adui katika kazi yake ya sanaa zenye ufundi wa hila! Ni kwa jinsi gani ambavyo wangezidharau na kuzichukia hatua zake katika kuleta dhambi kwenye familia ya kibinadamu! Ni kwa jinsi wangeichukia dhambi kwa chuki yote, wanapozingatia Ukweli kwamba iligharimu maisha ya Mkuu/Kamanda wa Mbinguni, ili wasiweze kuangamia, ili mwanadamu asifungwe mateka tena kwenye gari la shetani na kuwa mtumwa asiye na tumaini, aliyeshushwa hadhi chini ya mapenzi yake adui, nyara ya ushindi Wake na ufalme Wake. {FEsw 291.2}

Ni nani ataungana na Shetani? Nani atavaa beji yake? Ni nani atamchagua yeye kama nahodha, na kukataa kusimama chini ya bendera iliyotiwa madoa ya damu ya Kapteni wa wokovu wetu? Kristo alikufa kwa ajili ya kila mwana na binti wa Adamu; na wakati Mwana wa Mungu ameonyesha upendo wa ajabu namna hii, kwa kutoa dhabihu hii kuu kwa ajili ya mwenye dhambi, ili kwa njia ya kumwamini Yeye asipotee bali awe na uzima milele, inawezekanaje basi, somo hili la upendo huu mkuu linaweza kuwa lisilojaliwa na kusimama katika dhambi na uasi, na watu wasimkiri Kristo kwa moyo wote bila ya kuchelewa hata nukta moja? Je, mtu yoyote yule, anawezaje kupenda kufanya uovu? Vijana wanawezaje kutoa uwezo wao wa kufikiri kwa Shetani kama malaya anavyotoa mwili wake kwa Shetani, na kutoa ushawishi wao kwa kile ambacho kitadhoofisha nguvu zao za maadili na ufanisi? Katika kufanya mapenzi Yake Yeye aipendaye dunia, na Yeye aliyemtoa Mwanawe pekee ili afe kwa ajili yao, wanaimarisha kila kitivo/uwezo wa nafsi, na kuongeza furaha yao wenyewe na amani. {FEsw 291.3}

Bwana amewaheshimu sana wanadamu, kwa kumtoa Yesu Kristo wapone/waokoke na kurudishwa kutoka kwenye madai ya Shetani. Je, wewe utarejeshwa? Je, wewe utakuwa na zawadi ya thamani kwa Kristo? au utakataa huduma/utumishi Wake? Yesu amesema, "Yeye asiyekusanya pamoja nami hutawanya." Amewahi alisema, "Pasipo Mimi ninyi hamwezi kufanya neno lolote," na, "Neema Yangu yatosha kwa ajili yako." Kila mtu anayetaka kufanya vyema kwa uwezo wake dhaifu ulio na kikomo, atapata juhudi zake zinafeli/zinashindwa; bali wale wanaomkubali Kristo kwa imani, watampata Mwokozi wao binafsi. Watajiandikisha katika jeshi Lake, nao wao watakuwa askari Wake, na kupigana vile

vita vizuri vya imani. Kama wapo wanafunzi shuleni, watahisi kuwa wamesajiliwa hapo ili kuifanya shule kuwa taasisi yenye utaratibu, iliyoinuliwa, na yenye kustahili kupata sifa Duniani. Wataweka kila nukta ya ushawishi wao upande wa Mungu, upande wa Kristo, na upande wa akili za Mbinguni. Watahisi kuwa ni wajibu wao kuunda jumuiya ya Kikristo ijiibidishayo, ili waweze kumsaidia kila mwanafunzi mwenendo usiokubalika, ule ambao Mungu hataukubali. Watavuta pamoja na Kristo, na kufanya kila wawezalo ili kuwakamilisha wahusika wa Kikristo. Watachukua wao wenyewe kazi ya kuwapeleka vilema na wanyonge kwenye njia salama ile iendayo juu. Wataunda mikutano ya bidii ya Kikristo ili kuweka mipango ambayo itakuwa baraka kwa taasisi ya kujifunza/elimu, na kufanya yote yaliyo katika uwezo wao wa kuifanya shule kuwa kile ambacho Mungu alibuni kwa ajili yake na kuashiria kwamba inapaswa kuwa. Watazingatia thamani na ufanisi wa Jitihada za Kikristo katika mikutano ya kutiana moyo kiimani, katika kuwatayarisha wamishonari waende kutoa onyo kwa ulimwengu. {FEsw 292.1}

Wanafunzi wanapaswa kuwa na misimu binafsi ya maombi, ambapo wataweza kutoa maombi ya bidii, sahili na dhati, ili kwamba Mungu ambariki mkuu wa shule na nguvu za mwili, uwazi wa kiakili, nguvu ya maadili, na utambuzi wa kiroho, na kwamba kila mwalimu atakuwa amehitimu kwa neema ya Kristo kufanya kazi yake kwa uaminifu na kwa bidii ya upendo. Wanapaswa kusali ili walimu wawe mawakala Mungu, ambao kupitia kwao Bwana atamfanya wema kuushinda ubaya, kupitia ujuzi wa Yesu Kristo ambaye amemtuma. Hebu Mungu awape wanafunzi wanaohudhuria taasisi zetu za elimu, neema na ujasiri kutenda kulingana na kanuni zilizofunuliwa katika sheria ya Mungu, ambayo ni udhihirisho wa tabia Yake. Kamwe usipatikane ukiidharau shule ambayo Mungu ameisimika. Ikiwa umeshindwa wakati wowote, nawe ukangukia majaribuni kwa sababu hukumfanya Mungu kuwa nguvu zako, kwa sababu hamkuwa na imani itendayo kazi kwa upendo na kuwatakasia Roho. {FEsw 293.1}

Hebu kila Mkristo mwaminifu ambaye ana uhusiano na shule yetu, aazimie kuwa mtumishi mwaminifu katika kazi ya Kristo, na amsaidie kila mwanafunzi kuwa mwaminifu, msafi wa moyo, na mtakatifu maishani. Hebu kila mtu anayempenda Mungu atafute kuwaleta Kwake wale ambao bado hawajamkiri Kristo. Kila siku wanaweza kutoa ushawishi wa kimya, wa maombi, na kushirikiana na Yesu Kristo, Mmisionari Mkuu kwa ulimwengu wetu. Hebu kila nafsi—mwanamume, mwanamke, na kijana—ikue katika ubora wa tabia na uchaji Mungu, katika usafi wa moyo na utakatifu, na kuishi kwa kukita au kukaza jicho kwa Utukufu wa Mungu, ili adui wa imani yetu asijipatie ushindi. Hebu kuwe na kifungo kama hicho katika vifungo vyetu vya imani takatifu, ili mvuto wetu wa umoja uweze kuwa juu ya upande wa Bwana kikamilifu na uweze kufanya kazi kwa ajili ya mabadiliko ya wale ambao tunashirikiana nao. Acha idhihirishwe kuwa una muunganiko hai na Mungu, na una matamano ya Bwana kupata Utukufu, mkitafuta kukuza ndani yenu, kila neema ya tabia ambayo kwayo mwaweza kumheshimu Yeye aliyetoa maisha Yake kwa ajili

yenu. Hebu upendo wa Kristo utende nguvu inayowavuta wengine kama sumaku, ili kuingia kwenye ile njia iliyotengenezwa kwa ajili ya waliokombolewa na Bwana ili kutembea ndani. Wakati wanafunzi katika shule zetu watajifunza kuyapenda mapenzi ya Mungu, wataona kuwa ni rahisi kuyatenda wanapofanya ulinganifu. {FEsw 293.2}

Iwapo wanafunzi wataona kasoro za tabia kwa wengine, wacha washukuru kwamba wametambua kasoro hizi, na kwa hiyo wanaweza kujiwekea ulinzi dhidi yao (ili wasianguke kama wenzao). Bila shaka, mtaona watu ambao hawajifunzi upole na unyenyekevu wa Kristo, lakini wanapenda kujionyesha, ubatili, futuhi au mambo ya kipuuzi, na ya kidunia. Dawa pekee ya hilo ni kumtazama Yesu,

{FEsw 293.2}

na kwa kujifunza tabia Yake watakuja kudharau kila kitu kisicho na maana, cha upuuzi au futuhi, kidhaifu na kibaya. Tabia ya Kristo imejaa ustahimilivu, uvumilivu, fadhili, rehema, na upendo usio na mfano. Kwa kutazama tabia kama hiyo, watanyanyuka juu ya udogo/ujinga wao uliowatengeneza na kuwafinyanga. na kuwafanya wasiwe watakatifu na wasiopendeza. Watasema, “Sikuketi pamoja na watu wa ubatili, Wala sitaingia mnamo wanafiki.” Wao watatambua kwamba “yeye aendaye na wenye hekima atakuwa na hekima; bali rafiki wa wapumbavu ataangamia.” {FEsw 294.1}

Hebu kila mtu anayetafuta kuishi maisha ya Kikristo, akumbuke kwamba kanisa vitani kwenye mapambano sio kanisa lililopata ushindi. Wale walio nia ya tamaa za mwili watapatikana kanisani. Wanapaswa kuhurumiwa zaidi ya kulaumiwa. Kanisa halipaswi kuhukumiwa kuwa linategemeza watu wa tabia za namna hii, ingawa wanapatikana ndani ya mipaka yake. Je! kanisa liwafukuze, wale ambao walipata makosa na uwepo wao huko, hao wangelilaumu kanisa kwa limewapeleka katika ulimwengu wazimu; wangedai kwamba walitendewa bila huruma. Huenda ikawa kwamba katika kanisa kuna wale ambao ni ubaridi, kiburi, majivuno, na wasio na tabia za Kikristo, lakini huhitaji kujihusisha na tabaka hili. Kuna wengi wenye moyo wa uchangamfu, wenye kukana nafsi, na wenye kujinyima; ambao, kama ingehitajika, wangeyatoa maisha yao ili kuokoa Roho. Yesu aliona mabaya na mazuri katika uhusiano wa kanisa, na akasema, “Acheni mimea yote miwili kukua pamoja mpaka wakati wa mavuno.” Hakuna wanaohitaji kuwa magugu eti kwa sababu kila mmea shambani si ngano. Ikiwa Ukweli ulijulikana, walalamikaji hawa, wanatoa shutuma zao kwa makusudi kunyamazisha dhamiri iliyosadikishwa, wanahukumu dhamiri zao. Mwenendo wao wenyewe, hakika si wa hatua ya kupongezwa. Hata wale wanaojitahidi kumshinda adui, wakati mwingine wamekuwa na makosa na kutenda mabaya. Uovu unashinda wema wakati hatumtumaini kikamilifu Kristo, na kukaa ndani Yake. Na kisha tabia zinazobadilika

-badilika zitadhihirishwa ambazo zisingefunuliwa ikiwa tungeihifadhi ile imani ambayo hufanya kazi kwa upendo na kutakasa Roho. {FEsw 294.2}

Hatulazimishwi kuchagua wale wanaokataa upendo wa Mungu, alioonyesha katika kumtoa Wake Mwana kwa ulimwengu “ili kila mtu amwaminiye asipate kupotea, bali uwe na uzima wa milele.” kuwa kama marafiki zetu au watu tunaohusiana kwa karibu, “ili kila mtu amwaminiye asipate kupotea, bali uwe na uzima wa milele.” Wale wanaompenda Mungu hawatachagua maadui za Mungu kuwa marafiki zao. Swali lilikuwa limeulizwa “Je, unadhani ni vema kuwasaidia waovu na kuwapenda wamchukiao Mwenyezi-Mungu? Je, utachagua wale wasiopenda mambo ya kiroho, na wasio waaminifu, badala ya kushirikiana na wale wanaompenda Mungu? Je, utajitenga mbali na wale wanaompenda Mungu, na kujiweka mbali iwezekanavyo kutoka kwenye mkondo wa Nuru? Unahitaji kuweka angahewa safi na imani karibu yako, na kuileta tabia yako kwenye kanuni ambazo zitakuwa kama mbao imara za kujenga tabia ya Kristo. Wakristo hawatachagua na kukuza jamii ya wasio Wakristo. Ikiwa Bwana anakupa nafasi maalum duniani, kama alivyowafanyia Yusufu na Danieli, basi atakutegemeza na kukuweka katikati ya majaribu. Lakini hutawahi kuwa pale ambapo utapata mwanga mwingi, katika dunia yetu. Basi ni hatari kiasi gani kuchagua ushirika wa wale ambao wanapenda giza kuliko Nuru, wala hawatakuja kwenye Nuru, isipokuwa matendo yao yakemewe. {FEsw 295.1}— The Review and Herald, Januari 16, 1894.

The Review and Herald, January 16, 1894 |

Kwa Marejeleo ya Ziada

-The childhood of Jesus, The Youth's Instructor. Agosti 30, 1894.

MANENO KWA WANAFUNZI

Kila nafsi imezungukwa na mazingira ya kipekee ya mtu binafsi. Hali hii inaweza kuwa imejaa uchafuzi wa hewa wa kiroho (malaria) ambayo ni sumu kwa kanuni za haki. Lakini wakati tunapoletwa kushirikiana na wengine, haihitaji kutuchukua siku au wiki kadhaa ili kujua kama angahewa ya Roho ni ya Kristo au ya Shetani. Ushawishi wa ushirika hauna nguvu zaidi kuliko katika maisha ya shule; lakini mwanafunzi anayekuja shuleni kwa hamu ya dhati ya kuwa msaada na baraka kwa wenzake, atakuwa mwangalifu kutupa ushawishi wake upande wa kulia, na utafute maswahaba watakao ungana naye kusitawisha kanuni na mazoea sahihi. {FEsw 297.1}

Wanafunzi wanapaswa kuhisi wajibu wao katika suala la kufanya maisha yao ya shule yafanikiwe. Wanapaswa kuhenyeka kwa kila juhudi kuelekea kwenye haki, ili wasiwakatishe tamaa wazazi wao au walezi wao wanaofanya kazi kwa bidii ili kuwaweka shuleni, na ambao wana wasiwasi mwingi kwa ajili ya ustawi wao wa sasa na wa milele. Wanafunzi wanapaswa kuamua hilo, nao watafanya rekodi ambayo hawataoionea haya watakapokutana nayo katika siku ya hukumu. Mwanafunzi ambaye ni mwangalifu, ambaye hataki kuruka mahali na kujitumbukiza katika mwenendo wake, yule ambaye hatayumbishwa kwenda kulia au kushoto na ushawishi mbaya, atatumia uwezo wake kupinga juu ya waliopo shuleni ambao wanaoona ni raha yao kuonyesha uhuru wao, na kujihusisha na michezo yenye uovu, na katika kuasi sheria, na ambao hujaza mioyo ya walimu wao na huzuni na kukata tamaa. {FEsw 297.2}

Maisha ni shida ambayo lazima kila mmoja wetu aitatie mwenyewe. Hakuna anayeweza kutengeneza tabia kwa ajili ya mwingine; kila mmoja wetu ana sehemu yake kuchukua hatua katika kuamua hatima yetu wenyewe. Sisi ni mawakala huru wa Mungu tunaowajibika, na kila mtu lazima aifanyie kazi wokovu wake mwenyewe kwa hofu na kutetemeka, huku Mungu akitenda kazi ndani yake kunia na kutenda kwenu, kwa kulitimiza kusudi Lake jema. Wanafunzi wanaweza kufanya mema, au wanaweza kufanya mabaya, ila “chochote apandacho mtu, ndicho atakachovuna.” {FEsw 297.3}

Kila mmoja wetu yuko katika kujaribiwa/kutahiniwa akithibithishwa na Mungu. Akili za Mbinguni zote zimeorodheshwa ili kusaia kila nafsi itakayovutwa na Yesu, na kila mpenzi wa Kweli wa Yesu atashirikiana na mawakala wa Mbinguni katika kutafuta kuzivuta Roho mbali na kile kilicho cha upumbavu, duni na chenye kejeli. Wafuasi wa Kristo hawatafanya kazi upande wa Shetani ili kuidhoofisha imani katika dini ya Kweli, na kuwapotosha wengine kwa kuwatengenezea mazingira ambayo yanaharibu maadili na tabia. Lakini tunasikitika kusema hivyo, kwamba

hata katika shule zetu kuna watu ambao ni Wakristo kwa jina tu. Haitachukua muda kufahamiana nao na kugundua kwamba maprofesa hawa ni mawakala wa Shetani wenye ufanisi. Katika shule zetu kuna watu ambao ni mafisadi mioyoni, ambao bado wana lebo/maneno ya kupendeza, na ambao wamefaulu katika kuvutia tabaka fulani la watu, na kabla watu hawajachukua tahadhari, ushawishi wa watu hawa unakuwa umeshabadilisha tayari hisia zao, na kuziunda kulingana tabia za kuchukiza za hawa mafisadi. Lakini wale wanaovaa vazi la Ukristo, na huku bado wanatawaliwa na mitindo na kanuni za ulimwengu, ni waharibifu wa maadili. Wanadai kuwa wanatafuta hazina za Mbinguni, lakini angahewa ambayo nafsi zao zimezungukwa nayo ni moja ambayo imechajiwa uvundo wa kiroho wenye mauti, na wanapaswa kuepukwa na wale ambao wangebaki bila mawaa na ulimwengu.

{FEsw 298.1}

Kijana aliye na utambuzi anaweza kuona kwa urahisi watu hawa ni wa aina gani, ingawa yeye hana madai yoyote kwa Ukristo; kwani anajua kwamba wao sip kama Kristo. Lakini, yeye awaruhusu hawa kuwa vikwazo kwake? Ana kitabu cha mwongozo kinachoeleza wale walio upande wa Bwana. Ikiwa anajua huo mwenendo wao hauendani na taaluma ya Ukristo, ikiwa anaelewa nini maana ya kuishi maisha ya kumcha Mungu, atawajibishwa kwa mwanga na maarifa aliyo nayo. Atawajibika kufanya mapenzi ya Mwalimu, kwa kuuonyesha ulimwengu wazo la Kweli la Ukristo—ni nini maana ya kuwa na maisha na tabia kama ya Kristo.

{FEsw 298.2}

Tuna adui mwenye nguvu, na sio tu kwamba anamchukia kila mwanadamu aliyeumbwa kwa mfano wa Mungu, lakini kwa uadui mchungu zaidi yeye anamchukia Mungu na Mwanawe wa pekee Yesu Kristo. Wakati wanaume wanajitoa wenyewe kuwa watumwa wa Shetani, yeye haonyeshi uadui anaowafanyia wale walishikao Jina ya Kristo, na kujitoa kwa ajili ya utumishi wa Mungu. Yeye huwachukia hao kwa chuki ya kufisha. Anajua kwamba anaweza kumhuzunisha Yesu akiwatia chini ya nguvu za udanganyifu wake, kwa kuwajeruhi; kwa kudhoofisha imani yao, kwa kuwafanya washindwe kumtendea Mungu huduma kama wanavyotakiwa kuhudumu chini ya Kapteni wao Yesu Kristo. Shetani ataruhusu wale ambao wamefungwa kama watumwa kwenye gari lake wawe na kiwango fulani cha mapumziko, kwa maana wao ni mateka wake wa hiari; bali uadui wake huamshwa wakati ujumbe wa rehema unapowafikia watumwa wake, na wanatafuta kujinasua kutoka kwenye uwezo wake, ili waweze kumfuata Mchungaji wa Kweli. Kisha ni hapo atataka kuwafunga na minyororo ya ziada ya kuwashikilia katika utumwa wao. Mzozo kati ya nafsi na Shetani huanza wakati mateka anapoanza kuvuta mnyororo ghafla, na kutamani kuwa huru; maana hapo ndipo wakala wa mwanadamu huanza kushirikiana na akili za Mbinguni, wakati imani inamshikilia Kristo. Ndipo Yule Mwenye nguvu, kuliko mtu mwenye nguvu mwenye silaha, ambaye Ndiye msaidizi wa Roho anayemsaidia huyu mateka maskini, naye hutiwa nguvu kwa Roho Mtakatifu kupata uhuru wake. {FEsw 299.1}

Mungu ana upendo wa dhati kwa kila mwanachama wa familia ya wanadamu; hakuna aliyesahaulika, hakuna hata mmoja aliyeachwa bila msaada akidanganywa na kushindwa na adui. Na ikiwa wale waliojiandikisha kwenye jeshi la Kristo watavaa silaha zote za Mungu, na kwa kuzivaa hizo, watakuwa uthibitisho dhidi ya mashambulio yote ya adui. Wale ambao wana matamania ya kweli ya kufundishwa na Mungu, na kutembea katika njia Yake, wana ahadi ya uhakika kwamba ikiwa wanahisi mapungufu yao ya hekima na kuuliza Mwenyezi Mungu atatoa kwa ukarimu, wala hatawakemea. Mtume anasema, “Hebu na aombe kwa imani, pasipo shaka yo yote; maana mwenye shaka ni kama wimbi la bahari lililochukuliwa na upepo, na kupeperushwa huku na huku. Maana mtu kama yule asidhani ya kuwa atapokea kitu kwa Bwana. Mtu wa nia mbili husita-sita katika njia zake zote.” Mungu Yuko nyuma ya kila ahadi Yake, na hatuwezi kumvunjia heshima Yeye zaidi kwa kuulizauliza, kusitasita na kutokuamini, na kisha kuzungumza kwa mashaka. Ukiomba nawe usipate papo hapo kile ulichoomba, je, utazira, na kupata huzuni na kutoamini? Amini; amini kwamba Mungu atafanya kile Ameahidi. Yadumishe maombi yako kupanda juu, na uwe macho, ufanye kazi, na kusubiri. Piga vita vile vizuri vya imani. Sema moyoni mwako, “Mungu amenialika kuja Kwake. Naye amesikia maombi yangu. Ametoa ahadi Yake kwenye Neno kwamba atanipokea, na atatimiza ahadi Yake. Naweza kumwamini Mungu; kwa maana Yeye alinipenda hata akamtoa Mwanawe pekee kufa kwa ajili yangu. Mwana wa Mungu ni Mkombozi wangu.” “Ombeni, nanyi mtapewa kupewa wewe; tafuteni, nanyi mtapata; bisheni, na itafunguliwa kwako.” “Basi ikiwa ninyi, mlio waovu, mnajua kuwapa mema watoto wenu; si zaidi sana Baba yenu wa Mbinguni atawapa Roho Mtakatifu kwa hao wamwombao?” {FEsw 299.2}

Vijana wanaoingia na kuendelea na maisha ya shule wakiwa na lengo lenye ukweli mbele yao, hawatatamani kurudi nyumbani {homesick} au kukatishwa tamaa. Hawatakosa utulivu na kuwa na wasiwasi, bila kujua lipi walifanye kuhusu maisha yao wenyewe. Watapata msaidizi kwa Yule aliye Muweza wa yote. Watakuwa na moja lengo kwa mtazamo, na hiyo ni kuwa wanaume na wanawake wa kanuni, ambao watafikia kiwango cha Mungu, na kufaidisha ubinadamu na kumtukuza Mungu. Wao hawatachukulia maisha yao ya shule kama wakati wa kutafuta anasa, kwa maana maburudisho/pumbao la uvivu na utani wa kipumbavu, lakini watajitahidi kuitumia fursa na mapendeleo waliyopewa na Mungu, ili wasiweze kuwaangusha wazazi wao na waalimu wao, au kumhuzunisha Mwenyezi Mungu akili za Mbinguni. {FEsw 300.1}

Ni jambo zito kufa, lakini ni jambo zito zaidi kuishi, na kuunda tabia ambayo itatustahilisha kuingia shule ile iliyo katika nyua za Mbinguni juu. Tunaishi katika nchi ya adui, na tunaweza kutarajia magumu na migogoro. Vijana itabidi waweze

kustahimili ugumu kama askari wazuri wa Yesu Kristo. Sio vyema kwa njia yao kufanywa laini na rahisi kabisa, kwamba wapewe pesa, na wasifundishwe kuhisi umuhimu wa kufanya mazoezi ya kujinyima nafsi na kutenda mambo wakitilia umakini uchumi. {FEsw 300.2}

Wakati kijana anafanya uamuzi kwamba anataka kupata elimu, anapaswa kuzingatia kwa makini kwamba, ni nini nia yake katika kwenda shuleni? Anapaswa kujiuliza, Nitautumiaje vipi vyema muda wangu ili kuvuna faida zote zinazowezekana kutokana na fursa zangu na mapendeleo yangu? Je, nivae silaha zote za Mungu ambazo Mungu amenizawaidia kwa njia ya Mwana pekee wa Mungu? Je, nifungue moyo wangu kwa Roho Mtakatifu, ili kila amana ya uwezo/kitivo na nguvu zangu ambazo Mungu amenipa ziweze kuamshwa na kutumiwa ipasavyo? Mimi ni mali ya Kristo, na nimeajiriwa katika utumishi Wake. Mimi ni wakili na msimamizi wa neema Yake. {FEsw 301.1}

Ingawa, kwa maamuzi yako ya kibinadamu, baadhi ya wanaodai Ukristo hawakifikii kipimo chako cha tabia ya Kikristo, wewe haupaswi kuuhuzunisha moyo wa Kristo kwa kuishi maisha yasiyo na ulinganifu (yasiyoendana na Maandiko); kwa maana wengine wako katika hatari ya kuathiriwa na hatua unazochukua za mwenendo ulio mbaya. Unapigania taji ya uzima, na hupaswi usibweteke au kupumzika ukiwa umeridhika kufikia kiwango cha chini. {FEsw 301.2}

Bwana hakubali kazi nusu (nusunusu); upande wako haupaswi kuboronga kazi hii takatifu ya Mungu. Usijiamini, lakini salimisha mapenzi, mawazo na njia zako kwa Mungu, na kisha ufanye mapenzi Yake peke yake. Ishi kwa kumpendeza Yeye aliyekufikiria kuwa wa thamani, hata akamtoa Yesu, Mwana Wake wa pekee, ili akuokoe kutoka katika dhambi zako. Kupitia haki na Sifa yake, wewe unaweza kukubaliwa. Katika maisha yako ya shule daima weka mbele yako kwamba jambo lile la thamani ambalo linastahili kufanywa, basi lifanywe kwa ubora. Mtegemee Mungu akupe hekima, usije ukakatisha tamaa hata nafsi moja katika kutenda haki. Fanya kazi pamoja na Kristo katika kuzivuta Roho Kwake. Lakini haitakusaidia lolote wewe, wakati unalaani wengine kwa kazi inayofanywa kwa moyo nususu, ukiyasonda na kidole makosa yao, lakini nawe unashindwa kufanya vizuri kama wao, kwa sababu hujiweki upande wa haki na uaminifu. Ingawa sheria na kanuni zinaonekana ni makini na kali bila sababu, wewe uwe mtiifu kwazo; kwa maana unaweza kukosea katika uzoefu wako. Jitahidi sana katika kila unachokishika kukifanya. Yesu ni Mwokozi wako, na umtegemee Yeye kukusaidia siku baada ya siku, usipande magugu, bali mbegu njema za ufalme. {FEsw 301.3}

"Taa ya mwili ni jicho; basi jicho lako likiwa safi, mwili wako wote utakuwa na Nuru. Bali jicho lako likiwa bovu, basi lako mwili wote utakuwa na giza." Kama mwanafunzi, lazima ujifunze kuona kwa ubongo wako pamoja na macho yako.

Lazima uelimishe maamuzi yako ili yasiwe dhaifu na yasiyofaa. Lazima uombe kwa ajili ya kuongozwa, na kumkabidhi njia yako kwa Bwana. Ni lazima ufunge moyo wako dhidi ya upumbavu na dhambi zote, na ufungue wazi kwa kila ushawishi wa Mbinguni. Lazima utumie wakati wako vizuri na fursa, ili kukuza tabia linganifu. Michezo-michezo na upumbavu na uvivu hauwezi kutumbuizwa kama wageni wako, ikiwa unakiri Kile Kielelezo, yaani Kristo Yesu, na kuwa na akili zaidi kila siku kwa kile utakachofanya ili uokoke. {FEsw 302.1}

Wanafunzi vijana, maisha yenu hayawezi kutawaliwa na mihemko/msukumo bila kuthibitishwa kutofaulu kabisa. Huwezi kufuata mielekeo yako ya asili bila ya kukutana na hasara kubwa. Ikiwa utasonga mbele salama, basi ni lazima uishike njia ya Bwana. Uelewa wako lazima utakaswe na kusafishwa; lazima ufanye kazi kulingana na mpango wa Mungu, au la sivyo uamue kushindwa kufanikiwa (kufeli). Lazima uwe unakua na kusonga mbele katika neema na maarifa. Hutaweza kufanya chochote kinachokubalika katika maisha yako ya shule bila kujizoesha mfumo na utaratibu. Kazi ya kubahatisha au holela, italeta kushindwa fulani. {FEsw 302.1}

Unahitaji kuchunguza na kujifunza kwa uangalifu swali la burudani. Jiulize mwenyewe, Je! ni ushawishi gani utaletwa na burudani kwenye akili na tabia, na juu ya kazi ambayo nimekuja kuifanya? Jiulize mwenyewe kuhusiana na suala la burudani kwamba linashinikiza nini, au linaleta mvuto gani katika maisha yangu ya kidini/kiroho, na kwenye tabia yangu kama Mkristo? Je, michezo ambayo unashiriki inakustahilisha wewe kushiriki katika maombi na katika utumishi wa Mungu? Je, hii michezo au burudani vinakusaidia kuleta ari, usongo, bidii na unyofu katika kazi ya Bwana unaposhiriki kuicheza au kuiangalia Je, maburudisho/pumbao hizi ambazo umekuwa ukijishughulisha hazijachota matamania, yako mno kiasi kwamba hauwezi kuweka bidii katika ujifunzaji wa masomo yako kama wewe ilipaswa kufanya? Ambayo ndiyo yanapaswa kuchukua kipaumbele----- huduma ya Mungu, au huduma ya nafsi yako? Hebu kila mwanafunzi na achunguze kwa ukaribu ardhi ambayo amesimama. {FEsw 302.2}

Vijana wapendwa, sasa mnaamua hatima yenu ya milele. Hivyo ni lazima wewe uweke bidii isiyochoka kamwe katika maisha yako ya Kikristo ikiwa ungekamilisha uundaji wa tabia kamilifu. Itakuwa kwa hasara yako ya milele ikiwa una uzoefu wa kiroho/kidini ambao ni dhaifu na kitoto kidogo. Tunapaswa kuwa "kamili katika Yeye." "Basi kama mlivyompokea Kristo Yesu, Bwana, enendeni vivyo hivyo ninyi ndani yake." Hii ina maana kwamba unapaswa kujifunza maisha ya Kristo. Unapaswa kuisoma kwa bidii zaidi kuliko vile unavyosoma maarifa ya kilimwengu, kwani *masilahi ya milele* ni muhimu zaidi kuliko shughuli za muda, za kidunia. Ikiwa unathamini, hazina ya thamani na utakatifu wa mambo ya milele, utaleta mawazo yako yenye umakini {yenye ukali} zaidi, nguvu zako bora zaidi, kwenye utatuzi wa shida inayohusisha ustawi wako wa milele; kwa kuwa kila maslahi mengine

huzama na kuwa sufuri tu na batili ukilinganisha na hilo. {FEsw 303.1}

Una Kielelezo, Kristo Yesu; kutembea katika nyayo Zake, kutakustahilisha/kutakuhitimisha kujaza nafasi yoyote na kila unyadhifa utakayoitwa kuichukua. “Mtatiwa mizizi na kujengwa ndani Yake, na mmeimarishwa katika imani, kama mlivyofundishwa, mkizidi sana katika Imani kwa kushukuru.” Usijisikie kuwa wewe ni mtumwa, bali mwana wa Mungu; nawe umependelewa sana kwa kuwa umekuwa unachukuliwa kuwa wa thamani kubwa sana hata Mungu amekufanya kuwa Wake kwa kulipa fidia isiyo na ukomo kwaajiil ya uhuru wako. Yesu anasema, “Siwaiteni watumishi; ... lakini nimewaita marafiki.” Unapothamini Upendo Wake wa ajabu, upendo na shukrani vitakuwa moyoni mwako kama chemchemi ya furaha. {FEsw 303.2}

Usikubali kupokea sifa za kutia chumvi au kupakwa mafuta kwa chupa ya mgongo hata katika maisha yako ya kiroho/kidini. Kusifia kwa kutia chumvi au kumpaka mtu mafuta kwa chupa ya mgongo na kumbembeleza, ni sanaa ambayo kwayo Shetani huvizia nayo ili kuwadanganya wanadamu na kuwavimbisha kichwa kwa kiburi wale watu ambao wanakuwa wakala wake na kisha wanaishi hizo fikra zake shetani mwenyewe. “Angalieni mtu asiwafanye mateka kwa elimu yake ya bure na madanganyo matupu, kwa jinsi ya mapokeo ya wanadamu, kwa jinsi ya mafundisho ya awali ya ulimwengu, wala si kwa jinsi ya Kristo.” Kumsifia mtu kwa kutia chumvi kimekuwa chakula ambacho wengi wa vijana wetu wamelishwa; na wale ambao wamekuwa wakiwasifu kwa kutia chumvi na kuwabembeleza wamedhani kuwa walikuwa wanafanya lililo sawa; lakini wamekuwa wakifanya makosa, yaani jambo baya. Sifa, kusifiwa kwa kutia chumvi au kubembelezwa, na kujifurahisha au kujiendekeza kwa anasa kumefanya zaidi katika kuziongoza Roho za thamani kwenye njia za uongo, kuliko usanii mwingine wowote ambao Shetani ameubuni. {FEsw 304.2}

Kusifiwa kwa udangayifu au kwa kutia chumvi ni sehemu ya sera ya ulimwengu, lakini si sehemu ya sera ya Kristo. Kupitia kusifia watu kwa kutia chumvi, au kuwabembeleza binadamu maskini, walio na udhaifu na unyonge tele, wanakuja katika hatua ya kufikiri kwamba wao ni wana ufanisi mwingi na wanastahili ile sifa, na kichwa chao kinavimba katika akili zao za kimwili. Wanakuwa walevi kwa dhana kwamba wao wana uwezo zaidi ya ule walio nao, na uzoefu wao wa kidini unakuwa hauna usawa/balansi. Isipokuwa katika majaliwa ya Mungu watageuzwa kutoka katika madanganyo haya, na kuongoka, kwa kujifunza A Be Che ya dini katika shule ya Kristo, hao watapoteza Roho zao. {FEsw 304.2}

Vijana wengi wamepakwa mafuta kwa mgongo wa chupa, wakidanganywa kwamba wana uwezo wa asili, au karama ya kuzaliwa nayo; wakati uwezo huo wa asili wanaofikiri wanao, unaweza kupatikana tu kupitia mafunzo ya bidii na kukuza utamaduni wa akili, na katika kujifunza upole na unyenyekevu wa Kristo. Kwa kuamini kuwa wamejaliwa kwa asilia au wamezaliwa na wanadhani hakuna

umuhimu wa kuweka akili zao katika kazi ya kusimamia masomo yao; na bila ya kujua, kufumba na kumbua, anajikuta ametegwa katika mtego wa Shetani. Na Mungu anaruhusu ashambuliwe na adui, ili apate kuelewa udhaifu wake mwenyewe. Anamruhusu aboronge mambo fulani aliyoazimia kuyafanya, na kisha anatumbukizwa katika fedheha zenye uchungu. Lakini wakati yeye yupo chini ya uchungu wa hisia za udhaifu wake mwenyewe, hatakiwi kuhukumikiwa kwa ukali. Huu ni wakati kuliko mwingine wowote, anaohitaji mshauri mwenye busara, rafiki wa kweli, mwenye utambuzi wa tabia. Huu ndio wakati anapohitaji rafiki anayeongozwa na Roho wa Mungu, na ambaye atawatendea wenye kukosea kwa subira na uaminifu, na kuinua uso wa mkosefu ulioinama. Hatakiwi kuinuliwa kwa kupakwa mafuta kwa chupa ya mgongo (kusifiwa kwa kutia chumvi, au kupewa faraja za udanganyifu). Hakuna mtu aliyepewa idhini ya kushughulika na Roho kwa kutumia mvinyo/kileo cha udanganyifu wa Shetani. Badala yake anapaswa kuelekezwa kwenye raundi za kwanza ya ngazi, na miguu yake yenye kujikwaa iwekwe katika ngazi ya chini kabisa katika mwendelezo au mzunguko wa ngazi ili aanze kupanda akielekea juu. (kwenye ile ngazi inayoitwa ngazi ya Petro). Petro anasema, "Katika imani yenu ongezeni wema; na kwa wema ujuzi; na katika maarifa kiasi; na kwa uvumilivu wa kiasi; na katika saburi utauwa; na kwa utauwa wema wa kindugu; na katika upendano wa kindugu upendo. Kwa maana kama hawa mambo yakiwa ndani yenu na kujaa tele, yanawafanya ninyi kuwa hamtakuwapo tasa, wala wasio na matunda, katika kumjua Bwana wetu Yesu Kristo." {FEsw 304.3}

Hebu mkosaji ahimizwe kupanda hatua kwa hatua, pembezoni, na pembezoni pande zote. Jitihada inaweza kuwa chungu kwake, lakini itakuwa somo bora alilopata kujifunza kwa mbali zaidi; maana kwa kufanya hivyo atajua udhaifu wake mwenyewe, na hivyo kuwezesha kuepuka makosa ya zamani baadaye. Kupitia msaada wa washauri wenye busara, kushindwa kwake kutageuzwa kuwa ushindi. Lakini mtu asijaribu kuanza na ngazi ya juu kabisa. Hebu kila mtu aanze kwa raundi ya ngazi ya chini kabisa, na ***kupanda hatua kwa hatua, kupanda na Kristo pamoja***, kumng'ang'ania Kristo; kupanda hadi kwenye kilele cha Kristo. Hii ndiyo njia pekee ya kusonga mbele kuelekea Mbinguni. Usiruhusu chochote kugeuza umakini kutoka kwa kazi hii kuu ambayo inafaa kufanywa. Wacha mawazo, uwezo, mazoezi ya bidii ya nguvu za ubongo, viwekwe kwa matumizi ya juu zaidi katika kusoma Neno na mapenzi ya Mungu. Bwana ana nafasi ya ule uwezo bora ambao amewakabidhi wanadamu kama amana. Katika kazi ya kuujenga ufalme Wake, sisi tunaweza kutumia kila uwezo uliotolewa na Mungu, kwa uaminifu na bidii kama ile aliyofanya Danieli huko Babeli, alipoonekana kuwa mwaminifu kwa kila kazi ya mwanadamu, na mwaminifu kwa Mungu wake. {FEsw 305.1}

Mungu anataka kuwe na busara zaidi katika usimamizi na kuongoza/uongozi, hekima katika kuheshimu utawala Wake, kuliko ambavyo wametenda Kwake kupitia mawakala Wake wa kibinadamu. Kuna haja ya umakini, fikra iliyotakaswa,

na kazi kubwa ya kupinga mipango ya hila na werevu wa Shetani. Kuna wito wa kufikia kiwango cha juu zaidi, ulio mtakatifu zaidi, wenye jitihada iliyoazimia zaidi, na yenye juhudi ya kujitoa mhanga katika kazi ya Bwana kazi. Vijana wetu lazima waelimishwe kufikia kiwango cha juu, ili kuelewa kwamba sasa wanaamua hatima yao ya milele. Hakuna usalama/ulinzi kwa yeyote, isipokuwa kuweka moyo kwenye ile Kweli kama ilivyo ndani ya Yesu. Hii lazima ipandwe ndani ya moyo na Roho takatifu. Mengi ambayo sasa yanaitwa dini yatazama bila kuonekana yanaposhambuliwa na majeshi ya Shetani. Hakuna kitakachosimama isipokuwa ile Kweli, –hekima itokayo juu, ambayo itatakasa nafsi. {FEsw 306.1}

Hebu Mtu yoyote asifikirie kuwa kujiendekeza au kujifurahisha mwenyewe ndiyo dini. Usiruhusu ubinafsi ubembelezwe/kudekeshwa. Waache vijana wajifunze kuzuia tamaa zao, na kujihadhari na ubadhirifu katika matumizi ya fedha. Wacha wote wamwangelie Yesu, na kutafakari tabia Yake, na wafuate nyayo zake. “Maana katika Yeye unakaa utimilifu wote wa Mungu, kwa jinsi ya kimwili. Na ninyi mmetimilika katika Yeye, aliye kichwa cha enzi yote na nguvu.” {FEsw 306.2} – [The Youth’s Instructor, Mei 3, 10, 17, 24, 1894.](#)

JIFUNZENI BIBLIA KWA AJILI YENU WENYEWEE

Usiruhusu mtu yeyote kuwa ubongo wako, usimruhusu mtu yeyote kufikiri badala yako, kufanya uchunguzi wako, kufikiri na kutoa sala aumaombi yako. Haya ndiyo maagizo tunahitaji kuyatilia maanani leo. Wengi wenu mnaamini kuwa hazina ya thamani ya ufalme wa Mungu na wa Yesu Kristo iko kwenye Biblia ambayo umeishika mkononi mwako. Mnajua kwamba hapana hazina ya kidunia inayoweza kupatikana bila juhudi kubwa zenye maumivu. Kwa nini basimnatarajia kuelewa hazina za Neno la Mungu bila kuyachunguza Maandiko kwa bidii na uadilifu? {FEsw 307.1}

Inafaa na ni vema kuisoma Biblia; lakini wajibu wenu hauishii hapo; kwa maana mnapaswa kuchunguza kurasa zake ninyi wenyewe. Maarifa ya Mungu si ya kupatikana bila juhudi za kiakili, bila maombi ya hekima ili upate kutenga mbegu safi ya Ukweli na yale makapi ambayo binadamu na Shetani wamepotosha kwa kuwakiilsha vibaya hayo Mafundisho Makuu ya ile Kweli (Doctrines). Shetani na washirika wake wa mawakala wa kibinadamu wanajitahidi kuchanganya makapi ya upotovu na ngano ya kweli. Tunanapaswa kutafuta kwa bidii hazinahii iliyofichwa, na kutafuta hekima kutoka Mbinguni ili kutenganisha uvumbuzi wa wanadamu dhidi ya amri za Mungu. Roho Mtakatifu atamsaidia mtafutaji wa zile Kweli kuu na za thamani zinazohusiana na mpango wa ukombozi. Napenda kusesitiza kwa ukweli wote kuwa usomaji wa kawaida wa Maandiko hautoshi kabisa. Ni lazima tuchunguze, na hii inamaanisha kufanya yote Neno linalodokeza. Kama vile mchimbaaji wa madini anavyofanya utafiti wa ardhi kwa shauku ya kugundua mifereji yake ya dhahabu, hivyo ndivyo unatakiwa kuchunguza Neno la Mungu kwa ajili ya hazina iliyofichwa ambayo Shetani kwa muda mrefu ametafuta kuificha kutoka kwa mwanadamu. Bwana asema, “Mtu akipenda kuyatenda mapenzi Yake, atajua habari ya yale mafunzo.” Yohana 7:17 (R. V.) {FEsw 307.2}

Neno la Mungu ni Kweli na Nuru, nalo linapaswa kuwa taa ya miguu yako, ili kukuongoza kila hatua ya njia kuelekea kwenye malango ya mji wa Mungu. Ni kwa sababu hii ndio maana Shetani amefanya jitihada zisizochoka za juu na chini, ili kuzuia njia ambayo imetolewa kwa ajili ya waliokombolewa wa Bwana kuiendea. Hampaswi kuyapeleka mawazo yenu kwenye Biblia, mkiyafanya maoni yenu kuwa ndiyo kitovu/kiini ambacho ile Kweli ndiyo inapaswa kuyazunguka mawazo hayo. Mnapaswa kuweka kando mawazo yenu nje ya mlango wa uchunguzi/utafiti, na kwa mioyo iliyonyenyekea, iliyotiishwa, na ubinafsi uliofichwa ndani ya Kristo, kwa maombi ya kina, mnatakiwa kutafuta hekima kutoka kwa Mungu. Mnapaswa kuhisi kwamba ni lazima kuyajua mapenzi ya Mungu yaliyofunuliwa, kwa sababu yahusu ustawi wenu binafasi, wa milele. Biblia ni kitabu cha kumbukumbu na mwongozo

ambao kwa huo unaweza kuijua njia ya uzima wa milele. Mnapaswa kutamani kuliko vitu vyote mwezavyo kwamba mjue mapenzi na njia za Bwana. Hampaswi kuchunguza kwa kusudi la kupata mafungu ya Maandiko ili uweze kutafsiri au kufafanua ili kuthibitisha nadharia zako; kwa maana Neno la Mungu linatangaza kwamba huku ni kuyatundika mahali Maandiko kwa uharibifu wako mwenyewe. Mnapaswa kuondoa kila chuki, na kuja katika Roho ya maombi kwa uchunguzi wa neno la Mungu. {FEsw 307.3}

Kosa kuu la Kanisa la Rumi linapatikana katika uhalisia kwamba Biblia inafasiriwa kulingana na maoni ya “mababa.” Maoni yao yanazingatiwa kuwa madhubuti na hayakosei kamwe na waheshimiwa wa vyeo vya juu wa kanisa hudhani kwamba ni haki yao kufanya wengine kuamini kama wanavyoamini, na kutumia nguvu kulazimisha dhamiri. Wale wasiokubaliana nao wanatamkwa kuwa ni wazushi. Lakini Neno la Mungu si la kufasiriwa hivyo. Linapaswa kusimama katika sifa na thamani yake ya milele, kusomwa kama Neno la Mungu, kutiwa kama sauti ya Mungu, ambayo inatangaza mapenzi Yake kwa watu. Mapenzi na sauti ya mwanadamu mwenye ukomo hayatakiwi kufasiriwa kama sauti ya Mungu. {FEsw 308.1}

Biblia iliyobarikiwa inatupa ujuzi wa mpango mkuu wa wokovu, na inatuonyesha jinsi kila mtu anavyoweza kuwa na uzima wa umilele. Mwandishi wa kitabu hicho ni nani basi?, ni Yesu Kristo. Yeye Ndiye Shahidi wa Kweli, na anawaambia walio Wake, “Nami nawapa uzima wa milele; wala hawatapotea kamwe, wala hakuna mtu atakayewapokonya katika mkono Wangu.” Biblia inapaswa kutuonyesha njia ya Kristo, na katika Kristo uzima wa milele umefunuliwa. Yesu aliwaambia Wayahudi na wale ambao wakalionga katika makutano mengi, “Yachunguzeni Maandiko.” Wayahudi walikuwa na Neno katika Agano la Kale, lakini walikuwa wamelichanganyana kulikoroga sana na maoni ya wanadamu, kiasi kwamba Kweli zake zilifichwa, na mapenzi ya Mungu kwa mwanadamu yalifunikwa. Walimu wa dini wanafuata mfano wao katika zama hizi. {FEsw 308.2}

Ingawa Wayahudi walikuwa na Maandiko yaliyomshuhudia Kristo, hawakuweza kumtambua Kristo katika Maandiko; na ingawa tuna Agano la Kale na Agano Jipya, watu huyatundika Maandiko mahali ambapo wataupindisha ukweli wake (Kupotosha); na katika tafsiri Maandiko, wao kufundisha, kama Mafarisayo, kanuni na mapokeo ya wanadamu mahali pa amri za Mungu. Katika siku ya Kristo viongozi wa kidini walikuwa kwa muda mrefu wakiwasilisha mawazo ya kibinadamu mbele za watu, ndio maana mafundisho ya Kristo yalikuwa kwa kila namna ni kinyume na nadharia na matendo yao. Mahubiri Yake ya mlimani yalipingana kabisa na mafundisho ya watu, waandishi na Mafarisayo wanaojihesabia haki. Walikuwa wamemwakilisha Mungu vibaya sana kiasi kwamba alionwa kama hakimu mkali, asiye kuwa na huruma, asiye na rehema, na upendo. Waliwasilisha kwa watu kanuni zisizo na mwisho na mapokeo kama yaliyotoka kwa Mungu, wakati hawakuwa na

“Hivi ndivyo asemavyo Bwana” kwa mamlaka yao. Ingawa walikiri kumjua na kumwabudu Mungu wa Kweli na aliye hai, walimwakilisha vibaya kabisa; na tabia ya Mungu, kama ilivyowakilishwa na Mwanawe, ilikuwa kama somo la asili, zawadi mpya kwa ulimwengu. Kristo alifanya kila juhudi kufagilia mbali uwakilishi mbaya wa Shetani, ili imani ya mwanadamu katika upendo wa Mungu iweze kurejeshwa. Alimfundisha mwanadamu kumwendea Mtawala Mkuu Zaidi wa ulimwengu wote na kumwita kwa Jina jipya— “Baba Yetu.” Jina hili linaashiria uhusiano Wake wa kweli na halisia nasi/kwetu, na linaposemwa kwa unyofu kwa midomo ya mwanadamu, ni muziki katika masikio ya Mungu. Kristo hutuongoza kwenye kiti cha enzi cha Mungu kwa njia mpya na iliyo hai, ya kumwasilisha Yeye kwetu katika upendo Wake wa Baba. {FEsw 309.1} — [The Review and Herald, September 11, 1894.](#)

KAZI NA ELIMU

Akili zetu zimepata mazoezi mengi kufikiri mchana na usiku kuhusu shule shule zetu. Je, zitaendeshwa vipi? Na mafunzo ya elimu ya vijana yatakuwaje? Shule yetu ya Biblia Australia itajengwa wapi? Niliamshwa leo saa saba usiku na mzigo mzito juu ya nafsi yangu. Somo la elimu imewasilishwa mbele yangu katika mistari tofauti, katika nyanja mbalimbali, na vielelezo vingi, na kwa maelezo maalumu ya moja kwa moja (wazi), kilikuja kipengele kimoja, na kipengele kingine tena, na ikaendelea hivyo. Hakika ninahisi kwamba. tuna mengi ya kujifunza. Sisi ni wajinga katika mambo mengi. {FEsw 310.1}

Katika kuandika na kuzungumza juu ya maisha ya Yohana Mbatizaji na maisha ya Kristo, nimejaribu kuwasilisha yale ambayo yamewasilishwa kwangu kuhusu elimu ya vijana wetu. Tuko chini ya wajibu kwa Mungu kujifunza somo hili kwa unyoofu; kwa maana linastahili uchunguzi na upembuzi muhimu katika kila upande. Kuhusu Yohana Mbatizaji, Kristo alisema, "Katika wale waliozaliwa na wanawake hajatokea aliye mkuu zaidi." Nabii huyo aliongozwa na Roho wa Mungu mpaka jangwani, mbali kutoka kwenye athari za jiji zinazochafua na kuambukiza, kupata elimu hiyo kungemstahilisha kupokea maagizo kutoka kwa Mungu badala ya kutoka kwa yeyote kati ya waandishi wenye elimu. Hakutakiwa kujiunganisha na marabi; kadiri alivyokuwa anayafahamu mafundisho yao kwa udogo, na kanuni zao, na mapokeo, ndivyo Bwana angaliweza kuivutia kwa urahisi zaidi akili na moyo, na kumpa msimamo bora wa elimu safi ya ile Kweli ambayo ilipaswa kupewa wale watu waliokuwa wanaenda kuitengeneza njia ya Bwana. Mafundisho ya waandishi na Mafarisayo yalikuwa na tabia ya kuwageuza watu mbali na ule Ukweli usioghoshiwa ambao ungewasilishwa na Mwalimu Mkuu wakati anapopaswa kuingia katika utume Wake. Tumaini pekee la watu lilikuwa kufungua mioyo na akili zao kwenye Nuru iliyotumwa kutoka Mbinguni na nabii Wake, mtangulizi wa Kristo. {FEsw 310.2}

Mafunzo haya ni kwa ajili yetu. Wale tunaodai kuwa tunajua Ukweli na kuelewa kazi kubwa ya kufanywa kwa wakati huu wanapaswa kuwekwa wakfu wenyewe kwa Mungu, nafsi, mwili, na Roho, moyoni, katika mavazi, katika lugha/maneno, na kwa kila jambo wanapaswa kujitenga na mitindo na mazoea ya ulimwengu. Wanapaswa kuwa watu wa kipekee na watakatifu. Sio mavazi yao ndiyo yanayowafanya kuwa wa kipekee, lakini kwa sababu wao ni watu wa kipekee na watakatifu, hawawezi kubeba alama za kufanana na dunia. {FEsw 311.1}

Kama watu tunapaswa kuitayarisha njia ya Bwana. Kila chembe ya uwezo ambao Mungu ametupa lazima tuutumie katika kuwatarisha watu kulingana na umbo la Mungu, kulingana na umbo Lake la kiroho, kusimama katika jambo hili kuu

siku ya maandalizi ya Mungu; na swali zito linaweza kuamshwa katika mioyo inayopenda ulimwengu, “Umilele ni nini kwetu? Kesi yangu itakuwaje nitakaposimama katika hukumu ya upelelezi? Sehemu yangu (kura) na nafasi yangu itakuwa ipi?” Wengi wanaodhani kuwa wanaenda Mbinguni wamefunikwa macho na dunia. Mawazo yao ya nini kinajumuisha elimu ya dini na nidhamu ya kidini ni yasiyoeleweka, yaani ni kama ukungu, yanategemea tu uwezekano (labda); hapo ni wengi ambao hawana tumaini lenye busara/akili, na wamo katika hatari kubwa kutenda mambo yale yale ambayo Yesu amefundisha kwamba wanapaswa wasiyafanye, katika kula, kunywa, na kuvaa, wanajifunga wenyewe na ulimwengu kwa njia mbalimbali. Bado hawajajifunza masomo makini na muhimu sana katika ukuaji wa kiroho, kutoka nje ulimwengu na kujitenga. Moyo umegawanyika, nia ya tamaa ya mwili inatamani kufanana, kufanana na ulimwengu kwa njia nyingi ambazo alama ya utofauti na ulimwengu ni shida kupatikana. Pesa, pesa ya Mungu, hutumiwa ili kujidhihirisha na kujionyesha kuendana na desturi za ulimwengu; uzoefu wa kidini umechafuliwa na ulimwengu, na ushahidi wa ufuasi—mfano wa Kristo katika kujikana nafsi na kubeba msalaba—hautambuliki na ulimwengu, wala ulimwengu wa Mbinguni. {FEsw 311.2}

Katika nchi hii, Shetani amejitawaza yeye mwenyewe kwa njia ya kushangaza zaidi ili kudhibiti watu wakuu katika serikali ya taifa. Elimu waliyoipata tangu utotoni ina makosa. Vitu vingi vinachukuliwa kuwa muhimu vina majeraha yenye athari kwa watu. Likizo nyingi zimekuwa na ushawishi wenye maumivu juu ya akili za vijana; matokeo yake ni ya kukatisha tamaa kwa serikali, na ni kinyume kabisa na mapenzi ya Mungu. Athari moja kwa tabia ni kuhimiza msisimko wa bandia, na hamu ya kujifurahisha. Watu wanaongozwa kupoteza wakati wa thamani ambao wanapaswa kuutumia katika kazi inayoleta manufaa ili kuendeleza familia zao kwa uaminifu na kujiepusha na madeni. Shauku ya burudani na ufujaji wa pesa katika mbio za farasi, kamari, na kubeti na aina mbalimbali za michezo kama hiyo, ambayo huishia kuongeza umaskini wa nchi, na kuongezeka kina cha huzuni, ambayo ni matokeo ya uhakika ya aina hii ya elimu. {FEsw 311.3}

Kamwe elimu ifaayo haiwezi kutolewa kwa vijana katika hii nchi, au nchi nyingine yoyote, isipokuwa wametenganishwa kwa umbali, kutoka mijini. Mila na desturi za mijini hazifai akili za vijana katika kuingiza ile Kweli kwenye mioyo yao. Unywaji wa vileo, uvutaji sigara na kamari, mbio za farasi, ukumbi wa michezo-drama na sinema, umuhimu mkubwa unaowekwa kwenye siku kuu, - zote hizo ni aina ya ibada za sanamu, ni kutoa dhabihu juu ya madhabahu za sanamu. Ikiwa watu kwa kwa kufuata dhamiri njema wanaenda kwenye shughuli zao au kazi halali wakati wa siku kuu hizi, wanazingatiwa kama watu wenye Roho mbaya na wasio wazalendo. Bwana hawezi kutumikiwa katika hili njia. Wale wanaozidisha siku za starehe na pumbao wanatoa upendeleo kwa wauzaji pombe, na wanachukua kutoka masikini kwa masikini, fedha yao ya kuwanunulia chakula na mavazi watoto wao, pesa ile ambayo, ikitumiwa kwa busara ya uchumi,hivi karibu wangeweza kuwaandalia

familia zao makazi, kwa kujenga nyumba. Maovu haya tunaweza tu kugusa. {FEsw 312.1}

Sio mpango sahihi, kutafuta majengo ya shule mahali ambapo mara kwa mara wanafunzi watakumbana na vitendo potovu na macho yao, ambavyo vitaunda elimu kichwani wakati wa maisha yao, haijalishi kama matukio au vitendo hivi potofu, ni vya muda mfupi au mrefu. Siku kuu hizi, pamoja na mlolongo wake wote wa uovu, husababisha huzuni. Shida mara ishirini zaidi kuliko wema. Kwa kiwango kikubwa maadhimisho siku hizi yanalazimishwa. Hata watu ambao walioongoka kweli wanaona ni vigumu kuachana na desturi hizi na mazoea. Endapo shule zipo ndani ya miji au maili chache kutoka hizi shule, itakuwa vigumu zaidi kukabiliana na ushawishi wa elimu ya awali ambayo wanafunzi wamepokea kuhusu sikukuu hizi na desturi zinazohusiana nazo, kama vile kama mbio za farasi, kamari, kubeti na utoaji wa zawadi. Eneo la anga la miji hii limejaa hewa (malaria) yenye sumu na uvundo. Uhuru wa mtu binafsi kuchukua hatua fulani hauheshimiwi; wakati wa mtu hauzingatiwi kama ni wake kweli; anatarajiwa kufanya kama wengine wanavyofanya. Endapo shule yetu itakuwa katika mojawapo ya miji hii, au ndani ya maili chache kutoka hapo, kutakuwa na ushawishi wa kukabiliana nao kila wakati, ambao unakinzana na utendaji wa elimu bora na kufaulu. Kujitolea kwa burudani na maadhimisho ya sikukuu nyingi, hutoa soko/biashara kubwa kwa mahakama, kwa maafisa na mahakimu, na kuongeza umaskini na ufukara ambao hauhitaji kuongezeka. {FEsw 312.2}

Yote haya ni elimu ya uwongo. Tutaona ni muhimu kuanzisha shule zetu nje, na mbali ya, miji, na bado zisiwe mbali sana kiasi kwamba haziwezi kuwasiliana na miji ili kuitendea mema, kuwaachia Nuru wakazi wake ili iangaze katikati ya giza la maadili. Wanafunzi wanahitaji kuwekwa chini ya mazingira mazuri ili kukabiliana elimu yenye ukinzani waliyoipata. {FEsw 313.1}

Wanachama wote wa familia nzima wanahitaji mabadiliko ya kina katika tabia zao na mawazo kabla ya kuwa wawakilishi wa Kweli wa Yesu Kristo. Na kwa kiasi kikubwa watoto wanaopaswa kupata elimu katika shule zetu, watafanya maendeleo zaidi ikiwa watatengana na duru ya familia ambayo wamepata elimu yenye makosa. Huenda ikawa lazima kwa baadhi ya familia kutafuta mahali wanapoweza kuwaweka watoto wao na kuokoa gharama, lakini katika kesi nyingi hilo la kuwaacha watoto wao mbali nao lingethibitisha kuwa kizuizi badala ya baraka kwa watoto wao. Watu nchi hii wana ufahamu mdogo sana ulio muhimu katika kufanya kazi kwa bidii na kujifunza stadi (tasnia), watoto hawajaelimishwa kuwa na tabia za kufanya kazi halisi za maisha, kwa unyofu na bidii. Hii ni lazima iwe sehemu ya elimu inayotolewa kwa vijana. {FEsw 313.2}

Mungu aliwapa Adamu na Hawa ajira. Edeni ilikuwa shule ya kwanza kwa wazazi

wetu, na Mungu alikuwa mwalimu wao. Walijifunza jinsi ya kulima udongo na kutunza vitu vitu ambavyo Bwana alikuwa amevipanda. Hawakuiona kazi kama jambo la kudhalilisha au kuwashushia hadhi yao, bali kama mbaraka mkubwa. Kufanya kazi kwa bidii na ustadi, ilikuwa starehe na raha kwa Adamu na Hawa. Kuanguka kwa Adamu kulibadilisha mpangilio wa mambo; dunia ililaaniwa: lakini agizo la kwamba mtu ajipatie chakula chake kwa jasho linalotiririka usoni mwake, halikutolewa kama laana. Kupitia imani na tumaini, kazi ilipaswa kuwa baraka kwa uzao wa Adamu na Hawa. Mungu hakuwahi kumpangia mwanadamu kukaa bila la kufanya (hata kabla ya maanguko ya dhambi, Mungu alitaka mwanadamu afanye kazi). Lakini laana ya dhambi ilivyozidi kuzama kwa kina zaidi, ndivyo mpango/utaratibu wa Mungu ulivyoendelea kubadilika. Mzigo wa kazi ngumu huwa mabegani mwa tabaka fulani, ila laana ya uvivu ikojuu ya wengi walio na mali ya Mungu, na yote ni kwasababu ya wazo lenye udanganyifu kwamba pesa huongeza thamani ya maadili ya wanaume. Ufanisi au kuzorota kwa utendaji wa kazi ni jinsi binadamu mwenyewe anavyoifanya iwe {wengine wanapenda kazi na wengine wanaichukia, ni vile unavyoamua ndiyo jinsi inavyokuwa}. Kuzama katika taabu ya kudumu, kutafuta unafuu wa muda mfupi katika unywaji wa vileo na burudani za kuisimua, mapenzi na kutawafanya watu kuwa bora kidogo tu kuliko wanyama.

{FEsw 314.1}

Tunahitaji shule katika nchi hii za kuelimisha watoto na vijana ili wawe watu waliobobea ufanisi wa kazi, na wala si watumwa wa kazi. Ujinga na uvivu hautamwinua mhusika hata mmoja wa familia ya ubinadamu. **Ujinga haumtapunguzia fungu la taabu mtenda kazi anayehenyaka kwa mitulinga ya shughuli nzito.** Hebu mfanyakazi ayaone manufaa yaliyopo kwenye kila kazi, hata ile iliyo ndogo na nyenyekevu zaidi, kwa kutumia uwezo aliopewa na Mungu kama majaliwa au amana kwake (atumie hekima, akili, pembejeo nk). Ndivyo yeye anaweza kuwa mwelimishaji, akifundisha wengine sanaa ya kufanya kazi kwa akili {kwa kutumia ubongo wake vizuri}. Hivyo yeye anaweza kuwa mwalimu, akifundisha wengine sanaa ya kuifanya kazi kwa kutumia ubongo wake. Ndivyo anavyoweza kuelewa maana ya kumpenda Mungu wake kwa moyo, nafsi, akili, na nguvu zake zote. Nguvu za kimwili zinapaswa kuletwa katika **huduma kutoka kwenye kuipenda kazi ya Bwana, mpaka kwenda kwenye kumpenda Mungu.** Bwana anataka nguvu za kimwili, nawe unaweza kudhihirisha upendo wako Kwake kwa kutumia nguvu zako za kimwili kwa njia iliyo ya haki, au sawa {halali}, kufanya kazi ile ile inayohitaji kufanyika. Mungu hana ubaguzi au upendeleo wa mtu yoyote mbele Zake, tukilinganisha na mtu mwingine (Yeye anatupenda sote). {FEsw 314.2}

Wakati maskani ya hema la kukutania (Patakatifu) lilijengwa jangwani kwa ajili ya utumishi ya Mungu, kazi ilifanywa chini ya uongozi wa Mungu. Mungu alikuwa mbunifu (dezaina wa ramani), watenda kazi walifundishwa Naye, nao waliweka moyo, Roho na nguvu katika kazi. Kulikuwa na kazi ngumu ya kufanywa, na fundi

mjenzi (mhandisi) mwenye mwili imara, aliishughulisha misuli na kano kwa bidii nyingi, akidhihirisha upendo wake kwa Mungu katika kazi ngumu kwa ajili ya heshima Yake Bwana. {FEsw 315.1}

Ulimwenguni kuna kazi nyingi ngumu, za kutumia nguvu za mwili na kuchosha, yaani zinazotoza ushuru mwili, yeye ambaye hufanya kazi pasipo kutumia nguvu za akili, moyo na Roho, alizopewa na Mungu, na badala yake akatumia nguvu za mwili wake peke yake, hufanya kazi iwe mzigo mzito wenye kuchosha, unaotoza ushuru mwili. Kuna watu walio na akili, moyo, na Roho ambao wanaiona kazi kuwa ni jambo duni na la kuchosha (mitulinga tu!) nao hutulia kwa ujinga wakiwa wameridhika na mafaniko yao na hisia za kujitosheleza, bila ya kutafakari au kufikiri katika kuushughulisha uwezo wao wa kiakili ili kufanya kazi vizuri zaidi. {FEsw 315.2}

Kuna sayansi kwenye kazi zote, hata ile yenye wadhifa mdogo na duni, na endapo wote waiona kwa jinsi hivyo, basi wangeona ubora na Utukufu katika kazi hiyo. Moyo na Roho vinafaa kuwekwa katika kazi ya aina yoyote; kisha uchangamfu na ufanisi uingie hapo pia. Katika kazi za kilimo au zile za suluba zinazotumia nguvu za mwili (mechanical work au mitulinga ya kuhenyeka) watu wanaweza kutoa Ushahidi/ushuhuda kwa Mungu kwamba wathamini zawadi Yake ya nguvu za kimwili, na uwezo wa kiakili pia. Hebu uwezo wa ulioelimishwa na utumike ndani katika kubuni mbinu bora za kazi. Hili ndilo jambo Bwana anataka lifanyike. Kuna heshima katika tabaka lolote la kazi ambayo ni muhimu kufanywa (hata kuosha choo). Hebu basi sheria ya Mungu ndiyo ifanywe kuwa kiwango cha utendaji, nayo itatukuza na kutakasa kazi yote. Uaminifu katika utekelezaji wa kila wajibu hufanya kazi bora, yenye kuleta Utukufu, na kufunua tabia ambayo Mungu anaweza kuidhinisha. {FEsw 315.3}

“Mpende Bwana, Mungu wako, kwa moyo wako wote, na kwa nguvu zako zote, na kwa Roho yako yote, na kwa akili zako zote, na kwa nguvu zako zote.” Mungu hutamani upendo unaoonyeshwa katika huduma ya moyo, katika huduma ya Roho, na katika huduma ya nguvu za kimwili. Hatupaswi kuwa duni katika aina yoyote ile kwenye utumishi wetu kwa Mungu. Chochote alichotuazima Yeye, tunapaswa kukitumia kwa akili kwa ajili Yake. Mtu anayeufanyia mazoezi uwezo wake kwa kuutumia, hakika atafanya uimarisha, lakini ni lazima atafute kufanya yote yaliyo katika juhudi zake kwa kadri awezavyo. Kuna haja ya kuwa na uwezo wa akili ulioelimishwa kubuni mbinu bora zaidi katika kilimo, ujenzi, na katika kila idara nyingine, ili mtendakazi asitoke bure bila faida au matunda. {FEsw 315.4}

Sio fadhila au wema kwa wanaume au wanawake kutoa udhuru kwa kazi isiyo na ufanisi, isiyo nadhifu, iliyoborongwa au inayofanywa pole pole (kama kinyonga). Tabia za kufanya kazi polepole lazima zishindwe/ziachwe. Mtu ambaye anatenda kazi pole pole, anafanya kazi yake kwa hasara, ni mtendakazi asiye na faida. Utendaji wake wa kazi polepole ni kasoro inayohitaji kuonekana na kusahihishwa.

Anatakiwa kutumia na kuizoesha akili yake katika kuweka mikakati ya jinsi ya kutumia muda wake ili kupata matokeo bora. Wakati mtu anakuwa daima kazini, na kazi haikamiliki kamwe, ni kwa sababu akili na moyo havijawekwa kazini. Inachukua baadhi ya watu masaa kumi kukifanya kile ambacho mwingine hutimiza kwa urahisi kabisa kwa masaa matano. Wafanyikazi kama hao hawahusishi busara, mikakati na mbinu katika kazi zao. Kuna kitu cha kujifunza kila siku kuhusu jinsi ya kuboresha namna ya kufanya kazi ili kumaliza kazi, na kuwa na wakati wa kitu kingine. Ni wajibu wa kila mfanyakazi kutoa sio nguvu zake tu bali zake nia na akili kwa kile anachoazimia kukifanya. Baadhi ya wanaojishughulisha na kazi ya ndani au nyumbani daima wako kazini; si kwa sababu wao wana mengi ya kufanya, bali hawaweiki mikakati ya kuwa na wakati. Wanapaswa kujipa goli la muda fulani wa kukamilisha kazi yao, na kufanya kila hatua wanayochukua kunena hilo lengo lao. Kuwa butu au mjinga sio wema (kama si wema utakuwa ni ubaya!). Unaweza kuchagua kuwa na unyanyapaa kuelekea kwenye hatua zenye mwenendo mbaya kwa sababu huna dhamira ya kujikagua mwenyewe na kujithibithi na kufanya matengenezo/kurekebisha, au unaweza kusitawisha uwezo wako wa kutenda huduma kwa ubora zaidi, na kisha utajipata mwenyewe ukiwa na soko kila mahali, yaani watu wakikuhitaji. Utathaminiwa kwa jinsi unavyostahili. “Lolote mkono wako utakalolipata kulifanya, ulifanye kwa nguvu zako.” “Msiwe wavivu katika biashara; bidii katika Roho; kumtumikia Bwana.” {FEsw 316.1}

Australia inahitaji chachu ya hekima thabiti, akili ya kuzaliwa nayo au busara itambulishwe kwa wingi/ukarimu kwenye miji na vijiji vyake vyote. Kuna haja ya elimu sahihi. Shule zianzishwe sio kwa madhumuni ya kupata tu maarifa kutoka kwenye vitabu, bali maarifa ya sekta ya vitendo na stadi. Watu wanahitajika katika jumuiya tofauti kuonyesha watu jinsi utajiri unavyopatikana kutoka kwenye udongo. Kilimo cha ardhi kitaleta matunda yake. {FEsw 316.1}

Kupitia maadhimisho ya siku kuu watu wote wa dunia na wa makanisa wameelimishwa kuamini siku hizi za kuishi kivivu ni muhimu kwa afya na furaha; lakini matokeo yanadhihirisha kwamba zimejaa uovu, ambao unaiangamiza nchi. Vijana kwa ujumla hawajaelimishwa kuhusiana na tabia za uadilifu wenye bidii. Miji na hata vijiji vinazidi kuwa kama Sodoma na Gomora, na kama ulimwengu katika siku za Nuhu. Mafunzo ya vijana siku hizo yalikuwa na utaratibu na kanuni ambazo watoto wa zama hizi wanafundishwa, kupenda msisimko, kujitukuza wenyewe, kufuata mawazo ya mioyo yao miovu. Sasa kama wakati huo, upotovu, ukatili, uharamia, na uhalifu ndiyo matokeo yake. {FEsw 316.2}

Mambo haya yote ni mafunzo kwetu. Wachache sasa, ndiyo walio na bidii ya kazi na stadi na wanaishi kwa kujali uchumi. Umaskini na dhiki viko kila upande. Kuna wanaume wanaofanya kazi kwa bidii, na kupata mishahara au matunda kidogo sana kwa kazi yao. Kuna haja ya maarifa mengi zaidi kuhusiana na kuuandaa udongo. Jicho halijaweza kuona kwa upana kile kinachoweza

kupatikana kutoka kwenye ardhini. Utaratibu finyu na usiobadilika unafuatwa na matokeo yake yanakatisha tamaa. Uuzaji wa ardhi ili kujipatia pesa kwa haraka {land boom kama ya Florida} umelaani nchi hii, bei ya kupita kiasi imelipwa kwa ardhi iliyonunuliwa kwa mkopo; kisha ardhi hii lazima isafishwe na kukatuliwa, na pesa nyingi zinatumika; kisha kujenga nyumba hapo kunagharimu fedha zaidi, na kisha riba inakuja na kinywa chake kikubwa kutafuna faida yote. Madeni hujilimbikiza, na kisha huja kufungwa na kufilisika kwa mabenki, na kisha mkopaji anaposhindwa kufanya malipo yake ya rehani. Yeye anazuiliwa kuimiliki nyumba na kujaribu kuiuza nyumba hiyo {anakuwa amepoteza nyumba na pesa yote aliyoanza kuitoa ili kuanza kuilipia nyuma na kiwanja-foreclosure}. Hii hutokea kwa sababu mikopo ya nyumba inalindwa na makampuni yanayouza nyumba ikimaanisha kuwa nyumba yako itatumika kama dhamana. Maelfu wamefukuzwa kazi ghafla; familia hupoteza kila kitu kidogo, wanakopa na kukopa, halafu wanalazimika kutoa mali zao na kutoka bila senti (nyumba na ardhi). Pesa nyingi na kazi ngumu zimewekwa katika mashamba yaliyonunuliwa kwa mikopo, au kurithiwa kwa kulazimishwa. Wakazi hawa waliishi kwa matumaini ya kuwa wamiliki halisi, na ingeweza kuwa hivyo, lakini kwa kufilisika kwa mabenki nchini kote hilo halikuwezekana. (angalia jinsi unavyoweza kuisimulia foreclosure na mtu aelewe kirahisi) {FEsw 317.1}

Sasa kuna zile kesi za watu ambao wanamiliki eneo lao bila kuwa na madeni na mtu, hawa wana furaha, na ndio pekee yao wasiohusika na taabu hii iliyoelezwa. Wafanyabiashara wanashindwa, familia zinaateseka kwa kutopata chakula na mavazi. Hakuna kibarua kinachojitokeza chenyewe. Lakini sikukuu au sherehe zimejaa tele. Kwenye maburudisho hayo, watu wanajiingiza kwa hamu kubwa. Wote wanaoweza kufanya hivyo watatumia shilingi, dola na senti zao walizochuma kwa bidii ili tu waonje starehe, kwa vileo vikali, au kujifurahisha kwa anasa zinginezo. Magazeti yanayoripoti umaskini wa watu, yanaweka kwenye matangazo yao mara kwa mara juu ya mbio za farasi, na zawadi zinazokabidhiwa kwa ajili ya aina mbalimbali za michezo ya kisisimua. Maonyesho, drama, sinema, na burudani hizo zote za kuharibu maadili, vinachukua pesa kutoka kwa taifa, na kisha umaskini unazidi kuongezeka. Watu maskini kabisa watawekeza shilingi yao ya mwisho kwenye bahati nasibu, wakitumaini kupata tuzo, na kisha wanalazimika kuombaomba chakula ili kudumisha uhai, au kutembea na njaa. Wengi hufa kwa njaa, na hukomesha maisha yao. Mwisho wa dunia haujafika bado. Wanaume wanakupeleka kuona bustani zao za michungwa na malimau, na matunda mengineyo, na kukuambia kuwa mazao ya mashambani na kazi ya kilimo hailipi ukilinganisha na uwekezaji uliofanya wa hali na mali. Haiwezekani kupata riziki ya mwaka mzima, ndipo wazazi huamua kwamba watoto wao hawatakuwa wakulima; nao hawana ujasiri na matumaini ya kuwaelimisha kulima udongo tena. {FEsw 318.1}

i Kinchohitajika katika hizi shule kuelimisha na kuwafunza vijana ili wajue jinsi ya

kuishinda hali hii ya mambo. Kuna ulazima wa kuwa na elimu katika sayansi, na elimu katika mipango na mbinu katika kufanyia kazi udongo. Kuna matumaini katika udongo, lakini ubongo na moyo na nguvu lazima viletwe katika kazi ya kuilima. fedha zinazotolewa kwa mbio za farasi, kwenda ukumbi wa michezo/sinema, kamari na bahati nasibu; pesa zinazotumiwa katika baa kwa ajili ya bia na vileo vikali, —acheni hizi zitumike katika kuifanya ardhi kuwa na tija, na tutaona hali tofauti ya mambo. {FEsw 318.1}

Nchi hii inahitaji wakulima walioelimika. Bwana huwapa manyunyu ya mvua na miale ya jua yenye baraka. Huwapa wanadamu uwezo wao wote; Hebu na watoe moyo na akili na nguvu katika kufanya mapenzi Yake utiifu kwa amri Zake. Hebu na waache tabia yoyote hatarishi/haribifu, kamwe wasitoe senti kwa ajili ya bia, pombe ya aina yoyote, wala tumbaku, wasiwe na uhusiano wowote na mbio za farasi au michezo kama hiyo, na kisha wajikabidhi wenyewe kwa Mungu, wakifanya kazi pamoja na karama waliojaliwa ya nguvu za kimwili, na kisha kazi yao haitakuwa bure. Mungu ambaye ameiumba dunia kwa manufaa ya mwanadamu, atatoa njia na uwezo kutoka kwenye ardhi ili kumtegemeza mtenda kazi mwadilifu. Mbegu iliyowekwa ndani udongo uliotayarishwa vizuri, itazaa mavuno yake. Mungu anaweza kuandaa na kutandaza meza kwa ajili ya watu wake nyikani/jangwani. {FEsw 319.1}

Stadi, ufundi na kazi mbalimbali zinapaswa kujifunzwa, na zinataka mtu azifanyie mazoezi [katika nyanja mbalimbali \(anuwai\) za kiakili na kimwili](#); kazi zinazozohusicha kukaakaa kwenye kiti zina hatari zaidi, kwa kuwa zinawaondoa watu kutoka kwenye anga wazi na jua, na kufundisha seti moja tu ya vitivo (uwezo wa akili tu), wakati viungo vingine vinakuwa dhaifu kutoka kutotumiwa. Watu huendeleza kazi zao, hukamilisha biashara zao kwa uzuri, na punde wanaingia kaburini kulala mapema. Mazingira mazuri zaidi ni yule mtu ambaye kazi yake inamweka kwenye hewa iliyo wazi nje ya nyumba, akifanya mazoezi ya misuli, wakati ubongo unatozwa ushuru sawa, na viungo vyote vina fursa ya kufanya kazi zake. Kwa wale ambao wanaweza kuishi nje ya miji, na kufanya kazi chini ya anga lililo wazi, wakitazama kazi za Msanii Mkuu, mandhari mpya inaendelea kufunuliwa. Wanavyoendelea kufanya kitabu cha asili (uumbaji) kuwa somo lao, ushawishi wa kulainisha na kutiisha huwajia juu yao; kwa maana wanatambua utunzaji wa Mungu uko juu ya yote, kuanzia kwenye kwenye jua tukufu Mbinguni mpaka kwa shomoro mdogo wa kahawia au mdudu mdogo kabisa aliye na uzima. Ukuu wa Mbinguni umetuelekeza kwenye mambo haya ya uumbaji wa Mungu kama ushahidi wa upendo Wake. Yeye aliyeyaumba maua amesema: “Fikirini maua ya mashamba, jinsi yameavyo; hayafanyi kazi, wala hayasokoti nami nawaambia, ya kwamba hata Sulemani katika fahari yake yote hakuvikwa vizuri kama mojawapo la hayo. Basi, ikiwa Mungu huyavika hivi majani ya kondeni, yaliyopo leo, na kesho hutupwa kalibuni, je! Hatazidi sana kuwavika ninyi, enyi wa imani haba?” Bwana Ndiye Mwalimu wetu, na chini ya maagizo Yake tunaweza kujifunza masomo ya thamani

zaidi kutoka kwa uumbaji/maumbile. {FEsw 319.2}

Ulimwengu uko chini ya laana ya dhambi, na bado katika uozo wake bado ni mzuri sana. Ikiwa haukutiwa unajisi na waovu, watu wafisadi wanaotembea juu ya udongo, tungeweza, kwa baraka ya Mungu, kufurahia ulimwengu wetu kama ulivyo. Lakini ujinga, kupenda anasa, na mazoea ya dhambi, yanayochafua Roho, mwili na Roho, hujaza ulimwengu wetu na ukoma wa maadili; hewa mbaya ya kimaadili {malaria ya maadili} inaangamiza maelfu na makumi ya maelfu. Nini kifanyike basi ili kuokoa vijana wetu? Sisi tunaweza kufanya kidogo tu, lakini Mungu anaishi na kutawala, Naye Anaweza kufanya mengi. Vijana ndio tumaini letu la kazi ya umishonari. {FEsw 320.1}

Shule zinapaswa kuanzishwa mahali ambapo kuna mengi kwa kadri iwezekanavyo kupatikana katika maumbile/uumbaji vile ambavyo vinafurahisha hisia na kutoa anuwai kwa mandhari. Wakati tunaepuka vilivyo vidanganyifu (feki) na bandia, na kutupilia mbali mbio za farasi, uchezaji wa karata, bahati nasibu, magomvi ya zawadi, unywaji pombe, na kwa utumiaji wa tumbaku, lazima tutoe vyanzo vya burudani au starehe ambavyo ni safi na tukufu na zenye kuinua. Tunapaswa kuchagua eneo kwa ajili ya shule yetu mbali na miji mahali ambako jicho halitatulika daima kwenye makao ya wanadamu, bali juu ya kazi za Mungu za uumbaji; ambapo kutakuwa na maeneo ya kuvutia kutembelea, zaidi ya yale ambayo jiji linaruhusu. Waache wanafunzi wetu wawekwe mahali ambapo asilia inaweza kuzungumza na hisia, na kwa sauti yake wapate kusikia sauti ya Mungu. Hebu na wawe pale wanapoweza kutazama kazi Zake za ajabu, na kupitia asili kumtazama Muumba. {FEsw 320.2}

Vijana katika nchi hii wanahitaji bidii za dhati zaidi kuhusiana na kazi ya kiroho kuliko katika nchi nyingine yoyote ambayo tumetembelea. Majaribu yana nguvu nyingi na ni mengi; Siku kuu nyingi na tabia za kivivu ni nyingi na zisizofaa kwa vijana wetu. Shetani humfanya mtu asiye na kazi kuwa mshiriki na mfanyakazi mwenza katika mipango yake, na Bwana Yesu hakai ndani ya moyo wake kupitia imani. Watoto na vijana hawajaelimishwa kutambua kwamba ushawishi wao ni nguvu ya wema au kwa uovu. Ni lazima umilele uwekwe mbele yao na kuonyesha ni kiasi gani wanaweza kutimiza; wanapaswa kuhimizwa kufikia kiwango cha juu cha uadilifu. Lakini kutoka ujana wao wameelimishwa kwa wazo maarufu kwamba sikukuu zilizoteuliwa lazima zichukuliwe kwa heshima na kuzingatiwa. Kutokana na Nuru ambayo Bwana amenipa, siku hizi za sikukuu hazina ushawishi kwa wema kuliko zile ibada zinazotolewa kwa miungu ya kipagani; hakika hizi sikukuu hazina tofauti na kuabudu hiyo miungu ya kipagani. Siku hizi tunazoishi ni misimu maalumu ya Shetani kujipatia mavuno. Pesa inayopatikana kwa wanaume na wanawake inatumika kwa kile ambacho simkate. Vijana wameelimishwa kupenda vitu ambayo vinakatisha tamaa na kupoteza ujasiri, mambo ambayo Neno la Mungu linashutumu. Ushawishi kwa uovu na uovu peke yake unaendelea daima.

{FEsw 320.3}

Kazi za mikono kwa vijana ni muhimu. Akili haipaswi kuchoshwa kila mara kwa kupuuzoa nguvu za kimwili. Ujinga wa fiziolojia (utendaji wa mwili na sehemu zake), na kupuuzwa kufuata sheria za afya; zimewaleta wengi makaburini ambao wangeishi na kufanya kazi ngumu na kujifunza kwa kutumia akili zao ipasavyo. Mazoezi sahihi ya akili na mwili, yataendeleza na kuimarisha uwezo wote wa mwili. Akili na mwili itaweza kuhifadhiwa, na itakuwa na uwezo wa kufanya kazi za aina mbalimbali. Wachungaji na waalimu wanahitaji kujifunza kuhusiana na mambo haya, na kuyafanyia kazi kivitendo. matumizi sahihi ya nguvu zao za kimwili, kama ya nguvu za kiakili, yatasawazisha mzunguko wa damu, na kuweka kila kiungo cha mashine hai ya mwili katika utaratibu na uendeshaji unaofaa. Akili mara nyingi hutumiwa vibaya; Inachochewa au kuchokozwa na wazimu wa kufuata mstari mmoja wa mawazo; na kutumiwa kwa kupitiliza kwa nguvu za ubongo na kupuuzwa kwa viungo vya kimwili hujenga hali ya ugonjwa katika mfumo. Kila kitivo cha akili kinaweza kuzoezwa kutenda kwa usalama kwa kulinganisha, ikiwa nguvu za kimwili zinatumia kwa usawa, na masomo yanatofautiana (anuwai, akili isilishwe somo lile lile saa zote). Tunahitaji mabadiliko ya kazi, na asili ni mwalimu aliye hai, na aliye na afya. {FEsw 321.1}

Wanafunzi wanapoingia shuleni kupata elimu, waalimu wanapaswa kujitahidi kuwazunguka na vitu vyenye tabia ya kupendeza zaidi, ya kuvutia, ili akili isifungiwe kwenye masomo ya vitabu ambavyo ni mfu (uumbaji ni vitabu hai, masomo yake ni halisi, yana uzima). Shule haipaswi kuwa ndani au karibu na mji, ambamo ubadhirifu wake, anasa zake ovu, na uovu wake katika mila na desturi, utahitaji kazi ya mara kwa mara ili kuupinga uovu ulioenea, ili usije ukatia sumu kwenye angahewa yenyewe ambayo wanafunzi wanapumua. Shule zote kwa kadiri inavyowezekana zinapaswa kuwepo pale ambapo jicho litatulia juu ya mambo ya asili badala ya makundi ya nyumba. Mandhari inayobadilika kila wakati itaridhisha ladha, na kudhibiti mawazo. Hapa kuna mwalimu aliye hai, anayefundisha daima.

{FEsw 321.2}

Nimekuwa nikisumbuliwa na mambo mengi kuhusiana na shule yetu. Katika kazi zao, vijana wanahusishwa na wasichana, na wanafanya kazi ambayo ni ya wanawake. Hii ndiyo kazi pekee inayoweza kupatikana hapo kutokana na mazingira ya pale walipo sasa; lakini kutokana na Nuru niliyopewa, hii sio aina ya elimu ambayo vijana wa kiume wanahitaji. Haiwapi maarifa wanayohitaji kwenda nayo majumbani mwao. Kunapaswa kuwa na aina tofauti ya kazi iliyofunguliwa mbele yao, ambayo ingewapa nafasi ya kuzitunza nguvu zao za kimwili kwa kuzishughulisha sawa na zile za kiakili. Ardhi inapaswa iwepo kwajili ya kilimo. Muda hauko mbali wakati sheria zinazopinga Kazi kufanywa siku ya Jumapili zitakuwa ngumu zaidi, na juhudi inapaswa kufanywa ili kupata ardhi mbali na miji, ambapo matunda na mboga vinaweza kuoteshwa/kulimwa. Kilimo kitafungua

vyanzo vya shule kujitegemea, na stadi au biashara nyingine mbalimbali pia zinaweza kufunzwa. Kazi hii ya bidii na ya dhati inahitaji nguvu ya akili na misuli. Mbinu na busara vyahitajika hata katika kukuza matunda na mboga kwa mafanikio. Na tabia za uadilifu katika kazi, na stadi zitaonekana kuwa msaada muhimu kwa vijana katika kupinga majaribu. {FEsw 322.1}

Hapa panafunguliwa uwanja wa kutoa nguvu zao ambazo zilikuwa zimefungiwa ndani, nguvu ambazo ikiwa hazitatumika katika ajira yenye manufaa, zitakuwa chanzo cha kudumu kwa majaribu kwao wenyewe na kwa walimu wao. Kazi nyingi na za aina mbali mbali kutokana na haiba ya mtu au watu tofauti zinaweza kubuniwa. Lakini kufanya kazi na ardhi, kutakuwa, baraka maalum kwa mfanyakazi. Kuna hitaji kubwa la watu wenye akili kulima udongo, watu ambao watakuwa makini na watendaji wakamilifu katika kazi zao. Maarifa haya hayatakuwa kikwazo kwa elimu muhimu za biashara au kwa manufaa katika mstari wowote ule. Kukuza uwezo wa udongo kunahitaji umakini na akili. Kazi hii haitakuza misuli tu, lakini hata uwezo wa kujifunza, kwa sababu ubongo na misuli hutenda kazi kwa usawa {balansi}. Tunapaswa kuwafundisha vijana kwa njia ambayo watapenda kufanya kazi na ardhi, na kufurahia kuiboresha. Matumaini ya kuendeleza kazi ya Mungu katika nchi hii yanahusiana na kujenga maadili mapya katika ladha ya kupenda kazi, ambayo itageuza akili na tabia. {FEsw 322.2}

Ushahidi wa uwongo umetolewa katika kulaani ardhi ambayo, kama kazi inayostahili ingefanyika hapo, basi faida kubwa ingepatikana. Mipango finyu, nguvu kidogo zilizowekwa, utafiti mdogo kuhusu mbinu bora, vinatoa sauti kubwa kwa ajili ya matengenezo ya dhana hizi. Watu wanahitaji kujifunza kwamba kazi yenye subira italeti maajabu. Kuna maombolezo mengi juu ya udongo usio na rutuba, na usioleta mazao, endapo watu wangesoma Maandiko ya Agano la Kale wangeona kwamba Bwana alijua vizuri zaidi kuliko wao kuhusiana na tiba sahihi ya ardhi. Baada ya kulimwa kwa miaka kadhaa, na kutoa hazina yake kwa milki ya mwanadamu, sehemu za ardhi ziruhusiwe kupumzika (yubilee ya miaka saba), na kisha mazao yaweze kubadilishwa (crop rotation). Tunaweza kujifunza mengi pia kutoka kwenye Agano Jipya kuhusiana na tatizo la kazi. Ikiwa watu wangepuata maagizo ya Kristo kuhusiana na kuwakumbuka maskini na kuwasaidia katika mahitaji yao, mahali hapa pangukuwa na tofauti ya ajabu kiasi gani! {FEsw 323.1}

Hebu Utukufu wa Mungu uwekwe daima machoni; na ikiwa mavuno yameharibika, basi usivunjike moyo; jaribu tena; lakini kumbuka kuwa huwezi kuvuna vyema isipokuwa ardhi imetayarishwa ipasavyo kwa ajili ya mbegu; kushindwa kunaweza kuwa ni kwa ajili ya kupuuzia kabisa kipengele hiki. {FEsw 323.2}

Shule itakayoanzishwa Australia inapaswa kuleta suala la tasnia mbele, na kufichua ukweli kwamba kazi ya kimwili ina nafasi yake katika mpango wa Mungu kwa kila mtu, na kwamba baraka Zake zitahudhuria kazi yao. Shule zilizoanzishwa

na wale wanaofundisha na kuishi Ukweli wa wakati huu, zinapaswa kushughulikiwa kwa jinsi inayoleta motisha za kuburudisha na mpya katika kila aina ya kazi ya vitendo zenye manufaa katika maisha ya kila siku. Kutakuwa na mengi ya kujaribu/kutahini waelimishaji, lakini jambo kubwa na adhimu litakuwa limepatikana wakati wanafunzi watapojisikia kwamba upendo wa Mungu umefunuliwa mioyoni mwao, si tu katika kujitoa moyo, akili na nafsi tu, lakini katika matumizi ya nguvu zao kwa busara. Majaribu yao yatakuwa pungufu sana; kutoka kwao kanuni na mfano, Nuru itaangaza katikati ya nadharia potofu na desturi za mapokeo/mitindo ya ulimwengu. Ushawishi wao utaelekea kusahihisha wazo potofu lisemalo kwamba 'ujinga au kutojua ndio alama ya muungwana'. {FEsw 323.3}

Mungu angetukuzwa ikiwa watu kutoka nchi zingine ambao wamejipatia maarifa ya akili ya kilimo, wangefikia kwenye hii nchi, na kwa kanuni na mfano wangewafundisha watu jinsi ya kulima udongo/ardhi, ili wapate mazao yenye hazina nyingi. Wanatafutwa watu wa kuelimisha wengine jinsi ya kulima, na jinsi ya kutumia zana za kilimo. Ni nani ambao watakuwa wamisionari kuifanya kazi hii, wakaofundisha mbinu sahihi vijana, na kwa wale wote wanaojisikia wana utayari na unyenyekevu wa kutosha kujifunza? Kama hakuna yoyote ambaye anataka umpe mawazo haya bora, hebu masomo haya yawe yakitolewa kimyakimya, ikionyesha nini kifanyike katika kutengeneza bustani ya miti ya matunda, kupanda nafaka/mahindi; acha mavuno yazungumze kwa ufasaha na kuonyesha upendeleo wa njia sahihi ya kazi. Toa neno kwa majirani zako unapoweza, endelea kuboresha utamaduni wa ardhi yako mwenyewe, na hiyo itaelimisha. {FEsw 324.1}

Inaweza kuhimizwa na wengine kwamba shule yetu lazima iwe katika jiji ili kutoa ushawishi kwa kazi yetu, na kwamba ikiwa iko vijijini, ushawishi unapotea kwa miji; lakini hii si lazima iwe hivyo. {FEsw 324.2}

Vijana wanaohudhuria shule yetu kwa mara ya kwanza, hawajatayarishwa kutoa ushawishi sahihi katika jiji lolote kama taa zinazomulika katikati ya jiji. giza. Hawatakuwa tayari kuakisi mwanga hadi giza la elimu yao potofu linaondolewa. Katika siku za usoni shule yetu haitakuwa sawa kama ilivyokuwa zamani. Miongoni mwa wanafunzi kumekuwa na watu wa kuaminika, wenye uzoefu ambao wamechukua faida ya fursa ya kupata maarifa zaidi ili kufanya kazi ya akili katika kazi ya Mungu. Hawa wamekuwa msaada katika shule, kwa kuwa wamekuwa kama gurudumu lililo na usawa; lakini katika siku zijazo shule itajumuisha wengi wanaohitaji kubadilishwa katika tabia, na watakaohitaji kazi nyingi ya subira kufanyika kwao; hawana budi kuondoa mawazoni yale waliyojifunza awali na kisha, kujifunza mengine. Itachukua muda kukuza Roho ya kweli ya kimisionari, na kadri wanavyosogezwa mbali zaidi na miji na majaribu yanayofurika huko, ndivyo itakavyopendeza zaidi kwao kupata maarifa ya Kweli na kukuza tabia zenye uwiano mzuri. {FEsw 324.3}

Wakulima wanahitaji akili zaidi katika kazi zao. Katika hali nyingi ni kosa lao wenyewe ikiwa hawaoni ardhi ikitoa mavuno yake. Wao wanapaswa kujifunza daima jinsi ya kupata aina mbalimbali za hazina kutoka ardhini. Watu wanapaswa kujifunza kadri inavyoweze kutegemea juu ya bidhaa ambazo wanaweza kupata kutoka kwenye udongo. Katika kila awamu ya aina hii ya kazi wanaweza kuelimisha akili kufanya kazi kwa ajili ya kuokoa Roho ambazo Kristo alizifia. “Ninyi ni shamba la Mungu; ninyi ni jengo la Mungu.” Waache walimu katika shule zetu wachukue wanafunzi pamoja nao kwenye bustani na mashamba, na wawafundishe jinsi gani wafanye kazi na udongo kwa namna bora zaidi. Ingekuwa vyema kama wachungaji ambao ni watenda kazi kwa Neno au kwa Mafundisho (Doctrines) wangeweza kuingia mashambani na kutumia kiasi fulani cha sehemu ya siku katika mazoezi ya viungo na wanafunzi. Wao angeweza kufanya kama Kristo alivyofanya katika kutoa masomo kutoka kwenye uumbaji/asili ili kuonyesha Ukweli wa Biblia. Walimu na wanafunzi wangekuwa na mengi zaidi yenye uzoefu wenye afya katika mambo ya kiroho, na akili zenye nguvu zaidi na mioyo safi katika kutafsiri siri na mafumbo ya milele, kuliko wanavyoweza katika kusoma vitabu kila mara, na kuutumikisha ubongo bila kuichosha misuli. Mungu amewapa wanaume na wanawake uwezo wa kufikiri, na Angetaka wanadamu watumie akili zao kuhusiana na matumizi ya miili yao (mashine ya mwili). Swali laweza kuulizwa, Je! anawezaje kupata hekima, yeye ashikaye jembe, na kuendesha plau ya ng'ombe? - Kwa kuitafuta hekima kama fedha, kuitafuta kama hazina iliyositirika. “Kwa maana Mungu wake anamwagiza vizuri na kumfundisha” “Hayo nayo yatoka kwa Bwana wa majeshi, mwenye shauri la ajabu, apitaye wote kwa hekima yake.” {FEsw 325.1}

Yeye aliyewafundisha Adamu na Hawa katika Edeni jinsi ya kutunza bustani, anawafundisha watu leo. Kuna hekima kwa kila anayeshikilia jembe kulima, na kuotesha au kupanda mbegu. Ndani ya ardhi imefichwa hazina, na Bwana angetaka maelfu na makumi ya maelfu ya watu waliosongamana katika miji kufanya kazi juu ya udongo badala ya kukaa mijini wakiangalia jinsi ya kubahatisha kujipatia visenti kidogo; katika hali nyingi visenti hivyo vidogo havijageuzwa kuwa mkate, bali huwekwa katika uwekezaji wa mtoza ushuru na mwuza pombe, ili kupata kile ambacho huharibu hekima na akili ya mwanadamu aliyeumbwa kwa mfano wa Mungu. Wale ambao watazipeleka familia zao mashambani, huziweka pale palipo na majaribu machache. Watoto walio na wazazi wanaompenda na kumcha Mungu, wako katika kila hali bora zaidi ya kujifunza juu ya Mwalimu Mkuu, ambaye ni chanzo na chemchemi ya hekima. Wana nafasi nzuri zaidi ya kupata kufaa kwa ajili ya ufalme wa Mbinguni. Wapeleke watoto kwenye shule zilizoko mjini, mahali ambapo kila awamu ya majaribu inangoja kuwavutia na kuwakatisha tamaa, na kazi ya kujenga tabia ni ngumu mara kumi kwa wazazi wote wawili na watoto. {FEsw 326.1}

Dunia itafanywa kutoa nguvu zake; lakini bila baraka za Mungu haitaweza kufanya lolote. Hapo mwanzo, Mungu alitazama vile vyote alivyoviumba, na

akavitangaza kuwa vyema sana. Laana ililetwa duniani kwa sababu ya dhambi. Lakini Je, hii laana iongezeke kwa kuongezeka dhambi? Ujinga unafanya kazi yake isiyo rafiki. Watumishi wavivu wanazidisha uovu kwa tabia zao za uvivu. Wengi hawataki kupata chakula chao kwa jasho la nyuso zao wenyewe, na wanakataa kulima udongo. Lakini ardhi ina baraka zilizofichwa ndani yake kina chake, kwa wale walio na ujasiri, nia na uvumilivu kukusanya hazina zake. Baba na mama ambao wana kipande cha ardhi na nyumba inayoleta faraja, hakika wao ni wafalme na malkia. {FEsw 326.2}

Wakulima wengi wameshindwa kupata mapato ya kutosha kutoka kwenye ardhi kwa sababu wamefanya kazi kana kwamba ni ajira duni; hawaoni kuwa kuna baraka ndani yake kwa ajili yao na familia zao. Wanachoweza kutambua ni chapa tu ya utumwa. Mashamba yao ya matunda yamepuuzwa, mazao hayajapandwa wakati wa msimu sahihi, na kazi ya juu juu tu inafanywa katika kulima udongo. Wengi hupuuza mashamba yao ili kutunza sikukuu, na kuhudhuria mbio za farasi na vilabu vya kubeti pesa zao zinatumika kwenye maonyesho, bahati nasibu na uvivu, na kisha wanasihi kwa kulia kwamba hawawezi kupata fedha za kulima udongo na kuboresha mashamba yao; lakini wangukuwa na pesa zaidi, matokeo bado yangukuwa yale yale tu. {FEsw 327.1} —[Special Testimonies on Education, FEswbruari, 1894.](#)

Sura ya 42

MAANDALIZI YA HARAKA YA KAZI

Nimekuwa nikisumbuliwa sana kwa usiku kadhaa. Nimesumbuliwa hadi nikashindwa kulala vizuri. Mambo yanasisitizwa kwenye umakini wangu, ambayo ni lazima niyawasilishe kwenu. {FEsw 334.1}

Walimu katika shule zetu katika kituo cha Sanitarium cha tiba mbadala na Chuo cha Battle Creek lazima wawe macho kila wakati, ili mipango yao na usimamizi wao wa kibinadamu visije kujigandamiza na kuwakatisha tamaa wanafunzi na kisha kuzima imani ya wanafunzi ambayo wamekuwa nayo mioyoni kwa kuvutiwa kwa kina wa Roho Mtakatifu. Wamesikia sauti ya Yesu ikisema, “Mwanangu, nenda ukafanye kazi leo katika shamba Langu la mizabibu.” Wanahisi hitaji la kozi inayofaa ya masomo, ili waweze kuwa tayari kufanya kazi kwa ajili ya Bwana, na kila juhudi inapaswa kufanywa ili kuharakisha maendeleo yao; lakini lengo la elimu yao lazima liweke mbele daima. Ucheleweshaji usio wa lazima haupaswi kushauriwa wala kuruhusiwa. Wale watu ambao wamejishughulisha na kusaidia

kuwakimu wanafunzi hawa wakati wa masomo yao hupata hasara kubwa ya muda na pesa zilizotumika bila busara. Watu hawa wamedhihirisha bidii, unyofu na utayari wao wa kusaidia; lakini wanakata tamaa kwani wanaona muda uliokadiriwa hapo awali kuwa muhimu kwa wanafunzi kupokea kufaa kwao kwa ajili ya kazi, unarefushwa, na bado wanafunzi wanahimizwa kuchukua kozi nyingine ya masomo kwa gharama yao. Miaka inapita; na bado wanafunzi wanahimizwa hitaji la elimu zaidi. Mchakato huu wa muda mrefu, na wa kuongeza na kuzidisha muda zaidi, na kozi nyingine, ni mojawapo ya mitego ya Shetani kuwaridisha nyuma watendakazi.

{FEsw 334.2}

Wanafunzi wenyewe hawangefikiria uchelewesho huo katika kuingia kazini, ikiwa hawakushurutishwa na wale wanaopaswa kuwa wachungaji na walezi, na ambao ni walimu na matabibu wao. Kama tungekuwa na miaka elfu moja mbele yetu, kina kama hicho cha maarifa kisingehitajika, ingawa kunaweza kuwa na mengi zaidi ya kufaa; lakini sasa wakati wetu ni mchache. Imesemwa, “Leo kama mtaisikia sauti Yake, wala msifanye migumu mioyo yenu.” {FEsw 334.3}

Sisi si wa kundi lile ambalo hufafanua kipindi halisi/mahususi cha wakati ule utakaopita kabla ya kuja kwa Yesu mara ya pili kwa nguvu na Utukufu mwingi. Wengine wameweka muda, na muda huo umepita, Roho zao za ‘kulabudisha’ hazijakubali kukemewa, lakini wameweka muda mwingine na mwingine (tarehe); lakini wengi wameshindwa mfululizo na wakawapigwa chapa kama manabii wa uongo. “Mambo ya siri ni mali yake BWANA Mungu wetu; lakini mambo yaliyofunuliwa ni yetu sisi na watoto wetu milele.” Licha ya ukweli kwamba wapo manabii wa uongo, wapo pia wanaohubiri Ukweli kama unavyofunuliwa katika Maandiko. Kwa unyofu wa kina, kwa Imani yenye uaminifu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu, wanachochea akili na mioyo kwa kuwaonesha kwamba tunaishi karibu na ujio wa pili wa Kristo, lakini siku na saa ya kuja Kwake ni zaidi ya ufahamu wa mwanadamu; kwa maana “hakuna aijuaye siku ile wala saa ile, hata malaika wa Mbinguni, bali Baba peke yake.” {FEsw 335.1}

Lakini ipo siku ambayo Mungu ameiweka kwa ajili ya kufunga historia ya dunia hii. Injili hii ya ufalme itahubiriwa katika ulimwengu wote kuwa ushuhuda kwa mataifa yote; na hapo ndipo ule mwisho utakapokuja.” Unabii unatimia kwa haraka. Mengi, mengi zaidi, yanapaswa kusemwa kuhusu mada hizi muhimu sana. Siku imekaribia ambayo hatima ya kila nafsi itaamuliwa milele. Siku hii ya Bwana inafanya haraka kuja. Walinzi wa uongo wanapaza sauti, “Ni amani-mambo yote yako sawa”; lakini siku ya Mungu inakaribia upesi. Nyayo za hii siku zimezibwa mdomo sana kiasi kwamba sauti yake haiuamshi ulimwengu kutokana na usingizi wa mauti ambao umeiangukia. Wakati walinzi wakilia, “Amani na salama,” “uharibifu huwajia ghafula,” “nao hawataoka”; “Kwa maana ni kama mtego utakavyowajia wale wote wakao juu uso wa dunia yote.” Humnasa mpenda anasa na mwenye dhambi kama mwizi wa usiku. Wakati kila kitu kiko salama, na watu

wameenda kulala na kuridhika kwa mapumziko, ndipo mwizi anayezunguka-zunguka akiwinda kwa siri, usiku wa manane huiba mawindo yake Wakati kumecheleweshwa sana kuuzuia uovu, itagunduliwa kuwa mlango au dirisha fulani halikufungwa ili kuleta usalama. "Jiwekeni tayari; kwa maana katika saa msiyodhani Mwana wa Adamu Yuaja. "Watu sasa wanatulia katika pumziko, wakijiwazia wakiwa salama katika makanisa maarufu; lakini wote sasa tujihadhari, pasiwepo mahali palipoachwa wazi ili adui apate kuingia. Maumivu makubwa yanapaswa kuchukuliwa kuliweka somo hili mbele za watu. Ukweli mzito haupaswi kuwekwa tu mbele ya watu wa ulimwengu, bali pia mbele ya makanisa yetu wenyewe, kwamba siku ya Bwana itakuja ghafula, bila kutazamiwa. Onyo la kuogofya la unabii linaelekezwa kwa kila nafsi. Hebu asiwepo mtu wa kuhisi kwamba yuko salama kutokana na hatari ya kushangazwa. Hebu kusiwepo tafsiri ya mtu yeyote ya unabii itakayokunyang'anya imani ya maarifa ya matukio ambayo yanaonyesha kwamba tukio hili kubwa liko karibu. {FEsw 335.2}

Pesa ambazo zimekuwa zikitumika katika majengo ya ziada na katika upanuzi kwenye yale majengo yaliyopo huko Battle Creek, zinapaswa kuwa zimetumika kuunda miundombinu ya kufanyia kazi mahali fulani ambapo hakuna chochote kilichofanyika. Mungu hafurahishwi na namna hiyo ambayo mali Zake zimekuwa zikielekea. Kwake Yeye hakuna upendeleo au ubaguzi wa mahali au wa watu. {FEsw 336.1}

Mazoea ya kuwapa watu wachache kila fursa ya Kukamilisha elimu yao katika mistari mingi kiasi kwamba haiwezekani kwao kuitumia yote, ni jeraha badala ya faida kwa yule ambaye ana fursa nyingi, zaidi ya hilo, jambo hilo huwanyima wengine fursa muafaka sana. Kama kungekuwa na pungufu zaidi ya maandalizi haya yanayoendelea kwa muda mrefu, na kujielekeza kusikokuwa kwa kipekee kwa kusoma vitabu tu, basi kungekuwa na fursa nyingi zaidi za kuongeza imani ya wanafunzi kwa Mungu. Yeye ambaye kwa muda mrefu hutumia nguvu zake zote kwa masomo peke yake, anavutwa na kuisimuliwa, - anazama ndani ya vitabu vyake, na kupoteza mwelekeo wa lengo ambalo alianza wakati alipokuja shuleni. Imenyeshwa kwangu kuwa baadhi ya wanafunzi wanapoteza hali yao ya kiroho/ukiroho, kwamba imani yao inazidi kuwa dhaifu, na kwamba hawana ushirika au mawasiliano ya kudumu na Mungu. Wanatumia karibu muda wao wote katika kusoma vitabu; wanaonekana kujua machache sana kuhusu mambo mengineyo. Lakini maandalizi haya yote yatakuwa na faida gani kwao? Je, watapata faida gani kwa muda na pesa zote wanazotumia? Nawaambia, itakuwa mbaya zaidi kuliko hasara. Lazima kazi ya namna hii ifanywe kwa udogo sana, na la zaidi ni kukita imani katika nguvu za Mungu. -Watu wanaozipenda amri za Mungu wanapaswa kuushuhudia ulimwengu imani yao kwa matendo yao. {FEsw 336.2}

Wanafunzi wanapokuja Battle Creek kutoka umbali mrefu na kwa gharama kubwa, wakitarajia kupokea maelekezo ya jinsi ya kuwa wamishionari waliofaulu,

wazo hilo halipaswi kuzamishwa katika masomo mbalimbali/anuwai. Hebu Mfikirie Musa; mzigo wake mmoja uliokuwa mkubwa katika nafsi yake ulikuwa kwamba uwepo wa Mungu uwe pamoja naye, na kwamba aweze kuutazama Utukufu Wake. Lakini ikiwa wanafunzi watapelewa masomo mengi zaidi ya ilivyo muhimu, itakuwa ni mkakati wa kuwafanya wasahau lengo lao la halisi la kuja Battle Creek. Sasa ni wakati ambao kazi kama hii muhimu inapaswa kufanywa. Muda mrefu wa miaka ya maandalizi sio hitaji chanya. Maandalizi ya wanafunzi yamesimamiwa kwa kanuni sawa na shughuli za ujenzi. Jengo limeongezwa juu ya jengo, sababu ni kujipatia urahisi zaidi katika kufanya mambo na ukamilifu. Mungu anaita, na ametoa wito kwa miaka kadhaa, kwa ajili ya matengenezo kwenye mistari hii. Anatamani kwamba kusiwepo na matumizi yasiyo ya lazima ya mali. Bwana hapendelei kuona muda na pesa nyingi sana zinazotumika kwa watu wachache wanaokuja Battle Creek kupata maandalizi bora kwa ajili ya kazi. Katika hali zote inapaswa kuzingatiwa kwa uangalifu sana njia bora ya kutumia pesa katika elimu ya wanafunzi. Wakati mali nyingi inatumika kuwaweka wachache kupata kozi zinazopitiliza katika masomo, kuna wengi ambao wana kiu ya ujuzi huo na wangeweza kuupata ndani ya miezi michache; mwaka mmoja au miwili ingezingatiwa kuwa baraka kubwa. Kama mali zote zitatumika katika kuweka wachache kwenye miaka kadhaa ya masomo, wengi wa vijana wa kike na kiume wanaostahili wasingesaihiwa hata kidogo. {FEsw 337.1}

Natumaini wasimamizi wa shule ya Battle Creek na kituo cha Sanitarium, yaani tiba mbadala, watazingatia jambo hili kwa sala, kwa akili, na bila upendeleo. Badala ya kuelimisha wachache kupita kiasi (kwa kupitiliza), panueni nyanja zenu za misaada. Azimieni kuwa mali mnazokusudia kutumia katika kuwaelimisha wafanyakazi kwa ajili ya kazi hazitatumika kwa mtu mmoja tu, kwa kumwezesha kupata zaidi ya anavyohitaji, huku wengine wakiachwa bila kitu chochote. Wape wanafunzi mahali pa kuanzia, lakini usihisi kuwa ni wajibu wako kuwabeba mwaka baada ya mwaka. Ni wajibu wao kutoka nje kwenye shamba na kufanya kazi, na ni nafasi yako kupanua misaada yako kwa wengine wanaohitaji msaada. {FEsw 338.1}

Kazi ya Kristo haikufanywa kwa njia ya kuwashangaza wanadamu na uwezo Wake wa hali ya juu. Alitoka kifuni mwa Mwenye hekima yote, na angeweza kuushtua ulimwengu na mshangao na kwa elimu kuu na tukufu aliyokuwa Nayo; lakini hakuwa tayari kuulezea ukuu Wake na hakuzungumzia kuhusu hayo. Haukuwa utume Wake kuwalemea watu kwa ukuu wa talanta Zake, bali kuenenda katika upole na unyenyekevu ili awafundishe wajinga njia za wokovu. Kujiweka sana katika kusoma, hata sayansi ya Kweli, huleta hamu isiyo ya kawaida, ambayo huongezeka kadri inavyolishwa. Hii inaunda hamu ya kutafuta zaidi maarifa kuliko ilivyo muhimu kufanya kazi ya Bwana. Kufuata elimu kwa ajili ya elimu tu peke yake, hugeuza akili kutoka kujielekeza kwa Mungu, hupunguza kasi katika njia ya utakatifu wa matendo, na huzuia nafsi kutoka kwenye kusafiri katika njia

inayoongoza katika maisha matakatifu na yenye furaha zaidi. Bwana Yesu alitoa tu kiwango cha maagizo ambacho kingeweza kutumika. Ndugu zangu, njia yenu ya kuwakilisha hitaji la kusoma miaka mingi, haimpendezi Mungu. {FEsw 338.2}

Bwana Yesu angetaka watu wachuuze talanta zao, na Yesu ameahidi kwamba atatoa neema juu ya neema. Tunapotoa kwa wengine, tutapokea kwa wingi zaidi. Na tunapofanya kazi hivyo, akili haitaziba na kwa ajili ya wingi wa mambo ambayo yamekuwa yakishonana kwa msongamano ndani yake bila nafasi ya kutoa kwa wengine kile kilichopokelewa. Mwanafunzi anakuwa na kuvimbiwa na kiungulia cha akili kubannana kichwani kwa mengi ambayo hawezi kuyatumia. Muda mwingi umepotea, na manufaa ya maendeleo endelevu ya wanafunzi yamezuiwa, na ufundishaji wa yale ambayo hayawezi kutumiwa na Roho wa Mungu. {FEsw 338.3}

Wale wanaokuja kwenye shule ya Battle Creek wanapaswa kusukumwa kwa haraka kabisa kwenye kozi ya masomo ambayo ingekuwa yenye thamani kwa maisha ya kila siku na vitendo katika ukuaji wa afya ya mwili na shughuli ya utakatifu wa Roho. Katika injili Yake, Mungu hasemi tu ili kufaidisha ukuaji wa uwezo wa kiakili wa mwanadamu, bali kuelekeza jinsi hisia za maadili zinavyoweza kuhuishwa. Hii inaonyeshwa kwenye habari ya Danieli na wale Waebrania watatu. Waliweka uchaji na upendo wa Mungu daima mbele yao, na matokeo yameandikwa kama ifuatavyo: "Basi kwa habari za hao vijana wanne, Mungu aliwapa maarifa na ujuzi katika elimu na hekima; Danieli naye alikuwa na ufahamu katika maono yote na ndoto." {FEsw 339.1}

Kristo alisema, "Heri walisikiao Neno la Mungu, na kulishika." Mkate wa uzima pekee yake ndio unaweza kuishibisha nafsi yenye njaa. Maji ya uzima pekee ndiyo yatakayokata kiu ya nafsi yenye kiu. Akili za wanafunzi mara nyingi zilisisimka kwa udadisi, lakini badala ya kukidhi hamu yao ya kujua mambo ambayo hayakuwa ya lazima kwa mwenendo mzuri wa kazi zao, alifungua njia mpya za mawazo katika akili zao. Aliwapa maagizo yaliyohitajika sana juu ya utauwa. {FEsw 339.2}

Matawi mengi ambayo wanafunzi wanashawishiwa kuchukua katika masomo yao, huwashikilia wasiende kazini kwa miaka kadhaa, jambo ambalo haliko katika mpangilio wa Mungu. Kristo alikuja kutafuta na kuokoa kile kilichopotea. Aliposema, "Nifuate," Yeye alichukua nafasi ya mwalimu. Nuru yote aliyowaletea wanadamu kutoka Mbinguni itatumika katika kuwafunulia watu shimo la uharibifu ambalo wametumbukizwa na dhambi zao, na kuwabainishia njia pekee wanayoweza kuipitia kwa matumaini ya kufika mahali pa usalama. Miale angavu ya Jua ya Haki inaangaza juu ya njia hii, na msafiri ingawa ni mpumbavu, hana haja ya kukosea humo njiani. Wale wanaokuja Battle Creek hawapaswi kuhimizwa kuchukua miaka kadhaa katika masomo. {FEsw 339.3}

Kutokuwa na kiasi katika kusoma ni aina ya ulevi, na wale wanaokoendekeza

katika hilo, ni kama mlevi, anayetangatanga kutoka katika njia salama, na kujikwaa na kuanguka katika giza. Bwana anahitaji kila mwanafunzi kukumbuka kwamba jicho lazima liwekwe moja kwa moja kwenye Utukufu wa Mungu tu. Hawapaswi kujichosha na kupoteza nguvu zao za kimwili na kiakili katika kutafuta kupata maarifa yote yanayowezekana ya sayansi; lakini kila mtu anatakiwa kuhifadhi upya na nguvu zote za uwezo wake wa kushiriki katika kazi ambayo Bwana amemweka kuifanya kusaidia Roho kupata njia ya haki. Wote wanapaswa kuhifadhi nguvu za maisha yao, nishati ya nafsi na matamanio yao, na kujiandaa kuacha masomo yao shuleni, na kuchukua masomo ya vitendo zaidi katika nyanja ya shughuli, ambapo malaika hushirikiana nao. Akili za Mbinguni zitafanya kazi kupitia kwa mawakala wa kibinadamu. Amri ya Mbinguni ni kufanya kazi, kutenda kazi, - kufanya kitu ambacho kitaakisi Utukufu kwa Mungu na kuwa faida kwa wanadamu wenzetu walio tayari kuangamia. {FEsw 340.1}

Kuna hatari kubwa ambayo wanafunzi shuleni watahindwaku jifunza somo muhimu sana ambalo Bwana wetu angetaka wafundishwe. Somo hili limetolewa kwetu katika maandiko yafuatayo: “Jitieni nira Yangu, mjifunze Kwangu; kwa maana Mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo: nanyi mtapata raha nafsi ni mwenu. Kwa maana nira Yangu ni laini, na mzigo Wangu ni mwepesi.” Wengine wameshindwa sio tu kujifunza kubeba nira ya Yesu, mpole na mnyenyekevu, bali wameshindwa kusimama dhidi ya majaribu ambayo yanawazunguka. Vijana wasio na uzoefu ambao wamesafiri umbali mrefu ili kupata faida ya elimu katika shule yetu, wamepoteza uelekeo wao kwa Yesu. Haya mambo hayapaswi kuwa hivyo. {FEsw 340.2}

Bwana hawachagui au kuwakubali watenda kazi kulingana na faida nyingi ambazo wamefurahia, au kulingana na elimu ya juu waliyoipata. Thamani ya wakala wa binadamu hupimwa kulingana na uwezo wa moyo kumjua na kumwelewa Mungu. “Basi wewe, mwanangu, uwe hodari katika neema iliyo katika Kristo Yesu. Na mambo uliyoyasikia kwangu mbele ya mashahidi wengi, hayo uwakabidhi watu waaminifu watakaofaa kuwafundisha wengine. Ushiriki taabu pamoja nami, kama askari mwema wa Kristo Yesu.” Mema ya juu kwa kadri iwezekanavyo hupatikana kwa kumjua Mungu. “Huu ndio uzima wa milele, ili wakujue Wewe, Mungu wa pekee wa Kweli, na Yesu Kristo, uliyemtuma.” {FEsw 341.1}

Ujuzi huu ni chemchemi ya siri ambayo nguvu zote hutiririka. Ni kwa kutumia nguvu ya imani tunawezeshwa kupokea na kutenda Neno la Mungu. Hakuna udhuru unaoweza kukubaliwa, hakuna ombi la kuhesabiwa haki lililopokelewa kwa kushindwa kujua na kuelewa mapenzi ya Bwana. Bwana atatia Nuru moyo ulio na uadilifu Kwake. Anaweza kusoma mawazo na makusudi ya moyo. Ni bure kusihi kwamba kama ingekuwa hivi na hivi, tungefanya hivi na vile. Hakuna ningejua kuhusu madai ya Mungu; Neno Lake ni ndiyo na amina. (1Kor 1:20). Hakuwezi kuwa na swali katika moyo wa imani kuhusu uwezo wa Mungu kutimiza ahadi Zake.

Imani iliyo safi hutenda kazi kwa upendo, na kuitakasa nafsi. {FEsw 341.2}

Kwa baba yule mwenye huzuni, aliyekuwa akitafuta upendo mwororo na huruma ya Kristo kutolewa kwa ajili ya mwana wake aliyeteseka, Yesu alisema hivi: “Ukiweza kuamini, yote yawezekana kwake aaminiye.” Mambo yote yanawezekana kwa Mungu, na kwa imani tunaweza kushikiria nguvu Zake. Lakini imani si kuona; imani si hisia; imani sio uhalisia. “Imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana.” Kukaa katika imani ni kuweka kando hisia na tamaa za kibinafsi, kutembea kwa unyenyekevu na Bwana, kuchukua ahadi zake, na kuzitumia katika hali na matukio yote, kwa kuamini kwamba Mungu atafanya mapenzi Yake na makusudi katika moyo wako na maisha yako kwa utakaso wa tabia yako; ni kutegemea kabisa, kutumaini, kuamini kabisa, juu ya uaminifu wa Mungu. Ikiwa hili litafuatwa, wengine wataona matunda maalum ya Roho yanayodhihirishwa katika maisha na tabia. {FEsw 341.2}

Elimu aliyopokea Musa, kama mjukuu wa Mfalme, ilikuwa ya kina sana. Hakuna kitu kilichopuuzwa ambacho kilihesabiwa kingeweza kumtengeneza ili awe mtu mwenye hekima, kama Wamisri walivyoifahamu hekima. Elimu hii ilikuwa msaada kwake katika mambo mengi; lakini sehemu ya thamani zaidi ya kufaa kwake kwa kazi ya maisha yake ni ile iliyopokelewa akiwa anatumika kama mchungaji wa kondoo. Alipokuwa akiongoza mifugo yake katika nyikani kwenye milima na katika malisho mabichi ya mabonde, Mungu wa asili alimfundisha hekima ya juu na kuu mno. Katika shule ya asili, na Kristo Mwenyewe akiwa mwalimu, alitafakari na kujifunza masomo ya kujidhili, upole, imani, na uaminifu, na namna ya unyenyekevu hai kwa maisha yasiyo na maonyesho au gharama kubwa, yote hayo yaliifunga nafsi yake karibu na Mungu. Katika upweke wa milimani alijifunza mafundisho yake yote ambayo ikulu ya Mfalme haikuweza kumpa (jumba la kifalme), - imani rahisi, isiyoyumba, na ya kumtumaini Bwana daima. {FEsw 342.1}

Musa alidhani kwamba ile elimu yake katika hekima ya Misri aliyokuwa nayo, ilimstahilisha kabisa kuwaongoza Israeli kutoka utumwani. Je, hakujifunza katika mambo yote muhimu ya jemadari wa kijeshi? Je, Hakuwa na faida kubwa zaidi za shule bora zaidi nchini? —Ndiyo; alihisi kwamba aliweza kuwakomboa. Kwanza alianza kazi yake kwa kujaribu ili kupata upendeleo wa watu wake mwenyewe kwa kurekebisha makosa yao. Yeye alimuua Mmisri ambaye alikuwa anamwonea mmoja wa ndugu zake. Katika hili aliidhihirisha Roho yake yeye aliyekuwa mwaaji tangu mwanzo, na kujidhihirisha kuwa hafai kumwakilisha Mungu wa rehema, upendo, na huruma. Alishindwa vibaya katika jaribio lake la kwanza. Kama wengine wengi, basi mara moja alipoteza imani yake kwa Mungu, na kuipa kisogo kazi yake aliyomuagiza; alikimbia ghadhabu ya Farao. Alihitimisha kwamba kwa sababu ya kosa lake, dhambi yake kubwa katika kumuua yule Mmisri mkatili, Mungu hangemruhusu kuwa na sehemu yoyote katika kazi ya kuwakomboa watu Wake kutoka katika ukatili wao wa utumwa. Lakini Bwana aliruhusu mambo haya ili

aweze kumfundisha upole, wema, na ustahimilivu, ambavyo ni muhimu kwa kila mtendakazi kwa Bwana kumiliki; maana hizi sifa ndizo zinazounda mtenda kazi aliyefanikiwa katika kazi ya Bwana. {FEsw 342.2}

Ujuzi wa sifa za tabia ya Kristo Yesu hauwezi kupatikana kwa njia ya elimu ya juu kabisa katika shule za kisayansi. Hekima hii inafunzwa kutoka kwa Mwalimu Mkuu peke yake. Masomo ya upole kama wa Kristo, unyenyekevu wa moyo, kicho kwa mambo matakatifu, hayafundishwi popote kwa ufanisi isipokuwa katika shule ya Kristo. Musa alikuwa amefunzwa kutarajia sifa, kubembelezwwa na kupongezwa kwa sababu ya uwezo wake wa juu; lakini sasa alipaswa kujifunza somo tofauti. Akiwa mchungaji wa kondoo, Musa alifundishwa kuchunga kondoo wenye shida/taabu, kuwajali wagonjwa, kutafuta kwa subira waliomangamanga, kuwavumilia watundu ambao hawapendi nidhamu au kutii, na kuwatimizia kwa upendo mahitaji ya wana-kondoo wachanga na mahitaji ya wazee na walio dhaifu. Kadri awamu hizi za tabia yake zilivyoendelezwa, akasogezwa karibu zaidi na Mchungaji wake Mkuu. Akaunganishwa na kuzama ndani ya Mtakatifu Mmoja wa Israeli. Akamwamini Mungu mkuu. Alifanya ushirika pamoja na Baba kwa maombi ya unyenyekevu. Alimtazama Yule Aliye Juu kwa ajili ya elimu katika mambo ya kiroho, na kwa ajili ya ujuzi wa wajibu wake kama mchungaji mwaminifu. Maisha yake yakaunganishwa na mbingu kwa ukaribu sana hata kwamba Mungu alizungumza naye uso kwa uso. {FEsw 343.1}

Akiwa amejitayarisha hivyo, alikuwa tayari kutii wito wa Mungu kwa kubadilisha fimbo yake ya uchungaji wake na kupewa fimbo ya mamlaka; kuliacha kundi la kondoo na kisha kubeba kazi ya kuongoza waabudu sanamu zaidi ya milioni moja, watu ambao walikuwa waasi. Lakini alipaswa kumtegemea Kiongozi asiyeonekana kwa macho. Kama vile ile fimbo ilivyokuwa tu chombo mkononi mwake, ndivyo yeye alivyokuwa chombo cha kilicho tayari kwa hiari yake, kufanyiwa kazi kwa mkono wa Yesu Kristo. Musa alichaguliwa kuwa mchungaji wa watu wa Mungu Mwenyewe, na ilikuwa ni kwa njia ya imani yake dhabiti na tumaini lake la kudumu kwa Bwana ndivyo baraka nyingi ziliwafikia wana wa Israeli. Bwana Yesu anatafuta ushirikiano wa watu kama hao ambao watakuwa mifereji isiyo na vizuizi ambayo kwayo utajiri wa Mbinguni unaweza kumimina upendo Wake juu ya watu. Anafanya kazi kupitia mwanadamu kwa ajili ya kuinua, na wokovu wa wateule Wake. {FEsw 343.2}

Musa aliitwa kufanya kazi kwa ushirikiano na Bwana, na ilikuwa usahili/urahisi wa tabia yake, pamoja na elimu ya vitendo inayosaidia maisha siku kwa siku, ambayo ilimfanya kuwa mwakilishi wa Bwana. Katika hali ya juu sana ya Utukufu wake wa kibinadamu Bwana alimruhusu Musa kufunua upumbavu wa hekima ya mwanadamu, udhaifu wa nguvu za kibinadamu, ili apate kuongozwa kuelewa kutojiweza kwake kabisa (nyanganyanga), na kukosa ufanisi kwake endapo asiposhikiliwa na Bwana Yesu. {FEsw 344.1}

Harara na haraka ya Musa katika kumuua Mmisri ilichochoewa na Roho ya kiburi. Imani hutembea katika nguvu na hekima ya Mungu, na si katika njia za wanadamu. Kwa imani rahisi/sahili Musa aliwezesha kusonga mbele wakati wa matatizo, na kushinda vikwazo ambavyo vilionekana haviwezi kushindika. Walipomtegemea Bwana, bila ya kutegemea nguvu zao wenyewe, Jemadari Mkuu wa majeshi alikuwa mwaminifu kwa Israeli. Aliwakomboa kutoka katika magumu mengi ambayo kwayo wasingeweza kuyaepuka, ikiwa wangeachwa peke yao. Mungu aliweza kudhihirisha nguvu Zake kuu kupitia Musa kwa sababu ya imani yake ya kudumu katika Ufalme wa Mungu na nia ya upendo kwa Mwokozi wao. Imani kupita imani hii aliyoielewa katika Mungu ndiyo iliyomfanya Musa kuwa vile alivyokuwa. Kulingana na yote Bwana aliyomwamuru, ndivyo alivyofanya. Mafunzo yote ya wenye hekima hayakuweza kumfanya kuwa mfereji ambao kwa huo Bwana angeweza kufanya kazi, ilikuwa mpaka pale alipopoteza kujiamini kwake, ndipo akagundua unyonge wake mwenyewe, na kuweka tumaini lake kwa Mungu; mpaka alipokuwa tayari kutii amri za Mungu iwe zilionekana kibinadamu kuwa ni sahihi au la. {FEsw 344.2}

Wale watu ambao wanakataa kusonga mbele hadi waone kila kitu kimekuwa sawa na wazi mbele yao, hawataweza kutimiza mengi; bali kila mtu anayeonyesha imani yake na kumtegemea Mungu kwa hiari yake akijisalimisha, akijitiisha kwake, na akistahimili ndihamu na adhabu iliyowekwa; atakuwa mtendakazi mwenye mafanikio katika shamba la Bwana la mizabibu. Katika jitihada zao za kustahili kuwa watenda kazi pamoja na Mungu, wanadamu mara kwa mara hujiweka katika nafasi ambazo zitawakosesha kabisa sifa za kufinyangwa na kutengenezwa jinsi atakavyo Bwana. Kwa hiyo wanakuwa wasioweza kusimama au kustahimili, kama alivyofanya Musa, ambaye alikuwa mfano wa Bwana. Kwa kutii nidhamu ya Mungu, Musa akawa chaneli/mfereji uliyotakaswa ambao kwa huo Bwana angeweza kufanya kazi. Hakusitasita kubadili njia yake kwa ajili ya njia ya Bwana, ingawa iliongoza katika njia za ngeni, kwa njia zisizojarihiwa. Hakuruhusu kuitumia elimu yake kwa kuonyesha jinsi amri za Mungu zisivyo na busara au sababu ya kuwepo kwake, na kutowezekana kwake kuzitii. Hapana; yeye aliweka mategemeo ya chini sana juu ya sifa zake za kukamilisha kwa ufanisi kazi kuu ambayo Bwana alikuwa amempa. Alipoanza utume wake kuwakomboa watu wa Mungu kutoka katika utumwa wao, ilionekana kwa ubinadamu wake, kuwa ilikuwa ni kazi isiyo na matumaini kabisa; lakini yeye alimwamini Yeye ambaye mambo yote yanawezekana Kwake. {FEsw 344.3}

Wengi katika siku zetu wamekuwa na fursa bora zaidi, wamefurahia kmapendeleo mapana zaidi, ya maarifa ya Mungu, kuliko ilivyokuwa kwa Musa; lakini imani yake inaonyesha aibu dhahiri ya kutokuamini kwao. Kwa amri ya Mungu, Musa alisonga mbele, ingawa hapakuwa na sakafu chini yake ya kuweka miguu yake ili kukanyaga. Zaidi ya watu milioni moja walimtegemea yeye, lakini akawaongoza mbele hatua kwa hatua, siku baada ya siku. Mungu aliruhusu hawa wapweke kusafiri nyikani ili wapate uzoefu katika kustahimili magumu, na ili

walipokuwa katika hatari, waweze kujua kwamba kulikuwa na unafuu na ukombozi ndani ya Mungu peke yake, na hivyo wapate kujifunza kumjua na kumtumaini Mungu, na kumtumikia kwa imani iliyo hai. Hayakuwa mafundisho ya shule za Misri yaliyomwezesha Musa kuwashinda adui zake wote, bali imani yenye kudumu daima, imani isiyoyumbayumba, imani isiyotikiswa katika hali ngumu zaidi. {FEsw 344.3}

Mungu alipomwamuru Musa kufanya jambo lolote, alilifanya bila kuacha kufikiria ni matokeo yapi yanaweza kuwa. Alitoa sifa kwa Mungu kwa hekima ya kujua alichomaanisha na uthabiti wa kusudi kumaanisha kile Alichosema; na kwa hiyo Musa akatenda kama yule anayemwona Yule Asiyoonekana kwa macho. Mungu hatafuti watu wenye elimu kamilifu. Kazi Yake si kusubiri wakati watumishi Wake wanapitia matayarisho ya kiwango cha ajabu, (chenye kusheheni au kurundika masomo mengi kichwani), kama vile shule zetu zinavyopanga kutoa; bali Bwana anataka watu wathamini fursa ya kuwa watenda kazi pamoja na Mungu, - watu ambao watamheshimu kwa kutoa utii kamili kwa maelekezo Yake bila kujali nadharia zilizoingizwa hapo awali. Hakuna kikomo cha manufaa ya wale wanaoweka ubinafsi kando, na kutoa nafasi ya utendaji kazi wa Roho Mtakatifu mioyoni mwao, na kuishi maisha ya utakatifu kabisa kwa ajili ya utumishi wa Mungu, wakistahimili nidhamu ambayo Bwana analazimika kuwapa bila ya wao kulalamika au kuzimia njiani. Ikiwa hawatazimia kwa kemeo/karipio la Bwana, na kuwa wenye mioyo migumu na wakaidi, Bwana atawafundisha vijana kwa wazee, saa kwa saa, siku kwa siku. Anatamani kudhihirisha wokovu Wake kwa wana wa wanadamu; na ikiwa wateule Wake wataondoa vikwazo, atayamimina maji ya wokovu katika mito mingi inayofurika, kupitia mifereji ya kibinadamu kibinadamu. {FEsw 346.1}

Wengi wanaotafuta ufanisi kwa ajili ya kazi ya Mungu iliyotukuka kwa kukamilisha elimu yao katika shule za wanadamu, watagunuda kuwa wameshindwa kujifunza masomo muhimu zaidi ambayo Bwana angewafundisha. Kwa kupuuza kujisalimisha kwenye mvuto wa Roho Mtakatifu, kwa kutoishi kwa utii kwa yote yaliyo maagizo ya Mungu, ufanisi wao wa kiroho umedhoofika; wamepoteza uwezo waliokuwa nao wa kufanya kazi yenye mafanikio kwa ajili ya Bwana. Kwa kujiepusha na shule ya Kristo, wameisahau sauti ya Bwana, wala hawezi kuongoza mwenendo wao. Watu wanaweza kupata ujuzi wote unaotolewa na mwalimu wa kibinadamu kwa kadri iwezekanavyo; lakini bado kuna hekima kubwa zaidi wanayotakiwa kuwa nayo na Mungu. Kama Musa, wao nao lazima wajifunze upole, unyenyekevu wa moyo, na kutojiamini. Mwokozi wetu mwenyewe, akibeba mzigo wa ubinadamu, alikubali kwamba hangeweza kufanya kitu Mwenyewe. Ni lazima pia tujifunze kwamba hakuna nguvu katika ubinadamu peke yake. Mwanadamu anakuwa na ufanisi tu kwa kuwa mshiriki wa asili ya Kiungu. {FEsw 346.2}

Kuanzia ufunguzi wa kwanza wa kitabu, mtafutaji wa elimu anapaswa

kumtambua Mungu kuwa Ndiye Mpaji hekima ya Kweli. Anapaswa kutafuta ushauri Wake katika kila hatua njiani. Hakuna mpangilio unaopaswa kufanywa ambao Mungu hawezi kufanywa kuwa sehemu yake, hakuna muungano ambao Yeye hajauidhinisha. Mwanzilishi wa hekima anapaswa kutambuliwa kama Kiongozi kuanzia mwanzo hadi wa mwisho. Kwa namna hii ujuzi unaopatikana kutoka katika vitabu utafungwa na imani Hai katika Mungu asiye na kikomo. Mwanafunzi hatakiwi kujiruhusu kuwa chini ya kozi yoyote ya maalum ya masomo yanayochukua muda mrefu au vipindi vya wakati virefu, lakini anapaswa kuongozwa katika mambo kama hayo na Roho wa Mungu. {FEsw 347.1}

Kozi ya kusoma huko Ann Arbor inaweza kuzingatiwa kuwa muhimu kwa baadhi; lakini mivuto miovu huwa inatenda kazi inayoweza kuathiri akili, ili kadiri wanavyosonga mbele katika masomo yao, ndivyo wanavyopungua kuona ni muhimu kutafuta ujuzi wa mapenzi na njia za Mungu. Hakuna anayepaswa kuruhusiwa kusoma kozi ya masomo ambayo inaweza kwa vyovyote vile kudhoofisha imani yao katika Ukweli na katika uweza wa Bwana, au kupunguza heshima yao kwa maisha ya utauwa. Napenda kuwaonya wanafunzi kutosonga mbele hata hatua moja katika jambo hili, —hata kwa ushauri wa wakufunzi wao au watu walio katika vyeo vya mamlaka, —isipokuwa kwanza wamemtafuta Mungu wao binafsi, huku mioyo yao ikiwa imewekwa wazi kwa mvuto wa Roho Mtakatifu, na kupata ushauri Wake kuhusu kozi inayokusudiwa ya masomo. Hebu kila tamaa ya ubinafsi inayochomoza iwekwe kando; lipeleke kila pendekezo kutoka kwa binadamu, kwa Mungu, ukitumainia uongozi wa Roho Mtakatifu; kila tamaa mbaya ifutiliwe mbali, Bwana asije akasema: “Nimewaona wapumbavu wakishusha mizizi; lakini mara niliyalaani maskani yao.” Kila mmoja anapaswa kujongea mbele ili aweze kusema: “Wewe, Ee Bwana, wanijua, umeniona, na kuujaribu moyo wangu.” “Wewe Mungu unaniona.” Bwana hupima kila nia. Yeye huyatambua mawazo na nia na makusudi ya moyo. Bila Mungu hatuna tumaini; kwa hivyo tuweke imani yetu juu Yake. “Wewe ni tumaini langu, Ee Bwana Mungu, Wewe Ndiwe tumaini langu tangu ujana wangu.” {FEsw 347.2}

Kila meli inayosafiri kwenye bahari ya uzima huhitaji kuwa na rubani wa Kiungu; lakini dhoruba zinapotokea, tufani zinapotisha, watu wengi humsukuma rubani wao baharini, na kuweka meli yao mkononi mwa mwanadamu mwenye ukomo, au kujaribu kuiongoza wenyewe. Kisha maafa na uharibifu kwa ujumla hufuata, na rubani analaumiwa kwa kuwaendesha katika yale maji hatari. Msitoe maisha yenu chini ya uangalizi wa watu, bali semeni Bwana Ndiye msaada wangu; Nitatafuta shauri Kwake; nitakuwa mtendaji wa mapenzi Yake. Faida zote ambazo unaweza kuwa nazo haziwezi kuwa baraka kwako, wala elimu ya daraja la juu zaidi haiwezi kukustahilisha wewe kuwa mfereji wa Nuru, isipokuwa kama una ushirikiano wa Roho wa Mungu. Haiwezekani kwetu kupokea sifa kutoka kwa mwanadamu, bila kuangaziwa na Mungu, kama ilivyokuwa kwa miungu ya Misri ilivyoathaminiwa kuwaokoa wale walioitumainia. Wanafunzi hawapaswi kusema kwamba kila

pendekezo kwao la kuongeza muda wa masomo hulingana na mpango wa Mungu. Hebu kila pendekezo kama hilo lichukuliwe Bwana kwa maombi, na utafute kwa bidii mwongozo Wake sio tu mara moja, lakini tena na tena. Msihi, mpaka uthibitike ikiwa shauri ni la Mungu au la mwanadamu. Usijichie, au usijiamini kwa mwanadamu. Tenda chini ya Mwongozo wa Bwana. {FEsw 348.1}

Umechaguliwa na Kristo. Umekombolewa na damu ya thamani ya Mwanakondoo. Omba mbele za Mungu ufanisi wa damu hiyo. Mwambie: "Mimi ni Wako kwa kuumbwa; Mimi ni Wako kwa ukombozi. Ninaheshimu mamlaka ya kibinadamu, na ushauri wa ndugu zangu; lakini siwezi kutegemea kabisa haya. Nataka Wewe, Ee Mungu, nifundishe. Nimeweka agano na Wewe kupokea Mwenyezi kiwango cha tabia Yako, na kukufanya Wewe kuwa mshauri wangu na kiongozi wangu, kukuweka Wewe kuwa Mwanatimu wangu katika kila mpango wa maisha yangu; kwa hiyo nifundishe." Hebu Utukufu wa Bwana uwe tafakari yako ya kwanza. Zuia kila tamaa ya kidunia iliyo tofauti, kila matamania ya ukuu katika kupata nafasi ya kwanza. Himiza moyo usafi na utakatifu, ili mpate kuwakilisha kanuni za Kweli za Mungu injili. Hebu kila tendo la maisha yako litakaswe na jitihada takatifu kufanya mapenzi ya Bwana, ili ushawishi wako usiwaongoze wengine katika njia zilizokatazwa. Mungu anapokuwa kiongozi, haki Yake itaenda mbele yako, na Utukufu wa Bwana utakuwa thawabu yako. {FEsw 348.2}

Bwana anasema, Kesheni, mkaomba, msije mkaingia majaribuni. Ushauri wa ndugu zako mwenyewe unaweza kukufanya ukengeuka kutoka katika njia ambayo Bwana amekuwekea ili uende; kwa maana mawazo ya watu si mara zote chini ya udhibiti wa Mtakatifu Roho. "Angalia" masomo yako yasije yakajilimbikiza kwa viwango hivyo, na kuwa ya kuvutia sana kwako, kwamba akili yako italemewa, na matamania y a utauwa kupondwa na kuminywa nje ya nafsi yako. Kwa wanafunzi wengi, nia na lengo ambalo liliwafanya waingie shuleni limepotea hatua kwa hatua, na tamaa mbaya ya kupata elimu ya juu imewaongoza kuutoa mhanga Ukweli. Nia yao kubwa ya kupata mahali pa juu miongoni mwa watu imewafanya kuacha mapenzi ya Baba yao wa Mbinguni nje ya hesabu zao; Lakini maarifa ya Kweli huongoza kwenye maisha ya utakatifu kupitia utakaso wa Ukweli. {FEsw 349.1}

Mara nyingi, kadri masomo yanavyojilimbikiza, hekima kutoka juu hupewa nafasi ya pili, na kadiri mwanafunzi anavyoendelea zaidi, ndivyo ujasiri wa imani yake kwa Mungu unavyozidi kupungua; anazingatia kujifunza huko kwingi ndio kiini cha mafanikio maishani; lakini ikiwa wote wangezingatia ipasavyo kauli ya Kristo, wafanya mipango tofauti : "Bila Mimi ninyi hamwezi kufanya neno lo lote." Bila kanuni muhimu za dini ya Kweli, bila ujuzi wa jinsi ya kumtumikia na kumtukuza Mkombozi, elimu ina madhara zaidi kuliko manufaa. Wakati elimu katika mistari ya kibinadamu inasukumwa mbali kiasi kwamba upendo wa Mungu unafifia moyoni, maombi nayo yanapuuzwa, na kuna kushindwa kusitawisha sifa za kiroho, hakika hiyo ni balaa kabisa (janga). Ingekuwa bora zaidi kuacha kutafuta elimu, na

kuirejesha nafsi yako kutokana na hali yake inayodhoofika, kuliko kupata elimu bora zaidi, na kupoteza mtazamo wa faida za milele. Kuna wengi ambao wanarundika masomo mengi kwa kipindi cha muda mchache. Wanashughulisha nguvu zao za akili kupita kiasii; na kama matokeo yake wanaona mambo mengi katika mwanga uliopotoka. Hawatosheki katika kufuata mwendo uliowekwa wa masomo, lakini wanahisi dhuluma inafanywa kwao wanapoonyesha tamaa zao za ubinafsi, hawapendi wanapokatazwa kuchukua masomo yale yote wanayotaka kuyafanya. Hawa wamepoteza usawa kwenye akili zao. Hawazingatii ukweli huo kwamba wangepata sifa bora zaidi kwa kazi ya Mwalimu/**Bwana** ikiwa wangepuata njia ambayo haitaleti madhara kwao, kwenye nguvu za kimwili, kiakili na kiadili; lakini katika kulemea akili, wanajiletea udhaifu wa kimwili wa maisha yote ambao hulemaza nguvu zao, na hili haliwastahilishi kwa manufaa ya siku zijazo. {FEsw 349.2}

Kwa vyovyote vile nisingeshauri kizuizi cha elimu ambayo Mungu hajaweka kikomo. Elimu yetu haifikii mwisho na faida ambazo ulimwengu huu unaweza kutoa. Wale wote waliochaguliwa wa Mungu, watakuwa wanafunzi milele zote. Lakini nisingeshauri kuweka mipaka/kizuizi katika kufuata zile njia za elimu zinazohatarisha Roho na **kwenda kinyume na madhumuni ya matumizi ya wakati na pesa**. Elimu ni kazi kubwa ya maisha; lakini ili kupata elimu ya Kweli, ni muhimu kuwa na ile hekima itokayo kwa Mungu peke yake. Bwana Mungu anapaswa kuwakilishwa katika kila awamu ya elimu; lakini ni kosa kutumia muda wa miaka kadhaa, kusoma mstari mmoja tu wa maarifa yaani elimu ya kitabu tu. Baada ya mwanafunzi kutoa kipindi cha muda kwa ajili ya kusoma, hebu mtu asimshauri wanafunzi kuingia tena kwenye mstari wa masomo, lakini, badala yake, kuwashauri kuingia kwenye kazi ambayo wamekuwa wakisomea. Hebu washauriwe kutekeleza kwa vitendo nadharia walizozipata. Danieli alifuata njia hii huko Babeli. Aliweka katika matumizi ya vitendo yale aliyojifunza chini ya waalimu. Hebu wanafunzi watafute Mbinguni njia yenye mwelekeo wa Mbinguni zaidi ya wanavyofanya hadi sasa, na wasiende katika kuchukua masomo zaidi, hata kama wanashauriwa na walimu wao, isipokuwa kwa unyenyekevu zaidi wameitafuta hekima kutoka kwa Mungu, na wamepokea Mwongozo na ushauri Wake. {FEsw 350.1}

Wanafunzi wameidhinishwa kwenda shule kwa urefu fulani wa muda ili kupata maarifa ya kisayansi; lakini kwa kufanya hivi wanapaswa kuzingatia mahitaji yao ya kimwili, na kutafuta elimu yao kwa namna ya kutojeruhi hata kidogo hekalu la mwili. Hebu wote wawe na uhakika wa kutojiendekeza katika mazoea yoyote ya dhambi, wasijibeebe na masomo mengi, wasizamishwe kwa kujitoa mhanga kwa masomo yao, hivi kwamba ile Kweli itawekwa chini na masomo yawekwe juu, na kisha ujuzi wa Mungu kufukuzwa kutoka kwenye nafsi, kwa ajili ya mavumbuzi ya mwanadamu. Wacha kila nukata ambayo umeitoa kwa ajili ya kusoma, iwe nafasi ambayo nafsi inatambua wajibu wake uliopewa na Mungu. Hapo hakutakuwa na haja basi ya kuwafundisha wanafunzi kuwa wakweli na waadilifu, na kuhifadhi

uadilifu wa nafsi zao. Watavuta pumzi ya anga la Mbinguni, na kila shughuli itaongozwa na Roho Mtakatifu, na uadilifu, kutenda mema na haki vitadhihirika.

{FEsw 351.1}

Lakini ikiwa mwili umepuuzwa, ikiwa masaa yasiyofaa yanatumiwa katika masomo, ikiwa akili imejaa shughuli nyingi na kuchoshwa, ikiwa nguvu za mwili zimeachwa bila kushughulishwa (hazijaajiriwa) na kuwa dhaifu, basi mashine ya mwili wa binadamu inakanyagwa chini, na mambo ambayo ni muhimu kwa ustawi wetu wa siku zijazo na amani ya milele hupuuza. Ujuzi wa kitabu unafanywa kuwa ndiyo kipaumbele cha umuhimu, na Mungu hapewi heshima. Mwanafunzi husahau maneno yaliyovuviwa, wala hafuati maagizo ya Bwana anaposema: “Basi, ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma zake Mungu, mpate miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu ndiyo huduma yako ya kuridhisha. Wala msiifuatishe namna ya dunia hii: bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika ni nini mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu.” akili za wengi zinahitaji kufanywa upya, kubadilishwa, na kufinyangwa Wengi wanajiharibu kimwili, kiakili, na kimaadili, kwa kujitolea kusoma kupita kiasi. Wanajidanganya wenyewe na kujipunja ule muda wa sasa na umilele kwa kujizoeza na tabia za kutokuwa na kiasi katika kutafuta kupata elimu. Wanapoteza hamu yao ya kujifunza, katika shule ya Kristo, masomo ya upole na unyenyekevu wa moyo. Kila wakati ambao unaopita, umejaa matokeo ya milele. Uadilifu utakuwa matokeo ya uhakika ya kufuata ile njia ya haki. {FEsw 351.2}

Je, ni muhimu kweli, kwamba katika kutatua tatizo la elimu mtu lazima amwibie Mungu, na kukataa kumpa Mungu huduma ya hiari ya nguvu za Roho, nafsi, na mwili? Mungu anawaita ninyi kuwa watendaji wa Neno Lake, ili mpate kuwa kuelimishwa kikamilifu katika kanuni ambazo zitakustahilisha kufaa kuwa Mbinguni. Hakuna njia ya elimu inayopaswa kufuatwa ambayo italisonga au kulibana Neno la Mungu. Hebu Neno la Mungu liwe Mshauri wako. Madhumuni ya elimu yanapaswa kuchukua Nuru ili kwamba uweze kutoa Nuru kwa kuiacha iangaze kwa wengine kupitia matendo mema. Elimu ya juu kuliko zote ni elimu ya Mungu. “BWANA asema hivi, Mwenye hekima asijisifu kwa sababu ya hekima yake; wala mwenye nguvu asijisifu kwa sababu ya uwezo wake, wala tajiri asijisifu kwa sababu ya uwezo wake ajisifu kwa ajili ya utajiri wake, bali yeye ajisifuye na ajisifu katika hili, ya kwamba yeye ananifahamu na kunijua, ya kuwa Mimi Ndimi Bwana nifanyaye mazoezi wema, na hukumu, na haki, katika nchi; mambo haya napendezwa nayo, asema Bwana.” Soma Wakorintho wa kwanza na ya pili (1Wakorintho) kwa umakini na kupendezwa sana, na usali ili Mungu akupe ufahamu wa kuziweka tenda kweli zilizofunuliwa hapo katika matendo. “Maana, ndugu, mwaona mwito wenu. ya kwamba si wengi wenye hekima katika mwili, si wengi wenye nguvu, si wengi wenye vyeo wameitwa, lakini Mungu aliyachagua yale yaliyo upumbavu wa ulimwengu ili kuwaaibisha wenye hekima; na Mungu alivichagua vilivyo dhaifu vya ulimwengu ili kuwaaibisha wenye nguvu; na vitu vya msingi ya dunia, na vitu

vinavyodharauliwa, Mungu alivichagua, naam, na vitu ambavyo havipo, ili kubatilisha vitu vilivyoko: hivyo hakuna mwenye mwili anayepaswa kujivunia uwepo wake. Bali kwake ninyi mmekuwa katika Kristo Yesu, ambaye amefanywa kwetu hekima na haki itokayo kwa Mungu; na utakaso, na ukombozi; ili kama ilivyoandikwa, Ajisifuye na ajisifu katika Bwana.” “Bwana ametukuka; maana Yeye hukaa juu; ameijaza Sayuni hukumu na haki. Na hekima na ujuzi ndio uthabiti wa nyakati zako, na nguvu za wokovu; kumcha Bwana ni hazina Kwake.” {FEsw 352.1}

Muda ni mfupi, na kuna wafanyakazi wachache tu katika shamba la mizabibu la Mungu. Watu kadhaa wametumwa kutoka sehemu hii ya dunia (Australia) ili kufundishwa huko Battle Creek, ili wapate kuwa watenda kazi pamoja na Mungu. Ilitarajiwa kwamba Roho Mtakatifu angefanya kazi pamoja nao kwa wokovu wa wale walio katika uvuli wa mauti. Wanafunzi hawa wameungwa mkono na dhabihu za wanaume na wanawake ambao, kwa ufahamu wangu nilio nao, wametoa pesa zao karo na gharama za kuishi (chumba na chakula). Ulimwengu unapaswa kuonywa; lakini mmeona ni muhimu kutumia wakati na pesa kwenye kufanya maandalizi makubwa yasiyo ya lazima kwa kazi ambayo hawa wanafunzi wanaweza kuitwa kuifanya. Mungu Yule Yule, anaishi leo ambaye Isaya alimwona katika maono yake, na anaweza kuwapa Nuru wale ambao wanafanya sehemu katika kazi ya kuwastahilisha wanaume kwa ajili ya kazi adhimu, na takatifu. Naye anasema: “Mimi, BWANA, napenda hukumu, nachukia wizi badala ya kuteketezwa sadaka; Nami nitaiongoza kazi yao katika Kweli, Nami nitafanya agano la milele pamoja nao.” {FEsw 353.1}

Wale ambao wanaongoza katika kazi ya elimu wanaweka kiasi kikubwa mno cha masomo mbele ya wale waliokuja kwenye Battle Creek kufanywa wafae kwa kazi ya Mwalimu. Wamedhani jambo hilo lilikuwa ni lazima kwao, yaani kuingia kina cha ndani zaidi katika mistari ya elimu; na huku wakiendelea na kozi anuwai (mbalimbali) za masomo, mwaka hata mwaka muda wa thamani unapita, na fursa za dhahabu zinapepea juu bila kurudi. Kuna msembo wa “kesho, tutafanya kesho” katika kuwaweka hawa wanafunzi kazinii; na wanafunzi wanapoteza mzigo moyoni kwa ajili ya nafsi zao, na wanaendelea kutegemea zaidi na zaidi elimu inayotokana na maarifa ya vitabu, badala ya ufanisi wa Roho Mtakatifu, na juu ya lile ambalo Bwana ameahidi kuwafanyia. {FEsw 354.2}

Mzigo huu umekuwa juu yangu kwa miaka. Njia inafuatwa Battle Creek ambayo Bwana haikubali. Mwisho wa mambo yote uko karibu. Siku ya dhiki, ya uchungu, ya tauni, ya malipizo, hukumu kwa ajili ya dhambi, inakuja juu ya ulimwengu kama mwizi anyemeleavyo usiku. Wakati umekaribia ambapo uharibifu wa ghafula utakuja ulimwenguni, nao hawataepuka. Nina neno la onyo kwako wewe. Unatazama vitu kwa mwanga hafifu sana, na umo zaidi katika mtazamo wa kibinadamu tu. Sehemu ndogo sana ya shamba kuu la Mungu la mizabibu la maadili bado halijafanyiwa kazi. Wachache tu, kwa kulinganisha, wamepokea

ujumbe wa mwisho wa rehema ambao unapaswa kutolewa kwa ulimwengu. Wanafunzi wanaongozwa kudhani kwamba ufanisi wao unategemea elimu na mafunzo yao; lakini mafanikio ya kazi hayategemei kiasi cha maarifa ambayo watu wanayo kwenye masomo ya sayansi. Wazo la kuwekwa mbele ya wanafunzi ni kwamba muda ni mfupi, na kwamba lazima wafanye maandalizi ya haraka kwa ajili ya kufanya kazi ambayo ni muhimu kwa wakati huu. Kila mtu, ndani na kupitia neema aliyopewa na Mungu, anapaswa kuifanya kazi, si kwa kutegemea unyofu wake au uwezo wa kibinadamu; kwa maana Mungu anaweza kuondoa uwezo wa mwanadamu ndani muda mfupi. Hebu kila mmoja katika nguvu za Mwokozi aliye hai, ambaye leo ni Wakili wetu katika mahakama za Mbinguni, ajitahidi kufanya mapenzi ya Mungu. {FEsw 354.1}

Nimeamriwa kukuambia kuwa haujui dhiki na mgogoro utakuja muda gani. Unanyemelea polepole kama mwizi. Jua huangaza Mbinguni, na kuendelea na mzunguko wake kama kawaida, na mbingu bado hutangaza Utukufu wa Mungu; na bado watu wanaendelea bado kufuata kawaida yao katika mwenendo wa kula na kunywa, kupanda na kujenga, kuoja na kuolewea; wafanyabiashara bado wanajishughulisha na kununua na kuuza; machapisho bado yanatolewa moja bada ya jingine: watu wanashindana dhidi ya wengine, wakitaka kupata nafasi ya juu zaidi; wapenda raha bado wanahudhuria kumbi za sinema, drama, mbio za farasi, kamari za kuzimu, na misisimko ya hali ya juu inatawala; ila mlango wa rehema unakimbilia kufungwa haraka, na kila kesi iko karibu kuamuliwa milele. Ni wachache tu wanaoamini kwa moyo na Roho kwamba tuna mbingu ya kujishindia/kushinda na kuzimu ya kuepukwa (kuipiga teke); lakini hawa wachache wanaonyesha imani yao kwa matendo yao. Ishara za kuja kwa Kristo zinatimia haraka. Shetani anaona kwamba ana muda mfupi tu wa kufanya kazi, na ameweka mawakala wake wa kishetani kazini kuchochea mambo ya dunia, ili watu wapate kudanganywa, na kulaghaiwa, na kushughulishwa na kurubuniwa akili na umakini wao (kuchukuliwa msukule Mawazo) mpaka siku ya rehema itakapofika mwisho, na mlango kufungwa milele. {FEsw 354.2}

Falme za ulimwengu huu bado hazijawa falme ya Bwana wetu na Kristo Wetu. Msijidanganye; kuweni macho kabisa, amkeni, nendeni upesi, kwa maana usiku waja, ambao mtu hawezi kufanya kazi. Usiwatie moyo wanafunzi wanaokuja kwako wakiwa na mizigo mizito ya kazi ya kuokoa wanadamu wenzao, kuingia kwenye kozi baada ya kozi ya masomo tofauti. Usiongeze muda wa kupata elimu kuwa miaka mingi. Kwa kozi hiyo wao wanadhani kuwa kuna wakati wa kutosha, na mpango huu huu unathibitisha mtego kwa nafsi zao. Wengi wametayarishwa kwa ubora, wana hekima ya kiroho na maarifa ya Mungu, na wanajua zaidi matakwa Yake, wanapoingia kuanza masomo kuliko wanapohitimu. Wanaongozwa na tamaa ya kuwa watu wasomi, na wanahimizwa kuongeza masomo yao mpaka wawe wanadanganyika kwa kuwa na matamanio yasiyo na uhalisia {infatuated}. Wanavifanya vitabu vyao kuwa sanamu, na wako tayari kutoa dhabihu afya na Roho

ili kupata elimu. Wanapunguza muda wanaopaswa kutenga kwa ajili ya maombi, na kushindwa kuboresha fursa wanazopata katika kutenda mema, na wanaacha kuwasilisha Nuru na maarifa. Hao wanashindwa kutumia maarifa ambayo tayari wameyapata, na hawasongi mbele katika sayansi ya kuleta Roho kwa Bwana. Kazi ya utume inawapendeza kwa udogo, na udogo zaidi, wakati shauku ya kufaulu katika maarifa ya vitabuni huongezeka isivyo kawaida. Katika kuendeleza masomo yao, wanajitenga na Mungu wa hekima. Wengine wanawapongeza kwa maendeleo yao ya usomi, na kuwahimiza kuchukua shahada baada ya shahada, japo sifa zao katika kufanya kazi ya Mungu kwa mfano wa mafundisho ya Kristo ni pungufu kuliko ilivyokuwa kabla hawajaingia shuleni Battle Creek. {FEsw 355.1}

Swali liliulizwa kwa wale waliokusanyika: “Je, mnaamini Ukweli? Je, Unaamini ujumbe wa malaika wa tatu? Ikiwa unaamini, basi tenda kile unachokiamini, wala msiwatie moyo watu kuendelea kukaa Battle Creek wakisoma wakati wanapaswa kuwa mbali na mahali hapo, wakifanya utume na shughuli ya Mwalimu wao.” Bwana hajatukuzwa katika uchelewesho huu. Watu huenda Battle Creek, na kupokea mawazo makubwa zaidi ya uwezo wao, kuliko wanavyopaswa. Wanahimizwa kuchukua kozi ndefu, inayochukua muda mrefu; lakini njia ya Mungu haimo ndani yake. Mbingu haijaidhinisha hili. Muda wa majaribio wa thamani hautaruhusu muda mrefu au miaka mingi katika kuhenyeka na masomo namna hii. Mungu anaita: sikia sauti Yake anaposema, “Nenda kufanya kazi leo katika shamba Langu la mizabibu.” Sasa, sasa hivi, ni wakati wa kufanya kazi. Je, unaamini kwamba Bwana anakuja, na kwamba janga kuu la mwisho liko tayari kupasuka juu ya dunia? {FEsw 356.1}

Hivi karibuni Mungu atashughulika kwa kubadilika. Ulimwengu katika upotovu wake unatembelwa na vifo, majeraha na ugonjwa, - na mafuriko, dhoruba, moto, matetemeko ya ardhi, njaa, vita na umwagaji damu. Mungu si mwepesi wa hasira, tena ana uweza mwingi; wala hatamhesabia mtu mwovu kuwa hana hatia kamwe. “Bwana ana njia Yake katika kisulisuli na tufani, na mawingu ni mavumbi ya miguu yake..” Laiti watu wangeweza kuelewa subira na uvumilivu wa Mungu! Yeye anazizuia Sifa zake Mwenyewe. Nguvu zake kuu ziko chini ya udhibiti wa Uweza Wake wote. Laiti wanadamu wangeelewa kwamba Mungu anakataa kuchoshwa na upotovu wa ulimwengu, na bado anashikilia tumaini la msamaha hata kwa wale wasiostahili! Lakini uvumilivu Wake hautaendelea daima. Ni nani yuko tayari kwa mabadiliko ya ghafla ambayo yatatokea katika kushughulika kwa Mungu na wanadamu wenye dhambi? Nani atakuwa tayari kutoroka au kuepuka adhabu ambayo itawaangukia wakosaji kwa hakika? {FEsw 356.2}

Hatuna milenia ya muda tu ya kufanya kazi ya kuuonya ulimwengu. Kuna haja ya mabadiliko ya nafsi. Akili bora na yenye ufanisi zaidi inayoweza kupatikana, hupatikana ndani shule ya Kristo. Elewa kwamba sisemi chochote katika maneno haya kupunguza thamani elimu, lakini kuwaonya wale walio katika hatari ya kubeba

yaliyo halali kwa kupitiliza kuliko haramu, na kuifanya elimu nyingi sana ya binadamu ijae maishani mwao, badala ya kusesitiza juu ya maendeleo ya uzoefu wa thamani, wa Kikristo; kwani bila huo, elimu ya mwanafunzi haitakuwa na faida yoyote. {FEsw 357.1}

Ikiwa unaona kwamba wanafunzi wako katika hatari ya kuzama kwenye masomo yao kiasi cha kupuuza kusoma Kitabu hicho ambacho huwapa habari kuhusu jinsi ya kupata ustawi wa siku zijazo wa nafsi zao, basi usiwasilishe jaribu la kujiingiza ndani zaidi, la kuongeza muda wa nidhamu ya elimu. Kwa njia hiyo utafanya elimu ya mwanafunzi inayopelekea kuuthamini ulimwengu ipotee machoni au izame. Kristo Yesu Anapaswa kupendwa zaidi na zaidi; lakini baadhi wamekwenda Battle Creek katika kutafuta elimu, wakati, wangekaa mbali na hapo, wangekuwa wamejitayarisha vyema zaidi kwa kazi ya Mungu. Wangeipeleka mbele kwa usahili kwa namna Kristo alivyofanya kazi. Wangetegemea Mungu zaidi na zaidi na juu ya uweza wa Roho Mtakatifu, na kidogo sana juu ya elimu yao. Kusoma muda mrefu huumiza kwa ustawi wa kimwili, kiakili na kimaadili. {FEsw 357.2}

Soma Agano la Kale na Agano Jipya kwa moyo wa toba. Soma kwa maombi na kwa uaminifu, ukisihi Roho Mtakatifu akupe ufahamu. Danieli alichunguza sehemu ya Agano la Kale aliyokuwa nayo ndani ya uwezo wake, naye akalifanya Neno la Mungu kuwa mwalimu Wake wa juu zaidi. Wakati huo huo aliboresha fursa ambayo alipewa kujipatia akili katika mistari yote ya kujifunza. Waandamani wake walifanya vivyo hivyo, nasi twasoma hivi: Katika kila jambo la hekima na ufahamu kuhusu kile Mfalme alichowauliza, aliwaona bora mara kumi zaidi kuliko waganga na wanajimu wote katika ufalme wake wote. “Na watoto hawa wanne [maana walikuwa vijana tu], Mungu akawapa maarifa na ujuzi katika elimu na hekima yote: na Danieli alikuwa na ufahamu katika maono yote na ndoto.” {FEsw 357.3}

Wanafunzi wanaoinua sayansi juu ya Mungu wa sayansi, watafanywa kuwa wajinga wakati wanajiona wenyewe kuwa ni wenye busara sana. Ikiwa huwezi kumudu kupata muda wa kuomba, huwezi kutoa muda kwa ajili ya ushirika na Mungu, muda wa kujichunguza, na usithamini hekima ile inayokuja kutoka kwa Mungu peke yake, basi masomo yako yote yaakuwa na mapungufu, na shule na vyuo vyako vitakutwa vimepunguka (katika Mizani). “Kumcha Bwana ni mwanzo wa hekima.” Je, tunathamini imani gani? Je, sisi tuna imani itendayo kazi kwa upendo na kuitakasa Roho? Je, tuna imani kulingana na Nuru tuliyopokea? Shetani angefurahi ikiwa angeweza kufanya kazi mwenyewe kule Battle Creek ili kuzuia kazi ya Mungu kwa kushinikiza mavumbuzi ya mwanadamu katika ushauri na nasaha. Angefurahi kama umakini wa wafanyakazi utafyonzwa katika miaka ya maandalizi, hivyo kwamba elimu itakuwa kikwazo badala ya maendeleo/uendelevu. {FEsw 358.1}

Roho Mtakatifu wa Mungu amekuwa akifanya jitihada na vijana wengi, na

amekuwa akiwahimiza kujitolea kwa kazi kufanya kazi ya Mungu. Wanapojitoa kwenye konferensi au Jimbo, wanashauriwa kuchukua kozi ya kusoma huko Battle Creek kabla ya kuingia kazini. Hii yote ni jambo nzuri sana ikiwa mwanafunzi ana usawa kwa kanuni (balansi); lakini mambo hayatakuwa thabiti endapo kwamba mtendakazi atachelewa kwa muda mrefu katika maandalizi. Kazi ya unyofu zaidi inapaswa kutolewa ili kuwaendeleza wale ambao wanapaswa kuwa wamisionari. Kila jitihada inapaswa kuzungumza kwa faida yao ya kuwa kazini, ili wapelekwe upesi iwezekanavyo kwenye shamba la Bwana. Hawawezi kumudu kusubiri hadi elimu yao ichukuliwe kwamba sasa ndiyo imekamilika. Hili haliwezi kufikiwa kamwe; maana kutakuwapo kozi ya mara kwa mara ya elimu inayoendelezwa daima bila kukoma zama zote za milele. {FEsw 358.2}

Kuna kazi kubwa ya kufanywa, na shamba la mizabibu la Bwana linahitaji vibarua. Wamishonari wanapaswa kuingia shambani kabla ya kulazimishwa kusitisha kazi. Hivi sasa kuna milango wazi kila upande; hawawezi kusubiri kukamilisha miaka ya mafunzo; kwa kuwa miaka iliyo mbele yetu si mingi, na tunahitaji kufanya kazi wakati bado tuna muda. Sio bora kuwashauri wanaume na wanawake kuchukua kozi huko Ann Arbor. Wengi ambao wamekuwa huko hawajanufaika huko awali, na hawatafaidika katika siku zijazo. {FEsw 359.1}

Weka alama katika vipengele vya kazi ya Kristo. Alisonga mbele katika kazi kwa usahili mkubwa. Ingawa wafuasi Wake walikuwa wavuvi, hakuwashauri waende kwanza katika shule za marabi kabla ya kuingia kazini. Aliwaita wanafunzi wake walipokuwa wanavuta nyavu na kusema: Nifuateni, Nami nitawafanya wavuvi wa watu. Kisha Yeye akamwita Mathayo kutoka kwenye ofisi ya kutoza ushuru, akisema, "Nifuate." Walichotakiwa kufanya ni kumfuata Yesu, kutenda kama Yeye alivyoamuru, na hivyo kuingia katika shule Yake, Mahali ambapo Mungu ataweza kuwa Mwalimu wao. Kadiri muda unavyoendelea kuwapo, kutakuwa na haja shule. Daima kutakuwa na haja ya elimu; lakini lazima tuwe waangalifu ili elimu isifyonze kila maslahi ya kiroho. {FEsw 359.2}

Kuna hatari chanya katika kuwashauri wanafunzi kufuata mstari mmoja wa elimu baada ya mwingine, na kuwaacha wafikiri kwamba watafikia ukamilifu. Elimu itakayopatikana itakuwa tu na mapungufu kwa kila namna. Bwana asema hivi: "Nitaiharibu hekima yao wenye hekima, Na akili zao wenye akili nitazikataa. Yu wapi mwenye hekima? Yu wapi mwandishi? Yu wapi mlete hoja wa zamani hizi? Je! Mungu hakuifanya hekima ya dunia kuwa ni upumbavu? Kwa maana katika hekima ya Mungu, dunia isipopata kumjua Mungu kwa hekima Yake, Mungu alipenda kuwaokoa waaminio kwa upuzi wa lile Neno linalohubiriwa. Kwa sababu Wayahudi wanataka ishara, na Wayunani wanatafuta hekima; bali sisi tunamhubiri Kristo, aliYesulibiwa; kwa Wayahudi ni kikwazo, na kwa Wayunani ni upuzi; bali kwao waitwao, Wayahudi kwa Wayunani, ni Kristo, nguvu ya Mungu, na hekima ya Mungu. Kwa sababu upumbavu wa Mungu una hekima zaidi ya

wanadamu, na udhaifu wa Mungu una nguvu zaidi ya wanadamu. Maana, ndugu zangu, angalieni mwito wenu, ya kwamba si wengi wenye hekima ya mwilini, si wengi wenye nguvu, si wengi wenye cheo walioitwa; bali Mungu aliyachagua mambo mapumbavu ya dunia awaabishe wenye hekima; tena Mungu alivichagua vitu dhaifu vya dunia ili aviaabishe vyenye nguvu; tena Mungu alivichagua vitu vinyonge vya dunia na vilivyodharauliwa, naam, vitu ambavyo haviko, ili avibatilishe vile vilivyoko; mwenye mwili awaye yote asiye akajisifu mbele za Mungu. Bali kwa yeye ninyi mmepata kuwa katika Kristo Yesu, aliyefanywa kwetu hekima itokayo kwa Mungu, na haki, na utakatifu, na ukombozi; kusudi, kama ilivyoandikwa, Yeye aonaye fahari na aone fahari juu ya Bwana.” Huu ni mpango uliopangwa na Mungu; na kupitia vizazi vinavyofuatana, kupitia karne nyingi za ukafiri, mpango huu umesonga mbele, si kama jaribio, bali kama njia iliyoidhinishwa kueneza injili. Kupitia njia hii kutoka kwa mwanzo, usadikisho ulimjia mwanadamu, na ulimwengu ukaangazwa kuhusu injili ya Mungu. Elimu daraja la juu ambayo mwanadamu yeyote anaweza kufikia ni ile inayotolewa na shule ya Mwalimu wa Mbinguni (Mungu). Huu ni ujuzi ambao kwa uhalisia, tunapaswa kuutilia mkazo na umakini, kwani tunauhitaji sana tunapokaribia ule mwisho wa historia ya ulimwengu huu, na kila mmoja atafanya vyema kujipatia aina hii ya elimu. Bwana anataka watu wawe chini ya mafunzo Yake (wafundishwe Naye). Kuna kazi kubwa inayopaswa kufanywa katika kuzitoa akili za wanadamu kutoka katika giza kuu na kuziingiza kwenye Nuru ya ajabu ya Mungu. Kama vyombo vyake vya kibinadamu, kwa imani hai tunapaswa kutekeleza mipango Yake. Je, tuko katika hali ambayo imani yetu haitafanya kazi kwa Utukufu wa Mungu, au sisi tu vyombo vinavyokutana kwa ajili ya matumizi ya Bwana, tayari kwa kila iliyo kazi njema?

{FEsw 359.3}

Musa alifunzwa katika hekima yote ya Wamisri. Yeye alipata elimu katika majaliwa ya mipango wa Mungu; lakini sehemu kubwa ya elimu hiyo ilibidi isiondolewe kwenye ubongo, na kuhesabiwa kuwa ni upumbavu. Maoni yake yalipaswa kufutwa na uzoefu wa miaka arobaini katika kuchunga kondoo na wana-kondoo wachanga. Kwa wengi ambao wameunganishwa na kazi ya Bwana wanaweza kutengwa kama ilivyokuwa kwa Musa, na wanaweza kulazimishwa na hali kufuata wito fulani wa stadi ya unyenyekevu hadi mioyo yao ifikie unyororo, Watakuwa wachunga kondoo waaminifu zaidi kuliko wanavyofanya sasa katika kushughulika na urithi wa Mungu. Kisha hawatakuwa na mwelekeo wa kukuza uwezo wao wenyewe, au kutafuta kuonyesha kwamba hekima ya elimu ya juu ya mwanadamu inaweza kuchukua mahali pa ujuzi ulio na hekima wa Mungu. Kristo alipokuja ulimwenguni, ushuhuda ulikuwa kwamba “ulimwengu kwa hekima haukumjua Mungu,” lakini “, Mungu alipenda kuwaokoa waaminio kwa upuzi wa lile Neno linalohubiriwa kuwaokoa wale wanaomini.” {FEsw 360.1}

Jaribio la hekima ya ulimwengu lilikuwa lilifanywa kikamilifu wakati ujio wa kwanza wa Kristo, na hekima ya kibinadamu iliyojivuna ikathibitika kupungua.

Wanadamu hawakujua hekima ya Kweli inayotoka kwenye Chanzo cha mema yote. Hekima ya ulimwengu ilipimwa katika mizani, na kupatikana imepungua. Unawapa wanafunzi chini ya malezi yako mawazo ambayo si sahihi. Lau wangelipata kidogo sana katika hayo basi wangelifaa zaidi kwa ajili ya kutekeleza kazi yao. Hauzingatii vizuri maagizo na njia ya Bwana wetu Yesu Kristo, ila Yeye Ndiye Mwalimu pekee mkamilifu katika dunia yetu. “Basi sisi hatukuipokea Roho ya dunia, bali Roho atokaye kwa Mungu; ili tupate kujua mambo hayo tumepewa bure na Mungu. Mambo ambayo pia tunazungumza, sivyo kwa Maneno ambayo hekima ya mwanadamu hufundisha, lakini ambayo ni Mtakatifu Roho hufundisha; tukilinganisha mambo ya Rohoni na ya Rohoni. Lakini mwanadamu wa tabia ya asili hayapokei mambo ya Roho wa Mungu; kwa kuwa ni upumbavu kwake; wala hawezi kuyafahamu, kwa sababu yanatambulika kiroho. Bali mtu wa Rohoni huyaamua yote; lakini yeye mwenyewe hahukumiwi na mtu. Maana ni nani aliyeijua akili ya Bwana, ili apate kumfundisha? Lakini tunayo akili Kristo.” {FEsw 361.1}

Unahitaji kuwa unajifunza katika shule ya Kristo leo. Mungu ana uwezo wa kufanya kazi na mawakala Wake Mwenyewe. Uwarundikia mzigo mzito watu masikini wenye ukomo na faida nzito zinazohusika na kufanya kazi kubwa, wakati wao hawatakuwa na fursa au wito wa kutumia sehemu kubwa ya mzigo wa masomo ambayo wamechukua muda kujipatia ustadi. Fursa za dhahabu zinapita katika umilele, na ushauri umetolewa ambao ulipaswa uzuiliwe; na kazi nyingi zaidi na bora zaidi zingeweza kufanywa, ambazo hazikufanyika, ikiwa mali na kipindi kilichotumiwa na wanafunzi hapo Battle Creek na watendakazi wengi vingefupishwa. Wanafunzi hao walipaswa kuwa kazini tayari, wakiwasilisha Nuru na maarifa waliyopokea kwa wale walio gizani. Mungu wa neema yote atatoa neema kwa neema. Wale wanaoenda kufanya kazi katika shamba la mizabibu la Bwana watajifunza jinsi ya kufanya kazi, na atawakumbusha maagizo ambayo wamepokea wakati wa maisha yao ya uanafunzi. Bwana hafurahii kuwatia kwenu moyo hawa wafanyikazi kutumia miaka katika kukusanya maarifa ambayo hawatakuwa na nafasi ya kutoa kwa wengine. Vijana wenye thamani, ambao wanapaswa kufanya kazi kwa ajili ya Mungu, wamekuja Battle Creek kupata elimu, na kupata maarifa bora ya jinsi ya kufanya kazi. Walipaswa kufundishwa yale ambayo ni muhimu katika kipindi kifupi sana. Hawapaswi kuhitajika kuchukua miaka kwa ajili ya elimu kabla ya kuitikia ule wito wa, “Nenda ukafanye kazi leo ndani shamba langu la mizabibu.” Badala ya kuwatumia wawe watenda kazi baada ya kuchukua miezi na miaka Chuoni, wao wanashauriwa kuchukua masomo mengine, na kufanya maendeleo katika mistari mingine ya ziada (vyeti au shahada zingine). Wao wanashauriwa kutumia miezi na miaka katika taasisi ambazo ile Kweli inakanushwa na kupingwa, na pale ambapo upotovu mkuu zaidi maana hauonekani kwa uwazi, ila ni wenye tabia isiyo ya kimaandiko unaingizwa kwa hila. Haya Mafundisho ya imani (doctrines) huchanganywa na masomo yao. Wanakuwa wamezama kwenye kusonga mbele katika mistari ya elimu, na wanapoteza upendo

wao kwa Yesu; na kabla ya kugundua shida ni nini, wanakuwa wameshaenda mbali kutoka kwa Mungu, na wote wanakuwa hawajajiandaa kuitikia amri, “Nenda fanya kazi leo katika shamba langu la mizabibu.” Matamanio ya juhudi za utume yamepotea/yameondoka. Wanafuata masomo yao kwa upendo mdanganyifu ambao unafunga mlango wa Kristo kuingia. Wanapohitimu, na kupata wito wa utume wa kwenda nje kama wanafunzi walioelimishwa ipasavyo, wengi wanakuwa ahwana mzigo wa kazi, na hawako tayari kujihusisha na kazi hiyo huduma kwa Mungu kuliko walipofika Battle Creek hapo kwanza. {FEsw 361.2}

Mjumbe aligeukia kusanyiko na kusema, “Je! unaamini unabii? Je, wewe unajua Ukweli, unaelewa ujumbe huo wa mwisho wa onyo, sasa unatolewa kwa ulimwengu, — Unajua kuwa mwito wa mwisho wa rehema unasikika sasa? Je, unaamini kwamba Shetani ameshuka akiwa na nguvu nyingi, akitenda kazi kwa udanganyifu wote wenye udhalimu kila mahali? Je! unaamini huo Babeli mkuu umekuja kama ukumbusho mbele za Mungu, na kwamba hivi karibuni atapokea kutoka kwa mkono wa Mungu mshahara mara mbili kwa kadri ya alivyotenda dhambi zake zote na maovu yake?” Shetani anafurahi ukiwashikilia na kuwachelewesha wanaume na wanawake katika Battle Creek ambao wanapaswa kuwa watenda kazi pamoja na Mungu katika shamba Lake kuu maadili la mizabibu. Ikiwa adui anaweza kuwazuia wafatendakazi nje ya uwanja kwa kisingizio chochote, yeye atafanya hivyo. Haya maandalizi ya hali ya juu ambayo yanazuia talanta zisiwepo shambani hayatoi nafasi kwa Bwana kufanya kazi na wafanyakazi Wake. Wengi wanaongozwa kukalia muda, talanta, na mali kwa ubinafsi katika kupata elimu ya juu, na wakati huo huo ulimwengu unaangamia kwa kukosa maarifa ambayo wangeweza kuyatoa. Kristo aliwaita wavuvi wasio na elimu, Naye akawapa watu hao maarifa na hekima wanaume hawa kwa kiwango ambacho wapinzani wao hawakuweza kuyakanusha au kuyapinga maneno yao. Ushuhuda wao umekwenda mpaka sehemu za mwisho za dunia. {FEsw 362.1}

Wanafunzi wa Kristo hawakuitwa kuwatukuza wanadamu, bali kumtukuza Mungu, Chanzo cha hekima yote. Waache waelimishaji watoe nafasi kwa Roho Mtakatifu kuifanya kazi yake juu ya mioyo ya wanadamu. Mwalimu mkubwa zaidi anawakilishwa katikati yetu na Roho Wake Mtakatifu. Haijalishi wewe umesoma kwa kiasi gani, na hata uweze kufikia elimu ya juu na bado juu zaidi, ingawa unachukua kila nukta ya muda wako kabla ya kufungwa kwa mlango wa rehema katika harakati ya kupata maarifa zaidi, hautakamilika. Wakati muda umekwisha, itakubidi ujiulize swali, “Nimeleta faida gani kwa wale walio katika giza la usiku wa manane? Ni kwa nani nimewasilisha maarifa ya Mungu, au hata maarifa ya mambo ambayo nimetumia muda mwingi na pesa kwa ajili yake?” Ni hivi karibuni tu maneno haya yatasikika yakitangazwa Mbinguni, “Imekwisha.” “Mwenye kudhulumu na azidi kudhulumu, na mwenye uchafu na aendelee kuwa mchafu; na yule mwenye haki na azidi kufanya haki; na mtakatifu na awe mtakatifu zaidi. Na tazama, Naja upesi; na ujira Wangu uko pamoja Nami, kumpa kila mtu kama kazi

yake ilivyo." Wakati tangazo hili lenye mamlaka likitolewa, kila kesi itakuwa imeamuliwa. Itakuwa bora zaidi watendakazi kuchukua kazi ndogo, na kuifanya polepole na kwa unyenyekevu, wakiivaa nira ya Kristo na kubeba mizigo yake, kuliko kujitolea miaka mingi katika maandalizi kwa ajili ya kazi kubwa, na kisha kushindwa kuleta wana na mabinti kwa Mungu, kushindwa kuleta nyara za ushindi na kuziweka miguuni pa Yesu. Wanaume na wanawake wanaganda au wanamangamanga hapo Battle Creek kwa muda mrefu sana (wanapoteza muda). Mungu anawaita, lakini hawasikii sauti Yake. Mashamba ya Bwana yametelekezwa, na hiyo ina maana kwamba akili hazina mwangaza. Mbegu za ufisadi zinapandwa kwa haraka katika mioyo ya vijana wetu, na zile Kweli kuu za vitendo lazima ziwasilishwe kwa watoto na vijana; kwani ile Kweli ina nguvu. {FEsw 363.1}

Walimu wakristo wameitwa kufanya kazi kwa ajili ya Mungu. Chachu ya Ukweli lazima itambulishwe kabla ya tabia kupata mabadiliko. Ingekuwa bora zaidi kwa vijana wetu kutobobea katika matawi ya masomo mbalimbali kuliko kukosa unyenyekevu na upole, na kukosa na mioyo minyofu na iliyopondeka. Kazi ya baadhi ya waelimishaji wetu imekuwa ni kuwafanya wanafunzi wasifae kuwa watenda kazi pamoja na Mungu. Unapaswa ujifunze ili kufahamu jinsi Yesu alivyofanya kazi na kuhubiri. Alikuwa akijinyima, akiikana nafsi na kujitoa mhanga. Hakuepuka kazi ngumu; Alipata shutuma, dharau, matusi, dhihaka, na manyanyaso/mateso; lakini je, wanafunzi wetu wameelimishwa kwa njia ambayo watajiandaa wapate kutembea katika nyayo Zake? Mungu hayuko katika kughaihirisha kwenu (kesho kesho tutamaliza shule!). Majaribu yenu yanayowapata ya kufuata mwaka baada ya mwaka kwenye mistari ya masomo, na kushikilia akili (za wanafunzi wasiende kazini), na mwishowe polepole wanapoteza Roho ambayo Bwana aliwavuvia kwenda kuifanya kazi katika shamba Lake la mizabibu. Kwa nini watu wanaowajibika hawawezi kutambua yale yatakayokuwa matokeo ya hakika ya kuwaweka kizuizini wanafunzi, na kuwafundisha kuhairisha badala ya kwenda kuifanya kazi ya Mungu? Wakati unapita kwa umilele, na bado wale waliotumwa kwenda Battle Creek ili kujitayarishwa kufanya kazi katika shamba la mizabibu la Bwana hawajahimizwa kufanya kile wanachoweza kufanya ili kuendeleza kazi ya Mungu. Fursa nyingi hutolewa kwa wale ambao tayari wanaujua Ukweli, na bado hawautendi ule Ukweli. Pesa na nguvu ambazo zingetawanywa katika njia kuu na vichochoro vya dunia, zinatumiwa kwa wale ambao hawajaboresha ile Nuru ambayo tayari wameipokea kwa kuwatangazia wale walio gizani. Filipo alipoipokea ile Nuru, alikwenda kumwita Nathanaeli; lakini vijana wengi ambao wanaweza kufanya kazi maalum kwa ajili ya Bwana, hawawezi kusogea mbele kwa kupiga hatua hadi wapate fursa nyingi. {FEsw 364.1}

Watumishi/wachungaji wa Yesu Kristo wanapaswa kugawanya sehemu fulani ya shamba la mizabibu la Mungu kwa watu wanaosimama sokoni bila kazi. Ikiwa wataboronga, basi warekebisheni makosa yao, na kuwaweka kazini tena. Wengi zaidi wamezuiwa kwenda kwenye kazi kuliko kuhimizwa katika kutumia talanta zao,

ila ni kwa kutumia uwezo wao walio nao sasa, ndipo watajifunza jinsi ya kutumia karama/vipaji vyao. Wengi wamekwenda Battle Creek kupata elimu ambao wangependa kuwa nayo kama wangependishwa vyema katika nchi zao (Leo vyuo vingi duniani vimeanzishwa, na si Marekani tu mfano AUA Nairobi imepunguza gharama kubwa). Muda umepotea, pesa imetumika bila sababu, kazi imeachwa bila kutekelezwa, na Roho zimepotea, kwa sababu ya kukorokotoa vibaya kwa hao ambao walidhani wanamtumikia Mungu. Bwana Yu hai, na Roho Wake Mtakatifu huongoza na hutawala kila mahali. Mtazamo kuwa Battle Creek ni Yerusalemu ya ulimwengu na kwamba wote lazima kwenda huko kuabudu haupaswi kutawala. Wale wanaotamani kujifunza, na wanafanya kila juhudi zinazowezekeza za kupata maarifa, wakitembea kwa uangalifu ndani ya ile Nuru ya Ukweli, hawahitaji kusafiri hadi Battle Creek. Mungu Ndiye Mwalimu wetu; na wale ambao wangeporesha vipaji vyao hapo walipo, watabarikiwa na walimu waliotumwa na Mungu ili kuwafundisha, —walimu ambao wamekuwa wakijiandaa kufanya kazi kwa ajili ya Bwana. Kutumia zaidi muda, kutumia pesa zaidi, ni kufanya makosa zaidi kuliko kupoteza; kwa wale wanaotafuta kupata elimu kwa gharama ya utauwa kwa vitendo wapo upande wa kushindwa (wanabadilishana elimu kwa utauwa wa vitendo). Kile wanachopata katikali mistari ya elimu wakati ambao walipaswa kuingia kwenye kazi, ni upotevu na hasara tu. Akili za Mbinguni zinasubiri mawakala wa kibinadamu ambao wanaweza kushirikiana nao kama wamisionari kwenye sehemu za giza duniani. Mungu anasubiri wanadamu washiriki kazi ya umishonari wa nyumbani katika miji yetu mikubwa (nchini kwetu), na wanaume na wanawake wanaendelea kubakia mjini Battle Creek wakati wanapaswa kusambazwa katika miji na vijiji, kando ya njia kuu na njia zile ambazo watu wengi hawapiti. Wanapaswa kuita na kuwaalika watu waje kwenye karamu ya arusi; kwani kila kitu sasa ki tayari. Kutakuwa na wamishonari ambao watafanya kazi nzuri katika shamba la mizabibu la Bwana ambao hawajakwenda Battle Creek (kusoma au kujipatia cheti). {FEsw 365.1}

Wale wanaokwenda Battle Creek hukutana na majaribu ambayo hawakudhani yangeweza kuwepo mahali hapo. Wanakutana na mambo ya kukatisha tamaa ambayo hawakuhitaji kuwa nayo, na hawasaidiwi katika uzoefu wao wa kidini kwa kwenda mahali hapo. Wanapoteza muda mwingi kwa sababu hawajui wanalopaswa kufanya, na hakuna aliye tayari kuwaambia. Wanapoteza muda mwingi katika kufuata kazi ambazo hazina mashiko katika kazi ambayo wangependwa kustahilishwa kuifanya. Kazi ya kawaida na ile takatifu zimechanganywa, na kusimama kwenye kiwango kimoja. Lakini hii sio sera ya busara. Mungu anatazama na wala haikubali. Mambo mengi yanaweza kuwa yamefanywa ambayo yangekuwa na ushawishi wa kudumu, kama wangepanya kazi kwa kiasi na kwa unyenyekevu mahali walipokuwa. Muda unapita; Roho zinaamua ama kwa ubaya au kwa wema, na vita vinaongezeka kila mara. Ni wangapi wanaoujua Ukweli wa wakati huu wanaofoaya kazi kwa kupatana na kanuni za

Ukweli wake? Ni kweli kuna jambo linafanyika; lakini zaidi, na mengi zaidi, yalipaswa kufanywa. Kazi ni inaongezeka, na muda wa kuifanya kazi unapungua. Sasa ni wakati wa wote kuwa na taa zinazowaka na kuangaza; na bado wengi wanashindwa kutunza utambi wa taa zao uwe ukiwaka na mafuta ya neema, na kuziweka tayari na kuwaka ili Nuru hiyo iweze kuangaza leo. {FEsw 366.1}

Wengi sana wanaitegemea kesho, ambayo iko mbali; lakini hilo ni kosa. Kila mtu na aelimishwe kwa namna ya kuonesha umuhimu wa kazi maalum inayopaswa kufanya leo. Hebu kila mmoja afanye kazi kwa ajili ya Mungu na kwa ajili ya Roho; hebu kila mmoja aonyeshe hekima, na kamwe asiwepo hata mmoja aliye goigoi, akimsubiri mtu aje karibu ili kumweka kazini. "Mtu fulani" ambaye anaweza kukufanya ufanye kazi analemewa na majukumu yaliyorundikana na muda unapotea katika kusubiri maelekezo yake. Mungu atakupa hekima katika kujirekebisha/matengenezo mara moja; kwani wito bado unatolewa, "Mwanangu, nenda ukafanye kazi leo katika shamba Langu la mizabibu." Baadhi wanaweza kuwa bado hawajaamua, ila bado wito unasikika, "Nenda ukafanye kazi leo katika shamba Langu la mizabibu." "Leo kama mtaisikia sauti Yake, msifanye migumu yenu mioyo." Bwana hutanguliza jambo linalohitajika kufanywa kwa Neno "mwanangu " ni nyororo kiasi gani, ni huruma iliyoje, lakini pamoja na hayo, ni dharura iliyoje! Mwaliko Wake wa kufanya kazi katika shamba Lake la mizabibu pia ni amri. "Au Hamjui ya kuwa miili yenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu; mliyepewa na Mungu? wala ninyi si mali yenu wenyewe. Maana mlinunuliwa kwa thamani; Sasa basi, mtukuzeni Mungu katika miili yenu na katika Roho zenu ambazo ni za Mungu." {FEsw 366.2}—*Special Testimonies On Education, March 21, 1895.*

Sura ya 43

ELIMU MUHIMU

Nimeandika kwa kiasi kikubwa nikirejelea wanafunzi kutumia muda mrefu bila sababu katika kupata elimu; lakini natumaini sitaleta kutoeleweka kuhusiana na kile ambacho ni elimu muhimu. Mimi simaanishi kuwa kazi ya juu juu inapaswa kufanywa kama inavyoonyeshwa na njia ambayo baadhi ya sehemu za ardhi zinafanyiwa kazi hapa nchini Australia. Katika kukatua jembe liliwekwa kwa kina cha inchi chache tu, ardhi haikuwa imetayarishwa kwa ajili ya mbegu, na mavuno yalikuwa machache, hakika yalilingana na maandalizi ya juu juu ambayo yalifanywa kwenye ardhi. {FEsw 368.1}

Mungu amewapa vijana na watoto akili za zenye udadisi ambazo zinauliza.

Uwezo wa kufikiri umekabidhiwa kwao kama talanta ya thamani. Ni wajibu wa wazazi kuweka suala la elimu mbele katika yao maana yake halisi; kwa maana inahusisha ufahamu wa mistari mingi. Wao wanapaswa kufundishwa ili kuboresha kila talanta na kiungo, ikitarajiwa kuwa wao watatumika kwenye utumishi wa Kristo kwa ajili ya kuinua ubinadamu ulioanguka. Shule zetu ni chombo maalum cha Bwana cha kuwafanya watoto na vijana waweze kufaa katika kazi ya umishonari. Wazazi wanapaswa kuelewa wajibu wao, na kuwasaidia watoto wao kuthamini mapendeleo makubwa na baraka ambazo Mungu amewaandalia wao katika faida za elimu. {FEsw 368.2}

Lakini elimu yao ya nyumbani inapaswa kuendana na elimu yao katika mistari ya kifasihi. Katika utoto na ujana mafunzo ya vitendo na fasihi yanapaswa kuunganishwa, na akili khifadhiwe na maarifa.

Wazazi wanapaswa kuhisi kwamba wana kazi adhimu/nzito ya kufanya, na wanapaswa kufanya kuishika kazi hii kwa dhati, bidii na umakini. Wanapaswa kuwafunza na kuwafinyanga tabia za watoto wao. Hawapaswi kuridhika na kufanya kazi ya juu juu. Kabla ya maisha ya kila mtoto kufunguliwa kuhusiana na maslahi ya juu; kwa maana wanapaswa kukamilishwa katika Kristo kwa njia ya vyombo ambavyo Mungu ameviweka. Udongo wa moyo unapaswa kushughulishwa; mbegu za Ukweli zinapaswa kupandwa humo katika miaka ya awali. Ikiwa wazazi watakuwa wazembe katika suala hili, wataitwa kutoa hesabu ya uwakili wao usio na uaminifu. Watoto wanapaswa kushughulikiwa kwa upole, huruma na upendo, na kufundishwa kwamba Kristo ni Mwokozi wao binafsi, na kwamba kwa tendo rahisi/sahili la kutoa mioyo yao na akili Kwake, wao wanakuwa wanafunzi Wake.

{FEsw 368.3}

Watoto wanapaswa kufundishwa kushiriki katika kazi za nyumbani. Wanapaswa kuelekezwa jinsi ya kumsaidia baba na mama katika mambo madogo ambayo wanaweza kufanya. Akili zao zinapaswa kuzoezwa kufikiri, kumbukumbu zao zitozwe zishughulishwe ili kukumbuka kazi waliyoteuliwa kuifanya; na katika mafunzo ya mazoea yenye manufaa nyumbani, wanaelimishwa kufanya majukumu ya kiutendaji yanayolingana na umri wao. Ikiwa watoto wanapata mafunzo yanayofaa nyumbani, hawatapatikana mitaani wakipokea elimu ya kubahatisha au holela ambayo wengi huipata. Wazazi wanaopenda watoto kwa njia ya busara hawatawaruhusu kukua na tabia za kivivu, na kuwa wajinga katika kufanya kazi za nyumbani. Ujinga haukubaliki kwa Mungu, na siyo rafiki katika kufanya kazi Yake. Ujinga haupaswi kuchukuliwa kama alama ya unyenyekevu, au kitu ambacho watu wanapaswa kusifiwa wakiwa nacho. Lakini Mungu anafanya kazi na watu licha ya ujinga wao. Wale ambao hawakuwa na nafasi ya kupata maarifa, au ambao wamepata fursa na wameshindwa kuziboresha, na kisha wanaongoka na kuwa upande wa Mungu, wanaweza kuwa na manufaa katika huduma ya Bwana kwa utendaji wa Roho Wake Mtakatifu. Lakini wale waliyo na elimu, nao wakajiweka

wakfu kwa utumishi wa Mungu, anaweza kufanya huduma kwa njia nyingi zaidi, na kuweweza kutimiza kazi kubwa zaidi katika kuleta Roho kwenye maarifa ya ile Kweli kuliko wale ambao hawajasoma. Wako kwenye jukwaa lenye manufaa zaidi, kwa sababu ya nidhamu ya nia na akili ambayo wamekuwa nayo. Hatutapunguza thamani ya elimu hata kidogo, lakini tunganisha kwamba iendelezwe mbele na hisia kamili kwenye akili ya ufupi wa wakati tulio nao sasa, ukilinganisha na kazi kubwa inayopaswa kutimizwa kabla ya kuja Kwake Kristo. Hatungependa wanafunzi kupokea wazo kwamba wao anaweza kutumia miaka mingi katika kujielimisha. Hebu na watumie elimu ambayo wameweza kuipata kwa muda ambao ni wa busara katika kuendeleza kazi ya Mungu (sio mrefu sana). Mwokozi wetu Yuko katika Patakatifu akiomba na kusihi kwa niaba yetu. Yeye Ndiye Kuhani wetu Mkuu anayefanya upatanisho, dhabihu na maombezi ya upatanisho kwa ajili yetu, akiomba kwa niaba yetu kupitia wema na ufanisi wa damu Yake. Wazazi wanapaswa kutafuta kumwakilisha Mwokozi huyu kwa watoto wao kuanzisha katika nia zao mpango wa wokovu, kwamba kwa ajili ya uvunjaji wetu wa sheria ya Mungu, Kristo alifanyika mbeba dhambi wetu. Uhalisia kwamba Mwana pekee wa Mungu alitoa uhai Wake kwa sababu ya kosa la mwanadamu, kukidhi matakwa ya haki na kutetea heshima ya Sheria ya Mungu, inapaswa kuwekwa daima mbele ya akili za watoto na vijana. Lengo la dhabihu hii kubwa pia linapaswa kuwekwa mbele yao; kwani ilikuwa ni katika kumwinua mwanadamu aliyeanguka, na aliyeshushwa hadhi na dhambi ndiyo sababu sadaka hii kubwa ilitolewa. Kristo aliteseka ili kwamba kwa njia ya Imani katika Yeye dhambi zetu zipate kusamehewa. Akawa mbadala na mdhamini wa mwanadamu. Alichukua adhabu Mwenyewe, ijapokuwa yote hakustahili yote, hiyo sisi tuliostahili adhabu tuweze kuwekwa huru, na kisha kurudi kwenye utii wetu kwa Mungu kupitia haki na wema wa Mwokozi Aliyesulubiwa na kufufuka. Yeye ni tumaini letu pekee la wokovu. Kupitia dhabihu Yake sisi tuliowekwa huru ila tukiwa katika majaribio, sasa ni wafungwa wa matumaini (Zek 9:2). Tunapaswa kufunua kwa malimwengu yote (universe), kwa ulimwengu ulioanguka na kwa ulimwengu usioanguka, kwamba kuna msamaha kwa Mungu, ili kwa upendo wa Mungu tupatanishwe Naye Mungu. Mwanadamu anatubu, anakuwa na huzuni moyoni, yaani moyo wake unavunjika, anamwamini Kristo kama Dhabihu Yake ya upatanisho, na kutambua kwamba Mungu amepatanishwa Naye. {FEsw 369.1}

Tunapaswa kuthamini kuwa na shukrani ya moyo siku zote za maisha yetu kwa sababu Bwana ameandika Maneno haya: “Kwa maana ndivyo asemavyo Bwana Aliye juu na aliyetukuka akaaye milele, ambaye Jina Lake ni Mtakatifu; akaaye mahali palipoinuka, palipo Patakatifu, pamoja na yeye aliyetubu na Roho ya unyenyekevu, ili kufufua Roho ya wanyenyekevu, na kufufua mioyo ya waliotubu.” Upatanisho wa Mungu kwa/na mwanadamu, kwa/na mwanadamu na Mungu, ni hakika wakati masharti fulani yanatimizwa. Bwana asema, “Dhabihu za Mungu ni Roho iliyovunjika: moyo uliovunjika na kupondeka, Ee Mungu, Wewe hutaudharau.”

Tena anasema, “Bwana Yuko karibu nao walio na moyo uliovunjika; na kuwaokoa wale walio wa Roho iliyotubu.” “Ijapokuwa Bwana Yuko juu, bado anamheshimu mnyonge; lakini wenye kiburi anawajua tokea mbali.” “BWANA asema hivi, Mbingu ni kiti Changu cha enzi, na dunia ni mahali pa kuweka miguu yangu; nyumba mtakayonijengea Mimi? na mahali pa pumziko langu ni wapi? Maana mkono Wangu ndio uliofanya hivi vyote, na vitu hivi vyote vimepata imekuwa, asema Bwana; lakini mtu huyu nitakayemwangalia, yeye aliyeko maskini, mwenye Roho iliyopondeka, naye hutetemeka asikiapo neno langu.” “Roho ya Bwana Mungu yu juu yangu; kwa sababu Bwana amenitia mafuta wahubiri wanyenyekevu habari njema; Amenituma ili kuzifunga waliovunjika moyo, kuwatangazia mateka uhuru wao, na kufunguliwa kwao wa gereza kwa wale waliofungwa; kutangaza mwaka uliokubalika ya Bwana, na siku ya kisasi cha Mungu wetu; kuwafariji wote wanaoomboleza; kuwachagulia waliao katika Sayuni, kuwapa uzuri badala ya majivu, mafuta ya furaha badala ya maombolezo, vazi la sifa kwa Roho ya uzito; ili waitwe miti ya haki, iliyopandwa na Bwana, ili atukuzwe.” Mwandishi wa-Zaburi anaandika, “Huwaponya waliopondeka moyo, na kuyafunga majeraha yao.” Japokuwa Yeye Ndiye mrejeshaji wa ubinadamu ulioanguka, lakini “Yeye huhesabu idadi ya nyota; Anaziita zote kwa majina yao. Bwana wetu ni Mkuu, na Mwenye uwezo mwingi, Akili Zake hazina kikomo. Bwana huwainua wanyenyekevu, Huwaangusha chini wasio haki ardhi. Mwimbieni Bwana kwa kushukuru; kuimba sifa juu ya kinubi kwa Mungu wetu.... Bwana huwaridhia wamchao Yeye katika wale wanaotumainia rehema Yake. Ee Yerusalemu, msifu Bwana; umsifu Mungu wako, Ee Sayuni.” {FEsw 370.1}

Masomo ya Zaburi hii ni ya thamani sana. Tutafanya vyema kuchukua muda wetu kusoma Zaburi nne za mwisho za Daudi. Pia maneno haya ya nabii, ni ya thamani sana: “Je! Theluji ya Lebanoni itakoma katika jabali la kondeni? Au je! Maji ya baridi yashukayo toka mbali yatakauka? Maana watu Wangu wamenisahau, wameufukizia ubatili uvumba; nao wamewakaza katika njia zao, katika mapito ya zamani, ili wapite katika njia za kando, katika njia isiyotengenezwa;” “Bwana asema hivi, Amelaaniwa mtu yule amtegemeaye mwanadamu, Amfanyaye mwanadamu kuwa kinga yake Na moyoni mwake amemwacha Bwana. Maana atakuwa kama fukara nyikani, Hataona yatakapotokea mema; Bali atakaa jangwani palipo ukame, Katika nchi ya chumvi isiyokaliwa na watu. Amebarikiwa mtu yule anayemtegemea Bwana, Ambaye Bwana ni tumaini lake. Maana atakuwa kama mti uliopandwa kando ya maji, Uenezao mizizi yake karibu na mto; Hautaona hofu wakati wa hari ujapo, Bali jani lake litakuwa bichi; Wala hautahangaika mwaka wa uchache wa mvua, Wala hautaacha kuzaa matunda. Moyo huwa mdanganyifu kuliko vitu vyote, una ugonjwa wa kufisha; nani awezaye kuujua? Mimi, Bwana, nauchunguza moyo, navijaribu viuno, hata kumpa kila mtu kiasi cha njia zake, kiasi cha matunda ya matendo yake.” {FEsw 371.1}— [Special Testimonies on Education, Aprili 22, 1895.](#)

Sura ya 44

ELIMU KAMILI NA YENYE UADILIFU

Harakati zozote zinazopunguza kiwango cha elimu katika shule yetu huko Battle Creek zisifanywe. Wanafunzi wanapaswa kuipa akili yao mzigo na kuishughulisha; kila kitivo kifikie maendeleo ya juu kwa kadri iwezekanavyo. Wanafunzi wengi huja chuoni wakiwa tayari wameunda mazoea fulani ya kiakili ambayo kwa kiasi fulani ni kikwazo kwao. Gumu zaidi ni jinsi ya kusimamia mazoea yao katika kufanya kazi

zao, ili yasiwe ratiba ya kawaida ya kila siku, badala ya kuleta kwenye masomo yao juhudi makini zilizodhamiriwa na kuweza kuzishikilia kanuni kwenye msingi wa kila somo linalozingatiwa. Kwa njia ya neema ya Kristo ipo ndani ya uwezo wao kubadili tabia hii ya mazoea, kwa ajili ya maslahi yao na kwa manufaa ya baadaye katika kuuelekeza uwezo wa kiakili, kuwafundisha kufanya utumishi kwa ajili ya Mwalimu Mwenye busara zaidi, ambaye nguvu Zake wanaweza kuzidai kwa imani. Hii itawapa mafanikio katika juhudi zake za kiakili, kwa mujibu wa sheria za Mungu. Kila mwanafunzi anapaswa kuhisi kwamba, chini ya Mungu, anapaswa kupata mafunzo maalum, utamaduni wa binafsi; na anapaswa kutambua kwamba Bwana anataka kutoka kwake ajiboreshe mwenyewe kwa uwezo wake, kwa kadri anavyoweza ili apate kuwafundisha wengine pia. Uvivu, kutojali, kutokuwa na ratiba au utaratibu, ni jambo la kutazamwa kwa hofu, na isitoshe, kujifungia kwenye utaratibu mtu aliojiwekewa yeye binafsi ni jambo la kuogopwa vivyo hivyo (yote mawili ni mabaya!). {FEsw 371.1}

Natumai kuwa hakuna mtu atakayepokea hisia kutoka kwa maneno yoyote ambayo Nimeandika, kwamba kiwango cha shule kimeshushwa kwa njia yoyote ile. Kunapaswa kuwa na elimu ya bidii na ya kina ndani shule yetu, na ili kupata hii, hekima inayotoka kwa Mungu, lazima iwe ya muhimu, yaani ipewe kipaumbele cha kwanza. Dini ya Kristo kamwe haitoa penalti au adhabu kwa ajili ya uvivu wa kimwili au kiakili. {FEsw 373.2}

Tunayo mbele yetu mfano wa kisa/kesi ya Danieli na wenzake, ambao waliboresha zaidi fursa zao katika kupata elimu kwenye nyua za Babeli. Walipojaribiwa na wale waliotilia shaka imani na ujuzi wao, waliweza kutoa tumaini ambalo lilikuwa ndani yao, na, vile vile, kusimama dede walipopatiwa mtihani unaohusiana na maarifa katika elimu yote na hekima; na ikaonekana kuwa Danieli naye alikuwa na ufahamu katika maono yote na ndoto, akionyesha ya kuwa yeye alikuwa na uhusiano hai na Mungu wa hekima yote. "Katika masuala yote ya hekima na ufahamu, aliowauliza Mfalme, akapata walikuwa bora mara kumi kuliko waganga na wanajimu wote waliokuwako katika ufalme wake wote." Historia ya Danieli imetolewa kwetu kuwa kielelezo, ushauri wenye mamlaka na maonyo kwetu sisi ambao miisho ya dunia imetujilia. "Siri ya Bwana i pamoja na wamchao." Daniel alikuwa katika uhusiano wa karibu pamoja na Mungu. Wakati amri ilipotoka kwa Mfalme mwenye hasira kali, akiamuru kwamba wenye hekima wote wa Babeli waangamizwe, Danieli na wenzake walitafutwa ili wauawe. Kisha Daniel akajibu, si kwa kulipiza kisasi, bali kwa shauri na hekima kwa jemadari wa walinzi wa Mfalme, ambaye alikuwa ametoka kuwaua wenye hekima wa Babeli. Danieli akauliza, "Mbona amri hii ya Mfalme ina ukali namna hii?" Akajihudhurisha mbele ya Mfalme, akiomba apewe muda, na imani yake katika Mungu aliyemtumikia ilimsukuma kusema kwamba atamwonyesha Mfalme tafsiri hiyo. "Kisha Daniel akaenda nyumbani kwake, akawajulisha jambo hilo Hanania, na Mishaeli, na Azaria, wenzake; ili waombe rehema kwa Mungu wa Mbinguni kwa habari ya siri hiyo, ili kwamba

Danielii na wenzake wasiangamizwe pamoja na wenye hekima wa Babeli. Ndipo Danieli alipofunuliwa siri hiyo katika njozi ya usiku. Basi Danieli akamhimidi Mungu wa Mbinguni. Danieli akajibu, akasema, Na lihimidiwe Jina la Mungu milele na milele; kwa kuwa hekima na uweza ni Wake. Yeye hubadili majira na nyakati; huuzulu wafalme na kuwamilikisha wafalme; huwapa hekima wenye hekima; huwapa wenye ufahamu maarifa; Yeye hufunua mambo ya fumbo na ya siri; huyajua yaliyo gizani, na Nuru hukaa Kwake. Nakushukuru, nakuhimidi, Ee Mungu wa Baba zangu, uliyenipa hekima na uwezo, ukanijulisha hayo tuliyotaka kwako; maana umetujulisha Neno lile la Mfalme. Basi Danieli akaenda kwa Arioko, aliyewekwa na Mfalme kuwaangamiza wenye hekima wa Babeli; alikwenda akamwambia hivi, Usiwaangamize wenye hekima wa Babeli; niingize mimi mbele ya Mfalme, nami nitamwonyesha Mfalme ile tafsiri. Ndipo Arioko akamwingiza Danieli mbele ya Mfalme kwa haraka, akamwambia hivi, Nimemwona mtu wa hao wana wa Yuda waliohamishwa, atakayemjulisha Mfalme ile tafsiri. Mfalme akajibu, akamwambia Danielii, aliyekuwa akiitwa Belteshaza, Je! Waweza kunijulisha ile ndoto niliyoiona, na tafsiri yake. Danielii akajibu mbele ya Mfalme, akasema, Ile siri aliyoiuliza Mfalme, wenye hekima hawawezi kumfunulia Mfalme; wala wachawi, wala waganga, wala wanajimu; lakini yuko Mungu Mbinguni afunuaye siri, naye amemjulisha Mfalme Nebukadreza mambo yatakayokuwa siku za mwisho. Ndoto yako, na njozi za kichwa chako ulizoziona kitandani pako, ni hizi;" (Soma [Danieli 2:20-28](#).) Hapa ndipo tafsiri hiyo ilijulishwa kwa Danieli. {FEsw 373.3}

Matumizi ya vitendo kwa karibu sana kwa wanafunzi hao wa Kiebrania yalifanywa kama zawadi ya mafunzo ambayo waliyapata toka kwa Mungu. Huku wakifanya juhudi kwa bidii ili kupaa maarifa yote yaliyo salama kujitwalia, Bwana akawapa hekima ya Mbinguni. Maarifa waliyopata yalikuwa yaliwahudumia wao kwa jinsi kuu, pale walipoletwa katika maeneo magumu. Bwana Mungu wa Mbinguni hatajaza mapungufu yanayotokana na uvivu wa kiakili na kiroho. Wakati mawakala wa kibinadamu watatumia uwezo wao kupata maarifa, kuwa watu wenye mawazo ya kina; wakati wao wanakuwa mashahidi wakubwa kwa Mungu na ile Kweli, basi watakuwa wameshinda katika uwanja wa uchunguzi wa Mafundisho muhimu ya imani yanayohusu wokovu wa Roho, ili kwamba Mungu wa Mbinguni apewe Utukufu, kama Yeye aliye mkuu, kisha hata mahakimu na wafalme wataletwa kukiri, katika mahakama za haki, katika mabunge na mabaraza, kwamba Mungu aliyezifanya mbingu na dunia, Ndiye Mungu wa pekee wa Kweli na aliye hai, Mwanzilishi wa Ukristo, Mwandishi na Mwanzilishi wa Ukweli wote, ambaye alianzisha Sabato ya siku ya saba wakati misingi ya ulimwengu iliwekwa, wakati nyota za asubuhi zilipoimba pamoja, na wana wote wa Mungu wakapiga kelele pamoja kwa furaha. Asilia yote itatoa ushuhuda, kama ilivyopangwa, kwa mfano wa Neno la Mungu (Uumbaji wote utashuhudia). {FEsw 374.1}

Vile vya asili na vile vya kiroho yanapaswa kuunganishwa katika masomo kwenye shule zetu. Shughuli za kilimo vinatoa vielelezo kwenye masomo ya Biblia.

Sheria zinazotiiwa na dunia zinafunua Ukweli kwamba vipo chini ya uwezo mkuu wa Mungu asiye na mwisho. Ni kanuni zile zile zinazotumika katika ulimwengu wa kiroho na wa ulimwengu wa asili. Mtaliki Mungu na Hekima Yake katika kupata elimu, nawe utakuwa na elimu yenye ulema, iliyoegemea upande mmoja tu, iliyokufa kwa sifa zote za kuokoa ambazo humpa mwanadamu uwezo, na kumfanya asiweze kupata hali ya kutokufa kwa njia ya imani katika Kristo. Mwandishi wa asili (nature) Ndiye mwandishi wa Biblia. Uumbaji na Ukristo vina Mungu mmoja. Wote wanaojihusisha na upatikanaji wa maarifa, wanapaswa kulenga kufikia raundi ya juu zaidi ya maendeleo. Hebu wasonge mbele haraka na kadiri wawezavyo; hebu uwanja wao masomo uwe mpana kadiri uwezo wao unavyoweza kukumbatia, wakimfanya Mungu kuwa hekima yao, wakishikamana na Yeye asiye na kikomo katika elimu, Yule awezaye kufunua siri zilizofichwa katika enzi na enzi, ni nani anayeweza kutatua matatizo magumu zaidi katika akili za hao wamwaminio Yeye peke yake, asiyeweza kufa, akaaye katika Nuru ambayo hakuna mtu awezaye kuikaribia. Mashahidi hai wa Kristo, wakifuata kumjua Bwana, watamjua Yeye, ambaye kutokea Kwake ni yakini kama asubuhi. "Chochote mwanadamu apandacho, ndicho atavuna pia." Kwa uaminifu na tasnia, na kwa utunzaji sahihi wa mwili, kwa kutumia kila nguvu ya akili kupata maarifa na hekima katika mambo ya kiroho, kila nafsi lazima iwe kamilifu katika Kristo, ambaye Ndiye alielelezo kamili cha mtu mkamilifu. {FEsw 375.1}

Yeye anayechagua mwenendo wa kutotii sheria ya Mungu anaamua hatima yake ya wakati ujao; anapanda katika mwili, akijichumia mshahara wa dhambi, hata uharibifu wa milele, ambayo ni kinyume cha uzima wa milele. Kujisalimisha kwa Mungu na utii kwa sheria Yake takatifu huleta matokeo ya hakika. "Huu ndiyo uzima wa milele, wakujue Wewe, Mungu wa pekee wa Kweli, na Yesu Kristo, ambaye Wewe uliyemtuma." Huu ni ujuzi wa thamani kubwa, ambao hakuna lugha inayoweza kuelezea; ni wa thamani ya juu zaidi katika ulimwengu huu, na unafikia mbali, hata kule kwenye uzima wa umilele. "Bwana asema hivi, Mwenye hekima asijisifu kwa sababu ya hekima yake, wala mwenye nguvu asijisifu kwa sababu ya nguvu zake, wala tajiri asijisifu kwa sababu ya utajiri wake; bali ajisifuye na ajisifu kwa sababu hii, ya kwamba ananifahamu Mimi, na kunijua, ya kuwa Mimi ni Bwana, nitendaye wema, na hukumu, na haki, katika nchi; maana Mimi napendezwa na mambo hayo, asema Bwana." {FEsw 376.1}

Tunapolenga kiwango cha chini, tutafikia kiwango cha chini tu. Tunashauri kwa kila mwanafunzi Kitabu cha vitabu kama utafiti mkuu kwa akili ya binadamu, kama elimu muhimu kwa maisha haya, na kwa uzima wa milele. Lakini sikufikiria kuruhusu kiwango cha elimu cha chini katika utafiti wa sayansi. Nuru ambayo imetolewa juu ya mada hizi iko wazi, na haipaswi kupuuzwa hata kidogo. Lakini ikiwa Neno la Mungu litoalo Nuru, na kumfahamisha mjinga, limekaribishwa ndani akili na hekalu la Roho, kama mshauri, kama kiongozi na mwalimu, wakala wa mwanadamu anayeishi kwa kila Neno litokalo ndani katika kinywa cha Mungu, basi

kusingekuwa na haja ya kukemewa kwa sababu ya kurudi nyuma kwa wanafunzi baada ya Baraka ya Mungu kuja kwao katika miale tele ya Nuru ya Bwana, yenye kung'aa katika moto Mtakatifu juu ya Madhabahu ya mioyo yao. Wengi waliruhusu burudani kuchukua kipaumbele, kuwa na ukuu. Hii haikuwa njia ambayo Danieli alifuata katika kupata elimu iliyodhihirisha kupitia kwake, ukuu wa hekima ya Mbinguni ulioshinda hekima yote na maarifa ya shule za juu zaidi katika nyua za Babeli yenye kiburi. Mungu anafungua ufahamu wa wanadamu kwa namna ya kushangaza na inayoacha alama, ikiwa Maneno Yake yataletwa katika maisha ya vitendo ya mwanafunzi, na Biblia inatambulika kama kitabu cha thamani, cha ajabu kama kilivyo. Hakuna kingine chochote kinachopaswa kuja katikati ya kitabu hiki, na mwanafunzi kama ndiyo muhimu zaidi; maana ndiyo ile hekima ambayo ikiletwa katika maisha ya vitendo, huwafanya watu kuwa na hekima kupitia wakati na kupitia umilele. Mungu amefunuliwa katika asili; Mungu anafunuliwa ndani Neno Lake. Biblia ndiyo historia ya ajabu na ya kushangaza kuliko historia zote, kwa asili yake ni uzalishaji wa Mungu (ni kazi Yake), na wala sio wa akili yenye ukomo. Inaturudisha nyuma kupitia karne hadi mwanzo wa mambo yote, ikiwasilisha historia ya nyakati na matukio ambayo vinginevyo yasingejulikana kamwe. Inadhihirisha Utukufu wa Mungu katika utendaji kazi wa majaliwa Yake ili kuokoa ulimwengu ulioanguka. Inawasilisha kwa lugha rahisi, uwezo mkuu wa injili, ambayo, ikipokelewa, itakata minyororo iliyowafunga watu kwenye gari la Shetani.

{FEsw 376.2}

Nuru inang'aa kutoka kwa kurasa takatifu, kwa miale iliyo wazi, tukufu, ikituonyesha Mungu, Mungu aliye hai, akiwakilishwa katika sheria za serikali Yake, katika kuumba ulimwengu, katika mbingu ambazo Yeye amezipamba. Nguvu Zake zinapaswa kutambuliwa kama njia pekee ya kuukomboa ulimwengu kutokana na imani zenye ushirikina, ambazo zinamkosea Mungu heshima na kumdhalisha mwanadamu. Kila mwanafunzi wa Biblia ambaye haji tu kwenye ukweli uliofunuliwa kupitia elimu ya akili (ubongo tu), lakini pia kupitia uwezo wake wa unaobadilisha moyo na tabia, ataiwakilisha tabia ya Mungu kwa ulimwengu wetu katika maisha yenye utaratibu mzuri na mazungumzo ya utauwa (ya kimbingu). Kuingia kwa Neno hutoa mwanga (Kufafanusha kwa Maneno Yako kwatia Nuru, Na kumfahamisha mjinga [Zaburi 119:129](#)). Akili imepanuliwa, imeinuliwa, imetakaswa. Lakini wengi wamefuata mkondo wa hatua usioendana na maarifa ya Ukweli na Nuru ya ajabu kupitia kushuka kwa Roho Mtakatifu wa Mungu kwa namna ya ajabu iliyoweka alama juu ya mioyo katika Battle Creek. Dhambi kubwa na hasara zilikuwa matokeo ya kupuuza kutembea katika Nuru kutoka Mbinguni. Katika kutumbukia katika burudani/maburudisho, michezo ya mechi (ushindani kama vile soka, karata, kamari), maonyesho ya masumbwi au mieleka, waliutangazia ulimwengu kwamba Kristo hakuwa kiongozi wao katika mambo haya yote. Haya yote yalikaribisha maonyo kutoka kwa Mungu. Sasa kile ambacho kinanielemea moyoni ni hatari ya kwenda katika hali ya kupitiliza upande mwingine; hakuna

ulazima kwa hili; ikiwa Biblia imefanywa kuwa mwongozo, mshauri, itahamasisha na kutoa ushawishi juu ya akili na moyo wa wale wasioongoka. Ujifunzwaji na uchunguzi wake, zaidi ya usomaji mwingine wowote, utaacha mvuto wa Bwana/mbingu. Biblia Itapanua akili ya mwanafunzi mkweli na aliye wazi/muwazi, hivyo itaijalia akili hisia, misukumo na nguvu mpya. Itatoa ufanisi mkubwa wa vitivo kwa kuileta katika kuwasiliana na Ukweli mkuu unaoenda mbali sana. Daima hufanya kazi, ikichora, ikiumba; ni chombo chenye ufanisi katika kuongoa nafsi. Ikiwa akili ya mwanadamu inakuwa duni au na umbilikimo na dhaifu na isiyofaa, ni kwa sababu imeachwa kushughulikia masomo ya kawaida tu (yasiyo na umuhimu, yasiyostaajabisha). {FEsw 377.1}

Mungu anaweza na atafanya kazi kubwa kwa kila mwanadamu ambaye atafungua moyo wake kwa Neno la Mungu, na kuliruhusu liingie katika hekalu la nafsi na kufukuza kila sanamu. Akili na moyo zitaitwa kwa bidii kwenye mafunuo ya ajabu ya mapenzi ya Mungu. Roho iliyoongoka itafanywa kuwa na nguvu katika kupinga maovu. Katika kujifunza/kuichunguza Biblia nafsi iliyoongoka hula mwili na kunywa damu ya Mwana wa Mungu, ambayo Yeye Mwenyewe anaifasiri kama kupokea na kuyatenda Maneno Yake, ambayo ni Roho na uzima. Neno anafanyika mwili, na kukaa miongoni mwetu, katika wale wanaopokea Maagizo matakafu ya Mungu, Neno la Mungu. Mwokozi wa ulimwengu ameacha mfano mtakatifu, na safi kwa watu wote. Neno Linaangazia, linainua, na kuleta kutokufa kwa wote ambao wanatii matakwa ya Bwana. Hii ndio sababu yangu ya kukuandikia kama nilivyofanya. Mungu apishilie mbali kwamba kwa kukosa utambuzi makosa yafanyike kwa kutoyaelewa maneno yangu niliyoelekeza kwako wewe. Sijapata hisia nyingine zaidi ya ile ya kufurahia kujua kwamba wanafunzi wakiwa wametoka kujifunza Maneno ya uzima akili zao zinapanuliwa, zinainuliwa, zinakuzwa, na nguvu zao zilizozorota zinaamshwa ili kujihusisha na masomo ya sayansi kwa kuyathamini kwa umakini zaidi; wanaweza kuwa wasomi kama Danieli, wakiwa na kusudi la kukuza na kutumia kila nguvu ili kumtukuza Mungu. Lakini hili linakuwa jukumu la kila mwanafunzi, kujifunza kutoka kwa Mungu, Yeye atoaye hekima, jinsi ya kujifunza kwa faida bora zaidi; kwa kuwa wote ni **wataradhiwa** wa kutokufa.

{FEsw 378.1}

Bwana Mungu alishuka katika ulimwengu wetu akiwa amevikwa tabia za ubinadamu, ili afanye kazi katika maisha Yake Mwenyewe. pambano la kushangaza kati ya Kristo na Shetani. Yeye aliziaibisha/aliziumbua nguvu za giza. Historia hii yote inamwambia mwanadamu, Mimi, mbadala wako na mdhamini, nimechukua asili yako juu Yangu, kuonyesha kuwa wewe kwamba kila mwana na binti wa Adamu ana upendeleo wa kuwa mshiriki wa asili ya Uungu, na kupitia Kristo Yesu aweze kushikilia kutokufa. Wale ambao ni wataradhiwa wa baraka hii kuu, wanapaswa katika kila jambo kutenda kwa namna inayowakilisha manufaa yao katika kushirikiana na Bwana kupitia Ukweli Wake uliofunuliwa na kupitia utakaso wa Roho Wake Mtakatifu. Hii itapanua akili ya wakala wa kibinadamu, na kuifunga

juu ya mambo matakatifu, na kuiweka tayari ili kupokea ile Kweli, kufahamu Ukweli, ambao utasababisha kufanya kazi nje ya Ukweli kupitia utakaso wa moyo, nafsi na tabia. {FEsw 379.1}

Wale ambao wana uzoefu huu hawatakubali kujihusisha katika burudani ambazo zimekuwa zikifyonza na kupotosha mno katika ushawishi wake, ikifunua kwamba nafsi imekuwa haili na kunywa Maneno ya uzima wa milele. Kuondoka kutoka kwenye usahili, na unyenyekevu wa utauwa wa Kweli kwa upande wa wanafunzi lilikuwa jambo lenye ushawishi wa kudhoofisha tabia na kupunguza nguvu za kiakili. Maendeleo yao katika sayansi yalirudi nyuma, ilhali wangukuwa kama Danieli, wasikilizaji na watendaji wa Neno la Mungu, wangesonga mbele kama yeye alivyosonga katika matawi yote ya elimu wayoyaingia/waliyoyashughulikia. Kuwa na akili zenye usafi wa moyo, wangukuwa na nia zenye nguvu. Kila kitivo cha kiakili kingenolewa kwa ukali. Acha Biblia ipokelewe kama chakula pekee cha nafsi za watu, kwani ndiyo iliyo bora kabisa na yenye manufaa zaidi katika kutakasa na uimarishaji wa akili. {FEsw 379.2} -Special Testimonies on Education, April 22, 1895.

VITABU NA WAANDISHI KATIKA SHULE ZETU

Nina mambo kadhaa ambayo ningependa kuyawasilisha mbele yenu kuhusu elimu. Walimu katika shule zetu wana heshima kubwa kwa waandishi na vitabu vilivyo kwenye mzunguko unaoendelea sasa katika sehemu kubwa ya taasisi zetu za elimu. Mbingu zote zimekuwa zikiangalia taasisi zetu za elimu (ujifunzaji) na kuwauliza, Makapi ni nini kwa ngano? Bwana ametupa maagizo ya thamani zaidi katika Neno Lake, akitufundisha ni tabia gani tunapaswa kuunda katika maisha haya ili kututayarisha kwa siku zijazo, maisha yale ya kutokufa. Imekuwa desturi kuinua vitabu na waandishi ambao hawatoi msingi wa elimu wa kweli ufaao. Kutoka chanzo kipi waandishi hawa walipata hekima yao, sehemu kubwa ya machapisho haya hayastahili heshima yetu, hata kama waandishi hawa wanazingatiwa kuwa ni watu wenye hekima? Je, wamechukua masomo yao kutoka kwa Mwalimu Mkuu ambaye ulimwengu umewahi kujua? Ikiwa sivyo, wameamua kwa hiari kuwa kwenye makosa. Wale wanaojiandaa kwa makao ya Mbinguni wanapaswa kupendekezewa kuifanya Biblia kuwa kitabu chao kikuu cha mafunzo.

{FEsw 381.1}

Waandishi hawa wanaopenda na maarufu hawajawaelekeza wanafunzi kwenye njia inayoongoza kwenye uzima wa milele. “Na huu ndio uzima wa milele, wakujue Wewe, Mungu wa pekee na wa Kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma.” [Yohana 17:3](#). Waandishi wa vitabu vinavyotumiwa sasa katika shule zetu wanapendekezwa na kuinuliwa kama wasomi; elimu yao ina mapungufu kwa kila njia, isipokuwa wao wenyewe wameelimishwa katika shule ya Kristo, na kwa maarifa ya vitendo wanatoa ushuhuda kwa Neno la Mungu kama somo muhimu zaidi kwa watoto na vijana. “Kumcha Bwana ni chanzo cha hekima.” Vitabu vinapaswa kuwa tayari kuwekwa mikononi mwa wanafunzi, vitabu ambavyo vitawaelimisha wawe na upendo wa dhati, wenye kuheshimu Ukweli na uadilifu thabiti. Aina ya masomo ambayo ni chanya, na muhimu katika malezi ya tabia ya kuwapa maandalizi ya maisha ya baadaye, inapaswa kuwekwa mbele yao daima. Kristo anapaswa kuinuliwa kama Mwalimu Mkuu wa kwanza, Mwana pekee wa Mungu, ambaye alikuwa pamoja na Baba tangu enzi za milele zote. Mwana wa Mungu alikuwa Mwalimu mkuu aliyetumwa ulimwenguni kama Nuru ya ulimwengu. “Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu.” Baba aliwakilishwa katika Kristo, na umakini katika elimu lazima uwe wa tabia hiyo ambayo watamtazama na kumwamini Yeye kama Mfano wa Mungu. Alikuwa na utume wa ajabu sana kwa ulimwengu huu, na kazi Yake haikuwa katika mstari wa kutoa uhusiano kamili wa madai yake binafsi ya Uungu, lakini unyonge/kudhilishwa kwake kulikuwa ni mficho wa madai Yake. Hii ndiyo sababu taifa la Kiyahudi halikumkiri Kristo kama Mkuu wa uzima; kwa sababu hakuja na maonyesho na mwonekano wa nje, kwa maana alificha tabia Yake ya

Utukufu, chini ya vazi la ubinadamu Wake. {FEsw 381.2}

Familia ya kibinadamu ilipaswa kumzingatia katika Nuru ya Maandiko Matakatiifu, ambayo yangeshuhudia namna ya kuja Kwake. Kama angekuja akionyesha Utukufu Wake aliokuwa nao pamoja na Baba Yake, basi Njia Yake kisha kuelekea msalabani ingezuiliwa na kusudi la wanadamu, ambao wangemchukua kwa nguvu, na kumfanya Yeye kuwa Mfalme. Alitakiwa kufunga maisha Yake kwa kutoa dhabihu nzito/adhimu Ya mwili Wake Mwenyewe. Mfano ulipaswa kuufikia halisi katika Yesu Kristo (type ni mfano kama Adamu, antitype ni halisi yaani Yesu 1 Kor 15:22). Maisha Yake yote yalikuwa utangulizi wa kifo Chake msalabani. Tabia yake ilikuwa maisha ya utii kwa amri zote za Mungu, na ilipaswa kuwa kielelezo cha watu wote duniani. Maisha yake yalikuwa sheria hai katika ubinadamu. Sheria hiyo Adamu aliivunja. Lakini Kristo, kwa utii Wake mkamilifu kwa sheria alikomboa kushindwa kwa fedheha/aibu kwa Adamu na kuanguka. {FEsw 382.1}

Unabii unapaswa kuchunguzwa, na maisha ya Kristo yalinganishwe pamoja na maandiko ya manabii. Anajitambulisha Mwenyewe na unabii, akisema tena na tena, yaliandika kunihusu Mimi; yananishuhudia Mimi. Biblia ndicho kitabu pekee kinachotoa maelezo chanya wa Kristo Yesu; na kama kila mwanadamu angeisoma kama chake cha kiada/mafunzo, na kuitii, hakuna mtu ambaye angepotea. {FEsw 382.2}

Miale yote ya Nuru inayoangaza katika Maandiko huelekeza kwa Yesu Kristo, na kumshuhudia Yeye, ikiunganisha pamoja Agano la Kale na Jipya Maandiko. Kristo anaonyeshwa kama Mwanzilishi na Mkamilishaji wa imani yao, Yeye Mwenyewe ambaye matumaini yao ya uzima wa milele yamejikita ndani Yake. “Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili kila amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele” {FEsw 383.1}

Ni kitabu gani kinachoweza kujaribu kulinganishwa na Biblia? Ni cha muhimu kwa kila mtoto, kwa kila kijana, na kwa watu wazima kukielewa; kwa kuwa ni Neno la Mungu, Neno la kuongoza familia yote ya kibinadamu Mbinguni. Basi kwa nini Neno kutoka kwa Mungu halina vipengele muhimu ambavyo vinajumuisha elimu? Nao waandishi wasiovuviwa wamewekwa mikononi mwa watoto na vijana katika shule zetu kama vitabu vya kiada/somo— vitabu ambavyo wanapaswa kuelimishwa navyo. Vinawekwa mbele yavijana, vikichukua muda wao wa thamani katika kusoma mambo hayo ambayo hawawezi kuyatumia kamwe. Vitabu vingi vimeingizwa mashuleni ambavyo havikupaswa kuwekwa hapo. Vitabu hivi havineni kwa maana yoyote yale Maneno ya Yohana, “Tazama Mwana-Kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu.” Mada kuu ya somo katika shule yetu inapaswa kuwa kuwanda watu kwa siku zijazo, za maisha ya kutokufa. {FEsw 383.2}

Yesu Kristo ni maarifa/ ujuzi wa Baba, na Kristo ni Mwalimu wetu Mkuu

aliyetumwa na Mungu. Kristo ametangaza katika sura ya sita ya Yohana kwamba Yeye Ndiye mkate ulioshuka kutoka Mbinguni. “Amin, Amin, Nawaambia, Yeye aniaminiye Mimi yuna uzima wa milele. Mimi Ndimi mkate huo wa uzima. Baba zenu walikula mana jangwani, na wamekufa. Huu ndio mkate ushukao kutoka Mbinguni, kwamba mtu anaweza kula, asife. Mimi Ndimi mkate ulio hai uliokuja chini kutoka Mbinguni: mtu akila mkate huu, ataishi milele. na chakula nitakachotoa ni mwili Wangu, Na chakula nitakachotoa mimi ni mwili Wangu, kwa ajili ya uzima wa ulimwengu.” Wanafunzi hawakuelewa Maneno Yake. Kristo amesema, “Roho Ndiye atiaze uzima; mwili haufai kitu; Maneno hayo niliyowaambia ni Roho, tena ni uzima.” {FEsw 383.3}

Ni muhimu sana, katika mwanga wa masomo ya Kristo, kila mwanadamu ajifunze Maandiko, ili apate kusadikishwa kuhusu Yeye ambaye matumaini yake ya uzima wa milele yamejikita ndani Yake. Biblia ilipaswa kufanywa kuwa kitabu kikuu cha mafunzo, ambacho kimeshuka kwetu kutoka Mbinguni, nayo ni Neno la uzima. Je, kitabu hicho kinachotuambia kile tunachopaswa kufanya ili kuokolewa, kiwekwe kando katika kona, na machapisho au uzalishaji wa kibinadamu unuliwe kwamba ndiyo hekima kuu katika elimu? Maarifa yale ambayo watoto na vijana wanahitaji kuyapata kwa ajili ya manufaa katika maisha haya, na kwamba waweze kuyabeba pamoja nao katika maisha yajayo, hupatikana katika Neno la Mungu. Lakini hili halihimizwi na kuwasilishwa mbele yao kama maarifa ya muhimu zaidi, na kama yale ambayo yatatoa kwa usahihi zaidi habari za Mungu wa Kweli, na Yesu Kristo ambaye amemtuma. Kuna miungu mingi na mafundisho ni mengi. Kuna semi nyingi za binadamu zinazoeleza ukweli na jinsi ya kuenenda na amri zinazowekwa mbele ya vijana wetu kama amri za Mungu. Haiwezekani kwao kuelewa Ukweli ni nini, ni nini kilicho kitakatifu, na nini ni cha kawaida, ila tu pale wao watakapoyaelewa Maandiko ya Agano la Kale na Jipya. {FEsw 384.1}

Neno la Mungu linapaswa kusimama kama kitabu cha juu kabisa katika kuelimisha kwenye ulimwengu wetu, na kinapaswa kutendewa kwa tahadhari na kicho kitakatifu. Ni kitabu chetu cha mwongozo; tutapokea kutoka humo Ukweli. Tunahitaji kuwasilisha Biblia kama kitabu kikuu cha somo cha kuweka mikononi mwa watoto na vijana wetu, ili wamjue Kristo, ambaye kumjua Yeye ni uzima wa milele. Ni kitabu cha kujifunzwa na wale walio umri wa kati, na wale ambao ni wazee. Neno lina ahadi, maonyo, faraja, na uhakikisho wa upendo wa Mungu kwa wote wanaomkubali kuwa Mwokozi wao. Hivyo weka Neno takatifu mikononi mwao. Watie moyo kulitchunguza Neno, na kwa kufanya hivyo watapata hazina zake zilizofichwa, zenye thamani isiyo na kifani kwao katika maisha haya ya sasa, na katika kumpokea Kristo kama mkate wa uzima wanayo ahadi ya uzima wa milele. {FEsw 384.2}

Kitabu cha kiada cha mafundisho, Biblia, kina maagizo ya tabia- wanapayoswa kuwa nayo, ubora wa maadili ambayo ni lazima yakuzwe, ambayo Mungu na

mbingu wanahitaji. “Heri wenye moyo safi; maana hao watamwona Mungu.” “Fuata amani na watu wote, na utakatifu ambao hapana mtu atakayemwona Bwana asipokuwa nao.” “Mpenzi, sasa sisi ni wana wa Mungu, na bado haijadhihirika wazi jinsi tutakavyokuwa: lakini twajua ya kuwa, atakapodhihirishwa, tutafanana Naye; kwa maana tutamwona jinsi alivyo. Na kila mtu aliye na tumaini hili ndani Yake hujitakasa kama vile Yeye alivyo mtakatifu. Yeyote anayetenda dhambi anavunja sheria za Mungu; kwa maana dhambi ni uvunjaji wa sheria. Nanyi mnajua ya kuwa Yeye alidhihirishwa, ili aziondoe dhambi; na katika Yeye hakuna dhambi.” {FEsw 385.1}

Maarifa haya muhimu sana yanapaswa kuwekwa mbele ya watoto na vijana, sio kwa njia ya kiholela, ya kidikteta, bali kama ufunuo wa Bwana, ambao ni wa thamani kuu ya kupata amani yao ya sasa; burudiko, na utulivu wa akili katika ulimwengu huu wa sasa wa misukosuko, ugomvi na migogoro, na kama matayarisho ya siku zijazo, uzima wa milele katika ufalme wa Mungu, ambapo watamwona Mungu, na kumjua Mungu na Yesu Kristo, ambaye alitoa maisha Yake ya thamani ili kuwakomboa.” {FEsw 385.2}

Kristo alikuja katika umbo la mwanadamu kuishi sheria ya Mungu. Alikuwa Neno la uzima. Alikuwa kuwa injili ya wokovu kwa ulimwengu, na kutimiza kila bayana ya sheria. Yesu Ndiye Neno, kitabu cha mwongozo, ambacho lazima kipokelewe na kutiiwa katika kila kipengele maalumu. Ni muhimu kiasi gani kwamba mgodi huu wa Ukweli uchunguzwe, na hazina za thamani za Ukweli zigunduliwe na kutunzwa kuwa Tajiri vito. Kufanyika mwili kwa Kristo, Uungu Wake, Upatanisho Wake, Wake maisha Yake ya ajabu Mbinguni kama wakili wetu, ofisi ya Roho Mtakatifu—mandhari hizi zote zilizo hai na muhimu za Ukristo zinafunuliwa kutoka kitabu cha Mwanzo hadi Ufunuo. Viunganishi vya dhahabu vya Ukweli huunda mnyororo wa Ukweli wa kiinjili, na la kwanza, na kuu, hupatikana katika Mafundisho ya Kristo Yesu. Kwa nini, basi, Maandiko hayapaswi kutukuzwa, kupewa ubora wote na kuinuliwa katika kila shule iliyo katika ardhi yetu? Ni kwa udogo jinsi gani, watoto wadogo huelimishwa kujifunza Biblia kama Neno la Mungu, na kujilisha Ukweli wake, ambao ni mwili na damu ya Mwana wa Mungu! “Msipoula mwili Wake Mwana wa Adamu na kuinywa damu Yake, hamna uzima ndani yenu. Aulaye mwili wangu na kuinywa damu yangu [yaani, anaendelea kupokea Maneno ya Kristo, na kuyatenda], ana uzima wa milele; Nami nitamfufua siku ya mwisho. Kwa maana mwili Wangu ndio chakula cha Kweli, na damu yangu ni kinywaji cha Kweli. Aulaye mwili Wangu, na kuinywa damu Yangu, hukaa ndani Yangu, Nami hukaa ndani yake.” “Na yeye huyo azishikaye amri Zake hukaa ndani Yake, Nami ndani yake. Na Katika hili twajua ya kuwa anakaa ndani yetu, kwa huyo Roho aliyetupa.” {FEsw 385.3}

Kuna ulazima wa kila familia kuifanya Biblia kuwa kitabu chao cha mafunzo/masomo. Maneno ya Kristo ni dhahabu tupu, bila hata chembe moja ya takataka, isipokuwa watu, kwa ufahamu wao wa kibinadamu, watajaribu kuweka

huko (takataka), na kuufanya uwongo uonekane kama sehemu ya Ukweli. Kwa wale ambao wamepokea tafsiri ya uongo ya Neno, wakati wao kuchunguza Maandiko wameazimia kuyachunguza Maandiko kwa juhudi ili kupata mafuta ya mifupani (uboho) ya Ukweli uliomo ndani yake, Roho Mtakatifu hufungua macho ya ufahamu wao, na zile Kweli za Neno kwao ni mpya kama mafunuo. Mioyo yao inahuishwa kwa imani mpya na iliyo hai, na wanaona mambo ya ajabu katika sheria Yake. Mafundisho ya Kristo yana upana na kina kwa wengi ambao hawajawahi kuelewa kabisa kabla.” {FEsw 386.1}

Mafundisho ya neema na Ukweli hayaeleweki kwa hakika na idadi kubwa ya wanafunzi wetu na washiriki wa kanisa. Upofu wa akili umetokea kwa Israeli. Kwa mawakala wa kibinadamu kupotosha na kuunda ujenzi wa kulazimisha, ulio na nusu Kweli, na mafumbo juu ya Maneno ya Mwenyezi Mungu, ni kitendo kinachohatarisha Roho zao, na Roho za wengine. “Kwa maana namshuhudia kila mtu ayasikiaye Maneno ya unabii wa kitabu hiki. Mtu ye yote akiongeza katika hayo, Mungu atamwongezea hayo mapigo yaliyoandikwa katika kitabu hiki; na kama mtu yeyote ataondoa Maneno ya kitabu hiki cha unabii, Mungu atamwondolea sehemu yake katika kitabu cha uzima, na katika ule mji mtakatifu, ambao habari zake zimeandikwa katika kitabu hiki.

” Ufunuo 22:18, 19. Wale ambao, kwa ujenzi wao wa kibinadamu, watafanya Maandiko yatamke yale ambayo Kristo hajawahi kuyaweka ndani yake, hudhoofisha nguvu zake, na kuifanya sauti ya Mungu katika maagizo, mafundisho na maonyo ya kushuhudia uwongo, ili kuepuka usumbufu unaojitokeza katika utiifu kwa matakwa ya Mungu, zimekuwa mbao ishara na matangazo, zinazoelekeza katika njia isiyo sahihi, katika njia za uwongo, zinazoongoza kwenye uasi na kifo.” {FEsw 386.2}

Ushuhuda wa Alfa na Omega kuhusiana na adhabu ya kufanya neno moja lililotamkwa na Mwenyezi Mungu kuwa lisilo la maana ni tamko la uangamivu wa kutisha watakaoupata katika mapigo yaliyoandikwa katika Kitabu; majina yao yataondolewa kwenye kitabu cha uzima, na kutoka katika mji mtakatifu.” {FEsw 387.1}

Ni wangapi wanaweza kujibu swali hili ukweli wa moyoni mwao, Je! ni elimu gani iliyo muhimu kwa wakati huu? Elimu ina maana kubwa zaidi kuliko wengi wanavyodhani. Elimu ya Kweli inahusisha ndani mafunzo ya kimwili, kiakili, na kiadili, ili **uwezo wote ustahilishwe** kwa ukuaji bora zaidi, katika kumtumikia Mungu, na kufanya kazi ya kuuinua ubinadamu. Kwa kutafuta utambuliwe na watu, na kuitukuza nafsi yako, utajiacha wewe kama binadamu ukiwa umeondokewa na Roho wa Mungu, ukiwa huna neema hiyo ambayo ikumfanya kuwa mtenda kazi mzuri kwa ajili ya Kristo. Wale wanaotamani kumtukuza Mungu tu, hawatajitahidi kuleta sifa zao ili zionekane machoni pa watu, au kujibidisha watambuliwe, au kuonekana kuwa wapo mahali pa juu zaidi. Wale wanaosikia wito wa Mkombozi

wa ulimwengu, na kutii mwito huo, watatambuliwa kama watu tofauti, wenye kujitoa nafsi zao mhanga, watu watakatifu.” {FEsw 387.2}

Ikiwa wanafunzi katika shule zetu watasikiliza kwa madhumuni ya kusikia na kisha kutii mwaliko ule wa, “Njooni Kwangu, ninyi nyote msumbukao na kulemewa na mizigo, Nami nitawapumzisha. Jitieni nira Yangu, na jifunzeni Kwangu; kwa kuwa Mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo, nanyi mtapata raha nafsiini mwenu. Kwa maana nira Yangu ni laini, na mzigo Wangu ni mwepesi.” zitakuwa nyaraka zilizo hai, zinazojulikana na kusomwa na watu wote. “Hakika Mimi nawaambia, Msipoongoka na kuwa kama watoto wadogo; hamtaingia katika ufalme wa Mbinguni. Yeyote basi atajinyenyekesha kama mtoto huyu mdogo, **yeye ndiye aliye mkuu kuliko wote ufalme wa Mbinguni.**” Vijana wanahitaji waelimishaji ambao wataliweka Neno la Mungu daima mbele yao katika kanuni hai. Ikiwa wao wataweka maagizo ya Biblia daima kama kitabu chao cha kiada, watakuwa na ushawishi mkubwa zaidi juu ya vijana; kwa maana walimu watakuwa wanafunzi, wakiwa na mguso hai na Mungu. Wakati wote wanafundisha na kurudia mawazo na kanuni ambazo zitaongoza kuwa na maarifa zaidi ya Mungu, unyofu na bidii, kukua kwa imani kwa niaba yao katika damu ya Yesu, na nguvu na ufanisi wa neema ya Bwana wetu Yesu Kristo kuwatunza wasianguke; kwa sababu mara kwa mara wanatafuta ngome ya uzoefu wa Kikristo wenye afya na uwiano mzuri, wakibeba sifa pamoja nao kwa manufaa ya baadaye, na akili, na ucha Mungu. Waalimu wanaona na kuhisi kwamba ni lazima wafanye kazi ili wasizipunguze juhudi za wenzao kwa kuwafanya mbilikimo kiroho na kutia doa akili za washirika wao, kwa kuwa na huduma dhaifu/gonjwa ya nusu-dini (vuguvugu). Kuna haja ya kuondoa kwenye taasisi zetu za elimu fasihi potofu, zenye uchafuzi, ili mawazo yasipokelewe kama mbegu za dhambi. Hebu asiwepo mtu yoyote ambaye anadhani kwamba elimu maana yake ni kusoma vitabu ambayo itapelekea kupokea mawazo ya maandishi watakaopanda mbegu na kuchipua na kuzaa matunda ambayo lazima yafungwe kwenye matita ulimwengu, na kuwatenganisha na Chanzo cha hekima yote, ufanisi wote, na nguvu zote, wakiachwa kuwa mchezo (mwanasesere/toy) wa mdanganyifu mkuu wa Shetani. Elimu safi kwa vijana katika shule zetu, isiyochanganywa na falsafa ya kipagani, ni hitaji chanya katika mistari ya kifasihi. ” {FEsw 387.3}

Ustawi, furaha, maisha ya kidini katika familia ambayo wameunganishwa nayo, ustawi na uchaji wa kanisa ambao wao ni washiriki, unategemea sana elimu ya dini (ya kiroho) ambayo vijana wameipokea katika shule zetu. ” {FEsw 388.1}

— [Special Testimonies on education, Juni 12, 1895.](#)

Kwa Marejeleo ya Ziada

Let your Speech Be with Grace Always Seasoned with Salt, The

Youth's Instructor, June 27, 1895

Our Words, The Youth's Instructor, July 11, 1895

The Child Life of Jesus, The Youth's Instructor, November 21, 1895

Sura ya 46

KITABU KIKUU CHA KUJIFUNZIA

Sanitarium ni uwanja mpana wa kimisionari. Wanafunzi wenu wa utabibu, katika kusoma Neno la Mungu kwa uadilifu, wanakuwa wametayarishwa vyema zaidi kwa masomo mengine yote; kwa maana unyofu na bidii daima huja kwa utafiti wa Neno. Hebu ieleweke na wamishenari wa tiba/matibabu kwamba kwa kadri wanavyomfahamu vyema Mungu na Yesu Kristo ambaye Amemtuma, ndivyo jinsi wanavyoifahamu vyema historia ya Biblia, na ndivyo wanakuwa na sifa bora zaidi za kufanya kazi zao. Wanafunzi katika Chuo cha Battle Creek wanahitaji kuwania/kutamani maarifa ya juu zaidi, na hakuna kinachoweza kuwapa ujuzi wa masomo yote, na akili yenye kuhifadhi kumbukumbu vizuri, kama ilivyo katika kuyachunguza Maandiko. Hebu kuwe na nidhamu ya kweli katika kusoma. Kunapaswa kuwa na unyenyekevu zaidi, maombi yenye hamu ya moyo kuujua Ukweli. " {FEsw 390.1}

Kunapaswa kuwa na waalimu wengi waaminifu, ambao hujitahidi kuwafanya wanafunzi waelewe masomo yao, si kwa kueleza kila kitu wao wenyewe bali kwa kuwaachia wanafunzi waeleze kwa kina kila kifungu ambacho wamesoma. Akili za udadisi za wanafunzi ziheshimiwe. Yaheshimu maswali yao. Kuparaza juu juu tu hakutasaidia kitu. Uchunguzi wa makini na utafiti wa dhati, wenye bidii unaotoza ushuru (unaoshughulisha) unahitajika ili kuwa na ufahamu/kuelewa. Kuna Ukweli katika Neno ambao ni kama mishipa kwenye machimbo ya madini ya thamani yaliyofichwa chini ya ardhi. Kwa kuchimba kwa haya madini, kama vile mwanadamu anavyochimba dhahabu na fedha, hazina zilizofichika zinagunduliwa. Hakikisha

kwamba ushahidi wa Ukweli uko katika Maandiko yenyewe. Andiko moja ni ufunguo wa kufungua Maandiko mengine. Maana ya Maandiko ambayo ni hazina/utajiri uliyofichwa, inafunuliwa na Roho Mtakatifu wa Mungu, Yeye atafanua Neno nalo litkauwa wazi kwenye ufahamu wetu: “Kufafanuliwa kwa maneno Yako hutoa mwanga; humpa ufahamu mjinga.” {FEsw 390.2}

Neno ni kitabu kikuu cha masomo, cha kujifunzia kwa wanafunzi katika shule zetu. Biblia inafundisha mapenzi yote ya Mungu kuhusu wana na binti za Adamu. Biblia ni kanuni ya maisha, inatufundisha tabia ambayo ni lazima tuunde kwa ajili ya maisha yajayo, ya kutokufa. Imani yetu, mtindo wetu wa maisha (utendaji), vinaweza kutufanya kuwa nyaraka hai, zinazojulikana na kusomwa na watu wote. Watu hawahitaji mwanga hafifu wa mila na desturi kuyafanya Maandiko yaeleweke. Kufikiri hivyo, ni kukosa busara, kwani ni kama vile kudhani kwamba jua, linalong'aa Mbinguni wakati wa mchana, linahitaji mwanga wa tochi za watu wanaoishi katika dunia ili kuongeza Utukufu wake. Hekaya au semi za makuhani au ya wahudumu, hazihitajiki kumwokoza mwanafunzi kutoka kwenye makosa ya kutafsiri Maandiko. Pata ushauri kutoka kwenye Neno la Mungu, nawe utapata mwanga. Katika Biblia kila jukumu linawekwa wazi, kila somo linaeleweka, linaweza kuwastahilisha watu kufaa kwa maandalizi ya uzima wa milele. Zawadi ya Kristo na Nuru ya Roho Mtakatifu inatufunulia sisi kuhusu Baba na Mwana. Neno limewekwa na Mungu kwa namna ambayo itawahekimisha wanaume na wanawake na vijana wenye hekima hadi kufikia wokovu. Katika Neno, sayansi ya wokovu imefunuliwa wazi wazi. “Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema..” “Yachunguzeni Maandiko,” kwa kuwa ndani yake yamo shauri la Mungu, sauti ya Mungu inanena na nafsi. {FEsw 390.3}

— [Special Testimonies on Education Desemba 1, 1895.](#)

Sura ya 47

ELIMU YA JUU

Neno "elimu ya juu" linapaswa kuzingatiwa kwa mwanga kutokana na kile ambacho kimetazamwa na wanafunzi wa sayansi. Sala ya Kristo kwa Baba Yake imejaa Ukweli wa milele. "Maneno hayo aliyasema Yesu; akainua macho Yake kuelekea Mbinguni, akasema, Baba, saa imekwisha kufika. Mtukuze Mwanao, ili Mwana wako naye akutukuze wewe; kama vile ulivyompa mamlaka juu ya wote wenye mwili, ili kwamba wote uliomba awape uzima wa milele. Na uzima wa milele ndio huu, Wakujue Wewe, Mungu wa pekee wa Kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma." "Kwa kuwa Yeye aliyetumwa na Mungu huyanena Mmaneno ya Mungu; kwa sababu hamtoi Roho kwa kipimo. Baba ampenda Mwana, Naye amempa vyote mkononi Mwake. Amwaminiye Mwana yuna uzima wa milele; asiyemwamini Mwana hataona uzima, bali ghadhabu ya Mungu inamkalia." Nguvu na Roho ya elimu ya Kweli ni a ujuzi wa Mungu, na Yesu Kristo ambaye amemtuma. "Kumcha Bwana ni mwanzo wa hekima." {FEsw 392.1}

Imeandikwa hivi kumhusu Yesu: "Yule mtoto akakua, akaongezeka nguvu, amejaa hekima, na neema ya Mungu ilikuwa juu Yake.... Naye Yesu akazidi kukua katika hekima na kimo, akimpendeza Mungu na mwanadamu." Ujuzi wa Mungu utaunda aina ya maarifa ambayo yatadumu hata umilele. Kujifunza na kufanya kazi ya Kristo, ni kupata elimu ya Kweli. Ingawa Roho Mtakatifu aliifanya kazi nia ya Kristo, ili aweze kuwaambia wazazi Wake, "Akawaambia, Kwani kunitafuta? Hamkujua ya kuwa imenipasa kuwamo katika nyumba ya Baba Yangu?" bali aliendelea kufanya kazi ya useremala kama mwana mtiifu. Alifunua kwamba alikuwa na ujuzi wa kazi Yake kama Mwana wa Mungu, na bado hakuitukuza tabia Yake ya asili ya Kiungu. Hakutoa sababu kwanini Yeye abebe mzigo wa masumbufu ya kazi ambazo ni za muda mfupi, kwamba Yeye alikuwa na asili ya

Uungu; lakini alikuwa chini ya uongozi wa wazazi Wake. Yeye alikuwa Bwana wa Amri, lakini alikuwa mtiifu kwa amri zao zote mahitaji, na hivyo basi kutuachia mfano wa utii katika utoto, ujana, na utu uzima. {FEsw 392.1}

Ikiwa nia na akili imewekwa kwenye kazi ya kusoma Biblia ili kupata habari/maarifa, uwezo wa kufikiri utaboreshwa. Chini ya kusoma Maandiko, akili hupanuka, na kuwa na usawa zaidi kuliko pale inaposhughulishwa katika kupata taarifa za jumla kutoka kwenye vitabu ambavyo havina uhusiano wowote na Biblia. Hakuna maarifa yaliyo thabiti, yasiyopindapinda, na yanayofika mbali, kama yale yanayopatikana kutokana na utafiti ya Neno la Mungu. Ni msingi wa maarifa yote ya Kweli. Biblia ni kama chemchemi. Kadiri unavyoitazama, ndivyo inavyozidi kuonekana kuwa na kina zaidi. Kweli kuu za historia takatifu zina nguvu za ajabu na uzuri, na zinafikia mbali hata umilele. Hakuna sayansi inayolingana na sayansi inayofunua tabia ya Mungu. Musa alielimishwa katika hekima yote ya Wamisri, lakini akasema, "Angalieni nimewafundisha amri na hukumu, vile vile kama Bwana, Mungu wangu, alivyoni amuru, ili mazitende katika nchi mwingiayo ili kuimiliki. Zishikeni basi, mkazitende, maana hii ndiyo hekima yenu na akili zenu, machoni pa mataifa watakozisikia amri hizi zote, nao watasema, Hakika taifa hili kubwa ni watu wenye hekima na akili. Kwa maana liko taifa gani kubwa, lililo na Mungu aliye karibu nao, kama Bwana, Mungu wetu, alivyo, kila tumwitapo? Tena liko taifa gani kubwa, lililo na amri na hukumu zenye haki kama torati hii yote, ninayoiweka mbele yenu leo. Lakini, jihadhari nafsi yako, ukailinde Roho yako kwa bidii, usije ukayasahau mambo yale uliyoyaona kwa macho yako, yakaondoka moyoni mwako siku zote za maisha yako; bali uwajulishe watoto wako na watoto wa watoto wako." {FEsw 393.1}

Tutapata wapi sheria bora zaidi, safi, na za haki kuliko zile zilizoonyeshwa kwenye vitabu vya sheria ambavyo kumbukumbu ya maagizo/mwongozi iliandikwa na kupewa Musa kwa ajili ya wana wa Israeli? Katika vizazi vyote sheria hizi zinapaswa kudumishwa milele, ili tabia ya watu wa Mungu iweze kuundwa kwa mfano wa Wake Mwenyewe (mfano wa Mungu). Sheria ni ukuta wa ulinzi kwa wale wanaotii amri za Mungu. Kutoka kwa chanzo gani kingine tunaweza kukusanya nguvu kama hizo, au kujifunza sayansi bora kama hiyo? Ni kitabu kipi kingine ambacho kitawafundisha watu kumpenda, kumcha, na kumtii Mungu kama Biblia inavyofanya? Ni Kitabu kipi kingine, kinachowasilisha kwa wanafunzi sayansi inayoinua zaidi, na ya ajabu zaidi? Inaonyesha wazi haki, na inatabiri matokeo ya kukosa uadilifu kwa sheria ya Yehova. Hakuna mtu anayeachwa katika giza kuhusu yale ambayo Mungu anayakubali au kuyakataa. Katika kusoma Maandiko tunafahamiana na Mungu, na tunaongozwa kuelewa uhusiano kati yetu na Kristo, ambaye Ndiye mbeba/mchukua-dhambi na mdhamini, wa jamii yetu iliyoanguka. {FEsw 393.2}

Ukweli huu unahusu maslahi yetu ya sasa na hata ya milele. Biblia inasimama

juu zaidi miongoni mwa vitabu zaidi, na kujifunza hii ni muhimu zaidi ya masomo ya machapisho mengine katika kuipa nguvu na upanuzi akili. Paul anasema: “Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari, ukitumia kwa halali Neno la Kweli.” “Bali wewe ukae katika mambo yale uliyofundishwa na kuhakikishwa, kwa maana unajua ni akina nani ambao ulijifunza kwao; na ya kuwa tangu utoto umeyajua maandiko matakatifu, ambayo yaweza kukuhekimisha hata upate wokovu kwa imani iliyo katika Kristo Yesu. Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema.” “Kwa kuwa yote yaliyotangulia kuandikwa yaliandikwa ili kutufundisha sisi; ili kwa saburi na faraja ya Maandiko tupate kuwa na tumaini.”

Neno la Mungu ni kitabu cha elimu kilicho kikamilifu zaidi katika dunia yetu. Japo katika vyuo na shule zetu, vitabu vinavyozalishwa na akili ya binadamu vimewasilishwa kama kipaumbele kwa ajili ya wanafunzi wetu kusoma, na Kitabu cha vitabu, ambacho Mungu amewapa wanadamu ili kiwe mwongozo usio na makosa, kimefanywa kuwa jambo la pili. Uzalishaji wa machapisho ya binadamu umefanywa kuwa muhimu zaidi, na Neno la Mungu, limesomwa ili kuongezea ladha kwa masomo mengine (namba mbili). Isaya anaeleza matukio ya Mbinguni yenye Utukufu ambayo yaliwasilishwa kwake, kwa lugha ya wazi kabisa. Kwenye kitabu chote anatoa picha ya mambo matukufu ambayo yanapaswa kufunuliwa kwa wengine. **Ezekieli** anaandika hivi: “Neno la Bwana lilimjia Ezekieli, kuhani, mwana wa Buzi, kwa dhahiri, katika nchi ya Wakaldayo, karibu na mto Kebari; na mkono wa Bwana ulikuwa hapo juu yake. Nikaona, na tazama, upepo wa dhoruba ulitoka upande wa kaskazini, wingu kubwa sana, pamoja na moto, ukifanya duara ya Nuru, na mwangaza pande zote, na katikati yake kitu kama rangi ya kaharabu, katikati ya moto huo. Kukatokea katikati yake mfano wa viumbe hai vinne. Kuonekana kwao kulikuwa hivi; walikuwa na sura ya mwanadamu. Na kila mmoja alikuwa na nyuso nne, na kila mmoja alikuwa na mabawa manne. Na miguu yao ilikuwa miguu iliyonyoka; na nyayo za miguu yao zilikuwa kama nyayo za miguu ya ndama; zikimetameta kama rangi ya shaba iliyosuguliwa sana. Nao walikuwa na mikono ya mwanadamu chini ya mabawa yao, pande zote nne; na wote wanne walikuwa na nyuso zao na mabawa yao hivi; mabawa yao yaliungana, hili na hili; nao hawakugeuka walipokwenda, walikwenda kila mmoja kuelekea mbele. Kwa habari za mfano wa nyuso zao; walikuwa na uso wa mwanadamu; na hao wanne walikuwa na uso wa simba upande wa kuume; na hao wanne walikuwa na uso wa ng'ombe upande wa kushoto; na hao wanne walikuwa na uso wa tai pia.” Kitabu cha Ezekieli kinafundisha sana. {FEsw 394.1}

Biblia imekusudiwa na Mungu kuwa kitabu ambacho kwa kwacho ufahamu unaweza kutiwa nidhamu, nafsi kuongozwa na kuelekezwa. Kuishi katika ulimwengu bila ya kuwa wa ulimwengu, ni shida ambayo wengi wanaojiita

Wakristo hawajawahi kulifanyia kazi jambo hili katika maisha yao ya vitendo (mtindo wa maisha). Ukuaji wa akili utakuja kwa taifa kadiri watu wanavyorudi kwenye uaminifu wao kwa Mungu. Ulimwengu umejaa vitabu vya habari za jumla, na watu hutumia akili zao katika kutafuta historia zisizovuviwa; lakini wanapuuzia kitabu cha ajabu sana ambacho kinaweza kuwapa wao mawazo sahihi zaidi na uelewaji wa tosha. {FEsw 395.1}— [The Review na Herald, FEswbruari 25, 1896.](#)

Sura ya 58

MWALIMU WA KIMBINGU-MWALIMU WA MBINGUNI

Wale wanaojifunza kila siku juu ya Yesu Kristo wanastahilishwa kuchukua nafasi zao kama watenda kazi pamoja na Mungu, na haijalishi taaluma, stadi au shughuli yao ni nini, wao wanaweza kufanya jitihada kupitia nguvu zao, yaani kwa kushinikiza nguvu walizopewa na Mungu kulingana na mfano wa tabia ya Kristo wakati alipokuwa akiishi katika mwili. Vijana na watoto watabeba ushawishi wao ule waliopokea kwenye maisha yao ya nyumbani na katika elimu ya shule. Mungu anawawajibisha waalimu katika kazi zao kama waelimishaji. Lazima wajifunze kila siku katika shule ya Kristo, ili kuwainua vijana ambao wamekuwa na ulegevu wa mafunzo nyumbani, ambao hawajaunda tabia za kujifunza/kujisomea, ambao wana ujuzi mdogo wa maisha ya baadaye ya umilele {kutokufa}, ambayo ni ya thamani ya juu zaidi, yaliyolipiwa na Mungu wa Mbinguni kwa kumtoa Mwanawe wa pekee kuishi maisha ya kudhalilishwa na kufa kifo cha aibu zaidi, “ili kila amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.” {FEsw 397.1}

Mungu ametupa rehema ambayo kwayo tunaweza kujiandaa kwa shule iliyo ya juu zaidi. Katika shule hii vijana wanapaswa kuelimishwa, kunidhamishwa, na kufunzwa ili kuunda tabia, za kimaadili na kiakili, kwa namna ile ambayo Mungu

ataikubali. Wanapaswa kupokea mafunzo, si katika desturi na burudani na michezo ya jamii hii yenye uchafuzi wa maadili hapa duniani, bali katika mistari ya Kristo, mafunzo ambayo yatawafaa kuwa watenda kazi pamoja na akili za Mbinguni. Lakini itakuwa ni kichekesho cha namna gani, kama ile elimu inayopatikana katika vitabu, itakuwa lazima ingolewe kutoka kwa mwanafunzi, kama itabidi astahilishwe kuingia katika maisha yale yenye kipimo kinachoendana na maisha ya Mungu (milele), yeye mwenyewe ataokolewa kama kijinga kutoka kwa moto (ataponea chupuchupu) (Zek 3:2). *(Huko nyuma katika siku za maandishi haya, hasa katika miaka ya awali, elimu yao ilikuwa pamoja na misingi ya kitamaduni: Kilatini, falsafa, sarufi ya hali ya juu na kwa muda, Chuo cha Battle Cree hakikutoa hata darasa la Biblia! Kwa hiyo hilo ndilo analopinga—elimu ya kilimwengu ambayo haitegemei kujifunza Maandiko kama jambo la kwanza.)* {FEsw 397.2}

Hapo awali, elimu ilihusisha kushindilia akili kwa kujikulemea akili za wanafunzi na mizigo mizito ya matini au masomo ambayo hayawezi kuwa ya thamani hata kidogo kwao, na ambayo hayakutambuliwa katika shule ya upili. Walimu wa taifa la Kiyahudi walidai kuwaelimisha vijana kuelewa usafi na ubora wa sheria za ufalme ule ambao utasimama milele na milele, lakini waliipotosha Haki na usafi wa moyo. Ingawa walisema wenyewe, “Hekalu la Bwana, hekalu la Bwana ni sisi,” hata hivyo walimsulubisha Mwanzilishi wa uchumi wote wa Kiyahudi, Yeye ambaye sheria na alama zao zote za mifano zilielekeza Kwake (pasaka etc). Walishindwa kupambanua siri na fumbo lililofunikwa la utauwa; Kristo Yesu alibaki amefichwa kwao. Ukweli, uzima, moyo wao wote wa huduma, vilitupiliwa mbali. Walishikilia, na bado wanashikilia (taratibu hizo), mabua matupu tu, vivuli, vielelezo vinavyoashiria Ukweli (ila siyo Ukweli wenyewe). Vielelezo ambayo hukuo awali viliwekwa kwa wakati uliomariwa, ili wapate kutambua ile Kweli, ila ile Kweli ikapotoshwa sana kwa mavumbuzi yao wenyewe, hadi macho yao yakapofushwa. Hawakutambua kwamba Mfano (type) ulikuwa umekutana na Halisi (antitype) katika kifo cha Yesu Kristo. Kwa kadri upotovu wao ulivyokuwa mkubwa wa mifano, alama, takwimu na vielelezo, ndivyo walizidi kuchanganyikiwa akilini mwao, ili wasiweze kuona utimilifu mkamilifu wa uchumi wa Kiyahudi, ulioanzishwa na Kristo, na vikimwonyesha Yeye kama Ndiye Haswa, yaani Ndiye Halisi na si kivuli au kafara ya wanyama (substance). Nyama na vinywaji na taratibu au sherehe na maadhimsho vilizidishwa idadi na aina, hadi dini ya sherehe ikawa ndiyo ibada yao pekee (wakawa katika kuadhimisha mambo yaliyopitwa na wakati kama kuchinja dhabihu na yanayohusiana na hayo, mbadala Halisi aliyekuja kama Mwana-Kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya Ulimwengu). {FEsw 397.3}

Katika mafundisho Yake, Kristo alitaka kuwaelimisha na kuwafundisha Wayahudi kuona lengo la kile ambacho kilipaswa kukomeshwa na toleo la Kweli la Dhabihu Yake Yeye Mwenyewe, iliyo hai. “Nendeni,” Yeye alisema, “mkajifunze nini maana yake, nataka rehema wala si sadaka.” Aliwasilisha tabia safi kama ndiyo yenye umuhimu mkuu. Aliachana na fahari yote, na taratibu zenye maonyesho

mengi, akidai kwamba imani itendayo kazi kwa upendo na kutakasa Roho; kama ndiyo sifa pekee inayohitajika kwa ufalme wa Mbinguni. Yeye alifundisha kwamba dini ya Kweli haijumuishi taratibu, desturi au sherehe, vivutio vya nje au maonyesho ya nje. Kristo angeyachukua na kuyatenda haya Yeye Mwenyewe endapo yalikuwa muhimu katika uundaji wa tabia inayoendana na Mfano wa kimbingu/Bwana. Lakini uraia au wenyeji Wake, mamlaka ya Uungu Wake, yalitegemea sifa Zake za asili. Yeye, Mkuu wa Mbinguni, alitembea duniani, akiwa amevikwa vazi la ubinadamu. Mivuto Yake yote na ushindi vilikuwa vifunuliwe kwa ajili ya mwanadamu, na vilipaswa kushuhudia uhusiano Wake ulio hai na Mungu.

{FEsw 398.1}

Utabiri wa Kristo kuhusu uharibifu wa hekalu, ulikuwa somo la utakaso wa dini, na kutangua desturi, na maadhimisho/sherehe. Alijitangaza kuwa Yeye ni Mkuu kuliko hekalu, na akasimama akihubiri kuwa, “Mimi Ndimi njia, na Kweli, na uzima.” Yeye Ndiye ambaye ndani Yake sherehe zote za Kiyahudi na huduma ya Mfano ilimwakilisha na sasa ilikuwa imepata utimilifu Wake (Yeye Ndiye alikuwa kafara mara moja tu kwa ajili ya wakati wote **Warumi 6:9**). Yeye alisimama badala au mahali pa hekalu; ofisi zote za kanisa zilijikita ndani Yake Yeye peke yake. {FEsw

399.1}

Hapo zamani, watu walimfikia Kristo kwa njia ya maumbo, taratibu na sherehe, lakini sasa Alikuwa duniani, akiita usikivu wa moja kwa moja Kwake Mwenyewe, akiuwakilisha ukuhani wa kiroho, na akimweka mwanadamu mwenye dhambi kwenye Kiti cha Rehema (akimweka wakala wa kibinadamu Kwenye Kiti cha Rehema). “Ombeni, nanyi mtapewa,” Aliahidi; “tafuteni, nanyi mtapata; Bisheni, nanyi mtafunguliwa.” “Nanyi mkiomba lolote kwa Jina Langu, hilo nitalifanya, ili Baba atukuzwe ndani ya Mwana. Mkiniomba neno lolote kwa Jina Langu, nitalifanya. Mkinipenda, mtazishika amri Zangu.” “Yeye aliye na amri Zangu, na kuzishika, yeye ndiye anipendaye; **naye anipendaye atapendwa na Baba Yangu**; Nami nitampenda na kujidhihirisha kwake.” “Nanyi mkiomba lolote kwa Jina Langu, hilo nitalifanya, ili Baba atukuzwe ndani ya Mwana. Mkiniomba neno lo lote kwa Jina Langu, nitalifanya. Mkinipenda, mtazishika amri Zangu..” {FEsw 399.2}

Masomo haya Kristo alitoa katika mafundisho Yake, akionyesha kwamba desturi ya ibada ilikuwa inaenda kupita wakati wake, na haikuwa na fadhila au jema lolote. “saa inakuja,” Yeye alisema, “Lakini saa inakuja, nayo sasa ipo, ambayo waabuduo halisi watamwabudu Baba katika Roho na Kweli. Kwa maana Baba awatafuta watu kama hao wamwabudu. Mungu ni Roho, nao wamwabuduo Yeye imewapasa kumwabudu katika Roho na Kweli..” Tohara ya Kweli ni kumwabudu Kristo katika Roho na Kweli, na sio kwa namna ya desturi na taratibu, kwa kujifanya na unafiki (feki). {FEsw 399.3}

Hitaji kubwa la mwanadamu kwa mwalimu wa Kiungu lilijulikana Mbinguni. Huruma na sikitiko la Mungu lilitokelezwa kwa niaba ya mwanadamu, aliyeanguka

na kufungwa kwenye gari la farasi la Shetani; na wakati wa utimilifu ulipokuwa umewadia, Mungu akamtuma Mwanawe. Yule aliyeteuliwa/alijehusika kushiriki kwenye mashauri ya Mbinguni alikuja duniani kama mwalimu. Yeye hakuwa pungufu kuliko Muumba wa ulimwengu, Mwana wa Mungu Asiye na mwisho. Ukarimu uliosheheni wa Mungu ulitupatia Yesu kwa ulimwengu wetu; na ili kukidhi mahitaji ya ubinadamu, Alichukua juu Yake asili ya kibinadamu. Kwa mshangao wa jeshi la Mbinguni, Alitembea duniani kama Neno la Milele. Akiwa amejitayarisha kikamilifu, Aliondoka katika nyua za kifalme na kuja kwenye ulimwengu uliokuwa umeharibiwa na kuchafuliwa na dhambi. Alijijhusisha na kuambatana Mwenyewe kwa asili ya mwanadamu kwa namna ya ajabu. “Neno alifanyika mwili, Naye akakaa kwetu.” Bubujiko linalofurika la **wema** wa Mungu, **ukarimu**, na **upendo** ulioleta mshangao kwa ulimwengu, kuhusu **neema** ambayo inaweza kupatikana, lakini ilikuwa bado kuelezwa. (sifa hizi zilikuwa bado hazijaelezewa). {FEsw 399.4}

Ili Kristo, wakati wa utoto Wake, akue katika hekima, na kumpendeza Mungu na mwanadamu, halikuwa jambo la kushangaza; kwani ilikuwa kulingana na sheria za uteuzi Wake wa Kiungu kwamba talanta Zake zilipaswa kukuzwa, na uwezo Wake uimarishwe kwa mazoezi. Hakutafuta mafunzo Yake kwenye shule za manabii wala kutoka kwa Walimu walioitwa marabi; Hakuhitaji elimu iliyopatikana katika shule hizi; kwa maana Mungu alikuwa Mwalimu Wake. Wakati alipokuwa mbele ya waalimu na watawala. Maswali Yake yalikuwa na Masomo ya kujifunza, Naye aliwashangaza watu wakuu kwa hekima Yake na ilivyopenya kwa kina. Majibu yake kwa maswali yao, yalifungua uwanja wa mawazo juu ya masomo yaliyorejelea utume wa Kristo, ambayo hayakuwahi kuingia akilini mwao. {FEsw 400.1}

Ghala ya hekima na maarifa ya kisayansi ambayo Kristo alionyesha mbele ya wale watu wenye hekima (mamajusi), vilikuwa jambo la mshangao kwa wazazi Wake na ndugu Zake; kwa maana walijua kuwa hakuwahi kupokea mafundisho kutoka kwa walimu wakuu katika sayansi ya binadamu. Ndugu Zake walikerwa na maswali na majibu Yake; kwa maana wa kung’amua kwamba alikuwa Mkufunzi kwa hawa walimu wasomi. Hawakuweza kuwa na ufahamu wa kile alichokuwa anakifanya (hawakumwelewa); kwa maana hawakujua ya kuwa Yeye anaweza kuufikia ule mti wa uzima, chanzo cha maarifa ambayo hawakujua lolote kuhusu hayo. Daima alikuwa na hadhi ya kipekee na (upekee) uliokuwa tofauti na kiburi cha kidunia au dhana; kwani hakujitaidi kuwania ukuu. {FEsw 400.2}

Baada ya Kristo kujishusha kuja duniani na kuacha kuwa Kamanda Mkuu, na kuchukua hatua ya kushuka chini kutoka urefu usio na kikomo na kuuvaa ubinadamu, Angeweza kuchagua kuchukua juu Yake hali yoyote ya ubinadamu (tajiri, kiongozi nk). Lakini ukuu na cheo havikuwa jambo la maana Kwake, na Akachagua maisha ya chini kabisa, ya unyenyekevu na duni zaidi. Mahali pa kuzaliwa Kwake palikuwa Bethlehemu, na upande mmoja wa **mzazi** Wake ulikuwa

duni (mama), lakini Mwenyezi Mungu, Mmiliki wa ulimwengu, alikuwa Baba Yake. Hakuna athari ya starehe, uvivu, urahisi wa maisha, kuridhisha ubinafsi, anasa, kujiendekeza au kujifurahisha Mwenyewe, kuliletwa katika maisha Yake, ambayo yalikuwa ni duru ya kudumu katika kujikana nafsi na kujinyima. Kwa mujibu wa mazingira ya unyenyekevu aliyozaliwa kwayo, Hakuwa na ukuu wala utajiri uliokuwa unaonekana, ili kwamba mwamini mnyenyekevu au duni zaidi asihitaji kusema kwamba Kristo hakuwahi kujua shida au msongo wa umasikini unaomfinya mtu. Lau angekuwa na mwonekano wa nje wa utajiri, au wa ukuu, tabaka maskini zaidi la ubinadamu lingekwepa kushirikiana Naye; kwa hiyo alichagua hali iliyokuwa duni, kupita watu wengi walioishi siku hizo. Ukweli wa asili ya Mbinguni ilipaswa kuwa mada Yake: Alipaswa kupanda mbegu ya ile Kweli duniani; na Yeye alikuja kwa njia ambayo angeweza kufikiwa na wote (kila mtu angeweza kumpata), Ili tu ile Kweli peke yake, ndiyo ingeweza kuleta hisia kwenye mioyo ya wanadamu. {FEsw 401.1}

Kuridhika/kutosheka kwa Kristo katika nafasi yoyote kuliwaudhi ndugu Zake. Hawakuweza kueleza sababu ya amani na utulivu Wake; na hakuna ushawishi wao ambao ungeweza kumfanya aingie katika mipango yoyote ambayo ilikuwa na hisia ya kawaida au ya hatia. Katika kila tukio ambalo angejipusha nalo wakiwa pamoja, aliwaelezea waziwazi kwamba ilibidi afanye hivyo kwani wangewapotosha wengine, na hawakustahili kuwa wana wa Ibrahimu. Ni lazima aliweka mfano wa kipekee, kwani hata watoto wadogo, washiriki wachanga wa familia ya Bwana, hawakuona chochote katika maisha Yake au tabia ya kilichohalalisha tendo lolote baya. **Umejikita kwenye jambo moja, yaani umezingatia mno tabia yako hiyo ambayo inakutofautisha na wenzako, na kukufanya uwe wa kipekee**, walisema washiriki wa familia Yake Mwenyewe. Kwa nini usiwe kama watoto wengine? Lakini hii hakuwezekana; kwa maana Kristo alipaswa kuwa ishara na ajabu tokea ujana Wake, kwa kadiri utifu mkali na uadilifu ulivyoweza kuhusika. {FEsw 401.2}

Daima alikuwa mkarimu, mwungwana, mwenye kujistahi, mwenye adabu, anakikaa kwenye nafasi ya yule aliyedhulumiwa, awe Myahudi au Myunani, Kristo alipendwa na wote. Kwa ukamilifu maisha na tabia Yake, Alijibu swali lililoulizwa kwa kurejelea Zaburi ya kumi na tanoi: “Bwana, ni nani atakayekaa katika hema Yako? Ni nani atakayefanya maskani yake Katika kilima Chako kitakatifu? Ni yeye aendaye kwa ukamilifu na kutenda haki; na kusema kweli moyoni mwake.” Katika utoto na ujana Wake mwenendo Wake ulikuwa hivi kwamba alipokuwa akifanya kazi kama Mwalimu, Angeweza kuwaambia wanafunzi Wake, “Mkizishika amri Zangu, mtakaa katika pendo Langu: kama vile Mimi nilivyoizishika amri za Baba Yangu, na kukaa katika pendo Lake.” {FEsw 402.1}

Kadri Kristo alivyoendelea kukua na kuwa mtu mzima, kazi iliyoanza katika utoto Wake iliendelea, Naye akazidi kuongezeka katika hekima, na kumpendeza Mungu na mwanadamu. Hakuchukua sehemu ya familia Yake Mwenyewe kwa sababu tu walihusiana Naye kwa mahusiano ya asili au ya damu; Hakuwatetea katika kesi yao

hata moja, wakati walipokuwa na hatia ya ukosefu wa haki au kufanya makosa; ila daima alitetea au kuthibitisha tu kile alichojua kuwa ni Ukweli. {FEsw 402.2}

Kristo alijituma kwa juhudi katika kujifunza Maandiko; kwa kuwa alijua yalikuwa yamejaa mafundisho yenye thamani kwa wote watakayoyafanya kuwa mshauri wao. Alikuwa mwaminifu katika utekelezaji Wake kazi za nyumbani, na saa za asubuhi, badala ya kupotezwa kitandani (kwa kujigaragaza humo), mara nyingi yalimkuta mahali penye utulivu mbali na watu, akitafakari na kuchunguza Maandiko na katika maombi. Kila unabii kuhusu kazi Yake na upatanishi ilijulikana Kwake, hasa zile mada na kumbukumbu kwa kudhiliwa Kwake, mateso Yake, upatanisho, na maombezi Yake. Katika utoto na ujana, lengo la maisha Yake lilikuwa mbele Yake daima, kichocheo Chake kikuu kikiwa. kuchukua kazi ya upatanishi kwa niaba ya mwanadamu aliyeanguka. Angeona uzao Wake, ambao ungeishi siku nyingi, na kusudi la Bwana la neema litafanikiwa mikononi Mwake (Isaya 53:10). {FEsw 402.3}

“Basi na sisi pia, kwa kuwa tunazungukwa na wingu kubwa la mashahidi namna hii, na tuweke kando kila mzigo mzito, na dhambi ile ituzingayo kwa upesi; na tupige mbio kwa saburi katika yale mashindano yaliyowekwa mbele yetu, tukimtazama Yesu, Mwenye kuanzisha na mwenyekutimiza imani yetu; ambaye kwa ajili ya furaha iliyowekwa mbele Yake aliustahimili msalaba na kuidharau aibu, Naye ameketi mkono wa kuume wa kiti cha enzi cha Mungu.” Mada hizi Kristo alijifunza katika ujana Wake, na ulimwengu wa mbingu ulimtazama kwa shauku Yule ambaye kwa furaha hiyo iliyowekwa mbele Yake aliustahimili msalaba, na kuidharau aibu. Kwa kujitoa Mwenyewe kufanya maombezi kwa ajili ya uasi wa jamii ya mwanadamu, Kristo alitekeleza ofisi ya ukuhani. Kama malipo, alikuwa aone ya taabu ya nafsi Yake, na kuridhika. Uzao Wake ulipaswa kuzirefusha siku zao duniani milele. “Waheshimu baba yako na mama yako; ili siku zako zipate kuwa nyingi katika nchi upewayo na Bwana, Mungu wako.” Kwa utiifu wake kwa baba na mama Yake, Kristo alikuwa mfano kwa watoto na vijana wote; lakini leo watoto hawafuati mfano alioutoa, na matokeo ya hakika yatakuwa kufupisha siku zao. {FEsw 402.4}

“Atukuzwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye ametubariki kwa baraka zote za kiroho katika ulimwengu wa Roho Ndani Yake Kristo: kama vile alivyotuchagua katika Yeye kabla ya kuwekwa misingi wa ulimwengu, ili tuwe watakatifu na bila lawama mbele Zake katika upendo: alitangulia kutuchagua ili tufanywe wana kwa njia Yake Yesu Kristo Kwake Mwenyewe, kulingana na uradhi wa mapenzi Yake.” Kabla ya kuwekwa misingi ya dunia, agano lilifanywa kwamba wote waliokuwa watii, wote kupitia wingi wa neema iliyotolewa, watakuwa watakatifu wa tabia, na bila lawama mbele za Mungu, kwa kuipokea na kuidhinisha neema hiyo, wanakuwa watoto wa Mungu. Ibrahimu alipewa, Agano hili, lililofanywa tangu milele, mamia ya miaka kabla ya Kristo kuja. Ni kwa shauku na msukumo wa kiasi gani, Kristo wakati akiwa binadamu, alichunguza na kusomea jamii ya

wanadamu ili kuona kama wangejitoa na kukubali wenyewe, na kuwa tayari kupokea utoaji huu ulioofa (dhabihu Yake). {FEsw 403.1}

“Na Huu ndio uzima wa milele, wakujue Wewe, Mungu wa pekee na wa Kweli , na Yesu Kristo uliyemtuma.” Maneno haya ni kifungua macho kwa wote watakaona/watakaoyaona. Ujuzi wa Mungu ni maarifa ambayo hayatahitaji kuachwa nyuma wakati wa mlango wetu wa rehema kufungwa, elimu ambayo ni ya manufaa ya kudumu kwa ulimwengu na kwetu sisi binafsi. Kwa nini, basi, tuliweke Neno la Mungu Mwalimu wa Mbinguni nyuma, wakati ni hekima iletayo wokovu. “Kwa hiyo imetupasa kuyaangalia zaidi hayo yaliyosikiwa tusije tukayakosa. Kwa maana, ikiwa lile Neno lililonenwa na malaika lilikuwa imara, na kila kosa na uasi ulipata ujira wa haki, sisi je! Tutapataje kupona, tusipojali wokovu mkuu namna hii? Ambao kwanza ulinenwa na Bwana, kisha ukathibitika kwetu na wale waliosikia.” Tukiwapa waandishi ambao wana wazo lililochanganyikiwa kuhusu nini maana ya dini, jukwaa lililo juu na linaloonekana, na heshima yote na kuifanya Biblia kuwa ya pili basi tunapuuzia wokovu wetu. Wale ambao wameangaziwa kuhusiana na Kweli ya siku hizi za mwisho, hawatapata mwongozo ndani ya vitabu vinavyosomwa kwa ujumla leo kuhusiana na mambo yanayoujia ulimwengu wetu; lakini Biblia imejaa maarifa ya Mungu, na ina uwezo uliobobea katika kumwelimisha mwanafunzi kwa manufaa katika maisha haya ya duniani na kisha uzima wa milele. {FEsw 403.2}

Jifunze kwa makini sura ya kwanza ya Waebrania. Uwe na hamu katika Maandiko. Yasome na ujifunze kwa bidii. “Katika hayo ninyi mnadhani mna uzima wa milele,” Kristo alisema, “na hayo ndiyo hunishuhudia Mimi.” Inamaanisha kila kitu kwetu kuhusu kuwa na uzoefu na ujuzi binafsi juu ya Mungu na Yesu Kristo, “aliyemtuma.” “Kwa maana uzima wa milele ndio huu, wakujue Wewe Mungu wa pekee wa Kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma.” {FEsw 404.1} — *Special Testimonies on Education, Machi 23, 1896.*

ELIMU YA KWELI

“Kufafanusha Maneno Yako kwatia Nuru; na kumfahamisha mjinga,” kwa wale wasiojiweza, lakini ambao wana utayari wa kujifunza. Je, kazi ya mjumbe wa Mungu katika dunia yetu, ilikuwa nini? Mwana wa pekee wa Mungu aliuvisha Uungu Wake kwa ubinadamu, na akaja katika ulimwengu wetu kama Mwalimu, Kiongozi Mwelekezi, kuufunua Ukweli, na kuutofautisha na makosa. Ukweli, Ukweli unaoorkoa, haukuwahi kupungua nguvu kwenye ulimi Wake, kamwe Ukweli haukuteswa mikononi Mwake, bali ulifanywa kusimama wazi na kuelezewa kwa uwazi katikati ya giza la kimaadili linalotawala katika ulimwengu wetu. Ni kwa kazi hii ndiyo Yeye aliacha nyua za Mbinguni. Alisema Mwenyewe kwamba, “Kwa ajili ya haya nalikuja ulimwenguni ili niishuhudie Kweli.” Ukweli ulitoka katika midomo Yake kwa uchangamfu na nguvu, kama ufunuo mpya. Alikuwa Njia, Kweli na Uzima. Uhai Wake, uliotolewa kwa ajili ya ulimwengu huu wenye dhambi, ulikuwa umejaa unyofu, bidii, usadikisho na matokeo muhimu kwa siku zilizokuwa zinakuja; kwa kuwa kazi Yake ilikuwa kuorkoa Roho zinazoangamia. Yeye alikuja kuwa Nuru ya Kweli, inayoangaza katikati ya giza la maadili ya ushirikina na uovu, na ilitangazwa kwa sauti kutoka Mbinguni juu, ikisema, “Huyu ni Mwanangu, mpendwa Wangu, ninayependezwa Naye.” Na katika kugeuka Kwake sauti hii kutoka Mbinguni ikasikika tena. “Huyu ni Mwanangu, mpendwa Wangu, ninayependezwa Naye; msikieni Yeye.” {FEsw 405.1}

“Kwa maana Musa kweli alisema ya kwamba, Bwana Mungu wenu atawainulieni nabii miongoni mwa ndugu zenu kama Mimi; msikilizeni Yeye katika yote atakayowaambia. Na itakuwa kwamba kila mtu ambaye hatamsikia Nabii huyo ataangamizwa na kutengwa na watu wake.” Kristo alileta katika ulimwengu wetu maarifa fulani ya Mungu, na kwa wote waliompokea na kutii Neno Lake, aliwapa uwezo wa kufanyika wana wa Mungu. Yeye ambaye alikuja kutoka kwa Mungu kwa ajili ya ulimwengu wetu huu, alitoa maelekezo juu ya kila somo ambalo ni muhimu kwa mwanadamu, kila analopaswa kujua ili kuweza kuipata njia ya kwenda Mbinguni. Kwake Yeye, Ukweli ulikuwepo ndani Yake daima, Ukweli unaojidhihirisha wenyewe; Hakusema mapendekezo yoyote, wala hisia za hali ya juu, mawazo, au maoni, bali aliwasilisha tu Ukweli thabiti, ule unaoorkoa. {FEsw 405.2}

Kila kitu kisichoeleweka katika Ukweli ni dhana ya mwanadamu. Watu wanaojidai kuwa wa juu na wenye elimu wanaweza kuwa wapumbavu mbele za Mungu, na kama ni hivyo, kauli za juu na zilizofunzwa na kuzoezwa za mafundisho yao ya imani, haijalishi zinaweza kuwa za kupendeza, kufurahisha na kuchekesha hisia, na hata ingawa zinaweza kuwa zimekabidhiwa kutoka zama hadi zama (au kizazi hadi kizazi), na kubembelezwa toka utotoni katika kitanda cha mapokeo au

imani maarufu, inayopendwa, yote hayo ni udanganyifu na uwongo tu ikiwa hayapatikani katika masomo yaliyovuviwa na Kristo. Yeye Ndiye Chanzo cha hekima yote; kwa kuwa alijiweka mwenyewe moja kwa moja kwenye usawa na kiwango na Mungu wa milele. Katika uanadamu Wake, Utukufu wa Nuru ya Mbinguni ulimwangukia moja kwa moja, na kutoka Kwake hadi ulimwenguni, ili kuakisiwa nyuma na wote wanaompokea na kumwamini Yeye, ukichanganywa na ukamilifu wa tabia Yake na mng'aro wa tabia Yake Mwenyewe. Wakati Kristo alisimama wazi ndani ya Utu Wake wa ubinadamu, na akavutia kwa lugha ya kushangaza lakini sahili kwa ubinadamu, Alikuwa katika umoja kamili na Mungu hivi kwamba sauti Yake ilikuja na mamlaka, kama sauti ya Mungu kutoka katikati ya Utukufu. {FEsw 406.1}

Katika kumbukumbu ambayo Yohana aliagizwa na Roho Mtakatifu kuwasilisha, yeye alisema hivi juu ya Kristo, "Hapo mwanzo kulikuwako Neno, Naye Neno alikuwako kwa Mungu, Naye Neno alikuwa Mungu. Huyo mwanzo alikuwako kwa Mungu. Vyote vilifanyika kwa huyo; wala hakuna chochote kilichoumbwa ambacho Yeye hakukiumba. Huu ndio ufunuo wa thamani zaidi wa Ukweli dhahiri, ukimulika Nuru Yake takatifu na Utukufu juu ya wale wote wataoupokea. Ni maarifa gani muhimu zaidi yanayoweza kupokelewa kuliko yale yaliyotolewa katika Kitabu kinachofundisha juu ya anguko la mwanadamu na la matokeo ya dhambi, ambayo yalifungua milango ya msiba/ole juu ya dunia yetu; ambayo inafundisha pia juu ya kuja Kwake Kristo kwa mara ya kwanza, kama mtoto mchanga asiyejiweza, aliyezaliwa katika zizi la ng'ombe na kulazwa kwenye hori. Historia ya Kristo yabidi ichunguzwe, kwa kulinganisha maandiko na maandiko, ili tupate jifunze somo muhimu zaidi. Masharti ya wokovu ni yapi? Kama mawakala wenye akili, waliowekezewa sifa na majukumu ya kibinafsi, tunaweza kujua kuhusu maisha yetu ya baadaye, hatima ya milele; kwa kuwa kumbukumbu/rekodi ya Maandiko iliyotolewa na Yohana, kwa agizo la Roho Mtakatifu, haina Maneno ambayo hayawezi kueleweka kwa urahisi, na kwamba hayahitaji kushughulika na uchunguzi zaidi na utafiti wenye umakini au ukosoaji. {FEsw 406.2}

Kristo alikuwa mwalimu aliyetumwa kutoka kwa Mungu, na Maneno Yake hayakuwa na hata chembe ya makapi au mfano wa kile ambacho si cha lazima. Lakini msukumo wa mafundisho mengi ya kibinadamu yamo katika semi za nguvu na ujasiri, ambazo sio kweli. Walimu wa siku hizi wanaweza kutumia tu uwezo wa elimu uliolimbikizwa na walimu waliotangulia; na japo kuna uzito wote na umuhimu ambao unaweza kuambatanishwa na maneno ya waandishi mashuhuri kubwa zaidi, kuna kutokuwa na uwezo wa dhamira au akili kuyafuatilia nyuma hadi kufikia ile kanuni kuu, ambayo ndiyo Chanzo cha hekima isiyo na dosari, ambayo kwayo ndio walimu hupata mamlaka yao. Kuna kutokuwa na uhakika kuliko na uchungu, kutafuta mara kwa mara kufikia uhakikisho ambalo unaweza kupatikana kwa Mungu tu. Tarumbeta ya ukuu wa mwanadamu inaweza kupigwa, lakini huwa na sauti isiyo na uhakika; isiyo ya kutegemewa, na wokovu wa Roho za wanadamu

hauwezi ukawekwa kwenye hali ya hatari (wokovu wa mwanadamu ni nyeti hauwezi ukahatarishwa na mambo yakawa salama). {FEsw 407.1}

Lundo la mapokeo, yenye mfanano mdogo na ile Kweli, huingizwa kwenye elimu, jambo ambalo kamwe halistamstahilisha mwanafunzi kuishi

katika maisha haya ili apate maisha yale ya juu, ya kutokufa. Maandishi (Fasihi) zilizowekwa katika shule zetu, zilizoandikwa na makafiri na wale wanaoitwa watu wenye hekima, hayana elimu ambayo wanafunzi wanapaswa kuipata. Sio jambo la muhimu kwao kuelimishwa katika mistari hii ili wahitimu kutoka shule hizi za dunia ili waingie kwenye ile shule iliyo Mbinguni. Lundo la mapokeo yanayofundishwa hayatakuwa na ulinganifu (hayatafua dafu) wowote na mafundisho ya Yeye aliyekuja kuonyesha njia ya Mbinguni. Kristo alifundisha kwa mamlaka. Mahubiri ya mlimani ni uzalishaji mzuri sana, lakini bado ni rahisi hata kwa mtoto kuelewa,

yaani mtoto anaweza kuyasoma bila kupotoshwa. Mlima ya Baraka ni Nembo ya mwinuko wa juu ambao Kristo alisimama daima juu yake. Alizungumza kwa mamlaka ambayo yalikuwa ya kipekee, ambayo hakuna mwingine alikuwa nayo. Kila sentensi aliyoitoe ilitoka kwa Mwenyezi Mungu. Yeye alikuwa Neno na Hekima ya Mungu, na Yeye daima aliwasilisha Ukweli kwa mamlaka ya Mungu. “Maneno ninayowaambia ninyi,” Yeye alisema, “ni Roho na ni Uhai.” {FEsw 407.2}

Kile ambacho katika mabaraza ya Mbinguni Baba na Mwana walichukulia kuwa muhimu kwa wokovu wa mwanadamu, kilifafanuliwa kutoka umilele kwa Kweli zisizo na kikomo ambazo viumbe wenye ukomo hawawezi kushindwa kuzielewa. Mafunuo yamefanywa kwa ajili ya kuwaelekeza/kuwafundisha katika haki, ili kwamba mtu wa Mungu aweze kuyatukuza maisha yake na ya binadamu wenzake, si tu kwa kuumiliki Ukweli, bali kwa kuwasilisha. “Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema.. Nakuagiza mbele za Mungu, na mbele za Bwana Yesu Kristo, ambaye atawahukumu walio hai na waliokufa kwa kufunuliwa Kwake na Ufalme Wake; lihubiri Neno; uwe tayari wakati ukufaa, na wakati usiokufaa; karipia, kemea, na kuonya kwa uvumilivu wote na mafundisho. Kwa maana utakuja wakati watakapoyakataa mafundisho yenye uzima; lakini baada yake watajirundikia waalimu kwa tamaa zao wenyewe, wakiwa na kuwashwa masikio.” {FEsw 408.1}

Yesu hakuleta hata sayansi moja ya wanadamu katika mafundisho Yake. Mafundisho Yale yamejaa Ukweli mkuu, unaokuza, unaoboresha, na unaookoa, ambao matamano ya mwanadamu ya ukuu, na uvumbuzi wa kiburi chake, hauwezi kulinganishwa na hayo; na bado mambo yasiyo na matokeo madogomadogo hufyonza umakini wa akili za watu. Mpango juu mkuu wa ukombozi kwa jamii iliyoanguka ulifanyika katika maisha ya Kristo katika mwili wa

mwanadamu. Mpango huu wa kurejesha maadili sura ya Mungu katika ubinadamu uliohafifishwa, thamani uliingia katika kila kusudi la maisha na tabia ya Kristo. Ukuu Wake wa Mbinguni haukuweza kuchanganyika na sayansi ya binadamu, ambayo itatengana na chanzo kikuu cha hekima kwa muda wa kwa siku moja tu. Mada ya sayansi ya wanadamu, kamwe haikutamkwa kwenye midomo Yake mitakatifu. Kwa kuamini na kufanya Maneno ya Mungu, Alikuwa akiitenganisha kwa kuikata kwa nguvu familia ya kibinadamu kutoka kwenye gari la farasi la Shetani. Alikuwa Mtendaji hai kwenye maangamizo ya kutisha yaliyoning'inia juu ya jamii ya watu, Naye akafika ili kuokoa Roho za watu kwa haki Yake Mwenyewe, akaleta kwa ulimwengu uhakikisho wa matumaini na uponyaji kamili. Mkondo wa maarifa yaliyo ulimwenguni unaweza kupatikana; kwa maana watu wote ni mali ya Mungu, nayo yanafanyiwa kazi na Mungu ili kutimiza mapenzi Yake katika mistari fulani, hata wakati wao hukataa mwanadamu Yesu Kristo kama Mwokozi wao. Njia ambayo Mungu hutumia wanadamu haitambuliwi mara zote, lakini Yeye huwatumia. Mungu huwakabidhi watu vipaji vikubwa na fikra za uvumbuzi (genius), ili kusudi kazi Yake kuu katika ulimwengu wetu iweze kukamilika. Uvumbuzi unaotendwa na akili za wanadamu watu husema hutoka kwenye uwezo wanadamu, lakini Mungu yuko nyuma ya hayo yote (uwezo ni Wake). Ameleta ubunifu wa njia za usafiri wa haraka haraka, kwa ajili ya maandalizi ya ile kuu siku ya hukumu. Matayarisho ya kwenda Mbinguni. {FEsw 408.2}

Matumizi ambayo wanaume wamefanya chini ya uwezo wao, ya kutumia vibaya au isivyo, talanta zao walizopewa na Mungu, imeleta mkanganyiko ndani ya dunia. Wameuacha uongozi, ulinzi na malezi ya Kristo kwa ajili ya ulinzi na uongozi wa mwasi mkuu, mkuu wa giza. Mwanadamu pekee ndiye anayewajibika kwa moto wa mgeni ambao umechanganywa na ule moto mtakatifu. Mlundikano wa mambo mengi ambayo hutumikia tamaa ya mwili na tamaa ya makuu imeleta juu ya ulimwengu hukumu ya Mungu. Wakati mtu akiwa katika shida, wanafalsafa na watu wakuu duniani wanatamani kuzirishisha akili zao bila kumtafuta Mungu. Wanamwaga falsafa zao kwenye anga kuhusiana na masuala mbingu na nchi, wakileta mapigo na tauni, magonjwa ya mlipuko, matetemeko ya ardhi, tauni, na njaa, kwa kile wanachodhani wao ni sayansi. Mamia ya maswali yahusianayo na uumbaji, majaliwa ya Mungu au riziki toka Kwake, wanajaribu kusuluhisha/kutatua kwa kusema. Hii ni sheria ya asili. {FEsw 409.1}

Kuna sheria za asili, lakini zinaelewana, zina upatananifu na zinaendana na kazi yote ya Mungu; lakini wakati mabwana wengi na miungu mingi wanajiweka wenyewe katika kuelezea kanuni na majaliwa ya Mungu Mwenyewe, wakiwasilisha duniani mioto migeni na kuchukua nafasi ya Mungu, kuna mkanganyiko. Uumbaji na vyote vya duniani na Mbinguni vinahitaji nyuso nyingi kwenye kila gurudumu ili kuona Mkono chini ya magurudumu, ukileta utaratibu kamili kutoka kwenye machafuko. Mungu aliye hai na wa Kweli Ndiye wa Muhimu, Naye ni wa lazima, Kila mahali (yaani Anahitajika kila mahali ili mambo yaendeleo kuwa!). {FEsw 409.2}

Historia ya kuvutia na muhimu zaidi, imetolewa katika Danieli 2. Nebukadneza, Mfalme wa Babeli, aliota ndoto ambayo hakuweza kuikumbuka alipoamka. “Ndipo Mfalme akaamuru kuwaita waganga, na wanajimu, na wachawi; na Wakaldayo,” wale ambao alikuwa amewainua na akawategemea sana, kuhusiana na hali ya mambo, aliwaamrisha kwamba wamtafsirie ndoto. Wenye hekima wakasimama mbele ya Mfalme kwa hofu kubwa; kwa maana hawakuwa hata na mwale mmoja wa mwanga kuhusiana na ndoto yake. Walichoweza kusema tu ni, “tuambie sisi watumishi wake ile ndoto, nasi tutamwonyesha tafsiri yake.” “Mfalme akajibu, akasema, Najua hakika ya kuwa mnataka kupata nafasi, kwa sababu mmeona ya kuwa lile neno lenyewe limeniondoka. Lakini msiponijulisha ile ndoto, iko amri moja tu iwapasayo; maana mmepatana kusema maneno ya uongo, na maneno maovu, mbele yangu, hata zamani zitakapobadilika; basi niambieni ile ndoto, nami nitajua ya kuwa mwaweza kunionyesha tafsiri yake.” Bado wenye hekima walirudi vile vile na wakajibu, “Mfalme na awaambie watumishi wake ndoto hiyo, nasi tutaonyesha tafsiri yake.” {FEsw 410.1}

Nebukadneza alianza kuona kwamba wanaume hawa aliowaamini kufunua mafumbo kupitia hekima waliyojivunia, walimwangusha kwa fadhaa kuu, na akasema, “Mfalme akajibu, akasema, Najua hakika ya kuwa mnataka kupata nafasi, kwa sababu mmeona ya kuwa lile neno lenyewe limeniondoka. Lakini msiponijulisha ile ndoto, iko amri moja tu iwapasayo; maana mmepatana kusema maneno ya uongo, na maneno maovu, mbele yangu, hata zamani zitakapobadilika; basi niambieni ile ndoto, nami nitajua ya kuwa mwaweza kunionyesha tafsiri yake. Wakaldayo wakajibu mbele ya Mfalme, wakasema, Hapana mtu duniani awezaye kulionyesha neno hili la Mfalme; “Ni neno la ajabu, hili analolitaka Mfalme, wala hapana mwingine awezaye kumwonyesha Mfalme neno hilo, ila miungu, wasio na kikao pamoja na wenye mwili..... Ni neno la ajabu, hili analolitaka Mfalme, wala hapana mwingine awezaye kumwonyesha Mfalme neno hilo, ila miungu, wasio na kikao pamoja na wenye mwili.” Kisha Mfalme “basi Mfalme akaghadhabika, akakasirika sana, akatoa amri kuwaangamiza wenye hekima wote wa Babeli.” {FEsw 410.2}

Aliposikia amri hiyo, “Danieli akaingia, akamwomba Mfalme kwamba ampe muda, na kwamba atamwonyesha Mfalme tafsiri. Ndipo Danieli akaenda nyumbani kwake, naye akawajulisha wenzake ambao walikuwa Hanania, Mishaeli, na Azaria; kwamba wangeomba pamoja rehema za Mungu wa Mbinguni kuhusu siri hiyo.” Roho ya Bwana akatulia juu ya Danieli na wenzake, na siri hiyo ikafunuliwa kwa Danieli katika maono ya usiku. Alipoanza kumsimulia Mfalme ile tafsiri, ukweli au matukio ya ile ndoto yalikuja upya kwenye akili yake, na tafsiri yake ilitolewa na Danieli, ikionyesha matukio ya ajabu ambayo yangetokea kwenye historia ya unabii. {FEsw 411.1}

Bwana alikuwa akifanya kazi katika ufalme wa Babeli, akiwasilisha Nuru kwa

mateka wanne wa Kiebrania, ili aweze kuwakilisha kazi Yake mbele ya watu. Angefunua kwamba Yeye alikuwa na uwezo na nguvu juu ya falme zote za dunia, akiwaweka wafalme na kuwondoa wafalme. Mfalme aliyekuwa juu ya wafalme wote alikuwa akiwasilisha Ukweli mkuu kwa Mfalme wa Babeli, akiamsha akilini mwake hisia ya wajibu wake kwa Mungu. Aliona tofauti kati ya hekima ya Mungu na hekima ya watu walioelimika zaidi katika ufalme Wake. {FEsw 411.2}

Bwana aliwapa wawakilishi wake waaminifu masomo kutoka Mbinguni, Danieli akatangaza mbele ya watu wakuu wa Mfalme wa Babeli, “Jina la Mungu lihimidiwe Milele na Milele, kwa kuwa hekima na uweza ni Wake, Naye hubadili majira na nyakati, na huondoa wafalme, na kuwatawaza wafalme, huwapa wenye hekima, na maarifa kwao wajua ufahamu; Yeye Ndiye anayefunua vilindi na mambo ya siri: Yeye anayajua yaliyo gizani na na Nuru hukaa kwake. Nakushukuru, nakuhimidi, Ee Mungu wa baba zangu, uliyenipa hekima na uwezo, ukanijulisha hayo tuliyotaka kwako; maana umetujulisha Neno lile la Mfalme.” “Kuna Mungu Mbinguni afunuaye siri, na kumjulisha Mfalme Nebukadreza mambo yatakayotokea katika siku za mwisho.” Utukufu haukutolewa kwa wanadamu waliosimama kama waaguzi au washauri wenye busara kwenye ufalme; bali watu ambao waliweka imani yao yote kwa Mungu, wakitafuta neema na nguvu na Nuru ya Bwana, walichaguliwa kama wawakilishi wa ufalme wa Mungu katika Babeli ya waovu walioabudu sanamu. {FEsw 411.3}

Matukio ya kihistoria yanayohusiana na ndoto ya Mfalme yalikuwa na matokeo kwake; lakini ndoto ikaondolewa kutoka kwake, ili wale wenye hekima kwa madai ya uelewa wao wa mafumbo, wasije kuweka tafsiri ya uongo. Masomo yaliyofundishwa ndani ya hii ndoto, yalitolewa na Mungu kwa wale wanaoishi katika siku zetu za mwisho. Kutoweza kwa wenye hekima kueleza ndoto hiyo ni mfano wa wenye hekima wa siku hizi, ambao hawana utambuzi, elimu na maarifa kutoka Kwake Yeye Aliye Juu, na kwa hiyo hawawezi kuelewa unabii. Watu wasomi sana, wale Waliojifunza zaidi katika hekaya au hadithi za mapokeo ya ulimwengu huu, ambao hawaangalii ili kusikia kile Mungu anakisema kupitia Neno Lake, na hivyo kufungua mioyo yao ili kupokea hayo Maneno haya na kuwapa wengine pia, hao si wawakilishi Wake. Sio watu mashuhuri, wenye elimu ya dunia, wafalme na wakuu, ndiyo ambao watapokea ile Kweli mpaka kuupata uzima wa milele, ingawa huo Ukweli utaletwa kwao. {FEsw 412.1}

Ufafanuzi wa Danieli wa ndoto ilitoyolewa kwa Mfalme na Mungu, ulisababisha yeye kupokea heshima, cheo na hadhi. “Mfalme Nebukadneza akaanguka kifudifudi, akamsujudia Danieli, na kuwaamuru wanapaswa kumtolea sadaka na uvumba wa harufu nzuri. Mfalme akajibu, akamwambia Danieli, Hakika Mungu wenu Ndiye Mungu wa miungu, na Bwana wa wafalme, awezaye kufumbua siri, kwa kuwa wewe uliweza kuifumbua siri hii. Basi Mfalme akamtukuza Danieli, akampa zawadi kubwa nyingi sana, akamfanya kuwa mkubwa juu ya uliwali wote wa Babeli, na kuwa liwali

mkuu juu ya wote wenye hekima wa Babeli. Tena, Danieli akamwomba Mfalme, naye akawaweka Shadraka, na Meshaki, na Abednego, wawe juu ya mambo yote ya uliwali wa Babeli; lakini huyo Danieli alikuwa akiketi katika lango la Mfalme.”-- mahali ambapo hukumu ilitolewa, na wenzake watatu wakafanywa washauri, watawala, na waamuzi katikati ya nchi. Wanaume hawa hawakujivuna kwa ubatili, bali waliona na kushangilia kwamba Mungu alitambuliwa juu ya watawala wote wa kidunia, na kwamba ufalme Wake ulikuwa umetukuzwa juu ya falme zote za dunia.

{FEsw 412.2}

Hivyo tunaona kwamba mstari wa juu zaidi wa elimu ya kidunia unaweza upatikane, ila watu walio na elimu hiyo wanaweza kuwa bado wajinga wa kanuni za awali/mwanzo tu za Mungu, ambazo hizo zingewafanya wao kuwa raia wa ufalme wa Mungu. Mafunzo ya kibinadamu hayawezi kumstahilisha mtu kuingia kwenye ufalme huo. Raia wa Ufalme wa Kristo hawaundwi kwa maadhimisho ya sherehe, taratibu za mwanadamu, au usomaji na uchunguzi wa vitabu vikubwa. “Huu ndio uzima wa milele, wakujue Wewe, Mungu wa pekee wa Kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma.” Washiriki wa ufalme wa Kristo ni viungo vya mwili Wake, ambao Yeye Mwenyewe Ndiye kichwa. Wao ni wana wateule wa Mungu, “Bali ninyi ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu” ambao wanapaswa kuzitangaza sifa Zake Yeye aliyewaita kutoka gizani, waingie kwenye Nuru Yake ya ajabu. {FEsw 413.1}

“Kwa maana wewe u taifa takatifu kwa Bwana, Mungu wako; Bwana Mungu wako, amekuchagua kuwa watu wake hasa, zaidi ya mataifa yote walioko juu ya uso wa nchi. Bwana hakuwapenda ninyi, wala hakuwachagua ninyi, kwa sababu mlikuwa wengi kuliko mataifa yote, maana mlikuwa wachache kuliko watu wote; bali kwa sababu Bwana anawapenda, na kwa sababu alitaka kuutimiza uapo wake aliowaapia baba zenu, ndiyo sababu Bwana akawatoa kwa mkono wa nguvu, akawakomboa katika nyumba ya utumwa, katika mkono wa Farao, Mfalme wa Misri. Basi jueni ya kuwa Bwana, Mungu wenu, ndiye Mungu; Mungu mwaminifu, ashikaye agano lake na rehema zake kwao wampendao, na kushika amri zake, hata vizazi elfu; naye huwalipa wamchukiao mbele ya uso wao, kuwaangamiza. Hatakuwa mlegevu kwake yeye amchukiaye, atamlipa mbele ya uso wake. Basi zishike amri, na sheria, na hukumu ninazokuamuru leo, uzitende.” Ikiwa amri za Mungu zinapaswa kuwa na mashiko kwa vizazi elfu, zitawapeleka katika ufalme wa Mungu, mbele ya Mwenyezi Mungu na malaika Zake watakatifu. Hii ni hoja ambayo haiwezi kupingwa. Amri za Mungu zitadumu kwa nyakati zote na milele. Je, basi, zimetolewa kwetu sisi kuwa mzigo? — Hapana. “Naye Bwana akatuamuru kuzifanya amri hizi zote, tumche Bwana, Mungu wetu, tuone mema sikuzote ili atuhifadhi hai kama hivi leo.” Bwana aliwapa watu Wake amri, ili kwa kuzitii wapate kuhifadhi afya yao ya kiakili na kimaadili. Walipaswa kuishi kwa utii; bali kifo ni matokeo ya hakika ya uasi wa sheria ya Mungu. {FEsw 413.2}

Maandiko ya Agano la Kale na Agano Jipya yanahitaji kujifunzwa kila siku.

Maarifa ya Mungu na hekima ya Mungu humjia mwanafunzi ambaye daima anajifunza njia na kazi Zake Mungu. Bibilia inapaswa kuwa Nuru yetu, mwalimu wetu (mwelimishaji wetu). Wakati tutamkiri Mungu katika njia zetu zote; wakati vijana wameelimishwa kumwamini Mungu kama mleta mvua na jua kutoka Mbinguni, na Yeye asababishaye mimea kustawi; wanapofundishwa kwamba baraka zote zinatoka Kwake, na kwamba shukrani na sifa ni Zake; wakati kwa uadilifu wao wanamkiri Mungu, na kutekeleza wajibu wao siku baada ya siku, Mungu itakuwa katika mawazo yao yote; wanaweza kumwamini kwa ajili ya kesho, na masumbufu na wasiwasi ambayo huleta kutokuwa na furaha au huzuni katika maisha ya watu wengi, yataweza kuepukwa. “Utafuteni kwanza ufalme wa Mungu, na haki Yake; na hayo yote mtazidishiwa.” {FEsw 414.1}

Somo kubwa la kwanza katika elimu yote ni kujua na kufahamu mapenzi ya Mungu. Chukua maarifa ya Mungu pamoja nawe katika katika kila siku ya maisha. Hebu na ifyonze nia na akili na kiumbe chote (mwili mzima). Mungu alimpa Sulemani hekima, lakini hekima hii iliyotolewa na Mungu ilipotoshwa wakati aligeuka kutoka kwa Mungu ili kupata hekima kutoka vyanzo vingine. Tunahitaji hekima ya Sulemani baada ya sisi kujifunza hekima ya Mmoja Yule aliye mkuu kuliko Sulemani. Hatupaswi kupitia hekima ya kibinadamu, ambao unaitwa upumbavu, ili kutafuta hekima ya Kweli. Ili wanadamu kujifunza sayansi kupitia tafsiri ya mwanadamu, ni kupata elimu danganyifu, lakini kujifunza juu ya Mungu na Yesu Kristo ni kujifunza sayansi ya Biblia. Mkanganyiko katika elimu umekuwa kwa sababu hekima na ujuzi wa Mungu haukutukuzwa na kuinuliwa kwenye ulimwengu wa kidini/kiroho. Wenye moyo safi humwona Mungu katika kila riziki (majaliwa Yake), ndani ya kila awamu ya elimu ya Kweli. Wanatoa mwitikio na kusonga mbele wanapotembelewa mara ya kwanza ya Nuru itokayo katika kiti cha enzi cha Mungu. Mawasiliano kutoka mbingu zinafanywa kwa wale ambao watapata mng'ao wa kwanza wa kiroho maarifa. {FEsw 414.2}

Wanafunzi katika shule zetu wanapaswa kuzingatia maarifa/ujuzi wa Mungu juu ya kila kitu. Kuchunguza Maandiko peke yake kutaleta ujuzi wa Mungu wa Kweli na Yesu Kristo ambaye alimtumwa. “Mahubiri ya msalaba kwao wanaopotea ni upuuzi; lakini kwetu sisi tunaokolewa ni nguvu ya Mungu. Kwa maana imeandikwa, Nitaiharibu hekima ya wenye hekima, Nami nitawabatilisha hao ufahamu wa wenye busara.” “Kwa sababu upumbavu wa Mungu una hekima zaidi ya wanadamu, na udhaifu wa Mungu una nguvu zaidi ya wanadamu.” “Bali kwa Yeye ninyi mmekuwa katika Kristo Yesu, aliyefanywa kwetu hekima itokayo kwa Mungu, na haki, na utakatifu, na ukombozi; kusudi kama ilivyoandikwa, Yeye ajisifuye na ajisifu juu ya ya Bwana.” {FEsw 415.1}—*Special Testimonies on Education, Machi 26, 1896.*

Rejea za ziada

Our Children Demand Our Care and Attention, The Review and Herald, April 28,

Sura ya 50

MAFUNZO YA KAZI ZA MIKONO

Uhai haujatolewa kwetu ili tuutumie katika uvivu au kujifurahisha wenyewe; lakini uwezekano mkubwa umewekwa mbele ya kila mmoja anayetaka kukuza uwezo wake aliopewa na Mungu. Kwa sababu hii mafunzo ya vijana ni suala la umuhimu wa juu. Kila mtoto aliyezaliwa ndani ya nyumba ni amana takatifu. Mungu anawaambia wazazi, Chukua huyu mtoto, umlee kwa ajili Yangu, ili awe Utukufu kwa Jina Langu; na mfereji ambao baraka Zangu zitatiririka kwa ulimwengu. Ili kumstahilisha mtoto kwa maisha kama hayo, kitu fulani zaidi kinahitajika kuliko elimu ile nusu nusu, inayoegemea upande mmoja, ambayo itakuza akili kwa gharama ya nguvu za kimwili. Vitivo vyote vya akili na mwili vina haja ya kuendelezwa; na hii ndiyo kazi ambayo wazazi, wakisaidiwa na mwalimu, wanapaswa kuwafanyia watoto na vijana walio chini utunzaji wao. {FEsw 416.1}

Masomo ya kwanza ni muhimu sana. Ni desturi kupeleka watoto wadogo sana shuleni. Watoto hawa wanatakiwa kusoma kutoka kwenye vitabu vitu ambavyo huchosha/hutinga akili zao changa, na mara nyingi hufundishwa muziki. Mara nyingi wazazi wana uwezo mdogo wa kifedha, na gharama inahitajika ambayo hawawezi kuimudu; lakini bidi yote inafanywa ili kupinda katika mstari huu wa elimu bandia. Mwenendo huu sio busara. Mtoto mwenye wasiwasi au shida ya neva (mishipa ya fahamu) hapaswi kushughulishwa kupita kiasi katika mwelekeo wowote, na pia asijifunze muziki hadi atakapokuwa ameimarika kimwili. {FEsw 416.2}

Mama anapaswa kuwa mwalimu, na nyumbani ndiyo pawe shule ambayo kila mtoto hupokea masomo yake ya kwanza; na masomo haya yanapaswa kujumuisha

mazoea ya stadi za kazi na bidii katika kazi za mikono. Akina mama, waacheni watoto wadogo wacheze kwenye hewa ya wazi; wasikilize nyimbo za ndege, na wajifunze upendo wa Mungu kama ulivyoonyeshwa katika kazi Zake nzuri. Wafundishe masomo sahili kutoka kitabu cha maumbile na mambo yanayowahusu; na kadri akili zao zitakavyopanuka, masomo kutoka vitabuni yanaweza kuongezwa, na kuwekwa kwa uthabiti kwenye kumbukumbu. Lakini hata katika miaka yao ya mapema. Hata katika miaka yao ya mapema, Hebu na wajifunze umuhimu wa kuwa watu wenye manufaa. Waleeni na kuwazoeza kufikiri, kama washiriki wa familia/kaya, wao wanapaswa kutenda kwa kusaidia katika kushiriki mizigo ya nyumbani, na kutafuta mazoezi ya afya kupitia utendaji wa majukumu muhimu ya nyumbani. {FEsw 416.3}

Ni muhimu kwa wazazi kuangalia kazi muhimu kwa ajili ya watoto, ambayo itahusisha kubeba majukumu kadri umri na nguvu zao zitakavyoruhusu. Watoto wanapaswa kupewa kitu cha kufanya si kwa ajili ya kupata shughuli ya kufanya peke yake tu, bali pia ili kuvutiwa. Mikono na akili inayoweza kujongea, sharti ishughulishwe kutoka miaka ya awali. Ikiwa wazazi wanapuuzia kuzigeuza nguvu za watoto kueleka kwenye mifereji yenye manufaa, wanawaletea watoto madhara makubwa; kwa maana Shetani yuko tayari kuwatafutia kitu cha kufanya. Je! kazi haitachaguliwa kwa ajili yao, Na wazazi wawe walimu wao? {FEsw 417.1}

Mtoto anapokuwa na umri wa kutosha kupelekwa shuleni, mwalimu anapaswa kushirikiana na wazazi, na mafunzo ya kazi za mikono yanapaswa kuendelezwa kama sehemu ya majukumu yake ya shule. Kuna wanafunzi wengi wanaopinga aina hii ya kazi shuleni. Wanafikiri kuwa ajira zenye manufaa, kama kujifunza stadi ya kazi ya mikono, ni jambo la kudhalilisha; lakini watu hao wana wazo lisilo sahihi kwa kile kinachojumuisha hadhi au utu wa kweli. Mola wetu na Mwokozi Yesu Kristo, ambaye ni mmoja na Baba, Kamanda kwenye nyua za Mbinguni, alikuwa Mwalimu aliyewaongoza Mwenyewe wana wa Israeli; na miongoni mwao wote, kila kijana alipaswa kujifunza jinsi ya kufanya kazi. Wote walipaswa kuelimishwa katika mstari wa shughuli fulani, ili wapate ujuzi wa maisha ya vitendo, ili wajitegemee na kuwa watu wa manufaa. Hili lilikuwa ni agizo ambalo Mungu alilitoa kwa watu Wake. {FEsw 417.2}

Katika maisha Yake ya duniani, Kristo alikuwa kielelezo kwa familia yote ya ubinadamu, na Alikuwa mtiifu na mwenye kusaidia nyumbani. Alijifunza stadi ya useremala, na akafanya kazi kwa mikono Yake Mwenyewe katika karakana ndogo Nazareti. Alikuwa ameishi katikati ya Utukufu wa Mbinguni; bali aliuvika Uungu Wake na ubinadamu, ili ashirikiane na wanadamu. na kufikia mioyo kupitia njia ya kawaida ya kuonyesha huruma. Tena, alipoonekana ana umbo kama mwanadamu, alijinyenyekeza, na kufanya kazi kwa ajili ya kurejesha Roho ya mwanadamu, kwa kujihusisha Mwenyewe kulingana na hali iliyopo, ambayo Yeye Aliipata kwenye ubinadamu. {FEsw 417.3}

Biblia inasema hivi kumhusu Yesu, “Yule mtoto akakua, akaongezeka nguvu, amejaa hekima; na neema ya Mungu ilikuwa juu Yake.” Alipokuwa Akifanya kazi katika utoto na ujana, akili na mwili vilikuzwa. Hakutumia nguvu Zake za kimwili kizembe, bali alizipa mazoezi kadri iwezekanavyo ili vipate afya, ili Yeye afanye kazi bora zaidi katika kila mstari. Hakuwa tayari kuwa na kasoro, hata katika utumiaji wa zana za kazi. Alikuwa mtendakazi mkamilifu. kama jinsi alivyokuwa mkamilifu katika tabia. Kwa kanuni na mfano, Kristo ameipa hadhi kazi yenye manufaa.

{FEsw 418.1}

Muda unaotumika katika mazoezi ya mwili haupotei. Mwanafunzi ambaye anaendelea kuchungulia vitabu vyake muda wote, huku akifanya mazoezi kidogo tu katika hewa wazi, anajiumiza. Zoezi sawia la viungo vyote na vitivo vyote vya mwili ni muhimu kwa utendaji kazi bora wa kila kimoja. Ubongo unapotozwa ushuru wakati viungo vingine vya mwili vimepumzishwa, kuna upotezaji wa nguvu za kimwili na kiakili. Mfumo wa kimwili unaibiwa toni yake ya afya, akili hupoteza uchangamfu wake na nguvu, na msisimko mbaya ni matokeo. {FEsw 418.2}

Faida kubwa haipatikani kutokana na zoezi ambalo linachukuliwa kama mchezo au kufanya mazoezi tu. Kuna faida fulani inayotokana na kuwa kwenye hewa safi, na pia kutoka na mazoezi ya misuli; lakini acha kiasi sawa cha nishati kitolewe katika utekelezaji wa majukumu ambayo ni msada kwa jamii ya ubinadamu, na kisha faida itakuwa kubwa zaidi, na hisia za kuridhika zitahisiwa kwenye akili; kwa kuwa mazoezi kama hayo hubeba pamoja nayo, maana ya kusaidia na idhini ya dhamiri kwa ajili ya wajibu uliofanywa vizuri. {FEsw 418.3}

Kwa watoto na vijana shauku inapaswa kuamshwa katika kufanya mazoezi yao kwa njia ambayo italeta manufaa kwao wenyewe na kusaidia wengine. Zoezi linalokuza akili na tabia, ambayo hufundisha mikono kuwa na manufaa, na kuwafunza walio wadogo kubeba na kuhuisha kila kitivo. Na kuna malipo katika bidii ya maadili kwenye stadi za kazi, katika kukuza tabia ya, uadilifu, ya kuishi kwa kutenda mema. {FEsw 418.4}

Watoto wa matajiri wasinyimwe mbaraka mkuu wa kuwa na kitu cha kufanya ili kuongeza nguvu ya ubongo na misuli. Kazi sio laana, bali ni baraka. Mungu alitoa kazi katika bustani nzuri, kwa Adamu na Hawa, ambao hawakuwa na dhambi. Hii ilikuwa kazi ya kupendeza, na hakuna kazi yoyote ila ya kupendeza ingeingia katika ulimwengu wetu, kama ile jozi ya kwanza yaani, wanandoa wa kwanza wasingevunja amri za Mungu. Uvivu wa kujidai kuwa wewe ni dhaifu kama ‘mayai’ na kujifurahisha mwenyewe kwa ubinafsi hufanya watu kuwa vilema; wanaweza kufanya maisha kuwa tupu na tasa kwa kila namna. Mungu hakuwapa wanadamu utashi, na kuyatia maisha yao taji ya wema Wake, ili wapate laana kwa matokeo ya uhakika ya uvivu. Matajiri hawatakiwi kunyimwa fursa na baraka ya nafasi miongoni mwa wafanyakazi wa dunia. Wanapaswa kutambua kwamba wanawajibika kwa matumizi wanayofanya na mali zao walizokabidhiwa; kwamba

nguvu zao, wakati wao, na fedha zao, zinapaswa kutumika kwa busara, na si kwa malengo ya ubinafsi au uchoyo. {FEsw 419.1}

Dini ya Kikristo ni ya vitendo. Haimfanyi mtu abweteke na hivyo kutotekeleza kwa uaminifu majukumu yote muhimu ya maisha. Wakati Mwanasheria akimwuliza Yesu, “Nifanye nini ili niurithi uzima wa milele?” Yesu alimrudishia swali lake mwenyewe, akisema, “Ni nini kimeandikwa ndani ya sheria? unasomaje? Akajibu akisema, Umpende Bwana, Mungu wako, kwa moyo wako wote, na kwa Roho yako yote, na kwa Roho yako yote nguvu zako zote, na kwa akili zako zote; na jirani yako kama nafsi yako.” Yesu akamwambia, “Umejibu sawa; fanya hivi, nawe utafanya kuishi.” Luka 10:25-28. Dini ya kutotenda haikuchorwa hapa (haikuelezwa), lakini ambayo ile ambayo inahitaji matumizi ya nguvu za akili yote na nguvu za kimwili. {FEsw 419.2}

Kutafakari kwa uvivu tu, na kutafakari kwa uzembe, hiyo sio dini. Mungu anatumia kuzithamini karama zetu mbalimbali, na kuzidisha kwa kuzitumia mara kwa mara, kwa vitendo. Watu wake wanapaswa kuwa mifano sahihi katika mahusiano yote ya maisha. Kila mmoja wetu anayo kazi ambayo amepewa kuifanya, kulingana na uwezo wake; na ni fursa yetu kufurahia baraka Zake huku tukijitolea nguvu za mwili na akili katika utendaji wake wenye uaminifu, na huku Utukufu wa Jina Lake ukionekana. {FEsw 419.3}

Kibali cha Mungu kinakita kwenye uhakikisho wa upendo kwa watoto wanaoshiriki kwa uchangamfu katika majukumu ya maisha ya nyumbani, katika kushiriki mizigo ya baba na mama. Watazawadiwa na afya ya mwili na amani ya akili; na watafurahia raha ya uhakika ya kuwaona wazazi wao wakichukua sehemu yao ya starehe za kijamii (social enjoyment) na burudani/tafiriya yenye afya, na hivyo kurefusha maisha yao. Watoto waliofunzwa majukumu ya kimatendo ya maisha, watatoka nyumbani ili kuwa wanachama wenye manufaa katika jamii. Elimu yao ni bora kuliko ile waliyoipata kwa kufungiwa kwenye vyumba vya madarasa shuleni, katika umri mdogo, wakati akili na mwili havina nguvu za kutosha kustahimili mkazo/suluba. {FEsw 420.1}

Watoto na vijana wanapaswa kuwa na somo mbele yao daima nyumbani na shuleni, kwa maagizo na mfano, kuwa wakweli, wasio na ubinafsi, wasio na uchoyo na wenye bidii. Hawapaswi kuruhusiwa kutumia muda wao katika uvivu; mikono yao haipaswi kukunjwa ndani kwa uvivu au kutojishughulisha. Wazazi na walimu wanapaswa kufanya kazi ili kutimiza lengo hili, - kukuza uwezo na nguvu zote, na malezi ya tabia sahihi; pale wazazi wanapotambua wajibu wao, hakika walimu watakuwa na kiasi kidogo cha kufanya katika kuwafundisha na kuwalea watoto wao. {FEsw 420.2}

Mbingu inapendezwa na kazi hii kwa niaba ya vijana. Wazazi na walimu ambao kwa maelekezo ya busara, kwa utulivu, waliamua namna ya kuwazoeza kufikiria na

kuwajali wengine, itawasaidia wao kuushinda ubinafsi wao, na watafunga mlango dhidi ya majaribu yao mengi. Malaika wa Mungu watashirikiana na wakufunzi hawa waaminifu. Malaika hawakuagizwa kufanya kazi hii wao wenyewe; lakini watawapa nguvu na ufanisi wale ambao, katika kumcha Mungu, watajitahidi kuwalea na kuwazoeza vijana kuishi maisha yenye manufaa. {FEsw 420.3} – [Special Testimonies n Education, Mei 11, 1896.](#)

Sura ya 51

MVUTO WA KIELIMU KWA MAZINGIRA

Katika uteuzi wa mahali pa kuishi, yaani pale nyumba itakapokuwa, wazazi hawapaswi kuongozwa na mambo ya kitambo tu. Mahali pa kuishi hapahusiani na suala la mahali ambapo pesa nyingi zaidi, au wapi ndipo patakuwa na mazingira ya kupendeza zaidi, au faida kubwa za kijamii zitapatikana huko. Athari ambazo zitawazunguka watoto wao, na kuwavuta kwa mema au mabaya, ina matokeo makubwa zaidi kuliko mazingatio yote haya. Jukumu zito zaidi liko juu ya wazazi katika kuchagua mahali pa kuishi. Kwa kadiri inavyowezekana waweke familia zao katika mkondo wa Nuru, mahali ambapo mapenzi n ashauku yatakuwa safi, na upendo wao kwa Mungu na wao kwa wao utakuwa hai. Kanuni hiyo hiyo inatumika kwa eneo la kujenga shule zetu, pale ambapo vijana watakusanywa, na familia zitavutiwa kwa ajili ya faida za elimu. {FEsw 421.1}

Hakuna maumivu yanayopaswa kuepukika wakati wa kuchagua maeneo kwa ajili ya kuweka shule zetu, mahali hapo panapaswa kuwa katika angahewa yenye

afya njema kimaadili kwa kadri iwezekanavyo ; kwa maana athari zinazotawala zitaacha hisia ya kina kwa vijana na kuunda tabia. Kwa sababu hiyo basi, eneo lililotulia ni bora zaidi. Miji mikubwa, vituo vya biashara na kujifunzia, vinaweza kuonekana kuwa vinabeba faida fulani; lakini faida hizi zinazidiwa/zinapitwa na mazingatio mengine. {FEsw 421.2}

Jamii ya wakati huu ni ovu, kama ilivyokuwa siku za Nuhu. Watu hawa waliaoishi muda mrefu, kabla ya gharika, hatua chache au muda mfupi tu kutoka paradiso (bustani ya Edeni), Mungu aliwapa karama nyingi, nao walikuwa na nguvu za mwili na akili ambazo watu wa sasa hawana ufahamu kwenye fikra zao hata kidogo jinsi mambo yalivyokuwa; lakini hao walizitumia fadhila Zake, na nguvu na ujuzi Aliowapa, kwa ajili ya makusudi ya ubinafsi/uchoyo, kuhudumia tamaa ya ladha ya chakula au matumbo yao yasiyo halali, na kuridhisha kiburi. Walimfukuza Mungu katika fahamu zao; wakaidharau sheria Yake; walikikanyaga-kanyaga kiwango Cchake cha tabia kwenye mavumbi. Walifurahia anasa za dhambi, wakiziharibu njia zao mbele za Mungu, na kuziharibu njia za wengine. Jeuri na uhalifu vilijaza dunia. Uhusiano wa ndoa, na haki za kumiliki mali havikuheshimiwa; na vilio vya waliodhulumiwa viliingia masikioni mwa Mungu. Kwa kuyatazama maovu, wanadamu wakabadilishwa na kuwa mfano wake huo uovu, hadi Mungu hakuweza kuvumilia uovu wao tena, nao wakafagiliwa mbali kwa gharika. {FEsw 421.3}

Vijana walioelimishwa katika miji mikubwa wamezungukwa na mivuto sawa na ile iliyokuwepo kabla ya gharika. Kanuni ile ile ya kutomjali Mungu na sheria Yake; Kupenda kulekule kwa anasa, kwa kujifurahisha na kuendekeza tamaa binafsi, na kiburi na ubatili vinatenda kazi wakati huu. Ulimwengu umejitoa kwa anasa; maadili mabaya yametawala; haki za wanyonge na watu wa chini hupuuzwa; na, duniani kote, miji mikubwa inazidi kitovu cha maovu. {FEsw 422.1}

Kupenda anasa ni moja ya hatari kubwa, kwa sababu ni moja ya hila ambayo ni vigumu kuigundua, hila hii ina majaribu mengi ambayo hushambulia watoto na vijana mijini. Siku kuu ni nyingi; michezo na mbio za farasi huvuta maelfu, na kimbunga cha msisimko na raha huwavuta watu mbali na majukumu ya kimaisha. Pesa ambayo ilipaswa kuhifadhiwa kwa matumizi bora—mara nyingi mapato duni ya masikini-yanapukutika pamoja na muda na nishati, kwa ajili ya burudani.

Uchu unaoendelezwa wa kupenda burudani za anasa huonesha shauku ya kina ya Roho/moyo. Lakini wale wanaokunywa kwenye chemchemi hii ya anasa za kidunia, watapata kuwa kiu yao ya nafsi bado haijatosheka. Wanadanganywa; wanachanganya burudani inayoleta vicheko, na kuwa na furaha moyoni; na msisimko unapokoma, wengi huzama ndani ya kina sonona, kukosa matumaini na kuvunjika moyo. Tazama ni wazimu wa kiasi gani, ni upumbavu wa jinsi gani kuiacha “Chemchemi ya maji ya uzima” kwa ajili ya “mabirika yaliyovunjika” ya raha za kiulimwengu! Tunahisi kwa kina kuhusu kila hatari inayozunguka nafsi za vijana katika siku hizi za mwisho; Je, kwanini basi wale wanaotujia kwa ajili ya elimu, na

familia ambazo zinavutiwa na shule zetu, waasiondolewe, kwa kadri inavyowezekana, ili kuwa mbali na mivuto hii ya kushawishi na kukatisha tamaa maadili mazuri? {FEsw 422.2}

Katika kuchagua maeneo ya kuweka shule zetu, hatudai hata kwamba sisi tutawaweka vijana nje ya kufikiwa na majaribu. Shetani ni mfanyakazi mwenye bidii sana, na hachoki kupanga njia za kuharibu kila akili iliyo wazi kwa mapendekezo yake. Yeye anapokutana na familia na watu binafsi huendana na mazingira/hali za watu hawa, akiyanyumbulisha majaribu yake kutokana na mielekeo na udhaifu wao. Lakini katika miji mikubwa uwezo wake juu ya akili ni mkubwa zaidi, na nyavu zake kwa ajili ya kunasa miguu ya watu waliojiziuka, na wasio na ufahamu ni nyingi zaidi, nao baada ya kunaswa, wanashindwa kujitoa kwenye mtego wake. Kuhusiana na shule zetu, mazingira yenye eneo la kutosha yanapaswa yawekwe. Kuna wanafunzi ambao hawajawahi kujifunza uchumi, na hutumia kila shilingi waliyoweza kupata. Pesa hizo zinazotumiwa ovyo ovyo, hazipaswi kukatwa kutoka kwenye pesa za kujipatia elimu. Vibarua vnapaswa kutolewa kwao, kisha masomo yao ya vitabu yanapaswa kuchanganywa dhidi ya mafunzo kazi za stadi mbambali, na kuepuka tabia mbaya za ubaradhifu wa pesa (kutumia pesa ovyo ovyo). Hebu na ajifunze kuthamini uhumuhimu wa kujisaidia wenyewe. {FEsw 422.3}

Kunapaswa kuwa na vibarua vya kazi kwa wanafunzi wote, iwe wanaweza kulipa au la; nguvu za kimwili na kiakili zinapaswa kupewa ulinganifu sawia. Wanafunzi wanapaswa kujifunza kulima ardhi; kwa maana hii itawaleta katika mawasiliano ya karibu na asili (kilimo ni ABC ya Elimu). {FEsw 423.1}

Kuna usafishaji, ushawishi wa kutiisha katika asili ambayo inapaswa kuzingatiwa katika kuchagua eneo mahalia la shule. Mungu anaizingatia kanuni hii katika kuwafunza watu kwa ajili ya kazi Yake. Musa alitumia miaka arobaini katika nyika la Midiani. Yohana Mbatizaji asingeweza **kufaa** kwa wito wake mkuu kama mtangulizi wa Kristo kwa kushirikiana na watu wakuu wa taifa katika shule za Yerusalemu. Alienda jangwani, ambapo desturi na mafundisho ya wanadamu hayangeweza kufinyanga akili yake, na mahali ambapo angeweza kushikilia ushirika usiozuilika pamoja na Mungu. {FEsw 423.1}

Wakati watesi wa Yohana, mwanafunzi mpendwa, walipotafuta kuinyamazisha sauti yake na kuharibu ushawishi wake kati ya watu, walimpeleka uhamishoni, huko kwenye Kisiwa cha Patmo. Lakini hata hivyo hawakuweza kumtenganisha na Yule Mwalimu wa Kimbingu. Katika Patmo iliyo ya upweke, Yohana angeweza kusoma mambo ambayo Mungu aliumba. Katika miamba iliyochongoka na rafu, katika maji yaliyozunguka kisiwa, aliweza kuona ukuu na uweza wa Mungu. Na wakati akiwa anazungumza na Mungu, na kusoma kitabu cha asili, akasikia sauti ikisema naye, sauti ya Mwana wa Mungu. Yesu alikuwa mwalimu wa Yohana kwenye Kisiwa cha Patmo, na hapo akafunua kwa mtumishi Wake mambo ya ajabu ambayo

yangetokia kwa wakati ujao. {FEsw 423.2}

Mungu angependa tuthamini baraka Zake katika kazi Zake za Uumbaji. Kuna watoto wangapi katika miji yenye watu wengi ambao hata hawajaona doa la majani mabichi kuweka miguu yao hapo. Kama wangeweza kupewa elimu mashambani/vijijini, katikati ya uzuri, amani, na usafi wa asili, ingeonekana kwao kwamba hapo mahali pa karibu zaidi na Mbinguni. Mahali ambapo kuna maeneo yaliyotulia, ambayo yako mbali zaidi na desturi mbovu, mazoea na misisimko ya ulimwengu, na karibu kabisa na moyo wa asili (nature), Kristo hufanya uwepo Wake hapo kuwa halisi kwetu, na kishaanazungumza na Roho zetu juu ya amani Yake na upendo. {FEsw 424.1} — *Special Testimonies on Education, Mei 11, 1896.*

Sura ya 52

UMUHIMU WA UTAMADUNI WA KIMWILI

Utamaduni wa kimwili ni sehemu muhimu ya mbinu zote sahihi za elimu. Vijana wanahitaji kufundishwa jinsi ya kukuza nguvu za mwili wao, jinsi ya kuhifadhi nguvu hizi katika hali bora, na jinsi gani kuzifanya ziwe na manufaa katika majukumu ya maisha kwa maisha. Wengi wanafikiri kuwa mambo haya si sehemu ya kazi za shule; lakini hili ni kosa. Masomo muhimu yanayomstahilisha mtu awe mwenye manufaa katika utendaji wa shughuli za kila siku maishani, lazima yafundishwe kwa kila mtoto nyumbani na kwa kila mwanafunzi shuleni. {FEsw 425.1}

Mahali pa kuanzia mafunzo ya mwili au kazi za mikono, ni nyumbani na mtoto mdogo. Wazazi wanapaswa kuweka msingi wa afya, na maisha ya furaha. Moja ya maswali ya kwanza kuamuliwa ni yale ya chakula mezani mwao; kwa maana hili ni

msingi wa maendeleo ya watoto wadogo na afya ya familia inategemea. Ujuzi katika maandalizi ya chakula ni muhimu sana, basi, ni muhimu kwamba kiwango na kiasi cha chakula kiwe kile ambacho kinafaa? {FEsw 425.2}

Sote tunahitaji kutumia hekima katika kula. Ikiwa chakula kingi kinaliwa kuliko tumbo linavyoweza kumeng'anya na kutunza, lundo la chakula hujilimbikiza na kuoza ndani ya tumbo, na kusababisha pumzi ya mdomo inayokera watu (kunuka) na ladha mbaya katika mdomo. Nguvu muhimu ni zinatindikiwa katika jitihada za kutupilia mbali chakula cha ziada, na ubongo huibiwa nguvu ya neva (mishipa ya fahamu). Chakula pungufu kingeweza kurutubisha mfumo, na kupotezwa kwa nishati kusingekuwepo katika kufanya kazi kupita kiasi. Hata hivyo chakula cha afya, yaani kisichokobolewa wala kusindikwa kinapaswa kutumiwa/kuliwa, nacho kiwe cha kutosha kwa wingi na ubora katika kuulisha mfumo. Tukifuata kanuni ya Biblia isemayo, "Basi, mlapo, au mnywapo, au mtendapo neno lo lote, fanyeni yote kwa Utukufu wa Mungu." hatutaendekeza hamu ya kula kwa gharama ya afya ya miili yetu, ambayo ni wajibu wetu kuihifadhi. {FEsw 425.3}

Kila mama anapaswa kuweka umakini, kwamba watoto wake wanaiielewa wenyewe miili yao wenyewe, na jinsi ya kuitunza. Anapaswa kueleza ujenzi na matumizi ya misuli tuliyopewa na Baba yetu wa Mbinguni Mwenye Fadhili. Sisi ni kazi Yake Mungu, na neno Lake linatangaza kwamba sisi "tumeumbwa kwa jinsi ya ajabu na kushangaza" Ametayarisha makao haya ya kuishi kwa akili (miili yetu ni makao); "imetengenezwa kwa njia ya kuamsha udadisi," hekalu ambalo Bwana Mwenyewe amelistahilisha kwa ajili ya kukaa kwa Roho Wake Mtakatifu. Akili humdhibiti mtu (akili ndiyo inatawala mwili wote). Matendo yetu yote, mazuri au mabaya, yana chanzo chake katika akili. Ni akili ndiyo inayomwabudu Mungu, na kutushirikisha na viumbe vya Mbinguni. [Walakini wengi hutumia maisha yao yote bila kuwa na akili au kujipatia ujuzi kuhusu sanduku hili {yaani ubongo}, ambalo lina hazina hii](#) {FEsw 425.4}

Viungo vyote vya mwili ni watumishi wa akili, na neva ni matarishi/wajumbe ambao hupeleka amri zake kwenye kila sehemu ya mwili, na kuongoza mwendo wa mashine hai ambayo ni mwili wetu. Mazoezi ni msaada muhimu kwa maendeleo ya kimwili. Yanaharakisha mzunguko wa damu, na kutoa afya au toni kwa mfumo. Ikiwa misuli inaachwa bila kutumiwa, hivi karibuni itakuwa dhahiri kwamba damu hatoi lishe ya kutosha kwenye misuli hiyo. Basi badala ya hiyo misuli kuongezeka kwa ukubwa na nguvu, itapoteza uimara na unyumbulifu wake, na kuwa laini na dhaifu. Kutofanya kazi sio sheria ambayo Bwana aliweka ndani ya mwanadamu mwili. Kutenda kwa usawa kwenye viungo vyote (sehemu zote)- ubongo, mfupa, na misuli, - ni muhimu kwa maendeleo kamili na yenye afya kwa mwili mzima wa binadamu (kwa kiumbe chote). {FEsw 426.1}

Kazi ya mafunzo ya kimwili, iliyoanza nyumbani, inapaswa kuwa ikiendelea mashuleni. Ni mpango wa Muumba kwamba mwanadamu atajijua mwenyewe;

lakini mara nyingi sana katika kutafuta maarifa ya vitabuni, muundo huu umepotea. Wanafunzi hutumia miaka kwa masomo ya mistari tofauti; wanaweka umakini mwingi katika masomo ya sayansi na ya vitu katika ulimwengu wa asili; wanakuwa na akili juu ya masomo mengi, lakini hawajitambui mwenyewe (fiziolojia ya mwili inavyofanya kazi). Wanaangalia mwili wa mwanadamu ulio nyeti kana kwamba ni kitu ambacho kitajitunza chenyewe; na yale ambayo ni muhimu kwa kiwango cha juu zaidi—yaani maarifa ya miili yao wenyewe—yanapuuzwa. {FEsw 426.2}

Kila mwanafunzi anapaswa kuelewa jinsi ya kutunza mwili wake kwa ufanisi ili kuhifadhi hali bora zaidi ya afya, kupinga udhaifu na ugonjwa; na ikiwa ugonjwa unatokea kwa sababu yoyote ile, au ajali itokee, basi yeye apaswa kujua jinsi ya kukutana na dharura za kawaida bila ya kumwita daktari, na kujitwalia dawa zake zenye sumu. {FEsw 426.3}

Bwana Mwenyewe amesema juu ya somo hili la utunzaji wa mwili. Anasema katika Neno Lake, “Mtu akiharibu hekalu la Mungu, huyo Mungu atamharibu; kwa maana hekalu la Mungu ni takatifu, ambalo ninyi ni hekalu.” 1Wakorintho 3:17. Andiko hili linaamuru kutunza mwili kwa uangalifu, na kulaani ujinga au uzembe au upuuziaji wa aina yoyote. Na tena: “Hamjui ya kuwamiili yenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, mliyepewa na Mungu, nanyi si mali yenu wenyewe? Kwa maana mmenunuliwa kwa thamani kubwa; basi mtukuzeni Mungu katika miili yenu, na katika Roho zenu, ambazo ni za Mungu.” “Basi, mlapo, au mnywapo, au mtendapo neno lolote, fanyeni yote kwa Utukufu wa Mungu.” 1Wakorintho 6:19, 20; 10:31. {FEsw 427.1}

Utunzaji wa miili yetu kwa uangalifu na akili, unatokana na Baba yetu wa Mbinguni, ambaye “aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee; bali awe na uzima wa milele.” Sisi binafsi ni mali ya Kristo, Mali Yake Mwenyewe iliyonunuliwa Naye. Inatakiwa kila mmoja wetu ahifadhi afya na nguvu zetu kwa kujizoea katika kuwa na kiasi katika mambo yote. Uchu wa chakula na tamaa za mwili lazima zithibitiwe, ili kwamba kupitia kwazo hatutadhoofisha au kulitia unajisi hekalu la kibinadamu la Mungu. {FEsw 427.2}

Chochote kinachopunguza nguvu ya mwili hudhoofisha akili, na hilo kuleta ukungu akilini, unaofanyaa akili isiweze kutofautisha kati ya mema na mabaya, kati ya sahihi na makosa. Kanuni hii inaonyeshwa katika kisa cha Nadabu na Abihu. Mungu aliwapa kazi takatifu zaidi ya kufanya, akawaruhusu hao wamkaribie Yeye katika utumishi wao ulioagizwa; ila wao walikuwa na mazoea ya kunywa divai, nao wakaingia katika ibada takatifu katika Patakatifu wakiwa wenye akili zilizochanganyikiwa. Kulikuwa na moto mtakatifu, ambao uliwashwa na Mungu Mwenyewe; lakini wao walitumia moto wa kawaida (mgeni na ule wa Mungu) juu ya vyetezo vyao, walipotoa uvumba ili upande kama harufu tamu/nzuri pamoja na maombi ya watu wa Mungu. Kwa sababu akili zao zilikuwa zimegubikwa na kujifurahisha na kuendekeza mambo yasiyo matakatifu, wakapuuzia matakwa ya

Bwana; “Moto ukatoka kwa Bwana, ukawateketeza nao wakafa mbele za BWANA.”
{FEsw 427.3}

Mungu alikataza matumizi ya divai kwa makuhani wanaohudumu katika Patakatifu Pake kwenye Madhabahu, na amri hiyo hiyo ingetolewa dhidi ya tumbaku, kama matumizi yake yangellijulikana siku hizo; kwa kuwa, hii pia, ina ushawishi wa kupooza/kudhoofisha ubongo. Na zaidi mbali ya kutia ukungu akili, ni najisi na inachafua mwili. Hebu kila mtu na apinge kishawishi cha kutumia mvinyo, tumbaku, nyama, chai, au kahawa. Uzoefu umeonyesha kazi bora zaidi inaweza kukamilishwa bila vitu hivi vyenye madhara. {FEsw 428.1}

Hebu ivutiwe sana kwenye akili za vijana na wazazi wote wawil na walimu, kwamba Kristo amelipa gharama isiyo na kikomo kwa ajili ya ukombozi wetu. Hajaacha kufanya jambo lolote lile litakalotusaidia kurudi kwenye uaminifu Kwake Yeye. Anataka tukumbuke sisi ni watoto wa Mfalme, na kuzaliwa kwetu kifalme na hatima yetu kuu kama wana na binti za Mungu, na kuwa na heshima ya kweli kwetu binafsi (kwa kuanza na kuiheshimu miili yetu). Anapenda nguvu zetu zote ziendele vyema, na kuwekwa katika hali iliyo bora kabisa, ili aweze kutujza neema Yake na kisha atutumie katika utumishi Wake, akitufanya watenda kazi pamoja Naye kwa ajili ya wokovu wa Roho. {FEsw 428.2}

Ni wajibu wa kila mwanafunzi, kila mtu binafsi, kufanya yote katika uwezo wake, katika kuutoa mwili wake kwa Kristo, hekalu lililosafishwa, kamilifu kimwili, na pia kimaadili liwe huru kutokana na unajisi, —makao yanayofaa kwa ajili Uwepo wa Mungu ndani yake. {FEsw 428.3}—[Special Testimonies on Education, Mei 11, 1896.](#)

Sura ya 53

ELIMU YA JUU YA KWELI

Mungu ni upendo. Uovu uliomo duniani hautoki kwenye mikono Yake, lakini hutoka kwa adui yetu mkuu, ambaye kazi yake daima ni kumharibia mwanadamu, kudhoofisha na kupotosha uwezo wake. Lakini Mungu hakutuacha katika uharibifu ulioletwa na anguko. Kila kitivo kimewekwa ili kiweze kufikiwa na Baba yetu wa Mbinguni, ili wanadamu. kupitia juhudi zilizoelekezwa vyema, waweze kupata tena ukamilifu wao wa kwanza, na kusimama wakiwa wakamilifu katika Kristo. Katika

kazi hii Mungu anatutazamia tufanye sehemu yetu. Sisi ni Wake—mali Yake iliyonunuliwa/aliyoinunua. Familia ya kibinadamu ilimgharimu Mungu na Mwanawe Yesu Kristo bei isiyo na kikomo. {FEsw 429.1}

Mkombozi wa ulimwengu, Mwana pekee wa Mungu, kwa utii mkamilifu kwa sheria, kwa maisha na tabia yake, alikomboa kile ambacho kilipotea katika anguko, na kufanya iwezekane kwa mwanadamu kutii hiyo sheria takatifu ya haki ambayo Adamu aliivunja. Kristo hakubadilisha Uungu Wake kwa ubinadamu, lakini aliweka ubinadamu na Uungu kwa pamoja; na katika ubinadamu Aliishi sheria kwa niaba ya familia ya mwanadamu. Dhambi za kila mtu atakayempokea Kristo ziliwekwa kwenye akaunti Yake, na Ameitimiza na kuiridhisha kikamilifu haki ya Mungu. {FEsw 429.2}

Mpango wote wa ukombozi unaonyeshwa katika maneno haya ya thamani: “Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.” Kwa hakika Kristo aliibeba adhabu ya dhambi za ulimwengua, ili haki yake ihesabiwe kwa wenye dhambi, na kupitia toba na imani watu wanaweza kuwa kama Yeye katika utakatifu Wake wa tabia. Anasema, “Ninabebana kuchukua hatia ya dhambi za mtu huyo.” Acha Mimi (Yesu) Nichukue adhabu na mwenye dhambi anayetubu anayesimama mbele Zako awe bila hatia.” Punde pale mwenye dhambi anapomwamini Kristo, anasimama mbele ya macho ya Mungu bila kuhukumiwa; kwa maana haki ya Kristo ni yake: tii mkamilifu wa Kristo, Unawekwa kwake. Lakini lazima yeye ashirikiane na uweza wa Mungu, na kuweka juhudi zake za kibinadamu kuitiisha dhambi, na kusimama akiwa kamili katika Kristo. {FEsw 429.3}

Fidia iliyolipwa na Kristo inatosha kwa ajili ya wokovu wa watu wote; lakini itawasaidia wale tu watakaokuwa viumbe vipya katika Kristo Yesu, raia waaminifu wa ufalme wa milele wa Mungu. Mateso hayatawakinga na adhabu wale wasiotubu, wenye dhambi wasio waaminifui. {FEsw 430.1}

Kazi ya Kristo ilikuwa kumrudisha mwanadamu katika hali yake ya asili ile aliyomuumba nayo kwanza, kumponya yeye, kwa uwezo wa Mungu, kutoka kwa majeraha na michubuko iliyofanywa na dhambi. Sehemu ya mwanadamu ni kushika kwa imani wema wa Kristo, na kushirikiana na wakala wa Kiungu katika kutengeneza tabia ya haki; ili Mungu amwokoe mwenye dhambi, na wakati huo huo awe ametenda haki na uadilifu, na sheria Yake ya haki imethibitishwa na kuondolewa lawama. {FEsw 430.2}

Bei iliyolipwa kwa ajili ya ukombozi wetu inaweka wajibu mkubwa juu ya kila mmoja wetu. Ni wajibu wetu kuelewa kile ambacho Mungu anataka kuktoka kwetu, na vile angetaka tuwe. Waelimishaji wa vijana wanapaswa kutambua wajibu ulio juu yao, na kufanya wawezavyo kuondoa kasoro za kimwili, kiakili au kimaadili.

Wanapaswa kulenga kwenye ukamilifu katika hali zao wenyewe, ili wanafunzi wawe na mfano ulio sahihi. {FEsw 430.3}

Walimu wanapaswa kufanya kazi kwa uangalifu. Wale ambao mara nyingi huwa na Mungu katika maombi, wana malaika watakatifu karibu nao. Angahewa inayozingira nafsi zao ni safi na takatifu; kwa maana nafsi zao zote zimejaa na ushawishi wa utakaso wa Roho wa Mungu. Wanapaswa kuwa wanafunzi kila siku katika shule ya Kristo, ili wawe walimu chini ya Mwalimu mkuu. Lazima wajifunze kwa Kristo, na wawe kitu kimoja pamoja Naye katika kazi ya kufundisha akili, kabla ya kuwa na ufanisi walimu katika elimu ya juu—ujuzi wa Mungu. {FEsw 430.4}

Mungu anadhihirishwa katika Neno Lake. “Kwa kuwa yote yaliyotangulia kuandikwa yaliandikwa ili kutufundisha sisi; ili kwa saburi na faraja ya maandiko tupate kuwa na tumaini.” “Na tena, Enyi Mataifa yote, msifuni Bwana; Enyi watu wote, mhimidini. Na tena Isaya anena, Litakuwako shina la Yese, Naye aondokeaye kuwatawala Mataifa; Ndiye Mataifa watakayemtumaini..” {FEsw 430.5}

Elimu ya Kweli ya juu ndiyo huwafanya wanafunzi kufahamiana na Mungu na Neno Lake, na kuwastahilisha kwa uzima wa milele. Ilikuwa katika kuyaweka maisha haya katika mfikio wao binadamu, Ndiyo maana Kristo alijitoa Mwenywe kama dhabihu kwa ajili ya dhambi. Kusudi Lake la upendo na rehema linaonyeshwa katika sala Yake Wanafunzi Wake. “Maneno hayo aliyasema Yesu; akainua macho yake kuelekea Mbinguni, akasema, Baba, saa imekwisha kufika. Mtukuze Mwanao, ili Mwana Wako Naye akutukuze Wewe; kama vile ulivyompa mamlaka juu ya wote wenye mwili, ili kwamba wote uliomba awape uzima wa milele. Na uzima wa milele ndio huu, Wakujue Wewe, Mungu wa pekee wa Kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma.” Kila mwalimu ya vijana anapaswa kufanya kazi kwa kupatana na sala hii, kuwaongoza wanafunzi kwa Kristo. {FEsw 431.1}

Yesu anaendelea, akionyesha kujali Kwake wale walio Wake: “Wala mimi simo tena ulimwenguni, lakini hawa wamo ulimwenguni, Nami naja Kwako. Baba mtakatifu, kwa Jina Lako ulilonipa uwalinde hawa, ili wawe na umoja kama Sisi tulivyo. Nilipokuwapo pamoja nao, Mimi naliwalinda kwa Jina Lako ulilonipa, nikawatunza; wala hapana mmojawapo wao aliyepotea, ila yule mwana wa upotevu, ili andiko litimie. Na sasa naja Kwako; na Maneno haya nayasema ulimwenguni, ili wawe na furaha Yangu imetimizwa ndani yao. Mimi nimewapa Neno Lako; na ulimwengu umewachukia; kwa kuwa wao si wa ulimwengu,....” {FEsw 431.2}

Hebu tuseme kwamba tumeidaka ile Roho iliyopumua ombi hili ambayo ilipaa Mbinguni. Kristo hapa anaonyesha mbinu na msukumo upi Alikuwa akiutumia kuwazuia wanafunzi Wake kutoka kwa mazoea ya kidunia, taratibu, kanuni, na tabia: “Nimewapa Neno Lako; na ulimwengu umewachukia wao, kwa sababu wao si wa ulimwengu.” Matendo yao, maneno yao, Roho zao, hazina mapatano na ulimwengu, “kama mimi nisivyo wa ulimwengu.” Na Mwokozi anaongeza tena,

“Mimi siombi kwamba uwatoe katika ulimwengu; bali uwalinde na yule mwovu. Watoto na vijana wanapaswa kupata elimu katika mstari ambao Kristo ameonyesha hapa, ili wapate kutengwa na dunia. {FEsw 431.3}

“Uwatakase kwa ile Kweli; Neno Lako ndiyo Kweli.” Neno la Mungu linapaswa kufanywa kuwa nguvu kuu ya kuelimisha. Wanafunzi watajuaje Ukweli, isipokuwa kwa kusoma Neno kwa karibu, kwa bidii, na kwa kudumu? Hapa kuna kichocheo kikuu, msukumo uliofichwa ambyo huhuisha nguvu za kiakili na kimwili, na kuyaelekeza maisha katika njia sahihi. Hapa kwenye Neno kuna hekima, mashairi, historia, wasifu, na falsafa ya kina zaidi. Huu hapa ni utafiti ambao huhuisha akili katika maisha za nguvu na afya, na kuiamsha kwa uzoefu wa juu zaidi. Haiwezekani kabisa kuisoma Biblia kwa Roho ya unyenyekevu, inayofundishika, na kisha akili isikuzwe au kuimarika. Wale wanaojua vyema hekima na kusudi la Mungu kama lilivyofunuliwa katika Neno Lake, wanakuwa wanaume na wanawake wenye nguvu za kiakili; na wanaweza kuwa watendakazi wenye ufanisi pamoja na Mwalimu mkuu, Yesu Kristo. {FEsw 432.1}

“Kama vile ulivyonituma Mimi ulimwenguni, Nami vivyo hivyo naliwatuma hao ulimwenguni.” Kuna kazi ya kufanywa kwa ajili ya ulimwengu, na Kristo anawatuma wajumbe Wake, ambao wanapaswa kuwa watenda kazi pamoja Naye Mwenyewe. Kristo amewapa watu Wake Maneno ya Kweli, na wote wanaitwa kuchukua sehemu ya kuwafanya wajulikane ulimwenguni. {FEsw 432.2}

“Na kwa ajili yao Mimi najiweka wakfu, ili wao pia waweze kutakaswa kwa ile Kweli.” Walimu wanaweza kudhani wanaweza kuichomekeza/kuifundisha hekima yao wenyewe, wakihifadhi kutokamilika au mapungufu yao ya kibinadamu; bali Kristo, Mwalimu wa Kimungu/Mbinguni, ambaye kazi Yake ni kumrejeshea mwanadamu kile ambacho kilipotea wakati wa anguko, alijitakasa Mwenyewe kwa ajili ya kazi Yake. Yeye alijitoa kwa Mungu kuwa dhabihu kwa ajili ya dhambi, akitoa uhai Wake kwa ajili ya uzima wa dunia. Alinuia kuwa wale aliowalipa vile, ile fidia ya gharama kubwa watakaswe “kupitia ile Kweli,” na amewawekea wao mfano. Mwalimu huwa vile angetaka wanafunzi Wake wawe. Hakuna utakaso kando na ile Kweli, -Neno. Kisha ni jinsi gani ilivyo muhimu kwamba hili lipaswe kueleweka kwa kila mtu! {FEsw 432.3}

Ombi la Kristo linajumuisha/linakumbatia zaidi ya wale waliokuwa Wanafunzi Wake wakati huo ; linawazoa/linawachukua wale wote wanaopaswa kumpokea kwa imani. Yeye anasema, “Wala siwaombe hawa peke yao, bali na hao watakaopenda kuniamini Mimi kwa sababu ya neno lao; ili wote wawe kitu kimoja; kama Wewe, Baba, ulivyo ndani Yangu, Nami ndani Yako, ili hao nao wawe ndani Yetu; ulimwengu upate kusadiki ya kuwa Ndiwe uliyenituma. Nami Utukufu ule ulionipa nimewapa wao; ili wawe na umoja kama sisi tulivyo umoja: Mimi ndani yao, Nawe ndani yangu, ili wapate kukamilishwa katika umoja; na ili ulimwengu ujue ya kuwa Ndiwe uliyenituma, na umewapenda wao, kama ulivyonipenda Mimi.” {FEsw

Ajabu hakika, Maneno ya ajabu, yaani yako juu zaidi ya ufahamu wetu! Je, walimu katika shule zetu wataelewa hili? Je, watachukua Neno la Mungu kama kitabu cha somo kinachoweza kuwahakimisha hata kuufikia ule wokovu? Kitabu hiki ni sauti ya Mungu akizungumza nasi. Bibilia inatufunulia/inatufungulia sisi Maneno ya uzima; kwa maana inatufanya sisi tumfahamu Kristo ambaye Ndiye uzima wetu. Ili kuwa na imani ya Kweli ndani yetu, imani ile yenye kudumu katika Kristo, ni lazima zizi tumjue jinsi ile tu anavyowakilishwa katika Neno. Imani inaamini kabisa. Sio suala la kufaa na kuanza, kulingana na msukumo na hisia ya saa/muda; lakini ni kanuni ambayo ina msingi wake ndani Yesu Kristo. Na imani lazima iwekwe katika mazoezi ya mara kwa mara kupitia kusoma kwa uadilifu, uvumilivu na kudumu katika lile Neno. Ndipo Neno linakuwa wakala hai; na kisha tunatakaswa kupitia ile Kweli. {FEsw 433.2}

Roho Mtakatifu ametolewa kwetu kama msaada katika kujifunza Neno. Yesu anaahidi, “Lakini huyo Msaidizi, huyo Roho Mtakatifu, ambaye Baba atampeleka kwa Jina Langu, atawafundisha yote, na kuwakumbusha yote niliyowaambia.” Wale walio chini ya mafunzo ya Roho Mtakatifu wataweza kufundisha Neno kwa akili. Na wakati inafanywa kuwa kitabu cha mafunzo (Somo la kujifunza, uchunguzi), kwa maombi ya dhati, yenye usadikisho wa bidii kwa ajili ya mwongozo wa Roho Mtakatifu, na kujisalimisha kikamilifu ili moyo utakaswe kupitia ile Kweli, basi litatimiza (Neno) yale yote ambayo Kristo ameyaahidi. Matokeo wa kujifunza hivyo Biblia itakuwa akili zilizosawazishwa vizuri; kwani nguvu za mwili, akili na maadili zitaendelezwa/zitakuzwa kwa upatanifu. Hapo hakutakuwa na ulemavu au kupooza katika maarifa ya kiroho. uelewa utahuishwa; hisia zitaamshwa; busara na dhamiri zitafanya kuwa nyeti; huruma, mihemko na hisia vitatakaswa; na mazingira bora ya kimaadili yataundwa; na uwezo mpya wa kupinga majaribu utatolewa. Na walimu na wanafunzi kwa pamoja, watakuwa watendaji hai na dhati, walio na bidii katika kazi ya Mungu. {FEsw 433.3}

Lakini kuna tabia kwenye upande wa walimu wengi, ya kutokuwa na ukamilifu/umakini katika elimu ya dini (elimu ya kiroho). Hao wenyewe wanaridhika na utumishi wa moyo nusunu, wakimtumikia Bwana ili kuepuka tu adhabu ya dhambi. Moyo wao ulio nusu-nusu unaathiri mafundisho yao (na kufundisha kwao). Uzoefu ambao hata wao wenyewe hawana matamania nao, hawana shauku au wasiwasi kuona wanafunzi wao wakipata faida. Kile ambacho wao wamepewa kama baraka kimetupwa kando kama kipengele cha hatari. Ziara au ugeni wa Roho Mtakatifu kwao hukutana na maneno kama yale ya feliki kwa Paulo, “Unaweza kwenda sasa. Nitakapokuwa na msimu unaofaa, nitakuia.” Baraka zingine wao huzitamani sana; bali kile ambacho Mungu Yupu tayari kutoa zaidi kuliko baba anavyotamani kuwapa watoto wake zawadi nzuri; Huyu Roho Mtakatifu, ambaye

hutolewa kwa wingi kulingana na utimilifu usio na kikomo wa Mungu, na ambaye, ikiwa atapokelewa, basi ataleta baraka zingine zote ndani ya mabehewa Yake ya treni, —ni maneno gani yanayotesheleza ambayo mimi ningeweza kuyatumia ili kuelezea vile ilivyo {kile kimefanywa tayari} kwa kurejelea hili jambo? Mjumbe wa Mbinguni amechukizwa, amesukumwa nyuma kwa ajili ya dhamira/nia hii iliyogangamaa (yenye ukaidi). “hivyo, wewe unaweza kwenda mpaka hapo tu na wanafunzi wangu, lakini usisonge zaidi ya hapo. Hatuhitaji shauku katika shule yetu, hatuhitaji kuisisimuka. Tumeridhika zaidi kabisa, kufanya kazi pamoja na wanafunzi sisi wenyewe.” Mambo yako hivyo basi, licha ya yale ambayo yamefanywa na mjumbe wa neema wa Mungu, Roho Mtakatifu. {FEsw 434.1}

Je, walimu katika shule zetu hawajaingia katika hatari ya kukufuru, ile ya kumshtaki Roho Mtakatifu wa Mungu kuwa ni nguvu ya udanganyifu, na hivyo kusababisha ushabiki. Wako wapi waelimishaji wanaochagua theluji ya Lebanoni itokayo katika mwamba wa kondeni, au katika mwamba wa maji baridi, yanayotiririka kutoka mahali pengine, badala ya yale maji yenye weusi na ukungu ya bondeni? ((Yer 18:14)) Mfululizo wa mvua kutoka kwenye maji ya uzima yamewajia ninyi huko Battle Creek. Kila mvua bubujiko la ushawishi wa Bwama uliowekwa wakfu; lakini ninyi humkutambua ndiyo hivyo. Badala ya kunywa/kuyabugia maji haya ya mito ya wokovu, yalitolewa bure na kwa ukarimu mwingi kupitia ushawishi wa Roho Mtakatifu, ninyi mkageuka mifereji ya maji machafu yanayotoka chooni (sewer), na kujaribu kukidhi kiu yenu kwa maji machafu ya sayansi za kibinadamu. Matokeo yake ni mioyo iliyokauka na yenye kiu shuleni na kanisani. Wale ambao wameridhika na mambo ya kiroho kidogo (ukiroho mdogo) wameenda mbali katika kutojistahilisha wenyewe katika kuthamini mwendo wa kina wa Roho wa Mungu. Lakini mimi natumai kuwa walimu bado hawajauvuka mstari ambao sasa wamegubikwa na ugumu wa moyo na upofu wa nia na akili. Ikiwa wanatembelewa tena na Roho Mtakatifu, natumaini kuwa wao hawataita haki kuwa dhambi, na dhambi ndiyo haki. {FEsw 434.2}

Kuna haja ya wongofu wa moyo, miongoni mwa walimu. Mabadiliko ya Kweli ya mawazo na mbinu za kufundisha yanahitajika ili kuwaweka mahali ambapo watakuwa na uhusiano wa kibinafsi na Mwokozi aliye hai. Ni jambo moja kuidhinisha kazi ya Roho Mtakatifu katika uongofu, ila ni jambo jingine katika kumkubali Yeye Roho kama ndiye wakala anayekemea na kusahihisha, anayewaita watubu. Ni muhimu kwamba walimu na wanafunzi pamoja, hawaidhinisha ile Kweli tu, lakini watakuwa na maarifa ya kina, na ya vitendo kuhusiana na jinsi Roho anavyofanya shughuli Zake. Tahadhari Zake zinatolewa kwa sababu ya ukafiri, yaani kutoamini kwa wale ambao wanadai kuwa ni Wakristo. Mungu atakuja karibu na wanafunzi kwa sababu wanapotoshwa na waelimishaji ambao wameweka usadikisho wao kwao (wanawaamini); lakini walimu na wanafunzi, wote pamoja, wanahitaji kuwa na uwezo wa kutambua sauti ya Mchungaji. {FEsw 435.1}

Wewe ambaye kwa muda mrefu umepoteza Roho ya maombi, omba, omba, kwa bidii, “Uionee sikitiko sababu ya mateso yako; lionee huruma kanisa; Mwonee huruma kila muumini, Ee Baba wa rehema. Tunaomba uondoe kutoka kwetu kila kitu kinachotia unajisi, utunyime Utakacho; lakini usituondolee Roho Wako Mtakatifu.” {FEsw 435.2}

Kuna watu, na daima watakuwako watu, wasioenenda kwa busara, ambao, ikiwa maneno ya shaka au kutoamini yatazungumwa, yatatupilia mbali usadikisho na watachagua kufuata mapenzi yao wenyewe; na kwa sababu ya mapungufu yao, Kristo ameshutumiwa. Watu maskini wenye ukomo wameuhukumu ukarimu na utajiri wa kumwagwa kwa Roho Mtakatifu wa thamani, na kutoa hukumu juu Yake, kama vile Wayahudi walipotoa hukumu juu ya kazi ya Kristo. Hebu na ieleweke katika kila taasisi ya Marekani kwamba ninyi hamjaagizwa kuisimamia au kuiongoza kazi ya Roho Mtakatifu, na kumwambia jinsi ambavyo anapaswa kujiwakilisha Mwenyewe. Umekuwa na hatia ya kufanya hivi. Ninasihi Bwana akusamehe, ndiyo maombi yangu. Badala ya kukandamizwa na kusukumwa nyuma, kama ambavyo imekuwa, Roho Mtakatifu ni lazima akaribishwe na uwepo Wake uwepo (utiwe moyo). Unapojitakasa kupitia utii kwa Neno, Roho Mtakatifu atakupa mpenyo kidogo au macho ya kuona mambo ya Mbinguni. Unapomtafuta Mungu kwa kujidhili na bidii, maneno ambayo umezungumza kwa lafudhi ya baridi yenye kuganda yatawaka moto ndani ya moyo wako; basi ile Kweli haitadorora au kudhoofika katika ndimi zenu. {FEsw 435.3}

Maslahi ya milele yanapaswa kuwa kauli mbinu au mada kuu ya walimu na wanafunzi. Kuridhiana na ulimwengu kunapaswa kulindwa vikali. Walimu wanahitaji kutakaswa kupitia ile Kweli, na jambo la muhimu n amaana sana liwe ni kuongoka kwa wanafunzi wao, ili waweze kuwa na moyo na maisha mapya. Lengo la Mwalimu Mkuu ni kurejeshwa kwa sura ya Mungu katika nafsi, na kila mwalimu ndani ya shule zetu anapaswa kufanya kazi kulingana na kusudi hili. {FEsw 436.1}

Waalimu, mtegemeeni Mungu, na songeni mbele, “Neema Yangu yatosha kwa ajili yenu” ni uhakikisho wa Mwalimu Mkuu. Pata uvuvio yaani msukumo wa maneno, na kamwe, kamwe usizungumze mashaka na kutoamini. Uwe na juhudi. Hakuna huduma ya nusunusu katika dini safi na isiyo na taka/unajisi. “Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, kwa Roho yako yote, kwa nguvu zako zote na kwa akili yako yote.” Matamania makuu kupita yaliyotakaswa yanadaiwa kwa wale ambao wanaliamini Neno la Mungu. {FEsw 436.2}

Walimu, waambieni wanafunzi wenu kwamba Bwana Yesu Kristo ametoa kila majaliwa/riziki ili wasonge mbele, wakishinda na kuendelea kushinda. Waongoze hao kutumainia ahadi hii ya Mungu: “Lakini mtu wa kwenu akipungukiwa na hekima, na aombe dua kwa Mungu, awapaye wote, kwa ukarimu, wala hakemei; naye atapewa. Ila na aombe kwa imani, pasipo shaka yo yote; maana mwenye shaka ni kama wimbi la bahari lililochukuliwa na upepo, na kupeperushwa huku na huku. Maana mtu kama yule asidhani ya kuwa atapokea kitu kwa Bwana. Mtu wa nia

mbili husita-sita katika njia zake zote..” {FEsw 436.3}

Kutoka kwa Mungu, chemchemi ya hekima, hutoa ujuzi wote ambao ni wa thamani kwa mwanadamu, yaani yote yale ambayo akili inaweza kukamata au kuhifadhi. Tunda la mti ule unaowakilisha mema na uovu halipaswi kuchumwa kwa pupa kwasababu ni pendekezo (limependekezwa) la yule ambaye hapo awali alikuwa malaika mwenye mng’ao katika Utukufu. Amesema kuwa watu wakila hilo, basi watajua mema na mabaya/uovu. Lakini wewe liache hilo tunda likae huko peke yake. Ujuzi wa Kweli hautoki wa wasioamini {makafiri} au watu waovu. Neno la Mungu ni Nuru na Kweli. Nuru ya Ukweli huangaza kutoka kwa Yesu Kristo, ambaye “humtia Nuru kila mtu ajaye duniani.” Kutoka kwa Roho Mtakatifu hutoka maarifa ya Mungu/Kiungu. Anajua kile ambacho wanadamu wanakihitaji ili kuwatia moyo katika kuendeleza amani, furaha, na utulivu hapa, katika ulimwengu huu, na kuhakikishiwa kupata pumziko la milele katika ufalme ya Mungu. {FEsw 437.1}

“Mimi Yesu nimemtuma malaika Wangu kuwashuhudia ninyi mambo haya makanisani. Mimi Ndimi niliye shina na Mzao wa Daudi yenye kung’aa ya asubuhi. Na Roho na Bibi-arusi wasema, Njoo! Naye asikiaye na aseme, Njoo. Na mwenye kiu na aje. Na yeyote anayetaka, na ayatwae maji ya uzima bure.” {FEsw 437.2}—
[Special Testimonies on Education, Juni 12, 1896.](#)

Sura ya 54

MFANO WA KRISTO KINYUME NA MAONESHU YA NJE

Kuhusiana na Bwana Yesu Kristo, ujana Wake ulikuwa ni Ushuhuda wa Bwana/Kiungu umetolewa, “Yule mtoto akakua, akaongezeka nguvu, amejaa

hekima; na neema ya Mwenyezi Mungu ilikuwa juu Yake.” Baada ya ziara kule Yerusalemu katika ujana Wake, alirudi pamoja na wazazi Wake, “akaja Nazareti, akawa chini yao.... Yesu akazidi kuendelea hekima na kimo, akimpendeza Mungu na wanadamu.” {FEsw 438.1}

Katika siku za Kristo, waelimishaji wa vijana walikuwa watu wenye kufuata utaratibu kwa ukali (formalist). Wakati wa huduma Yake, Yesu alitangaza kwa marabi, “Mwapotea, kwa kuwa hamyajui maandiko wala uweza wa Mungu.u.” Naye akawashtaki kwa “Wakifundisha mafundisho Yaliyo maagizo ya wanadamu.” Watu walifanya makazi kwenye Mapokeo ya jadi, nayo yalikuzwa, na kuheshimiwa sana kuliko Maandiko. Maneno na semi za wanadamu, na mzunguko usio na mwisho wa maadhimisho/sherehe, ulichukua sehemu kubwa ya maisha ya mwanafunzi, na hivyo elimu ambayo hutoa mafunzo ya Mungu ilipuuzwa. Waalimu wakuu walikuwa wakiendelea kupanua mambo madogo, wakibainisha kila jambo lizingatiwe kwa undani katika sherehe ya dini, na wakafanya kuadhimisha huko, liwe jambo la wajibu wa juu kabisa. Walilipa “zaka za mnanaa na bizari na jira,” huku “wakiacha mambo mazito zaidi ya sheria, mmeacha mambo makuu ya sheria, yaani, adili, na rehema, na imani.” Ndiyo jinsi walivyoleta lundo la takataka ambayo iliyaficha kutoka kwa mtazamo wa vijana, mambo muhimu ya utumishi wa Mungu. {FEsw 438.2}

Katika mfumo wa elimu hapakuwa na nafasi ya uzoefu wa mtu huyo, pale ambapo nafsi hujifunza yenyewe nguvu ya “Bwana Asema hivi,” na kupata tegemeo hilo juu ya Neno takatifu ambalo ndilo peke yake linalonaweza kuleta amani, na nguvu pamoja na Mungu. Wakiwa wanajishughulisha na mzunguko ya taratibu au desturi, wanafunzi katika shule hizi hawakupata masaa ya utulivu ambayo wangewasiliana na Mungu na kusikia sauti Yake ikinena na mioyo yao. Kile ambacho marabi walikiona kuwa ni elimu bora, katika hali halisi, kilikuwa kikwazo kikubwa cha elimu ya Kweli. Kilikuwa kinapinga maendeleo yote halisi. Chini ya mafunzo yao, uwezo wa vijana ulikandamizwa, na akili zao zilibanwa na kufinywa. {FEsw 438.3}

Ndugu na dada za Yesu walifundishwa umati wa mila na sherehe za marabi, lakini Kristo Mwenyewe hakuweza kuvutiwa kuwa na shauku katika mambo haya. Japo alisikia kila upande, maneno yaliyorudiwa “Usi yaani Usifanye,” na “Fanya,” Alitembea kwa uhuru bila hivi vikwazoi. Matakwa ya jamii na matakwa ya Mungu daima yalikuwa katika mgongano; na wakati katika ujana Wake hakufanya mashambulizi ya moja kwa moja juu ya desturi, kanuni au maagizo ya walimu wasomi, Yeye hakuwa mwanafunzi katika shule zao. {FEsw 439.1}

Yesu hangefuata desturi yoyote ile ambayo ingemtaka aachane na mapenzi ya Mungu, wala hakujiweka chini ya mafundisho ya wale walioyainua maneno ya wanadamu kuliko Neno la Mungu. Alifungia {kufuli} akili Yake kuhusiana na hisia na taratibu zote hizo ambazo Mungu hakuwa msingi wake. Hakutoa nafasi kwa

mambo hayo kumvuta. Kwa jinsi hiyo, Yeye alifundisha kwamba ni bora kuzuia uovu kuliko kujaribu kusahihisha wakati umeshapata nafasi ya mahali pa kukanyagia kwenye akili. Kwa mfano Wake, Yesu hakuweza kuwaongoza wengine kujiweka katika hatari ya kuharibiwa. Wala hakujianika bila sababu katika nafasi ambayo angeingizwa kwenye mzozo pamoja na marabi, ambayo ingeweza kusababisha kudhoofisha ushawishi Wake kwa watu miaka ijayo. Kwa sababu zile zile, Yeye hakuweza kushawishiwa kufanya maadhimisho au taratibu zisizo na maana au kukariri na kurudia-rudia semi ambazo baadaye katika huduma Yake, Yeye alizihukumu kwa kuazimia. {FEsw 439.2}

Ingawa Yesu alikuwa chini ya wazazi Wake, katika umri mdogo alianza kutenda kwa ajili Yake mwenyewe katika kuunda tabia Yake. Wakati Mama Yake alikuwa mwalimu Wake wa kwanza wa kibinadamu, Alikuwa akipokea kila mara elimu kutoka kwa Baba Yake aliye Mbinguni. Badala ya kuzama kwenye mafundisho yaliyotolewa na marabi kutoka karne hadi karne, Yesu, chini ya Mwalimu wa Kiungu, alisoma Maneno ya Mungu, yasiyogoshiwa na kupotoshwa (safi), alijifunza pia masomo kutoka kwenye kitabu kikuu cha asili. Maneno, “Bwana asema hivi,” yalikuwa midomoni Mwake kila wakati, na “Imeandikwa,” ilikuwa ni sababu Yake kwa kila tendo lililotofautiana na desturi za familia. Alileta hali ya usafi wa moyo zaidi katika angahewa la maisha ya nyumbani. Ingawa hakujiweka chini ya maelekezo ya marabi kwa kuwa mwanafunzi katika shule zao, lakini mara nyingi aliletwa katika mawasiliano nao, na maswali aliyouliza, kana kwamba alikuwa mwanafunzi anayejifunza, yaliwashangaza wenye hekima (kilikuwa ni kitendawili); kwa maana matendo yao hayakupatana na Maandiko, na hawakuwa na hekima inayotoka kwa Mungu. Hata kwa wale waliochukizwa na kutoafikiana kwake na desturi maarufu, elimu Yake ilionekana kuwa ya aina ya juu kuliko yao mwenyewe.

{FEsw 440.1}

Maisha ya Yesu yalitoa ushahidi kwamba alitarajia mengi, na kwa hiyo alidiriki mengi. Tangu utotoni Mwake alikuwa Nuru ya Kweli inayoangaza katikati ya giza la kiadili la ulimwengu. Yeye Alijidhihirisha kuwa Ndiye Ukweli, na kiongozi wa watu. Fikra Zake kuhusu Ukweli na uwezo Wake wa kupinga majaribu vililingana na lkuliishi lile Neno ambalo Yeye Mwenyewe aliwavuvia watu watakatifu kuandika. Ushirika na Mungu, kujitoa Roho yake kwa ukamilifu kwa Mungu, katika kulitimiza Neno Lake bila ya kujali elimu ya uwongo au desturi au mapokeo ya wakati Wake, viliashiria maisha ya Yesu.

Kuwa daima katika msongamano wa shughuli, na kutafuta kwa utendaji wa nje kuonyesha uchaMungu wao wa hali ya juu, ndiyo yaliyokuwa mahesabu ya marabi vichwani mwao daima, jumla ya dini yote; wakati huo huo, wao kwa kutotii kwao Neno la Mungu mara mara, walikuwa wakipotosha njia ya Bwana. Lakini elimu ambayo ina Mungu nyuma yake, itaongoza watu wamtafute Mungu, “ili wamtafute Mungu, ingawa ni kwa kupapasa-papasa, wakamwone.” (Mdo 17:27). Yeye Asiye na

mwisho hajafungiwa, na kamwe hatafungwa na mashirika ya mwanadamu au kwa mipango ya kibinadamu. Kila nafsi lazima iwe na uzoefu binafsi katika kupata maarifa ya mapenzi na njia za Mungu. Kwa wote walio chini ya mafunzo ya Mungu watafunuliwa maisha ambayo hayapatani na ulimwengu, kwa desturi zake, mazoea yake, au uzoefu wake. Kupitia kujifunza Maandiko, na maombi ya dhati na bidii, wao wanaweza kusikia ujumbe Wake kwao, “Tulieni na mjue kuwa Mimi ni Mungu.” Wakati kila sauti nyingine inaponyamazishwa, wakati kila maslahi ya kidunia maslahi yanageuzwa kando, ukimya wa nafsi hutofautisha kwa umakini sana, sauti ya Mungu. Hapa pumziko linapatikana ndani Yake Yeye. Amani, furaha, uzima wa nafsi, ni Mungu. {FEsw 440.2}

Wakati mtoto anatafuta kuwa karibu na baba yake, juu ya kila kitu mtu mwingine, anaonyesha upendo wake, imani yake, tumaini lake kamili. Na katika hekima na nguvu za baba mtoto hukaa salama. Ndivyo Hivyo na kwa watoto wa Mungu. Bwana anatuambia, “Niangalieni Mimi, mkaokolewe!” “Njooni Kwangu ninyi, ... nami nitawapumzisha.” “Kama kuna yeyote kati yenu aliyepungukiwa na hekima, na aombe dua kwa Mungu, awapaye wote, kwa ukarimu, wala hakemei; naye atapewa.” {FEsw 441.1}

“BWANA asema hivi; Na alaaniwe mtu yule amtegemeaye mwanadamu, na amfanyaye mwanadamu kuwa kinga yake, Na moyoni mwake amemwacha Bwana. Maana atakuwa kama fukara nyikani, Hataona yatakapotokea mema; Bali atakaa jangwani palipo ukame, Katika nchi ya chumvi isiyokaliwa na watu, ardhi ya chumvi na isiyokaliwa na watu. Amebarikiwa mtu yule anayemtumainia Bwana, na ambaye Bwana ni tumaini lake. Maana atakuwa kama mti uliopandwa kando na maji, na kueneza mizizi yake karibu na mto; usione hari ijapo, lakini jani lake litakuwa bichi; Wala hautahangaika mwaka wa uchache wa mvua, Wala hautaacha kuzaa matunda.” {FEsw 441.2}—[Special Testimonies On Education, August 27, 1896.](#)

Kwa marejeleo ya Ziada

[The Child of Jesus, The Youth's instructor, Oktoba 8, 1896.](#)

KIELELEZO CHA KIMBINGU

Tangu nyakati za kale waaminifu katika Israeli walikuwa wameweka umakini katika suala la elimu. Bwana alikuwa ameagiza kwamba watoto, hata tangu uchanga, wanapaswa kufundishwa wema na ukuu Wake, haswa kama ulivyofunuliwa katika sheria Yake, na kuonyeshwa katika historia ya Israeli. Kwa njia ya wimbo na sala, na masomo kutoka katika Maandiko, yakipokelewa kwa akili ya iliyo wazi, baba na mama walikuwa wakiwafundisha watoto wao kwamba sheria ya Mungu ni kielelezo cha tabia Yake, na kwamba kadri walivyolipokea kanuni za sheria ndani ya moyo, sura ya Mungu ilionekana katika akili na nafsi. Shuleni na nyumbani pia, sehemu kubwa ya mafundisho yalikuwa ya mdomo (kwa kuzungumza), lakini vijana pia walijifunza kusoma maandishi ya Kiebrania; na magombo ya ngozi za Maandiko ya Agano la Kale yalikuwa wazi kwa mafunzo yao.

{FEsw 442.1}

Katika siku za Kristo, mafundisho ya kidini ya vijana yalifikiriwa kuwa muhimu sana kiasi kwamba mji au jiji ambalo halikujenga shule kwa kusudi hili, lilionekana kuwa chini ya laana ya Mungu. Walakini katika shule hizo na zile za nyumbani, mafunzo ambayo yalikuwa ya mfano wa desturi au mapokeo, na yalimfanya mwanafunzi awe kama mashine tu, yaani alikuwa kama roboti asiyeonyesha hisia, au dhamira na utashi {mechanical alisoma vitu kama mazoea na kukariri semi fulani}. Kwa kuwa “katika mambo yote ilimpasa afananishwe na ndugu Zake” (Waebrania 2:17), na Yesu alipata ujuzi kama tunavyofanya sisi, kuyafahamu kwa ukaribu Maandiko, ambayo aliyadhihirisha katika huduma Yake, yashuhudia bidii ambayo alikuwka nayo, katika miaka hiyo ya mwanzo, Alijitoa kwa ajili ya kujifunza Neno takatifu. {FEsw 442.2}

Na siku baada ya siku Alipata elimu kutoka kwenye maktaba kubwa ya asili, kutoka kwa vile vyenye uhai, na vile visivyo na uhai. Yeye aliyeviumba vitu vyote, sasa alikuwa mtoto wa kibinadamu, na Akasoma masomo ambayo Mkono Wake Mwenyewe ulikuwa umeyaandika katika ardhi na bahari na anga. Mifano ambayo, wakati wa huduma Yake, Alipenda kuitumia katika kufundisha masomo Yake ya ile Kweli, huonesha jinsi Roho Yake ilivyokuwa wazi kwa mivuto ya asili, na jinsi, katika ujana Wake, Alivyofurahia kukusanya mafundisho ya kiroho kutoka katika mazingira ya maisha Yake ya kila siku. Kwa Yesu umuhimu ya Neno na kazi za Mungu vilifunuliwa hatua kwa hatua taratibu, kwa kadri Alivyokuwa akitafuta kuelewa sababu ya mambo, kama vile kijana yeyote anavyoweza kutafuta kuelewa. Utamaduni wa mawazo matakatifu na ushirika vilikuwa Vyake. Madirisha yote ya nafsi Yake yalikuwa wazi kulielekea jua; na katika Nuru ya Mbinguni, hali Yake ya kiroho ikapata nguvu, na maisha Yake yakadhihirisha hekima na neema ya Mungu.

{FEsw 442.3}

Kila mtoto anaweza kupata ujuzi kama Yesu alivyofanya, yaani kutokana na kazi hizo za asili na kurasa za Neno takatifu la Mungu. Tunapojaribu kujizoeza katika kumwelewa Baba yetu wa Mbinguni kupitia Neno Lake, malaika watakuja karibu nasi, akili zetu zitaimarishwa, tabia zetu zitainuliwa na kusafishwa, nasi tutakuwa kama Mwokozi wetu zaidi. Na tunapotazama uzuri, ukuu na ubora wa asili, mapenzi yetu yatamwendea Mungu; huku Roho ikistaajabu na kuwa na kicho, nafsi itatiwa nguvu na kuwasiliana na Yeye Asiye na mwisho kupitia kazi Zake. Ushirika pamoja na Mungu kupitia maombi hukuza uwezo wa kiakili na kimaadili, na nguvu za kiroho huimarika tunapokuza mawazo juu ya mambo ya kiroho. {FEsw 443.1}

Maisha ya Yesu yalikuwa maisha yenye upatanifu na Mungu. Alipokuwa angali mtoto, alifikiri na kunena kama mtoto, lakini hakuna alama ya dhambi iliyoharibu sura ya Mungu ndani Yake. Kuanzia Nuru ya kwanza ya akili ilipoingia kwenye ubongo Wake, Yeye alikuwa akiendelea kukua daima katika neema ya Mbinguni, na maarifa ya ile Kweli. {FEsw 443.2} – *Special Testimonies on Education, 159 1896.*

Sura ya 56

BIBLIA KITABU MUHIMU ZAIDI KWA ELIMU KATIKA SHULE ZETU

Biblia ni ufunuo wa Mungu kwa ulimwengu wetu, ikituambia tabia tunayopaswa kuwa nayo ili kuifikia paradiso ya Mungu. Tunapaswa kuiona kama ufunuo wa Mungu kwetu kwa mambo ya milele, --mambo yenye hatima muhimu sana kwetu kujua. Dunia inaitupa kando, kana kwamba kusomwa kwake kumekamilika, lakini miaka elfu moja utafiti haungemaliza hazina iliyofichwa humo. Milele peke yake ndiyo itakayofichua hekima ya kitabu hiki. Vito vilivyozikwa ndani yake haviishi/havimalizi; kwani ni hekima ya akili isiyo na kikomo. {FEsw 441.1}

Hakuna kipindi cha wakati ambacho mwanadamu amejifunza yote ambayo anaweza kujifunza ndani ya Neno la Mungu. Bado kuna maoni mapya ya Ukweli yanayosomwa, na kuonwa, na mengi kuna yanayopaswa kueleweka kuhusu tabia na sifa za Mungu, --Fadhili Zake, rehema Zake, ustahimilivu Wake mrefu, na mfano Wake wa utii mkamilifu. "Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kati yetu (nasi tukauona Utukufu Wake, Utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba,) amejaa neema na Kweli." Huu ni utafiti/uchunguzi muhimu sana, Kushughulisha akili, na kutoa nguvu kwenye uwezo wa kiakili. Baada ya kulisoma/kulichunguza Neno kwa bidii, hazina iliyofichwa hugunduliwa, na mpenda Ukweli huibuka kwa ushindi, "Na bila shaka siri ya utauwa ni kuu. Mungu alidhihirishwa katika mwili, Akajulikana kuwa na haki katika Roho, Akaonekana na malaika, Akahubiriwa katika mataifa, Akaaminiwa katika ulimwengu, Akachukuliwa juu katika Utukufu." "Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu ambayo ilikuwamo pia ndani ya Kristo Yesu; ambaye yeye mwanzo alikuwa yuna namna ya Mungu, naye hakuona kule kuwa sawa na Mungu kuwa ni kitu cha kushikamana nacho; bali alijifanya kuwa hana Utukufu, akatwaa namna ya mtumwa, akawa ana mfano wa wanadamu." {FEsw 444.2}

Biblia, iliyopokelewa na kujifunzwa kikamilifu kama sauti ya Mungu, inatoa mwongozo kwa familia ya kibinadamu jinsi ya kufikia makao ya furaha ya milele, na kujipatia hazina za Mbinguni. "Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema." Je, sisi akili zetu ni duni sana, kiasi kwamba hatuwezi kulielewa? Je, tutakuza njaa kali au uchu kwa ajili ya maandishi ya wasomi, na kisha kupuuzia Neno la Mungu? Ni hamu hii au ladha ambayo hawapaswi kuwa

nayo, ndiyo huwafanya wanadamu kutafuta mbadala wa maarifa, ambayo hayawezi kuwafanya kufikia ile hekima iletayo wokovu. {FEsw 444.3}

“Maana hatukufuata hadithi zilizotungwa kwa werevu, tulipowajulisha ninyi nguvu Zake Bwana wetu Yesu Kristo na kuja Kwake; bali tulikuwa tumeuona wenyewe ukuu Wake. Maana alipata kwa Mungu Baba heshima na Utukufu, hapo alipoletewa sauti iliyotoka katika Utukufu mkuu, Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa Naye. Na sauti hiyo sisi tuliisikia ikitoka Mbinguni tulipokuwa pamoja Naye katika mlima ule mtakatifu. Nasi tuna lile Neno la unabii lililo imara zaidi, ambalo, mkiliangalia, kama taa ing'aayo mahali penye giza, mwafanya vyema, mpaka kutakapopambazuka, na nyota ya asubuhi kuzuka mioyoni mwenu. Mkijua Neno hili kwanza, ya kwamba hakuna unabii katika maandiko upatao kufasiriwa kama apendavyo mtu fulani tu. Maana unabii haukuletwa popote kwa mapenzi ya mwanadamu; bali wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu.” “Kwa kuwa yote yaliyotangulia kuandikwa yaliandikwa ili kutufundisha sisi; ili kwa saburi na faraja ya maandiko tupate kuwa na tumaini.” “Uyatafakari hayo; ukae katika hayo; ili kuendelea kwako kuwe dhahiri kwa watu wote.” “Kwa maana wote wenye mwili ni kama majani, na fahari yote ya mwanadamu kama ua la nyasi. Majani hunyauka na ua lake huanguka; bali Neno la Bwana hudumu milele.” {FEsw 445.1}

Ni kwa kusoma Biblia ndipo akili hutiwa nguvu, husafishwa, na kuinuliwa. Kama kungekuwa hakuna kitabu kingine ulimwenguni kote, Neno la Mungu, likichukuliwa na kutendwa maishani kupitia neema ya Kristo, litamfanya mwanadamu kuwa mkamilifu katika ulimwengu huu, akiwa na tabia inayofaa kwa siku zijazo, katika maisha ya kutokufa. Wale walisomao Neno, wakilichukulia kwa imani kuwa ndilo Ukweli, na kulipokea katika tabia, watakuwa kamili ndani Yake Yeye ambaye ni yote na katika yote. Asante kwa Mungu kwa uwezekano uliowekwa hapo awali kwa ubinadamu. Lakini usomaji wa waandishi wengi tofauti tofauti, unachanganya na kuchosha akili, na huwa na ushawishi mbaya kwenye maisha ya kidini/kiroho ya watu. Katika Biblia wajibu wa mwanadamu kwa Mungu na kwa wanadamu wenzake umebainishwa kwa uwazi kabisa; lakini bila kujifunza Neno, utawezaje kutimiza haya matwakwa? Ni lazima tuwe na maarifa ya Mungu; kwa hii; kwa kuwa “Huu ndiyo uzima wa milele,” Kristo alisema, “wakujue Wewe Mungu wa Kweli na wa pekee, na Yesu Kristo uliyemtuma.” {FEsw 445.2}

Hebu madai ya mwanadamu yasichukuliwe kama ndiyo Ukweli yanapokuwa kinyume na Neno la Mungu. Bwana Mungu, Muumba wa mbingu na nchi, chimbuko la hekima yote, Yeye ni nambari moja, na siyo mbili kwa kitu kingine chochote kile. Lakini wale wanaodhaniwa kuwa waandishi wakubwa, wanaozipa shule zetu vitabu vyao vya kiada, ambavyo vinapokelewa na kutukuzwa, kana kwamba wao hawana uhusiano muhimu na Mungu. Kwa masomo kama haya mwanadamu ameongozwa mbali na Mwenyezi Mungu, kwenye njia zilizopigwa marufuku (zilizokatazwa); akili

zimechoshwa hadi kufa kupitia kazi isiyo ya lazima katika kujaribu kupata kile ambacho kwao kinalinganishwa na ule ujuzi ambao Adamu na Hawa katika kuupata, waliacha kumtii Mungu. Kama Adamu na Hawa, wasingegusa mti wa ujuzi, basi wangeweza kuwa mahali ambapo Bwana angeweza kuwapa ujuzi kutoka Kwenye Neno Lake maarifa ambayo wasingeyaacha nyuma na vitu vya dunia hii, lakini ambayo wangeweza kuyabeba na kwenda nayo mpaka paradiso ya Mungu. Lakini leo vijana wa kiume na wa kike hutumia miaka miaka na miaka (mingi) katika kupata elimu ambayo ni mabua na makapi tu, ambayo yatateketezwa katika moto mkubwa wa siku ya mwisho. Wengi hutumia miaka ya maisha yao katika masomo ya vitabu, kupata elimu ambayo itakufa nao. Elimu kama hiyo Mungu haithamini. Hii inayodhaniwa kuwa ni hekima inayopatikana kutokana na uchunguzi wa vitabu vya waandishi mbalimbali, inatenga na kupunguza mwangaza na thamani ya Neno la Mungu. Wanafunzi wengi wameacha shule na kushindwa kupokea Neno la Mungu kwa kicho na heshima waliyoitoa kabla ya kuingia chuoni/shuleni, imani yao ilifunikwa, katika juhudi za kufaulu katika masomo mbalimbali. Biblia haijafanywa kuwa kiwango katika elimu yao, lakini vitabu vilivyochanganyika na ukafiri na kusambaza nadharia zisizo sahihi, vimekwa vikiwekwa mbele yao. {FEsw 446.1}

Hakuna kitu kinachotia nguvu, kinachoinua, kinachoboresha na kutia moyo kama utafiti wa Mada kuu zinazohusu uzima wetu wa milele. Waache wanafunzi watafute kufahamu Kweli hizi zilizotolewa na Mungu; watafute kupima hayavitu vya thamani, na kisha akili zao zitatanuka na kuwa na nguvu wanapoweka juhudi. Lakini akili ikirundikwa wingi wa mambo ambayo haitakuwa na uwezo wa kuyatumia {inavembiwa}, ni akili mbilikimo, dhaifu na duni, kwa sababu huwekwa katika kazi ya kushughulikia machapisho ya kawaida. Haijawekwa katika kazi ya kuzingatia mfichuo wa juu, ulioinuliwa, ule unaotoka Mungu. {FEsw 447.1}

“Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.” Ikiwa akili inaitwa kwa umakini/dharura kuzingatia mada hizi kuu, basi itapanda juu zaidi na zaidi katika ufahamu wa masomo haya ya umuhimu wa milele, na ikiacha vile duni, na visivyo na maana vidondoke chini kwani havina faida, ni ‘uzito uliokufa’. {FEsw 447.2}

Mambo yote yasiyo ya lazima yanahitaji kupaliliwa na kungolewa kwenye mafunzo/machapisho, na kisha yale masomo yaliyo na thamani halisi kwa wanafunzi, ndiyo tu peke yake yaachwe na kisha yawekwe mbele ya wanafunzi. Ni haya tu ndiyo ambayo mwanafunzi anahitaji kufahamiana nayo, ili apate maisha yale yanayopimika na maisha ya Mungu (milele). Na anapojifunza haya, akili yake itaimarika na kutanuka kama vile ilivyokuwa akili ya Kristo na ya Yohana Mbatizaji. Nini kilimlifanya Yohana kuwa mkuu? -Yeye alifunga mawazo yake kwa wingi wa mapokeo yaliyofundishwa na walimu wa taifa la Kiyahudi, na akaifungua kwa hekima “ishukayo kutoka juu Mbinguni.” Kabla ya kuzaliwa kwake, Roho Mtakatifu

alimshuhudia Yohana: “Kwa maana atakuwa mkuu machoni pa Bwana, wala hatakunywa divai wala kileo; naye atajazwa na Roho Mtakatifu, hata tangu tumboni mwa mamaye. Na wengi wa wana wa Israeli atawarejeza kwa Bwana, Mungu wao. Naye atatangulia mbele zake katika Roho na nguvu za Eliya, ili kugeuza mioyo ya baba kwa watoto, na kuwatilia waasi akili za wenye haki; ili kuwaweka tayari watu walioandaliwa kwa ajili ya Bwana. Na wengi katika Waisraeli atawarejeza kwa Bwana Mungu wao.” Na katika unabii wake, Zakaria alisema juu ya Yohana, “Nawe, mtoto, utaitwa nabii wake Aliye juu, Kwa maana utatangulia mbele za uso wa Bwana umtengenezee njia Zake; Uwajulishe watu Wake wokovu, Katika kusamehewa dhambi zao. Kwa njia ya rehema za Mungu wetu, Ambazo kwa hizo mwangaza utokao juu umetufikia, Kuwaangaza wakao katika giza na uvuli wa mauti, Na kuiongoza miguu yetu kwenye njia ya amani. Yule mtoto akakua, akaongezeka nguvu Rohoni, akakaa majangwani hata siku ya kutokea kwake kwa Israeli.” {FEsw 447.3}

Simeoni alisema juu ya Kristo, “Sasa, Bwana, wamruhusu mtumishi Wako, Kwa amani, kama ulivyosema; Kwa kuwa macho yangu yameuona wokovu Wako, Uliouweka tayari machoni pa watu wote; Nuru ya kuwa mwangaza wa Mataifa, Na kuwa Utukufu wa watu Wako Israeli.” “Naye Yesu akazidi kukua katika hekima na kimo, akimpendeza Mungu na mwanadamu.” Yesu na Yohana waliwakilishwa na waelimishaji wa siku zile kama watu wajinga, kwa sababu hawakujifunza chini yao. Lakini Mungu wa Mbinguni alikuwa mwalimu wao, na wote waliosikia walishangaa kwa ujuzi wao wa Maandiko Matakatifu, wakiwa hawajajifunza miongoni mwao, hakika hawakujifunza kutoka kwao; lakini kutoka kwa Mungu walikuwa wamejifunza aina ya juu zaidi ya hekima. {FEsw 448.1}

Hukumu na maamuzi ya wanadamu, hata ya walimu, inaweza kuwa pana sana kuhusiana na kigezo kinachohusu elimu ya Kweli. Walimu wa siku hizo za Kristo hawakuwaelimisha vijana katika maarifa sahihi ya Maandiko, ambayo ndiyo msingi wa elimu yote inayostahili jina ‘Elimu’. Kristo alitangaza kwa Mafarisayo, “Mwapotea, kwa kuwa hamjui Maandiko, wala uweza wa Mungu,” “Wakifundisha mafundisho Yaliyo maagizo ya wanadamu.” Naye akawaombea wanafunzi Wake, “Uwatakase kwa ile Kweli, Neno lako Ndiyo Kweli. Kama vile ulivyonituma ulimwenguni, vivyo hivyo na Mimi nimewatuma ulimwenguni. Na kwa ajili yao najiweka wakfu, ili wao pia watakaswe kupitia Ukweli.” {FEsw 448.2}

“Kisha, nena wewe na wana wa Israeli, na kuwaambia, Hakika mtazishika Sabato Zangu, kwa kuwa ni ishara kati ya Mimi na ninyi katika vizazi vyenu vyote; ili mpate kujua ya kuwa Mimi Ndimi Bwana niwatakasaye ninyi..” “Kazi itafanywa siku sita; lakini siku ya saba ni Sabato ya kustarehe kabisa, takatifu kwa Bwana; kila mtu atakayefanya kazi yo yote katika siku ya Sabato, hakika yake atauawa.” Je, Shetani amefanikiwa kuondoa utakatifu kutoka siku hiyo ambayo ilitofautishwa na Mungu kwa zingine zote? Amefanikiwa kuiweka siku nyingine badala yake, lakini kamwe

hawezi kuondoa baraka za Bwana kwenye siku hii. “Kwa ajili ya hayo wana wa Israeli wataishika Sabato, kuiangalia sana hiyo Sabato katika vizazi vyao vyote, ni agano la milele..” Nini kinaweza kuwa chanya na wazi zaidi kuliko maneno haya? Na je, Mungu amebadilika? Yeye Atabaki kuwa Yule Yule milele zote, lakini mwanadamu “ametafuta mavumbuzi mengi.” {FEsw 449.1}

Biblia imejaa maarifa, na wote wanaokuja kwenye mafunzo yake kwa moyo wao kuyaelewa, watapata akili iliyopanuliwa na uwezo wa vitivyo vyao kuimarishwa ili kuzifahamu Kweli hizi zenye thamani, zinazofikia mbali. Roho Mtakatifu atasisitiza kwenye hisia/akili na nafsi. Lakini wale ambao hutoa mafundisho kwa vijana, wanahitaji kwanza kuwa wajinga ili kwamba waweze kuwa na hekima. Wakipuuza uwazi uliotamkwa wa “Bwana asema hivi,” na kuchuma katika mti wa ujuzi kile ambacho Mungu amewakataza kutwaa, ambayo ni elimu ya uasi, uasi wao huwaleta katika hukumu na dhambi. Je, tuwasifu watu kama hao kwamba wanao ujuzi mkuu? Je, sisi tuketi miguuni mwa wale wanaopuuzia zile Kweli zinazotakasa nafsi? “Kama mimi niishivyo, asema Bwana MUNGU, hakika kwa mkono hodari, na kwa mkono ulionyoshwa, na kwa ghadhabu iliyomwagika, nitakuwa Mfalme juu yenu.” Mbona waelimishaji wa siku hizi hawasikilizi maonyo haya? Kwa nini wanajikwaa, na hawajui wanajikwaa kwenye nini? Ni kwa sababu Shetani ameyapofusha macho yao, na kikwazo cha uovu wao kinaletwa mbele ya wengine kwa kanuni na mfano wao. Hivyo macho mengine yamepofushwa pia, na wale ambao inawapasa kuenenda Nuruni, wanaenenda gizani; maana hawamtazami Yesu kwa mkazo na uthabiti, ambaye Ndiye Nuru ya ulimwengu. {FEsw 449.2}

Nuru kuu ilitolewa kwa Wanamatengenezo, lakini wengi wao walipokea udanganyifu na makosa ya hali ya juu kwa njia ya kufafanua vibaya Maandiko. Makosa haya yameshuka chini kwa karne nyingi, na japo yana mvi kwa uzee, nyuma yake hayana “Bwana asema hivi.” Kwa maana Bwana amesema, “Sitabadilisha Neno ambalo limetoka katika midomo Yangu.” Kwa rehema Zake nyingi, bado Bwana ameuhusu Nuru kubwa zaidi kuangaza katika siku hizi za mwisho. Ametuma kwetu sisi ujumbe Wake, akifunua sheria Yake na kutuonyesha Ukweli. {FEsw 450.1}

Ndani ya Kristo kuna chemchemi ya maarifa yote. Katika Yeye matumaini yetu ya uzima wa milele yamejikita. Yeye Ndiye mwalimu mkuu zaidi ambaye ulimwengu wetu umewahi kujua, na ikiwa tunataka kupanua akili za watoto na vijana, na kupata mioyo, ili waweze kuipenda Biblia, sisi tunapaswa kukaza akilini mwao juu ya Ukweli ulio wazi na rahisi, tukichimba na kutoa nje kile amacho kimezikwa chini ya takataka za mila/mapokeo, na kuachilia vito kung'aa. Wahimize wanafunzi kutafuta haya masomo, na jitihada itakayofanywa itakuwa nidhamu yenye thamani sana. Kufunuliwa kwa Mungu, kama inavyowakilishwa katika Yesu Kristo, kunatoa mada ambayo ni nzuri kutafakari, na ambayo, ikiwa itasomwa/itachunguzwa, itaboresha akili, itanoa, itainua na kuimarisha uwezo. Kila wakala wa kibinadamu

anapojifunza masomo haya katika shule ya Kristo, na kujaribu kuwa kama Kristo kwa upole, na unyenyekevu wa moyo, yeye atajifunza masomo yenye manufaa kupita yote, —akili huwa ya hali ya juu kabisa kadri inavyotakaswa na uhusiano hai na Mungu. {FEsw 450.2}

Onyo na maagizo yanayotolewa katika Neno la Mungu kuhusu wachungaji wa uongo, linapaswa kuwa na uzito fulani kwa walimu na wanafunzi katika shule zetu. Ushauri unapaswa kutolewa kwa wanafunzi kutowachukulia wachungaji kama hao kuwa ndiyo mamlaka yao kuu (au kiwango). Kuna haja gani basi kwa wanafunzi kumalizia masomo yao kwa kuhudhuria chuo cha Ann Arbor kwa kusema wanapata mambo muhimu ya kumalizia shahada yao? {Ann Arbor kilikuwa chuo cha serikali, sasa kinaitwa University of Michigan}. Imeonekana kwenda kwao huko kumalizia shahada, pia kumemaliza mambo yote ya kiroho na imani katika ile Kweli ilivyo. Ni zoezi au kisomo kisicho na ulazima, ni kufungua akili ili kupandikiza magugu kati ya ngano; na jambo hilo halimpendezi Mwalimu wetu Mkuu kwani ni kuwatukuza walimu ambao hawana masikio ya kusikia wala akili kutii amri ya Mungu iliyo wazi isemayo “Bwana asema hivi.” Kwa kuwaheshimu wale ambao huelimisha moja kwa moja mbali na Ukweli au kinyume na ile Kweli, sisi hatuwezi kupata kibali cha Mungu. Hebu Maneno ya Bwana, yaliyonenwa kwa ulimwengu kupitia nabii Isaya, yawe na uzito mioyoni mwetu. “Kwa maana ndivyo asemavyo Yeye Aliye juu na aliyetukuka, akaaye milele, ambaye Jina Lake ni Mtakatifu; asema hivi; Nakaa Mimi mahali palipoinuka, palipo Patakatifu; tena pamoja na yeye aliye na Roho iliyotubu na kunyenyekea, ili kuzifufua Roho za wanyenyekevu, na kuifufua mioyo yao waliotubu.” “Bwana Yu karibu nao waliovunjika moyo, Na waliopondeka Roho huwaokoa.” “lakini mtu huyu ndiye nitakayemwangalia,” asema Bwana. “Mtu aliye mnyonge, mwenye Roho iliyopondeka, atetemekaye asikiapo Neno Langu.” Wanyenyekevu, wanaomtafuta Bwana, wanayo hekima hata kufikia uzima wa milele. {FEsw 450.3}

Hekima kuu, na muhimu zaidi, ni maarifa ya Mungu. Nafsi inazama chini katika kutokuwa na maana inapomtafakari Mungu na Yesu Kristo ambaye amemtuma. Biblia lazima iwe msingi kwa masomo yote. Kila mmoja wetu ni lazima lazima ajifunze kutoka kwa kitabu hiki cha somo ambacho Mungu ametupa, hali ya wokovu wa Roho zetu; maana ni kitabuhiki pekee kinachotuambia kile tunachopaswa kufanya ili kuokolewa. Sivyo hivo tu, bali kutoka kwa hiki kitabu, nguvu inaweza kupokelewa kwenye akili. Vitabu vingi ambavyo elimu inadhaniwa kuwa imekumbatiwa, vinawewesha akili, vinapotosha, na kudanganya kwani “Makapi ni nini kwa ngano?” Shetani sasa inachochea akili za watu kutoa machapisho ya fasihi ya ulimwenguni ambayo ni ya bei nafuu, vya elimu ya juu juu tu, lakini ambavyo vinavutia akili, na kuifunga katika mtandao wa hila za Shetani. Baada ya kusoma vitabu hivi, akili huishi katika ulimwengu usio wa uhalisia, na maisha yenye manufaa yanakuwa hatarini, ni tasa kama mti usio na matunda. Ubongo unasumishwa na kileo, na kufanya isiwezekane kwa ule Ukweli wa milele,

ambao ni muhimu kwa sasa na siku zijazo, kushinikizwa nyumbanim, yaani kwenye moyo wa mtu. Akili ya aliyeelimishwa kujilisha takataka haiwezi kuona katika Neno la Mungu, uzuri uliopo. Upendo kwa Yesu na mwelekeo wa uadilifu unapotea; kwani akili hujengwa kutokana na kile ambacho hujilisha. Kwa kuilisha akili juu hadithi za kuisimua za uongo, mwanadamu analeta kwenye ujenzi wa msingi “mbao, nyasi, makapi.” Anapoteza ladha yote ya Kitabu cha Mwongozo wa Mungu, na hajali kujifunza tabia anayopaswa kuunda ili kukaa pamoja na lile jeshi lililokombolewa, na mwishowe akae katika makao makuu ambayo Kristo amekwenda kuitayarisha.

{FEsw 451.1}

Mungu kwa Zake neema nyingi zaidi, ametujalia rehema ambayo kwayo yatufanya tujiandae kwa mtihani utakaoletwa juu yetu. Kila faida inatolewa kwetu kwa njia ya upatanishi wa Kristo. Ikiwa mwanadamu atasoma Neno, ataona kuwa kila uwezeshaji umetolewa kwa ukarimu mwingi kwa uwezeshaji kwa ajili ya wale wanaotafuta kuwa washindi. Roho Mtakatifu yupo ili kutia nguvu kwa ushindi, na Kristo ameahidi, “Tazama, Mimi nipo pamoja nanyi sikuzote, hata ukamilifu wa dahari.” **{FEsw 451.2}**— *Special Testimonies on Education*, 157 {1896}.

Kwa Marejeleo ya Ziada

1896 Publication of “ *Special Testimonies on Education*” A Lesson from One of the Prophets of God, The Youth’s Instructor, January 7, 1897 Worldly Amusements, The Youth’Instructor, February 4, 1897

Words to Parents, The Review and Herald, April 6, 1897,

The Review and Herald, April 13, 1896

Benefits of Nature, The Youth’s Instructor, May 6, 1897

Don’t Send the Children too Early to School, The Bible Echo, June 28, 1897.

Sura ya 57

NIDHAMU SAHIHI YA SHULE

Tulikuwa shuleni na---- wanafunzi wasio na adabu, wasio na utiifu, wanaopenda kujifanyia wanachotaka, ambao walikuwa na mwelekeo kupuuza maagizo yaliyotolewa kutoka katika Neno la Mungu, na kwa mwenendo wao wanasaliti zile amana takatifu. Bwana aliangalia chini kutoka Mbinguni juu yao, na kuyaona matendo yao ya udanganyifu, na kukana kwao, kwa matendo yao ya uwongo. Walifanyiwa kazi kwa uaminifu {kuwainjilisha katika Neno}; lakini walikuwa karibu sana na mji, na majaribu yakawa yanainua kichwa chake mara kwa mara. Walisahau kuwa waaminifu kwa sheria takatifu ya Mungu. Walivunja amri Zake. Walikuwa wamedanganyika kwa shauku kali ya vitu vya muda mfupi, na hiyo ikafichua kwamba kama wanafunzi, wao hawakuwa na uadilifu wa kimaadili wa kuwa wakweli. Ilionekana kuwa wakala wa Kishetani akiwa kazini kuwakatisha tamaa walimu na kuifanya shule kukosa ujasiri wa matumaini yao. Wengine wakitenda kazi kama walimu hawakutoa ushawishi sahihi. Wakati kila yodi ya ushawishi inapaswa kuwekwa upande wa nidhamu na utaratibu, walimu hawa, japo walijua majaribu yote ambayo wanafunzi wakorofi walikuwa wanaleta juu ya mkuu wa shule na wafanyakazi wenzake, ambao walikuwa na mizigo na walioonewa, na ambao walikuwa wakimtafuta Bwana kwa bidii zaidi, walionyesha huruma kwa wale ambao walikuwa wakimtumikia adui kwa bidii zaidi. Wanafunzi wahalifu walilijua hili. Wachache walichukua ujasiri wa kujishughulisha na njia yao mbaya, hadi ilipoletwa nyumbani kwao kwa nguvu sana hata wakakiri kwamba walikuwa wameasi sheria za shule, na walikuwa wamejaribu kujificha nyuma ya uwongo. {FEsw 454.1}

Wafanya kazi washule walifanya mashauriano ya faragha ili kuzingatia nini kilikuwa bora kufanywa. Kulikuwa na sauti katika mashauri haya ambayo ilijaribu kupingana na mipango iliyoanzishwa ili kuweka nidhamu na utaratibu. Kwa sauti hii

ya huruma, maneno yaliangushwa na kufunua kwa wanafunzi mambo yanayoendelewa kuzingatiwa katika baraza hilo. Mambo haya yalikamatwa na wanafunzi. Nao wakadhani kwamba mwalimu kama huyo alikuwa sawa; kwamba alikuwa mwalimu mwerevu. Naye atakuwa na huruma kwa mkosaji. Kwa hivyo mikono ya wale waliobeba mzigo mzito haikuimarishwa, bali kudhoofishwa. Juhudi zilizofanywa kuuzuia uovu zilitazamwa kama ukali na jambo lisilo na hisani. "Vijana lazima wawe na nyakati zao za kufurahisha," ilirudiwa, pamoja na hotuba zingine zisizo na ladha kutamka. Neno lililotupwa hapa na neno jingine lilitupwa kule, liliacha hisia yake mbaya; na wakosaji wakajua kwamba kuna wale shuleni ambao hawakufikiri kwamba mwenendo wao wa udanganyifu na uwongo ulikuwa dhambi kubwa. Lakini kuchukua hatua ya kutetea haki ya mkosaji daima, bila kutoa hesabu ya kuondoka kwake kwenye mstari wa haki, ile Kweli na uadilifu thabiti ni dhambi kubwa dhidi ya Mungu. {FEsw 454.2}

Kulikuwa na wale katika shule ambao walikuwa wamebeebwa katika kusaidiwa karo kwa masharti, sababu wao wenyewe hawakuwa na mali. Hawa wanapaswa kufanya kila juhudi ili kujipatia faida zote zinazowezekana, na hivyo kuonyesha shukrani zao kwa Mungu, na kwa wema wa marafiki waliokuwa wamewasaidia. {FEsw 455.1}

Vijana wa kiume na wa kike wanapoongoka katika vitendo na ile Kweli na kubadilishwa, mabadiliko hayo yaliyoazimiwa yataonekana kwa wote walio na uhusiano wowote nao. Upuuzi wao utawatoka kichwani; hamu endelevu ya maburudisho na anasa za ubinafsi, au matamaniao ya kuwa kwenye pati/karamu na safari za anasa, haitaonekana tena. {FEsw 455.2}

Sikia maneno ya Mwalimu mkuu: "Kwa maana chakula cha Mungu ni Yule aliyeshuka kutoka Mbinguni na kuupa ulimwengu uzima ." Hakuna haja ya kuwa duni na mvivu, kuishi kwa mambo ya kawaida tu, yale ya msisimko wa kidunia. Uhai hutolewa kwa kila mwamini, pamoja na faraja na kiasi. Wote wanaweza kuwa na furaha, kwa sababu ya kuridhika kwamba sisi tuna Kristo kama mgeni wa kudumu moyoni mwetui. {FEsw 455.3}

Yesu alipowaambia makutano, "Chakula cha Mungu ni kile kishukacho kutoka Mbinguni na kuupa ulimwengu uzima," wengine katika umati wakasema, "Bwana, sikuzote utupe chakula hiki." Mkate ya Mbinguni alikuwa katikati yao, lakini hawakumtambua kuwa Ndiye mkate wa uzima. Kisha Yesu alisema waziwazi, "Mimi Ndimi chakula cha uzima Yeye ajaye Kwangu hataona njaa kamwe, na yeye aniaminiye Mimi, hataona kiu kamwe." {FEsw 455.4}

Sura hii ya sita ya Yohana ina masomo ya thamani zaidi na muhimu kwa wote wanaoelimishwa katika shule zetu. Ikiwa wanataka elimu hiyo ambayo itadumu kwa wakati wote, milele zote, hebu na waletе zile Kweli za ajabu za sura hii ndani

maisha yao ya vitendo. Sura nzima inafundisha na kuelekeza mengi, lakini inaeleweka kwa uhafifu tu. Tunawahimiza wanafunzi kuchukua Maneno haya ya Kristo, ili wapate kuelewa upendeleo walio nao. Bwana Yesu anafundisha sisi, jinsi Yeye alivyo kwetu, na itakuwa faida kwetu sisi binafsi kuyala Maneno Yake, tukitambua kwamba Yeye Mwenyewe ndiye kitovu kikuu cha maisha yetu maisha, “Maneno ninayowaambia ninyi,” Akasema, “ni Roho, na ni uzima.” {FEsw 456.1}

Tukiwa na Kristo moyoni, jicho letu litakuwa limekaza kwa Utukufu wa Mungu. Tunapaswa kujitahidi kuelewa maana ya kuwa na

muungano kamili na Kristo, ambaye Ndiye kipatanisho/mpatanishi kwa dhambi zetu; na kwa ajili ya dhambi za ulimwengu wote, mbadala wetu na mdhamini wetu mbele ya Bwana Mungu wa Mbinguni. Maisha yetu yanapaswa kufungwa katika maisha ya Kristo, tunapaswa kuchota kutoka Kwake daima, tukila mwili Wake, Uzima ulioshuka kutoka Mbinguni, unaotoka katika chemchemi safi daima, daima hutoa hazina zake nyingi. Wakati jambo hili litakuwa kweli katika uzoefu wa Mkristo, Upya, usahili, na unyenyekevu vitaonekana katika maisha yake, na wale wenzake anaoshirikiana nao watajua kwamba amekuwa na Yesu, na kujifunza kutoka Kwake. {FEsw 456.2}

Uzoefu huu unampa kila mwalimu sifa ambazo zitamfanya kuwa mwakilishi wa Kristo Yesu. Mbinu za Mafundisho ya Kristo, zikifuatwa, zitatoa msukumo na uwazi katika mawasiliano na maombi yake. Ushahidi wake kwa Kristo hautakuwa finyu, wenye woga, na usio na uhai, bali utakuwa kama anakatua ardhi na jembe la plau, akihuisha dhamiri, akifungua moyo na kutayarisha mbegu za Ukweli. {FEsw 456.3}

Yule anayeshughulika na vijana hapaswi kuwa na moyo wa chuma, lakini awe mwenye mapenzi na watu, mwororo, mwenye huruma, mwenye adabu, mwungana, anayependeka/mchangamfu (winning), anayeshinda, na mwenye urafiki; lakini wanapaswa kujua kwamba kwa wakati unaotakiwa karipio lazima litolewe, na kwamba kuna wakati watapasa kukemea ili kukata uovu fulani. Tia moyo vijana kumtukuza Mungu kwa kutoa maelezo ya shukrani zao kwa Bwana kwa rehema Zake zote. Hebu shukrani zao zizungumzwe mara kwa mara, moyoni na kwa sauti, na hebu kujikana nafsi, kujinyima na kujitoa nafsi vionyeshwe. Ikiwa wale wanaodai kuwa wanafunzi wa Kristo watakula mwili Wake na kuinywa damu Yake, ambayo ni Neno lake, watakuwa na uzima wa milele. “Nami nitamfufua siku ya mwisho,” Kristo asema. “Kwa maana mwili Wangu ni chakula cha Kweli, na damu Yangu ni kinywaji cha Kweli. Anayekula Yangu mwili na kuinywa damu Yangu, hukaa ndani Yangu, Nami ndani yake.” {FEsw 456.4}

“Kama vile Baba aliye hai alivyonituma mimi, nami ni hai kwa Baba; kadhalika naye mwenye kunila atakuwa hai kwa mimi.” Ni wangapi wana uzoefu huu? Ni wangapi wanaotambua maana halisi ya haya Maneno? Je, sisi binafsi tutatafuta kuelewa Neno la Mungu, na kulifanyia mazoezi kwa vitendo? Neno hili, likiaminiwa,

ni zawadi ya bure ya neema kwa kila ambaye moyo wake umeongoka. Haliwezi kununuliwa kwa pesa. Sisi tunapaswa kutambua daima kwamba hatustahili neema kwa sababu ya sifa zetu wenyewe, kwa kuwa yote tuliyo nayo ni zawadi ya Mungu. Yeye natuambia, “ mmepokea bure, toeni bure.” {FEsw 457.1}

Mazingira ya kutokuamini ni mazito na ya kukandamiza. Kicheko cha furaha kubwa, mzaha, futuhi, huumiza Roho inayojilisha Kristo. Mazungumzo yasiyo na maana ya ovyo ovyo, ya kipumbavu ni huleta maumivu Kwake. Kwa moyo mnyenyekevu soma kwa makini 1 Petro 1:13-18. Wale wanaofurahia kuzungumza wanapaswa kuona kwamba Maneno yao yamechambuliwa na kuchaguliwa vyema. Uwe makini jinsi unavyozungumza. Kuwa mwangalifu jinsi unavyoiwakilisha dini uliyoikubali. Unaweza kuhisi sio dhambi kusengenywa na kuzungumza upuuzi, lakini hii inamhuzunisha Mwokozi wako, na huwahuzunisha malaika wa Mbinguni. {FEsw 457.2}

Petro anatoa ushuhuda gani? “kwa hiyo tuweke kando yote uovu, na hila zote, na unafiki, na husuda, masingizio yote. Kama watoto wachanga waliozaliwa sasa yatamanini maziwa ya akili yasiyoghoshiwa, ili kwa hayo mpate kuukulia wokovu ikiwa mmeonja ya kwamba Bwana ni mwenye fadhili.” Hapa tena kanuni hiyo hiyo inatolewa waziwazi. Hakuna haja ya kufanya makosa. Ikiwa kama watoto wachanga waliozaliwa sasa tuyatamani maziwa ya akili yasiyoghoshiwa, ili kwa hayo mpate kukua, hamtakuwa na hamu ya kushiriki sahani la maneno ya uovu, bali vyakula vile vyote vibaya vitakataliwa mara moja, kwa sababu wale wote ambao wameonja na kuona kwamba Bwana mwenye neema hawezi kushiriki sahani ya upuuzi, na upumbavu, na kusengenywa. Watasema kwa kuazimia, “Ondoa sahani hili. mimi sitaki kula chakula kama hicho. Kwani hicho sio mkate kutoka Mbinguni. Bali ni kula na kunywa Roho ya Ibilisi; maana ni shughuli yake kuwa mshitaki wa ndugu.” {FEsw 457.3}

Ni vyema kwa kila nafsi kufanyia utafiti wa karibukuhusiana na chakula gani kimetayarishwa ili kiliwe. Wale watu ambao wanaishi ili kuzungumza wanapokuja kwako, na ambao wote wamejihami na silaha na vifaa vya kusema, “Ripoti, nasi tutaripoti,” Simama/sitisha na ufikirie ikiwa mazungumzo hayo yatatoa msaada wa kiroho, ufanisi wa kiroho, ili katika mawasiliano ya kiroho mpate kula mwili na kuinywa damu ya Mwana wa Mungu. “Mmwendee Yeye, jiwe lililo hai, lililokataliwa na wanadamu, bali kwa Mungu ni teule, lenye heshima.” Maneno haya yanaeleza mengi. Hatupaswi kuwa wachochezi, au wambeya, waropokaji wa mambo ya watu au wafunuaji siri za watu {shihata}; hatupaswi kushuhudia uongo. Sisi tumekatazwa na Mungu kujihusisha na mazungumzo yasiyo na maana, ya kipumbavu, mizaha, kejeli, au kusema maneno yoyote yasiyokuwa na sababu yaani maneno ;sifuri au tupu’, ya kutia chumvi, yasiyo ya dhati n.k. Lazima tutoe hesabu ya kile tunachomwambia Mungu. Tutaletwa hukumuni kwa ajili ya maneno yetu tunayozungumza kwa haraka bila ya kufikiri, pengine kwa jazba ambayo hayamfai

mzungumzaji au msikilizaji. Basi sote tunene maneno yana tabia ya kujenga. Kumbuka kwamba wewe ni wa thamani mbele za Mungu. Usiruhusu mazungumzo duni (ya bei rahisi), ya kipumbavu au kanuni mbovu za kuunda uzoefu wako wa Kikristo. {FEsw 458.1}

"Waliochaguliwa na Mungu na wa thamani." Fikiria maneno hayo, kwa kila mtu anayetaja Jina la Kristo, Je, wewe umeonja na kuona kwamba Bwana ni Mwenye neema? Je, hii imekuwa sehemu ya uzoefu wako halisi unaowakilishwa katika Yohana sita kama kula mwili na kunywa damu ya Mwana wa Mungu? Kama watoto wachanga waliozaliwa, je, unajifunza kutamanii maziwa ya akili yasiyoghoshiwa ya Neno, upate kukua kwa hilo Neno? Je, katika maisha yako, kuna wakati wewe umefikia wongofu wa Kweli? Je, umezaliwa mara ya pili? Kama hujazaliwa bado, basi ni wakati wa wewe kupata uzoefu ambao Kristo alimwambia mmoja wa watawala wakuu kwamba ni lazima awe nao. "Ni lazima uzaliwe mara ya pili," Yeye alisema. "Mtu asipozaliwa kwa mara ya pili, hawezi kuuona ufalme wa Mungu." Hiyo inamaanisha kwamba, mtu huyo hawezi kutambua mahitaji/matakwa muhimu anayohitaji kuwa ili awe na sehemu katika ufalme huo wa kiroho. "Usistaajabu kwa kuwa nilikuambia, hauna budi kuzaliwa mara ya pili." Ukifungua akili ubongo ili Neno la Mungu liingie, ukiwa na azimio moyoni la kutenda Neno hilo, Nuru itakuja; maana Neno hili humpa ufahamu mjinga. {FEsw 458.2}

Hii ndiyo elimu ambayo kila mwanafunzi anaihitaji. Wakati hii inapatikana, endapo wataongoka, maisha ya kipuuzi waliyo nayo kabla ya hapo yatatelekezwa. Ulimwengu wa Mbinguni utaangalia wahusika ambao wamebadilishwa. Upuuzi, futuhi na mambo ya kawaida-kawaida yatachwa, na miguu yao itawekwa kwenye mzunguko wa ngazi ya kwanza, ambayo ni Kristo Yesu (watakuwa tayari kupanda ngazi zile nane za 2 Petro!: 5-6). Watapanda hatua kwa hatua, ngazi moja baada ya nyingine, kuelekea Mbinguni. Kristo atafunuliwa ndani ya mioyo yao kwa maneno, na katika matendo yao. {FESW 459.1}

"Ninyi nanyi, kama mawe yaliyo hai, mmejengwa kuwa nyumba ya Roho, takatifu ukuhani, ili kutoa dhabihu za kiroho zinazokubaliwa na Mungu kwa njia ya Yesu Kristo." Je, walimu na wanafunzi watasoma mfano huu unaowakilishwa hapa, na kuona ikiwa wamo katika tabaka lile ambalo, kwa njia ya neema nyingi walizopewa, wako wao wanajipatia uzoefu ambao unapatana na kile kisicho bandia, yaani kile kilicho halisi, ule uzoefu wa kweli ambao kila mtoto wa Mungu lazima awe nao pale anapoingia darasa/daraja la juu. {FEsw 459.2}

Nikodemo alipomjia Yesu, Kristo alimwekea masharti ya uzima wa mbingu/Bwana, akimfundisha alfabeti ya uongofu. Nikodemo akauliza, "Mambo haya yanawezekanaje?" "Wewe ni mwalimu wa Israeli," Kristo akajibu, "na hujui mambo haya?" Hii swali linaweza kuulizwa kwa wengi wanaoshikilia nyadhifa za wajibu kama walimu leo, ila ambao wamepuuza kazi muhimu ambayo walipaswa kufanya kabla hawajahitimu kuwa walimu. Kama maneno ya Kristo yatapokelewa

katika moyoni, kungekuwa akili za ubora wa hali ya juu zaidi, na maarifa ya ndani zaidi ya kiroho ya kile kinamchofanya mtu kuwa mwanafunzi wa Kristo na mfuasi wa kweli wa Kristo. Wakati jaribu na mthani unaifikia kila nafsi, kutakuwa na uasi. Wasaliti, werevu, waungwana wenye maadili na kanuni na wanaojitosheleza watageuka kutoka kwenye ile Kweli, wakiivunjilia mbali imani yao. Kwa nini? —Kwa sababu hawakuchimba kina kirefu, na kuhakisha msingi wao uko imara. Hawakuvutiwa na Mwamba wa milele. Wakati Maneno ya Bwana, kupitia kwa wateule Wake, wajumbe waliochaguliwa yanaletwa kwao, wao wananung'unika na kufikiria njia imefanywa nyembamba sana. Kama wale ambao walidhaniwa kuwa wanafunzi wa Kristo, lakini ambao hawakupendezwa na Maneno Yake, na hawakutembea tena pamoja Naye, watamgeuka Kristo. {FEsw 459.3}

“Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu, asipovutwa na Baba aliyenipeleka; Nami nitamfufua siku ya mwisho..” Nini mchoro? — “Imeandikwa katika manabii, Na wote watakuwa wamefundishwa na Mungu. Basi kila aliyesikia na waliofundishwa na Baba, huja kwangu.” Kuna wanaume wanasikia, lakini ambao hawajifunzi somo kama wanafunzi wenye uadilifu na bidii. Wana namna ya utauwa, lakini si waamini. Hawajui Ukweli wa vitendo. Hawakupokea Neno lililopandikizwa. “Kwa hiyo wekeeni mbali uchafu wote na ubaya uzidio, na kupokea kwa upole Neno lile lililopandwa ndani, liwezalo kuziokoa Roho zenu. Lakini iweni watendaji wa Neno, wala si wasikiaji tu, hali mkijidanganya nafsi zenu. Kwa sababu mtu akiwa ni msikiaji wa Neno tu, wala si mtendaji, mtu huyo ni kama mtu anayejiangalia uso wake katika kioo. Maana hujiangalia, kisha huenda zake, mara akasahau jinsi alivyo.” Hakupokea hisia ya iliyowekwa akilini mwake wakati wa kulinganisha mwenendo wake na kile kioo kikuu cha maadili (sheria). Hakuona kasoro zake za tabia. Hakufanya matengenezo, na akasahau hisia za uvuvio wote alizozipata, naye hakwenda katika njia ya Mungu, bali njia yake, akiendelea kuwa mtu asiye na matengenezo. {FEsw 460.1}

Sikia njia pekee iliyo sahihi kwa kila mwanadamu kutenda ikiwa yeye angekuwa na uzoefu salama, wenye hekima ya pande zote. “Lakini anayetazama ndani sheria kamilifu iliyo ya uhuru, na akaaye humo, yeye sio msikiaji msahaulifui, bali mtendaji wa kazi, [kwa maana kuna kazi inayopaswa kufanywa, nayo hupuuzwa kwa hatari ya nafsi], mtu huyo atakuwa heri katika kutenda kwake. Mtu akidhani ya kuwa anayo dini, wala hauzuii ulimi wake kwa hatamu, hali akijidanganya moyo wake, dini yake mtu huyo haifai. Dini iliyo safi, na isiyo na taka mbele za Mungu Baba ni hii, Kwenda kuwatazama yatima na wajane katika dhiki yao, na kujilinda na dunia pasipo mawaa.” Tenda hivi, kama mthani wa usafi wa moyo na dini isiyo na taka, na baraka ya Mwenyezi Mungu hakika itafuata. {FEsw 461.1}

“Kwa kuwa imeandikwa katika maandiko Tazama, naweka katika Sayuni jiwe kuu la pembeni, teule, lenye heshima, Na kila amwaminiye hatatahayarika..” Weka alama kwenye kielelezo kilichowasilishwa katika mstari tano: “Ninyi nanyi, kama

mawe yaliyo hai, mmejengwa kuwa nyumba ya kiroho; ukuhani mtakatifu, ili kutoa dhabihu za Roho, zinazokubalika kwa Mungu kwa njia ya Yesu Kristo.” Kisha mawe haya hai yanafanya yanashinikiza kazi inayoonekana. ushawishi wa vitendo katika nyumba ya kiroho ya Bwana. Wao ni ukuhani mtakatifu, unaofanya huduma safi, iliyo takatifu. Wanajitoa dhabihu za kiroho zinazokubalika kwa Mungu. {FEsw 461.2}

Bwana hatakubali huduma isiyo na moyo ndani yake, kwani ni msururu wa maadhimisho au sherehe ambazo kwa kweli hazina Kristo. Watoto Wake lazima wawe mawe hai katika jengo la Mungu. Ikiwa wote wangejitoa bila kujibakiza kwa Mwenyezi Mungu, kama wangeacha kusoma na kupanga mambo yao ya kujiburudisha wenyewe. kwa utalii na safari, na ushirika wa kupenda anasa, na kusoma Maneno yasemayo, “Au hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, mliyepewa na Mungu? Wala ninyi si mali yenu wenyewe; maana mlinunuliwa kwa thamani. Sasa basi, mtukuzeni Mungu katika miili yenu,” wasingepata njaa au kiu ya msisimko au mabadiliko. Ikiwa ni matamano yetu ya kweli kuwa watu wa kiroho, na ikiwa ni wokovu wa watu wetu unategemea kushikilia kwetu kwa uhodari kwenye Mwamba wa Milele, Je! haitakuwa bora kujishughulisha katika kutafuta yale ambayo yatasaidia kushikilia jengo lote kwenye lile Jiwe kuu la Pembeni, ili tusifadhaike na kuchanganyikiwa katika imani yetu. {FEsw 461.3}

“Basi, heshima hii ni kwenu ninyi mnaoamini. Bali kwao wasioamini, Jiwe walilolikataa waashi, Limekuwa jiwe kuu la pembeni. Tena, Jiwe la kujikwaza mguu, na mwamba wa kuangusha, Kwa maana hujikwaza kwa Neno lile, wasiliamini, nao waliwekwa kusudi wapate hayo.” Wanaume, wanawake, na vijana wote wanateuliwa kufanya kazi fulani. Lakini wengine hujikwaa kwa Neno la Kweli. Hili Neno halipatani na mielekeo yao na kwa hiyo wanakataa kuwa watendaji wa Neno. Hawavai nira ya Kristo ya utii mkamilifu kwa sheria ya Mungu. Wao hutazama nira hii kama mzungu, naye Shetani anawaambia kwamba kama wao watajitenga na hiyo nira ya Bwana, basi watakuwa kama miungu. Hakutakuwa na mtu kuwatawala au kuwaamuru; wataweza kufanya wapendavyo, na kuwa na uhuru wote wanaoutaka. Ni kweli, wameonewa na wamebanwa kwa kila njia katika maisha yao ya kidini, lakini yale ya maisha ya kidini yalikuwa ni kichekesho au mchezo tu. Wao waliteuliwa kuwa watenda kazi pamoja na Yesu Kristo, na kujifunga nira pamoja na Kristo ndiyo ilikuwa nafasi yao pekee ya wao kuwa na pumziko kamilifu na uhuru. Kama wangepanya hivi, kama wangepanya hivi wasingekerwa aukuona usumbufu. {FEsw 462.1}

“Bali ninyi ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa miliki ya Mungu; ili mwonyeshe [utoshelevu wenu, na kuvutia umakini wa watu kwenu, na kujitafuta Utukufu wenu mwenyewe? Hapana; hapana] *ni ili* mpate kuzitangaza fadhili Zake Yeye aliyewaita [kwa maisha ya kuchukiza, magumu ya utumwa?] *la ni ili* mtoke gizani mkaingie katika Nuru Yake ya ajabu.” {FEsw 462.2}

Je, unaweza kufikiria nafasi ya juu ambayo uliteuliwa kwayo, au ambayo ndiyo wito wako ulioitiwa? Je, wale wanaolitaja Jina la Kristo wataacha maovu yote? Je, wewe au mimi tutakuwa na wasiwasi na kuhangaikahangaika chini ya nira ya Kristo? Unapopenda misukosuko na ukosefu wa amani na pumbao, na kuwa na wakati wa kulisimka kwa mihemko kwa ajili ya kujionyesha mwenyewe (maonyesho binafsi), je, kuna pumziko lolote katika kuridhisha na kufurahisha mapenzi ya asili (anachopenda mtu wa asili au tamaa za mwili) badala ya kufanya mapenzi ya Mungu?, Je, hekalu la Mungu linazidi kuongezea kwa kimo katika maisha yako kwa ule mtazamo wa kipuuzi unaouchukua kwenye maisha yako ya Ukristo? "Mwe na mwenendo mzuri kati ya Mataifa, ili, iwapo huwasingizia kuwa watenda mabaya, wayatazamapo matendo yenu mazuri, wamtukuze Mungu siku ya kujiliwa." Je, Neno la Mungu halipaswi kuwa kiongozi na mwongozo wetu? Je, mtu achelewe kusoma Neno hilo? Je! Yule mtu anayedai kuwa Mkristo, aendelee tu na mwenendo wa matendo yanayoshutumu imani, kwa sababu tu, yeye anataka kuishi kwa kufurahisha mielekeo yaje mwenyewe ya asili? (mtu wa kale) Japo wameikiri imani katika ile Kweli, Je, watu hawa waendeleo kufuata njia ya kuitumia au kuiwakilisha vibaya imani hiyo na kudharau ile Kweli yenye asili ya Mbinguni? Watu ambao kabla ya hapa, wamethamini fursa za thamani walizopewa kabla ya muda wa kufungwa kwa mlango wa rehema, ili waweze kuunda tabia ambazo Mungu anaziidhinisha, kwa sababu wao wanavaa nira yao utii ambayo Kristo aliivaa? Je, Yeye Anasema nini kuhusiana na hili? "Jitieni nira Yangu, mjifunze Kwangu; kwa maana Mimi ni mpole na mnyenyekevu moyoni, nanyi mtapata raha nafsini mwenu. Kwa maana nira Yangu ni laini, na mzigo Wangu ni mwepesi." {FEsw 462.3}

Wengi wanaodai kumwamini Kristo hawavai nira yake. Wanafikiri kuwa wanafanya hivyo, lakini ikiwa hawakudanganyika na kuweweseshwa na Shetani, wangekuwa na mawazo yanayolingana na imani yao, na zile Kweli kuu wanazodai kuziamini. Wangeweza kutambua kwamba Maneno ya Kristo yana maana fulani kwao. "Kama ipo mtu atanifuata, na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake; na unifuata Mimi." Ukimfuata Yesu, wewe ni mfuasi Wake; ikiwa wewe unaifuata mihemko au misukumo yako mwenyewe, na moyo wako mwenyewe usiotakaswa, basi wewe unasema waziwazi, 'sitaki njia Yako, Ee Bwana, bali yangu.' {FEsw 463.1}

Tunapaswa kuipembua hali hiyo halisi, na kuamua kusudi letu ni nini. Nina shauku kubwa kwa vijana wa kiume na wa kike ambao wamejiandikisha katika jeshi la Bwana. Upendo wangu kwa Yesu Kristo unanibisha kwa Roho za wote ambao Kristo alikufa kwa ajili yao. Maneno, "Ninyi ni watendakazi pamoja na Mungu," yanamaanisha mengi. Hakuna mtu anaweza kuweka masharti na Mungu. Sisi ni watumishi wa Mungu aliye hai, na wote watacaoelimishwa katika shule yetu, wanapaswa kufundishwa kuwa watendakazii. Wanajitahidi/wanahenyeka kupata kanuni sahihi. Wanapaswa kuungana na Kristo kwa imani. Hivyo wanaweza kutoa ushuhuda wa kuridhika kukubwa kwa ulimwengu wa Mbinguni. Ikiwa kila mmoja aliyejitolea katika jeshi la Bwana atajitahidi kutenda kwa ubora wote kwa kadri

awezavyo, Mungu atafanya yaliyosalia. Hawapaswi kuita chochote kuwa chao. Wakati wa kujitahidi kupata ushindi, wanapaswa kujitahidi kwa uhalali. Neno linapaswa kuwa mwalimu wao. Tamaa isiyo takatifu haitawaendeleza, kwa maana Mungu pekee Ndiye anayeweza kuwapa hekima na ufahamu wa Kweli; Lakini Yeye hatafanya kazi na Shetani. Ikiwa husuda na tamaa isiyo takatifu inathaminiwa na kupendwa, ikiwa wanapigana mieleka ili kupata ushindi na kisha watukuzwe na wanadamu, akili itajazwa na kuchanganyikiwa. Jitahidi kufanya kile kilicho bora. Songeni mbele haraka iwezekanavyo ili kufikia kiwango cha juu katika mambo ya kiroho. Zamisheni nafsi zenu ndani ya Yesu Kristo, na kulenga daima kulitukuza Jina Lake. Kumbukeni kwamba talanta, elimu, cheo, mali, na ushawishi ni zawadi kutoka kwa Mungu; kwa hivyo mnapaswa kuviweka wakfu vitu vyote hivi Kwake. Itafuteni elimu ambayo itawastahilisha kuwa mawakili wenye hekima wa neema mbalimbali za Kristo Yesu, watumishi chini ya Kristo, walio tayari kutenda agizo Lake. {FEsw 463.2}

Hebu wanafunzi wote watafute kuwa na maoni mapana kuhusiana na wajibu wao kwa Mungu kwa kadri iwezekanavyo. Hawapaswi kungoja kufanya kazi kubwa inayoonekana mwisho wa muhula, wakati shule imefungwa. Lakini wanapaswa kujifunza kwa bidii jinsi wanavyoweza kuanza kufanya kazi kwa vitendo katika maisha yao ya uanafunzi kwa kujifunga nira pamoja na Kristo. Hebu kila msukumo uwe upande wa Bwana. Msiwavute chini na kuwakatisha tamaa walimu wenu. Msizilemee nafsi zao kwa kudhihirisha Roho yautovu wa nidhamu, mizaha na kutozingatia sheria. {FEsw 464.1}

Wanafunzi, wanaweza kuifanya shule hii kuwa ya daraja la kwanza kwa mafanikio, kwa kuwa watendakazi pamoja na walimu wenu na kuwasaidia wanafunzi wengine, kwa kujiinua kwa ari kutoka kwenye kiwango duni na cha chini, kile cha cha kawaida. Acheni kila mmoja aone maendeleo anayoweza kufanya ili kupatanisha mwenendo wake na sheria za Biblia. Wale ambao wanatafuta kuinuliwa na kuheshimiwa watashirikiana na Yesu Kristo kwa kusafisha semi zao (ndimi), katika tabia, na kuwa chini ya udhibiti wa Roho Mtakatifu. Wao wamefungwa nira pamoja na Yesu Kristo. Hawatamangamanga kwa hasira huku na kule, na kuwa watukutu na kujijali wenyewe, wakiwekea umakini anasa zao za ubinafsi na kujiridhisha. Wanaweka juhudi zao zote kutembea pamoja na Yesu Kristo kama wajumbe wa rehema na upendo Wake, wakiwahudumia wengine kwa kuwapa neema ya Bwana. Mioyo yao inadunda kwa umoja na moyo wa Kristo. Wao wako pamoja na Kristo katika Roho, wamoja na Kristo katika utendaji. Wanatafuta kuhifadhi akili pamoja na hazina za thamani za Neno la Mungu, ili kila moja afanye kazi aliyoteuliwa na Mungu kuifanya, kukusanya kwenye miale angavu ya Jua la Haki, ili wawaangazie wengine. {FEsw 464.2}

Ikiwa utakesha na kuomba, na kufanya juhudi za dhati katika mwelekeo ulio sahihi, utajazwa kabisa na Roho ya Yesu Kristo. “Bali mvaeni Bwana Yesu Kristo,

wala msiuangalie mwili, hata kuwasha tamaa zake.” Azimia kwamba utaifanya hii shule ifanikiwe, na ikiwa utatii maagizo yaliyotolewa katika Neno la Mungu, unaweza kusonga mbele kwa maendeleo ya uwezo wa kiakili na kiadili ambao utawafanya hata malaika wafurahi; na Mungu atakushangilia kwa kuimba. Ikiwa uko chini ya nidhamu ya Mungu, utapata maelewano na ushirikiano wa nguvu za kimwili, kiakili na kimaadili, na ukuaji kamili wa uwezo wako uliopewa na Mungu. Hebu misukumo ya furaha za kueleaelea angani na tamaa za mwili za ujana kupitia majaribu mengi zisitengeneze fursa na hali itakayoleta kushindwa. Siku kwa siku mvae Kristo, na katika msimu mfupi wa kutahiniwa na majaribu yako hapa chini duniani, dumisha uadilifu wako ndani ya nguvu za Mungu, kama mtendakazi pamoja na mawakala wa hali ya juu zaidi, wakati wa kipindi cha maisha yako ya usomi. {FEsw 465.1}

Wote wanapaswa kusema, sitashindwa. Kupitia ushawishi wangu, mimi sitasaliti nafsi yangu au maswahaba zangu mikononi mwa adui. Nitalishika Neno ya Bwana. “Au azishike nguvu Zangu, Afanye amani Nami; Naam, afanye amani Nami.” Siku zote kumbuka kwamba una Mmoja kando yako ambaye anakuambia, “Kuwa usiogope.” “Mimi nimeushinda ulimwengu.” Kumbuka kwamba Kristo alikuja kama Mkuu wa Mbinguni, na amehusika katika vita vya milele kinyume na kanuni za dhambi. Wote watakaoungana na Kristo watakuwa watendakazi pamoja na Mungu katika vita hivi. {FEsw 465.2}

“Kwa ajili yao najiweka wakfu Mwenyewe,” Kristo alisema, “ili na hao watakaswe kwa ile Kweli.” Bwana Yesu Ndiye Njia, Ukweli, na Uzima; na wale walioungana Naye, wakimvaa Yeye, watafanya kazi kama watendakazi pamoja Naye, kwa kuifuata kanuni ya Ukweli. Kwa kutazama, wanahuishwa na ile Kweli, na kuungana pamoja na Kristo kubadilisha hekalu hai lililotolewa kwa sanamu kabla ya hapo, kisha mwanadamu anaweza kutakaswa, kusafishwa, kuboreshwa, na kuwa hekalu kwa ajili ya kukaa kwa Roho Mtakatifu. {FEsw 466.1}

“Nimewatangazia Jina Lako,” Kristo alisema, “Tena nitawajulisha hilo; ili pendo lile ulilonipenda Mimi liwe ndani yao, Nami niwe ndani yao.” Bwana ametoa riziki tele kiasi ili kwamba Upendo Wake uweze kutolewa kwetu kama neema Yake ilivyo ya bure, na tele, kama urithi wetu katika maisha haya, ili kutuwezesha kusambaza kwa wengine sawa Naye, kwa kufungwa nira pamoja na Kristo. Yesu anabeba na kuleta uhai wenye nguvu, unaozunguka, ulio safi, uliotakaswa, upendo kama wa Kristo kupitia kila sehemu ya asili yetu ya kibinadamu. Upendo huu unapoonyeshwa katika tabia, huwawafunulia wale wote ambao tunashirikiana nao kwamba inawezekana kwa Mungu kuumbwa ndani yetu (Kol 1:27,28), tumaini la Utukufu. Inaonyesha kwamba Mungu aliwapenda wale watiifu jinsi anavyompenda Yesu Kristo; na hakuna chochote kidogo zaidi ya hiki kitakachoweza kuridhishamatamano Yake kwa niaba yetu. Punde tu mwanadamu anapounganishwa pamoja na Kristo moyoni, nafsini na Rohoni, Baba anaipenda

nafsi hiyo kama sehemu ya Kristo, kama kiungo cha mwili wa Kristo, Yeye Mwenyewe akiwa kichwa Kitukufu. {FEsw 466.2}— *MSS., June 21, 1897.*

Sura ya 58

BIBLIA KATIKA SHULE ZETU

Sio busara kuwapeleka vijana wetu kama wanafunzi katika vyuo vikuu ambavyo watatoa muda wao mwingi ili kupata ujuzi wa Kigiriki na Kilatini, wakati vichwa na mioyo yao inaendelea kujazwa na hisia za waandishi ambao ni makafiri, **nao wanakazana kuvisoma vitabu hivi ili kuziboboea lugha hizi.** Mwishowe hupata maarifa ambayo sio ya lazima kabisa, au yasiyopatana na masomo ya ya Yule Mwalimu mkuu. Kwa ujumla wale walioelimika kwa njia hii huwa watu wenye kiburi, wakijithamini wenyewe mno. Wanafikiri wamefikia kilele cha elimu yote, na kujivuna, kana kwamba wao hawahitaji kujifunza tena au kuwa wanafunzi kamwe. Hawa wanaharibiwa kwa ajili ya utumishi wa kazi ya Mungu. Ule wakati, mali, na masomo

ambayo wengi wametumia ili kuipata elimu hiyo isiyo na maana, wangepaswa kuutumia ili kupata elimu ambayo ingewafanya wao kuwa wanaume na wanawake wenye busara pande zote, wanaofaa katika maisha ya vitendo. Hapo ndipo elimu kama hiyo itakuwa ya thamani kubwa zaidi kwao. {FEsw 467.1}

Wanafunzi hubeba nini wanaondoka katika shule zetu? Je, wanaenda wapi? Na kisha watafanya nini huko? Je, wana ujuzi utakaowawezesha kuwafundisha wengine? Je, wameelimishwa ili kuwa wakina baba na mama wenye busara? Je, wanaweza kusimama kwenye kichwa cha familia kama wakufunzi wenye hekima? Je, katika maisha yao ya nyumbani wao wanaweza kuwaelekeza watoto wao kwamba wao watakuwa familia ambayo Mungu anaweza kuitazama kwa furaha, kwa sababu ni ishara ya familia Mbinguni? Je, ni kweli kwamba wao wamepata elimu pekee ambayo ndiyo inastahili kiukweli au kiuhalisia kuitwa “Elimu ya juu zaidi elimu”? {FEsw 467.2}

Elimu ya juu ni nini? Hakuna elimu inayoweza kuitwa ya juu zaidi elimu isipokuwa iwe na mfano wa Mbinguni, isipokuwa inaongoza vijana wa kiume na wa kike kuwa kama Kristo, na kuwastahilisha kusimama kama viongozi au wakuu wa kaya na familia zao mahali pa Mungu. Ikiwa, wakati wa shule maisha yake ya shule, kijana ameshindwa kupata ujuzi wa Kigiriki na Kilatini na hisia zilizomo katika kazi za waandishi makafiri, hakika hakujipatia hasara nyingi. Ikiwa Yesu Kristo angeona aina hii ya elimu ni muhimu, basi asingewapa wanafunzi Wake, ambao alikuwa akiwaelimisha kufanya kazi kubwa zaidi kuwahi kukabidhiwa kwa wanadamu, kumwakilisha Yeye katika ulimwengu? Lakini, badala yake, aliweka ile Kweli takatifu mikononi mwao, ili itolewe kwa ulimwengu kwa usahili/urahisi wake. {FEsw 467.3}

Kuna nyakati ambapo wasomi wa Kigiriki na Kilatini wanahitajika. Wengine inabidi wajifunze/wasomee lugha hizi. Jambo hili ni zuri. Lakini sio wote, na si wengi wanapaswa kuzisoma. Wale wanaodhani kuwa elimu ya Kigiriki na Kilatini ni muhimu kwa ile elimu ya juu, hawaoni mbali sana au mbele zaidi. Wala hakuna ujuzi, siri au mafumbo katika ile sayansi wanayoisomea au kuifanya wanadamu wa ulimwengu huu ambayo itakuwa msaada kwenye kuingia katika ufalme wa Mungu. Ni Shetani ndiye anayeijaza akili kwa ujanja na mapokeo ambayo yanatupilia mbali ile elimu ya juu na ya Kweli, na kuchukua hiyo elimu ambayo itaangamia na mwanafunzi anayeipata. {FEsw 468.1}

Wale ambao wamepokea elimu ya uwongo hawaonekani kuwa wanaelekea Mbinguni au wanaweka macho yao kuitazama mbingu kule juu. Hawawezi kumwona Yule aliye Nuru ya weli, “ambayo humtia Nuru kila mtu ajaye ulimwenguni.” Wanaangalia uhalisi wa milele kama uhalisia (fantomu), wakiita atomi ulimwengu, na ulimwengu atomi (chembe ndogo kabisa ya maada). Kati ya wengi waliopata kile kinachoitwa elimu ya juu, Mungu anatangaza, “Umepimwa katika mizani, nawe umeonekana umepunguka,” — kupunguka katika ujuzi wa

shughuli au stadi za vitendo, kuwa na mapungufu katika ufahamu wa jinsi ya kutumia vyema muda, kupungua katika maarifa ya jinsi ya kufanya kazi kwa ajili ya Yesu. {FEsw 468.2}

Asili ya mafundisho kwa vitendo ya Yule ambaye aliyatoa maisha Yake ili kuokoa watu ni, ushahidi tosha wa thamani ambayo anaiweka juu ya wanadamu. Alitoa elimu ambayo ndiyo peke yake tu inayoweza kuitwa Elimu Ya Juu. Yeye hakuwakataa wanafunzi Wake kwa sababu hawakupokea mafundisho yao kutoka kwa walimu wa kipagani na makafiri. Wanafunzi hawa walipaswa kutangaza Ukweli ambao utatikisa ulimwengu, lakini kabla hawajaweza kufanya hili, yaani kabla ya kuwa chumvi ya dunia, iliwapaswa kwanza waunde mazoea mapya, lazima waondoe vichwani mwao mengi yale mambo waliyojifunza kutoka kwa makasisi na marabi. Na hata hivi leo, wale ambao wange mwakilisha Kristo, lazima watengeneze mazoea mapya. Nadharia zenye asili inayotokana na ulimwengu lazima zitelekezwe. Maneno na matendo yao lazima yawe na mfano wa Bwana/mbingu. Hawapaswi kujiweka katika mahusiano yanayopelekea kufanya kanuni za Mungu kwenda chini, na kupungua thamani, na hisia ambazo ni za ibada kwa miungu mingine. Hawawezi kupata elimu yao kwa usalama kutoka kwa wale wasiomjua Mungu wala kumkiri kuwa Yeye Ndiye uzima na Nuru ya wanadamu. Watu hawa hakika ni wa ufalme mwingine. Wanatawaliwa na mkuu asiye mwaminifu, na wanachanganya viini macho au maluelue na uhalisia /ukweli. {FEsw 468.3}

Shule zetu hazipaswa kuwa kama zilivyo sasa. Muda ambao unapaswa kutolewa kufanya kazi kwa ajili ya Kristo umeshughulishwa na hata kuleta mchoko kwa mada zisizofaa na kujipendeza nafsi. Mabishano hutokea baada ya muda mfupi ikiwa maoni ambayo yametolewa na mtu yanapingwa/yanakatwa. Hivyo ndivyo ilivyokuwa kwa Wayahudi. Ili kutetea maoni yao binafsi maoni na maslahi madogo-madogo, ili kukidhi tamaa matamania ya ukuu wadunia, wao walimkataa Mwana wa Mungu. Muda unapita. Nasi tunakaribia mgogoro mkubwa katika historia ya dunia hii. Ikiwa walimu wataendelea kufumbia macho mambo muhimu yahusuyo wakati tunaoishi, basi wanapaswa kuachishwa kazi (watengwe na hiyo kazi). {FEsw 469.1}

Wengi wa wakufunzi katika shule za siku hizi hutenda udanganyifu kwa kuwaongoza wanafunzi wao kwenye uwanja wa masomo ambayo kwa kulinganisha hayana manufaa wala maana kabisa, masomo haya yanamchukulia mtu muda na fedha, kusoma, ambazo zilipaswa kutumika kupata elimu ile ya juu ambayo Kristo alikuja kutoa. Yeye alichukua juu Yake umbo la ubinadamu, ili Aweze kuinua akili kutoka kwa masomo ambayo watu waliyaona kuwa ya muhimu kwa masomo ambayo yanahusisha matokeo ya milele. Aliuona ulimwengu umefungwa katika udanganyifu wa kishetani. Yeye aliwaona watu wakifuata mawazo yao wenyewe kwa unyofu na bidii, wakifikiri kwamba wamepata kila kitu kama

wangeweza kupata jinsi ya kuitwa wakuu katika dunia hii. Lakini hawakupata chochote isipokuwa kifo. Kristo alichukua msimamo Wake, akisimama katika njia kuu na vichochoro visivyoonekana vya dunia hii, na kutazama juu ya umati unaotafuta furaha kwa matamania makubwa, wakifikiri katika mikakati yao na ubunifu wanaoupanga kwa siri na hila, walikuwa wamegundua jinsi wanavyoweza kuwa miungu katika dunia hii. Kristo aliwaelekezea watu juu, akiwaambia kuwa maarifa pekee yaliyo Kweli ni ujuzi (kumjua)wa Mungu na wa Kristo. Maarifa haya yataleta amani na furaha katika maisha haya ya sasa, na yaitwaa ile salama tuzo/Zawadi ya bure ya Mungu, uzima wa milele. Aliwahimiza wasikilizaji Wake, kama watu wenye uwezo wa kufikiri na hekima, wasipoteze umilele katika mahesabu au kukadiria kwao. "Tafuteni ninyi kwanza ufalme wa Mungu, na haki Yake," Yeye alisema, "na hayo yote mtazidishiwa." Ninyi basi ni watendakazi wenza pamoja na Mungu. Kwa sababu hii, Mimi Nimekununua kwa mateso Yangu, fedheha, na kifo. {FEsw 469.2}

Funzo kubwa la kutolewa kwa vijana ni kwamba, kama wale watu wanaomwabudu Mungu, wao wanapaswa kuthamini kanuni za Biblia, na kuuona ulimwengu ni wa chini au pungufu (kwa Bwana). Mungu angependa wote waelekezwe jinsi wanavyoweza kufanya kazi za Kristo, na kuingia kwenye milango ya mji wa Mbinguni. Hatupaswi kuuacha ulimwengu utuongoe sisi; bali sisi tunapaswa kujitahidi zaidi kwa bidii ili kuugeuza ulimwengu. Tumepewa na Kristo jukumu na fursa kwetu ya kusimama kwa ajili Yake chini ya hali zote. Nawasihi wazazi kuwaweka watoto wao mahali ambapo hawatarogwa ya elimu uongo/udanganyifu. Usalama wao pekee ni katika kujifunza juu ya Kristo. Yeye Ndiye Nuru kuu ambayo ni kitovu cha ulimwengu. Taa nyingine zozote, hekima nyingine zote, ni upumbavu.

Wanaume na wanawake ni ununuzi wa damu ya Mwana pekee wa Mungu. Wao ni mali ya Kristo, na elimu yao na mafunzo yanapaswa kutolewa, si kwa kurejelea maisha haya mafupi, yasiyo na uhakika bali katika yale maisha ya kutokufa, ambayo yanapimwa na kulinganishwa na maisha ya Mungu (milele). Sio mpango Wake kwamba wale ambao amenunua huduma zao watafunzwa kutumikia mali, kufunzwa kupokea sifa za kibinadamu, Utukufu wa mwanadamu, au kuwa chini ya ulimwengu. {FEsw 470.2}

"Basi Yesu akawaambia, Amin, amin, nawaambia, isipokuwa mnaula mwili Wake Mwana wa Adamu na kuinywa damu Yake, hamna maisha ndani yenu. Aulaye mwili Wangu na kuinywa damu Yangu yunao uzima wa milele; Nami nitamfufua siku ya mwisho. Kwa maana mwili Wangu ndio chakula hakika, na damu Yangu ni kinywaji hakika. Aulaye mwili Wangu, na kuinywa damu Yangu, hukaa ndani Yangu, Nami ndani yake." Haya ndiyo masharti ya maisha yaliyofanywa na Mkombozi wa ulimwengu, kabla ya misingi za ardhi ziliwekwa. Je, walimu katika shule zetu wanawapa wanafunzi kula mkate wa uzima? Wengi wao wanaongoza wao

wanafunzi kwenye njia ile ile ambayo wao wenyewe wameikanyaga. Wafikiria hii ndiyo njia pekee sahihi. Wanawapa wanafunzi chakula ambacho hakiwezi kudumisha maisha ya kiroho, lakini kile ambacho kitawafanya wale wanaoshiriki kufa. Wanavutiwa na kile ambacho Mungu haitaji wakijue. {FEsw 470.3}

Wale walimu ambao wamedhamiria kama vile makuhani na watawala, kubeba wanafunzi wao juu ya njia ile ile ya zamani ambayo dunia inaendelea kusafiri, wataingia kwenye giza kubwa zaidi. Wale ambao wangeweza kuwa watenda kazi pamoja na Kristo, lakini wamewakataa kwa chuki wajumbe na jumbe zao, watapoteza dhima/nanga zao. Wao watatembea gizani, bila kujua ni nini wanachojikwaa kwacho. Hao watakuwa tayari kudanganywa na udanganyifu unaorubuni akili wa siku ya mwisho. Akili zao zimejishughulisha na shauku ya mambomadogo, na hupoteza nafasi iliyobarikiwa ya kufungwa nira pamoja na Kristo, na kuwa watenda kazi pamoja pamoja na Mungu. {FEsw 471.1}

Mti unaoitwa wa ujuzi, umekuwa chombo cha kifo. Shetani amefuma kwa ustadi, kanuni za mafundisho yake ambayo anataka watu wayaone ndiyo ile Kweli, zile nadharia zake za udanganyifu ameziweka katika mafundisho yanayotolewa. Kutoka kwenye mti wa ujuzi yeye anazungumza maneno ya kupendeza yenye udanganyifu na kutia chumvi kwa kusifia watu zaidi kuhusian elimu ya juu. Maelfu hushiriki matunda ya mti huu, lakini kwao inamaanisha kifo. Kristo anawaambia: “Mnatumia fedha kwa kitu ambacho si chakula. Unatumia talanta zako ulizokabidhiwa na Mungu kupata elimu ambayo Mungu hutamka kuwa ni upumbavu.” {FEsw 471.2}

Shetani anajitahidi kupata kila faida. Anataka kujipatia, si wanafunzi tu, bali walimu pia. Ameweka mikakati yake tayari. Akiwa amejificha kama malaika wa Nuru, atatembea duniani kama mfanya miujiza. Katika lugha nzuri akiwasilisha hisia za juu. Maneno mazuri yatasemwa naye, na pia matendo mema. Watu watakuja kama makristo bandia (watamwigiza-Kristo atabinafsishwa), lakini katika hatua moja kutakuwa na tofauti kubwa ya alama. Shetani atawageuza watu kutoka kwa sheria ya Mungu. Licha ya hivyo, ataigiza haki bandia kwa kudanganya sana, hata yamkini, awadanganye wale walio wateule. Wafalme, marais, watawala katika mahali pa juu, watasujudia nadharia zake za uongo. Badala ya kutoa nafasi kwa ukosoaji, migawanyiko, wivu, na kushindana, wale walio katika shule zetu wanapaswa kuwa wamoja katika Kristo. Ni kwa njia hii tu ndiyo wanaweza kupinga vishawishi vya mdanganyifu mkuu. {FEsw 471.3}

Muda unapita, na Mungu anamwita kila mlinzi awe katika kituo chake. Amependezwa kutuongoza kwenye mgogoro mkubwa zaidi, kuliko yote iliyowahi kuweko tokea ujio wa kwanza wa Mwokozi wetu. Tufanye nini? Roho Mtakatifu wa Mungu ametuambia nini cha kufanya; lakini, kama vile Wayahudi walivyoikataa Nuru na kuchagua giza katika siku ya Kristo, vivyo hivyo ulimwengu wa kiroho/kidini utaukataa ujumbe wa leo. Watu wanaokiri utauwa wamemdharau Kristo katika

nafsi za wajumbe Wake. Kama Wayahudi, wao hukataa ujumbe wa Mungu. Wayahudi waliuliza kuhusu Kristo, "Huyu si Yesu mwana wa Yusufu?" Hakuwa Kristo ambaye Wayahudi walimtazamia. Kwa hivyo hata leo mawakala ambao Mungu hutuma sio wale ambao wanadamu wamewatazamia. Lakini Bwana hatamuuliza mtu yeyote, kwamba Yeye ampeleke nani. Atatuma yule amtakaye. Wanadamu wanaweza wasielewe kwa nini Mungu anamtuma huyu na si yule. Kazi Yake inaweza kuwa mada ya udadisi. Mungu hatakidhi udadisi huu; na Neno Lake halitarudi bure. {FEsw 472.1}

Acha kazi ya kuwatayarisha watu kusimama katika siku ya Mungu matayarisho ifanywe na wote waliaminio Neno. Kwa miaka michache iliyopita kazi kubwa, na makini imefanywa. Maswali mazito yamesumbua akili za wale wanaoamini Ukweli wa sasa (Ukweli wa leo). Nuru ya Mwana wa Haki imekuwa aking'aa kila mahali, na imepokelewa na baadhi, na kushikiliwa kwa ustahimilivu. Kazi ina imeendelezwa mbele katika mistari ya Kristo. {FEsw 472.2}

Kila nafsi inayotaja Jina la Kristo inapaswa kuwa chini ya utumishi. Wote wanapaswa kusema, "Mimi hapa; nitume." Midomo ambayo iko tayari kusema, ingawa ni najisi, itaguswa na kaa hai, na kutakaswa. Watawezeshwa kusema maneno ambayo yatawaka moto yakiwa njiani kuingia Rohoni. Wakati utakuja ambapo watu wataitwa kutoa hesabu ya nafsi ambazo wangepaswa kuwasilisha Nuru kwao, lakini ambao bado hawajaipokea. Wale ambao wameshindwa kutenda huo wajibu wao, ambao tayari walipewa Nuru, lakini hawakuithamini; na hivyo hawakuwa na cha kutoa kwa wengine, kwenye vitabu vya Mbinguni, wao wamewekwa pamoja na wale watu walio na uadui na Mungu, wasiotii mapenzi Yake au kuwa chini ya uongozi Wake. {FEsw 472.3}

Ushawishi wa Kikristo unapaswa kuenea katika shule zetu, nyumba zetu za Sanitarium, yaani tiba rahisi, nyumba zetu za uchapishaji. Chini ya uongozi wa Shetani, mashirikisho yataundwa, na yataundwa ili kuufunika Ukweli kwa njia ya ushawishi wa binadamu. Wale wanaojiunga na mashirikisho haya hawawezi kamwe kusikia ukaribisho unaosema, "Vema, mtumwa mwema na mwaminifu; ... ingia nawe katika furaha ya Bwana wako." Vyombo vilivyoanzishwa na Mungu vinapaswa kusonga mbele, bila kupatana na nguvu ya giza. Mengi zaidi lazima yafanywe katika mistari ya Kristo kuliko yale ambayo yamefanyika. {FEsw 473.1}

Uadilifu mkali unapaswa kuthaminiwa na kila mwanafunzi. Kila akili/nia na inapaswa kugeuka kwa uangalifu kwenye uchaji wa lile Neno la Mungu lililofunuliwa. Nuru na neema zitatolewa kwa wale wanaomtii Mungu kwa namna hiyo. Wataona mambo ya kushangaza katika sheria Yake. Kweli kuu ambazo zimelala bila kutiliwa umakini na kuonekana tangu siku ya Pentekoste, nazo zinatakiwa kung'aa kutoka kwa Neno la Mungu katika usafi wake wa asili. Kwa wale ambao wanampenda Mungu kweli, Roho Mtakatifu atafunua zile Kweli ambazo zimefifia akilini, na pia atafichua zile Kweli ambazo ni mpya kabisa. Wale ambao

hula mwili na kunywa damu ya Mwana wa Mungu, wataleta kutoka vitabu vya Danieli na Ufunuo vya Kweli ambayo imeihushwa na Roho Mtakatifu. Wataanza kwa msukumo wa vitendo ambavyo haviwezi kukandamizwa. Midomo ya watoto itafunguliwa kutangaza siri na mafumbo ambayo yamefichwa kutoka akilini mwa wanadamu. Bwana amechagua mambo ya kipumbavu ya dunia hii ili kuwaaibisha na kuwashangaza wenye hekima, na vitu dhaifu vya dunia, ili kuwaaibisha na kuwashangaza wenye nguvu. {FEsw 473.2}

Biblia haipaswi kuletwa katika shule zetu ili ichomekwe humo ndanindani kwenye ukafiri, kama tunavyoweka shimo kwenye tonge la ugali ili kuweka kitoweo (sandwiched). Biblia lazima iwe msingi na mada ya elimu. Ni kweli kwamba tunajua mengi zaidi ya Neno la Mungu aliye hai kuliko tulivyojua hapo awali, lakini bado kuna mengi ya kujifunza. Inapaswa kutumika kama Neno la Mungu aliye hai, na kuhesabiwa kuwa la kwanza (nambari moja), na la mwisho, na bora katika kila kitu. Ndipo kutaonekana ukuaji wa kweli wa kiroho. Wanafunzi watakuza tabia za kidini/kiroho zenye afya, kwa sababu wanakula nyama na kuinywa damu ya Mwana wa Mungu. Lakini bila ya kukesha na kuipa lishe tabia hii, afya ya Roho huharibika. Kaa kwenye mkondo wa Nuru. Jifunze Biblia. Wale wanaomtumikia Mungu kwa uaminifu watabarikiwa. Yeye asiyeruhusu kazi yoyote ya uaminifu kupita tu bila kutoa thawabu, atavika kila tendo la uaminifu na uadilifu kwa ishara za tuzo maalum la upendo Wake na idhinisho. {FEsw 474.1}— [The Review and Herald, August 17, 1897.](#)

Kwa Marejeleo ya Ziada

[A Lesson from the Three Hebrew Children, Signs of the Times, September 2, 1897](#)
[What Think Ye of Christ? The Youth's Instructor, September 16, 1897](#)

[The True Object of Education, The Youth's Instructor, March 31, April 7, 1898](#)
[Timothy, The Youth's Instructor, May 5, 1898](#)

[Parental Responsibility, The Review and Herald, May 10, 17, 1898](#)

[The Unseen Watcher, The Youth's Instructor, May 19, 26, 1898](#)

[God's Word Our Study Book, The Youth's Instructor, June 30, July 7, 1898](#)

[Prayer Our Stronghold, The Youth's Instructor, August 18, 1898](#)

[And the Grace of God was upon Him, The Youth's Instructor, September 8, 1898](#)
[The Higher Education, The Youth's Instructor, December 8, 1898](#)

[As a Child, The Desire of Ages, 68-74 {1898}](#)

[The Passover Visit, The Desire of Ages, 75-83 {1898}.](#)

USHUHUDA MAALUM KUHUSIANA NA SIASA

Kwa Walimu na Wasimamizi wa Shule zetu:

Wenye dhamana ya taasisi zetu na shule zetu wanapaswa kujilinda kwa uadilifu, ili kwa maneno na hisia zao wasiwaongoze wanafunzi katika njia za udanganyifu. Wale wanaofundisha Biblia katika makanisa yetu na katika shule zetu hawana uhuru wa kuungana katika kuzifanya dhahiri chuki zao kwa au dhidi ya watu au harakati za kisiasa (upendeleo wao), kwa sababu kwa kufanya hivyo wanachochea akili za wengine, wakiongoza kila mmoja kutetea nadharia yake anayoipenda. Wapo miongoni mwa wale wanaokiri kuuamini Ukweli wa sasa, ambao watachochewa kueleza hisia zao na matakwa ya kisiasa ili mgawanyiko huo uletwe kanisani.

{FEsw 475.1}

Bwana angetaka watu Wake wazike masuala na maswali ya kisiasa. Kwenye mada/washa hizi, ukimya ni ufasaha. Kristo anawaita wafuasi Wake kuja katika umoja juu ya kanuni safi za injili ambazo zimefunuliwa wazi katika Neno la Mungu. Hatuwezi kupiga kura kwa usalama kwa vyama vya siasa; maana hatujui tunampigia kura nani. Hatuwezi na usalama kushiriki katika mipango yoyote ya kisiasa. Hatuwezi kusumbuka kuwapendeza/kuwafurahisha watu ambao watatumia ushawishi wao kukandamiza uhuru wa kidini, na kuweka katika utendaji hatua kandamizi za kuwaongoza au kuwalazimisha wenzao (watu) kushika Jumapili kama Sabato. Siku ya kwanza ya juma sio siku ya kuheshimiwa. Ni sabato ya uongo, na washiriki wa familia ya Bwana hawawezi kushiriki na watu wanaoinua siku hii, na kuvunja sheria ya Mungu kwa kuikanyaga Sabato Yake. Watu wa Mungu hawapaswi kupiga kura kuwaweka watu kama hao katika ofisi; kwa kuwa wafanyapo hivi, wao wanashiriki pamoja nao katika dhambi watendazo wakiwa madarakani. {FEsw 475.2}

Hatupaswi kuafikiana na kanuni kwa kukubali maoni na chuki ambazo huenda tulizihimiza kabla ya kuungana pamoja na watu wa Mungu wazishikao amri. Tumejiandikisha katika jeshi la Bwana, na hatupaswi kupigana upande wa adui, lakini katika upande wa Kristo, ambapo tunaweza kuwa umoja kamili, katika hisia, katika matendo, katika Roho, na katika ushirika. Wale ambao ni Wakristo kweli watakuwa matawi ya mzabibu wa Kweli, nao watazaa matunda sawa, kama mzabibu. Watatenda kwa upatano, katika ushirika wa Kikristo. Hawatavaa beji za kisiasa, bali ni beji ya Kristo. {FEsw 475.3}

Tufanyeje basi? —Tuache masuala/maswali ya kisiasa. “Usifungiwe nira pamoja na wasioamini: Tena pana shirika gani kati ya Nuru na giza? Tena pana ulinganifu gani kati ya Kristo na Beliari? Au yeye aaminiye ana sehemu gani pamoja na yeye

asiyeamini?” Nini kinaweza kuwa cha kushirikiana pamoja kati ya vyama hivi? Hakuwezi kuwa na ushirika, hapana ushirika wenye umoja kiakili au kiroho. Neno ushirika lina maana ya ushiriki, ushirikiano. Mungu hutumia takwimu zenye nguvu zaidi kuonyesha kwamba inapaswa kuwa hakuna muungano kati ya vyama vya kidunia na wale wanaotafuta haki ya Kristo. Kuna ushirika gani kati ya Nuru na giza, Ukweli na udhalimu? —Hata hivyo. Nuru inawakilisha haki; haiwakilishi giza, makosa, dhambi, au udhalimu. Wakristo wametoka gizani na kuingia kwenye Nuru. Wamemvaa Kristo, nao wanavaa beji ya Ukweli na utii. Wao hutawaliwa na kanuni zilizoinuliwa na takatifu ambazo Kristo alizieleza katika maisha Yake. Lakini ulimwengu unatawaliwa na kanuni za ukosefu wa uaminifu na udhalimu. {FEsw 476.1}

“Kwa sababu hiyo, kwa kuwa tuna huduma hii, kwa jinsi tulivyopata rehema, hatulegei; lakini tumekataa mambo ya aibu yaliyositirika, wala hatuenendi kwa hila, wala kulichanganya Neno la Mungu na uongo; bali kwa kuidhihirisha iliyo Kweli twajionyesha kuwa na haki, dhamiri za watu zikitushuhudia mbele za Mungu. Lakini ikiwa injili yetu imesitirika, imesitirika kwa hao wanaopotea; ambao ndani yao Mungu wa dunia hii amepofusha fikira zao wasioamini, isiwazukie Nuru ya injili ya Utukufu Wake Kristo aliye sura Yake Mungu. Kwa maana hatujihubiri wenyewe, bali Kristo Yesu ya kuwa ni Bwana; na sisi wenyewe kuwa tu watumishi wenu kwa ajili ya Yesu. Kwa kuwa Mungu, aliyesema, Nuru itang'aa toka gizani, Ndiye aliyeng'aa mioyoni mwetu, atupe Nuru ya elimu ya Utukufu wa Mungu katika uso wa Yesu Kristo.” Vikundi viwili vimeletwa hapa ili kutazamwa, na imeonyeshwa kuwa hakuwezi kuwa na muungano kati yao. {FEsw 476.2}

Wale walimu kanisani au shuleni wanaojitofautisha wenyewe kwa bidii yao katika siasa, waondolewe/watolewe katika kazi na majukumu yao bila kuchelewa; kwa kuwa Bwana hatashirikiana pamoja nao. Zaka isitumike kumlipa mtu yeyote kufanya hotuba ya kujibu maswali ya kisiasa. Kila mwalimu, mchungaji, au kiongozi katika nyadhifa zetu ambaye anachochewa na nia ya kutoa maoni yake katika maswali ya kisiasa, anapaswa kuongolewa/kubadilishwa kwa imani katika Ukweli, au aache kazi yake. Ushawishi wake lazima ujulikane kama mtendakazii pamoja na Mungu katika kuleta Roho kwa Kristo, au cheo/sifa zake lazima ziondolewe kwake. Ikiwa hatabadilika, atafanya madhara, na madhara tu. {FEsw 477.1}

Kwa jina la Bwana ningewaambia walimu katika shule zetu, Shughulikieni kazi mliyopangiwa. Hujaitwa na Mungu kujihusisha na siasa. “Ninyi nyote mmekuwa ndugu,” Kristo atangaza, “na kawa watu wenye umoja mtasimama chini ya bendera ya Mkuu Imanueli (Prince Emmanuel).” “Na sasa, Israeli, Bwana, Mungu wako, anataka nini kwako, ila umche Bwana, Mungu wako, na kwenda katika njia Zake zote, na kumpenda, na kumtumikia Bwana, Mungu wako, kwa moyo wako wote, na kwa Roho yako yote; kuzishika amri za Bwana na sheria Zake, ninazokuamuru leo, upate uheri? ... Kwa maana Bwana, Mungu wenu, Yeye Ndiye Mungu wa miungu, na

Bwana wa mabwana, Mungu Mkuu, Mwenye kuogofya, asiyependelea nyuso za watu, wala hakubali rushwa. Huwafanyia yatima na mjane hukumu ya haki, Naye humpenda mgeni, akimpa chakula na mavazi. Basi, mpendeni mgeni, kwa sababu ninyi wenyewe mlikuwa wageni katika nchi ya Misri. Mche Bwana, Mungu wako, umtumikie Yeye; ambatana Naye, na kuapa kwa Jina Lake. Yeye Ndiye fahari yako, na Yeye Ndiye Mungu wako.....” Bwana ametoa Nuru kuu na mapendeleo kwa watu Wake. "Angalieni nimewafundisha amri na hukumu,” Anasema; "Zishikeni basi, mkazitende, maana hii ndiyo hekima yenu na akili zenu, machoni pa mataifa watakozisikia amri hizi zote, nao watasema, Hakika taifa hili kubwa ni watu wenye hekima na akili. Kwa maana liko taifa gani kubwa, lililo na Mungu aliye karibu nao, kama Bwana, Mungu wetu, alivyo, kila tumwitapo? Tena liko taifa gani kubwa, lililo na amri na hukumu zenye haki kama torati hii yote, ninayoiweka mbele yenu leo. Lakini, jihadhari nafsi yako, ukailinde Roho yako kwa bidii, usije ukayasahau mambo yale uliyoyaona kwa macho yako, yakaondoka moyoni mwako siku zote za maisha yako; bali uwajulishe watoto wako na watoto wa watoto wako;” {FEsw 478.1}

Kama watu, tunapaswa kusimama chini ya bendera ya Yesu Kristo. Tunapaswa kujiweka wakfu kwa Mungu kama watu wa tofauti, waliojitenga, na watu wa kipekee. Anazungumza nasi, akisema, “Tegeni masikio yenu, na njooni kwangu: sikieni, na nafsi zenu zitaishi; nami nitafanya agano la milele pamoja nanyi, rehema za hakika za Daudi.” “Utathibitika katika haki; utakuwa mbali na kuonewa, kwa maana hutaogopa; na mbali na hofu, kwa maana haitakukaribia. Tazama, yamkini watakusanyana; lakini si kwa shauri langu. Watu wo wote wataokusanyana juu yako wataanguka kwa ajili yako..... Kila silaha itakayofanyika juu yako haitafanikiwa na kila ulimi utakaoinuka juu yako katika hukumu utauhukumu kuwa mkosa. Huu ndio urithi wa watumishi wa Bwana, na haki yao inayotoka Kwangu Mimi, asema Bwana.” {FEsw 478.2}

Natoa wito kwa ndugu zangu walioteuliwa kuelimisha, kubadilisha mwenendo wao. Ni makosa kwako kuunganisha shauku yako na chama chochote cha kisiasa, kupiga kura yako pamoja nao au kwa ajili yao. Wale wanaosimama kama waelimishaji, kama wachungaji, kama watenda kazi pamoja na Mungu katika mstari wowote, wasiwe na mapambano ya kupigana katika ulimwengu wa kisiasa. Wenyeji wao uko Mbinguni. Bwana anawaita wasimame kama watu tofauti na wa kipekee. Yeye hapendi kuwe na mafarakano ya mwili wa waumini. Watu wake wanapaswa kumiliki vipengele vya upatanisho. Je, ni kazi yao kutengeneza maadui katika ulimwengu wa kisiasa? —La, hapana. Wanapaswa kusimama kama raia wa ufalme wa Kristo, wakiwa na bendera ambayo imeandikwa, “Amri za Mungu, na imani ya Yesu.” Wanapaswa kubeba mzigo wa maalum kazi, ujumbe maalum. Tuna jukumu la kibinafsi, na hili litafunuliwa mbele ya ulimwengu wa Mbinguni, mbele ya malaika, na mbele ya wanadamu. Mungu hatuiti sisi kuongeza ushawishi wetu kwa kuchanganyika na jamii, kwa kuungana na watu katika masuala ya kisiasa, bali kwa

kusimama kama mtu mmoja mmoja ambao ni sehemu ya ufalme Wake mzima, pamoja na Kristo kama kichwa chetu. Kristo Ndiye Mkuu wetu, na kama raia Wake tunapaswa kufanya kazi aliyotuagiza Mungu. {FEsw 478.3}

Ni jambo la muhimu sana kwamba vijana waelewe hivyo, kwamba Watu wa Kristo wanapaswa kuunganishwa katika umoja; kwa kuwa umoja huu unawafunga wanadamu na Mungu kwa kamba za dhahabu za upendo, na humweka kila mmoja chini ya wajibu wa kufanya kazi kwa wanadamu wenzake. Kapteni wa wokovu wetu alikufa kwa ajili ya jamii ya wanadamu iweze kufanywa kuwa kitu kimoja Naye na kila mmoja wao (kati yao wenyewe). Kama washiriki wa familia ya wanadamu sisi ni sehemu ya mtu mmoja, mmoja binafsi, sisi ni kiungo kimoja kimoja katika mwili wenye uwezo. Hakuna nafsi inayoweza kuwa huru kutoka kwa nyingine. Kusiwe na ugomvi wa chama katika familia ya Mungu; kwani ustawi ya kila mmoja ni furaha ya ujumla {wote}. Hakuna kuta zinazopaswa kujengwa kati ya mtu na mtu. Kristo kama kituo kikuu lazima aunganishe wote kuwa kitu kimoja. {FEsw 479.1}

Kristo Ndiye mwalimu wetu, mtawala wetu, nguvu zetu, haki yetu; na ndani Yake tumeahidiwa kujiepusha na mwenendo wowote utakaofanya kusababisha mgawanyiko. Maswali yanayozungumzwa ulimwenguni hayapaswi kuwa mada ya mazungumzo yetu {trending news}. Tunapaswa kuuita ulimwengu umtazame Mwokozi aliyeinuliwa, ambaye kupitia Kwake tunabidishwa kuwa wa lazima kwa mmoja mwingine na kwa Mungu. Kristo anawazoeza raia Wake kuiga wema Wake, Upole na unyenyekevu Wake, wema Wake, subira, na upendo. Hivyo Anauweka wakfu moyo na mkono kwa ajili ya huduma Yake, na kumfanya mwanadamu kuwa chaneli/mfereji ambao kwao upendo wa Mungu unaweza kutiririka katika mikondo yenye utajiri/wingi ili kubariki wengine. Basi kusiwe na kivuli cha ugomvi kati ya Waadventista Wasabato (Waadventista wa siku ya Saba). Mwokozi anaalika kila nafsi, "Njooni Kwangu, ninyi nyote msumbukao na kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha. Chukueni nira Yangu na jifunzeni Kwangu; kwa maana Mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo; nanyi mtapata raha nafsiini mwenu. Kwa maana nira Yangu ni laini, na Mzigo Wangu ni mwepesi." Yeye anayekaribia kwa ukaribu zaidi, ukamilifu wa Ukarimu wa Kimungu wa Kristo husababisha furaha kati ya malaika wa Mbinguni. Baba hufurahi juu yake kwa kuimba; kwani yeye hufanya kazi ndani ya Roho wa Bwana, mmoja na Kristo kama Yeye alivyo mmoja na Baba {FEsw 479.2}

Katika majarida yetu hatupaswi kuinua kazi na tabia za watu katika nafasi za ushawishi, kuweka binadamu mbele ya watu daima. Lakini unaweza kumwinua Kristo Mwokozi wetu kwa kadiri upendavyo. "Lakini sisi sote, kwa uso usiotiwa utaji, tukiurudisha Utukufu wa Bwana, kama vile katika kioo, tunabadilishwa tufanane na mfano uo huo, toka Utukufu hata Utukufu [kutoka tabia hadi tabia], kama vile kwa Utukufu utokao kwa Bwana, aliye Roho. Wale wanaompenda na kumtumikia Mungu wanapaswa kuwa Nuru ya Mungu ulimwenguni, ikiangaza katikati ya giza la kiadili.

Lakini katika maeneo ambayo yamepewa Nuru kuu zaidi, ambapo injili imehubiriwa watu wengi zaidi, –baba, mama, na watoto–wamekuwa wakiongozwa na nguvu kutoka chini ili kuunganisha maslahi yao na miradi na makampuni ya kidunia.

{FEsw 480.1}

Upofu mkubwa uko juu ya makanisa, na Bwana anawaambia watu Wake, “Tena pana mapatano gani kati ya hekalu la Mungu na sanamu? Kwa kuwa ninyi ni hekalu la Mungu aliye hai; kama Mungu alivyosema, nitakaa ndani yao, na kuenenda ndani yao; Nami nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu Wangu. Kwa hiyo tokeni kati yao, na kuwa ninyi jitengeni, asema Bwana, wala msiguse kitu kilicho najisi; Nami nitawapokea, nami nitakuwa baba kwenu, nanyi mtakuwa Wanangu na binti, asema Bwana wa majeshi.” {FEsw 480.2}

Tena pana mapatano gani kati ya hekalu la Mungu na sanamu? Kwa maana sisi tu hekalu la Mungu aliye hai; kama Mungu alivyosema, ya kwamba, Nitakaa ndani yao, na kati yao nitatembea, Nami nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu Wangu. Kwa hiyo, Tokeni kati yao, Mkatengwe nao, asema Bwana, Msiguse kitu kilicho kichafu, Nami nitawakaribisha. Nitakuwa Baba kwenu, Nanyi mtakuwa kwangu Wanangu wa kiume na wa kike, Asema Mwenyezi Mungu.” Hali ya kupokelewa katika familia ya Bwana ni kutoka katika ulimwengu, kujitenga na athari zake zote, zinazoambukiza na kuchafua. Watu wa Mungu hawapaswi kuwa na uhusiano wowote na ibada ya sanamu ya maumbo yake. Wanapaswa kufikia kiwango cha juu zaidi. Tunapaswa kuwa kutofautishwa na ulimwengu, na kisha Mungu anasema, “Nitakupokea kama Washiriki wa familia Yangu ya kifalme, watoto wa Mfalme wa Mbinguni.” Kama waaminio Ukweli tunapaswa kuwa tofauti kimatendo na dhambi na wenye dhambi. Uraia wetu uko Mbinguni. {FEsw 481.1}

Tunapaswa kutambua kwa uwazi zaidi, thamani ya ahadi ambazo Mungu ametuwekea sisi, na kuthamini kwa undani zaidi heshima ambayo ametupa. Mungu hawezi kuwapa wanadamu heshima kubwa zaidi ya ile ya kuwaasilisha (adopt) katika familia Yake, akiwapa upendeleo wa kumwita Yeye Baba. Hakuna kudhalilishwa katika kufanyika watoto wa Mungu. “Watu Wangu watalijua Jina Langu,” asema Bwana; “Kwa hiyo watu Wangu watalijua Jina Langu kwa hiyo watajua siku ile ya kuwa Mimi Ndimi ninenaye; tazama ni Mimi.” Mungu Mungu muweza wa yote anatawala. “Jinsi ilivyo mizuri juu ya milima Miguu yake aletaye habari njema, Yeye aitangazaye amani, Aletaye habari njema ya mambo mema, Yeye autangazaye wokovu, Auambiaye Sayuni, Mungu wako anamiliki! Sauti ya walinzi wako! Wanapaza sauti zao, wanaimba pamoja; Maana wataona jicho kwa jicho, Jinsi Bwana arejeavyo Sayuni.” {FEsw 481.2}

Kwa nini umakini mkubwa unatolewa kwa mawakala wa kibinadamu, wakati kuna ufikiaji mdogo sana wa akili kwa Yule Mungu wa milele? Kwa nini wale wanaodai kuwa watoto wa Mfalme wa Mbinguni wanazama/wanamezwa sana na mambo ya dunia hii? Hebu Bwana na atukuzwe. Acha Neno la Bwana litukuzwe na

kukuzwa. Wanadamu na wawe chini, na Bwana ainuliwe. Kumbuka kwamba falme za kidunia, mataifa, wafalme, viongozi, washauri, majeshi makubwa, na fahari zote za kidunia na Utukufu ni kama tu mavumbi kwenye mizani. Mungu ana hesabu ya kufanya na mataifa yote. Kila ufalme unapaswa kushushwa chini. Mamlaka ya binadamu yanapaswa kufanywa kuwa si kitu (sifuri). Kristo ni Mfalme wa ulimwengu, na Ufalme Wake ni utatukuzwa (na kuinuliwa). {FEsw 481.3}

Bwana anatamani wote wanaobeba ujumbe wa siku hizi za mwisho kuelewa kuwa kuna tofauti kubwa kati ya wale wanaokiri dini ambao si watendaji wa Neno (maprofesa wa dini), na watoto wa Mungu, ambao wametakaswa kwa ile Kweli, ambao wana imani ile itendayo kazi kwa upendo na kutakasa Roho. Bwana anazungumza juu ya wale wanaodai kuamini Ukweli kwa wakati huu, lakini wasione ubaya wowote kwa wao kushiriki katika siasa, kuchanganyika na vipengele vinavyoshindana au kugombana vya siku hizi za mwisho, kama wale waliotahiriwa wanaochangamana na wasiotahiriwa, Naye anatangaza kwamba atawaangamiza watu wa tabaka zote mbili pamoja. bila ubaguzi. Wanafanya kazi ambayo Mungu hajawawekea kufanya. Wanamvunjia Mungu heshima kwa Roho ya 'vyama' na ugomvi, na Naye atawahukumu wote wawili sawa. {FEsw 482.1}

Swali linaweza kuulizwa, Je, tusiwe na muungano wowote na dunia? Neno la Bwana ndilo liwe kiongozi wetu. Uhusiano wa aina yoyote na makafiri na wasioamini ambao ungetutambulisha pamoja nao umepigwa marufuku na Neno. Tunapaswa kutoka kwao, na kujitenga. Kwa hali yoyote hatupaswi kujihusisha nao katika mipango au kazi zao. Lakini hatupaswi kuishi maisha ya kujitenga. Sisi ni tunapaswa kuwafanyia walimwengu mema yote tuwezayo. Kristo ametupa mfano kwa hili. Alipoalikwa kula pamoja na watoza ushuru na wenye dhambi, Yeye hakukataa; kwani hakuna njia nyingine isipokuwa kuchanganyika nao ndiyo angeweza kulifikia tabaka hili. Lakini katika kila tukio aliwapa talanta za maneno na ushawishi. Alifungua mada za mazungumzo ambazo zilileta mambo yenye maslahi/manufaa ya milele katika akili zao. Na Mwalimu huyu anatuagiza, "Vivyo hivyo Nuru yenu na iangaze mbele ya watu, wapate kuona matendo yenu mema, na kumtukuza Baba yenu aliye Mbinguni." Kuhusiana na suala la kiasi chukua msimamo wako bila kuyumba. Kuwa imara kama mwamba. Msishiriki dhambi za watu wengine. Matendo ya ukosefu wa uaminifu katika biashara (dili za biashara), na waumini au wasioamini, unapaswa kukemewa; na kama hawatoi ushahidi wa matengenezo, basi tokeni kutoka miongoni mwao na kujitenga. {FEsw 482.2}

Kuna shamba kubwa la mizabibu la kulimwa; japo Wakristo wanapaswa kufanya kazi miongoni mwa wasioamini, hawapaswi kuwa na mwonekano kama wa walimwengu. Hawapaswi kutumia muda wao kuzungumza siasa au kutenda kama wanasiasa; kwani kwa kufanya hivyo, watampa adui nafasi ya kuingia na kusababisha tofauti na mifarakano. Wale walio katika huduma wanaotamani kusimama kama wanasiasa wanapaswa kuondolewa katika nyadhifa zao; kwa

maana kazi hii Mungu hajaiweka juu au chini miongoni mwa watu Wake. Mungu anawaita wote wanaohudumu katika Mafundisho ya imani, kutoa tarumbeta sauti fulani. Wote waliompokea Kristo, wachungaji na walei (wanaolipwa na wasiolipwa), wanapaswa kuinuka na kuangaza; kwa maana hatari kubwa iko karibu yetu kabisa. Shetani anachochea nguvu za dunia. Kila kitu duniani ni kiko katika hali ya kuchanganyikiwa. Mungu anawaita watu Wake kuinua juu bendera inayobeba ujumbe wa malaika wa tatu. Hatupaswi kwenda kwa Kristo kupitia kwa mwanadamu yeyote, lakini kwa njia ya Kristo tunapaswa kuelewa kazi ambayo ametupa kufanya kwa ajili ya wengine. {FEsw 483.1}

Mungu anawaita watu Wake, akisema, “Tokeni kati yao, na jitengeni.” Anauliza kwamba upendo ambao Yeye ameuonyesha kwa ajili yao, wao wanaweza kurudisha mwitikio kwa huo na kuuonyesha kwa utii wa hiari kwa Amri Zake. Watoto Wake wanapaswa kujitenga na siasa, kutoka kwa muungano wowote na wasioamini. Hawapaswi kuunganishwa maslahi yao na maslahi ya dunia. “Toa uthibitisho wako wa utii Kwangu” Anasema, “kwa kusimama kama urithi Wangu mteule, kama watu wenye juhudi katika matendo mema.” Usishiriki katika ugomvi wa kisiasa. Jitenge na ulimwengu, na ujiepushe katika kuleta kanisani au shule mawazo ambayo yatasababisha ugomvi, utengano au machafuko. Mfarakano ni sumu ya kimaadili inayoingizwa kwenye mfumo na wanadamu ambao ni wabinafsi. Mungu anataka watumishi Wake wawe na utambuzi ulio wazi, ulio wa kweli na hadhi bora, ili ushawishi wao uweze kuonyesha nguvu ya ile Kweli. Maisha ya Kikristo hayapaswi kuwa ya kubahatisha au kiholela, maisha ya kihisia. Ushawishi wa Kweli wa Kikristo, ulioshinikizwa kwa ajili ya kukamilisha kazi ambayo Mungu ameweka, ni wakala wa thamani, na hayapaswi kuwa na umoja na siasa, au kufungwa katika muungano na makafiri. Mungu anapaswa kuwa kitovu cha kivutio. Kila akili inayofanyiwa kazi na Roho Mtakatifu itaridhika/itaridhishwa Naye. {FEsw 483.2}

Mungu anawataka walimu katika shule zetu kutovutiwa na masomo ya masuala/maswali ya kisiasa. Chukua maarifa ya Mungu katika shule zetu. Usikivu wako unaweza kuitwa kwa watu wenye hekima wa kidunia, ambao hawana hekima ya kutosha kuelewa Maandiko yanasema nini ndani yake kuhusu sheria za ufalme wa Mungu; bali geuka kutoka kwa watu hawa na kuelekea kwa Yule ambaye Ndiye chanzo cha hekima yote. Utafuteni kwanza ufalme wa Mungu na Haki Yake. Fanya hili la kuwa la kwanza na la mwisho. Tafuta kwa bidii zaidi kumjua Yeye ambaye kumjua Yeye kwa usahihi ni uzima wa milele. Kristo na haki Yake ni wokovu wa Roho. Wafundishe watoto wadogo nini maana ya utii na kujisalimisha maana yake ni nini. Katika shule zetu sayansi, fasihi, kupaka rangi, uchoraji, na muziki, na yote ambayo ulimwengu unaweza kufundisha hayapaswi kufanywa nambari moja. Hebu ujuzi Wake Yeye ambaye umilele maisha yetu umekita Kwake, awe wa kwanza. Panda katika mioyo ya wanafunzi lile ambalo litapamba tabia na kufaa nafsi, kwa njia ya utakaso wa Roho, ili kujifunza masomo kutoka kwa Mwalimu

mkuu zaidi ambaye ulimwengu umewahi kujua. Hivyo wanafunzi watafaa kuwa warithi wa ufalme ya Mungu. {FEsw 484.1} – *Letter 95, June 16, 1899.*

Kwa Marejeleo ya Ziada

God's Purpose Concerning Our Youth Today, The Youth's Instructor, June 22, 29, 1899

Marriages, Wise and Unwise, The Youth's Instructor, August 10, 1899

Self-culture, The Youth's Instructor, August 17, 1899

True Education, The Youth's Instructor, August 31, 1899

The Need of Reform in Our Educational Work, General Conference Daily Bulletin, March 6, 1899

The Tree of Life and the Tree of Knowledge, General Conference Daily Bulletin, March 6, 1899

The Need of Church Schools, General Conference Daily Bulletin, March 6, 1899

The Apostle Paul and Manual Labor, The Review and Herald, March 6, 13, 1900

The student's s Privileges and Responsibilities, The Youth's Instructor, May 3, 10, 1900

The example of Solomon, The Bible Echo, May, 1900

Our Words, The Youth's Instructor, July 26, 1900

Our Influence, The Youth's Instructor, August 2, 1900

A Lesson from Daniel's Experience, The Youth's Instructor, September 6, 1900

Words to the Youth, The Youth's Instructor, October 25, 1900

The Burning Bush, The Youth's Instructor, December 13, 1900

From the Natural to the Spiritual, Christ's Object Lessons, 17-27

The Talents, Christ's Object Lessons, 325-369

Children's Meetings and Church Schools, Testimonies for the Church, 6:105-109

Need of Educational Reform, Testimonies for the Church, 6:126- 140

Hindrances to Educational Reform, Testimonies for the Church, 6:141-151

Character and Work of Teachers, Testimonies for the Church, 6:152- 161

Words from a Divine Instructor, Testimonies for the Church, 6:162- 167

School Homes, Testimonies for the Church, 6:168-170
 Industrial Reform, Testimonies for the Church, 6:176-180
 The Avondale School Farm, Testimonies for the Church, 6:181-198
 Church Schools, Testimonies for the Church, 6:193-205
 School Management and Finance, Testimonies for the Church, 6:206-218
 The Importance of Voice Training, Testimonies for the Church, 6:380-383
 The Relief of Our Schools, Testimonies for the Church, 6:468-478
 Idleness is Sin, The Youth's Instructor, January 31, February 7, 1901
 Our Duty as Parents, Signs of the Times, April 3, 1901
 How to Meet Criticism, The Youth's Instructor, April 4, 1901
 No Other Gods Before Me, The Review and Herald, September 10, 1901
 The Mother's Work, Signs of the Times, January 1, 1902
 God's Purpose for the Youth, The Youth's Instructor, February 13, 1902
 Lesson for Mothers Signs of the Times, Signs of the Times, February 26, 1902
 The Blessing of Labor, The Youth's Instructor, February 27, 1902
 What Shall the Youth Read? The Youth's Instructor, October 9, 1902
 Centers of Influence, Testimonies for the Church, 7: 231-234
 To the Teachers in Our Schools, Testimonies for the Church, 7: 267- 276
 The Divine Teacher, The Youth's Instructor, March 19, 1903
 Sowing Beside all Waters, The Review and Herald, July 14, 1903
 Words to Parents Signs of the Times, Signs of the Times, September 16 , 1903
 Lessons from the Life of Daniel, The Youth's Instructor, April 23- February 2, 1904
 1903 Publication of the book "Education (See table of contents for topics treated)
 Lessons from the Life of Daniel, The Youth's Instructor, March 8, 1904
 Cooperation between the Home and School, The Review and Herald, April 21, 1904

Sura ya 60

KUPANDA KANDO YA MAJI YOTE

Kwa mwaliko nilihudhuria mkutano uliofanyika Healdsburg uliohusiana na kufungwa kwa mwaka wa shule, Mei 29, 1903. nimefurahi kujua kwamba walimu na wanafunzi walikuwa wameungana pamoja katika kuyaondoa mazoezi ya kuchosha na yasiyo na faida ambayo kwa kawaida hufanyika wakati wa kufungwa kwa shule, na kwamba nguvu za wote, kwa kiasi kikubwa sana, zilijitolewa kwa mafunzo yenye faida. {FEsw 487.1}

Siku ya Ijumaa asubuhi vyeti vilikabidhiwa kimya kimya kwa wale ambao walikuwa na haki ya kuvipata, na kisha wanafunzi na walimu wakaungana katika mkutano wa uzoefu (ushuhuda), ambapo wengi walisimulia baraka walizokuwa wamepokea bure kutoka kwa Mungu katika mwaka huo. {FEsw 487.2}

Asubuhi ya Sabato nilizungumza na hadhira kubwa katika jumba la mikutano la kanisa la Healdsburg. Wanafunzi na walimu walikuwa wameketi mbele, na nilibarikiwa kuwasilisha kwao wajibu wao kama watenda kazi pamoja na Mungu. Mwokozi anatoa wito kwa walimu na wanafunzi wetu kutoa huduma kwa ufanisi kama wavuvi wa watu. {FEsw 487.3}

Jioni umati mkubwa ulikusanyika kanisani kusikiliza programu ya muziki inayotolewa na Ndugu Beardslee na wanafunzi wake. Uimbaji mizuri ni sehemu muhimu ya kumwabudu Mungu. Nimefurahi kwamba Ndugu Beardslee anawafunza wanafunzi, ili waweze kuwa wainjilisti waimbaji. {FEsw 487.4}

Nilifurahishwa sana na kile nilichokiona shuleni. Mwaka uliopita umekuwa na maendeleo makubwa. Walimu na wanafunzi pia, wanafikia juu na bado juu zaidi katika maisha ya kiroho. Kipindi cha mwaka uliopita kumekuwa na uongofu wa ajabu. Kondoo waliopotea walipatikana na kurudishwa kundini. {FEsw 487.5} — *The Review and Herald, July 14, 1903.*

Sura ya 61

KAZI YA SHULE ZETU ZA MAFUNZO

Kazi za vyuo vyetu na shule za mafunzo zinapaswa kuimarishwa mwaka hadi mwaka. {FEsw 488.1}

Hakuna Wakati wa Kuchelewa

Muda ni mfupi. Watenda kazi kwa ajili ya Kristo wanahitajika kila mahali. Leo kunapaswa wawepo watenda kazi mia moja wenye bidii, na waaminifu ndani na nje ya nchi kwenye maeneo ya utume ambapo sasa kuna mmoja tu. Barabara kuu na vinjia visivyopitwa na watu wengi, bado havijafanyiwa kazi. Vivutio vya haraka vinapaswa kutolewa kwa wale ambao wanajishughulisha na kazi ya umishonari kwa ajili ya Bwana. {FEsw 488.2}

Dalili zinazoonyesha kwamba kuja kwa Kristo kumekaribia zinazidi kutimizwa haraka sana. Bwana anawaita vijana wetu kufanya kazi kama wamishenari wa vitabu na wainjilisti, kufanya kazi ya kwenda nyumba kwa nyumba katika maeneo ambayo bado hayajaisikia ile Kweli. Anazungumza na vijana wetu, akisema, “Au hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, mliyepewa na Mungu? Wala ninyi si mali yenu wenyewe; maana mlinunuliwa kwa thamani. Sasa basi, mtukuzeni Mungu katika miili yenu.” Wale ambao watakwenda kufanya kazi chini ya maelekezo ya Mungu watabarikiwa kwa namna ya ajabu. Wale ambao katika maisha haya wanatenda vyema kwa kadri wawezavyo ili watajistahilisha kwa ajili ya siku zijazo, yale maisha ya kutokufa. {FEsw 488.3}

Bwana anawaita watu wa kujitolea ambao watachukua msimamo wao kwa uthabiti Upande Wake, na watajitolea wenyewe kuungana na Yesu wa Nazareti katika kufanya kazi ile ile inayohitaji kufanywa sasa, **sasa hivi hivi.** {FEsw 488.4}

Wapo miongoni mwetu vijana wengi wa kiume na wa kike ambao kama ilivyo kawaida yao, endapo vivutio vitatolewa, wao wangependelea kuchukua kozi za masomo kwa miaka kadhaa huko Battle Creek. Lakini je, jambo hili litalipa? Vipaji

vya Watu wa Mungu vinapaswa kuajiriwa katika kutoa ujumbe wa mwisho wa rehema kwa ulimwengu. Bwana anawaita wale waliounganishwa na Sanitarium, nyumba za uchapaji, na taasisi nyingine kuwafundisha vijana kufanya kazi ya uinjilisti. Wakati na pesa zetu hazipaswi hazipaswi kushughulishwa/kuajiriwa kwa wingi katika kuanzisha vituo vya Sanita, viwanda vya chakula, maduka ya vyakula, na migahawa, wakati kazi zingine zimepuuzwa. Vijana wa kike na wa kiume ambao wanapaswa kushiriki katika huduma ya Kazi ya Biblia, na katika kazi ya kuhubiri, hawapaswi kufungwa kwa ajira ya shughuli za kila siku kama mashine au roboti bila hata kufikiria mambo kwa hekima (mechanical work). {FEsw 488.5}

Vijana wanapaswa kuhamasishwa kuhudhuria shule zetu, ambazo kuwa kama shule za manabii zaidi na zaidi. Shule zetu zimeanzishwa na Bwana; na iwapo zitaendeshwa kwa kupatana na kusudi Lake, vijana waliotumwa huko shuleni, watafanya maandalizi hayo kwa haraka ili kushiriki katika matawi mbalimbali ya kazi ya umisionari. Wengine watazoezwa kuingia shambani kama wamishonari wauguzi, wengine kama wainjilisti wa vitabu, wengine kama wainjilisti, wengine kama waalimu na wengine kama wachungaji. {FEsw 489.1}

Bwana amenielekeza wazi kwamba vijana wetu wanapaswa wahimizwe kutumia muda wao mwingi na nguvu zao katika kazi ya umishonari wa matibabu/tiba kama ilivyotendwa mbele hivi karibuni. Maagizo wanayopokea kuhusu Mafundisho Makuu ya Biblia {Doctrines} huwa hayawafai kufanya kazi ambayo Mungu amewakabidhi watu, ipasavyo. {FEsw 489.2}

Shetani anajitahidi sana kuwaongoza watu mbali na kanuni sahihi. Umati wa watu wanaodai kuwa wa kanisa la Kweli la Mungu ni wanaanguka chini ya udanganyifu wa adui. Hao wanaongozwa kukengeuka kutoka kwenye utii wao kwa Yule aliyebarikiwa, Aliye wa pekee na Mfalme Mwenye Nguvu. {FEsw 489.3}

Wajibu wa Sasa

Vyuo vyote vya madhehebu yetu, na shule za mafunzo vinapaswa kuweka utaratibu wa kuwapa wanafunzi wao elimu muhimu kwa wainjilisti na kwa wafanyabiashara Wakristo. Vijana na wale walioendelea zaidi katika miaka (watu wazima), ambao wanahisi kuwa ni jukumu lao kujistahilisha kufaa kwa kazi inayohitaji kufaulu mitihani fulani, kwa ajili ya kupata hati/vyeti fulani vya kisheria {certification}, wanapaswa kujipatia kwa kadri iwezekanavyo katika shule zetu za mafunzo za Makoferensi/majimbo- yote yale ambayo ni muhimu, bila kulazimika kwenda Battle Creek kwa elimu yao ya maandalizi. {FEsw 489.4}

Maombi yatawatimizia maajabu wale wanaojitoa kwa maombi, mkikesha katika hayo. Mungu anataka sisi sote tuwe katika kusubiri, nafasi ya matumaini. Kile Yeye alichohidi atafanya, na ikiwa kuna i hitaji la kisheria linalotakiwa kukidhiwa, kwa kuchukua kozi fulani kwa ajili ya maandalizi ya masomo kwa wanafunzi wetu wanaosomea mambo ya tiba/afya, basi vyuo vyetu na vifundishe hayo masomo ya

ziada yanayohitajika kwa njia inayoendana na Elimu ya Kikristo. Bwana ameonyesha kutofurahishwa Kwake, kwa mkondo wa watu wetu wengi kuingia huko chuoni Battle Creek; na kwa vile Yeye hataki watu wengi sana waende huko, tunapaswa kuelewa kwamba Yeye anataka shule zetu katika maeneo mengine ziwe na walimu bora, na kufanya vyema kazi inayopaswa kufanywa. Wanapaswa kufanya mikakati ya kuwabeba wanafunzi katika vipengele vya mafunzo muhimu ya fasihi na sayansi. Mengi ya matakwa haya yamejitokezea kwa sababu kazi nyingi za maandalizi zinazofanywa katika shule za kawaida ni za juu juu. Hebu kazi zetu zote ziwe kamili, za uaminifu, na za kweli. {FEsw 490.1}

Katika shule zetu za mafunzo, Biblia inapaswa kufanywa kuwa msingi wa elimu yote. Na katika masomo yanayotakiwa kufunzwa, siyo lazima kwa walimu wetu kuleta vitabu visivyofaa ambavyo Bwana ametuagiza tusivitumie katika shule zetu. Kutokana na Nuru ambayo Bwana amenipa, najua kwamba mafunzo ya shule zetu katika sehemu mbalimbali za shamba la Bwana, yanapaswa kuwekwa katika nafasi nzuri zaidi kwa kadri iwezekanavyo ili kuwastahilisha vijana wetu kupasi mitihani iliyoainishwa na sheria za nchi kwa wanafunzi wa tiba. Kwa njia hii, talanta bora zaidi za walimu watakaofundisha zitapatikana hapa, ili shule zetu ziweze kuletwa katika kiwango kinachohitajika. {FEsw 490.2}

Ila vijana wa kiume na wa kike katika makanisa yetu wasishauriwe kwenda Battle Creek ili kupata elimu ya maandalizi. Kuna hali ya msongamano wa mambo huko Battle Creek ambayo hupafanya kuwa mahali pabaya kwa elimu ifaayo watenda kazi Wakristo. Kwa sababu maonyo kuhusu kazi katika kituo hicho chenye msongamano hayajazingatiwa, Bwana aliruhusu taasisi zetu mbili kuteketezwa kwa moto. Hata baada ishara Zake zilizo wazi za kutopendezwa kwa hakika, maonyo Yake hayakuzingatiwa. Sanitarium bado ipo. Kama ilikuwa imegawanywa katika vituo kadhaa, na kazi yake na ushawishi itolewe kwenye sehemu mbalimbali, ni kwa kiasi gani zaidi, Mungu angekuwa ametukuzwa! Lakini sasa kwa vile Sanitarium imejengwa upya, sisi lazima tufanye vyema kwa kadri tuwezavyo, ili kusaidia wale ambao wako huko wakihangaika na matatizo mengi. {FEsw 490.3}

Acha nirudie: Si lazima kwa vijana wetu wengi kusomea udaktari. Lakini kwa wale ambao wanapaswa kuchukua masomo ya tiba, Maconferensi/Majimbo yanapaswa kutoa utoaji/msaada wa kutosha katika miundombinu na vifaa kwa ajili ya elimu ya maandalizi. Na hivyo vijana wa kila konferensi/Jimbo wanaweza kufundishwa karibu na nyumbani kwao, na kuepushwa na majaribu maalum yanayohudhuria kazi katika Battle Creek. {FEsw 491.1} – [The Review and Herald, Oktoba 15, 1903.](#)

Sura ya 62

JE, SOTE TUTAHAMIA KARIBU NA TAASISI ZETU NA KUJAZANA HUKO {KUFANYA KOLONI}

Nuru maalum imetolewa kwangu kuhusu kuhamisha nyumba zetu za uchapishaji na Sanitarium (vituo vya tiba mbadala) na shule nje ya miji hadi mahali ambapo patakuwa pema zaidi kwa kazi hiyo. Mahali pale ambapo wale waliounganishwa na hizi kazi hawataanikwa kwenye majaribu yote yahusianayo na maisha ya mjini. Shule zetu haswa, lazima ziwe mbali na miji. Haina manufaa ya kiroho kwa wafanyakazi wa taasisi zetu kuwa mijini, mahali ambapo majaribu ya adui yamejaa kila upande. {FEsw 492.1}

Maagizo yaliyotolewa kuhusu kuhamishwa kwa kazi ya uchapishaji kutoka Battle Creek hadi sehemu fulani ya mashambani karibu na Washington, D.C., yalikuwa wazi na kueleweka vyema, nami ninatumai kwa dhati kwamba kazi hii itawezeshwa kwa haraka. {FEsw 492.2}

Maagizo yametolewa pia kuhusiana na nyumba ya uchapaji ya Pasifiki Press ihamishwe kutoka Oakland (California). Jinsi miaka ilivyo zidi kuendelea mbele, mji wa Oakland umekuwa mkubwa, na hii inatulazimisha sasa kukipeleka kiwanda hiki cha uchapishaji mahali pa mashambani zaidi, mahali ambapo ardhi inaweza kupatikana kwa ajili ya nyumba za wafanyakazi. Wale ambao wameunganishwa na ofisi zetu za uchapishaji, hawapaswi kulazimishwa kuishi katika miji iliyo na msongamano wa watu. Wanapaswa kuwa na nafasi ya kupata nyumba za kuishi, mahali ambapo wataweza kuishi bila kuhitaji mishahara mikubwa. {FEsw 492.3}

Wanafunzi wanaojifunza kazi kwenye nyumba zetu za uchapaji wanapaswa kupokea zaidi malezi ya wakina 'baba'* kuliko ambavyo wamekuwa wakipokea. Wanapaswa kupewa mafunzo ya kina mafunzo katika mistari tofauti ya stadi/taaluma ya uchapishaji (printing business); pia wanapaswa kupewa kila nafasi ya kujipatia maarifa ya Biblia; kwa maana wakati umefika ambapo waamini watatawanyika katika nchi nyingine. Wafanyakazi katika Nyumba zetu za

uchapishaji wanapaswa kufundishwa ni nini inamaanisha kwa kuwa wafuasi wa Kweli wa Bwana na Mwokozi wetu Yesu Kristo. Hapo zamani, Roho nyingi zimeachwa bila ulinzi. Hawakufundishwa ufahamu/ujuzi katika sayansi ya utauwa. Wengine waliobeba majukumu hapo, hawakuishi maisha ya Kikristo. *(wanagenzi walikuwa wanafunzi wanaojifunza stadi ya uchapaji chini ya wazee waliobobea kazi hii kwa miaka mingi, na hivyo kujipatia taaluma ya uchapaji na kuweza kufanya kazi na hatimaye kusimamia kazi wakati wazee wamestaafu, wazee hawa walikuwa kama baba wa kiroho na kazi-apprentices who needed mentors). {FEsw 492.4}

Wafanyakazi Waliowekwa wakfu Wanahitajika

Nilisikiliza Maneno yaliyosemwa na Yule anayeelewa yaliyopita, ya sasa, na yajayo. Maelezo mazito yalitolewa kubainisha kinagaubaga tabia zinazopaswa kumilikiwa na wale ambao wanakubalika kama wenzi/washirika katika taasisi zetu (wenzi ambao wanaweza kufungiwa nira Pamoja). Taasisi hizi zinahitaji watu wanaoweza kutawala nafsi (kiasi) kama neno hilo linavyokubalika kikamilifu Mungu atuepushe watu ambao hawajajifunza kujidhibiti nafsi zao wenyewe, na ambao hupuuza kujijengea tabia ili kupanga mipango kwa ajili ya mtu mwingine, ili wasiletwe katika taasisi zetu huko Washington, D.C., na Mountain View, California. {FEsw 493.1}

Wafanyakazi katika taasisi zetu wanapaswa kuzingatia maagizo yaliyotolewa kwa Kristo. Ie Kweli itakapokaa katika mioyo ya wasimamizi (watawala). wanapotembea katika Nuru inayoangaza kutoka kwa Neno la Mungu, wafanyakazi wale walio wadogo kwa umri (vijana) watataka kuelewa vyema maneno wanayosikia katika kusanyiko la watu wa Mungu. Wataomba maelezo kamili zaidi. na kutakuwa na msimu maalum wa kumtafuta Bwana na kujifunza Neno Lake. Ilikuwa katika chumba fulani tulivu au sehemu fulani ya mapumziko kwenye vijiji, Kristo alichukua muda kuelezea zaidi kwa wanafunzi mifano ambayo Yeye alikuwa ameisema kabla, mbele ya umati. Hii ndio kazi ambayo itahitaji ifanyike kwa vijana katika nyumba zetu za uchapishaji. {FEsw 493.2}

Tabia ya kufanya makoloni

Wale ambao ni lazima wawepo karibu na taasisi zetu wanapaswa kuwa makini jinsi wanavyotuma ripoti za kufurahisha/kung'aa kuhusu mahali hapo. Kila mahali kuna watu ambao hawana utulivu na wasioridhika, na ambao wanatamani kwenda mahali fulani ambapo wanadhani watafanya vizuri zaidi kuliko mazingira yao ya sasa-pale walipo. Wanafikiri kwamba kama wangeweza kupewa kazi zinazohusiana na baadhi ya taasisi zetu, wao wangekuwa na nafasi nzuri ya kupata riziki. {FEsw 493.3}

Wale wanaojaribiwa kukusanyika karibu na taasisi zetu wanapaswa kuelewa kwamba ni wafanyakazi wenye ujuzi, ndio ambao wanahitajika, na kwamba mizigo mzito unawashukia wale wote wanaohusiana na kazi hiyo jinsi ipasavyo. Wale

ambao wameunganishwa na taasisi zetu lazima wawe wazalishaji, na vile vile watumiaji (wasiwe wanyonyaji/kupe). Kwa wale wanaotaka kubadilisha eneo lao, na kufanya makazi karibu na moja ya taasisi zetu, ningesema: Je, unafikiri kwamba katika kuishi karibu na taasisi utaweza kujipatia riziki bila mahangaiko au kazi ngumu? Je, umeshauriana na Bwana kuhusu jambo hili? Je, una ushahidi kwamba matamaniao yako ya kubadili eneo la makazi, hayana doa la ubinafsi, na yatakuwa kwa ajili ya Utukufu kwa Mungu? {FEsw 494.1}

Kutoka kwa barua zilizopokelewa na wale walio na uhusiano na taasisi zetu, na kwa harakati zilizofanywa tayari, tunaona kwamba matamaniao ni kupata nyumba karibu na taasisi hizi. Akili yangu imelemewa na kitendawili/mkanganyiko juu ya hili, kwa sababu nimepokea maagizo kutoka kwa Bwana kuhusu ushawishi ambao utashinikizwa juu ya watu binafsi na juu ya kazi yetu kwa watu wetu kwa ubinafsi, katika kukusanyika karibu na taasisi zetu. {FEsw 494.2}

Kwa miaka mingi, katika maonyo ambayo yamerudiwa mara nyingi, nimeshuhudia kwa watu wetu kwamba Mungu hakupendezwa kuona familia zikiacha makanisa madogo, na kujikusanya mahali ambapo nyumba zetu za uchapishaji, vituo vya tiba rahisi-Sanitarium, na shule vimejengwa, ili tu watafute urahisi wao wenyewe, maisha ya kivivu, au faida za kidunia. {FEsw 494.3}

Wale wanaohisi kufanya makazi yao karibu na nyumba yetu ya uchapishaji au sanitarium yetu na shule ya Takoma Park, wanapaswa kupata ushauri kabla ya kuhamu. {FEsw 494.5}

Kwa wale ambao wanatazamia kwamba Mountain View ni mahali panapopendeza kuishi, kwa sababu Nyumba ya uchapishaji ya Pacific itasimikwa huko, ningesema: Angalia sehemu zingine za ulimwengu, ambazo zinahitaji Nuru ambayo umepokea kama amana. Kumbuka kwamba Mungu amempa kila mtu kazi yake. Chagua eneo ambalo utakuwa na nafasi ya kuacha Nuru yako iangaze katikati ya giza la kimaadili. {FEsw 494.6}

Wakati taasisi inapoanzishwa mahali fulani, daima kuna familia nyingi zinazotamani kukaa karibu nayo. Hivyo ndivyo imekuwa katika Battle Creek na katika Oakland, na, kwa kiasi fulani, karibu kila mahali ambapo tuna shule au Sanitarium. {FEsw 495.1}

Kuna watu ambao ni wahaka (wasiotulia), ambao kama wangeenda mahali fulani papya kuishi, bado wasingeridhika, kwa sababu Roho ya kutoridhika imo ndani mioyo yao, na badiliko la mahali halileti badiliko la mioyo yao. Tabia zao hazijasafishwa na kukuzwa na Roho wa Kristo. Wanahitaji kujifunza somo la kuridhika. Hawafanyi hivyo utafiti kutoka kwa sababu hadi athari. Hawatafuti kuelewa vipimo vya tabia vya Biblia, ambavyo ni muhimu kwa mafanikio ya Kweli. {FEsw 495.2}

Wapo wengi wanaotamani kubadili ajira zao. Wanatamani kupata faida ambazo wanadhani zipo mahali pengine. Acha wajiulize itakuwa na faida gani kwao kuhama ikiwa hawajajifunza kuwa wema na wavumilivu na wenye kusaidia wengine hapo walipo. Hebu na wajitazame wenyewe katika Nuru ya Neno la Mungu, na kisha wafanye kazi pale ambapo uboreshaji unahitajika. {FESW 495.3}

Hebu wale wanaofikiria kuhamia Mountain View wakumbuke kwamba hii si hekima isipokuwa wameitwa huko ili kuungana na kazi ya uchapishaji. Dunia ni kubwa; mahitaji yake ni makubwa. Nenda, ukaanze vituo vipya mahali ambapo Nuru inahitajika. Msisongamane katika sehemu moja mkifanya kosa lile lile ambalo limefanywa huko Battle Creek. Kuna mamia ya maeneo ambayo yanahitaji Nuru ambayo Mungu amekupa. {FEsw 495.4}

Na popote pale unapoishi, haijalishi mazingira yako, ninyi hakikisheni kuwa mnaleta mafundisho ya Neno la Mungu ndani ya nyumba zenu, katika maisha yenu ya kila siku. Mtafute Mungu kama Nuru yako, nguvu zako, na njia yako ya kwenda Mbinguni. Kumbuka kwamba Mungu amemkabidhi kila mtu talanta, ili zitumike kwa ajili Yake. Jifunze miguuni pa Yesu masomo ya upole na unyenyekevu, na kisha fanya kazi katika Roho ya Mwokozi kwa wale walio karibu nawe. Kwa utii wa hiari kwa amri, fanya nyumba yako iwe mahali ambapo Utukufu wa Mungu utapenda kukaa. "Hivi ndivyo asemavyo Yeye aliye juu, aliyetukuka, akaaye milele, ambaye Jina lake ni Mtakatifu; Mimi nakaa mahali palipoinuka, palipo patakatifu, pamoja naye yeye aliye na Roho iliyotubu na kunyenyekea, ili kuzifufua Roho za wanyenyekevu, na kuifufua mioyo yao waliotubu." {FEsw 495.5}

Kila mmoja wetu ana kazi yake binafsi ya kufanya. Tunapaswa kujiweka wakfu wenyewe, kwa Mungu, yaani mwili, nafsi na Roho, zetu. Kila mtoto Wake ana kitu cha kufanya kwa ajili ya heshima na Utukufu wa Jina Lake. Popote ulipo, unaweza kuwa mbaraka. {FEsw 496.1}

Ikiwa inaonekana kuna nafasi ndogo tu ya kupata riziki mahali ulipo, tumia kila fursa vizuri zaidi. Panga mipango ya busara. Tumia kila nukta ya uwezo ambao Mungu amekupa. Fanya wajibu wako kwako mwenyewe, ukiboresha uelewa wako na kuchukuliana ipasavyo na mazingira yako, kila siku ukiwa bora zaidi katika kutoa hesabu ya nguvu za akili na kimwili ambazo Mungu amekupa. Yeye anataka uwe na mafanikio. Anataka uwe baraka katika nyumba yako na katika jumuiya unayoishi. {FEsw 496.2} .

Wazazi, wasaidieni watoto wenu kuwasaidia na kusaidiana wao kwa wao. Uwe mwema na mwenye adabu kwa majirani zako. Kwa matendo yako mema, iache Nuru yako iangaze katikati ya giza la kiadili. Ikiwa ninyi ni Wakristo wa Kweli, mtazidi kuwa na uwezo wa kuelewa mapenzi ya Bwana ni nini, na mtasonga mbele hatua kwa hatua katika Nuru ya Neno Lake. {FEsw 496.3}

Jifunze maisha ya Kristo, na ujitahidi kufuata kielelezo ulichopewa Naye.

Jiulizeni kama mmetimiza wajibu wenu wote kwa kanisa katika nyumba yako mwenyewe, na wajibu wako kwa jirani zako. Je, umekuwa mwaminifu katika kuwafundisha watoto wako masomo ya adabu ya Kikristo? Je, hakuna fursa nyingi za kuboresha serikali ya nyumbani kwako? Usiache kuwajali watoto wako. Jifunze jinsi ya kujirudi mwenyewe, na kuwa na nidhamu, ili upate kustahili heshima ya watoto wako na majirani zako. Ikiwa Kristo hakai ndani ya mioyo yenu, mnawezaje kuwafundisha wengine masomo ya subira na wema ambayo lazima yadhihirike katika maisha ya kila Mkristo? Uwe na hakika ya kuwa unaishika njia ya Bwana, na kuwafundisha Ukweli wale wanaokuzunguka. {FEsw 496.4} — [The Review and Herald, June 2, 1904.](#)

Kwa Masomo ya Ziada

[Training Children for God, The Review and Herald, September 8, September 15, 1904](#) [How Shall Our Youth be Trained, Testimonies for the Church, 8:221- 230](#) [God in Nature, Idem, 8:239-243](#) [A Personal God, Idem, 8:263-278](#) [A False and True Knowledge of God, Idem, 8: 279-289](#) [Danger in Speculative Knowledge, Idem, 8:290-308](#) [The False and True in Education, Idem, 8:305-311](#) [Importance of Seeking True Knowledge, Idem, 8:312-318](#) [Knowledge Received Through God's Word, Idem, 8:319-328](#) [Lessons from the Life of Daniel, The Youth's Instructor, April 4, 1905](#) [416 Fundamentals of Christian Education Instruction for Helpers and Students at Tahoma, The Review and Herald, April 27, 1905.](#)

Sura ya 63

MASOMO KUTOKA KATIKA MAISHA YA SULEMANI

“Jitengeni”

Akiwa amewekwa kama kichwa cha taifa ambalo lilikuwa limewekwa kama Nuru kwa mataifa yaliyowazunguka, huenda Sulemani angeliweza kuleta Utukufu mkubwa Bwana wa Malimwengu yote kwa maisha ya utii. Anaweza kuwa aliwatia moyo watu wa Mungu kuepuka maovu ambayo yalikuwa yakitendwa na mataifa ya jirani. Huenda alitumia hekima yake aliyopewa na Mungu na nguvu ya ushawishi katika kuandaa utaratibu na kuongoza harakati kubwa za umisionari kwa ajili ya kuangaza wale ambao walikuwa hawamjui Mungu na ile Kweli Yake. Hivyo watu wengi wanaweza kuwa waliletwa kwenye uaminifu kwa Mungu, na kumtii Mfalme wa wafalme. {FEsw 498.1}

Shetani alijua vizuri matokeo ambayo yangeletwa kwa utii, wakati wa miaka ya awali ya utawala wa Sulemani, —miaka yenye Utukufu kwa sababu ya hekima, wema, na unyofu wa Mfalme; na hivyo alijaribu kuleta ushawishi ambao ungedhoofisha kwa siri uadilifu wa Sulemani kwa kanuni za Mungu, na hivyo kumfanya ajitenge na Mungu. Na huyu adui alifanikiwa katika juhudi hii, tunajua kutoka kumbukumbu ya maandishi haya kuwa: “Huyo Sulemani akafanya ujamaa na Farao, Mfalme wa Misri, akamwoa binti yake Farao, akamleta mjini mwa Daudi” {FEsw 498.2}

Katika kuunda muungano na taifa la makafiri, na kutia muhuri kwa kuunganishwa katika ndoa na binti wa kifalme aliyeabudu sanamu, Sulemani bila kufikiri kwa makini, akapuuza maandalizi ya hekima ambayo Mungu alikuwa

amefanya ili kudumisha usafi wa watu Wake. Matumaini ambayo mke huyu wa nchi ya Misri anaweza kuongoka, yalikuwa ni kisingizio dhaifu cha dhambi. Katika ukiukaji wa amri ya moja kwa moja ya kujitenga na mataifa mengine, Mfalme aliunganisha nguvu zake kwa mkono wa binadamu badala ya mkono wa Mungu (mkono wa mwanadamu au wa nyama). {FEsw 498.3}

Kwa muda fulani, Mungu katika rehema zake za huruma alitumia majaliwa yake kushughulikia kosa hili baya. Mke wa Sulemani akaongoka; na Mfalme, kwa njia ya busara, angeweza kufanya mengi ili kuzuia nguvu za uovu ambazo uzembe kwa wake alikuwa amezianzishia mchakato. Lakini Sulemani alianza kusahau Chanzo cha nguvu na Utukufu wake. Mwelekeo wa uovu ukainuka na kuwa juu ya hekima. Kujiamini kwake kulipoongezeka, alitafuta kutimiza kusudi la Bwana kwa njia yake mwenyewe aliyotaka. Alitoa sababu kwamba mapatano ya kisiasa na ya kibiashara pamoja na mataifa yaliyowazunguka yangesaidia kuleta ujuzi wa Mungu wa Kweli; na hivyo akaingia katika miungano isiyo mitakatifu kati yake na taifa baada ya taifa. Mara nyingi miungano hii ilitiwa muhuri kwa ndoa na binti wa kifalme aliye pagani. Amri za Yehova ziliwekwa kando kwa ajili ya desturi za mataifa yaliyowazunguka. {FEsw 498.4}

Wakati wa miaka ya ukengeufu wa Sulemani, kuzorota kwa kiroho kwa Israeli kulikuwa kwa haraka. Ingekuwaje vinginevyo, wakati Mfalme wao aliunganishwa na mawakala wa kishetani? Kupitia vyombo hivi adui alifanya kazi ya kuchanganya akili za watu kuhusiana na ibada ya kweli na ibada ya uwongo. Nao wakawa mawindo rahisi. Ikaja kuwa mazoea kwao kuoana na makafiri. Waisraeli wkapoteza kwa hakara chuki yao kwa ibada ya sanamu. Desturi za mataifa/kipagani zilianzishwa. Akina mama waabudu sanamu walilea watoto wao kwa maadili ya kuabudu/ kuadhimisha ibada za wapagani. Imani ya Kiebrania ikawa mchanganyiko wa mawazo yenye mkanganyiko kwa haraka. Biashara na mataifa mengine iliwaingiza Waisraeli kwenye mawasiliano ya karibu na wale ambao hawakuwa na upendo kwa Mungu, na wao wenyewe upendo wao Kwake ukapungua sana. Hisia zao kali kuhusu tabia iliyoinuka na takatifu ya Mungu zilikufa. Kukataa kwao kufuata njia ya utii, ikahamisha utii wao kwa Shetani. Adui alifurahia kufaulu kwake katika kuondoa sura ya Mungu kutoka kwenye akili ya watu ambao Mungu alikuwa amewachagua ili kuwa wawakilishi Wake. Kupitia kuoana na waabudu sanamu na kushirikiana nao daima. Shetani alileta kile ambacho alikuwa akikifanyia kazi kwa muda mrefu, —yaani, uasi wa kitaifa. {FEsw 499.1}

Ushirikiano usio wa Kimaandiko

Bwana anatamani watumishi Wake wahifadhi utakatifu wao wenye tabia ya kipekee. “Msifungiwe nira pamoja na wasioamini kwa jinsi isivyo sawasawa,” ni Amri Yake; “Maana pana urafiki gani kati ya haki na udhalimu? Tena pana shirika gani kati ya Nuru na giza? Tena pana ulinganifu gani kati ya Kristo na Beliari? au

yeye aaminiye ana sehemu gani? na kafiri? Tena pana mapatano gani kati ya hekalu la Mungu sanamu? kwa maana ninyi ni hekalu la Mungu aliye hai; kama Mungu alivyosema, Mimi nitatkaa ndani yao, na kutembea ndani yao; Nami nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu Wangu. Kwa hiyo tokeni kati yao, jitengeni, asema Bwana, wala msiguse kitu kilicho kichafu; Nami nitawapokea, na nitakuwa Baba kwenu, nanyi mtakuwa Wanangu na binti Zangu, asema BWANA Mwenye Nguvu Zote.” {FEsw 499.2}

Kamwe hapakuwa na wakati katika historia ya dunia ambapo onyo hili lilikuwa linafaa zaidi kuliko wakati wa sasa. Wengi wanaojiita Wakristo hufikiria, kama Sulemani, kwamba wapate kuungana na wasiomcha Mungu, kwa sababu ushawishi wao juu ya wale walio katika maovu utakuwa na manufaa; lakini mara nyingi wao wenyewe, hunaswa na kushindwa, huisalimisha imani yao takatifu, hutoa dhabihu kanuni, na kujitenga na Mungu. Hatua moja ya uwongo inaongoza kwa nyingine, hadi mwishowe wanajiweka wenyewe mahali ambapo hawawezi kutumaini kuvunja minyororo inayowafunga. {FEsw 500.1}

Uangalifu mkubwa unapaswa kuchukuliwa na vijana wa Kikristo katika kujenga urafiki na katika uchaguzi wa masahaba. Jihadharini, isije ikawa kile ninyi mnachofikiria kuwa ni dhahabu safi badala yake kikawa chuma kisicho na thamani. Kushirikiana na ulimwengu huleta vikwazo katika njia ya huduma yako Mungu, na Roho nyingi zimeharibiwa na miungano isiyo na furaha, ama biashara au ya ndoa, na wale ambao hawawezi kuwainua au kuwafanya kuwa bora kamwe. Kamwe watu wa Mungu wasidiriki kujitumbukiza kwenye uwanja ambao wamekatazwa. Ndoa baina ya waumini na makafiri imepigwa marufuku na Mwenyezi Mungu. Ila mara nyingi moyo ambao haujaongoka hufuata matamania yake yenyewe, na kisha ndoa zisizoidhinishwa na Mungu huundwa. Kwa sababu hii wanaume na wanawake wengi duniani, hawana tumaini na hawana Mungui. Matamania yao bora yamekufa; kwa mnyororo wa hali ilivyo, wao wanashikiliwa kwenye Wavu wa Shetani. Wale wanaotawaliwa na shauku na msukumo watakuwa na mavuno machungu katika maisha haya, na mwenendo wao unaweza kusababisha kupoteza Roho zao. {FEsw 500.2}

Kazi ya Taasisi

Wale waliowekwa kusimamia taasisi za Bwana ni wanahitaji nguvu nyingi, neema na uwezo wa utunzaji wa Mungu, ili wasiende kinyume cha kanuni takatifu za ile Kweli. Wengi, wengi ni hawana ufahamu kuhusiana na wajibu wa kuhifadhi ile Kweli katika usafi wake, bila ya kuchafuliwa na doa la makosa. Hatari yao ni katika kuthamini Ukweli kwa njia ya wepesi, na hivyo kuacha akilini hisia kwamba, kile tunachoamini kina matokeo madogo, ikiwa, kwa kutekeleza mipango ya wanadamu, sisi tunaweza kujiinua mbele ya ulimwengu kama vile tunashikilia nafasi ya juu zaidi, kana kwamba tunakalia kiti cha juu zaidi. {FEsw 501.1}

Mungu anawaita watu ambao mioyo yao ni ya kweli kama chuma, na ambao watasimama imara katika uadilifu, bila kutishwa na hali ya hewa. Yeye anatoa wito kwa watu ambao wataendelea kujitenga na maadui wa ile Kweli. Anawaita watu ambao hawatathubutu kukimbilia mkono wa mwandamu/nyama kwa kuingia ubia na walimwengu ili kupata fedha au njia za kuendeleza kazi Yake—hata kwa ajili ya ujenzi wa taasisi. Sulemani, kwa mapatano yake na makafiri, alijipatia dhahabu na fedha tele, lakini ufanisi wake ulithibitisha uharibifu wake. Watu wa siku hizi hawana hekima kuliko yeye, na wana mwelekeo wa kukubali mvuto uliosababisha anguko lake. Kwa maelfu ya miaka, Shetani amekuwa akijipatia uzoefu katika kujifunza jinsi ya kudanganya wanadamu; na kwa wale ambao wanaishi katika enzi hii, yeye anakuja na nguvu kubwa {balaa haswa}. Usalama wetu pekee unapatikana katika kutii Neno la Mungu, ambalo tumepewa kama mwongozo na mshauri wa uhakika. Watu wa Mungu leo wanapaswa kujiweka tofauti na kujitenga na ulimwengu, Roho yake, na athari zake. {FEsw 500.2}

"Tokeni kati yao, na jitengeni." Je, tusikie sauti ya Mungu na kuitii, au tuje nusu-nusu katika kazi ya Mungu, na kujaribu kumtumikia Mungu na Mali? Kuna kazi ya dhati na bidii mbele ya kila mmoja wetu. Mawazo sahihi, makusudi safi na matakatifu, hayaji kwetu kwa asili au kirahisi. Itabidi tujitahidi kwa ajili ya hayo mawazo yanayotakikana kwetu. Kwenye taasisi zetu, nyumba zetu za uchapishaji, vyuo na vituo vya Sanitarium, kanuni safi na takatifu lazima ziweke mizizi. Kama taasisi zitakuwa vile Mungu alipanga ziwe, wale waliunganishwa nazo hawataweza kufuata miundo ya kidunia. Watasimama kama watu wa kipekee, wanaotawaliwa na kuongozwa na viwango vya Biblia. Hawataingia kupatana na kanuni za ulimwengu ili kupata upendeleo wa fedha n.k. Hakuna nia itakayokuwa na nguvu za kutosha kuwasogeza kando, kutoka kwenye njia iliyonyooka, inayopita kwenye mstari wa wajibu. Wale walio chini ya udhibiti wa Roho wa Mungu hawatatafuta anasa zao wenyewe au pumbao/matumbuizo. Ikiwa Kristo anaongoza mioyo ya washiriki wa kanisa Lake, wataitikia wito, "Tokeni kati yao, na jitengeni." "Msishiriki dhambi zake." {FEsw 501.3}

Mungu angetaka tujifunze somo zito ambalo tunalifanyia kazi nje ya hatima yetu wenyewe. Tabia tunazounda katika maisha haya huamua kwamba sisi tumefaa au la!, kuishi katika enzi za milele. Hakuna mtu anaweza kujaribu kwa usalama kumtumikia Mungu na Mali. Mungu anao uwezo kamili wa kutuweka sisi ulimwenguni bila kuwa wa ulimwengu. Upendo Wake una uhakika na haubadiliki, badiliki. Yeye huwaangalia watoto Wake kwa umakini/uangalifu usio na kipimo na wa milele. Lakini anatuhitaji tumpe Yeye utii wetu usiogawanyika. "Hakuna mtu awezaye kutumikia mabwana wawili: kwa maana atamchukia huyu, na kumpenda huyu; ama atashikamana na huyu, na kumdharau huyu. Hamwezi kumtumikia Mungu na mali." {FEsw 502.1}

Sulemani alijaliwa hekima ya ajabu; bali dunia ikamvuta mbali na Mungu.

Tunahitaji kulinda Roho zetu, kwa bidii yote, ili masumbufu na vivutio vya dunia visichukue wakati ambao unapaswa kutolewa kwa mambo ya milele. Mungu alimwonya Sulemani juu ya hatari yake, Naye leo pia anatuonya tusizihatarishe nafsi zetu kwa kushirikiana na na ulimwengu. “Tokeni kati yao,” anasihi, “Jitengeni, ... wala msiguse kitu kilicho najisi; Nami nitawapokea, Nami nitakuwa Baba kwenu, nanyi mtakuwa Wanangu na binti, asema Bwana, Mungu Mwenyezi.” {FEsw 502.2}

— The Review and Herald, February 1, 1906.

Kwa Marejeleo ya Ziada

Lessons in Economy and Self-denial, The Youth’s Instructor, September 10, 1907.

Sura ya 64

WALIMU KAMA MIFANO YA WAKRISTO WAADILIFU

Nina ujumbe kwa wale wanaosimama kama wakuu wa taasisi zetu za elimu. Nimeagizwa kuita usikivu wa kila mmoja anayeshika nafasi ya wajibu, kwa sheria ya Bwana kama msingi wa mwenendo wote sahihi. Ninapaswa kuanza kwa kuita umakini wenu kwa sheria iliyotolewa katika Edeni, na kwa tuzo la utii na adhabu ya kutotii. {FEsw 504.1}

Kwa matokeo ya kosa la Adamu, dhambi iliingizwa ndani ya ulimwengu mzuri ambao Mungu aliuumba, na wanaume na wanawake wakawa na ujasiri zaidi na zaidi katika kuitotii sheria Yake. Bwana alitazama chini juu ya ulimwengu usio na toba, na akaamua kwamba lazima awape waasi onyesho la uweza Wake. Alimjulisha Nuhu Kusudi Lake, na akamwagiza kuwaonya watu wakati wa kujenga safina ambamo watiifu wangeweza kupata hifadhi mpaka ghadhabu ya Mungu ipitei. Kwa miaka mia moja na ishirini Nuhu alitangaza ujumbe wa onyo kwa ulimwengu wa kabla ya gharika (antediluvian); lakini wachache tu walitubu. Baadhi ya maseremala aliowaajiri katika kujenga safina, waliamini ujumbe, lakini walikufa kabla ya gharika; baadhi ya wongofu wa Nuhu walirudi nyuma. Wenye haki duniani

walikuwa wachache tu, kisha wanane tu ndio waliishi na kuingia ndani ya safina. Hawa walikuwa Nuhu na familia yake. {FEsw 504.2}

Jamii ya waasi ilichukuliwa na mafuriko/gharika. Kifo kilikuwa sehemu yao. Kwa utimilifu wa onyo la kinabii kwamba wote ambao hatazishika amri za Mbinguni wanywe maji ya gharika, Ukweli wa Neno la Mungu ulidhihirishwa. {FEsw 504.3}

Baada ya gharika watu wakaongezeka tena juu ya nchi, na uovu pia uliongezeka. Ibada ya sanamu ikawa karibia ulimwenguni pote, na hatimaye Bwana aliwaacha wacosaji wagumu kufuata njia zao za uovu, wakati Yeye alimchagua Ibrahimu, wa ukoo wa Shemu, na kumfanya kuwa mtunza sheria Yake kwa vizazi vijavyo. Kwake huyo ujumbe akaja, "Ondoka katika nchi yako, na jamaa zako, na kutoka kwa nyumba ya baba yako, hata nchi nitakayokuonyesha." Na kwa Imani Abrahamu alitii. "Akatoka, asijue alikokwenda." {FEsw 504.4}

Uzao wa Abrahamu ukaongezeka, na hatimaye Yakobo na wanawe na jamaa zao walishuka mpaka Misri. Hapo, wao na vizazi vyao wakakaa ugenini kwa miaka mingi, mpaka hatimaye Bwana akawaita watoke, na kuwaongoza waende mpaka nchi ya Kanaani. Lilikuwa kusudi Lake kufanya taifa hili la watumwa, watu ambao wangedhihirisha tabia Yake kwa watu mataifa, waabudu sanamu duniani. Lau wangelikuwa watiifu kwa Neno Lake. Haingechukua muda kwao kuingia katika nchi ya ahadi. Lakini walikuwa waasi na wakaidi, na wakasafiri miaka arobaini Nyikani. Wawili tu kati ya watu wazima waliotoka Misri waliingia Kanaani. {FEsw 505.1}

Ilikuwa ni wakati wa kutangatanga jangwani kwa Waisraeli, ndipo Mungu aliwapa sheria Yake. Aliwaongoza mpaka Sinai, na huko, katikati ya matukio ya Ukuu wa kutisha, alitangaza amri kumi. {FEsw 505.1}

Tunaweza kujifunza kwa faida, kumbukumbu/rekodi ya maandalizi yaliyofanywa na kusanyiko la Israeli kwa ajili ya kusikilizwa kwa sheria. "Mwezi wa tatu baada ya kutoka Waisraeli katika nchi ya Misri, siku iyo hiyo wakafika jangwa la Sinai. Nao walipokuwa wameondoka Refidimu na kufika jangwa la Sinai, wakatua katika lile jangwa; Israeli wakapiga kambi huko wakiukabili mlima. Musa akapanda kwa Mungu, na Bwana akamwita toka mlima ule, akisema, Utawaambia nyumba ya Yakobo, na kuwaarifu wana wa Israeli, Maneno haya; Mmeona jinsi nilivyowatendea Wamisri, na jinsi nilivyowachukua ninyi juu ya mbawa za tai, nikawaleta ninyi Kwangu Mimi. Sasa basi ikiwa mtaitii sauti Yangu kweli kweli, na kulishika agano lLngu, hapo ndipo mtakapokuwa tunu Kwangu kuliko makabila yote ya watu; maana dunia yote pia ni mali Yangu." {FEsw 505.3}

Basi, ni nani anayepaswa kuonwa kuwa Mtawala wa mataifa? — Bwana Mungu mweza wa yote, Mwenye nguvu. Wafalme wote, watawala wote, mataifa yote, ni Wake, chini ya utawala na serikali Yake. {FEsw 505.4}

“Musa akaja na kuwaita wazee wa watu, na wakaweka mbele ya nyuso zao maneno hayo yote Bwana aliyoyaamuru Yeye.” (Musa akaenda akawaita wazee wa watu, akawafunulia maneno hayo yote, Bwana aliyokuwa amemwagiza) {FEsw 506.1}

BWANA akamwambia Musa, Pita mbele ya watu, ukawachukue baadhi ya wazee wa Israeli pamoja nawe; na ile fimbo yako ambayo uliupiga mto kwayo, uitwae mkononi mwako, ukaende. Tazama, nitasimama mbele yako huko, juu ya lile jabali katika Horebu; nawe utalipiga jabali, na maji yatatoka, watu wapate kunywa. Musa akafanya hivyo mbele ya wazee wa Israeli.

likiwa na idadi kubwa zaidi ya watu milioni moja? Je, kutaniko liliitikiaje? {FEsw 506.2}

“Watu wote wakitika pamoja wakisema, Hayo yote aliyoyasema Bwana tutayatenda. Naye Musa akamwambia Bwana maneno ya hao watu.” {FEsw 506.3}

Hivyo wana wa Israeli walifanywa kuwa watu maalum. Kwa agano zito kabisa walihidi kuwa waaminifu kwa Mungu. {FEsw 506.4}

Kisha watu wakaambiwa wajitayarisha kuisikiliza sheria. Asubuhi ya siku ya tatu sauti ya Mungu ilisikika. Akiongea kutoka katika giza nene lililomfunika, alipokuwa amesimama juu ya mlima, nakuzungukwa na kundi la malaika, Bwana alifanya sheria Yake Ijulikane. {FEsw 506.5}

Mungu alisindikiza tangazo la sheria Yake na udhihirisho wa nguvu na Utukufu Wake, ili watu Wake waweze kuvutiwa kwa heshima kubwa kwa Mtunzi wa sheria, Muumba wa mbingu na nchi. Angewaonyesha pia watu wote utakatifu, utakatifu umuhimu, na kudumu kwa sheria Yake. {FEsw 506.5}

Watu wa Israeli waliingiwa na woga. Wakajikunja na kwenda mbali na mlima, kwa hofu na woga. Umati ukamlilia Musa, “Sema nasi wewe, lakini Mungu asiseme nasi, tusije kufa.” {FEsw 506.7}

Akili za watu, zikiwa zimepofushwa na kudhalilishwa na utumwa, zilikuwa haziko tayari kufahamu kikamilifu kanuni za Mungu zenye hatima nzito, Kanuni kumi. Ili majukumu ya dekalojia yaweze kueleweka kikamilifu zaidi na kutekelezwa, maagizo ya ziada yalitolewa, yakionyesha mfano na kutumia maagizo ya zile amri kumi. Tofauti dekalojia, maagizo hayo yalitolewa faraghani kwa Musa, ambaye alipaswa kuyawasilisha kwa watu. {FEsw 506.8}

Aliposhuka kutoka mlimani, Musa “Musa akaenda akawaambia watu maneno yote ya Bwana, na hukumu Zake zote; watu wote wakajibu kwa sauti moja, wakasema, Maneno yote aliyoyanena Bwana tutayatenda. Basi Musa akayaandika Maneno yote ya Bwana, akaondoka asubuhi na mapema, akajenga madhabahu chini ya mlima, na nguzo kumi na mbili, kwa hesabu ya kabila kumi na mbili za

Israeli, akapeleka vijana wa wana wa Israeli, waliotoa sadaka za kuteketezwa, wakamchinja Bwana sadaka za amani za ng'ombe. Musa akatwaa nusu ya ile damu, akaitia katika mabakuli; na nusu ya ile damu akainyunyiza juu ya madhabahu. Kisha akakitwaa kitabu cha agano akakisoma masikioni mwa watu; wakasema, Hayo yote aliyoyanena Bwana tutayatenda, nasi tutatii. Musa akaitwaa ile damu, akawanyunyizia watu, akasema, Hii ndiyo damu ya agano alilolifanya Bwana pamoja nanyi katika Maneno haya yote.” {FEsw 506.9}

Hivyo wana wa Israeli kwa ibada hiyo iliyo makini walitengwa kama watu wa kipekee. Kunyunyizia damu iliwakilisha kumwagika kwa damu ya Yesu, ambayo mwanadamu anatakaswa kutoka dhambini. {FEsw 507.1}

Kwa mara nyingine tena Bwana ana Maneno maalum ya kuzungumza na watu Wake. Katika sura ya thelathini na moja ya Kutoka tunasoma: {FEsw 507.2}

“Bwana akasema na Musa, na kumwambia, Kisha, nena wewe na wana wa Israeli, na kuwaambia, Hakika mtazishika Sabato Zangu, kwa kuwa ni ishara kati ya mimi na ninyi katika vizazi vyenu vyote; ili mpate kujua ya kuwa Mimi Ndimi Bwana niwatakasaye ninyi..... Kwa hiyo wana wa Israeli wataishika Sabato, kuitunza Sabato katika vizazi vyao, kwa agano la milele. Ni ishara kati Yangu na wana wa Israeli milele; kwa maana katika siku sita Bwana alizifanya mbingu na nchi, akastarehe siku ya saba, akastarehe iliburudishwa. Na akampa Musa alipokwisha maliza kuzungumza naye juu ya Mlima Sinai, mbao mbili za ushuhuda; mbao za mawe, zilizoandikwa kwa kidole cha Mungu.” {FEsw 507.3}

Maandiko mengine mengi juu ya utakatifu wa sheria ya Mungu yamekuwa yakiwasilishwa mbele yangu. Onyesho baada ya onyesho, kufikia chini hadi wakati wa sasa, ulipita mbele yangu. Neno lililonenwa na Mungu kwa Israeli lilikuwa limethibitishwa. Watu hawakutii, na ni wawili tu kati ya watu wazima walioondoka Misri waliingia Kanaani. Wengine walikufa nyikani. Je, Bwana hatathibithisha Neno Lake leo, ikiwa viongozi wa watu Wake wataondoka kutoka kwa amri Zake? {FEsw 508.1}

Nilirejelewa kwenye sura ya nne ya Kumbukumbu la Torati. Sura yote ya sura hii ni ya kujifunza. Angalia hasa kauli: “Kwa hiyo ujue, leo hivi, ukaweke moyoni mwako, ya kuwa Bwana Ndiye Mungu katika mbingu juu, na katika nchi chini; hapana mwingine. Basi, zishike sheria Zake, na amri Zake, ninazokuamuru leo, upate kufanikiwa, wewe na watoto wako baada yako, na siku zako ziwe nyingi katika nchi ile akupayo Bwana, Mungu wako, milele.” {FEsw 508.2}

Sura ya nane na ya kumi na moja ya Kumbukumbu la Torati pia ina maana sana kwetu. Masomo yaliyomo ndani yake ni ya umuhimu mkubwa, na yametolewa kwetu kama vile kwa Waisraeli. Ndani ya sura ya kumi na moja Mungu anasema: {FEsw 508.3}

“Angalieni, naweka mbele yenu leo baraka na laana; baraka ikiwa mtatii amri za Bwana Mungu wenu, ambazo Mimi ninawaamuru leo; na laana ikiwa hamtaki kuzitii amri za Bwana, Mungu wenu, na kukengeuka katika njia ninayowaamuru leo, kuifuata miungu mingine mliyo nayo msiyoijua.” {FEsw 508.4}

Nimeagizwa, kama mjumbe wa Mungu, kukaa hasa juu ya kumbukumbu ya dhambi ya Musa na matokeo yake ya kusikitisha, kama somo zito kwa wale walio katika nafasi za uwajibikaji katika shule zetu, na hasa kwa wale watenda kama maraisi au makaimu wa taasisi hizi (mkuu wa chuo na makamu wake). {FEsw 508.5}

Neno la Mungu linatangaza hivi kumhusu Musa: “Basi mtu huyo Musa alikuwa mpole sana kuliko wanadamu wote waliokuwa juu ya uso wa nchi.” Alikuwa amevumilia kwa muda mrefu uasi na ukaidi wa Israeli. Lakini hatimaye subira yake ikatekewa. Walikuwa kwenye mipaka ya Nchi ya ahadi. Lakini kabla hawajaingia Kanaani, lazima waonyeshe kuwa waliamini ahadi ya Mungu. Ugavi wa maji ulikoma. Hapa ilikuwa nafasi ya wao kutembea kwa imani badala ya kuona kwa macho yao. Lakini walisahau mkono ambao kwa miaka mingi ulikuwa umewapa mahitaji yao, na badala ya kumgeukia Mungu ili awasaidie, walimnung'unikia. Vilio vyao vilielekezwa dhidi ya Musa na Haruni: “Mbona mmewaleta kusanyiko la Bwana hata jangwa hili ili tuFEsw huku, sisi na wanyama wetu? Na mbona mmetupandisha kutoka Misri ili kutuleta hata mahali hapa pabaya? Si mahali pa mbegu, wala tini, wala mizabibu, wala makomamanga; wala hapana maji ya kunywa.” {FEsw 509.1}

Wale ndugu wawili wakatangulia mbele ya umati. Lakini badala ya kuzungumza na mwamba, kama Mungu alivyomwagiza, Musa akaupiga ule mwamba kwa hasira, akipaza sauti, “Sikieni sasa, enyi waasi; je! Tuwatokezee maji katika mwamba huu?” {FEsw 509.1}

Hukumu ya uchungu na kufedhehesha sana ilitammkwa mara moja. “Bwana akamwambia Musa na Haruni, Kwa kuwa hamkuniamini Mimi, ili kunistahi mbele ya macho ya wana wa Israeli, basi kwa sababu hiyo, hamtawaingiza kusanyiko hili katika ile nchi niliyowapa.” Pamoja na Israeli walioasi Musa na Haruni, lazima wafe kabla ya kuvuka Yordani. {FEsw 509.2}

Kutokana na uzoefu wa Musa Bwana angetaka watu Wake wajifunze kwamba pale wanapofanya nafsi ijitukuze, Yake kazi inapuuzwa, na Yeye anavunjiwa heshima. Bwana atafanya kazi kinyume kwa wale wanaofanya kazi kinyume Naye. Jina Lake, na Lake pekee, linapaswa kutukuzwa duniani. {FEsw 509.3}

Kwa zaidi ya miaka ishirini kuna mambo ya ajabu yamekuwa yakija katika nyakati tofauti, miongoni mwetu. Wale ambao wamekosa uaminifu, ambao hawajainua kanuni za haki, wanahitaji sasa kumtafuta Bwana kwa kujidhili Roho zao kwa kina, na kuongoka, Ili Mungu aweze kuponya makosa yao. {FEsw 509.4}

Anayesimama katika kichwa cha shule anapaswa kuweka maslahi yasiyogawanyika katika kazi ya kuifanya shule kuwa kama vile Bwana alivyopanga iwe. Ikiwa ana matamania ya ukuu wa kupanda juu na bado juu zaidi, ikiwa atakuwa kando ya wema halisi wa kazi yake, na kando ya usahili wake, na kupuuza kanuni takatifu za Mbinguni, hebu na ajifunze kutoka kwa uzoefu wa Musa, kwamba Bwana hakika atadhihirisha kutofurahishwa Kwake kwa sababu ya kushindwa kwake kufikia kiwango kilichowekwa mbele yake hapo awali. {FEsw 510.1}

Mkuu wa shule haswa, anapaswa kuangalia kwa makini fedha za taasisi. Anapaswa kuelewa kanuni za uwekaji mahesabu {bookkeeping}. Awe mwaminifu kuripoti matumizi yote ya pesa zinazopita mkononi mwake kwa ajili ya matumizi ya shule. fedha za shule hazipaswi kuwa na **ovadrafti**, lakini kila juhudi zinapaswa kufanywa ili kuongeza manufaa ya shule. Wale walioaminiwa kwenye usimamizi wa fedha wa taasisi zetu za elimu, katu wasiruhusu uzembe katika matumizi ya fedha. Kila kitu kilichounganishwa na fedha za shule zetu kinapaswa kuwa sawa kabisa. Njia ya Bwana lazima ifuatwe kikamilifu {kwa ukali}, ijapokuwa hii inaweza kuwa haina maelewano na njia za mwanadamu. {FEsw 510.2}

Kwa wale wanaosimamia shule zetu ningesema, Je! Unaifanya sheria Yake Mungu kuwa furaha yako? Je, kanuni unazozifuata, zina busara, ni safi na zisizoghoshiwa? Je, mnajilinda, katika maisha ya vitendo, chini ya udhibiti wa Mungu? Je, unaona ulazima wa kumtii Yeye katika kila jambo? Ikiwa unajaribiwa kutumia pesa zinazolingia shuleni, kwa njia zisizoleta faida maalum kwa shule, kiwango chako cha kanuni kinahitaji kukosolewa kwa uangalifu, ili usije wakati ambapo utakosolewa na kuonekana umepunguka. Mtunza hesabu wako ni nani? Nani mweka hazina wako? (business manager) meneja wa biashara yako ni nani? Je! Ana umakini na ana uwezo wa hiyo kazi? Angalia hili. Inawezekana kwa pesa kufanyiwa ubaradhifu bila ya mtu yeyote kuelewa wazi jinsi gani hali hii ilikuja; na inawezekana kwa shule kuwa na hasara kila mara kwa sababu ya matumizi yasiyo ya busara. Wale wanaosimamia wanaweza kuhisi hasara hii kwa umakini/uchungu, wanaweza kusema kuwa wamefanya kazi kwa ubora kwa kadri walivyoweza. Lakini kwa nini basi wanaruhusu madeni kujilimbikiza? Hebu wanaosimamia shule wajue kila mwezi hali halisi ya kifedha ya shule. {FEsw 510.3}

Ndugu zangu katika wajibu, tukuzeni sheria ya ufalme wa Kristo kwa kuipa utii wa hiari. Ikiwa ninyi wenyewe hampo chini ya udhibiti wa Mtawala wa malimwengu/ulimwengu, mnawezaje kuitii sheria Yake, kama inavyohitajika katika Neno Lake? Wale waliowekwa katika nyadhifa za mamlaka ndio hasa wanaohitaji kwa ukamilifu zaidi kutambua umuhimu wa kujisalimisha kwao kwa Sheria ya Mungu na umuhimu wa kutii matakwa Yake yote. {FEsw 511.1}

Katika baadhi ya matukio fulani (au visa Fulani), wengi wenye kuunganika na shule zetu wanapaswa kusimama kwenye jukwaa la juu. Tunajua kwamba ni kusudi la wengine kutii kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu. Wanaume na

wanawake kama hao watapewa uwezo wa akili kutambua tofauti kati ya haki na udhalimu. Wana imani itendayo kazi kwa upendo na husafisha Roho, na humdhihirishia Mungu kwa ulimwengu. {FEsw 511.2}

Sote tunahitaji kupata uzoefu wa ndani zaidi katika mambo ya Mungu kuliko tulivyopata. Nafsi inapaswa kufa, na Kristo anapaswa kuchukua milki ya hekalu la Roho. Madaktari, wachungaji, walimu, na wengine wote katika nyadhifa za kuwajibika, lazima wajifunze unyenyekevu wa Kristo kabla Yeye hajafunuliwa ndani yao. Mara nyingi sana ubinafsi huwa muhimu kwa **wakala wa** maisha ya mtu ambayeBwana hawezi kumfinyanga na kumtengeneza. Ubinafsi unatawala kulia na kushoto, na mtu husonga mbele apendavyo. Kristo anauambia ubinafsi, “kaa kando ya njia Yangu. Yeye anayetaka kunifuata Mimi na ajikane nafsi yake mwenyewe. na kuuchukua msalaba wake, na kunifuata. Kisha ninaweza kumkubali yeye kama mwanafunzi Wangu. Ili kunitumikia Mimi inavyokubalika, lazima afanye kazi niliyompa kwa kupatana na maagizo Yangu.”{FEsw 511.3} – *The Review na Herald, Agosti 16, 23, 1906.*

Sura ya 65

UMUHIMU KATIKA ELIMU

Elimu muhimu zaidi kwa vijana wetu leokupata, ni ile ambayo itawafaa kwa madarasa ya shule iliyopo juu, ni elimu ambayo itawafundisha jinsi ya kufunua mapenzi ya Mungu duniabu. Kupuuza awamu hii ya mafunzo yao, na kuleta ndani shule zetu mbinu ya kidunia, ni kuleta hasara kwa walimu na wanafunzi. {FEsw 512.1}

Kabla tu Eliya kuchukuliwa kwenda Mbinguni, alitembelea shule za manabii, na

kuwaelekeza wanafunzi juu ya pointi, vipengele vilivyo muhimu zaidi katika elimu yao. Masomo aliyokuwa amewapa kwenye ziara za hapo awali, sasa aliyarudia, akikazia kwenye hisia za mawazo ya vijana umuhimu wa kuruhusu usahili kutia alama katika kila kipengele cha elimu yao. Ni kwa njia hii tu ndio wangeweza kupokea umbo la Mbinguni, na kwenda kufanya kazi katika njia za Bwana. Zikiendeshwa kama Mungu alivyopanga zinapaswa, shule hizi zetu katika siku hizi za kufunga ujumbe wa injili, zitafanya kazi sawa na ile iliyofanywa na shule za manabii. {FEsw 512.2}

Wale wanaotoka katika shule zetu ili kujihusisha na kazi ya utume watatahitaji uzoefu katika kilimo cha udongo na kwenye mistari mingine ya kazi ya mikono. Wanapaswa kupata mafunzo ambayo yatawafaa kushika kazi yoyote katika mashamba ambayo wao wataitwa. Hakuna kazi itakayokuwa na ufanisi zaidi kuliko ile iliyofanywa na wale ambao wamepata elimu ya maisha kwa vitendo, na kwenda kwa utayari kufundisha kama walivyoelekezwa. {FEsw 512.3}

Katika mafundisho Yake Mwokozi aliwakilisha ulimwengu kama shamba la mizabibu. Tungefanya vyema kujifunza mifano ambayo kielelezo hiki kinatumika. Ikiwa ardhi italimwa katika shule zetu kwa uaminifu zaidi, na kupenda kukaa ndani ya majengo wakati wote kuepukwe na wanafunzi, upendo wa michezo na burudani, ambayo husababisha mkanganyiko mwingi katika kazi yetu ya shule, ungeyoyoma. {FEsw 512.4}

Wakati Bwana aliwaweka wazazi wetu wa kwanza katika bustani ya Edeni, ilikuwa pamoja na amri kwamba “wailime” na “waitunze.” Mungu alikuwa amemaliza kazi Yake ya uumbaji, na alikuwa ametamka vitu vyote kuwa vizuri sana. Kila kitu kiliendana na hali na matumizi ambayo Mungu aliumba kwayo. Wakati Adamu na Hawa walimtii Mungu, kazi yao katika bustani ilikuwa burudani (furaha); nchi ilitoa wingi wake wa mazao kwa mahitaji yao. Lakini wakati mwanadamu aliacha utiifu wake kwa Mungu, alikuwa amepata ole au hukumu kupigana mieleka na mbegu zilizopandwa na Shetani (magugu, miiba), na kupata mkate wake kwa jasho la uso wake. Kuanzia wakati huo, ilikuwa lazima yeye apigane katika taabu na shida dhidi ya uwezo ambao alikuwa amejitolea mapenzi yake kwa huo. {FEsw 512.5}

Lilikuwa ni kusudi la Mungu kupitia kazi (kuhenyeka) kuondoa uovu ambao mwanadamu aliufanya kwa taabu kuletwa duniani kwa kutotiii. Kwa kutoa jasho anapofanya kazi, majaribu ya Shetani yaweze kupunguzwa ufanisi wake, na wimbi la uovu lizuiwe. Mwana wa Mungu alitolewa kwa ulimwengu, kwa kifo Chake upatanisho ulifanywa kwa ajili ya dhambi za ulimwengu, kwa kupitia maisha Yake awafundishe watu jinsi mipango ya adui inavyowezwa kuzuiwa. Kwa kuchukua juu Yake asili ya mwanadamu, Kristo aliingia katika huruma na maslahi ya ndugu Zake, na kwa maisha ya kazi isiyochoka, aliwafundishwa wanadamu jinsi wanavyoweza kuwa watendakazi/vibarua pamoja na Mungu katika ujenzi wa ufalme wake duniani.

{FEsw 513.1}

Ikiwa wale ambao wamepokea maagizo kuhusu mpango wa Mungu kuhusiana na elimu ya vijana katika siku hizi za mwisho, watasalimisha mapenzi yao kwa Mungu, Yeye atawafundisha mapenzi Yake na njia Yake. Kristo anapaswa kuwa Mwalimu katika shule zetu zote. Ikiwa walimu na wanafunzi watampa Yeye nafasi Yake anayostahili, basi atafanya kazi kupitia kwao ili kutekeleza mpango wa ukombozi. {FEsw 513.1}

Wanafunzi wanapaswa kufundishwa kutafuta ushauri wa Mungu katika maombi. Wanapaswa kufundishwa kumtegemea Muumba wao kuwa kiongozi wao asiyekosea. Wanapaswa kufundishwa masomo ya ustahimilivu na uaminifu, ya utuwema wa kweli wema na wema wa moyo. Wanapaswa kujifunza somo la uvumilivu. Tabia zao zinapaswa kuitikia/kujibu maneno ya Daudi, “Ili wana wetu wawe kama mimea iliyokua katika ujana wao; Binti zetu kama nguzo za pembeni Zilizonakishwa kwa kupamba ikulu.” Katika haya yote wanastahili utumishi katika shamba la umishonari. {FEsw 513.3}

Mwanafunzi aliyeongoka amevunja mnyororo uliomfunga kwenye utumishi wa dhambi, na amejitokea mwenyewe katika uhusiano sahihi na Mungu. Jina lake limeandikwa katika kitabu cha uzima cha Mwana-Kondoo. Yeye yuko chini wajibu ulio wa wakfu (mzito) wa kukataa uovu, na kuwa chini ya mamlaka ya Mungu. Kupitia maombi ya bidii anapaswa kushikamana na Kristo. Kupuuza hili, kwa kukataa kutoa utumishi wake, ni kupoteza upendeleo wa Mwalimu Mkuu, na kuwa mchezo wa hila za Shetani. Ilikuwa ni mpango wa mbingu kwa dhabihu isiyo na kikomo ya Kristo, kuwaleta wanaume na wanawake [katika kibali na Mungu](#) tena. Elimu inayomleta mwanafunzi kwa ukaribu na uhusiano na Mwalimu aliyetumwa kutoka kwa Mungu ni elimu ya Kweli. {FEsw 514.1}

Watu wa Mungu ni vyombo Vyake vilivyochaguliwa kwa ajili ya upanuzi wa kanisa Lake duniani. Wanapaswa kutafuta shauri la Mungu. Burudani, matumbuizo na maburudisho ya kidunia yasiwe na nafasi katika maisha ya Mkristo. Kuifuata njia ya Bwana, itakuwa nguvu za watu Wake. Imani yao katika zawadi ya Mwana ambaye ni Mzaliwa-pekee wa Mungu, inapaswa kujidhihirishwa. Hii itafanya hisia zake kwenye akili ya walimwengu. Yeye ambaye huchukua nafasi yake kama yule aliye tofauti na ulimwengu, na kujitahidi kuwa kitu kimoja na Kristo, atafanikiwa katika kuzileta Roho kwa Mungu. Neema ya Kristo itakuwa dhahiri katika maisha yake kiasi kwamba ulimwengu utamjua kwamba, yeye amekuwa pamoja na Yesu, na amejifunza Kwake. {FEsw 514.2}

“Nenda ukafanye kazi leo katika shamba Langu la mizabibu,” Mwokozi anaamuru. “Basi mlapo, au mnywapo, au mtendapo neno lolote, fanyeni yote kwa Utukufu wa Mungu.” Hebu kila anayedai kuwa mtoto wa Mfalme wa Mbinguni atafute daima kuwakilisha kanuni za ufalme wa Mungu. Hebu kila mmoja

akumbuke hilo katika Roho, katika maneno na katika matendo yake, anapaswa kuwa mwadi na mwaminifu kwa maagizo na amri zote za Bwana. Tunapaswa kuwa raia waaminifu na wa kutegemewa wa ufalme wa Kristo, ili wale wenye hekima ya kidunia wawe na mfano wa kweli wa ukarimu/utajiri, wema, rehema, upole, uungwana na adabu ya raia wa ufalme wa Mungu. {FEsw 514.3} —Review and Herald, October 24, 1907.

Sura ya 66

UJUMBE KWA WALIMU

Nimepewa ujumbe kwa walimu katika shule zetu zote. Wale wanaolikubali jukumu takatifu lililoko juu ya walimu wana haja ya kuendelea mbele daima katika uzoefu wao. Hawapaswi kuridhika kubaki kwenye nyanda za chini, ila daima wawe wakipanda kuelekea juu Mbinguni. Wakiwa na Neno la Mungu mikononi mwao, na upendo kwa Roho, wakizielekeza kwenye uadilifu, wanapaswa kusonga mbele hatua kwa hatua katika ufanisi. {FEsw 516.1}

Uzoefu wa kina wa Kikristo utaunganishwa na kazi ya elimu ya Kweli. Shule zetu zinapaswa kukua kwa kasi katika Maendelea ya Kikristo {ukristo endelevu}; na ili kufanya hivi, maneno na mfano wa mwalimu unapaswa kuwa msaada kila wakati. “Ninyi nanyi, kama mawe yaliyo hai,” Mtume anatangaza, “mmejengwa kuwa nyumba ya kiroho, ukuhani mtakatifu; ili kutoa dhabihu za kiroho, zinazokubalika kwa Mungu kupitia Yesu Kristo.” Ingekuwa vyema kwa kila mwalimu na mwanafunzi kusoma kwa makini haya Maneno, akijiuliza swali, Je, mimi, kupitia ule wingi wa neema iliyotolewa, ninapata uzoefu uleule ambao kama mtoto wa Mungu lazima niwe nao ili kusonga mbele kila mara hatua kwa hatua kwenda daraja la juu zaidi? {FEsw 516.2}

Katika kila mstari wa mafundisho, walimu wanapaswa kutafuta kutoa Nuru kutoka katika Neno la Mungu, na kuonyesha umuhimu wa utii kwa “Hivi ndivyo asemavyo Bwana.” Elimu inapaswa kuwa ile ambayo wanafunzi watafanya kanuni sahihi kuwa mwongozo wa kila tendo: Hii ni elimu itakayodumu katika zama za milele zote. {FEsw 516.3}

Ninapewa maneno ya tahadhari kwa walimu katika taasisi zetu zote za shule. Kazi ya shule zetu lazima iwe na muhuri tofauti na ambao unachukuliwa na baadhi ya shule zetu maarufu, zile zinazopendwa. Usomaji wa vitabu vya kiada vya kawaida tu hautoshi; na vitabu vingi vinavyotumika sio vya lazima kwa shule ambazo zimeanzishwa kuwanda wanafunzi kwa shule iliyo juu. Matokeo yake, ni kuwa wanafunzi katika shule hizi hawapati elimu kamilifu zaidi ya Kikristo. Vipengele vingi vya kujifunza hupuuzwa ambayo vingehitajika sana ili kuwatayarisha wanafunzi kusimama kwenye mtihani mkuu wa mwisho, na kuwastahilisha kwa ajili ya kazi ya umishonari nchini hapa {Marekani} na nchi za kigeni. Elimu inayohitajika sasa ni ile itakayowawezesha wanafunzi kupata sifa za kuhitimu kwa vitendo kazi ya umishonari, kwa kuwafundisha kuweka kila nguvu chini ya udhibiti wa Roho wa Mungu. Kitabu cha masomo ambacho ni cha thamani ya juu zaidi ni kile kilicho na mafundisho ya Kristo, Mwalimu wa walimu. {FEsw 516.4}

Bwana anatazamia walimu wetu kuondoa katika shule zetu hivyo vitabu vinavyofundisha hisia zisizoendana na Neno Lake, na kuvipa nafasi vile vitabu ambavyo ni vya thamani kuu. Bwana anakusudia kwamba walimu katika shule zetu watafaulu katika hekima ya ulimwengu, kwa sababu wao wanajifunza hekima Yake. Mungu ataheshimiwa kutoka ngazi za juu hadi za chini, ikiwa walimu katika shule zetu, wataonesha kwa ulimwengu kuwa wana hekima zaidi ya ile ya wanadamu, kwa sababu Mwalimu Mkuu amesimama kama kichwa chao. {FEsw 517.1}

Walimu wetu wanapaswa kuwa wanafunzi wa kudumu. Wanamatengenezo wote wanahitaji kujiweka chini ya nidhamu ya Mungu. Maisha yao wenyewe yanahitaji yarekebishwe/yatengenezwe, mioyo yao itiishwe kwa neema ya Kristo. Kila mazoea na mawazo ya kidunia ambayo hayapatani na nia ya Mungu yanapaswa kuachwa.

{FEsw 517.2}

Nikodemo, mwalimu msomi katika Israeli, alipomwendea Yesu kumwuliza, Kristo alianika wazi mbele yake kanuni za kwanza. Nikodemu, ingawa alikuwa na cheo cha heshima katika Israeli, hakuwa na uelewa wa kweli wa kile mwalimu katika Israeli anachopaswa kuwa. Alihitaji kufundishwa katika kanuni za kwanza kabisa za maisha ya Mbingu/Kiungu, kwa kuwa hakuwa amejifunza alfabeti ya uzoefu wa Kweli wa Kikristo. {FEsw 517.3}

Kwa kujibu maagizo ya Kristo Nikodemo alisema, “Yawezekanaje kuwa mambo haya?” Kristo akajibu, “Je! wewe u mwalimu wa Israeli, na mambo haya huyafahamu?” Swali kama hilo linapaswa kuulizwa wengi ambao wanashikilia nyadhifa za kuwajibika kama walimu, madaktari, na wachungaji/wahubiri wa injili, lakini ambao wamepuuza sehemu muhimu zaidi ya elimu yao, ambayo ingewafaa kushughulikia akili za kibinadamu kwa Namna ya Kristo. {FEsw 517.4}

Katika mafundisho ambayo Kristo aliwapa wanafunzi Wake, na kwa watu wa tabaka yote waliokuja kuyasikia Maneno Yake, kulikuwa na yale mambo ambayo yaliwainua/yaliwapandisha kwenye kiwango cha juu cha mawazo na matendo. Ikiwa Maneno ya Kristo, badala ya maneno ya wanadamu, yangetolewa kwa wale watu wanaojifunza leo, tungeona ushahidi wa akili za juu, ufahamu sahihi zaidi wa mambo ya Mbinguni, maarifa ya ndani zaidi ya Mungu, maisha safi na yenye nguvu zaidi ya Kikristo. “Amin, amin, nakuambia wewe,” Kristo alisema, “yeye aniaminiye Mimi anao uzima wa milele. Mimi Ndimi chakula cha uzima. Baba zenu waliila mana jangwani, wakafa. Hiki ni chakula kishukacho kutoka Mbinguni; ili mtu akile wala asife. Mimi Ndimi chakula chenye uzima kilichoshuka kutoka Mbinguni: mtu akila chakula hiki, ataishi milele.” {FEsw 518.1}

“Naye Yesu akafahamu nafsini Mwake ya kuwa wanafunzi Wake wanalining'unikia Neno hilo, Akawaambia, Je! Neno hili linawakwaza? Itakuwaje basi mwonapo Mwana wa Adamu akipaa huko alikokuwa hapo kwanza? Roho ndiyo itiayo uzima; mwili haufai kitu; Maneno hayo niliyowaambia ni Roho, tena ni uzima.” {FEsw 518.2}

Tunakuwa wazito kuelewa ni kiasi gani tunahitaji kujifunza Maneno ya Kristo na mbinu Zake za kazi. Kama mafundisho Yake yangeeleweka vema, mengi ya mafundisho ambayo sasa yanatolewa katika shule zetu yangepewa thamani yake halisi kama ilivyo. Ingeonekana kuwa mengi ya yale sasa yanayofundishwa hayaendelezi usahili wa utauwa katika maisha ya mwanafunzi. Ndipo hekima yenye kikomo ingepokea heshima ndogo, na Neno la Mungu lingekuwa na nafasi ya heshima zaidi. {FEsw 518.3}

Walimu wetu watakapoongoka kweli kweli, watapata uzoefu wa njaa ya nafsi ya kumjua Mungu, na kama wanafunzi wanyenyekevu ndani ya shule ya Kristo, watajifunza ili kujua haki Yake. Kanuni za haki zitatawala maisha, na zitafunzwa

kama kanuni zinazotawala katika elimu ya Mbinguni. Walimu watakapotafuta kwa moyo wao wote kuleta kanuni za Kweli katika kazi ya elimu, malaika wa Mungu watakuwepo ili kufanya misukumo juu ya moyo na akili. {FEsw 518.4} – *The Review and Herald, November 7, 1907.*

Kwa Marejeleo ya Ziada

With Full Purpose of Heart, The Youth's Instructor, November 12, 1907

From Prison Cell to Egypt's Throne, The Youth's Instructor, March 17, 1908

Knowing God, The Youth's Instructor, April 7, 1908

Wise Counsel to the Youth, The Youth's Instructor, April 28, 1908.

Sura ya 67

UTOAJI ULIOFANYWA KWA AJILI YA SHULE ZETU

Wito kwa Watumishi, Madaktari, na Walimu wa Kusini California

Wanaume wanaosimama kama viongozi katika sehemu yoyote ya kazi nzito ya ujumbe wa mwisho wa injili lazima wakuze na kuthamini maoni mapana na mawazo. Ni fursa ya wote wanaobeba majukumu katika kazi ya injili kuwa wanafunzi wanaofaa katika shule ya Kristo. Yule anayedai kuwa ni mfuasi wa Kristo hapaswi kuongozwa na maagizo yake mwenyewe; akili yake lazima izoezwe kuwaza mawazo ya Kristo, na kuangaziwa kufahamu mapenzi na njia ya Mungu. Muumini wa namna hiyo atakuwa mfuasi wa mbinu za Kristo za kazi. {FEsw 520.1}

Ndugu zetu wasisahau kwamba hekima ya Mungu imefanya utoaji kwa shule zetu kwa njia ambayo italeta baraka kwa wote ambao kushiriki katika biashara. Kitabu, "Vielelezo vya Kikristo /Christ's Object Lessons," kilitolewa kwa kazi ya elimu, kwamba wanafunzi na wengine marafiki wa shule waweze kushughulikia vitabu hivi, na kwa mauzo yao kuongeza njia nyingi zinazohitajika ili kuondoa deni la shule. Lakini mpango huu haujawasilishwa kwenye shule zetu inavyopaswa imekuwa; walimu na wanafunzi hawajaelimishwa kushika hatamu ya kitabu hiki kwa ujasiri na kusukuma uuzaji wake kwa manufaa ya kazi ya elimu. {FEsw 520.2}

Zamani walimu na wanafunzi katika shule zetu walipaswa kuwa navyo na kujifunza kutumia fursa ya kuongeza njia kwa uuzaji wa kitabu "Vielelezo vya Kikristo" Katika kuuza vitabu hivi wanafunzi wataitumikia kazi ya Mungu, na, wakifanya hivi, kwa kueneza Nuru ya thamani, watajifunza masomo ya thamani katika Ukristo zoefu. Shule zetu zote sasa zinafaa kuja kwenye mstari, na kwa bidii kujitahidi kutekeleza mpango uliowasilishwa kwetu kwa ajili ya elimu ya wafanyakazi, kwa ajili ya kusaidia shule, na kwa ajili ya kujipatia Roho kwa huduma ya Kristo. {FEsw 520.3}

Katika miji ya Riverside, Redlands, na San Bernardino uwanja wa misheni umefunguliwa kwetu ambao bado tumeugusa kidogo tu kwa vidole vyetu. Kazi nzuri imefanywa huko na wafanyakazi wamekuwa na moyo wa kuifanya; lakini kuna haja ya kuwa na fedha ili kuendeleza kazi hiyo kwa mafanikio. Ilikuwa ni kusudi la Mungu kwamba kwa uuzaji wa kitabu "Huduma ya Uponyaji" na "Vielelezo vya Kikristo" fedha nyingi zilipaswa kupatikana kwa kazi ya Sanitarium (vituo vya afya kwa tiba mbadala) na shule, na kwamba watu wetu wangeachwa huru zaidi kutoa mali zao kwa ajili ya ufunguzi wa kazi katika umishonari wa mashamba au maeneo mapya. Ikiwa watu wetu sasa watashiriki katika uuzaji wa vitabu hivi kama wanavyopaswa, tutakuwa na fedha zaidi ya kutenda kazi kama jinsi Bwana alivyopanga. {FEsw 520.3}

Popote ambapo kazi ya kuuza kitabu "Masomo ya Kitu cha Kristo" imekuwa ikishikiliwa kwa dhati na bidii, kitabu kimefanya mema. Na masomo ambayo yamefunzwa na wale ambao wamejishughulisha na kazi hii, zimelipa vyema juhudi zao. Na sasa watu wetu wanapaswa kuwa wote kutiwa moyo kushiriki katika jitihada hii maalum ya umishonari. Nuru ina nimepewa mafundisho kwa kila njia iwezekanayo kwa watu wetu kuhusu mbinu bora za kuwasilisha vitabu hivi kwa

watu. {FEsw 521.1}

Nimeagizwa kwamba katika mikusanyiko yetu mikubwa, wafanyakazi wanapaswa kuwepo na kuwafundisha watu wetu jinsi ya kupanda mbegu za Ukweli. Hii ina maana zaidi ya kuwaelekeza jinsi ya kuuza gazeti “Ishara za Nyakati” na majarida mengine. Inajumuisha maagizo kamili ya jinsi kushughulikia vitabu kama vile “Vilelezo Vya Kikristo” na “Huduma ya Uponyaji.” Hivi ni vitabu ambavyo vina Ukweli wa thamani, na kutoka ambayo msomaji anaweza kuteka masomo ya thamani ya juu. {FEsw 521.2}

Kwa nini hakuteuliwa mtu katika mkutano wenu wa kambi [in 1907] kuwasilisha masilahi ya safu hii ya kazi kwa watu wetu? Kwa kushindwa kwenu kufanya hivi, mlipoteza nafasi ya thamani ya kuweka baraka kubwa zinazoweza kufikiwa na watu, na pia mlipoteza fursa ya kuchangisha fedha kwa ajili ya kusaidia taasisi zetu. Ndugu yangu, hebu tuwatie moyo watu wetu wafanye kazi hii bila kuchelewa zaidi. {FEsw 521.3}

Kuna wale ambao wamekuwa na uzoefu katika uuzaji wa vyakula vya afya ambao sasa wanapaswa kuwa na shauku katika uuzaji wa vitabu vyetu vya thamani; maana ndani yake mna chakula cha uzima wa milele. Los Angeles imekuwa ikiwasilishwa kwangu kama shamba lenye matunda mengi katika uuzaji wa “Vilelezo Vya Kikristo au Lulu za Uzima” na “Huduma ya Uponyaji.” Maelfu ya muda mfupi wakazi na wageni wanguenufaika na masomo yaliyomo, na wale wanaobeba majukumu katika Sanitarium zetu wachukue hatua kwa hekima katika jambo hili, wakiwawatia moyo wote, yaani wauguzi, wasaidizi, na wanafunzi; kukusanya fedha zinazohitajika kwa kadiri iwezekanavyo ili kukidhi gharama za taasisi mbalimbali. {FEsw 521.4}

Kwa nini watu wetu wanachelewa sana kuelewa kile ambacho Bwana angetaka wafanye? Wafanyakazi wetu wanaoongoza, wanapaswa kujiandaa mapema kutumia fursa zao kwenye mikusanyiko yetu mikubwa na midogo, kuwasilisha vitabu hivi kwa watu wetu, na wito kwa watu wa kujitolea ambao watashiriki katika mauzo yao. Kazi hii inapoanzwa kwa bidii kama ambavyo nyakati zetu zinadai, deni ambalo sasa liko juu ya shule zetu litapungua sana. Na kisha watu ambao sasa wanaitwa kutoa mali kwa kiasi kikubwa kusaidia hizi taasisi, watakuwa huru kutoa sehemu kubwa ya matoleo yao kwa kazi ya umishonari katika maeneo mengine yenye uhitaji, ambapo juhudi maalum bado hazijafanywa. {FEsw 522.1}

Matunda mazuri yatapatikana kwa kuleta vitabu hivi kwenye umakini wa viongozi wa chama cha ‘Umoja wa Wanawake wa Kikristo wa Kudhibiti Kiasi’. Sisi tunapaswa kuwaalika wafanyakazi hawa kwenye mkutano yetu, na kuwapa fursa ya kufahamiana na watu wetu. Wekeni vitabu hivi vya thamani mikononi mwao, na waelezeni ushuhuda wa zawadi yao kwa kazi hii, na matokeo yake. Elezeni jinsi uuzaji wa “Huduma ya Uponyaji,” unavyoweza kusaidia wagonjwa kuletwa kwenye

Sanitariamu kwa ajili ya uponyaji ambao wanaweza wasiupate bila ya kufika huko; na kwa kupitia njia hii msaada utaweza kutolewa katika uanzishwaji wa Sanitarium zetu katika maeneo ambayo zinahitajika sana. Ikiwa sanitariamu zetu zinasimamiwa kwa busara na wanaume na wanawake wanaomcha Mwenyezi Mungu na kumweka mbele, hao watakuwa njia ya kutuleta katika uhusiano na wafanyakazi wa chama cha 'Umoja wa Wanawake wa Kikristo wa Kudhibiti Kiasi.Woman's Christian Temperance Union'. Mwanamke , na wafanyikazi hawa hawatachelewa kuona faida ya tawi hili la matibabu la kazi yetu. Kama matokeo ya mawasiliano yao na kazi yetu ya kitiba, baadhi yao watajifunza zile Kweli ambazo wanahitaji kuzijua ili kuwa na tabia kamilifu ya Kikristo. {FEsw 522.2}

Jambo moja ambalo halipaswi kusahaulika na wafanyikazi wetu ni kwamba Bwana Yesu Kristo Ndiye Kiongozi na mkurugenzi wetu mkuu. Ameeleza mpango ambao kwa huo shule zetu zinaweza kuondokana na madeni yake; na Yeye atashughulika na mwenendo wa wale wanaoweka mpango huu kando kwa kukosa ujasiri katika mafanikio yake. Wakati watu Wake Mungu watakuja kwa umoja na kuwa msaada wa kazi Yake hapa duniani, hakuna lile jambo jema aliloahidi Mwenyezi Mungu, ambalo litazuiliwa. {FEsw 523.1}

Katika maeneo kama Los Angeles, ambapo watu daima hubadilika, fursa nzuri zinawasilishwa kwa uuzaji wa yetu vitabu. Hasara kubwa imepatikana kwa sababu watu wetu hawajapata kuchangamkia kwa kikamilifu zaidi fursa hii. Kwanini walimu na wanafunzi kutoka Shule ya San Fernando wasifanye Los Angeles uwanja maalum wa uuzaji wa "Vilelezo Vya Kikristo au Lulu za Uzima"? Ikiwa kuna bidii na imani watatekeleza mpango ambao tumepewa kwa ajili ya matumizi ya kitabu hiki, malaika wa Mungu watatembea nao hatua kwa hatua, na baraka za Mbinguni zitakuwa juu ya juhudi zao. {FEsw 523.2}

Lingekuwa jambo zuri kama walimu wa Shule ya San Fernando wakati wa likizo, wanatoa nafasi hii katika kusukuma kazi na kitabu "Vilelezo Vya Kikristo au Lulu za Uzima." Wangepata baraka kwa kwenda nje na wanafunzi na kuwafundisha jinsi ya kukutana na watu, na jinsi ya kukitambulisha kitabu hiki. Kisa cha zawadi ya kitabu hiki na lengo lake, ingeongoza baadhi yao kuwa na shauku maalum kwa kitabu na katika shule hii ambayo kitabu hicho kinauzwa. {FEsw 523.3}

Kwa nini walimu katika shule zetu hawajafanya kazi hii zaidi? Ikiwa watu wetu wangetambua tu, kwamba hakuna kazi inayokubalika tena kufanyika katika uwanja wa nyumbani kuliko kujihusisha na uuzaji wa "Vielelezo vya Kikristo"; kwa maana wakati wanasaidia katika kutimiza mpango wa Bwana mpango na kwa ajili ya kuleta unafuu kwenye shule zetu, wao pia watakuwa wanaleta zile Kweli za thamani za Neno la Mungu kwenye umakini wa watu. {FEsw 523.4}

Kutokujali ambako kumedhihirishwa na baadhi ya watu kuhusu shughuli hii hakumpendezi Mungu. Anataka itambulike na watu wetu wote kama hii ni mbinu

Yake ya kuzikomboa shule zetu kutokana na madeni. Ni kwa sababu mpango huu umepuuzwa kwamba sasa tunahisi kwa ukali zaidi ukosefu wetu wa fedha za kuendeleza kazi hii. Kama shule zingejitoa zenyewe kwa majaliwa yaliyotolewa kwa ajili yao, kungekuwako fedha zaidi katika hazina ya shule, na fedha zaidi katika mikono ya Watu wake, ili kunusuru mahitaji ya idara nyingine zenye uhitaji wa sababu, na, bora zaidi, walimu na wanafunzi wangepokea masomo yale yale ambayo walihitaji kujifunza katika utumishi wa Bwana/Mwalimu. {FEsw 524.1}

Ninakutumia mistari hii kwa sababu naona kwamba kuna haja ya busara na uvuvio zaidi, mtazamo mpana zaidi, kwa upande wa wafanyakazi wetu wa afya na elimu, ikiwa wangetaka kupata manufaa yote ambayo Mungu anakusudia wayapate kupitia kitabu cha “Vilelezo Vya Kikristo au Lulu za Uzima” na “Huduma ya Uponyaji.” Nawaomba, ndugu zangu, wasomeeni watu wetu maneno haya ili wapate kujifunza kuonyesha Roho ya hekima, na ya nguvu, na moyo wa hekima, na kiasi. {FEsw 524.2}— *The Review and Herald, September 3, 1908.*

MWALIMU, JITAMBUE

Kujijua/kujitambua mwenyewe ni maarifa makubwa. Maarifa ya kujijua mwenyewe husababisha unyenyekevu ambao utamruhusu Bwana kuizoeza akili, na kuiumba na kuitia nidhamu tabia. Neema ya unyenyekevu vinahitajika sana na watenda kazi kwa ajili ya Kristo katika kipindi hiki cha historia ya ulimwengu. Hapana mwalimu anayeweza kufanya kazi inayokubalika kwa Kristo ikiwa hatazingatia mapungufu ya tabia yake mwenyewe na ambaye hatazitupilia mbali tabia zote zinazodhoofisha maisha yake ya kiroho. Wakati walimu wako tayari kudondosha chini kila kitu kwenye kazi zao kisicho cha lazima kwa ajili ya uzima wa milele, basi wanaweza kusemwa kuwa wanafanyia kazi wokovu wao kwa hofu na kutetemeka, na kuwa wanajenga kwa busara ule umilele. {FEsw 525.1}

Nimeagizwa kusema kwamba baadhi ya walimu wetu wako nyuma sana katika kuelewa aina ya elimu inayohitajika kwa kipindi hiki ya historia ya dunia. Huu sio wakati wa wanafunzi kujikusanyia wingi wa maarifa ambayo hawawezi kwenda nayo shule ya Mbinguni juu. Wacha tukuze na kupalilia kwa uangalifu kutoka katika kozi yetu, masomo yote ambayo tunaweza kuepukana nayo, ili tupate nafasi ya kupanda mbegu za haki katika akili za wanafunzi. Mwongozo huu utazaa matunda ya uzima wa milele. {FEsw 525.2}

Kila mwalimu anapaswa kuwa mwanafunzi wa kila siku katika shule ya Kristo, ili asije akapoteza maana halisi ya kile ambacho ni kweli kimwili, kiakili, na ubora wa maadili. Hakuna mtu anayepaswa kujiweka kama mwalimu wa wengine kama hafanyii kazi wokovu wake mwenyewe kwa kupokea na kutoa elimu nyanja zote (kiroho, kimwili, kiakili, kijamii, kiuchumi). Mwalimu wa kweli atajielimisha yeye mwenyewe kuwa na maadili bora, ili kwa amri na mfano aongoze wengine katika kuelewa masomo ya Yule Mwalimu Mkuu. Hakuna anayepaswa kuhimizwa kufanya kazi ya kufundisha kama ana viwango vya chini. Hakuna mtu anayefaa kufundisha mafumbo na siri kuu za utauwa hadi Kristo tumaini la Utukufu, aumbike ndani yake. {FEsw 525.3}

Kila mwalimu anahitaji kupokea ile Kweli kwa kuzipenda kanuni Zake takatifu; ndipo hataweza kushindwa kushinikiza mvuto ambao ni wa kutakasa na kuinua. Mwalimu ambaye Roho yake imekaa juu ya Kristo atazungumza na kutenda kama Mkristo. Mtu kama huyo hataridhika mpaka Ukweli umetakasa maisha yake kutokana na kila jambo lisilo la lazima. Hataridhika, isipokuwa akili yake itakuwa ikiumbwa siku baada ya siku kwa mivuto mitakatifu ya Roho wa Mungu. Ndipo Kristo aweza kusema na moyo wake, na sauti Yake, itasikika ikisema “Njia ni hii; tembee ni ndani yake,” naye ataisikia sauti hiyo na kuitii. {FEsw 526.1}

Mwalimu ambaye ana ufahamu sahihi wa kazi ya elimu ya Kweli, hatafikiria kuwa inatosha sasa na kisha kumnukuu Kristo katika kumbukumbu yake, kwa Njia ya kawaida. Kwa moyo wake mwenyewe, wenye joto na upendo wa Mungu, atamwinua daima Mtu wa Kalvari. Nafsi yake mwenyewe akiwa amejazwa na Roho wa Mungu, atatafuta kukazia kwa wanafunzi juu ya Kile Kielelezo, yaani Kristo Yesu, mkuu kati ya kumi elfu, Mmoja Mwenye kupendeza kabisa (**Wimbo wa Sulemani 5**). {FEsw 526.2}

Roho Mtakatifu anahitajika sana katika shule zetu. Wakala huyu wa Kiungu, huja ulimwenguni kama mwakilishi wa Kristo. Yeye sio tu shahidi mwaminifu na wa Kweli wa Neno la Mungu, lakini ni mchunguzi ya mawazo na makusudi ya moyo. Ni chanzo ambacho lazima tutafute ufanisi katika kurejesha taswira ya maadili ya Mungu ndani ya mwanadamu. Roho Mtakatifu alitafutwa kwa hamu kwenye shule za manabii; ushawishi Wake wa kubadilisha uliyaleta hata mawazo katika upatanifu na mapenzi ya Mungu, na kuanzisha muunganiko kati ya mbingu na nchi. {FEsw 526.3}

Walimu, kama mtafungua mioyo yenu kuwa makazi Roho wa Mungu, ikiwa mtamkaribisha Mgeni wa Mbinguni, Mungu atawafanya ninyi kuwa watenda kazi pamoja Naye. Kwa kushirikiana na Mwalimu Mkuu, Roho ya ubinafsi itatupwa nje, na mabadiliko ya ajabu yatachukufa nafasi moyoni. {FEsw 526.4}

Katika majira ya usiku niliambiwa maneno haya: “Waamuru walimu katika shule zetu kuwatayarisha wanafunzi kwa yale yanayokuja juu ya dunia.” Bwana amekuwa akiwangojea walimu wetu kwa muda mrefu, watembee katika Nuru aliyowatumia. Kuna haja ya kujinyenyekeza nafsi, ili Kristo arudishe sura ya maadili ya Mungu ndani ya mwanadamu. Tabia ya elimu inayotolewa lazima ibadilishwe sana kabla ya kutoa umbo sahihi kwenye taasisi zetu. Ni pale tu ambapo nguvu za kiakili na kimaadili zimeunganishwa kwa pamoja kwa ajili ya kupata elimu, ndipo kiwango cha Neno la Mungu hufikiwa. {FEsw 526.5}

Maneno haya yalisemwa kwa uwazi na kwa nguvu: “Hivyo muungame dhambi ninyi kwa ninyi, na kuombeana ninyi kwa ninyi ili muweze kuponywa. Maombi yanayofanywa na mtu mwenye haki yana nguvu sana na yana matokeo makubwa sana.” Bwana amelipa gharama ya damu Yake Mwenyewe kwa ajili ya wokovu wa watu dunia. Alikumbana na kudhaliishwa na kila aibu ambayo wanadamu wangeweza kupanga, na yale ambayo Shetani angeweza kubuni, ili kutekeleza mpango wa wokovu. Hebu mwalimu asitafute kujiinua, lakini aone umuhimu wa kujifunza Kristo kila siku, na kumfanya Yeye kuwa kielelezo. Kwa walimu na wanafunzi Bwana na Mwokozi wetu Yesu Kristo Ndiye anapaswa kuwa mfano wetu pekee. {FEsw 527.1}

Kumbukeni kwamba Bwana atakubali walimu wale tu ambao watakuwa walimu wa injili. Wajibu mkubwa ni juu ya wale ambao watajaribu kufundisha ujumbe wa

mwisho wa injili. Wanapaswa kuwa watendakazi pamoja na Mungu katika kufunza akili za wanadamu. Mwalimu ambaye anashindwa kuweka kiwango cha Biblia mbele yake daima, hukosa fursa ya kuwa mtenda kazi pamoja na Mungu katika kuipa akili umbo ambalo ni muhimu kwa ajili ya nyua za Mbinguni. {FEsw 527.2}—
[The Review and Herald, September 3, 1908.](#)

Kwa Marejeleo ya Ziada

[The Business Principles of the Christian, Signs of the Times, February 24, 1909](#)

[The Aim of Our Schools, The Review and Herald, March 4, 1909](#)

[Higher Education a Preparation for Service, The Review and Herald, March 25, 1909](#)

[God in Nature, The Signs of the Times, May 5, 12, 19, 1909](#)

[Home Schools, The Review and Herald, May 6, 1909.](#)

[Christ the Example of the Children and Youth, The Youth's Instructor, May 25, 1909](#)

Sura ya 69

KAZI ILIYO MBELE YETU

Kuna kazi kubwa na muhimu sana ya kufanya kwenye Konferensi zetu Marekani. Tunapaswa kubeba kazi hii hapa Marekani kwa njia ambayo itakuwa na nguvu na msaada kwa wale wanaoutangaza ujumbe katika nchi za mbali. Kila taifa, lugha, na watu wanapaswa kuamshwa na kuletwa kwenye ujuzi wa ile Kweli. Kuna kitu kinaendelea kufanywa, lakini kuna mengi bado ya kufanywa, mengi ya kujifunza hapa hapa kwenye konferensi/jimbo hili, ili kazi iendelee kwa njia ambayo itamheshimu na kumtukuza Mungu. {FEsw 529.1}

Nafsi yangu imelemewa sana kiasi kwamba sijaweza kupumzika. Ni mstari gani tunaweza kukaa juu yake ambao utafanya hisia ya ndani zaidi juu ya akili ya mwanadamu? Ni shule zetu. Hizi zinapaswa kuendeshwa kwa namna ambayo zitazalisha wamisionari ambao watakwenda kwenye barabara kuu na viunga ili kupanda mbegu za Ukweli. Hili lilikuwa ndilo agizo la Kristo kwa wafuasi Wake. Walipaswa kwenda kwenye barabara kuu na vinjia wapitavyo watu wakipeleka ujumbe wa ile Kweli, kwa Roho ambazo zingeletwa kwenye imani ya injili. Nilihisi kwa dhati sana mapungufu, wakati niliona uhitaji mkubwa katika maeneo niliyoyatembelea hivi karibuni. Ni lazima tusimame katika nguvu za Mungu ikiwa tutafanya hivyo kukamilisha kazi hii. {FEsw 529.2}

Katika kazi zake kila mtenda kazi amtazame Mungu. Tunapaswa kufanya kazi kama wanaume na wanawake ambao wana muunganiko hai na Mungu. Tunapaswa ujifunza jinsi ya kukutana na watu pale walipo. Hebu hali hizo mbaya zisiwepo tena katika baadhi ya maeneo tutakaporudi Marekani, ambamo washiriki wa kanisa badala ya kutambua wajibu wao binafsi, walitazama watu wengine kuwaongoza, na watu ambao walikuwa wamekabidhiwa amana takatifu katika kuendeleza kazi, walishindwa kuelewa thamani ya wajibu wa kibinafsi na wakajikobeka kazi ya kuwaamrisha wengine, na wakawa kama madiktea kwa ndugu zao wakiwaambia kitu kufanya na cha kutofanya. Haya ni mambo ambayo Mungu hataruhusu katika kazi yake. Ataweka mizigo Yake juu ya wale wabeba mizigo. Kila nafsi ina wajibu mbele za Mungu, na haitakiwi kufundishwa kiholela na wanadamu wengine kuhusu kile watafanya, watakachosema, na mahali watakapokwenda. Hatutakiwi kuweka ujasiri au tumaini letu katika shauri la wanadamu na kukubaliana kila watakalotaka isipokuwa tuna ushahidi kwamba wako chini ya ushawishi wa Roho wa Mungu. {FEsw 529.3}

Jifunze sura ya kwanza na ya pili ya Matendo. Nuru imetolewa kwangu, kwamba

kazi yetu lazima iendelezwe kwa hali ya juu na pana kuliko ilivyowahi kubebwa. Nuru ya Mbinguni inapaswa kuthaminiwa na kupendwa. Nuru hii ni ya watendakazi. Ni kwa ajili ya wale wanaohisi kwamba Mungu amewapa ujumbe, na kwamba wao wana jukumu takatifu la kubeba na kutangaza. {FEsw 530.1}

Ujumbe wa Ukweli wa sasa ni katika kuwatayarisha watu kwa ajili ya ujio wa pili wa Bwana. Hebu tuelewe hili, na hebu wale waliowekwa katika nafasi za uwajibikaji wakutane katika umoja ili kazi iende mbele kwa uthabiti. Usimruhusu mtu yeyote aingie kwenye hii kazi kama mtawala holela na kuamrisha, “ni lazima uende hapa, haupaswi kwenda huko; ni lazima ufanye hivi, na hupaswi kufanya vile.” Tuna kazi kubwa na muhimu ya kufanya, na Mungu angetaka tuishike kazi hiyo kwa akili. Uwekaji wa watu katika nafasi za uwajibikaji katika Konferensi/majimbo mbalimbali, haiwafanyi wao kuwa miungu. Hakuna aliye na hekima ya kutosha kutenda bila ushauri. Wanaume wanahitaji kushauriana na ndugu zao, kushauriana pamoja, kuomba pamoja, na kupanga pamoja kwa ajili ya kuiendeleza kazi. Hebu na watenda kazi na wapige magoti pamoja na kumwomba Mungu, aongoze mwenendo na njia yao. Kumekuwa na ukosefu mkubwa kwetu kwenye kipengele hiki. Tumeiamini sana mipango ya watu. Hatuwezi kumudu kufanya hivi. Nyakati za hatari zimetufikia, na lazima tufike mahali ambapo tunajua kwamba Bwana anaishi na kutawala, na kwamba anakaa ndani ya mioyo ya wana wa wanadamu. Ni lazima tuwe na imani kwa Mungu. {FEsw 530.2}

Popote pote mtakapotumwa, thaminini ndani ya mioyo na akili zenu hofu ya Mungu na upendo Kwake. Nenda kwa Bwana kila siku kwa mafundisho na mwongozo; Mtegemee Mungu kwa Nuru na maarifa. Ombea mwongozo na Nuru hii, mpaka uipate. Haitakufaa kumwuliza Bwana, na kisha ukasahau jambo uliloliombea. Weka akili yako kwenye jambo uliloliombea. Unaweza kufanya hivyo wakati unafanya kazi na mikono yako. Unaweza kusema, Bwana, naamini; kwa moyo wangu wote naamini. Hebu nguvu za Roho Mtakatifu zije juu yangu. {FEsw 530.3}

Ikiwa kungekuwa na kusali zaidi kati yetu, mazoezi zaidi ya imani hai, na kutegemea kwa udogo sana maombi ya mtu mwingine kuwa kama mbadala wa uzoefu wetu, basi tungekuwa mbali zaidi na mahali tulipo leo katika akili ya kiroho. Tunachohitaji ni uzoefu wa kina, wa moyo na Roho ya mtu binafsi. Ndipo tutaweza kusema ni nini MUNGU anafanya na jinsi anavyofanya kazi. Tunahitaji kuwa na uzoefuhai katika mambo ya MUNGU; na sisi hatuko salama mpaka tutakapokuwa na uzoefu huo. Kuna wengine ambao wana uzoefu mzuri, na wanaweza wakuambie juu yake; lakini unapokuja kuupima, unaona kuwa huo sio uzoefu sahihi, kwani hauedani na Ukweli wa “Bwana asema hivi.” Ikiwa kuna wakati katika historia yetu tuliohitaji kujinyenyekeza Roho zetu binafsi mbele za MUNGU, basi ni leo. Tunahitaji kumwendea MUNGU kwa imani katika yote yaliyoahidiwa katika Neno, na kisha tutembeke katika Nuru na nguvu zote ambazo MUNGU anatoa.. {FEsw 531.1}

Niliguswa kwa ndani sana wakati ndugu zetu ambao walitoka nje ya nchi ya Marekani, ambao wapo kwenye mashamba ya Bwana waliponiambia kidogo kuhusu uzoefu wao na jinsi Bwana alivyotenda katika kuleta Roho kwenye Ukweli. Hiki ndicho tunachotaka katika wakati kama huu. Mungu hataki tuendeleze katika ujinga. Anataka tuweze kuelewa wajibu wetu binafsi Kwake. Atajifichua/atajifunua Yeye Mwenyewe kwa kila nafsi itakayomjia kwa unyenyekevu na kumtafuta Yeye kwa moyo wote. {FEsw 531.2}

Kuna shule zitaanzishwa katika nchi za nje na kwenye nchi yetu wenyewe. Ni lazima tujifunze kutoka kwa Mungu jinsi ya kuzisimamia shule hizi. Hazipaswi kuendeshwa jinsi ambavyo nyingi zimesimamiwa. Taasisi zetu zinapaswa kuzingatiwa kama nyenzo Zake Mungu kwa ajili ya kuendeleza kazi Yake hapa duniani. Ni lazima tumtazame Mungu katika kupata mwongozo na hekima; lazima tumsihi atufundishe jinsi ya kubeba kazi kwa uimara. Hebu tumtambue Bwana kama Mwalimu wetu na Kiongozi, na kisha tutabeba kazi kwa mistari sahihi. Tunahitaji kusimama kama kampuni yenye umoja ambayo tunafanya kazi kwa upatanifu (tunatazamana machoni bila ugomvi). Kisha tutaona wokovu wa Mungu ukifunuliwa mkono wa kuume na wa kushoto. Ikiwa tunafanya kazi kwa upatanifu, tunampa Mungu nafasi ya kufanya kazi kwa ajili yetu. {FEsw 531.3}

Katika kazi zetu zote zihusiano na shule tunahitaji kuwa na uelewa sahihi wa elimu muhimu ni nini. Wanaume huzungumza sana juu ya elimu ya juu, lakini ni nani anayeweza kufafanua elimu ya juu ni nini? Elimu ya juu zaidi hupatikana katika Neno la Mungu aliye hai. Elimu ile ambayo inatufundisha sisi kusalimisha Roho zetu kwa Mungu kwa unyenyekevu wote, na ambayo hutuwezesha kulichukua Neno la Mungu na kukiamini kile tu anachosema, hakika hiyo ndiyo elimu inayohitajika zaidi. Kwa elimu kama hii sisi tutaona wokovu wa Mungu. Tukiwa na Roho wa Mungu juu yetu, tunapaswa kubeba Nuru ya Ukweli katika njia kuu na njia ndogo, ili wokovu wa Mungu udhihirishwe kwa namna ya ajabu. {FEsw 532.1}

Je, tutaendeleza kazi katika njia ya Bwana? Je, sisi tu tayari kufundishwa na Mungu? Je, tutashindana na Mungu katika maombi? Je, tutapokea ubatizo wa Roho Mtakatifu? Hiki ndicho tunachohitaji na tunaweza kuwa nacho wakati huu. Kisha tutatoka na ujumbe kutoka kwa Bwana, na Nuru ya ile Kweli itang'aa kama taa inayoangaza, na kufika sehemu zote za dunia. Ikiwa tutatembea kwa unyenyekevu pamoja na Mungu, Mungu Naye atatembea pamoja nasi. Hebu tunyenyekee nafsi zetu mbele Zake Yeye, nasi tutaona wokovu Wake. {FEsw 532.2}— *The Review and Herald, October 21, 1909.*

Sura ya 70

USHAURI KWA WALIMU

[Bi. E. G. White na kikundi chake (wenzake) wakielekea kwenye Mkutano wa halmashauri kuu {General Conference/konferensi kuu} , ulitumia siku tano katika mji wa College View, California. Ijumaa asubuhi yeye alizungumza na wanafunzi mia tano katika kanisa la chuo, na Sabato na Jumapili alizungumza na makutaniko makubwa kanisani. Jumatatu asubuhi, kwa ombi, alikutana na wakufunzi wa chuo. Zifuatazo ni sehemu ya hotuba yake kwa walimu thelathini waliokusanyika. —W. C. White.]

Nitasoma Wakorintho 2, sura ya sita: {FEsw 533.1}

“Basi sisi, tukiwa watenda kazi pamoja Naye, twawasihi ninyi pia msipokee neema ya Mungu bure. (Kwa maana asema, Wakati uliokubalika nalikusikia, Siku ya wokovu nalikusaidia;tazama,wakati uliokubalika ndiyo sasa; tazama siku ya wokovu ni sasa). Tusiwe kwazo la namna yo yote katika jambo lo lote, ili utumishi wetu usilaumiwe; bali katika kila neno tujipatie sifa njema, kama watumishi wa Mungu; katikasaburi nyingi, katika dhiki, katika misiba, katika shida; katika mapigo, katika vifungo, katika fitina, katika taabu, katika kukesha, katika kufunga; katika kuwa safi, katika elimu, katika uvumilivu, katika utu wema, katika Roho Mtakatifu, katika upendo usio unafiki; katika Neno la kweli, katika nguvu ya Mungu; kwa silaha za haki za mkono wa kuume na za mkono wa kushoto; kwa Utukufu na aibu; kwa kunenwa vibaya na kunenwa vema; kama wadanganyao, bali tu watu wa Kweli; kama wasiojulikana, bali wajulikanao sana; kama wanaokufa, kumbe tu hai; kama wanaorudiwa, bali wasiouawa; kama wenye huzuni, bali siku zote tu wenye furaha; kama maskini, bali tukitajirisha wengi; kama wasio na kitu, bali tu wenye vitu vyote.....Vinywa vyetu vimefumbuliwa kwenu, enyi Wakorintho; mioyo yetu imekunjuliwa..... {FEsw 533.2}

“Msifungwe nira pamoja na wasioamini kwa jinsi isivyo sawasawa; Je, kuna ushirika wa haki na udhalimu? Tena pana shirika gani kati ya Nuru na giza? na

Kristo ana ulinganifu gani na Belial? Au yeye aaminiye ana sehemu gani pamoja na asiyeamini? Na Kuna mapatano gani kati ya hekalu la Mungu na sanamu? kwa maana ninyi ni hekalu la Mungu aliye hai; kama Mungu alivyosema, nitakaa ndani yao, na kutembea ndani yao; Nami nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu wangu. Kwa hiyo, tokeni kati yao, mkatengwe nao, asema Bwana, wala msiguse kitu kilicho kichafu; Nami nitawapokea ninyi, na nitakuwa Baba kwenu, nanyi mtakuwa wanangu wa kiume na wa kike; asema Bwana wa majeshi.” {FEsw 533.3}

Unapaswa kuichunguza, kujifunza na kusoma pia sura ya saba, lakini sitachukua muda kuisoma sasa. {FESW 534.1}

Kuna hatari ya mara kwa mara miongoni mwa watu wetu kwamba wale wanaojishughulisha na kazi katika shule zetu na nyumba Sanitarium (tiba rahisi na mbadala, nayotumia matabibu 8) watafurahia wazo hilo, kwamba lazima waendane/wapatane na ulimwengu, yaani wajifunze mambo ambayo ulimwengu unajifunza, na kuyafahamu mambo ambayo ulimwengu unayafahamu na kuwa na mazoea nayo. Hili ni moja ya makosa ya makubwa zaidi zaidi yanayoweza kufanywa. Tutafrica makosa ya kutisha isipokuwa tutatoa umakini maalum na kuchunguza Neno. {FEsw 534.2}

Swali Huulizwa, Elimu ya juu ni nini? Hakuna elimu ya juu kuliko ile iliyomo katika kanuni zilizowekwa katika Maneno niliyokusomea kutoka katika sura hii ya sita ya Nyaraka ya pili ya Wakorintho. Hebu wanafunzi wetu wajifunze jambo hili kwa uadilifu ili kufahamu. Hakuna elimu ya juu zaidi ya ile iliyotolewa kwa wanafunzi 12 wa kwanza, ambayo sisi tumepewa kwa Neno la Mungu. Roho Mtakatifu wa Mungu avute mawazo yako na usadikisho kwamba hakuna kitu katika ulimwengu wote, kilichoinuliwa juu kabisa, katika mstari wa elimu ambacho ni zaidi ya yale mafundisho yaliyomo katika sura ya sita na ya saba ya Barua ya Wakorintho wa Pili. Hebu tusonge mbele katika kazi zetu hadi kufikia lile Neno la Mungu litakalotuongoza. Hebu tufanye kazi kwa akili kuhusu hii elimu ya juu. Hebu haki yetu iwe tu ile ishara ya ufahamu wetu kuhusiana na mapenzi ya Mungu tuliyokabidhiwa kupitia wajumbe Wake. {FEsw 534.3}

Ni fursa ya kila mwamini kuchukua maisha ya Kristo na mafundisho ya Kristo kama somo lake la kila siku. Elimu ya Kikristo maana yake kukubali kwa hisia na kwa kanuni mafundisho ya Mwokozi. Inajumuisha kutembea kwa uangalifu kila siku katika nyayo za Kristo, aliyekubali kulivua vazi Lake la kifalme na taji na kuja katika ulimwengu wetu kwa umbo la ubinadamu, ili atoe kwa jamii ya wanadamu uwezo ambao hawangeweza kuupata kwa njia nyingine yoyote. Nguvu hiyo ilikuwa nini basi? Ilikuwa ni nguvu iliyoleta asili ya mwanadamu kuungana na Mungu, uwezo wa kuchukua mafundisho ya Kristo na kuyafuata mpaka kwenye yodi/nukta. Katika kupinga Kwake maovu na kazi Yake kwa ajili ya wengine Kristo alikuwa akiwapa wanadamu kielelezo cha Elimu iliyo ya juu kupita elimu zote, ambayo mtu yeyote anaweza kuipata. {FEsw 534.4}

Mwana wa Mungu alikataliwa na wale aliokuja kuwabariki. Alitwaliwa na mikono ya waovu na kusulubiwa. Lakini baada ya kufufuka kutoka kwa wafu, alikuwa pamoja na wanafunzi Wake siku arobaini, na wakati huu maalum, aliwapa mafundisho Wake mengi ya thamani. Aliweka msingi kwa wanafunzi Wake kufuata kanuni zinazohusisha haswa msingi wa elimu ya juu. Na wakati alipokuwa karibu kuwaacha na kwenda kwa Baba Yake, Maneno Yake ya mwisho kwao Yalikuwa, "Mimi Nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari." {FEsw 535.1}

Kwa wengi wanaowaweka watoto wao katika shule zetu, majaribu yenye nguvu yatakuja, kwa sababu wanatamani wapate kile ambacho ulimwengu umekipata na ambacho kinachukuliwa kuwa ndiyo elimu muhimu zaidi. Ni nani anajua kwa hakikai, kile kinachojumuisha elimu muhimu zaidi, isipokuwa ni elimu inayopatikana kutoka katika Kitabu kile ambacho ni msingi wa elimu yote ya Kweli? Wale ambao huona kwamba elimu muhimu ni ujuzi ule unaopatikana katika mstari huo wa elimu ya dunia, hawa wanafanya kosa kubwa, ambalo litawasababisha kuyumbishwa na maoni ya watu binafsi ambayo ni ya kibinadamu na yenye makosa. Kwa wale wanaohisi kwamba watoto wao lazima wawe na kile ulimwengu huita elimu muhimu, ningesema, Waletе watoto wako kwa usahili wa Neno la Mungu, nao watakuwa salama. Sisi ni Tutatawanywa sana kila mahali, si muda mrefu, na kile tunachofanya lazima kiweze kufanyika kwa haraka. {FEsw 535.2}

Nuru imetolewa kwangu kwamba shinikizo kubwa litakuwa kuletwa juu ya kila Madventista wa Sabato ambaye ulimwengu pamoja naye inaweza kuingia kwenye uhusiano wa karibu. Wale wanaotafuta elimu ambayo Dunia inathaminiwa sana, hatua kwa hatua inaongozwa zaidi na zaidi kutoka kanuni za ukweli hadi wawe walimwengu walioelimika. Katika wamepata bei gani elimu yao! Wameachana na Roho Mtakatifu wa Mungu. Wamechagua kukubali kile ambacho dunia inaita maarifa mahali pa ukweli ambao Mungu ametenda kwa watu kupitia watumishi wake na manabii na mitume. Na kuna ni baadhi ambao, baada ya kupata elimu hii ya dunia, wanadhani kuwa wao inaweza kuitambulisha katika shule zetu. Lakini wacha nikuambie kwamba lazima usichukue kile ambacho ulimwengu unakiita elimu ya juu na kuileta shule zetu na huduma za usafi na makanisa. Tunahitaji kuelewa mambo haya. Ninazungumza nawe bila shaka. Hili halipaswi kufanywa. {FEsw 535.3}

Juu ya akili ya kila mwanafunzi inapaswa kuvutiwa na wazo hilo kwamba elimu ni kutofaulu isipokuwa ufahamu umejifunza zifahamu kweli za ufunuo wa Mwenyezi Mungu, na isipokuwa moyo haukubali mafundisho ya injili ya Kristo. Mwanafunzi ambaye, katika nafasi ya kanuni pana za neno la Mungu, zitakubali mawazo ya kawaida, na itaruhusu wakati na umakini kufyonzwa katika kawaida, mambo madogo, atapata akili yake kuwa duni na kudhoofika. Amepoteza nguvu ya ukuaji. Akili lazima ifundishwe kufahamu kweli muhimu zinazohusu uzima wa milele. {FEsw 536.1}

Nimeagizwa kwamba tunapaswa kubeba akili za wanafunzi wetu kwenda juu kuliko inavyofikiriwa kuwa inawezekana. Moyo na akili vinapaswa kufunzwa kuhifadhi usafi wao moyo kwa kupokea ugavi wa kila siku kutoka kwenye ile chemchemi ya Ukweli wa milele. Akili na Mkono wa Mungu umehifadhi kupitia vizazi vyote, rekodi ya uumbaji katika usafi wake. Ni Neno la Mungu pekee Ndilo linatupa taarifa ya Kweli yote na Kweli halisi ya uumbaji wa dunia yetu. Neno hili ndilo linapaswa kuwa somo kuu katika shule zetu. Ndani Yake tunaweza kunena na Wazee wa Imani na Manabii. Ndani Yake tunaweza kujifunza bei ya ukombozi wetu, ilimgharimu Yeye nini, kwamba Yeye ambaye alikuwa sawa na Baba kutoka mwanzo, na ambaye alitoa dhabihu uhai Wake ili watu waweze kusimama mbele Zake wakiwa wamekombolewa kutoka kila kitu cha duniani na cha kawaida na kufanywa upya kwa mfano wa Mungu. {FEsw 536.2}

Ikiwa tunataka kujifunza juu ya Kristo, ni lazima tusali kama mitume walivyoomba, wakati Roho Mtakatifu alipomiminwa juu yao. Tunahitaji ubatizo wa Roho wa Mungu. Hatuko salama kwa saa hata moja wakati tunafeli/ukishindwa kutoa utii kwa Neno la Mungu. {FEsw 537.1}

Sisemi kwamba watu wasijifunze lugha mbalimbali. Lugha zinapaswa kujifunzwa. Muda si mrefu kutakuwa hili litakuwa chanya na la ulazima, kwa kuwa wengi wataondoka majumbani mwao na kwenda kufanya kazi miongoni mwa watu wenye hizo lugha zingine; na wale ambao wana ujuzi fulani wa lugha za kigeni watapata nafasi ya kuwasiliana na wale wasiojua ile Kweli. Baadhi ya watu wetu watajifunza lugha katika nchi wanazotumwa. Hii ndiyo njia bora zaidi. Na kuna Mmoja ambaye atasimama kando ya mtenda kazi mwaminifu na kufungua ufahamu kwa kuwapa hekima. Bwana anaweza kufanya yao kazi yenye matunda mahali ambapo wanaume hawajui lugha ya kigeni. Wanapokwenda kati ya watu, na kuwasilisha machapisho, Bwana atafanya kazi juu ya akili ili kutoa ufahamu wa ile Kweli. Baadhi wanaofanya kazi katika nchi za kigeni wanaweza kufundisha Meno kupitia mkalimani. Kama matokeo ya bidii yenye uaminifu, kutakuwa na mavuno zilizokusanywa, thamani ambayo sisi hatuelewi kwa sasa. {FEsw 537.2}

Kuna aina nyingine ya kazi inayopaswa kuendelezwa ili isonge mbele, kazi katika ile miji mikubwa. Kunapaswa kuwa na makampuni ya wafanyakazi wenye bidio wanaofanya kazi mijini. Wanaume wanapaswa kusoma kile kinachohitajika kufanywa kwenye umati wa watu ambao umepuuzwa. Bwana amekuwa akituita tutilie umakini kwa umati huu uliopuuzwa katika miji mikubwa, lakini suala hilo limezingatiwa kwa udogo sana. {FEsw 537.3}

Hatuko tayari kumsumbua Bwana kwa maombi yetu, na kumwomba kipawa cha Roho Mtakatifu. Bwana anataka sisi tumsumbue katika jambo hili. Anataka tushinikize maombi yetu kwenye kiti Chake cha enzi. Nguvu ya Mungu ya kuongoa inahitaji kuhisiwa katika safu zetu zote. Elimu ya thamani zaidi ambayo inaweza kupatikana itakuwa kupatikana ni ile ya kwenda nje na ujumbe wa ile Kweli mahali

ambapo sasa pako gizani. Tunapaswa kwenda nje kama vile wanafunzi wa kwanza walivyoenda kwa kutii agizo la Kristo. Mwokozi aliwapa wanafunzi maagizo.maelekezo yao. Kwa Maneno machache aliwaambia yale waliyoweza kutarajia kukutana nayo. “Nawatuma ninyi,” Yeye alisema, “kama kondoo miongoni mwa mbwa-mwitu: basi iweni wenye busara kama nyoka na kuwa watu wapole kama hua.” Wafanyakazi hawa walipaswa kwenda kama wawakilishi Wake, Yeye ambaye alitoa uhai Wake kwa ajili ya uhai wa dunia. {FEsw 537.4}

Bwana anatutaka tuingie katika upatanifu Naye. Ikiwa tutafanya hili, Roho Wake anaweza kutawala nia zetu. Ikiwa uelewa wa Kweli wa kile kinachojumuisha ile elimu muhimu, na jitahidi kuifundisha kanuni, Kristo atatusaidia. Aliwaahidi wafuasi Wake kwamba wakati watakapolazimishwa kusimama mbele ya mabaraza na mahakimu, hawakupaswa kuwaza maneno ya kujibu au kusema. Nitakufundisha, Alisema. Nitakuongoza. Tukijua kile ambacho Mungu anaenda kutufundisha, wakati Maneno ya hekima ya Mbinguni yanaletwa akilini mwetu, tutayatofautisha haya na mawazo yetu wenyewe. Tutaelewa kama haya ni Maneno ya Mungu, nasi tutaona katika Maneno ya Mungu hekima na uzima na nguvu....{FEsw 538.1}

Tunapaswa kuwaelimisha vijana kufanya mazoezi sawia ya kiakili na nguvu za kimwili (balansi ya kazi ya mikono na ya akili). Mazoezi yenye afya kwa mwili mzima yatatoa elimu ambayo ni pana na inayojumuisha kila kitu bora. Tulikuwa na ngumu kazi ya kufanya nchini Australia katika kuelimisha wazazi na vijana pamoja katika mistari hii; lakini tulivumilia katika juhudi zetu hadi somo likapatikana kwamba ili kuwa na elimu iliyokamilika, wakati wa kujifunza ni lazima ugawanywe kati ya kupata maarifa ya kitabu na kupata maarifa ya kazi za vitendo. Sehemu ya kila siku ilitumika katika kazi muhimu, yenye manufaa, wanafunzi walijifunza jinsi ya kusafisha ardhi, jinsi ya kukatua udongo, na jinsi ya kujenga nyumba, nao wakutumia muda kwa manufaa ambao vinginevyo ungetumika katika kucheza michezo na kutafuta pumbao/maburudisho. Na Bwana akawabariki wanafunzi ambao walitoa muda wao hivyo, kwa kujizoeza tabia zenye manufaa. {FEsw 538.2}

Waagize wanafunzi wasichukulie kuwa nadharia ndiyo sehemu muhimu zaidi kwenye sehemu ya elimu yao. Hebu hili liwe na hisia za kina zaidi juu ya kila mwanafunzi, kwamba tunapaswa kuwa na ufahamu wenye akili kuhusiana na jinisi ya kuutendea mfumo wa mwili. Na kuna wengi ambao wangekuwa na akili zaidi katika mambo haya kama hawangejifungia wenyewe kwa miaka ya kusoma bila uzoefu wa vitendo. Kwa jinsi tunavyojikabidhi kwa kikamilifu zaidi chini ya uongozi wa Mungu, ndivyo tunapata maarifa zaidi kutoka kwa Mungu. Hebu na tuwaambie wanafunzi wetu: Jiwekeni katika mahusiano na kile Chanzo cha nguvu zote. Ninyi ni watenda kazi pamoja na Mungu. Yeye Atakuwa Mwalimu wetu mkuu. {FEsw 539.1}

— [The Review and Herald, Novemba 11, 1909.](#)

Kwa marejeleo ya ziada

Reading Loma Linda College of Evangelists, Testimonies for the Church, 9:173-178 {1909}

The Physician an Educator, The Ministry of Healing, 125-136 {1909}

General Hygiene, The Ministry of Healing, 171-176 {1909}

Hygiene Among the Israelites, The Ministry of Healing, 276-186 {1909}

Dress, The Ministry of Healing, 287-294 {1909}

Diet and Health, The Ministry of Healing, 295-310 {1909}

True Education and Missionary Training, The Ministry of Healing, 395-406 {1909}

A True Knowledge of God, The Ministry of Healing, 409-426 {1909}

Danger in Speculative, The Ministry of Healing, 427-438 {1909}

Knowledge The False and True in Education, The Ministry of Healing, 439-450 {1909} Importance of Seeking True Knowledge, The Ministry of Healing, 451-458 {1909} The Knowledge Received through God's Word, The Ministry of Healing, 458-466 {1909}

Decision of Character. The Youth's Instructor, January 25, 1910

The Gift of Speech, The Review and Herald, May 12, 1910

Unholy Knowledge, The Review and Herald, August 4, 1910

Counsel to Teachers 453 Temperance in the Family, Signs of the Times, September 13, 1910

The Mother a Missionary, Signs of the Times, September 20, 1910

The Father's Duty, Signs of the Times, October 18, 1910

Christian Homes, The Review and Herald, November 22, 1910

The Home School, Signs of the Times, January 12, 1911

Walk in the Light, The Youth's Instructor, January 17, 1911

Woman in the Home, Signs of the Times, April 4, 1911

Woman in the Home, Signs of the Times, June 30, 1911

Parents as Character Builders, Signs of the Times, October 5, 1911

A Godly Example in the Home, Signs of the Times, October 12, 1911

A Message to Parents, The Review and Herald, February 1, 8, 1912

Words to the Young, The Youth's Instructor, April 23, 1912

Training the Youth to be Workers, The Review and Herald, May 16, 1912

Young Men as Missionaries, The Review and Herald, May 23, 1912

Sura ya 71

UELEWA BORA WA KWELI KWA VIJANA WETU

Kwa dhana potofu ya asili ya Kweli na kitu cha elimu wengi wameongozwa katika makosa makubwa na hata kusababisha kifo. Kosa kama hilo inafanywa wakati udhibiti wa moyo au uanzishwaji wa haki kanuni hupuuzwa katika jitihada za kupata utamaduni wa kiakili, au wakati masilahi ya milele yanapuuzwa katika hamu ya kupata faida ya muda. {FEsw 541.1}

Ni sawa kwa vijana kuhisi kwamba lazima wafikie kilele cha maendeleo ya nguvu zao za asili. Hatungewekea mipaka elimu ambayo Mungu hajaweka kikomo. Lakini mafanikio yetu yatafaa sifuri kama hayatatumika kwa ajili ya heshima ya Mungu na wema wa wanadamu. Isipokuwa ujuzi wetu ni ngazi ya kufikia mafanikio ya madhumuni ya juu, basi haina thamani. {FEsw 541.2}

Umuhimu wa kuanzisha shule za Kikristo umesisitizwa juu yangu kwa nguvu sana. Katika shule nyingi za siku hizi mambo mengi yanafundishwa ambayo ni vizuizi vinavyoleta uchelewesho badala ya baraka. Shule zinahitajika pale Neno la Mungu limefanywa kuwa msingi wa elimu. Shetani ndiye mkuu adui wa Mungu, na ni lengo lake daima kuwaongoza watu kutoka kwenye uaminifu wao kwa Yule aliye Mfalme wa Mbinguni. Makusudi ya mwovu ni kuishinikiza akili ya wanaume na wanawake kwa makusudi ya kutoa ushawishi wake kwenye upande ule wa ufiadini wa kimaadili, badala ya kutumia vipaji vyao katika utumishi wa Mungu. Lengo lake linapatikana kwa ufanisi, wakati, kwa kupotosha mawazo yao ya elimu, anafaulu kuwasajili wazazi na walimu kwenye orodha yake; kwa elimu mbaya, yeye mara nyingi huanzisha zoezi la kuziweka akili barabarani kwenye njia inayoelekea kwenye ukafiri. {FEsw 541.3}

Katika shule nyingi na vyuo vya leo, hitimisho ambalo watu wasomi wamefikia kama matokeo ya uchunguzi wao wa kisayansi, hufundishwa kwa uangalifu na kufafanuliwa kikamilifu; na maoni yanatolewa wazi kwamba ikiwa watu hawa wasomi ni sahihi, basi Biblia haiwezi kuwa sahihi. Miiba ya mashaka imefichwa;

miiba hiyo imefichwa vizuri kwa majani ya sayansi na falsafa yaliyonawiri na kuchanua na hata kupendeza machoni. Mashaka-mashaka {skepticism} huvutia akili ya mwanadamu. Vijana wanaona ndani yake uhuru unaovutia fikira, na wanadanganyika. Na kisha Shetani hushinda; kile alichotaka kumaanisha huyu adui, hatimaye kimekuwa. Anaipa lishe ile mbegu ya shaka ambayo imepandwa katika mioyo ya vijana, na hivi karibuni mavuno ya ukafiri tele huvunwa. {FEsw 541.4}

Hatuwezi kuruhusu akili za vijana wetu kutiwa chachu hivi; kwa maana ni lazima tutegemee kwamba ni kupitia vijana hawa ndiyo kutakuwa na kusonga mbele kwa kazi katika siku zijazo. Matamano yetu ni zaidi ya hiyo fursa ya elimu katika sayansi. Sayansi ya elimu ya kweli ni Ukweli (ile Kweli ni Neno la Mungu tu, ndiyo kweli yote, na kweli tupu, all truth and absolute truth), ambao unapaswa kugusa sana moyo na kukaziwa moyoni, hivi kwamba hauwezi kufutwa na makosa ambayo yameenea kila mahali. {FEsw 542.1}

Neno la Mungu linapaswa kuwa na nafasi—nafasi ya kwanza—katika kila jambo na mfumo wa elimu. Kama nguvu ya kuelimisha, lina thamani zaidi kuliko maandishi ya wanafalsafa wote, wa enzi au vizazi vyote. Katika upana wake anuwai ya mitindo na masomo kuna kitu cha kupendeza na kufundisha kila akili, ili kuimarisha na kuboresha kila maslahi. Nuru ya ufunuo wa Mungu inang'aa bila kufifia katika siku za nyuma za mbali ambapo kumbukumbu ya historia ya wanadamu haikutoa miale ya mwanga. Kuna mashairi ambayo yameita **mshangao, sifa na mastaajabu** ya ulimwengu. Katika uzuri unaong'aa, katika adhama tukufu, katika kugusa hisia za huzuni au huruma {pathos}, haina usawa na uzalishaji wa kipaji kikuu zaidi cha fikra za binadamu (genius). Kuna mantiki ya sauti na ufasaha wa shauku. Kuna taswira ya matendo matukufu ya watu wa vyeo, wakuu na waungwana, mifano ya fadhila binafsi na heshima ya umma, masomo ya uchaMungu na usafi wa moyo. {FEsw 542.2}

Hakuna nafasi katika maisha, hakuna awamu ya uzoefu wa binadamu, ambayo Biblia haina mafundisho yenye thamani hapo. Mtawala na mtumwa, bwana na mtumwa, mnunuzi na muuzaji, akopaye na mkopesaji; mzazi na mtoto, mwalimu na mwanafunzi, -wote hapa wanaweza kupata masomo hapa yenye thamani isiyo na kifani, isiyo na hesabu. , {FEsw 542.3}

Lakini zaidi ya yote, Neno la Mungu linaweka wazi mpango wa wokovu: linaonyesha jinsi mwanadamu mwenye dhambi anavyoweza kupatanishwa na Mungu, inaweka msingi wa kanuni kuu za ile Kweli na majukumu yayopaswa kutawala maisha yetu na inatuahidi msaada wa Bwana katika ushikaji wao. Inafikia mbele zaidi ya maisha haya yakimbiayo na ya mfupi, mbele zaidi ya historia fupi na yenye matatizo ya mbio za jamii yetu ya ubinadamu. Na inafungua katika maoni

yetu barabara refu ya maono ya kupendeza inayoelekea kwenye zama za milele, —zama zisizo na giza la dhambi, wala kivuli cha huzuni. Inatufundisha jinsi tunavyoweza kushiriki makao ya waliobarikiwa, na kutuagiza kutia nanga ya matumaini yetu na kukita mapenzi yetu huko. {FEsw 542.4}

Nia za kweli za huduma zinapaswa kuwekwa mbele ya wazee na vijana. Wanafunzi wanapaswa kufundishwa kwa njia ambayo watakuzwa na kuwa wanaume na wanawake wenye manufaa. Kila njia ambayo itawainua juu, itawaboresha na kuwaheshimisha inapaswa kutumiwa. Wanapaswa kufundishwa kuweka zao mamlaka na nguvu zao kwenye matumizi bora. Nguvu za kimwili na kiakili zinapaswa kutozwa ushuru sawia. Mazoea ya utaratibu na nidhamu yanapaswa kusitawishwa. Nguvu ambayo inasisitiza maisha ya usafi wa moyo, na ya kweli inapaswa kuwekwa mbele ya wanafunzi. Hii itawasaidia katika maandalizi ya huduma muhimu. Kila siku wao watakuzwa katika usafi wa moyo na nguvu zaidi, wakiwa wameandaliwa vyema kupitia neema Yake na kujifunza Neno Lake, na kuweka juhudi kali dhidi ya uovu. {FEsw 543.1}

Elimu ya kweli ni kukaziwa kwa mawazo hayo tena na tena kwenye ubongo, mawazo ambayo yatakutia akili na moyo kwenye maarifa ya Mungu, aliye Muumba na Yesu Kristo Mkombozi. Elimu kama hiyo itafanya akili upya na kuigeuza/kubadilisha tabia. Itaimarisha na kuipa nguvu akili dhidi ya minong'ono ya udanganyifu ya adui wa Roho, na kutuwezesha kuitambua/kuielewa sauti ya Mungu. Itawafaa waliojifunza kuwa watendakazi pamoja na Kristo. {FEsw 543.2}

Vijana wetu wakipata maarifa haya, wataweza kupata yote mengine ambayo ni muhimu; lakini ikiwa sivyo, ujuzi wote wanaoweza kupata kutoka kwa ulimwengu hakutawaweka katika safu za Bwana. Wanaweza kukusanya maarifa yote ambayo vitabu vinaweza kutoa, na bado kuwa wasiojua kanuni za kwanza za haki ambayo inaweza kutoa kwao tabia inayokubaliwa na Mungu. {FEsw 543.3}

Wale ambao wanatafuta kupata maarifa katika shule za dunia wanapaswa kukumbuka kwamba shule nyingine pia inawadai kuwa wanafunzi wake, —shule ya Kristo. Kwenye shule hii wanafunzi hawajawahi kuhitimu bado. Miongoni mwa wanafunzi, wapo wazee na vijana. Wale ambao huzingatia maagizo ya Mwalimu, ambaye ni Mungu Mwenyewe, daima wao hupata hekima zaidi, heshima na ubora wa nafsi, na hivyo wanatayarishwa kuingia katika shule ile ya ya juu, ambapo maendeleo yatasonga mbele milele zote. {FEsw 543.4}

Hekima isiyo na kikomo inaweka mbele yetu masomo makuu ya maisha, - masomo ya wajibu na furaha. Haya mara nyingi ni magumu kujifunza, lakini bila kuwa nayo, hatuwezi kufanya maendeleo ya kweli. Yanaweza kutugharimu juhudi, machozi, na hata uchungu; lakini tusilegee wala tusichoke. Ni katika ulimwengu huu, katikati ya majaribu na mitihani, ndipo tunapaswa kufunzwa kufaa kuwa miongoni mwa jamii ya malaika safi na watakatifu. Wale ambao wanajishughulisha

sana na masomo ambayo sio muhimu sana hivi kwamba wanaacha kujifunza katika shule ya Kristo, hakika wanakutana na hasara isiyo na kikomo. {FEsw 544.1}

Kila kitivo, kila sifa, ambayo Muumba amewakirimia watoto wa wanadamu, inapaswa kutumika kwa Utukufu Wake; na vijana wetu wakitumika hivi, ndani yao kupatikana zoezi usafi wa moyo, ubora na furaha zaidi. Kanuni za Mbinguni zinapaswa kufanywa kuwa kuu katika maisha, na kila hatua ya mapema inayochukuliwa katika upataji wa maarifa au katika Utamaduni wa akili inapaswa kuwa **hatua ya uwekezaji kwa mwanadamu ili afanane na Mungu.** {FESW 544.2}

Kwa wengi wanaowaweka watoto wao katika shule zetu, majaribu makali yatakuja kwa sababu wanatamani wapate kile ambacho ulimwengu unaendelea kuchukulia kuwa ndiyo elimu muhimu zaidi. Lakini nini kinajumuisha elimu muhimu zaidi, isipokuwa iwe ni elimu inayopatikana kutoka katika Kitabu kile ambacho ni msingi wa elimu yote ya Kweli? Wale ambao wanaona kuwa ujuzi unaopatikana katika mstari wa elimu ya kidunia ni muhimu, wanafanya makosa makubwa, ambayo yatasababisha wao kuyumbishwa na maoni ambayo ni ya kibinadamu na yenye makosa makubwa. {FEsw 544.3}

Wale wanaoitafuta elimu ambayo ulimwengu huu unaithamini sana, huongozwa hatua kwa hatua, mbali zaidi na zaidi kutoka kwenye kanuni za ile Kweli hadi wanakuwa walimwengu walioelimika. Je, wamepata elimu yao kwa gharama ipi! Wameachana na Roho Mtakatifu wa Mungu. Wao wamechagua kukubali kile ambacho ulimwengu unakiita maarifa, badala ya zile Kweli ambazo Mungu amewakabidhi wanadamu kupitia watumishi Wake na manabii na mitume. {FEsw 544.4}

Juu ya baba na mama limekabidhiwa jukumu la urithi la kutoa Elimu ya Kikristo kwa watoto waliokabidhiwa kama amana. Katu wao hawatakiwi kuruhusu mstari wowote wa biashara kunyonya akili yao, wakati na vipaji, kwamba watoto wao waruhusiwe kuondoka barabarani na kisha kutenganishwa mbali kutoka kwa Mungu. Hawapaswi kuwaruhusu watoto wao kutoroka kutoka mikononi mwao na kwenda kwenye mikono ya makafiri. Wanapaswa kufanya yote katika uwezo wao ili kuwazuia wasilete mvinyo wa mafundisho ya Roho ya ulimwengu. Wanapaswa kutoa mafunzo ili wawe watenda kazi pamoja na Mungu. Wanapaswa kuwa mkono wa Mungu, wakitenda kazi kwa niaba Yake, wakijitayarisha wenyewe na watoto wao kufaa kwa maisha yale yasiyo na mwisho. {FEsw 545.1}

Kuna kazi ya dhati na ya bidii, inayopaswa kufanywa kwa watoto. Kabla ya kuja kwa pigo kubwa juu ya wote wakao juu ya dunia. Bwana anawaita wale wote ambao ni Waisraeli kweli kweli kumtumikia. Kusanyeni watoto wenu katika nyumba zenu; wakusanyeni kutoka kwenye makundi ya watu wanaotamka maneno ya Shetani, ambao wanaziasi amri za Mungu. Hebu katika kazi yetu ya elimu tukumbatie watoto na vijana wengi zaidi, na kisha kutakuwa na jeshi zima la

wamisionari walioinuliwa kufanya kazi kwa ajili ya Mungu. {FEsw 545.2}

Taasisi zetu za elimu zinapaswa kufanya mengi katika kukidhi mahitaji mahitaji ya watendakazi waliofunzwa katika nyanja za misheni. Wafanyakazi ni zinahitajika duniani kote. Ukweli wa Mungu unapaswa kubebwa nchi za kigeni, ili walio gizani wapate Nuru. Vipaji vilivyokuzwa vinahitajika katika kila sehemu ya kazi ya Mungu.

Mungu amepanga kwamba shule zetu ziwe chombo cha matumizi katika kuendeleza watenda kazi kwa ajili Yake, - watenda kazi ambao Yeye hataletewa aibu nao. Anawataka vijana wetu kuingia katika shule zetu, na kujishughulisha kwa haraka ili wafae kwa ajili ya utumishi. {FEsw 545.3}— The Review and Herald, Agosti 22, 1912.

Kwa Masomo ya Ziada

Dangerous Amusements for the Young, The Review and Herald, August 29, 1912
Dignity of Labor, The Review and Herald, October 3, 1912

What Shall Our Children Read? The Review and Herald, January 23,

The Review and Herald, 30, 1913 1913 Publication of book “Counsels to Teachers” {for topics see table of contents}

Looking Unto Jesus, The Review and Herald, July 16, 1914

Simplicity and Economy, The Review and Herald, July 30, 1914

EfFEswct of Mind on Health, Signs of the Times, October 6, 1914 Women as Missionaries, The Review and Herald, December 10, 1914

Sura ya 72

UJUMBE KWA VIJANA WETU WADOGO

Kuna vitabu ambavyo vina umuhimu wa pekee ambavyo havijasomwa na Vijana. Vimetupiliwa mbali kwa sababu haviwavutii wao kama ilivyo kwa vitabu vyenye mambo mepesi kama vile futuhi. {FEsw 547.1}

Tuwashauri vijana kuvishikilia vitabu hivi vinatoa mwongozo wa makuzi mema ya tabia za Mkristo. Mawazo muhimu sana ya Imani yetu yanatakiwa yagongwe muhuri katika kumbukumbu za vijana. Wamekuwa wakitazama kwa haraka Kweli hizi, lakini hakuna cha kuwafanya kujua na kuwaongoza kutazama wanavyosoma kwa matamania makubwa. Vijana wetu wanatakiwa kusoma vile vilivyo na msaada wa uongofu, yenye matokeo ya utakaso mawazoni kwao. Wanahitaji hii ili kwamba waweze kuelewa dini ya Kweli. Kuna maandishi mengi mazuri ambayo hayatakasi. {FEsw 547.2}

Huu ni wakati wetu na nafasi yetu sasa kufanya kazi kwa ajili ya vijana. Waambie kwamba tuko kwenye dhahama ya kutisha, na tunataka kujua jinsi ya kuuishi utakatifu wa Kweli. Vijana wetu wadogo wanahitaji kusaidiwa, kuinuliwa na kutiwa moyo, lakini kwa njia sahihi; siyo, labda vile ambavyo wangelitamani, bali kwa njia ile ambayo itawasaidia kuwa na mawazo yaliyotakaswa. Wanahitaji dini nzuri na ya kutakasa kuliko kitu kingine chochote. {FEsw 547.3}

Sitarajii kuishi muda mrefu. Kazi yangu ni karibu ikamilike. Waambie vijana wetu kwamba ninahitaji maneno yangu yawatie moyo kwa jinsi ambavyo tabia ya maisha yao itakuwa ya kuvutia zaidi kwa zile akili za Mbinguni, na mvuto wao kwa vijana wengine unapasha kuwa bora zaidi. {FEsw 547.4}

Katika majira ya usiku nilikuwa nikichagua na kutenga pembeni vitabu ambavyo havina faida kwa vijana. Tunapaswa kuwachagulia vitabu ambavyo vitawasaidia katika unyofu wa moyo katika maisha halisi ya ile Kweli, na kuwaongoza kulifungua Neno. Hii ililetwa kwangu wakati uliopita, nilidhani ningeipata kabla hujaihifadhi. Hatutaweza kumudu kuwapatia vijana vitabu visivyokuwa na thamani. Vitabu vilivyo mbaraka kwa akili na Roho vinahitajika. Vitu hivi vinapewa nafsi kwa wepesi sana; hivyo, watu wetu wanapaswa kufahamu kile ninachokisema. {FEsw 547.5}

Sidhani kuwa ninaweza kuwa na shuhuda zaidi kwa watu wetu. Watu wetu waliopevuka mawazo wanajua kipi kilicho kizuri kwa ajili ya kuinua na kuijenga kazi. Lakini kwa upendo wa Mungu mioyoni mwao, wanahitajika kuzama ndani na ndani zaidi katika kujifunza mambo ya Mungu. Nina matamania makubwa kwamba vijana wetu watakuwa na aina fulani ya vitabu vya kusoma; baadaye watu wazima watalipata hili pia. Lazima tuweke macho yetu juu ya vivutio vya Ukweli wa dini. Lazima tuweke mawazoni na akili wazi kwenye Ukweli wa Neno la Mungu. Shetani huja mahala ambapo watu hawajui. Hatutakiwi kuridhika kwa sababu ujumbe wa onyo umetolewa huko awali. Tunatakiwa kuuwasilisha Ukweli huu tena na tena. {FEsw 548.1}

Tunaweza kuanza mafunzo ya kusoma kwa umakini na mvuto ambao unaweza kuvutia na kushawishi mawazo mengi. Kama nitapewa nafasi ya kufanya kazi zaidi, kwa furaha nitaandaa vitabu kwa ajili ya vijana. {FEsw 548.2}

Kuna kazi ya kufanywa na vijana ambapo mawazo yao yataavutiwa na kuuundwa na kutakaswa na Ukweli wa Mungu. Ni tumaini langu la dhati kwa vijana wetu kwamba wataupata Ukweli halisi wa mada ya haki kwa imani, na tabia kamili ambayo itawaandaa kwa uzima wa milele. Sitarajii kuishi muda mrefu sana, na ninawaachia ujumbe huu lwa vijana, kwamba ujumbe walionao haupotei. {FEsw 548.3}

Ninawasihi wapendwa wangu kuwatia moyo zaidi vijana kutunza thamani ya Ukweli wa Neema ya Mungu mbele yao kwa uzingativu wa hali ya juu. Kazi yenu na maombi yasiyokoma ni yenye thamani juu ya dini ya Kweli. Leta mibaraka na vivutio vya utakatifu na Neema ya Mungu. Ninahisi mzigo juu ya hili jambo kwa sababu ninajua limepuuzwa. {FEsw 548.4}

Sina uhakika kwamba Maisha yangu yatadumu kwa muda mrefu, lakini ninahisi kwamba nimekubaliwa na Bwana. Anajua ni kwa kiasi gani mimi nimeteseka na kuhangaika kwa kuwa nimeshuhudia viwango vya hali chini/duni ya maisha vikirithiwa na wale wanaoitwa Wakristo. Ninahisi kuwa ilikuwa ni muhimu kwamba Ukweli uonekane katika maisha yangu, na kwamba ushuda wangu unapaswa kwenda kwa watu. Ninahitaji kuwa ufanye kila linalowezekana maandishi yangu yawekwe mikononi mwa watu wengi nchi za kigeni. {FEsw 548.5}

Waambie Vijana kwamba wamekuwa na faida nyingi za kiroho. Mungu

anawataka kuwa na juhudi za pekee kupeleka ile Kweli kwa watu Mungu. Ninafurahishwa kwamba ni kazi yangu ya pekee kuyasema mambo haya. {FEsw 549.1}—[The Review and Herald, April 15, 1915](#)